# Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste

KITABU KIONGOZI KWA AJILI YA WACHUNGAJI WAAFRIKA

# Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste

## Kitabu Kiongozi kwa Ajili ya Wachungaji Waafrika

Denzil R. Miller, Mhariri
Jeffery Nelson, Mhariri Mwenza
Todd Churchill, Mhariri Mwenza

Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste: Kitabu Kiongozi kwa Ajili ya Wachungaji Waafrika. Hakimiliki © 2022 na Africa's Hope, Springfield, Missouri, USA. Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoweza kunakiliwa tena, kuhifadhiwa katika mfumo aina yoyote au kusambazwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote (ya kielektroniki, mitambo, nakala, kurekodi au vinginevyo) bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwenye hakimiliki, isipokuwa nukuu fupi kwa ajili ya kutumika katika majarida, magazeti, na hakiki.

Maandiko yote kwa sehemu kubwa, isipokuwa imeonyeshwa vinginevyo, yametoka katika Biblia ya Kiswahili: Habari Njema kwa Watu Wote, Tafsiri ya Ushirikiano wa Makanisa. Hakimiliki © 1995, 2001: Chama cha Biblia Tanzania na Chama cha Biblia Kenya. Haki Zote Zimehifadhiwa. Vile vile kuna maandiko kutoka Biblia ya Kiswahili: Union Version, Hakimiliki © 1952, 1997; Chama cha Biblia Tanzania na Kenya. Haki Zote Zimehifadhiwa. Lengo la kufanya hivyo ni ili mistari mingi ieleweke vizuri zaidi. Pia, itakuwepo tafsiri ya moja kwa moja ya mistari fulani fulani ili kuleta maana iliyokusudiwa na mwandishi, ikibidi.

Kamati ya Wahariri:
Denzil R. Miller, DMin, Mhariri
Jeffery Nelson, PhD, Mhariri Mwenza
Todd Churchill, Mhariri Mwenza

Kimetafsiriwa na Simon Joel Vomo

Miller, Denzil R., mhariri, 1946 -
Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste: Kitabu Kiongozi kwa Ajili ya Wachungaji Waafrika / Denzil R. Miller, Jeffery Nelson, na Todd Churchill

Kimetolewa na Taasisi ya Africa's Hope
580 West Central Street
Springfield, Missouri, USA 65802

Kimechapishwa Marekani

# Yaliyomo

Yaliyomo ........ 3
Orodha ya Wachangia Mada ........ 7
Utangulizi wa Randel Tarr ........ 11
Utangulizi wa Dkt. Barnabas Mtokambali ........ 13
Maneno ya Mwanzo ........ 15

**~ SEHEMU YA 1 ~**
**SIFA ZA MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE**

Sura ya 1 ~ Mtu wa Uzoefu ........ 21
Sura ya 2 ~ Mtu wa Roho ........ 31
Sura ya 3 ~ Mtu Mwenye Tabia Njema ........ 41
Sura ya 4 ~ Mtu Aliyeandaliwa Vizuri ........ 49

**~ SEHEMU YA 2 ~**
**VIPAUMBELE VYA MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE**

Sura ya 5 ~ Vipaumbele vya Kihuduma ........ 61
Sura ya 6 ~ Vipaumbele vya Kibinafsi ........ 71
Sura ya 7 ~ Vipaumbele vya Familia ........ 81
Sura ya 8 ~ Kipaumbele cha Maombi ........ 91

**~ SEHEMU YA 3 ~**
**ANAVYOVIAMINI MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE**

Sura ya 9 ~ Anaiamini Biblia ........ 103
Sura ya 10 ~ Husimamia Ukweli wa Kipentekoste ........ 113
Sura ya 11 ~ Hukuza Utendaji na Uzoefu wa Kipentekoste ........ 123
Sura ya 12 ~ Anathamini Urithi wa Kipentekoste ........ 133

**~ SEHEMU YA 4 ~**
**MAISHA BINAFSI YA MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE**

Sura ya 13 ~ Maisha Yanayosimamiwa Vizuri ........ 145
Sura ya 14 ~ Mahusiano Mazuri Yanayofaa ........ 155
Sura ya 15 ~ Tabia Imara ya Ibada Binafsi ........ 163

**~ SEHEMU YA 5 ~**
**HUDUMA YA MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE MBELE YA WATU**


Sura ya 16 ~ Mahubiri Yenye Upako wa Roho ............ 173
Sura ya 17 ~ Kufundisha kwa Ufanisi ............ 183
Sura ya 18 ~ Kuliongoza Kanisa Katika Kuabudu ............ 193
Sura ya 19 ~ Kuliongoza Kanisa Katika Uamsho wa Kipentekoste ............ 203
Sura ya 20 ~ Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho ............ 213
Sura ya 21 ~ Kuhudumu Katika Nguvu za Roho ............ 221
Sura ya 22 ~ Kujihusisha Katika Vita vya Kiroho ............ 231


**~ SEHEMU YA 6 ~**
**MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE KAMA MCHUNGAJI**


Sura ya 23 ~ Kuielewa Huduma ya Kichungaji ............ 241
Sura ya 24 ~ Kuwatunza Kondoo ............ 253
Sura ya 25 ~ Kuuimarisha Mwili ............ 261
Sura ya 26 ~ Kuwashauri Watu wa Mungu ............ 269
Sura ya 27 ~ Kulilinda Kundi ............ 279


**~ SEHEMU YA 7 ~**
**MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE KAMA KIONGOZI**


Sura ya 28 ~ Uongozi wa Kipentekoste ............ 291
Sura ya 29 ~ Uongozi wa Kitumishi ............ 301
Sura ya 30 ~ Uongozi Wenye Maono ............ 311
Sura ya 31 ~ Uongozi wa Kimisheni ............ 321


**~ SEHEMU YA 8 ~**
**MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE KAMA MSIMAMIZI**


Sura ya 32 ~ Kutunza na Kusimamia Taarifa, Fedha, na Mali ............ 331
Sura ya 33 ~ Kuhamasisha Viongozi Walei ............ 341
Sura ya 34 ~ Kuongoza Kanisa Katika Idara ............ 351
Sura ya 35 ~ Usimamizi wa Washirika wa Kanisa ............ 361

## ~ SEHEMU YA 9 ~
## MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE KATIKA UMISHENI

Sura ya 36 ~ Kuelewa Mkakati wa Agano Jipya ....373
Sura ya 37 ~ Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti ....383
Sura ya 38 ~ Kutumikia Jumuiya ....393
Sura ya 39 ~ Kupanda Makanisa Mapya ....403
Sura ya 40 ~ Kutengeneza Mpango wa Utume wa Kanisa la Mahali Pamoja ....413

## ~ SEHEMU YA 10 ~
## MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE NA IBADA MAALUM

Sura ya 41 ~ Kufanya Harusi na Mazishi ....425
Sura ya 42 ~ Kuendesha Meza ya Bwana, Kuweka Wakfu, na Kuingiza Kazini ....435

## VIAMBATISHO

Nyongeza ya 1 ~ Tamko la Imani la Umoja wa Assemblies of God Duniani ....447
Nyongeza ya 2 ~ Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10 ....451
Nyongeza ya 3 ~ Ufupisho wa Vitabu vya Biblia ....453

*Orodha ya Wachangia Mada*

# Orodha ya Wachangia Mada

Ifuatayo ni orodha ya waliochangia mada katika kitabu hiki. Namba zilizo kwenye mabano zinaonyesha sura na mada alizochangia anayetajwa.

---

Adade, Ayi, PhD. Katibu Mkuu, Togo Assemblies of God (29)

Ama, UcheChukwu. Naibu Mwenyekiti, Africa Assemblies of God Alliance World Missions (40)

Banda, Lipenga. Mwangalizi Mkuu wa Assemblies of God nchini Zambia (33)

Bogere, Richard, PhD. Mwanzilishi mwenza, Christ Chapel International, Kampala, Uganda; Mkufunzi Mshiriki, Kitivo cha Ualimu, Seminari ya Theolojia ya Pan-Africa (6)

Bomboko, Cécile, PhD. Mwakilishi wa Kanda ya Afrika ya Kati, Umoja wa Elimu ya Theolojia ya Kipentekoste Afrika (APTEA) (14, 32)

Bomboko, Marcel, PhD. Mwenyekiti, Bodi ya Wasimamizi, Kitivo cha Theolojia cha Assemblies of God, Lomé, Togo (14, 32)

Chipao, Lawrence, PhD. Mkuu wa Kitivo cha Theolojia na Malezi ya Kihuduma, Chuo Kikuu cha Malawi Assemblies of God (34)

Churchill, Todd. Mishenari wa AGWM nchini DR Congo; Mtumishi, Taasisi ya Africa's Hope (30)

Daplex Ouentchist, Honoré, PhD. Rais, Kanisa la Kiinjili la Assemblies of God, Cotê d'Ivoire (10)

Djakouti, Mitré. Rais, Togo Assemblies of God; Rais Mstaafu, Umoja wa Makanisa ya Assemblies Of God Afrika (AAGA) (15)

Dube, Andrew, PhD. Mwangalizi Mkuu, Malawi Assemblies of God (11)

Flindja, Douti Lallebili, PhD. Mkuu wa Masomo, Kitivo cha Theolojia cha Assemblies of God, Lomé, Togo (27)

Frimpong-Manso, Paul, PhD. Mwangalizi Mkuu, Assemblies of God, Ghana (37)

Gnanchou, Désiré Béchié, PhD. Rais Mstaafu, Evangelical Assemblies of God, Cotê d'Ivoire; Mkurugenzi, Taasisi ya Theolojia na Kichungaji ya Katadji (23)

Kitoto, Dina. Mke wa Philip Kitoto, Mwangalizi Mkuu wa Kenya Assemblies of God (7)

Kitoto, Philip. Mwangalizi Mkuu, Kenya Assemblies of God na Mkuu, Chuo Kikuu cha KAG Afrika Mashariki (7)

Kuoh, Jimmy, PhD. Mwangalizi Mkuu Mstaafu, Assemblies of God Liberia; Rais, Chuo cha Biblia cha Assemblies of God Liberia (21, 41)

Lebelo, Gordon, PhD. Mwangalizi Mkuu, International Assemblies of God, Afrika Kusini (26)

Lwesya, Enson, DMin. Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Malawi Assemblies of God (28)

Mba, Arthur, PhD. Makamu wa Kwanza wa Rais, Assemblies of God nchini Gabon (2, 18)

Mbiwan, Daniel. Msimamizi Mkuu, Misheni ya Full Gospel, Cameroon (25)

Miller, Denzil R., DMin. Mishenari wa AGWM; Mkurugenzi, Acts in Africa Initiative (1, 3, 8, 16, 20, 36)

N'sembe Loyela, Israël. Mchungaji, Kituo cha Kiinjili cha Sanduku la Agano, Kinshasa; Mwangalizi Mkuu Mstaafu wa Assemblies of God, DR Congo (22)

Ndayisaba, Jérôme. Rais, Burundi Assemblies of God Fellowship (24)

Nelson, Jeffery, PhD. Mishenari wa AGWM; Makamu Mkuu wa zamani, Chuo Kikuu cha KAG Afrika Mashariki, Nairobi, Kenya (5, 12, 39)

Ngabonziza, Emmanuel. Makamu Msimamizi Mkuu, Pentecostal Assemblies of God, Rwanda (38)

Niba, Felix, PhD. Mkurugenzi wa Umisheni wa Nje, Misheni ya Full Gospel, Cameroon (13)

Oganya, Ngozi Cecilia, PhD. Mratibu wa Elimu Enezi ya Theolojia, Assemblies of God Divinity School, Umuahia, Nigeria (17)

Sawadogo, Jephté, DMin. Makamu Mwangalizi Mkuu, Burkina Faso Assemblies of God; Mkurugenzi, Shule ya Biblia ya Koubri (4, 42)

Sebastião, Francisco. Rais wa Assembly of God Pentecostal, Angola (9)

Smith, Bernard, MA. Mishenari wa AGWM nchini Togo (15)

Swai, Ron. Mweka Hazina Mkuu, Tanzania Assemblies of God (35)

Turney, Mark, MA. Mishenari wa AGWM; Rais, Kitivo cha Theolojia cha Assemblies of God, Lomé, Togo (19)

Watt, C. Peter, ThD. Mwenyekiti, Assemblies of God, Afrika Kusini (31)

*Orodha ya Wachangia Mada*

# Utangulizi wa Randel Tarr

*Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste* utatumika kama nyenzo muhimu kwa wachungaji wa Kiafrika kwa miaka mingi ijayo. Kanisa Barani Afrika kwa muda mrefu limekuwa likihitaji rasilimali hiyo, inayoshughulikia changamoto za kipekee zinazowakabili wachungaji wa Kipentekoste Barani Afrika.

Katika hiki kitabu, Dkt. Denzil R. Miller na wahariri wenzake, Dkt. Jeffery Nelson na Todd Churchill, wamekusanya viongozi wa Kiafrika kushughulikia masuala mengi yanayowakabili wachungaji wa Kipentekoste barani Afrika leo. Kama vile "Orodha ya Wachangia Mada" mbele ya kitabu inavyoonyesha, viongozi hawa ni pamoja na wakuu wa kitaifa wa kanisa, wachungaji wakuu, wasimamizi na walimu wa shule za Biblia na seminari, viongozi wa misheni, wapanda kanisa, wainjilisti, na zaidi.

Uzoefu wa kina na ujuzi wa viongozi hawa huongeza thamani kubwa ya kazi hii. Baada ya kuhudumu na baadhi ya wanaume na wanawake hawa, binafsi naweza kuthibitisha uadilifu wao kama viongozi, shauku yao kwa Kristo na utume Wake, na hamu yao ya kuona Kanisa likipandwa kila pembe ya Afrika. Zaidi ya hayo, timu ya wahariri yenyewe huleta utajiri wa maarifa ya Afrika na watu wake katika mwendelezo wa hiki kitabu. Kila mmoja wao ametumika kama mishenari eneo la Kusini, Mashariki, au Kati ya Afrika kwa miaka mingi.

Kitabu hiki kitaimarisha huduma za wale ambao tayari wanaongoza makanisa ya mahali pamoja kote barani Afrika, pamoja na wale ambao bado wako katika shule ya Biblia na mifumo mingine ya mafunzo enezi wakijitayarisha kwa huduma ya baadaye. Hiki kitabu kimejaa msaada wa kimatendo utakaomsaidia mchungaji wa Kipentekoste kufanikiwa katika huduma na kuzaa matunda yatakayodumu.

Msisitizo mmoja mkubwa sana wa kitabu hiki ni wito kinachotoa kwa mchungaji wa Kipentekoste katika Afrika kuwa mwanamume au mwanamke wa uadilifu. Msisitizo mwingine muhimu ni wito wa mara kwa mara wa kitabu hiki kwa Mchungaji wa Kiafrika kuendelea kujazwa na Roho Mtakatifu na kujikita katika utume wa Kanisa uliotolewa na Mungu wa kuona kwamba kila mwanamume, mwanamke na mtoto barani Afrika anapewa fursa ya kusikia vizuri habari za Yesu Kristo na kumwamini. Katika siku hizi ambazo "injili ya mafanikio" imeyaondoa makanisa mengi sana barani Afrika kwenye utume wa

Mungu na kuyapeleka kwenye kutafuta baraka za kibinafsi, inatia moyo kuona kwamba kitabu hiki kimesimama imara kwenye kuhimiza utume. Wachangiaji wa kitabu hiki ni watendaji wa kweli wa Neno, wanaume na wanawake wa Mungu ambao wanatafuta kuishi kwa kuzingatia Agizo Kuu la Kristo katika maisha yao ya kila siku.

Kwa miongo sita, mimi nimehusishwa na Kanisa Barani Afrika, kwanza nikiwa mtoto niliyekulia Afrika na baadaye kama mishenari huko Afrika Magharibi kwa zaidi ya miaka 35. Inashangaza kuona kile ambacho Mungu amefanya kupitia kazi ya maelfu ya wanaume na wanawake wa Kiafrika ambao wameweka maisha yao wakfu ili kuwavuta kwa Yesu wote waliopotea kwa gharama yoyote. Ninaamini kitabu hiki kitatumika kuongeza ufanisi wao katika huduma. Ombi langu ni kwamba, kitabu hiki kinapotiwa mikononi mwa maelfu ya wachungaji na wanafunzi wa shule za Biblia kote Afrika, ufalme wa Mungu utakuja katika bara hili kwa njia kubwa zaidi.

Kwa kweli, viongozi waliowezeshwa na Roho, na kufundisghwa Biblia sawasawa ndiyo tumaini kwa ajili ya Afrika!

~ Mchungaji Randel Tarr
Mkurugenzi Mtendaji
Taasisi ya Africa’s Hope

# Utangulizi wa Dkt. Barnabas Mtokambali

Wachungaji wengi wa Kipentekoste barani Afrika wanaweza kujitambulisha na hisia za Paulo alipowaandikia waamini wa Korintho, kama ifuatavyo:

> "Nimekuwa nikihama mara kwa mara. Nimekuwa hatarini…nimetaabika mno na kusumbuka, na mara nyingi nimekosa usingizi; Nimejua njaa na kiu na mara nyingi nimekosa chakula; Nimepigwa na baridi na kuwa uchi. Zaidi ya hayo yote, kila siku nakabiliana na mahangaiko kwa ajili ya makanisa yote." (2 Kor. 11:26-28)

Ingawa hali zao mmoja mmoja zinaweza kutofautiana na jinsi Paulo alivyokuwa, wachungaji wengi wa Kipentekoste barani Afrika wanaweza kumwunga mkono katika hisia zake za "kusongwa kila upande" (4:8).

Hakuna wito wenye changamoto sana kama kuchunga kanisa la Kipentekoste barani Afrika. Hebu fikiri maeneo mengi maishani na katika huduma ambayo mchungaji wa Kipentekoste lazima aonyeshe umahiri wake. Ni lazima awe na uwezo wa kutunza kundi la Mungu ifaavyo, na huku akiweza pia kusimamia mambo ya kibinafsi na ya familia. Ni lazima awe mhubiri hodari, mwalimu, mshauri, na msimamizi – na vyote hivyo kwa wakati mmoja. Na wakati wote huo, lazima aweze kuongoza kanisa lake katika kutimiza agizo la Bwana wetu la kufanya wanafunzi kutoka mataifa yote. Orodha inaweza kuendelea. Ndiyo maana kutokea kwa mwongozo huu wa mchungaji wa Kipentekoste ni kitu cha kukaribishwa kabisa, tena kwa mikono miwili.

Kwa muda mrefu nimeona haja ya mwongozo wa kina wa mchungaji ulioandikwa kutoka mtazamo wa Kiafrika na wa Kipentekoste. Ninashukuru sana kwa kazi iliyofanywa na Africa's Hope kutoa kitabu hiki. Kinachotia moyo hasa ni kwamba mwongozo huu umeandikwa na wachungaji na viongozi wa Kipentekoste waliokomaa kutoka katika bara zima. Wakati huo huo, uko sahihi kitheolojia, unalenga umisheni, na unafaa kivitendo. Mwongozo huu unawapa wachungaji wa Kipentekoste maarifa mengi ya thamani katika maisha na huduma ya Kipentekoste. Utasaidia kuwaongoza wachungaji wa Kipentekoste barani Afrika katika huduma yenye tija zaidi. Na mikono ya wachungaji wetu ikiimarika, makanisa wanayoyaongoza yataimarika pia.

Natarajia kwamba *Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste* utakuwa na manufaa hasa wakati huu wa mkazo wa “Miaka Kumi ya Uamsho” wa Umoja wa Makanisa ya Assemblies of God Afrika (AAGA) kuanzia 2021 hadi 2030. Katika miaka hii kumi, makanisa ya Assemblies of God kote barani Afrika yamejitolea kumtafuta Mungu ili kumiminiwa nguvu ya Mungu Roho Mtakatifu, na kusababisha uamsho mkuu zaidi kuwahi kuonekana katika Afrika, na kuwawezesha waamini kupeleka injili kwa kila kabila, taifa, na watu kabla ya ujio wa Kristo, anayekuja upesi.

Katika kipindi hiki cha Miaka Kumi ya Uamsho, makanisa ya Assemblies of God yatazingatia kutiwa nguvu za Roho Mtakatifu, maisha ya utauwa na uchaji wa Mungu, mafunzo ya uanafunzi, uinjilisti, upandaji makanisa, na umishenari unaovuka mipaka ya kitamaduni baina ya watu ambao hawajfikiwa barani humu - haswa maeneo ya Afrika Kaskazini na Pembe ya Afrika. Ninaamini kuwa *Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste* utatumika kama chombo cha thamani sana, kusaidia wachungaji kuongoza makanisa yao kutimiza utume huu mkuu. Kisha, ikiwa Bwana Yesu atachelewa kurudi, kitabu hiki kitaendelea kufanya kazi katika kanisa la Kipentekoste barani Afrika kwa miaka mingi ijayo.

Ninapendekeza kitabu hiki kwa wachungaji na wahudumu wa Kipentekoste kote Afrika.

~ Dkt. Barnabas Mtokambali
Mwenyekiti
Africa Assemblies of God Alliance

# Maneno ya Mwanzo

Kiongozi mmoja Mwafrika, baada ya kuona jinsi kanisa la Afrika linavyokua, alisema hivi: "Mungu analibariki kanisa la Afrika ili liwe baraka kwa mataifa!" Sisi tunakubaliana kwa moyo wote na maoni haya. Tunaamini kwamba Mungu ameliita kanisa la Kiafrika liujie Ufalme kwa wakati kama huu (taz. Est. 4:14). Kanisa la Kipentekoste barani Afrika lina hatima kuu ya kitume. Katika siku hizi za mwisho wa nyakati, Bwana wa Mavuno anamimina Roho Wake juu ya watu Wake ili kuwatia nguvu kushiriki kikamilifu katika kutimiza Agizo Lake Kuu kabla hajarudi kutoka mbinguni (Mt. 24:14; Mdo. 1:8-11).

Ili kufanya hivyo, kanisa la Kiafrika litahitaji kuwa na nguvu. Na ili kuwa na nguvu, lazima kuwa na uongozi thabiti. Kitabu hiki cha *Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste* kimeandaliwa ili kushughulikia hitaji hili. Kimekusudiwa kuwaandaa wachungaji wa Kipentekoste katika Afrika kufanya sehemu yao katika kutimiza kusudi la Mungu kwa kanisa. Matumaini yetu ya dhati ni kwamba kitabu hiki kitakuwa chombo na hazina mikononi mwa wachungaji wa Kipentekoste katika bara zima. Kimetengenezwa kwa kuzingatia kanuni sita elekezi:

*1. Kina mtazamo wa Kibiblia.* Waandishi na waandaaji wa mwongozo huu wanaamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililofunuliwa kwa wanadamu. Ni mwongozo wa Mkristo unaotosha kwa maisha na utume. Kwa hiyo, watengenezaji wa kitabu wametafuta kuweka msingi wa Kimaandiko kwenye kila dhana.

*2. Kina msisitizo wa Kipentekoste.* Kitabu kimeandikwa na wachungaji wa Kipentekoste kwa ajili ya wachungaji wa Kipentekoste. Kinatafuta kushughulikia maswala ya kipekee ya wachungaji wa Kipentekoste kutoka katika mtazamo wa Kipentekoste. Kila mchangiaji katika kitabu hiki ni kiongozi wa Kipentekoste aliyekomaa na mwenye huduma iliyothibitishwa. Kwa sababu ya uzoefu wao katika kutembea na Roho, na ufahamu wao wa Maandiko, wapendwa hawa wanakumbatia njia ya kipekee ya Kipentekoste ya maisha na huduma. Jambo hilo linaonekana katika kitabu kizima.

*3. Kina lengo la utume.* Watengenezaji wa mwongozo huu wanaamini kwamba Kristo ameagiza kila mchungaji wa Kipentekoste na kila kanisa kushiriki

kikamilifu katika utume wa Mungu. Utume wa Mungu ni kuwakomboa na kuwaita kwake watu kutoka katika kila kabila, lugha, na taifa duniani kabla ya kurudi kwa Yesu mara ya pili (Mt. 24:14; Uf. 5:9). Kristo alitoa kwa ufupi utume wa Mungu katika Agizo Lake Kuu (Mt. 28:18-20; Mk. 16:15-17; Lk. 24:47-49; Yoh. 20:21-22; Mdo. 1:8). Msisitizo huu wa utume unafafanuliwa sana katika kitabu chote.

*4. Kina mwelekeo wa Kiafrika.* Mlengwa wa hiki kitabu ni mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika. Waandishi wanaelewa kwamba wachungaji wa Kiafrika hutekeleza huduma zao katika mazingira ya kipekee ya Kiafrika, na wanafanya hivyo kwa changamoto na mahangaiko ya kipekee ya Kiafrika. Kila sura imeandikwa kwa kuzingatia mazingira hayo.

*5. Kina upeo mpana.* Kitabu hiki kimeandaliwa kushughulikia masuala mbalimbali yanayowakabili wachungaji wa Kipentekoste leo katika bara la Afrika. Waliokiandaa wanatumaini kwamba kitakuwa rasilimali inayohitajika mikononi mwa wachungaji barani kote.

*6. Ni cha vitendo katika matumizi yake.* Ingawa mwongozo huu unaangazia masuala ya theolojia na mafundisho ya kichungaji, masomo yanayofundishwa humu yametayarishwa yafanyiwe kazi. Yanashughulikia sio tu kile ambacho mchungaji wa Kipentekoste lazima afanye, na kwa nini afanye, bali pia jinsi wanavyoweza kutekeleza huduma zao kwa ufanisi.

**Mchakato wa Kuandika**

Maono ya kuwepo kwa huu *Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste* kwa mara ya kwanza yalikuwa katika moyo wa Dkt. John Easter, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa Africa's Hope. Akaunda kikosi kazi kwa ajili ya kutoa mwongozo huu. Wakati Dkt. Easter alipo-ondoka, alifuatwa na Randy Tarr, mkurugenzi mpya wa taasisi hii, ambaye aliupokea mradi huo kwa moyo wote.

Kazi ya kwanza ya kamati ilikuwa kuandaa orodha kamili ya mada ambazo zingeshughulikiwa na kitabu chenyewe. Hili lilikuwa ni jukumu kubwa lililohusisha utafiti wa kina na masaa mengi ya majadiliano. Orodha ya mada ilihakikiwa tena na viongozi wakuu wa Kiafrika na waelimishaji kutoka kote barani Afrika. Mwishoni, mada arobaini na mbili zilizokuwa sura za kitabu hiki zilichaguliwa. Baada ya vichwa vya sura husika kupitishwa, halmashauri iliziweka katika vikundi kumi, ambavyo vilikuja kuwa sehemu kumi za hiki kitabu.

Baada ya kuamua ni mada gani zingeshughulikiwa, na mahali pake kitabuni, kamati ilichagua wachungaji wakuu wa Assemblies of God, waelimishaji, na

viongozi wa makanisa kutoka kote barani Afrika ili kuandika sura moja moja. Wamishenari wachache wa Kimarekani waliowahi kuishi na kuhudumu kwa muda mrefu barani Afrika pia walikaribishwa kuchangia. Majina ya waandishi hawa, pamoja na maelezo mafupi juu ya kila mmoja wao yanaonekana katika sehemu ya "Orodha ya Wachangia Mada" mwanzoni mwa kitabu hiki.

Mara baada ya mwandishi kumaliza kazi yake, aliwasilisha kazi yake kwa kamati kwa ajili ya tathmini na uhariri. Kisha kamati ilichunguza kila sura kwa maudhui na uhusiano na sura zingine. Lengo lao lilikuwa ni kuhakikisha kwamba kila sura inachangia dhamira ya Kipentekoste na ya kitume ya kitabu, na kuhakikisha kwamba mtindo wa uandishi unafanana katika kazi yote. Baada ya mchakato wa uhariri kukamilika, sura husika iliingizwa kwenye kitabu.

## Wanawake Katika Huduma

Tangu kuanzishwa kwake, Jumuiya ya Kipentekoste imethamini nafasi ya wanawake katika huduma. Wapentekoste wanaamini kwamba Roho yule yule anayewastahilisha wanaume kwa ajili ya huduma pia anawastahilisha wanawake. Imani yao imejengwa juu ya ahadi ya Yesu katika Matendo 1:8, ambapo anaahidi Roho Mtakatifu kwa waamini wote, wanaume na wanawake. Kila mtu anayepokea Roho, pamoja na wanawake, hupokea nguvu za kumshuhudia Kristo. Ushahidi huu unahusisha kutangaza Injili.

Wapentekoste pia wanataja ahadi ya nabii Yoeli iliyonukuliwa na Petro Siku ya Pentekoste: "Siku za mwisho, asema Mungu, nitamimina Roho yangu juu ya watu wote. Wana wenu na binti zenu watatabiri…. Hata juu ya watumishi wangu, *wanaume kwa wanawake*, nitamimina Roho yangu siku zile, nao watatabiri" (Mdo. 2:17-18, maneno mepesi kukazia; taz. Yoe. 2:28-29). Wapentekoste wanachukulia kauli hii kama kanuni ya ulimwengu wote ya kuaminiwa na kufanyiwa kazi katika kipindi hiki cha "Enzi ya Roho" wakati Mungu anapomimina Roho Wake kwa neema juu ya watu wote.

## Jinsi ya Kutumia Kitabu Hiki

Kama jina lake linavyodokeza, kitabu hiki kimeandaliwa kuwa mwongozo, au kitabu chenye kuongoza utendaji wa wachungaji wa Kipentekoste katika Afrika. Unaweza kutumia kitabu hicho kwa njia kadhaa zinazofaa. Itafaa ukisome kitabu hiki hadi mwisho kwa kuanzia. Zoezi hili litakupa muhtasari mpana wa dhana zilizojadiliwa katika kitabu. Pia utasaidika kupata ufahamu mpana kwa pande zote kuhusu kazi ya kimsingi ya mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika.

Unaposoma hiki kitabu, weka kalamu na daftari karibu ili uweze kuandika maarifa yatakayokugusa na yanayoweza kutumika hasa kwa maisha na huduma yako mwenyewe. Pia ni vizuri kuandika mawazo yako binafsi juu ya mada hiyo. Tambua maboresho fulani unayopaswa kufanya katika jinsi unavyofanya huduma kwa sasa. Hatimaye, na muhimu zaidi, unaposoma, isikilize sauti ya Roho, ukizingatia kile anachokuambia. Halafu, tumia daftari lako kama mwongozo wa maombi na kama ramani au dira kwa ajili ya maendeleo ya kibinafsi na ya kihuduma.

Unaweza pia kutumia mwongozo huu kama kitabu cha rejea. Wakati tukio maalum linapotokea kama vile arusi, mazishi, ushauri nasaha, mkutano wa uongozi, au tukio lingine, unaweza kukipitia katika sura husika ili kupata maarifa mapya na miongozo muhimu. Au unapotafuta usaidizi wa kusuluhisha tatizo kubwa au kukaribia kazi mpya ya watumishi na idara, tazama Yaliyomo ili upate sura zinazozungumzia suala hilo.

Mwisho: kitabu hiki kinaweza kutumiwa na waalimu katika vyuo vya Biblia na seminari kama kitabu cha kiada au cha ziada katika darasa la huduma za kichungaji. Kitabu hiki kinaweza kusaidia hasa katika shule za muda mfupi kama vile shule enezi au za kupanda makanisa.

Sisi, kamati ya usimamizi ya *Mwongozo wa Mchungaji Mpentekoste* tunatoa pongezi nyingi kwa wachungaji wa Kipentekoste barani Afrika. Ni maombi yetu ya dhati kwamba Mungu atakitumia kuwabariki wachungaji wa Kiafrika kwa miongo mingi ijayo, na kwamba kitabu hiki kitatumika kama chombo muhimu katika kuendeleza ufalme wa Mungu barani Afrika, na dunia nzima kwa ujumla kupitia kanisa la Afrika.

Tunakitoa kwa heshima zote,

~ Dkt. Denzil R. Miller, mhariri
~ Dkt. Jeffery Nelson, mhariri mwenza
~ Mchungaji Todd Churchill, mhariri mwenza

~ Sehemu ya 1 ~

# Sifa za Mchungaji wa Kipentekoste

~ Sura ya 1 ~

# Mtu wa Uzoefu

Hebu fikiri kuhusu mwanamume aliyesomea udaktari katika chuo kikuu maarufu. Alihudhuria mihadhara kuhusu upasuaji na kusoma vitabu bora zaidi juu ya mada hiyo. Walakini, hakuwahi kumfanyia mtu yeyote upasuaji. Je, ungependa mtu huyu akufanyie upasuaji? Bila shaka hapana. Ikiwa mtu atatamani kuwa daktari-mpasuaji, lazima apate uzoefu wa vitendo kwa kufanya upasuaji mara nyingi sana chini ya usimamizi wa daktari wa upasuaji mwenye ujuzi.

Vivyo hivyo, kabla ya mtu kuingia katika huduma ya uchungaji, lazima apate uzoefu. Uzoefu huu lazima uwe wa kiroho na wa vitendo. Katika sura hii, tutachunguza uzoefu unaohitajika kwa yeyote anayetaka kuwa mchungaji wa Kipentekoste.

## UZOEFU WA KIROHO

Kumjua Mungu ndio sehemu muhimu ya kuanzia kwa mchungaji yeyote wa Kipentekoste. Zaidi ya yote, lazima awe na uhusiano na Kristo, wa kina na wa kibinafsi. Yesu alipowachagua wale Kumi na Wawili, alifanya hivyo “ili wawe pamoja naye” (Mk. 3:14). Alijua kwamba, walipokuwa wakitembea na kuzungumza naye, wangezidi kuwa kama Yeye. Yesu alisema, “Kila mtu akiisha kuzoezwa kabisa atakuwa kama mwalimu wake” (Lk. 6:40). Ni vivyo hivyo kwetu leo. Tunapotumia muda pamoja na Kristo katika Neno Lake na katika maombi,

tunazidi kuwa kama Yeye (2 Kor. 3:18). Kabla ya kumtumikia Yeye , ni lazima tufanane Naye , na ili tufanane Naye, ni lazima tuwe na muda pamoja Naye.

Vuguvugu la Kipentekoste lilitokana na imani kwamba waamini leo wanaweza kuwa na uzoefu wa kiroho wa kubadilisha maisha kama ilivyokuwa kwa mitume na wanafunzi wengine katika Agano Jipya. Wapentekoste wanafundisha kwamba, ingawa mafundisho sahihi ni muhimu, hayatoshi. Zaidi ya kitu kingine chochote, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe na uhusiano endelevu na Yesu Kristo. Bila uhusiano kama huo, hutafaa kwenye huduma. Uhusiano huu unatokana na uzoefu wa kiroho.

Katika Biblia yote, wale waliowahudumia wengine walianza safari yao kwa kukutana na Mungu. Ibrahimu alisikia sauti ya Mungu (Mwa. 12:1-3). Musa alikutana na Mungu kwenye kijiti kilichowaka moto (Kut. 3:1-4). Isaya alimwona Mungu katika hekalu, akiwa juu sana na aliyeinuliwa (Isa. 6:1-5). Wanafunzi walitembea pamoja na Yesu (Mk. 3:13-14). Na Paulo alikutana na Kristo mfufuka akiwa njiani kwenda Dameski (Mdo. 9:15).

Vivyo hivyo, kila mtu anayetaka kuwa mchungaji wa Kipentekoste lazima awe amekutana na Mungu katika maeneo manne muhimu:

**Kuzaliwa Upya**

Nikodemu alikuwa kiongozi wa kidini. Alikuwa Farisayo mcha Mungu na mjumbe wa baraza tawala la Wayahudi. Hata hivyo, katika hayo bado haikutosha. Yesu alimwambia Nikodemo, “Lazima uzaliwe mara ya pili” (Yoh. 3:7). Yesu alimwambia kwamba hangeweza “kuingia,” au hata “kuona” ufalme wa Mungu mpaka awe amezaliwa upya kwa njia ya Roho (mst. 3-5).

Kila mchungaji wa Kipentekoste lazima azaliwe mara ya pili hasa. Ni lazima aweze kushuhudia kwamba, katika maisha yake, kuna wakati alipokutana na Yesu, akatubu dhambi zake, na kumpokea kama Bwana na Mwokozi wake. Wakati huo, Yesu alichukua nafasi stahiki kwenye kiti cha enzi cha maisha yake, na akafanywa upya. Paulo aliandika, “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya. Ya kale yamepita, mapya yamefika!” (2 Kor. 5:17, maelezo ya pembeni).

Je, umezaliwa mara ya pili? Je, jinsi ulivyo umebadilika toka ndani hadi nje? Kama bado, inawezekana kutokea sasa hivi. Geuka kutoka kwa dhambi zako na umwombe Mungu akusamehe. Weka tumaini lako kamili katika Kristo pekee kwa ajili ya wokovu, na umkaribishe ashike nafasi yake inayomstahili kama Bwana wa

maisha yako. Ili kumpokea Kristo kama Mwokozi wako, amini kwa moyo wako wote, na uombe sala ifuatayo kwa dhati:

"Yesu, ninaamini kweli kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, Mwokozi wa ulimwengu. Ninaamini kwamba ulikufa kwa ajili ya dhambi zangu na ukafufuka tena. Ninajua mimi ni mwenye dhambi, na nimepotea milele kama sitakuamini. Naomba nisamehe dhambi zangu na uwe Mwokozi na Bwana wa maisha yangu. Sasa ninaacha yote kukufuata Wewe. Nitakutumikia siku zote za maisha yangu. Ingia moyoni mwangu na uwe Bwana wa maisha yangu. Kwa jina lako nimeomba. Amina."

### Ubatizo Katika Roho Mtakatifu

Muda mfupi kabla ya Yesu kupaa mbinguni, aliwaamuru wanafunzi Wake kwamba, "Kaeni humu mjini hata mvikwe uwezo utokao juu" (Lk. 24:19). Walitakiwa kungoja Yerusalemu hadi watakapobatizwa kwa Roho Mtakatifu (Mdo. 1:4). Ndugu hawa walikuwa wamezaliwa mara ya pili. Walikuwa wamepokea mafundisho ya Yesu, na walikuwa wameshuhudia miujiza yake. Alikuwa amewaagiza kuhubiri injili katika ulimwengu wote. Na bado hawakuwa tayari.

Kazi ambayo Yesu aliwapa ilikuwa kubwa sana wasiweze kuifanya kwa nguvu zao wenyewe. Walihitaji kujazwa na nguvu za Mungu. Yesu aliwaahidi, "Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Mdo. 1:8).

Roho alikuja juu ya wanafunzi mara ya kwanza Siku ya Pentekoste, na kuwajaza. Wakati huo, walinena kwa lugha na kupokea nguvu na ujasiri waliohitaji ili kumtangaza Kristo kwa ufanisi, hata katika upinzani mkali. Yeyote anayetamani kumfuata Bwana katika huduma anapaswa kubatizwa katika Roho Mtakatifu.

Yesu alituambia jinsi tunavyoweza kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Aliahidi hivi, "Baba wa Mbinguni [atawapa] Roho Mtakatifu wale wamwombao!" (Lk. 11:13). Mtu yeyote anaweza kupokea nguvu za Roho kwa kuomba tu kwa imani. Huku kuomba kuna hatua tatu rahisi tu za imani:

*1. Omba kwa imani.* Anza kwa kumwomba Mungu akupe Roho Wake. Akizungumzia karama ya Roho, Yesu aliahidi na kusema, "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; pigeni hodi, nanyi mtafunguliwa" (Lk. 11:9).

Unapo-omba, amini kwamba Mungu anasikia na atajibu, na kwamba wakati huu huu, anakujaza na Roho Mtakatifu. Weka wazi moyo wako kwa Mungu, na usikie Roho akija juu yako. Unapomsikia Roho juu yako, uko tayari kuchukua hatua ya pili ya imani.

*2. Pokea kwa imani.* Tena, Yesu aliahidi hivi: "Kila aombaye hupokea" (Lk. 11:10). Katika tukio lingine alifundisha, "Lolote mtakaloomba katika sala, aminini kwamba mnalipokea, nalo litakuwa lenu" (Mk. 11:24). Amini kwamba Mungu anajibu maombi yako na kukujaza na Roho Mtakatifu. Unapofanya hivyo, jisikie uwepo wa Roho ndani yako, katika utu wako wa ndani (Yoh. 7:38). Hiyo ikitokea, chukua hatua yako ya tatu ya imani.

*3. Nena kwa imani.* Biblia inasema kwamba siku ya Pentekoste "wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine kama Roho alivyowajalia kutamka" (Mdo. 2:4. Maneno mepesi kukazia). Maneno utakayozungumza hayatakuwa yako mwenyewe; yatatoka kwa Mungu. Yatatoka ndani kabisa, kutoka rohoni mwako (1 Kor. 14:2). Na yatakuwa katika lugha usiyoifahamu. Hii ni ishara ya Mungu kwako na kwa kanisa kwamba, amekupa uwezo wa kunena kwa ajili yake. Bwana asifiwe! Umebatizwa kwa Roho Mtakatifu.

**Wito wa Kimungu**

Kuwa mchungaji wa Kipentekoste ni zaidi ya chaguo la kazi; ni wito kutoka kwa Mungu. Akisema habari za Yesu, Paulo aliandika hivi, "Yeye ndiye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu" (Efe. 4:11). Pamoja na majukumu mengine manne ya huduma, wachungaji ni zawadi iliyotolewa na Kristo kwa Kanisa Lake. Bwana mwenyewe huchagua atakayemteua kuwa mchungaji. Anachagua, Anaita, kisha Anaweka kazini. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kumi na wawili, "Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi na kuwaweka muende mkazae matunda, matunda yadumuyo" (Yoh. 15:16).

Hivyo Bwana alifunua kweli tatu muhimu kuhusu mwito wa Mungu: Kwanza, alifunua kwamba ni Mungu peke yake anayefanya uchaguzi. Mchungaji halisi wa Kipentekoste hajichagui mwenyewe. Yeye amechaguliwa na Kristo. Yesu alifafanua zaidi kwamba Yeye ndiye anayegawa kazi za huduma. Akaendelea kusema, "Nilikuchagua, nami nimekuweka." Kristo hachagui tu ni nani atakayehudumu, vile vile "anaandika maelezo ya kazi" na kuwapa wafanyikazi watimize hizo kazi.

Hatimaye, wale anaowachagua na kuwateua, anawapeleka. Yesu alimalizia usemi Wake namna hii: “[Mimi] nimewaweka muende mkazae matunda.” Yeye ndiye Bwana wa Mavuno, na ndiye anayetuamuru kwamba: “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa viumbe vyote” (Mk. 16:15). Kwa maneno mengine, wachungaji wa kweli wa Kipentekoste hawajajichagua wenyewe, kujiweka wenyewe, wala hawajajituma. Badala yake, wamechaguliwa na Mungu, wameteuliwa na Mungu, na wametumwa na Mungu. Sehemu yetu ni kusikia sauti yake, kujisalimisha kwa mamlaka yake, na kutii wito wake.

Wito wa Mungu unaweza kuja kwa njia mbalimbali. Unaweza kuja kwa wazi sana, kama ambavyo ilikuwa kwa Samweli. Yeye alimsikia Mungu akiliita jina lake (1 Sam. 3:1-11). Lakini mara nyingi zaidi wito wa Mungu huja kama hisia ya upole ndani katika utu wa mtu. Ndivyo ilivyokuwa kwa Eliya. Nabii huyo hakusikia sauti ya Mungu katika upepo wenye nguvu, tetemeko la ardhi, au moto. Ila alisikia sauti ya Mungu kama “sauti ndogo, nyororo, ya upole” (1 Wafalme 19:12).

Ushawishi huu wa upole mara nyingi huambatana na "ufahamu wa ndani" kwamba Mungu anazungumza. Baada ya muda, hupata nguvu, na kusababisha mtu kujisikia kwamba ni kitu cha haraka kinachotakiwa. Bila shaka Yesu akiwa mdogo alihisi hivyo alipowaambia wazazi wake, “Ilinipasa kuwa katika nyumba ya Baba yangu” (Lk. 2:49). Paulo alionyesha huo uharaka wa ndani kwa Wakorintho, alipowaandikia hivi: “Kwa maana nimewekewa sharti. Ole wangu nisipoihubiri Injili!” (1 Kor. 9:16). Nabii Mika alielezea hiyo imani yake ya ndani kutoka kwa Mungu: “Lakini mimi, nimejaa nguvu, na Roho ya Bwana, na haki na uweza, ili kumtangazia Yakobo kosa lake, na Israeli dhambi yake” (Mika 3:8).

Tunapoitikia kwa imani na utii sauti ya Roho, kusadiki huko hukua hadi tunajua kwa hakika kwamba Mungu ametuita kuyatoa maisha yetu kutangaza injili.

**Uhusiano Ulio Hai**

Mwisho: mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na uhusiano endelevu, ulio hai, kati yake na Mungu. Uzoefu na Mungu haupaswi kufikiriwa kuwa tukio la mara moja tu. Kitu cha mara moja, hata kikiwa cha ajabu kiasi gani, hakiwezi kudumisha maisha ya Kikristo. Hata wanafunzi wa kwanza, waliopokea Roho Siku ya Pentekoste, walihitaji kujazwa tena na tena (Mdo. 4:8, 31; 5:8).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujifunze kudumisha mwendo endelevu, wa kibinafsi, na Mungu wako. Paulo aliwaandikia hivi Wakristo wapya huko Galatia: "Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho" (Gal. 2:25). Katika barua hiyohiyo, aliwakemea na kusema, "Je, ninyi ni wapumbavu hivi? Baada ya kuanza kwa Roho, sasa mnajaribu kumaliza katika mwili?" (Gal. 3:2). Haitoshi kuwa umejazwa na Roho mara moja tu, lazima ubaki "umejaa Roho" (Lk. 4:1; Mdo. 6:3; 7:55; 11:24).

Yesu alielezea uhusiano huo kama kukaa, au kukaa ndani yake (Yoh. 15:4). Kukaa ndani ya Kristo kunahusisha kuishi katika Neno Lake na katika upendo Wake (mst. 7, 9). Pia huhusisha kushika amri zake (mst. 10) na kuishi katika Roho (1 Yoh. 2:27; 4:13).

## UZOEFU WA VITENDO

Kuna ujuzi ambao huwezi kujifunza katika vitabu. Mtu anaweza kusoma makala ya gazeti kuhusu jinsi ya kuogelea lakini, atakuwa mpumbavu kuingia kwenye maji marefu kabla ya kufanya mazoezi ya kuogelea kwa muda wa kutosha. Ndivyo ilivyo kwa huduma ya Kipentekoste. Kama ilivyo, hakuna kiasi cha masomo ya kitaaluma kinachoweza kukutayarisha vya kutosha kwa huduma ya kichungaji. Kabla ya kuingia katika huduma lazima upate uzoefu wa vitendo. Unaweza tu kupata uzoefu kama huo kwa kushiriki katika huduma ya vitendo.

Katika shule moja ya Biblia Kusini mwa Afrika, wanaotazamiwa kuwa wanafunzi wanatakiwa kutuma "Ombi la Kuandikishwa." Uongozi hutumia yaliyopatikana kutoka fomu hiyo ili kusaidia kubainisha kufaa kwa mwombaji kuandikishwa shuleni. Pamoja na maswali ya kawaida ya kibinafsi na ya kitaaluma, mwombaji anaulizwa kuandika ushuhuda wake binafsi. Katika ushuhuda huu, mwombaji anaombwa kuelezea mambo manne: (1) jinsi alivyofikia kumjua Kristo kama Mwokozi; (2) alivyobatizwa katika Roho Mtakatifu na matokeo yake katika maisha yake; (3) jinsi alivyoitwa katika huduma; na (4) jinsi ambavyo amekuwa akifanya huduma katika kanisa lake la mahali pamoja.

Msimamizi wa shule alieleza, "Tunauliza swali la mwisho kwa sababu tunaamini kwamba uzoefu wa vitendo ni sehemu muhimu ya mafunzo ya huduma yenye matokeo. Hapa shuleni kwetu, hatufundishi kuhusu huduma, tunafundisha kwa kufanya huduma." Ingawa mafunzo rasmi ni muhimu, hayo tu hayatakutayarisha kwa huduma ya kichungaji. Lazima upate uzoefu wa vitendo kwa kushiriki kikamilifu katika huduma.

Hutakuwa na busara sana kujaribu kuongoza kusanyiko kama mchungaji hadi upate uzoefu wa vitendo. Unaweza kupata uzoefu kama huo katika kanisa la mahali pamoja chini ya uongozi wa mchungaji aliyekomaa, aliyejazwa na Roho. Paulo alimwambia Timotheo kwamba mwangalizi, au mchungaji, "hapaswi kuwa aliyeongoka hivi karibuni" (1 Tim. 3:6). Aliongeza kwamba mchungaji lazima awe na "sifa nzuri kwa watu wa nje" (mst. 7). Maeneo manne muhimu kuhusu uzoefu wa vitendo katika huduma ni haya yafuatayo: katika kushuhudia, katika kuhubiri na kufundisha, katika kutoa, na katika sala.

### Uzoefu Katika Kushuhudia

Kwanza: katika kujiandaa kwa huduma ya kichungaji, lazima upate uzoefu wa kushuhudia. Lazima uwe stadi wa kuwashirikisha wengine Injili. Ushuhudiaji wa aina hiyo ni matokeo ya kawaida ya wewe kubatizwa katika Roho Mtakatifu, kama tulivyoona hapo juu. Akizungumza juu yake mwenyewe, Yesu alisema kwamba mchungaji "huwatangulia [kondoo wake], na kondoo wake humfuata" (Yoh. 10:4). Inatakiwa hivyo hivyo kwako wewe kama mchungaji wa Kipentekoste. Iwapo utatangulia mbele ya kondoo wako kuleta roho za watu kwa Kristo, wao watakufuata. Lakini ukishindwa, nao watashindwa pia.

Wajibu mmoja wa mchungaji yeyote wa Kipentekoste ni kuongoza kusanyiko lake kuanzisha makanisa mapya mahali ambapo hakuna kanisa la kitume lenye kuwezeshwa na Roho. Kwa hiyo ni muhimu uwe umeshiriki katika shughuli moja au zaidi za upandaji kanisa kabla hujashika uongozi wa kusanyiko la mahali pamoja. Hii inaweza kuwa shughuli ya kanisa lako la nyumbani, shule ya Biblia uliyosoma, au huduma nyingine. Uzoefu huu wa vitendo utakusaidia kujua jinsi ya kuhamasisha kanisa lako mwenyewe kuanzisha makanisa mengine.[1]

### Uzoefu Katika Kuhubiri na Kufundisha

Zaidi ya hayo, yeyote anayelenga kuwa mchungaji wa Kipentekoste lazima apate uzoefu katika kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu. Kwani mtu anawezaje kuliongoza vyema kanisa la Kipentekoste ikiwa hana ujuzi wa kuwasilisha Neno la Mungu kwa wengine? Paulo alimkumbusha Timotheo kwamba mchungaji

[1] Masuala haya yamejadiliwa kwa undani zaidi katika Sura ya 37: "Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti" na Sura ya 39: "Kupanda Makanisa Mapya."

lazima "aweze kufundisha" (1 Tim. 3:2). Alizidi kumwonya mwanawe katika imani kuwa tayari kuhubiri neno wakati wowote (2 Tim. 4:2).

Njia moja ya kupata uzoefu wa kufundisha na kuhubiri ni kujitolea kufundisha Darasa La Jumapili au Darasa La Kujifunza Biblia katika kanisa lako la nyumbani. Njia nyingine ni kuongoza kikundi cha nyumba kwa nyumba. Kwa njia hizi, ukiwa chini ya mchungaji wako, unaweza kujizoeza kutayarisha na kutoa mahubiri ya kiBiblia. Njia nyingine nzuri ya kupata uzoefu wa kuhubiri ni kuhubiri nje. Unaweza kufanya hivi kwa kupanga kikundi cha washirika waaminifu wa kanisa na kwenda masokoni na sehemu zingine zenye watu wengi karibu na kanisa lako ili kufanya huduma za uinjilisti wa nje hadharani.[2]

**Uzoefu Katika Utoaji**

Tatu: Mtu anayetaka kuwa mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na historia ya kutoa zaka kwa uaminifu na kutoa kwa ukarimu kwa ajili ya kazi ya Mungu. Mtu mbahili, mwenye mikono 'birika' iliyojifunga hawezi kamwe kumwakilisha Mungu mkarimu, mwenye mikono wazi. Yesu aliwatia moyo wanafunzi wake, "Mmepokea bure; toeni bure" (Mt. 10:8). Vivyo hivyo, Paulo aliwaonya waamini wa Korintho, "Fuateni mfano wangu, kama mimi ninavyoufuata mfano wa Kristo" (1 Kor. 11:1). Washiriki wa kanisa wanapotazama ukarimu wako uliojaa imani, wao pia watatiwa moyo kutoa kwa ukarimu kwa kazi ya Mungu, wakimtumaini Yeye kuwatimizia mahitaji yao yote (Flp. 4:19). Matokeo yake, kazi ya Mungu itafanikiwa.

**Uzoefu Katika Maombi**

Mwisho ni kwamba, yule anayetaka kuwa mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na uzoefu wa vitendo katika maombi. Maombi ndiyo msingi wa huduma zote za Kipentekoste. Uzoefu wa mtu katika maombi huanza na maisha ya maombi yenye nidhamu. Biblia inaeleza jinsi ambavyo "Yesu aliondoka mara nyingi kwenda mahali pasipokuwa na watu ili kuomba" (Lk. 5:16). Ili uwe mchungaji mzuri wa Kipentekoste lazima ufanye vivyo hivyo. Lazima ujifunze kutenga muda kila siku kwa ajili ya ushirika na Baba yako wa Mbinguni.[3]

---

[2] Ili kupata ufahamu zaidi kuhusu kuhubiri na kufundisha, tazama Sura ya 16: "Mahubiri Yenye Upako wa Roho" na Sura ya 17: "Kufundisha kwa Ufanisi."

[3] Kwa maelezo zaidi kuhusu maisha ya ibada ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi" na Sura ya 15: "Tabia Imara ya Ibada Binafsi."

Pia utataka kuungana na wengine katika maombi. Unaweza kufanya hivi kwa kushiriki katika vikundi vya maombi, maombi ya kufunga, na mikesha. Kupitia hizo taratibu, utajitayarisha kuwaombea wengine. Maeneo mengine mawili ambayo inabidi kupata uzoefu kwake ni katika kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka ili wapone, na katika kuombea waamini ili wajazwe na Roho Mtakatifu.[4]

[4] Mazoea haya yameelezewa kwa undani zaidi katika Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho" na Sura ya 21: "Kuhudumu Katika Nguvu za Roho."

## ~ Sura ya 2 ~

# Mtu wa Roho

Katika nchi fulani ya Kiafrika, kijana mmoja alijisikia Mungu akimwita. Alimwambia mchungaji wake jinsi alivyokuwa anajisikia. Huyo mchungaji pia alitambua wito wa Mungu juu ya maisha ya kijana huyo, kwa hiyo akamweka kwenye tawi la kanisa hilo katika mji wa karibu. Alimwambia kijana huyo, "Unapaswa kuendeleza kanisa hili na kupanda makanisa mengine katika eneo hili." Akiwa mwenye ari na shauku, kijana huyo alihamisha familia yake hadi mjini na kujiwekea kazi hiyo. Alifanya kazi kwa bidii na alijitahidi sana. Hata hivyo, alikuwa na mafanikio kidogo. Kisha kijana huyo akajiambia, "Ninahitaji ujuzi na mafunzo zaidi." Kwa hiyo akajiandikisha katika shule ya Biblia.

Katika shule ya Biblia, kijana huyo alijifunza Neno la Mungu. Kadiri alivyojifunza ndivyo alivyopata ujasiri zaidi. Pia alijifunza kuhusu tukio la kiBiblia linaloitwa ubatizo katika Roho Mtakatifu. Kijana huyo alimtafuta Roho kwa bidii, na akajazwa haraka, kama ilivyotokea kwa wale wanafunzi 120 Siku ya Pentekoste (Mdo 2:1-4).

Kisha, waalimu wake wakamfundisha jinsi ya kuenenda katika nguvu za Roho. Aliporudi katika kanisa lake, mambo yalibadilika. Sasa alihudumu kwa nguvu na imani. Watu waliponywa na kutolewa pepo, na wengi walikuja kwa Kristo. Kwa hiyo, kanisa likakua na kupata nguvu. Kwa muda mfupi, liliweza

kuanzisha makanisa mengine. Habari hii inaonyesha kwa nini ni muhimu sana kwa kila mchungaji wa Kipentekoste kuwa mwanamume au mwanamke wa kweli wa Roho.

Sura iliyopita ilitazama jinsi mchungaji wa Kipentekoste anavyotakiwa kuwa mtu wa uzoefu kiroho na kivitendo. Sura hii itapanua masuala haya. Itajadili ufahamu wa kimsingi wa mchungaji wa Kipentekoste kuhusu Roho na kazi Yake. Pia itashughulikia mwenendo wake binafsi na huduma katika Roho.

## ANAMWELEWA ROHO

Wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unapaswa kuwa mtu wa Roho kweli kweli. Basi, utahitaji kujua mambo haya manne, yafuatayo:

### Roho Ni Nani

Kwanza, utahitaji kuelewa Roho ni nani. Wakristo wengi sana siku hizi, hata Wapentekoste, hawajui vizuri Roho Mtakatifu ni nani. Wengi wanamwona kama aina ya nguvu fulani, isiyo na utu inayotoka kwa Mungu. Lakini mchungaji wa Kipentekoste lazima aelewe na kufundisha kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu. Yeye ni nafsi ya tatu katika Utatu Mtakatifu (Mt. 28:19; 2 Kor. 13:14). Kama ambavyo Baba ni Mungu, na Mwana ni Mungu, Roho Mtakatifu naye ni Mungu. Kama Mungu, Roho anafikiri (Mdo. 15:28), anazungumza (Mdo. 1:16), anaongoza (Rum. 8:14), na anaweza kuhuzunishwa (Efe. 4:30). Kwa sababu Roho Mtakatifu ni nafsi, kila mfuasi wa Kristo anaweza kuwa na uhusiano Naye, wa kibinafsi (Yoh. 14:16-18; 2 Kor. 13:14).

Tena, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uelewe na kufundisha kwamba Roho Mtakatifu ndiye Roho wa umisheni. Yeye ndiye sehemu ya Utatu ambaye, katika kipindi hiki cha Roho, anatekeleza utume wa Mungu wa ukombozi duniani. Anazidi kuwatia nguvu, kuwahamasisha, na kuwaongoza watu wa Mungu ili waungane Naye katika utume huu (Mdo. 1:8).

### Jinsi Roho Anavyofanya Kazi

Pamoja na kujua Roho Mtakatifu ni nani, lazima ujue jinsi anavyofanya kazi. Roho hufanya kazi katika watu na kupitia kwa watu wenye mzigo wa kufanikisha utume wa Mungu ambao ni Kanisa, ili ufanikiwe hapa duniani. Roho Mtakatifu alimwezesha Yesu kukamilisha kazi yake (Lk. 4:17-19; Mdo. 10:38). Vivyo hivyo, atawawezesha wafuasi wa Yesu kukamilisha kazi yao (Mdo. 1:8; Yoh.

14:12). Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uelewe kwa uwazi na ufundishe kweli hizi kwa nguvu na ushawishi mkubwa.[1]

Ili kufahamu vyema kazi ya Roho katika siku za leo, ni vizuri uelewe mambo makuu matatu ya kiBiblia, kama ifuatavyo:

*1. Utume wa Mungu.* Kwanza, ni lazima uelewe kwamba Biblia inamtambulisha Mungu kama Mungu anayefanya umisheni. Hii wakati mwingine hujulikana kama *missio Dei,* neno la Kilatini kuhusu utume wa Mungu . Utume wa Mungu ni kuwakomboa na kuwaita watu wa kila kabila na lugha na taifa duniani (Uf. 5:9). Kanisa lipo kama chombo cha Mungu cha kutimiza utume wake.

Yesu alijali huo utume wa Mungu alipotoa Agizo Lake Kuu, kwamba: “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru” (Mt. 28:19-20; taz. Mk. 16:15-16; Yoh. 20:21).

Kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima ujitoe kuwafundisha watu wa Mungu kuhusu utume wake. Lazima pia uwafundishe kuhusu jukumu lao katika kutimiza utume huo.

*2. Asili ya kimisheni ya ubatizo wa Roho.* Pamoja na kuelewa utume wa Mungu, kama mchungaji halisi wa Kipentekoste lazima uelewe jukumu muhimu la ubatizo wa Roho katika kutimiza utume. Ni lazima uelewe kwamba Mungu huwabatiza watu wake katika Roho ili kuwawezesha kutimiza utume wake (Lk. 24:49). Yesu alianza huduma yake baada tu ya kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu (Lk. 3:21-23; 4:17-19; Mdo. 10:38). Anatarajia wanafunzi wake wafanye vivyo hivyo hata siku hizi (Mdo. 1:4-8).

*3. Kuhamasisha umisheni.* Pia, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uelewe kwamba katika kuwaongoza watu wako kubatizwa katika Roho, unawatayarisha kwa ajili ya utume unaowezeshwa na Roho. Yesu alipowaagiza wanafunzi wake na kusema, “Kaeni humu mjini hata mvikwe uwezo utokao juu” (Lk. 24:49), alikuwa akiwatayarisha kwa ajili ya utume uliokuwa mbele yao (mst. 47-48). Na Paulo alipowauliza wale wanafunzi kumi na wawili huko Efeso kwamba, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" (Mdo. 19:2), alikuwa

[1] Kwa habari zaidi juu ya mada hii, tazama Sura ya 10: "Husimamia Ukweli wa Kipentekoste" na Sura ya 11: "Hukuza Uzoefu na Matendo ya Kipentekoste."

akiuliza juu ya utayari wao wa kuungana naye katika utume wa kueneza injili Efeso na sehemu nyingine ya Asia Ndogo (mst. 10).

Ni lazima iwe hivyo hata kwetu siku hizi. Ni lazima tuelewe kwamba, kwa kuwaongoza watu wetu katika ubatizo wa Roho, tunawatayarisha kwa ajili ya ushuhuda unaotiwa nguvu na Roho, upandaji kanisa, na umisheni.

**Kutafsiri Kitabu cha Matendo**

Tatu, kama mchungaji halisi wa Kipentekoste barani Afrika, lazima ufahamu asili ya utume na madhumuni ya kitabu cha Matendo. Jambo moja linalowatofautisha Wapentekoste na wasio Wapentekoste ni jinsi kila kundi linavyotafsiri kitabu cha Matendo. Wasio Wapentekoste wanaona kitabu cha Matendo kama hadithi ya zamani kuhusu Kanisa lilivyoanza na kutekeleza utume wake. Katika mawazo yao, kitabu cha Matendo husimulia jinsi Mungu alivyofanya kazi wakati huo na mahali pale, zamani hizo. Lakini, Wapentekoste wanaona kitabu cha Matendo ya Mitume kama kielelezo cha kudumu cha jinsi Mungu anavyotaka kufanya kazi ndani na kupitia Kanisa mahali hapa na sasa, kwa siku hizi.

Mchungaji wa Kipentekoste anaelewa kwamba kitabu cha Matendo ni zaidi ya kitabu cha historia ya zamani. Ni mwongozo wa mkakati uliovuviwa na Mungu kwa ajili ya umisheni katika siku za mwisho. Katika kitabu cha Matendo, Roho Mtakatifu amelipa Kanisa kielelezo, njia, na mkakati wa kukamilisha utume wa Mungu. Mbinu hiyo inaelezwa kwa kifupi katika ahadi ya mwisho ya Yesu kwa Kanisa, anaposema: “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Mdo. 1:8).

Mstari huu unaonyesha mpangilio wa ushuhuda wenye kuwezeshwa ambao umerudiwa katika kitabu chote. Kila kumwagwa kwa Roho katika Matendo kulisababisha ushuhuda uliowezeshwa na Roho. Kufahamu dhana hii ni ufunguo wa wewe kuelewa kitabu cha Matendo na kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya utume unaowezeshwa na Roho.

**Maana ya Kuwa Mpentekoste**

Mwisho: kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe na ufahamu wazi nini maana ya kuwa Mpentekoste. Upentekoste wa kweli ni zaidi ya mtindo mwingine wa kuabudu au mwelekeo wa mambo ya kimbinguni. Mungu aliinua kanisa la Kipentekoste kama vuguvugu la kimishenari la siku za mwisho lililowezeshwa na

Roho. Mchungaji wa kweli wa Kipentekoste amejitolea kufuata mtindo wa huduma uliowekwa na Yesu katika injili na kuigwa na mitume na wanafunzi wengine katika kitabu cha Matendo. Yuko tayari kwa kawaida nne za kiBiblia, zifuatazo:

*1. Ujumbe sahihi.* Kwanza, mchungaji halisi wa Kipentekoste amejitoa kutangaza kwa uaminifu ujumbe sahihi na ule wa mitume na wainjilisti katika kitabu cha Matendo. Ujumbe huo ni injili. Inaonyeshwa katika huduma ya Filipo ambaye "alishuka mpaka mji mmoja katika Samaria na kumhubiri Masiya [au Kristo] huko" (Mdo. 8:5; taz. mst. 12). Katika kitabu chote cha Matendo ya Mitume, Kanisa halikuyumba katika kutangaza ujumbe wa kifo na ufufuo wa Kristo (rej. 2:22-24; 3:15; 4:10-12). Zaidi ya hayo, mara kwa mara waliwaita watu watubu na kuiamini injili (rej. 2:38; 16:31; 20:21; 26:20). Ni lazima tufanye vivyo hivyo leo.

*2. Utume sahihi.* Pili, mchungaji halisi wa Kipentekoste amejitoa kufuata utume ule ule wa Kanisa katika kitabu cha Matendo. Kama ilivyotajwa hapo juu, utume huo umefupishwa vyema zaidi katika Matendo 1:8, ambapo Yesu alisema, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu… mpaka miisho ya dunia." Kitabu cha Matendo ya Mitume kinalionyesha Kanisa kama lenye kuendelea kuharibu na kuondoa mipaka, likihamia katika maeneo mapya, na kuhubiri habari njema katika nguvu za Roho. Kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uliongoze kanisa lako kufanya vivyo hivyo.

*3. Uzoefu sahihi*. Tatu, mchungaji halisi wa Kipentekoste anaendeleza uzoefu wa kiroho sawa na walivyofanya mitume katika kitabu cha Matendo. Matukio hayo yanajumuisha wongofu wa kubadilisha maisha (linganisha Mdo. 2:41; 8:5-6; 9:1-8), ubatizo wa maji kwa kuzamishwa (rej. 2:41; 8:13, 36-38; 9:17-19; 16:33), ubatizo katika Roho Mtakatifu unaothibitishwa na kunena kwa lugha (rej. 2:4; 10:44-46; 19:6), miujiza ya uponyaji (linganisha 3:1-10; 5; 12-16; 20:7-12), na miujiza ya kukombolewa kutoka mapepo (linganisha 8:7; 16:16-18). Kwa kipimo sahihi, mchungaji wa Kipentekoste atakataa muujiza wowote au uzoefu wa kiroho usioungwa mkono na Maandiko.

*4. Mbinu sahihi*. Mwisho: mchungaji halisi wa Kipentekoste atatumia njia zile zile zilizotumiwa na mitume na wengine katika kitabu cha Matendo. Mbinu hizi ni pamoja na utangazaji wa injili uliovuviwa na Roho unaozalisha mtu kujisikia hatia, imani, na toba (rej. Mdo. 2:14-41; 8:13). Mchungaji wa Kipentekoste zaidi

sana anatarajia Mungu kulithibitisha neno kwa ishara, pamoja na miujiza ya usemi, uponyaji, na ukombozi (taz. 5:12-16; 10:44-47; 14:6-10).[2]

Kwa kuongezea, mchungaji halisi wa Kipentekoste anamtarajia Roho Mtakatifu kuwaongoza katika utume (rej. Mdo. 8:29; 10:9-20; 16:6-10). Mwongozo huu unaweza kuja kupitia hisia za ndani (linganisha 8:29; 10:19), ndoto (linganisha 2:17; 16:9), na maono (linganisha 9:10-16; 10:9-20). Njia kuu ya uinjilisti iliyotumiwa na mitume katika kitabu cha Matendo ilikuwa ni kupanda makanisa ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho ambayo yangefikisha ujumbe wa Kristo katika maeneo ya jirani.[3]

## ANATEMBEA NA ROHO

Si lazima mchungaji wa Kipentekoste aelewe Roho ni nani tu, na jinsi anavyofanya kazi. Ni vizuri pia ajifunze kuishi chini ya uongozi wa Roho. Paulo aliwapa changamoto waamini wapya huko Galatia kwa kuwaambia hivi, “Mkiisha kuanza katika Roho, je mnataka kumaliza katika mwili?” (Gal. 3:3). Alikuwa akiwakumbusha jinsi walivyoanza mwendo wao wa Kikristo. Walikuwa wameanza kwa kuzaliwa kwa Roho na kujazwa na Roho. Sasa, walipaswa “kuenenda pamoja na Roho” (5:25). Hili lazima liwe lengo la dhati la kila mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika.

Njia mbili muhimu unazoweza kutumia kufanikisha hilo ni kwa kuomba katika Roho na kwa kukuza tunda la Roho.

### Maombi Katika Roho

Biblia inazungumza juu ya aina nyingi za maombi, ikiwa ni pamoja na maombezi, dua, maungamo, sala, kuabudu, shukrani, na zaidi. Lakini, maombi katika Roho yanafaa sana katika kudumisha mwendo wa kujazwa na Roho. Paulo anazungumza juu ya aina hii ya maombi katika Waefeso 6:18. Tena, katika Warumi 8:26, hueleza jinsi maombi katika Roho yanavyofanya kazi, kama ifuatavyo: “Roho hutusaidia udhaifu wetu. Hatujui cha kuomba, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.” Ingawa maombi katika Roho yanaweza kuwa maombi yoyote yanayoongozwa na Roho na ambayo

---

[2] Kwa habari zaidi kuhusu mada hizi, tazama Sura ya 16: “Mahubiri Yenye Upako wa Roho” na Sura ya 21: “Kuhudumu Katika Nguvu za Roho.”

[3] Kupata zaidi juu ya kupanda makanisa ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho, tazama Sura ya 39: “Kupanda Makanisa Mapya.”

yametiwa mafuta na Roho, mara nyingi ni maombi katika lugha (1 Kor. 14:14-15). Kama mchungaji wa Kipentekoste mwenye busara, unapaswa kutumia mara kwa mara silaha hii ya kiroho, yenye nguvu sana (2 Wakor. 10:4-5).4

**Tunda la Roho**

Njia nyingine muhimu unayoweza kutumia kuimarisha mwendo wako wa kiroho ni kusitawisha tunda la Roho. Paulo anabainisha tunda hili kuwa ni "upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi" (Gal. 5:22-23).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, haipasi ujue nguvu za Yesu tu, bali pia maisha yako lazima yaakisi tabia yake. Karama bila matunda zinakuwa "shaba iliayo au upatu uvumao" (1 Kor. 13:1). Wengi wasioweza kuja kwa Kristo kupitia maonyesho ya nguvu wanaweza kushawishiwa na matendo ya upendo. Unaweza kukuza matunda ya kiroho katika maisha yako kwa kutembea katika Roho (Gal. 5:16) na kwa kukaa ndani ya Kristo (Yoh. 15:4).

## WATUMISHI KATIKA ROHO

Yesu alishuhudia na kusema, "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kutangaza habari njema" (Lk. 4:18). Kufuatia mfano wa Bwana wake, Paulo alielezea huduma yake mwenyewe kama "onyesho la nguvu za Roho" (1 Kor. 2:4). Vivyo hivyo, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitoe kutekeleza huduma yako katika nguvu za Roho Mtakatifu. Kama Paulo, lazima ujitahidi kuwa mhudumu mwenye uwezo wa Roho (2 Kor. 3:6).

Kwa hivyo, unapaswa kuwa na ufahamu wa kazi ya Roho (au kushindwa Kwake kufanya kazi) katika maisha yako na huduma, na kati ya watu unaowaongoza. Ni lazima ukatae kwa uthabiti aina yoyote ya kidini ambayo ni tupu na isiyo na nguvu na uwepo wa Roho (2 Tim. 3:5), na unapaswa kushindania kwa nguvu mafundisho ya kweli ya Kipentekoste, uzoefu, na utendaji (taz. Yuda 1:3).5 Njia tatu unazoweza kufanya hivi ni kwa kutafuta upako wa Roho, kwa kutafuta mwongozo wa Roho, na kwa kutafuta kupata karama za Roho, kama ifuatavyo:

---

[4] Kujua zaidi juu ya maisha ya maombi ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama : "Kipaumbele cha Maombi."

[5] Unaweza kusoma zaidi kuhusu huduma iliyotiwa nguvu na Roho katika Sura ya 21: "Huduma Katika Nguvu za Roho."

### Kutafuta Upako wa Roho

Kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima ufuatilie upako wa Roho kwa hamu. Lazima utafute daima kuhubiri, kufundisha, na kuhudumu chini ya uwepo dhahiri wa Mungu. Yaani ni lazima uombe na kujitoa kwa Roho, ukimtarajia atulie juu ya maisha yako, akikuwezesha kuhudumu kwa nguvu na mamlaka iliyoongezeka. Upako wa Roho utawashawishi hata walio na mioyo migumu zaidi, kuwafanya wamgeukie Mungu na kutangaza, "Yesu ni Bwana!"

### Kutafuta Mwongozo wa Roho

Zaidi ya hayo, lazima umwamini Roho wa Bwana ili akuongoze katika huduma. Hii ilikuwa ndiyo kawaida ya Yesu na mitume. Mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima anaelewa kwamba Roho Mtakatifu ndiye mkurugenzi mkuu wa utume wa Mungu. Yeye pekee ndiye anayeelewa mahitaji na vipaumbele vya utume.

Roho alimwelekeza Filipo kwa towashi Mwethiopia (Mdo 8:26-38), Petro kwenda nyumbani kwa Kornelio (10:9-25), na Paulo na kikundi chake cha wamishenari hadi Ulaya Magharibi (16:6-40). Atatufanyia vivyo hivyo leo, ikiwa tutakuwa wazi na kukubaliana na sauti Yake. Roho wa Bwana atatuongoza katika kazi yetu kwa ajili ya Kristo.

### Kutafuta Sana Karama za Roho

Paulo aliwahimiza waamini wa Korintho "kutamani sana karama za Roho" (1 Kor. 14:1). Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima utii maagizo ya mtume kwa kukuza utendaji wa karama za kiroho katika maisha yako mwenyewe na katika maisha ya kanisa unalochunga. Ni kupitia karama hizi ndipo upako uliopokewa wakati wa ubatizo wa Roho unaachiliwa katika huduma. Paulo anazungumzia utendaji kazi wa karama katika 1 Wakorintho sura ya 12 hadi 14. Luka anafanya vivyo hivyo katika kitabu cha Matendo. Paulo anaangazia utendaji wa karama katika ibada ya kanisa zima (1 Kor. 14:23-26), wakati Luka anaonyesha jinsi karama zinavyofanya kazi katika uinjilisti huko mstari wa mbele na katika upandaji wa kanisa.[6]

---

[6] Karama za Roho zinazungumziwa zaidi katika Sura ya 21: "Kuhudumu Katika Nguvu za Roho." Zimeorodheshwa na kufafanuliwa katika Nyongeza 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

---

Katika ujumbe wake wa mwisho kwa Timotheo, Paulo alimhimiza mwanawe katika imani "kuichochea karama ya Mungu" iliyokuwa ndani yake, aliyoipokea alipowekewa mikono ya mtume huyo (2 Tim. 1:6). Alikuwa akimhimiza Timotheo kuwa mtu wa Roho. Kila mchungaji wa Kipentekoste katika Afrika angefanya vyema kufuata ushauri wa Paulo kwa Timotheo. Ni lazima wailinde sana na kwa makini ile "amana njema" ya Roho Mtakatifu waliyokabidhiwa (2 Tim. 1:14). Ili kufanya hivyo, hawana budi kuhakikisha kwamba wanadumu wakiwa wamejaa Roho Mtakatifu na kujitoa kwa utume wa Mungu. Na lazima wajitahidi kutekeleza huduma zao kwa nguvu na upako wa Roho Mtakatifu.

~ Sura ya 3 ~

# Mtu Mwenye Tabia Njema

NABII MAARUFU AKAMATWA KWA KUWAPA MIMBA WASICHANA WADOGO." Kichwa hiki cha habari cha kutatanisha kilionekana katika gazeti moja la Kusini mwa Afrika. Makala hiyo iliendelea kusimulia jinsi wasichana kadhaa wadogo, wengine wakiwa na umri wa miaka kumi na minne, walivyopewa mimba na "nabii mmoja Mkristo" maarufu sana Wasichana hao walikuwa wamekwenda pamoja kwa wahusika ili kuripoti tabia mbaya ya mhubiri huyo. Cha kusikitisha ni kwamba, kama ilivyokuwa kwa kashfa zilizopita, kanisa liliaibishwa, kazi ya Mungu ikatiwa doa, na jina la Kristo kuvunjiwa heshima.

Hata hivyo, si dhambi hizo za kashfa za waziwazi zinazozuia zaidi maendeleo ya kanisa; ni zile ndogo zilizofichwa. Akani alitenda dhambi kwa siri, lakini dhambi yake iliathiri kusanyiko lote (Yos. 7:1-12). Vivyo hivyo, makosa ya siri ya mchungaji yanaweza kuathiri kusanyiko zima. Kwa sababu ya ukosefu wao wa maadili, watumishi wengi wa Mungu waliopakwa mafuta wameiletea aibu kazi ya Mungu na kujiondoa wenyewe katika huduma.

Tabia njema ndio msingi ambao juu yake huduma ya kweli ya Kipentekoste inajengwa. Bila msingi huu, yote mengine mwishowe yatatikisika na kuanguka. Huduma ya kudumu haiwezi kamwe kujengwa juu ya talanta, haiba, hadhi ya

kijamii, mafanikio ya kielimu, au hata mvuto. Ni lazima ijengwe kwa uthabiti juu ya msingi wa tabia. Zaidi ya yote, watu wa Mungu lazima waweze kumwamini mchungaji wao.

## UMUHIMU WA MAADILI

Mchungaji wa Kipentekoste lazima awe mwanamume au mwanamke mwenye maadili ya hali ya juu sana. Paulo alimwandikia Timotheo hivi, ambaye alikuwa akihudumu kama mchungaji wa kanisa la Efeso, akimsihi aishi maisha ya kielelezo:

> "Mwangalizi awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mtu wa kiasi, mwenye kustahiwa, mkaribishaji - wageni, awezaye kufundisha" (1 Tim. 3:2-3)

Paulo pia alimsihi Tito kuhusu tabia ya mchungaji:

> "Mwangalizi, akiwa msimamizi - nyumba wa Mungu, lazima awe mtu asiye na lawama. Asiwe mwenye kiburi au mwenye hasira kali au mlevi au mjeuri au mwenye pupa, bali mkaribishaji - wageni, mwenye kupenda mema, mwenye kiasi, mwadilifu, mtakatifu na mwenye nidhamu." (Tito 1:7-8)

Angalia jinsi ambavyo katika hizo orodha zote mbili, Paulo anazungumzia masuala ya tabia badala ya uwezo wa kufanya vitu. Ingawa uwezo wa kufanya vitu ni muhimu kwa mchungaji wa Kipentekoste, tabia ni ya muhimu zaidi.

## MAANA YA TABIA

Nini basi maana ya neno tabia? Tabia inazungumza juu ya dira ya maadili ya mtu. Ni jinsi mtu alivyo kwa ndani. Kwa Mkristo, tabia ni kufanana na Kristo. Tabia huamua jinsi mtu anavyotenda (au anavyofanya) anapobanwa. Ni jinsi tulivyo wakati hakuna mtu mwingine anayetuona. Neno lingine ni uadilifu. Uadilifu huzungumza juu ya ukamilifu wa kiadili.

Kama wachungaji wa Kipentekoste, tunapaswa kujishughulisha zaidi na tabia zetu kuliko sifa zetu. Hii ni kwa sababu sifa yetu ni jinsi wengine wanavyotufikiria sisi, huku tabia zetu ni jinsi tulivyo. Kumbuka onyo la Mungu kwa Samweli alipojaribiwa kumtia mafuta ndugu mkubwa wa Daudi awe mfalme wa Israeli. Nabii alisema, "Watu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo" (1 Sam. 16:7). Samweli hatimaye alimtia mafuta Daudi kuwa mfalme kwa sababu alikuwa mtu aliyetafuta kumpendeza Mungu (1 Sam. 13:14; Mdo. 13:22).

Tabia ya kimungu inajidhihirisha katika maeneo matatu muhimu katika maisha na matendo ya mchungaji wa Kipentekoste, kama ifuatavyo:

**Ukweli**

Mchungaji wa kweli wa Kipentekoste anachagua kufuata nyayo za Yesu, ambaye "hakufanya dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake" (1 Pet. 2:22). Yeye ni mkweli katika mawasiliano yake yote na watu wengine. Yaani, mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste anakataa kusema uongo - hata wakati ambapo kusema uongo ndiyo njia isiyoumiza au kuingiza mtu kwenye hali ngumu. Paulo aliwahimiza Wakristo wa Efeso kuondoa "uongo na kusema kweli" (Efe. 4:25).

Ukiwa mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitahidi kuwa na sifa kama hiyo katika jamii ambayo kila unapozungumza, watu wajue kwamba wanasikia ukweli. Ikiwa hawawezi kukuamini unapozungumza sokoni, wanawezaje kukuamini unapozungumza kutoka kwenye mimbari? Lazima ujulikane kama mtu ambaye daima "[husema] ukweli katika upendo" (Efe. 4:15).

**Uaminifu wa Kifedha**

Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uwe mkweli katika mawasiliano yako yote, na lazima uwe mwaminifu kabisa katika shughuli zako zote za kifedha. Hii inajumuisha shughuli zako za kifedha na Mungu, na kanisa, na wale walio nje ya kanisa. Unafanya hivyo kwa sababu unajua kwamba Mungu anatazama. Na zaidi ya yote, unataka kumpendeza Yeye. Kwa hiyo, unakataa kumwibia Mungu zaka na sadaka zako (Mal. 3:8).

Baadhi ya wachungaji wanawahimiza washirika wa makanisa yao walipe zaka, huku wao wenyewe wakikataa kufanya hivyo. Kwa kufanya hivi, hawamwibii Mungu tu, wanafichua udanganyifu wa mioyo yao wenyewe. Ikiwa wewe ni mtu wa namna hiyo, tubu na ufanye kile unachojua kuwa ni sawa (rej. Mdo. 26:20).

Zaidi ya hayo, lazima uwe na heshima katika utunzaji wako wa fedha za kanisa. Ukweli kwamba wewe ni mchungaji haukupi haki ya kutumia pesa za kanisa upendavyo. Lazima ulinde kwa bidii matoleo yote yanayopokelewa na kanisa. Na lazima uhakikishe kuwa fedha zote zinatumika kwa madhumuni ya kutolewa kwake. Kwa mfano, hupaswi kutumia pesa zinazotolewa kwa ajili ya umisheni kununua gari, au pesa zinazotolewa kwa ajili ya uinjilisti kukarabati jengo la kanisa. Mbaya zaidi, hupaswi kamwe kuchukua pesa zilizotolewa

kusaidia maskini, au kuzitumia kwa faida yako mwenyewe, kama Yuda, ambaye alikuwa anaiba kutoka mfuko wa sadaka ya wanafunzi (taz. Yoh. 12:6).

Kwa kuongezea, kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uwe mwaminifu katika shughuli zako za kifedha na wale walio nje ya kanisa. Lazima ujulikane kama mtu mwenye uadilifu wa hali ya juu. Hupaswi kamwe kuiba, kutapeli, au kutolipa mara moja pesa zozote ulizokopa. Kufanya vinginevyo kutaleta sifa mbaya kwa kanisa na kusababisha watu kuuacha na kuukataa ujumbe wa Kristo.

**Usafi Kijinsia**

Kama mchungaji wa Kipentekoste, hupaswi tu uwe mkweli katika mawasiliano yako, na mwaminifu katika shughuli zako za kifedha, bali pia wakati wote onyesha kuwaheshimu watu wa jinsia tofauti. Ni lazima uwe mwaminifu kwa viapo vyako vya ndoa na "kukataa kila aina ya uovu" (1 Thes. 5:22).

Ni lazima uwatendee "wanawake wazee kama mama zako, na wanawake vijana kama dada zako, kwa usafi kabisa" (1 Tim. 5:2). Ili kufanya hivi, hakikisha kuwa hauko peke yako na mwanamke mwingine isipokuwa mke wako (au na wanamume mwingine isipokuwa mume wako). Ni lazima pia ujilinde dhidi ya uhusiano wa kihisia na mwanamke mwingine yeyote isipokuwa mke wako (au mume wako) kupitia mazungumzo ya ovyo au shughuli.

Ukiwa mtumishi wa Kristo, zingatia kwa uzito stahiki huu ushauri wa Paulo: "Lakini uasherati usiweko katikati yenu, wala uchafu wo wote, au kutamani, kwa maana mambo hayo hayawafai watakatifu " (Efe. 5:3).

## SIFA NYINGINE ZINAZOTAKIWA

Ukiwa mwakilishi wa Mungu, unapaswa kujitahidi kukuza sifa nyingine za kimungu pia. Sifa tano zinazostahili kutajwa hapa ni ujasiri, kutegemewa, unyenyekevu, huruma, na ukarimu.

**Ujasiri**

Ujasiri ni nguvu ya kiadili ya kufanya yaliyo sawa hata katika tishio, hali ngumu au hatari. Ni ujasiri wa kujihatarisha, kusimama kidete kwa lililo jema, na kumwamini Mungu inapoonekana hakuna njia ya kuendelea. Nelson Mandela aliandika katika wasifu wake, "Nilijifunza kwamba ujasiri haukuwa ukosefu wa woga, bali ushindi juu yake. Mtu jasiri sio yule asiyeogopa, lakini ni yule anayeishinda huo uoga."

Ujasiri ni kinyume cha uoga. Uoga ni mtoto wa kujijali; ila ujasiri hutokana na kuwajali wengine. Uoga unapunguza uwezo wa mtu wa kufanya au kusema yaliyo sawa; ujasiri humtia moyo mtu kubaki mkweli anapokabili hatari. Musa alikuwa jasiri aliposimama mbele ya Farao akidai kwamba mfalme wa Misri awaachilie watu wa Mungu (Kut. 5:7). Yesu alikuwa jasiri aliponyenyekea chini ya aibu na maumivu ya msalaba (Ebr. 12:2). Naye Stefano alikuwa jasiri alipowaambia viongozi wa Kiyahudi kwamba wamemuua Masihi wao (Mdo. 7:51-52).

Ikiwa tutajisalimisha kwa Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu, atatupa ujasiri tunaohitaji ili kusimama kwa ajili ya Kristo na kutangaza jina lake kwa wote. Petro na Yohana walipotishwa, waliomba hivi: "Sasa, Bwana, yaangalie matisho yao, ukawawezeshe watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri mwingi." Kwa kujibu maombi yao, Mungu aliwajaza Roho, nao "wakanena neno la Mungu kwa ujasiri" (Mdo. 4:29-31). Kama mchungaji wa Kipentekoste, wewe pia lazima utafute kudumu ukiwa umejaa Roho na kumtegemea Mungu akupe ujasiri unaohitaji ili kutimiza wito wako kwa uaminifu.

**Kutegemewa**

Zaidi ya hayo, kama msimamizi wa Kanisa la Kristo, lazima uwe wa kutegemewa. Bwana lazima awe na uwezo wa kuweka imani yake kamili kwako (Tito 1:7; 1 Pet. 4:10). Paulo aliandika, "Inatakiwa wale waliokabidhiwa [amana] wawe waaminifu" (1 Kor. 4:2). Kwa hivyo maisha yako lazima yaonyeshe sifa za tabia kama vile kutegemewa, kujali muda, bidii, na uvumilivu. Tabia kama hizo ni matunda ya kutembea katika ujazo wa Roho (Gal. 5:22).

Paulo aliwahimiza wazee wa Efeso hivi: "Jilindeni nafsi zenu, na lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi juu yake. Lichungeni kanisa la Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe" (Mdo. 20:28). Kama wachungaji, Bwana ametukabidhi roho za wanaume na wanawake. Na siku moja tutatoa hesabu kwa Mungu kuhusu uaminifu wetu katika jambo hili (Ebr. 13:17). Yakobo anaonya hivi: "Wengi wenu msiwe waalimu, waamini wenzangu, kwa maana mnajua ya kuwa sisi tufundishao tutahukumiwa vikali zaidi" (Yak. 3:1).

**Unyenyekevu**

Mchungaji wa Kipentekoste, kama mwenye kumwiga Kristo, lazima awe mnyenyekevu (Efe. 5:1). Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba, "Yeyote

anayetaka kuwa mkuu kati yenu lazima awe mtumishi wenu, na yeyote anayetaka kuwa wa kwanza lazima awe mtumwa wenu, maana, Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kutoa uhai wake kuwa fidia ya wengi" (Mt. 20:26-28).

Ni kero ya kutosha kumwona mchungaji wa Kipentekoste aliyejawa na kiburi na ubinafsi, mwenye kudai kuhudumiwa na wengine badala ya kuwahudumia. Mtazamo kama huo ni kinyume kabisa cha unyenyekevu unaoonyeshwa na Bwana wetu. Paulo aliwaandikia Wakristo wa Filipi hivi: "Katika uhusiano wenu ninyi kwa ninyi, iweni na nia moja kama Kristo Yesu. Alijifanya kuwa si kitu kwa kutwaa asili ya mtumwa, aliyefanywa kwa sura ya kibinadamu. Naye alipoonekana ana sura ya mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." (Flp. 2:5-8). Chifu mwenye kiburi anadai kuhudumiwa; mchungaji mcha Mungu hufurahia kuwahudumia wengine kwa unyenyekevu.

**Huruma**

Kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uwe mtu wa huruma. Huruma ni upendo katika matendo. Inajidhihirisha katika kujali walio wahitaji. Ni onyesho la nje la moyo uliojaa upendo wa Mungu. Biblia inasema hivi juu ya Yesu, "Alipouona umati wa watu, akawahurumia, kwa sababu walikuwa wametaabika na wanyonge, kama kondoo wasio na mchungaji" (Mt. 9:36).

Huruma ya Yesu ilimsukuma kushughulikia mahitaji ya kiroho na ya kimwili ya wengine. Tukiwa wachungaji wa kundi la Mungu, ni lazima sisi pia tuonyeshe hangaiko la upendo kwa watu Wake, na wale wasiomjua Kristo. Huruma itatufanya tuwajali wengine wakati wa uhitaji wao, na itatusukuma kutangaza injili kwa wote.

Kama wanaume na wanawake wa Mungu, mwenendo wetu endelevu pamoja na Roho Mtakatifu unapaswa kutuchochea kuwapenda na kuwajali wengine. Paulo alieleza hivi: "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa" (Rum. 5:5). Kati ya watu wote, sisi tunaodai kuwa tumejaa Roho wa Kristo tunapaswa kuonyesha huruma ya Kristo kwa wengine.

**Ukarimu**

Sifa ya mwisho muhimu ya mchungaji wa Kipentekoste ni ukarimu. Kama matokeo ya kujazwa na Roho siku ya Pentekoste, waamini wa kwanza waliingiwa na roho ya ukarimu. Biblia inasema hivi juu yao: "Waamini wote walikuwa pamoja na kuwa na vitu vyote shirika. Waliuza mali zao na vitu ili wampe mtu ye

yote aliyehitaji" (Mdo. 2:44-45). Vivyo hivyo, kama mchungaji aliyejazwa na Roho, lazima uwe mwepesi kuwashirikisha wengine kile ulicho nacho. Ni lazima mikono yako iwe imefunguka: kwa Mungu, kanisa, na wale wanaohitaji.

Alipokuwa akiwatuma wale Kumi na Wawili, Yesu aliwahimiza na kusema, "Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo. Mmepokea bure; toeni bure" (Mt. 10:8). Ukarimu kama huo unaambukiza. Watu wanapoona ukarimu wa mchungaji wao, wao pia watatiwa moyo kufungua mioyo yao na mikoba yao na kuwa wakarimu. Utamaduni huu wa ukarimu utaathiri kwa nguvu kanisa, jumuiya inayozunguka, na hatimaye, mataifa ya dunia.

## TABIA YA KUJENGA

Swali linakuja: Je, mchungaji wa Kipentekoste anawezaje kukuza tabia ya kiungu iliyoelezwa hapo juu? Tunafanya hivyo kwa kufuata mfano wa Yesu. Yeye ndiye kielelezo chetu cha maisha na huduma. Yohana aliandika na kusema, "Yeyote anayedai kwamba anaishi ndani yake lazima aenende kama Yesu alivyofanya" (1 Yoh. 2:6).

Kwa mujibu wa Paulo, tunapaswa "kumvaa Kristo" (linganisha Kol. 3:12-17; Rum. 13:14). Yesu alipowaamuru wanafunzi wake, "Nifuateni" (Mk. 4:19), alikuwa akiwaambia wamtazame na kuiga maisha yake. Walipofanya hivi, wangegeuzwa kuwa mfano wake (Rum. 8:29; 2 Kor. 3:18). Hatua kwa hatua, maisha yao yangekuwa kama Yake. Kwa uwezo wa Roho, wangeanza kuishi jinsi alivyoishi, kufikiri kama alivyofikiri, na kupenda kama alivyopenda (2 Pet. 1:3-4). Ikiwa unataka kuwa mchungaji halisi wa Kipentekoste, amua kuwa kama Yesu.

Wale Kumi na Wawili walipomfuata Yesu, waliongezeka na kuwa wengi kuliko walivyokuwa hapo awali. Hapo awali, walikuwa wavuvi tu. Lakini walipomfuata, wakafanyika wavuvi wa watu, kama Bwana wao. Kwa maneno mengine, walichukua tabia ya Yesu. Wasomi wa Biblia wakati mwingine huita mchakato huu malezi ya kiroho.

Hatupaswi kudhani hata hivyo kwamba, tunaweza kufikia tabia kama ya Kristo kupitia juhudi binafsi au uwezo wetu. Ni lazima tupate msaada wa Mungu. Tunaweza kupata msaada Wake kwa kufanya mambo matatu muhimu sana ya kiroho, kama ifuatavyo:

### Kudumu Ndani ya Kristo

Kwanza, tunaweza kupata msaada wa Kristo kusitawisha tabia ya kiungu kwa kukaa, au kubaki ndani Yake. Ni kwa kukaa ndani ya Kristo tu ndipo tunaweza kuwa kama Yeye. Yesu alisema, "Tawi lolote haliwezi kuzaa peke yake; lazima libaki kwenye shina. Wala hamwezi kuzaa matunda msipokaa ndani yangu" (Yoh. 15:4). Kukaa ndani ya Kristo ni kupata uzima kutoka Kwake kwa kuendelea katika Neno Lake na uwepo wake. Tunafanya hivi kupitia maombi ya kujitoa, kujifunza Biblia mara kwa mara, na kwa kumwamini Yeye kikamilifu kwamba atatupa mahitaji yetu yote.

### Kumkaribia Mungu

Tunakuza zaidi tabia ya Kristo kwa kumkaribia Yeye kila siku. Yakobo anatuhakikishia, "Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi" (Yak. 4:8). Kama kukaa ndani ya Kristo, tunamkaribia Mungu kupitia maombi, ibada, na huduma ya uaminifu. Tunapomkaribia Kristo, tunabadilishwa na kufanana naye. Paulo aliandika, "Sisi sote, ambao kwa nyuso zisizotiwa utaji twautafakari utukufu wa Bwana, tunabadilishwa tufanane na mfano wake katika utukufu unaozidi kuongezeka, utokao kwa Bwana, aliye Roho" (2 Kor. 3:18).

### Kuenenda Katika Roho

Mwisho: tunakuza tabia ya Kristo kwa kuenenda katika Roho. Kuenenda kwa Roho ni kuishi maisha kwa kumtii Roho Mtakatifu. Ni kutii amri zake. Paulo alisema kwamba "tumetakaswa na Roho Mtakatifu" (Rum. 15:16). Hii ina maana kwamba Roho wa Mungu hutupatia nguvu tunazohitaji ili kuishi kama Yesu. Paulo aliwatia moyo Wakristo wa Galatia kwa kuwaambia hivi: "Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili" (Gal. 5:16).

Sulemani aliandika, "Ingawa itakugharimu vyote ulivyo navyo, pata ufahamu. Mtunze, naye atakukweza; mkumbatie, naye atakuheshimisha" (Mit. 4:7-8). Mengi hayo yanaweza kusemwa kwa mchungaji wa Kipentekoste. Ingawa inakugharimu yote uliyo nayo, pata tabia; itunze, nayo itakukweza; ikumbatie, nayo itakuletea heshima. Zaidi ya yote, mchungaji wa Kipentekoste lazima awe mwanamume au mwanamke mwenye tabia.

~ Sura ya 4 ~

# Mtu Aliyeandaliwa Vizuri

Kama ilivyo kwa shirika lolote, kanisa linapaswa kuongozwa na wale ambao wamejitayarisha vyema kwa kazi hiyo. Mwinjilisti mmoja anayejulikana kimataifa aliwahi kusema, “Kama ningalijua nina miaka mitatu tu ya kuhubiri injili, ningetumia ile miwili ya kwanza katika maandalizi.” Mchungaji aliyefanikiwa alisema kwa hekima, “Mafanikio hutokea fursa inapokutana na maandalizi.” Hao wote wawili walikuwa wakisisitiza umuhimu wa maandalizi katika huduma ya injili.

Paulo alimwandikia Timotheo, ambaye alikuwa amemteua kama mchungaji wa kanisa la Efeso na kumwambia hivi: , “Yeyote anayetamani kuwa msimamizi [mchungaji] anatamani kazi nzuri” (1 Tim. 3:1). Kisha Paulo alitaja masharti kadhaa ya kuhudumu katika nafasi ya mchungaji. Mojawapo ya masharti hayo ni, “Hapaswi kuwa mtu aliyeongoka hivi karibuni” (mst. 6).

Neno la Kigiriki linalotafsiriwa “mwongofu wa hivi karibuni” katika kifungu hiki ni neophytos, ambalo kihalisi humaanisha “mpya aliyepandwa” au “aliyeanza.” Hii ni tofauti na jina lingine ambalo Paulo analitumia kwa mchungaji, yaani, “mzee,” au presbyteros katika Kigiriki . Neno hili linazungumza juu ya uzoefu na ukomavu, na linaonyesha maandalizi (1 Tim. 5:17-19; Tito 1:5). Paulo anasema kwamba mchungaji lazima asiwe mtu aliyeanza karibuni kutembea na

Kristo. Bali, awe mtu aliyekomaa katika imani na aliyeandaliwa vyema kwa ajili ya kazi ya huduma.

Mhubiri mmoja kijana wa Kipentekoste alimwambia mkuu wa shule ya Biblia hivi: “Sihitaji mazoezi; ninachohitaji ni kutiwa nguvu na Roho kama wanafunzi wa Siku ya Pentekoste.” Lakini, hiyo ni kauli ya kipumbavu. Kitu ambacho mhubiri huyo kijana alishindwa kutambua ni kwamba, kabla ya Siku ya Pentekoste, wanafunzi kumi na wawili walikuwa wametumia miaka mitatu pamoja na Yesu wakijifunza kutoka Kwake. Ingawa mhudumu huyo kijana alikuwa sahihi katika tathmini yake ya hitaji la kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu, alikosea kuhusu mtazamo wake wa umuhimu wa maandalizi ya kiroho, kiakili na kivitendo kwa ajili ya huduma.

Yesu aliwachagua wanafunzi wake kumi na wawili “ili wawe pamoja naye na kwamba awatume kuhubiri” (Mk. 3:14). Kabla ya kuwaagiza kwenda ulimwenguni kote na kuhubiri injili, Alitumia muda mwingi pamoja nao kuwatayarisha kwa ajili ya kazi hiyo.

Sura hii inazungumzia umuhimu wa mchungaji wa Kipentekoste kutayarishwa vyema. Inabainisha baadhi ya maeneo ambayo maandalizi yanahitajika. Kisha inazungumza kuhusu jinsi mchungaji wa Kipentekoste anavyoweza kupata na kudumisha maandalizi yanayohitajika.

## MAENEO YA MAANDALIZI

Maandalizi ya kichungaji huruhusu mhudumu anayetaka, kukuza ujuzi na mitazamo muhimu inayohitajika ili kutimiza wito wake kwa mafanikio. Inaweza kuzingatiwa kama kisanduku cha zana cha mchungaji au vifaa vya kuokoka. Maandalizi ya kutosha hayatakuwezesha tu kufanya kazi yako kwa ufanisi, yatakulinda kutokana na kushindwa wakati wa matatizo au hatari. Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe tayari vizuri kwa angalau njia tano:

### Tayari Kiroho

Zaidi ya yote, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe tayari kiroho kwa kazi hiyo. Utawezaje kuwasilisha neema ya Mungu kwa wengine kwa ufanisi ikiwa hujawahi kupata hiyo neema wewe mwenyewe? Kwa hiyo, ili uwe mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe umezaliwa kweli mara ya pili (Yoh. 3:3-7) na kujazwa na Roho Mtakatifu (Mdo. 1:8; Efe. 5:18). Tena, lazima uwe unaishi kwa uaminifu maisha ya kumheshimu Kristo (1 Yoh. 2:6), na kujitoa kikamilifu kwa Kristo na utume Wake (Mt. 16:24).

Paulo alimkumbusha Timotheo kwamba "mazoezi ya kimwili yafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote" (1 Tim. 4:8). Paulo alitumia mtindo huo wa mafunzo ili kuonyesha nidhamu ya kiroho inayohitajika katika kutayarisha huduma ya kichungaji (rej. 1 Kor. 9:24-27). Alikuwa akimwambia Timotheo kwamba, kama vile mwanariadha anavyopaswa kujizoeza vyema ili kujitayarisha kwa ajili ya mbio, mchungaji lazima ajitayarishe kiroho kwa ajili ya kazi ya huduma. Mcheza mpira ambaye anakataa kufanya mazoezi atajiondoa kwenye timu. Vivyo hivyo, mchungaji anayekataa kutumia nidhamu ya kiroho atajitenga na huduma.

**Tayari Kibiblia**

Pili, ili uwe mchungaji mzuri wa Kipentekoste, lazima uwe tayari kibiblia. Yaani, uwe na ufahamu kamili wa Maandiko. Wajibu mkuu wa mchungaji yeyote ni kulisha kundi la Mungu kwa kuwafundisha Neno la Mungu kwa uaminifu. Maelekezo yenye ufanisi ya Biblia yatawafanya watakatifu wakomae katika Kristo (1 Pet. 2:2), kuwapa silaha dhidi ya walimu wa uongo (Mdo. 20:28-29), na kuwatayarisha kwa ajili ya huduma ya Kikristo (Efe. 4:11-12). Haishangazi kwamba Paulo alimwambia Timotheo mara mbili kuwa, mchungaji lazima "aweze kufundisha" (1 Tim. 3:2; 2 Tim. 2:24). Huduma ya kufundisha kwa ufanisi inaweza tu kujengwa juu ya msingi wa maarifa mapana ya Biblia. Ili kuwafundisha watu wa Mungu ipasavyo, ni lazima ujue jinsi ya kutafsiri kwa usahihi na kutumia "kwa halali neno la kweli" (2 Tim. 2:15).

**Tayari Kiadili**

Kisha, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe tayari kimaadili kwa ajili ya huduma. Lazima uishi maisha matakatifu, yanayomheshimu Kristo. Paulo aliandika kwamba mwangalizi, au mchungaji, "asiwe na lawama,…asiwe mlevi, mkorofi, asiyefuata mapato ya aibu" (Tito 1:7). Aliongeza kwamba mchungaji lazima awe "mnyofu, mtakatifu, na mwenye nidhamu" (mst. 8). Vivyo hivyo, alimwambia Timotheo kwamba mwangalizi lazima "awe asiye na lawama, mwaminifu kwa mkewe,…asiwe mpenda fedha" (1 Tim. 3:2). Yeyote ambaye hajapata ushindi katika maeneo haya ya maisha amejiondoa mwenyewe kutoka katika huduma. Mtu huyo lazima ajiondoe mara moja kwenye huduma hadi apate ushindi dhidi ya maovu haya ya maadili.

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujilinde kwa uangalifu dhidi ya dhambi tatu kuu ambazo zimenasa na kuwaondoa viongozi wengi wa kidini. Maovu hayo matatu makubwa ni kupenda pesa, ashiki au tamaa mbaya ya kimwili

na tamaa ya kuheshimiwa kiasi cha kugandamiza wengine. Hakuna kiasi chochote cha mvuto binafsi au upako utakaokupa ushindi katika maeneo haya.

Katika barua ya Paulo kwa waamini wa Galatia, aliwaonya dhidi ya kukubali tamaa za asili ya dhambi (Gal. 5:19-21). Badala yake, wanapaswa kusitawisha tunda la Roho (mst. 22-23). Kisha Paulo aliwafunulia njia ya kutoka kushindwa kimaadili hadi ushindi wa kiadili: "Wale walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho" (mash. 24-25). Mtume aliwahimiza Wagalatia zaidi kwa kusema, "Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili" (mst. 16).

**Kiakili na Kihisia**

Mwisho: ili kutekeleza huduma yako kwa ufanisi lazima uwe tayari kiakili na kihisia kwa kazi hiyo. Yaani, lazima uweze kufikiri kwa busara, na lazima uweze kudhibiti hisia zako na kukabili ipasavyo changamoto unazokutana nazo.

Paulo alimwandikia Tito kama ifuatavyo: "Kwa kuwa mwangalizi anaisimamia nyumba ya Mungu, imempasa kuwa mtu asiye na lawama, asiwe mbabe, asiwe mwenye hasira kali..." (Tito 1:7-8). Katika barua yake ya kwanza kwa Timotheo, mtume aliongezea yafuatayo, "Mwangalizi awe…mwenye kiasi,…asiwe mjeuri bali mpole, asiwe mgomvi" (1 Tim. 3:2). Kumbuka jinsi ambavyo kila moja ya sifa zilizochaguliwa hapo juu husema juu ya ukomavu wa kiakili na kihisia. Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitahidi kusitawisha sifa hizi katika maisha yako na huduma yako.

Mchungaji ambaye ni mwerevu kiakili na amekomaa kihisia ataonyesha ujasiri katika kutumia karama na uwezo wake aliopewa na Mungu. Ujasiri huu utamsaidia kukabiliana na hali ngumu na kufanya maamuzi muhimu. Utamlinda zaidi dhidi ya kukwepa majukumu magumu kama vile kutangaza habari mbaya, kulilinda kanisa dhidi ya walimu wa uongo, na kazi nyingine za aina hiyo.

## NJIA ZA MAANDALIZI

Akijua thamani ya maandalizi mazuri, mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima atafanya kila juhudi kujitayarisha kwa ajili ya huduma. Hebu tuangalie njia tatu unazoweza kufanikisha hili:

**Kupitia Uzoefu kwa Vitendo**

Kwanza, unaweza kujitayarisha kwa ajili ya huduma kwa kutafuta uzoefu wa vitendo. Njia tatu muhimu za kupata uzoefu ni kama ifuatavyo:

*1. Kufanya huduma katika kanisa la mahali pamoja*. Kusanyiko la mahali pamoja ni mahali sahihi pa kuanzia huduma yako. Paulo na Barnaba walihusika katika huduma kwenye kanisa la Antiokia wakati Roho Mtakatifu alipowaelekeza katika huduma ya umishenari (Mdo. 11:25-26; 13:1-3). Paulo aliwashirikisha wenzake wengi katika umishenari kutoka miongoni mwa wale waliofanya kazi katika makanisa ya mahali pamoja. Kwa mfano, alimpa kazi Timotheo kutoka kanisa la Listra (Mdo. 16:1-2), Sopatro kutoka Beroya, Aristarko na Sekundo kutoka Thesalonike, na Gayo kutoka Derbe (20:4). Ndugu hawa walijifunza jinsi ya kuhudumu katika makanisa yao ya mahali pamoja. Mara tu walipojithibitisha, walichaguliwa kwa huduma pana zaidi.

Kwa hiyo, kama mchungaji mtarajiwa wa Kipentekoste, unapaswa kutafuta fursa za kuhudumu katika kanisa lako la nyumbani. Unapaswa kuwa tayari kujitolea fursa za huduma zinapotokea. Kwa kushiriki katika huduma za kusanyiko la mahali pamoja, utapata uzoefu wa thamani, karama zako za kiroho zitafunuliwa, tabia yako itaimarishwa, na wito wako kwa huduma pana zaidi utathibitishwa.

*2. Kutumika chini ya mchungaji mwenye uzoefu*. Njia nyingine ya ufanisi ya maandalizi kwa ajili ya huduma ya Kipentekoste ni kulelewa. Kulelewa hutokea wakati mtumishi mpya (au mwanafunzi) anapotembea na mchungaji mkongwe na kujifunza kutoka kwake. Hivi ndivyo Yesu alivyowazoeza wanafunzi wake (Mk. 3:14-15). Aliwaambia, "Njooni, mnifuate… nami nitawatuma mkavue watu" (Mk. 1:17). Walipokuwa wakitembea na kuhudumu pamoja na Yesu, walijifunza kuhudumu jinsi Yeye alivyohudumu. Alisema hivi juu ya hilo: "Kila mtu ambaye amefundishwa kikamilifu atakuwa kama mwalimu wake" (Lk. 6:40).

Mifano mingine ya kibiblia ya kulelewa ni Musa na Yoshua (Kut. 24:12-13), Eli na Samweli (1 Sam. 2:11), Eliya na Elisha (1 Wafalme 19:19-21), na Paulo na wamishenari washirika wenzake — akina Timotheo, Tito, Luka, na wengine. Kutumika chini ya mchungaji mwenye uzoefu kutakuruhusu kupata uzoefu katika mambo ya kikanisa na kujifunza kuhusu kazi ya uchungaji.

*3. Kushirikiana na wengine*. Unaweza pia kupata uzoefu muhimu kwa kushirikiana na wengine kwenye timu za huduma. Timu hizi zinaweza kuwa ni

timu za maombi, za maombezi, timu za uinjilisti, timu za upandaji kanisa, na nyinginezo. Faida moja ya kufanya kazi na wengine katika timu ni kwamba itakusaidia kujifunza jinsi ya kufanya kazi kwa ushirikiano na wengine katika huduma.

**Kupitia Mafunzo Yasiyo Rasmi**

Njia nyingine unayoweza kujitayarisha kwa huduma ni kupitia "mafunzo yasiyo rasmi." Mafunzo aina hii ni ujifunzaji unaotokea nje ya mazingira ya darasani yaliyopangwa. Ingawa haya mafunzo hayawi na mpangilio, usifikiri kwamba ni kutojali au kubahatisha. Yanaweza kuwa ya makusudi na yenye ufanisi. Mafunzo yasiyo rasmi yanaweza kujumuisha mafunzo ya kibinafsi ya Biblia, kusoma vitabu na makala, kuhudhuria makongamano, na mafunzo enezi.

*1. Funzo la Biblia kibinafsi.* Njia moja muhimu ya mafunzo yasiyo rasmi ni kujifunza Biblia kibinafsi. Kusoma Biblia yote kila mwaka ni mazoezi yenye manufaa. Yanaweza kukusaidia kuelewa mtiririko wa jumla wa Maandiko. Njia nyingine muhimu ya kusoma Biblia ni kusoma tena na tena kitabu fulani cha Biblia. Msomi mmoja wa Biblia alisema, "Siri ya kujua Biblia si kuisoma bali kuisoma tena ." Unaposoma kitabu mara kadhaa, utapata ufahamu mkubwa zaidi wa kweli nyingi zinazofundishwa humo.

Zaidi ya kusoma Biblia tu, utataka kusitawisha mazoea ya kujifunza Biblia kwa mpangilio. Ikiwezekana, unapaswa kupata Biblia nzuri ya kujifunzia iliyo na ramani, mihutasari ya vitabu na utangulizi, maelezo kuhusu mwandishi, mafafanuzi, makala, na chati.[1]

*2. Kusoma vitabu na makala*. Njia nyingine muhimu ya mafunzo yasiyo rasmi inayopatikana kwa kila mchungaji wa Kipentekoste ni usomaji wa makini wa vitabu na makala zilizochaguliwa. Mtu fulani ameona kwa usahihi na kutoa wazo hili: "Viongozi ni wasomaji." Kwa hivyo unapaswa kuwa msomaji mwenye bidii. Kusoma kila siku kutasaidia kuchangamsha ubongo wako, kupanua akili yako, na kuboresha ustadi wako wa kufikiri. Pia itakupa maarifa mapya kuhusu changamoto za maisha na huduma. Zaidi ya hayo, zoezi la kujisomea litakusaidia kuongeza msamiati wako, na hivyo kuboresha uwezo wako wa kuzungumza.

---

[1] Biblia bora kabisa ya kujifunza Upentekoste ni *Biblia ya Uzima Tele.* Biblia hii inapatikana kutoka Idara ya Uanafunzi na Maandiko ya Tanzania Asssemblies of God.

Hata hivyo, ni lazima uwe mwangalifu katika uchaguzi wako wa vitu vya kusoma. Vitabu na makala nyingi barani Afrika siku hizi vinafundisha dhana zisizo za kiBiblia na mafundisho ya uongo (linganisha 1 Tim. 4:7; 2 Yoh. 1:7-8). Achana na vitabu na makala aina hiyo.

*3. Kuhudhuria makongamano na semina.* Unaweza kukuza zaidi ujuzi wako wa huduma kwa kuhudhuria makongamano na semina za wachungaji. Mikutano hii mara nyingi hupangwa kuwasaidia wachungaji kuboresha ujuzi wao wa huduma. Hutumika zaidi kuwatia moyo wachungaji waliokata tamaa na kuwasaidia kupata maarifa mapya katika Maandiko na kazi ya kanisa. Semina pia hufahamisha wachungaji juu ya mipango ya kimadhehebu, na husaidia kukuza hisia inayohitajika ya kazi kati ya wenzao katika huduma.

**Kupitia Mafunzo Rasmi**

Mwisho: ikiwezekana, kama mchungaji wa Kipentekoste mtarajiwa, unapaswa kupata mafunzo rasmi. Mafunzo rasmi ni mafunzo yanayotolewa kupitia shule na taasisi za kudumu na za mawasiliano. Fursa za mafunzo rasmi ni pamoja na zifuatazo:

*1. Elimu ya duniani.* Elimu ya msingi, sekondari, na hata zaidi ya sekondari ikiwezekanani muhimu kwa mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika. Taasisi hizi husaidia kuandaa wanafunzi kwa maisha katika ulimwengu wa kisasa. Katika taasisi hizo, wanafunzi hujifunza kusoma, kuandika, na kufanya hesabu. Pia wanajifunza historia, jiografia, na mambo mengine muhimu. Kwa mchungaji mtarajiwa wa Kipentekoste, faida ya masomo ya shule ni kubwa sana. Husaidia kuamsha udadisi wao, kupanua mawazo yao, na kuwafanya wafahamu mienendo ya sasa katika jamii.

*2. Shule za Biblia na vyuo.* Ni muhimu zaidi kwamba, ikiwezekana, unapaswa kusoma katika taasisi ya Biblia inayotambulika na inayoheshimika au chuo kikuu. Ni upumbavu kukataa mafunzo rasmi ya udaktari! Vivyo hivyo, yule anayelenga kuwa mchungaji wa Kipentekoste atakuwa mpumbavu kukataa mafunzo rasmi ya kihuduma. Makanisa mengi ya kitaifa yanahitaji wachungaji wao kuhudhuria shule ya Biblia. Hata kama kanisa linahitaji au la, mchungaji wa Kipentekoste mwenye busara atafuata mafunzo rasmi ya kihuduma.

*3. Masomo enezi.* Baadhi ya shule za Biblia hutoa kozi enezi na kwa njia ya mawasiliano. Kozi hizi zinaweza kutolewa kibinafsi, kwa barua, au kupitia

mtandao. Wanamruhusu mchungaji kusoma akiwa nyumbani na akifanya huduma. Ni njia bora kwa mchungaji kuongeza maarifa na ujuzi wake.

Kwa sasa, makanisa ya Assemblies of God kote barani Afrika yanaendesha zaidi ya taasisi 300 za mafunzo ya watumishi. Shule hizi hutoa mafunzo kwa wanafunzi wa Assemblies of God na wa madhehebu mengine pia. Mchungaji wa Assemblies of God katika eneo lako anaweza kukusaidia kupata shule (au chuo) katika nchi yako.

*4. Masomo ya elimu ya juu.* Baadhi ya wahudumu wa Kipentekoste barani Afrika watataka kuendelea na masomo ya juu zaidi, au seminari. Hii ni kweli hasa kwa wale wanaofundisha katika vyuo vya Biblia na seminari. Lakini, ni muhimu kwamba mtu atafute masomo na kuhitimu katika seminari ya Kipentekoste iliyoidhinishwa na kutambuliwa. Idadi kubwa ya makanisa ya kitaifa ya Assemblies of God barani Afrika yanaendesha shule za ngazi ya Uzamili. Masomo ya udaktari hutolewa kupitia Pan-Africa Theological Seminary (PAThS). PAThS ni seminari iliyotambuliwa na tume husika ya elimu ya juu kitheolojia, inayoendeshwa na Assemblies of God huko Lomé, Togo, yenye vitivo (au vitengo) katika nchi nyingine za Afrika. Masomo hutolewa kwa Kiingereza na Kifaransa.

## MAANDALIZI YANAYOENDELEA

Kwa kweli, kama mchungaji wa Kipentekoste, maandalizi yako ya huduma hayana mwisho. Lazima uwe mwanafunzi wa maisha yote. Maisha yako lazima yawe na juhudi za mara kwa mara kutafuta ubora. Paulo alishuhudia kuhusu jitihada hii katika maisha yake mwenyewe alipoandika, “Si kwamba nimekwisha kupata haya yote, au nimekwisha kufikia lengo langu, bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake Kristo Yesu alinishika mimi.” (Flp. 3:12).

Utafutaji huu wa ubora lazima uendelee katika maisha yako yote. Ni lazima uendelee kujitayarisha kiroho kwa kutafuta kubaki umejaa Roho Mtakatifu na kupitia utendaji wa mambo ya kiroho kama maombi, kufunga, kuabudu, na kutafakari Maandiko.[2] Unapaswa kuendelea kujitayarisha zaidi kibiblia kupitia

[2] Kwa habari zaidi kuhusu maandalizi ya kiroho, tazama Sura ya 15: “Tabia Imara ya Ibada Binafsi.”

mafunzo ya utendaji w kusoma Maandiko, na kama Roho ataelekeza, kwa kufuata mafunzo ya hali ya juu.[3]

Zaidi ya hayo, lazima uendelee kutafuta kujiboresha kimaadili . Kwa maneno ya Sulemani, lazima ulinde moyo wako kwa bidii na kujiepusha na uovu, ukitafakari sana njia miguu yako inakopitia (Mit. 4:23-27).[4]

Mwisho: kama mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima, lazima uendelee kujiboresha kiakili na kihisia. Unaweza kufanya hivi kwa kusoma na kujifunza kwa nidhamu, na kwa kuruhusu Roho na Neno la Mungu kufanya kazi kwa nguvu katika maisha yako, kukutengeneza ufanane na Kristo (2 Kor. 3:18).

---

[3] Kwa mengi zaidi kuhusu uhusiano wa mchungaji wa Kipentekoste na Biblia, tazama Sura ya 9: "Anaiamini Biblia."

[4] Kwa mengi zaidi kuhusu kujiandaa kimaadili, tazama Sura ya 3: "Mtu wa Tabia Njema."

~ Sehemu ya 2 ~

# Vipaumbele vya Mchungaji wa Kipentekoste

~ Sura ya 5 ~

# Vipaumbele vya Kihuduma

Mchungaji mmoja mzee aliketi na kikundi cha wanafunzi wa shule ya Biblia wenye shauku. Mwanafunzi mmoja alimuuliza, “Mzee, uliwezaje kujenga kanisa lenye nguvu namna hii? Na unaelezaje mafanikio yako katika huduma?” Jibu lake liliwashangaza wanafunzi. Alisema hivi: "Ili kufanya kwa ubora, lazima uachane na kawaida." Alipoona sura za wanafunzi zimechanganyikiwa, alifafanua zaidi: “Katika maisha, kuna mambo mengi mazuri unayoweza kufanya. Ulimwengu utakudai mengi maana mahitaji ni makubwa. Washirika wa kanisa lako na wazee watatarajia mengi kutoka kwako. Wachungaji wengine watafanya mambo fulani, na watu wako watakutarajia na wewe ufanye vivyo hivyo.”

Mchungaji huyo mzee aliendelea, “Mambo yote haya yanaweza kuwa mazuri. Lakini kama mwanamume au mwanamke wa Mungu, utahitaji kuuliza, 'Bwana, wataka nifanye nini?' Kisha, mara tu unaposikia sauti ya Mungu, fanya kile Anachosema. Mambo mengine yanaweza kuwa mazuri, lakini kile ambacho Mungu anakuambia ufanye ndicho bora zaidi. Mungu ataleta watu katika kanisa lako kukusaidia kufanya hayo mambo mengine. Lakini wewe kila wakati zingatia kufanya yale ambayo Mungu amekuambia ufanye.”

Mchungaji huyo mzee alikuwa anazungumza kuhusu kuweka vipaumbele vya huduma. Kipaumbele ni kitu cha muhimu sana. Ni jambo ambalo mtu hufanya kabla ya kufanya mambo mengine ambayo sio muhimu sana.

## VIPAUMBELE VYA KIBIBLIA

Yesu na wanafunzi wake walikuwa njiani kutoka Yudea kwenda Galilaya. Akiwa njiani Yesu aliwaambia, "Ni lazima nipitie Samaria" (Yoh. 4:4). Bila shaka jambo hilo liliwashangaza wanafunzi, kwa sababu ingebidi wachepuke kutoka kwenye njia kuu ili kufika huko. Walipofika mjini Sikari, walifahamu kwa nini Yesu alilazimika kupitia Samaria. Kulikuwa na baadhi ya watu waliopotea pale ambao walikuwa tayari kupokea ujumbe wa wokovu. Naye alitaka kuwafundisha wanafunzi wake somo la kuvuna mavuno.

Wakati mwingine, Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, "Nitalijenga kanisa langu" (Mt. 16:18). Baadaye aliwaamuru, "Nendeni mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (Mt. 28:19). Katika kila moja ya matukio haya, Yesu alikuwa anazungumza juu ya vipaumbele ambavyo alikuwa amejiwekea yeye na kwa ajili yao.

Kwa kufuata kielelezo cha Bwana wao, mitume pia waliweka mambo ya kutanguliza huduma. Vipaumbele vyao vilikuwa kufanya kazi ambayo Kristo alikuwa amewapa. Siku moja, kikundi cha washirika wa kanisa walikuja kwa mitume wakiwa na malalamiko. Wajane wao walikuwa wakipuuzwa katika ugawaji wa chakula cha kila siku, na walitaka mitume washughulikie tatizo hilo. Lakini mitume walikuwa tayari wameweka vipaumbele vyao, kwa hiyo wakawajibu watu, "Si sawa kwetu kupuuza huduma ya neno la Mungu na kuhudumu mezani" (Mdo. 6:2).

Ingawa kuwatunza wajane lilikuwa jambo zuri na la lazima, haikuwa kile ambacho Kristo alikuwa amewaamuru wafanye. Kwa hiyo waliliomba kanisa kuwachagua mashemasi ili kushughulikia hitaji hili huku wao wakidumisha maombi na mahubiri. Kwa hiyo, "neno la Mungu likaenea. Idadi ya wanafunzi katika Yerusalemu ikaongezeka kwa kasi, na idadi kubwa ya makuhani ikaitii ile imani" (mst. 7).

Sura hii itashughulikia suala muhimu la vipaumbele vya huduma kwa mchungaji wa Kipentekoste leo barani Afrika.

## KUAMUA VIPAUMBELE VYA KIHUDUMA

Je, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuwa na vipaumbele gani? Ingawa kuna mambo mengi mazuri ambayo angeweza kufanya, kuna mambo machache ambayo wanapaswa kufanya. Vipaumbele saba kati ya hivyo ni (1) kutumikia utume wa Mungu, (2) kutimiza wito wa Mungu, (3) kuwafikia waliopotea, (4) kutangaza Neno la Mungu, (5) kuomba, (6) kushikilia maadili ya Kipentekoste, na (7) kuandaa watu wa Mungu ili kufanya huduma. Hebu tuangalie kwa karibu zaidi kila moja ya vipaumbele hivi.

### Kutumikia Utume wa Mungu

Kwanza, mchungaji wa Kipentekoste lazima atangulize huduma ya utume wa Mungu. Baada ya kujaribiwa kwake nyikani, Yesu alirudi Galilaya. Huko, aliingia katika sinagogi la Nazareti na akaanza kusoma gombo la Isaya: “Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema… kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa. (Lk. 4:18-19). Yesu alijua vipaumbele vya Baba yake kwa ajili ya maisha na huduma Yake. Alielewa kwamba Baba alikuwa amemtuma kutekeleza utume Wake. Pia alikuwa amemtuma Mwanawe kutoa uhai wake kuwa fidia kwa ajili ya watu wote (Mt. 20:28).

Wewe mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitoe katika kutumikia utume wa Mungu kama alivyofanya Yesu. Yeye aliwaambia wanafunzi wake, “Kama vile Baba alivyonituma mimi, mimi nawatuma ninyi” (Yoh. 20:21). Kama vile Mungu alivyomtuma Yesu ulimwenguni kutumikia utume Wake, sasa Yeye anakutuma wewe ulimwenguni kufanya vivyo hivyo. Utume wa Mungu, ambao wakati mwingine huitwa *missio Dei*, kwa lugha ya Kilatini, ni kuwakomboa na kuwaita kwake watu kutoka kila kabila na lugha na taifa duniani (Uf. 5:9).[1]

### Kutimiza Wito wa Mungu

Pili, mchungaji wa Kipentekoste lazima atie kipaumbele kwenye kutimiza wito wa Mungu katika maisha yake. Yesu hakupoteza mwelekeo wa kile ambacho Baba alikuwa amemwita kufanya. Katika saa yake ya giza kuu, alimwomba Baba Yake na kusema, “Si mapenzi yangu, bali yako yatendeke” (Lk. 22:42). Vivyo hivyo, mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika lazima aelewe wito wa Mungu

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu jukumu la mchungaji wa Kipentekoste katika kutimiza utume wa Mungu, tazama Sura ya 31: “Uongozi wa Kimisheni” na Sura ya 40: “Kutengeneza Mpango wa Umisheni wa Kanisa la Mahali Pamoja.”

juu ya maisha yake, na anapaswa kujitahidi kutimiza wito huo. Mungu ameweka njia kwa kila mhudumu wake kuipita. Kila mchungaji wa Kipentekoste lazima atafute njia hiyo. Na lazima akae kwenye njia hiyo hadi atakapomaliza mwendo wake (Ebr. 12:1-2; 2 Tim. 4:7).

**Kuwafikia Waliopotea**

Tatu, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kutanguliza kuwafikia waliopotea. Hiki kilikuwa kipaumbele kwa Yesu. Alishuhudia hivi: "Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea" (Lk. 19:10). Kuwafikia waliopotea lazima kubaki kuwa kipaumbele kwa kila mtu anayetafuta kumfuata Kristo. Yesu aliagiza hivi: "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa viumbe vyote" (Mk. 16:15).

Amri hii ya Kristo itaendelea kutumika hadi atakaporudi kutoka mbinguni (Mt. 24:14). Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uongoze njia katika kuhamasisha kanisa kwa ajili ya uinjilisti na umisheni unaotiwa nguvu na Roho. Unaweza kufanya hivyo kwa njia mbili:

Kwanza, lazima uwe kielelezo kwa kanisa kwa kuwashirikisha wengine Injili, ukilenga kuwaongoza kwa Bwana. Washirika wa kanisa lako wanapokuona ukishuhudia, watatiwa moyo kushuhudia pia. Pili, lazima uonyeshe kujali kwako waliopotea kwa kutoa sadaka ya umisheni kwa ukarimu, na kwa kuyaombea makabila ambayo hayajafikiwa Afrika kwa bidii na kwingineko. Lazima uhamasishe kanisa kufanya vivyo hivyo. Ni lazima ufanye uinjilisti na umisheni kuwa kipaumbele cha kwanza katika upangaji wa ratiba na bajeti ya kanisa.[2]

**Kuhubiri Neno**

Nne, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuweka mbele kuhubiriwa kwa Neno la Mungu. Paulo alimsihi Timotheo, mwanawe katika imani, "Lihubiri neno; uwe tayari wakati unaofaa na usiofaa; sahihisha, kemea, na kuhimiza kwa uvumilivu mwingi na mafundisho makini" (2 Tim. 4:2). Kuhubiri Neno ni pamoja na kutangaza injili kwa waliopotea, kuwafundisha na kuwatia moyo waaminio katika njia za Bwana. Yesu aliagiza hivi: "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili" (Mk. 16:15). Na tena aliagiza hivi: "Lisha kondoo zangu" (Yoh. 21:17). Ili kuhubiri vyema, ni lazima ujitoe kulishika na kulifafanua Neno la Kweli

---

[2] Kwa habari zaidi kuhusu kuwafikia waliopotea, tazama Sura ya 37: "Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti."

kwa usahihi (2 Tim. 2:15). Ili kufanya hivyo, ni lazima uwe mwanafunzi mwenye bidii wa Neno la Mungu.[3]

### Kuomba

Tano, mchungaji wa Kipentekoste lazima ayape maombi kipaumbele. Unapoishi maisha ya maombi ya kujitoa, unaonyesha jinsi unavyomtegemea Mungu. Unazidi kufuata nyayo za Yesu na mitume. Biblia inasema juu ya Yesu kwamba, katika siku za maisha yake duniani, "alifanya maombi, sala na dua pamoja na kulia sana na machozi" (Ebr. 5:7; taz. Mk. 1:35; Lk. 5:16). Inasema juu ya mitume kwamba walikuwa "katika kusali daima" (Mdo. 1:14; taz. 3:1; 6:2-4; 10:9).

Maombi hayabadilishi hali tu, bali yanambadilisha yule anayeomba. Martin Luther, aliyeleta Matengenezo katika kanisa, alielewa umuhimu wa maombi. Wakati fulani alisema, "Nina mengi ya kufanya leo hivi kiasi kwamba nitatumia saa tatu za kwanza katika kuomba!" Vivyo hivyo, maombi lazima yawe kipaumbele katika maisha ya kila mchungaji wa Kipentekoste.[4]

### Kudumisha Maadili ya Kipentekoste

Sita, mchungaji wa Kipentekoste lazima ajitahidi kushikilia maadili ya Kipentekoste katika huduma yake. Maadili ya Kipentekoste ni zile imani na ahadi ambazo humdhihirisha mtu kuwa mwamini halisi wa Kipentekoste. Maadili matatu ya msingi ambayo mchungaji wa Kipentekoste lazima azingatie ni kujitoa kuyashika mafundisho ya kweli ya Biblia, uaminifu mkubwa kwa Mungu na utume Wake, na kukubali kwake mtembeo wa Roho wa Mungu katika maisha yake.

Huku kuwa wazi kwa kazi ya Roho wa Mungu maishani hujumuisha msisitizo wa kuona waamini wakibatizwa katika Roho Mtakatifu.[5] Yesu na mitume walikazia uhitaji huo. Kabla ya kurudi mbinguni, Yesu aliwaamuru wafuasi wake, "Msiondoke Yerusalemu, bali ingojeni zawadi ambayo Baba yangu aliahidi…

---

[3] Kupata maelezo zaidi kuhusu huduma ya kuhubiri ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 16: "Mahubiri Yenye Upako wa Roho."

[4] Kwa maelezo zaidi kuhusu maisha ya maombi ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi."

[5] Kupata maelezo zaidi juu ya maadili ya Kipentekoste, tazama Sura ya 10: "Husimamia Ukweli wa Kipentekoste"; Sura ya 11: "Hukuza Uzoefu na Matendo ya Kipentekoste"; na Sura ya 12: "Anathamini Urithi wa Kipentekoste."

baada ya siku chache mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu" (Mdo. 1:4-5; taz. Lk. 24:49). Miaka mingi baadaye, Paulo alipokutana na wanafunzi kumi na wawili huko Efeso, swali lake la kwanza kwao lilikuwa, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" (Mdo. 19:2).

Yesu na mitume walisisitiza kwamba waamini wote wabatizwe katika Roho Mtakatifu kwa sababu walijua tukio hili lingewawezesha kuwa mashahidi wa Kristo "katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Mdo. 1:8)

**Kuwaandaa Watu wa Mungu**

Hatimaye, mchungaji wa Kipentekoste lazima aweke kipaumbele kwenye kutoa mafunzo ya watu wa Mungu kwa ajili ya huduma. Mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima anaelewa kwamba mojawapo ya majukumu yake ya msingi ni "kuwatayarisha watu [wa Kristo] kwa ajili ya kazi za huduma" (Efe. 4:12). Hii ina maana kwamba wewe kama mchungaji unatakiwa kufanya zaidi ya kuchunga kondoo, unapaswa kuwakuza watu wa Mungu waweze kushiriki kwa manufaa wa ufalme. Kwa hiyo ni lazima ufanye maendeleo ya wanafunzi kuwa kipaumbele katika huduma.[6]

## KUFUATA VIPAUMBELE VYA KIHUDUMA

Baada ya kuchunguza vipaumbele hivi saba vya kibiblia kwa wachungaji wa Kipentekoste, lazima sasa uamue kama utavipokea viwe vyako. Ni jambo moja kusoma kuhusu vipaumbele hivi katika kitabu. Ni jambo lingine kabisa kumruhusu Roho wa Mungu kuyaandika kwenye kurasa za moyo wako. Ili hili litokee, utahitaji kujitoa kwa mchakato wa kugeuza kanuni hizi kuwa vipaumbele, na kisha kugeuza vipaumbele hivyo kuwa vitendo vya kihuduma. Hebu tuangalie mchakato huu.

**Kuweka Vipaumbele**

Unaanza mchakato kwa kutambua kwamba kuwa mchungaji wa Kipentekoste mwenye uwezo kunahitaji juhudi. Umahiri wa kihuduma ndio mwisho wa safari ndefu. Na, kama ilivyo kwa safari yoyote, safari hii huanza kwa kuchagua pa kwenda. Inaendelea kwa kutengeneza na kutekeleza mpango wa kufika mahali

---

[6] Kwa habari zaidi kuhusu kuwaendeleza watu wa Mungu, tazama Sura ya 17: "Kufundisha kwa Ufanisi" na Sura ya 25: "Kuuimarisha Mwili."

hapo. Kuweka vipaumbele saba hapo juu katika huduma yako mwenyewe, na katika huduma za kanisa lako, utahitaji kujitoa kusafiri.

Unaweza kuanza safari kwa kuchukua vile vipaumbele saba vya huduma na kuviandika katika daftari. Kisha unaweza kutumia orodha hii kama mwongozo wa maombi ya kila siku. Unapoomba kupitia orodha hii kila siku, mwombe Mungu aingize hizo dhana za kibiblia ndani ya roho yako. Ukifanya hivi, mabadiliko yatatokea. Roho Mtakatifu ataanza kuandika vipaumbele hivi kwenye vibao vya moyo wako. Badala ya kubakia kama nadharia, baada ya muda, zitakua na kufanyika vipaumbele vya kihuduma.

Katika maombi jiulize hivi: "Ni mambo gani ninayotanguliza sasa katika huduma?" Vipaumbele vyako vya kihuduma vya sasa ni mazoea ambayo unawekeza muda mwingi na nguvu. Orodhesha vipaumbele hivyo. Kisha jiulize, "Vipaumbele hivi vinakubalianaje na vipaumbele vya Yesu na mitume?" Sasa, kulingana na tathmini yako, jiulize maswali yafuatayo:

- Je, ninafanya vyema wapi katika kutimiza utume wa Mungu?
- Je, ninafanya vizuri wapi katika kutimiza wito wa Mungu juu ya maisha yangu na maisha ya kanisa ninaloliongoza?
- Je, ninafanya vyema katika kufikia waliopotea katika eneo langu na duniani kote?
- Je, ninafanya vizuri kiasi gani katika kuhubiri Neno la Mungu?
- Je, maisha yangu ya maombi binafsi na huduma ya maombi ya kanisa ninaloongoza yana ufanisi kiasi gani?
- Je, ninafanya vyema kiasi gani katika kukuza maadili ya Kipentekoste katika kanisa langu?
- Je, ninafanya vizuri kiasi gani katika kuwatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya huduma?

Andika majibu yako kwenye daftari lako. Halafu jiulize, "Nifanye nini tofauti ili kufikia vizuri kila moja ya vipaumbele hivi katika maisha na huduma yangu?" Tena, andika majibu yako kwenye daftari lako, na uendelee kuyaombea kila siku.

### Utekelezaji wa Vipaumbele

Ukishakubali vipaumbele hivi vya huduma kama vyako, unapaswa kuanza kuvitekeleza katika huduma yako mwenyewe na katika huduma za kanisa. Ili kufanya hivyo, unaweza kutaka kutumia mikakati ifuatayo:

*1. Ongeza uelewa.* Utahitaji kuongeza uelewa wako wa kile ambacho Biblia inafundisha kuhusu kila kimoja katika hivi vipaumbele saba vya huduma. Unaweza kufanya hivyo kwa kuchunguza Maandiko na kutafuta maelezo zaidi juu ya mada hizi. Yesu anatuagiza "tujifunze Maandiko kwa bidii" katika kutafuta ukweli (Yoh. 5:39). Unaposoma, jiulize, "Roho ananiambia nini?" Andika mapya uliyoyapata kwenye daftari lako. Ikiwezekana, tafuta na usome vitabu vizuri kuhusu mada hizi.[7]

Njia nyingine ya kuongeza uelewa wako wa masomo haya ni kuhubiri na kufundisha juu yake mara kwa mara. Mkakati huu hautaongeza tu uelewa wako wa mada, utawatayarisha washirika wako kwa hatua inayofuata ambayo ni utekelezaji wa vipaumbele hivi katika kanisa.

*2. Tengeneza utaratibu.* Kisha, itakuwa vizuri kuendeleza mpango wa kutekeleza vipaumbele hivi katika huduma yako mwenyewe na katika huduma za kanisa. Ili kufanya hivi utahitaji kuongeza uelewa wa kanisa wa kila kimoja ya vile vipaumbele saba. Unaweza kuanza kwa kujibu maswali yafuatayo:

- Je, nifanye nini ili kuliongoza kanisa langu kutumikia vyema utume wa Mungu?
- Je, nifanye nini ili kutimiza vyema zaidi wito wa Mungu juu ya maisha yangu na kwa kanisa ambalo ameniita kuliongoza?
- Je, nifanye nini ili kuliongoza kanisa katika kuwafikia waliopotea kwa ufanisi zaidi?
- Nifanye nini ili kuhubiri na kufundisha vyema Neno la Mungu kanisani?
- Je, nifanye nini ili kukuza maombi vizuri zaidi kanisani?
- Je, nifanye nini ili kuliongoza kanisa katika uzoefu na matendo makuu ya Kipentekoste?
- Je, nifanye nini ili kuwatayarisha vyema watu wa Mungu kwa ajili ya huduma?

Andika majibu yako kwenye daftari lako na uhakiki mara kwa mara.

*3. Fanyia kazi mpango wako.* Lazima sasa ufanyie kazi mpango wako. Hii ina maana kwamba utahitaji kusonga mbele ili kutekeleza mikakati uliyotengeneza. Unapoendelea na mpango wako, utataka kutathmini mara kwa mara maendeleo yako. Inapobidi, fanya marekebisho yoyote yanayohitajika kwenye mpango wako.

[7] Kitabu bora kuhusu utume wa Mungu kiko katika Mfululizo wa Masomo ya Ugunduzi wa Africa's Hope. Kinaitwa *Theolojia ya Kibiblia ya Umisheni,* cha Paul York.

Kumbuka, hautafanikiwa mara moja. Itachukua muda, na matatizo yanapokuja, utahitaji kuvumilia. Ikiwa utafanya hivi, baada ya muda, kanisa lako litaanza kubadilika. Litakuwa kanisa lenye nguvu ambalo Kristo anakusudia liwe. Hebu maneno ya mtume yakutie moyo: "Tena tusichoke katika kutenda mema, kwa maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho" (Gal. 6:9).

---

Kila mchungaji wa Kipentekoste katika Afrika lazima afananishe vipaumbele vyake vya huduma na vile vya Yesu na mitume. Basi, ni lazima kuruhusu vipaumbele hivi kuongoza huduma zao. Ingawa mchakato huu unaweza kuwa mgumu, ni kitu kinachostahiki. Kwa kujitoa kwa Kristo, kwa mapenzi ya Mungu, na nguvu ya kuhuisha ya Roho Mtakatifu, mchungaji wa Kipentekoste anaweza kufikia malengo yake ya huduma.

## ~ Sura ya 6 ~

# Vipaumbele vya Kibinafsi

Watoto wa mama yangu walinikasirikia na kunifanya nisimamie mashamba ya mizabibu; ikabidi nilipuuze shamba langu" (Wimbo 1:6). Haya ni maneno ya kuhuzunisha ya msichana Mshulami. Alikuwa ameshughulika sana kutunza mashamba ya wengine mpaka akaacha kushughulikia lake mwenyewe. Lakini, hakuwa anazungumza kuhusu mashamba halisi ya mizabibu; alikuwa akizungumzia maisha yake. Alikuwa amewekeza wakati mwingi kwa wengine mpaka maisha yake yakajaa magugu.

Kinachosikitisha ni kwamba, hali hii inaweza kuelezea maisha ya wachungaji wengi wa Kipentekoste katika Afrika leo. Wametumia muda mwingi kushughulikia mambo ya huduma, na kuhudumia mahitaji ya wengine, wameshindwa kujijali wenyewe. Matokeo yake, wote wawili wameteseka. Maisha yao wenyewe ya kiroho yamedhoofika, na makanisa wanayoongoza yamedhoofika.

Paulo alimteua Timotheo kusimamia kanisa la Efeso. Baadaye alimwandikia huyo mtumishi mwenzake kijana, na kumwonya: "Chunga maisha yako na mafundisho yako. Dumu katika hayo, kwa maana ukifanya hivyo, utajiokoa wewe mwenyewe pamoja na wale wanaokusikia" (1 Tim. 4:16). Basi Paulo alimshauri Timotheo, si tu kujali huduma yake ya hadharani, bali pia maisha yake ya kibinafsi. Mchungaji mwenye busara hatatanguliza tu huduma yake kwa wengine

kama tulivyo-ona katika Sura ya 5, bali pia atajijali na kujitunza. Sura hii itachunguza vipaumbele sita vya kibinafsi vya mchungaji wa Kipentekoste.

## KIPAUMBELE CHA KUMJUA KRISTO

Zaidi ya yote, mchungaji wa Kipentekoste lazima atangulize uhusiano wake na Kristo. Kabla ya mchungaji kumjulisha kwa wengine, ni lazima yeye mwenyewe amjue vyema. Je, mtu anawezaje kumtambulisha mtu asiyemjua, kwa mwingine?

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima umjue Kristo kiakili na kiuzoefu. Kwa maneno mengine, ni lazima uelewe Yesu ni nani na amefanya nini. Na lazima uwe umekutana Naye binafsi, ukiwa na uhusiano wa karibu Naye.

### Kumjua Yeye Ni Nani

Kumjua Kristo kiakili ni kujua ukweli juu yake. Ni kuelewa kile kinachosemwa na Biblia kwamba Yeye ni nani na kwa nini alikuja duniani. Biblia inafundisha yafuatayo kuhusu Kristo.

- Yeye ni Neno la milele la Mungu, Muumba wa vitu vyote (Yoh. 1:1 -4).
- Yeye ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili (1 Tim. 3:16).
- Yeye ndiye "Masihi, Mwana wa Mungu aliye hai" (Mt. 16:16).
- Yeye ndiye "njia ya kweli na uzima," njia pekee ya kwenda kwa Baba (Yoh. 14:6).

Biblia pia inaeleza kwa nini Kristo alikuja duniani:

- Alikuja "kutafuta na kuokoa waliopotea" (Lk. 19:10; taz. 1 Tim. 1:15).
- Alikuja "kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mk. 10:45; taz. Yoh. 12:27; Tito 2:13-14).
- Alikuja "kuharibu kazi ya Ibilisi" (1 Yoh. 3:8; taz. Ebr. 2:14).
- Alikuja "ili [sisi] tuwe na uzima, kisha tuwe nao tele" (Yoh. 10:10).

### Kumjua Yeye Binafsi

Ingawa ni muhimu kwamba mchungaji wa Kipentekoste ajue Yesu ni nani na alikuja kwa nini, hiyo haitoshi. Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima umjue Kristo kibinafsi. Lazima uwe umekutana na Bwana binafsi, na lazima uwe na uhusiano endelevu Naye.

Paulo alizungumza juu ya jambo hili la kwanza katika maisha yake mwenyewe. Aliwaandikia waamini wa Filipi, "Nataka kumjua Kristo, kujua

uweza wa ufufuo wake na kushiriki katika mateso yake, nifanane naye katika kifo chake" (Flp. 3:10). Hamu ya Paulo ya kumjua Kristo ilikuwa kubwa sana hata alikuwa tayari, si tu kushinda pamoja naye, bali kushiriki mateso yake. Alikuwa tayari hata kufa kwa ajili Yake. Mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na shauku kama ya Paulo ya kumjua Kristo.

**Kumjua Yeye**

Hiki kipaumbele cha kumjua Kristo kinaweza kutimizwa kwa njia tatu:

*1. Kupitia kukutana naye kibinafsi.* Mtu hupata kumjua Kristo kwanza kupitia kukutana naye kibinafsi. Hii ni kwa kila mtu, hata mchungaji wa Kipentekoste. Sauli wa Tarso alijua habari za Kristo; hata hivyo, hakumjua Yeye binafsi hadi alipokutana Naye akiwa njiani kwenda Dameski (Mdo. 9:1-9). Hapo, Sauli akapaza sauti na kusema, "Wewe ni nani, Bwana?" Yesu akajibu, "Mimi ni Yesu, ambaye wewe unamtesa" (mst. 5). Maisha ya Sauli yalibadilika. Alikuja kumjua Kristo kama Bwana na Mwokozi wake. Kwa muda mfupi, mtesa mbaya na katili sana wa Kanisa alibadilika na kuwa mhamasishaji wake mkuu.

Akitafakari tukio hili, Paulo aliandika, "Basi, mtu akiwa ndani ya Kristo, anakuwa kiumbe kipya. Ya kale yanapita, naye anakuwa kiumbe kipya!" (2 Kor. 5:17). Yeyote anayetamani kuwa mchungaji wa Kipentekoste lazima aanzie hapa. Yesu alisema, "Amin, amin, nakuambia, hakuna mtu awezaye kuuona ufalme wa Mungu bila kuwa amezaliwa mara ya pili" (Yoh. 3:3).

*2. Kupitia neno la Mungu.* Njia ya pili ambayo mchungaji wa Kipentekoste anaweza kumjua Kristo vyema zaidi ni kukutana Naye katika Biblia - hasa katika injili na nyaraka. Injili zinasimulia maisha Yake, kazi Zake, na mafundisho Yake. Nyaraka zinaeleza maana yake. Kwa kusoma injili, unaweza kutembea kwenye barabara zenye vumbi za Galilaya pamoja na Yesu. Unaweza kuketi miguuni pake na kusikiliza mafundisho yake. Unaweza kusimama na kumtazama akifa msalabani. Na unaweza kutazama ndani ya kaburi tupu la Mwokozi wako na kumsikia malaika akipaza sauti, "Hayupo hapa. Amefufuka!"

Mchungaji kijana mmoja wa Kipentekoste aliwahi kujisemea, "Wanafunzi wa Yesu walitumia miaka mitatu wakitembea Naye na kujifunza kutoka Kwake. Maisha yao yalibadilishwa. Nitafanya vivyo hivyo. Nitatumia miaka mitatu ijayo kusoma na kurudia zile injili nne." Kweli alipojitoa hivyo, huyo mhubiri kijana alitumia miaka mitatu iliyofuata kusoma injili. Kila saa aliitumia kuzama katika hadithi ya Yesu. Baada ya hapo, maisha na huduma yake vilibadilika.

*3. Kwa njia ya maombi.* Njia ya tatu ambayo mchungaji wa Kipentekoste anaweza kumjua Yesu ni kupitia maombi. Biblia inazungumza juu ya aina nyingi za maombi, ikiwa ni pamoja na sala, toba, maombezi, shukrani, na kuomba katika Roho. Hata hivyo, aina ya maombi ambayo yatamsaidia mchungaji kumjua Yesu vizuri zaidi ni maombi ya ushirika. Yakobo alizungumza juu ya aina hii ya maombi. Alihimiza hivi: "Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi" (Yakobo 4:8). Musa pia alifanya maombi ya ushirika. Biblia inasema kwamba alizungumza na Mungu "uso kwa uso, kama mtu asemavyo na rafiki" (Kut. 33:11).

Mariamu, dada yake Martha, ni mfano mzuri wa hilo. Yesu alipomtembelea nyumbani kwake, aliketi miguuni pake akisikiliza kwa makini kila neno alilosema. Dada yake alilalamika, akimshutumu kuwa mvivu. Hata hivyo, Yesu alimsifu Mariamu, akisema, "[Yeye] amechagua lililo bora zaidi, wala halitaondolewa kwake" (Lk. 10:38-42). Kumjua Yesu lazima iwe kipaumbele cha kila mchungaji wa Kipentekoste. Mazoezi haya yataathiri vizuri sana maisha na huduma yake kuliko kitu kingine chochote.

## KIPAUMBELE CHA KUENENDA KATIKA ROHO

Mchungaji wa Kipentekoste hapaswi kuweka kipaumbele kwenye kumjua Kristo tu, bali pia kwenye kuenenda na kuishi katika Roho. Paulo aliwaonya Wakristo wa Galatia kwamba: "Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho" (Gal. 5:25).

### Maana ya Kuenenda kwa Roho

Kuenenda kwa Roho kunamaanisha angalau mambo matatu:

*1. Kujazwa na Roho.* Kwanza, maana yake ni kujazwa na Roho (Mdo. 1:4-8). Yaani, kabla ya mtu kuenenda kwa Roho, ni lazima kwanza ajazwe na Roho Mtakatifu kama ilivyokuwa kwa wanafunzi ile siku ya Pentekoste (Mdo. 2:1-4). Baada ya kupokea Roho, wanafunzi walianza kuishi na kuhudumu katika nguvu za Roho. Kitabu cha Matendo kinasimulia hadithi ya kusisimua ya huduma yao iliyotiwa nguvu na Roho. Kila mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na uzoefu huu muhimu.

*2. Kuongozwa na Roho.* Pili, kuenenda kwa Roho ni kuongozwa na Roho. Mchungaji wa Kipentekoste lazima awe msikivu kwa sauti ya Roho Mtakatifu. Kisha, wakati Roho anaposema, lazima kutii. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya. Kwanza, alijazwa na Roho Mtakatifu. Kisha, aliongozwa na Roho (Lk. 3:21-22 na 4:1). Paulo pia na timu yake ya wamishenari waliongozwa na Roho Mtakatifu

(Mdo. 16:6-10). Ndivyo ilivyo kwa wachungaji wa Kipentekoste leo. Kama Yesu na Paulo, wao pia lazima waongozwe na Roho Mtakatifu.

*3. Kuhudumu katika Roho*. Mwisho: kuenenda katika Roho maana yake ni kuhudumu katika nguvu za Roho. Yesu aliahidi kwamba, "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Mdo. 1:8). Hayo yalitokea kwa Yesu na mitume wake. Walijazwa na Roho Mtakatifu na wakaanza kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu (kwa mfano, Lk. 3:21-22 na 4:14; Mdo. 4:31-33). Unapoenenda katika Roho, wewe pia tarajia Roho atie nguvu huduma yako.

**Jinsi ya Kuenenda Katika Roho**

Hapa swali linatokea: Wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kufanya nini ili kuhakikisha kwamba unaishi na kuenenda katika Roho? Kama tulivyokwisha ona hapo juu, cha kwanza ni kuhakikisha kwamba umejazwa na Roho kwa kweli. Unapojazwa na Roho, kuna ushahidi wa kiBiblia kwamba, kwanza utanena kwa lugha kama Roho atakavyokuwezeshsa kutamka (Mdo. 2:4; 10:44-46; 19:6). Pili ni kwamba utapokea nguvu zisizo za kawaida za kumshuhudia Kristo (Mdo. 1:8; 4:31).

Mara tu unapojazwa na Roho Mtakatifu, weka moyo wako wazi ili kuongozwa na Roho Mtakatifu. Ndivyo ilivyokuwa kwa waamini wa kwanza katika kitabu cha Matendo. Katika Mkutano Mkuu wa kwanza wa kanisa huko Yerusalemu, mitume na wazee walifanya uamuzi kuhusu kujumuishwa kwa waamini wa Mataifa katika kanisa. Walianza barua yao kwa kusema, "Ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi" (Mdo. 15:28). Walitaka wasomaji wao wajue kwamba walikuwa wamesikiliza sauti ya Roho kabla ya kufanya uamuzi wao. Jambo moja ambalo linaweza kukusaidia kuenenda na kuishi katika Roho ni kila siku kuwa na muda wa kuomba katika Roho Mtakatifu (Rum. 8:26-27; Efe. 6:18).[1]

[1] Kupata zaidi kuhusu maisha ya maombi ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi."

## KIPAUMBELE CHA UKUAJI NA MAENDELEO BINAFSI

Pamoja na kumjua Kristo na kutembea katika Roho, mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na kipaumbele cha ukuaji na maendeleo ya kibinafsi. Daima ajitahidi kuwa bora kiasi anachoweza kuwa kwa ajili ya Bwana.

Akilinganisha maisha na shindano la riadha, Paulo aliwahimiza Wakristo wa Korintho watafute ubora. Akawakumbusha hivi: “Je, hamjui kwamba katika shindano la mbio wote wanaokimbia hukimbia, lakini ni mmoja tu anayepokea tuzo?” Kisha akawahimiza kwa kusema: “Kimbieni kwa njia ambayo mtapata tuzo” (1 Kor. 9:24). Pia aliwahimiza Wakolosai hivi: “Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo kama kumtumikia Bwana” (Kol. 3:23).

Mtazamo huo wa ubora haurithiwi kutoka kwa mababu wa mtu, wala hautolewi kwa kuwekewa mikono. Kufikia ubora katika huduma kunahitaji umakini, uamuzi, na nidhamu. Kutafuta ubora sio kujaribu kuwa bora kuliko mtu mwingine. Badala yake, ni kuwa bora kadiri uwezavyo kuwa katika kumtumikia Bwana.

Eneo moja ambalo mchungaji wa Kipentekoste lazima afuatilie ubora ni katika tabia zake za kusoma. Lakini kwa bahati mbaya, kuna tabia kwa baadhi ya wachungaji wa Kipentekoste kudharau kusoma. Kwa kutilia mkazo yaliyotolewa, wanapunguza utafutaji wa maarifa yaliyopatikana. Ila Biblia inafundisha kwamba, “moyo wa mwenye ufahamu hupata maarifa, kwa maana masikio ya wenye hekima huyatafuta” (Mit. 18:15).

Kwa hiyo, kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima utafute bila kuchoka kuongeza ujuzi wako wa Maandiko. Wakati huo huo, lazima ujitahidi kujiweka sawa na mwenendo wa sasa katika jamii. Ndipo utakapoweza kuchanganya haya mawili, ukitumia kwa namna ya kinabii kweli za kiBiblia kwa ajili ya nyakati za leo. Zaidi ya hayo, lazima uwe na mazoea ya kusoma vitabu vizuri vya waandishi wanaotambulika. Jambo hilo litaongeza ujuzi wako wa kufikiri. Ubora katika masomo utasaidia kutoa ubora katika huduma.

## KIPAUMBELE CHA KUJIJALI (KUJITUNZA)

Mchungaji mmoja wa Kipentekoste alikuwa akichoka sana na kujisikia maumivu ya mwili. Akaenda kwa daktari, akihofia kwamba amepatwa na ugonjwa hatari. Lakini baada ya kumchunguza, daktari alimwambia kuwa dalili zake zilisababishwa na msongo wa mawazo. Daktari alimwamuru kupumzika na kula

vizuri. Matibabu hayo yalifanya kazi! Punde si punde mchungaji alipata nguvu tena na kuendelea katika huduma.

Wachungaji wa Kiafrika wanajulikana kuwa wachapa kazi. Ni vizuri. Lakini, wanapaswa kujihadhari na tabia ya kuwa kila kitu kwa kila mtu. Mchungaji aliyechoka anaweza kuwa mzigo kwa familia na kwa kanisa lake. Kuzidiwa na kazi kunaweza kulemaza uwezo wa mchungaji kuomba, kusoma, na kuhubiri. Hali hiyo inaweza kuathiri sana jinsi anavyoshirikiana na hadhara ya watu, na kumfanya aonekane kutojali kuhusu watu. Na hali hiyo inaweza, kwa upande wake, kumfanya asikubalike katika kusanyiko na kumwongezea mchungaji husika msongo wa mawazo.

Wachungaji wa Kipentekoste wakati mwingine hukwepa kupumzika. Wanaona kwamba wakichukua muda wa kupumzika, wanakuwa sio waaminifu kwa wito wao. Hata hivyo, Yesu alielewa hitaji la kupumzika. Wakati fulani aliwaambia wanafunzi wake, "Njoni pamoja nami peke yenu mahali pa utulivu mpate kupumzika" (Mk. 6:31).

Mchungaji mwenye bidii anahitaji kukumbuka kwamba hata Mungu mwenyewe alipumzika siku ya saba ya uumbaji (Mwa. 2:2). Hakufanya hivyo kwa sababu alikuwa amechoka, bali ili kutoa mfano kwa wanadamu. Yesu alisema, "Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato" (Mk. 2:27). Mungu alitoa Sabato kama njia ya watu wake kumheshimu Muumba wao, na kama wakati wa kupata nguvu wanazohitaji ili kukabiliana na mahitaji ya maisha. Kanuni ya mapumziko ya Sabato inapokiukwa, inaweza kuleta hali ya kutofaulu katika huduma.

Kwa hiyo mchungaji wa Kipentekoste lazima atenge siku moja kila juma kwa ajili ya kupumzika na kurejesha nguvu yake. Na awajulishe watu kwamba hii ni siku ya mapumziko ya mchungaji, yaani Sabato yake. Mchungaji anapaswa kutumia hiyo siku kwa burudani akifurahia kukaa na mwanandoa mwenzake pamoja na watoto.[2]

## KIPAUMBELE CHA UTAKATIFU BINAFSI

Makala ilitokea katika gazeti moja la Afrika Mashariki ikisimulia kuhusu mchungaji mmoja mashuhuri ambaye alimtaliki mke wake kwa sababu ya tabia

[2] Kwa habari zaidi kuhusu kujijali na kujitunza, tazama Sura ya 13: "Maisha Yanayosimamiwa Vizuri."

yake ya uzinzi. Alikataa kumsamehe na akachagua kuoa tena. Mwanamume mmoja alipoona alichofanya mchungaji huyo alimwambia mke wake, "Kama mchungaji aliachana na mke wake, unafikiri wewe ni nani?" Yeye pia akamwacha mke wake kwa ajili ya mwanamke mwingine. Kama mchungaji, matendo yako bila shaka yataathiri maisha ya wale unaowaongoza, vizuri au vibaya.

Kama mchungaji wa Kipentekoste, Mungu anakuita uishi maisha ya mfano na ya kuigwa. Petro aliandika hivi: "Kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, iweni watakatifu katika kila mfanyalo; kwa maana imeandikwa, Iweni watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu" (1 Pet. 1:15-16). Paulo aliandika kwamba mwangalizi lazima aishi maisha "yasiyo na lawama, awe mwaminifu kwa mkewe, mwenye kiasi, anayejitawala na kujiheshimu,…sio mlevi" (1 Tim. 3:2-3). Aliongeza kwamba mwangalizi "lazima pia awe na sifa njema kwa watu wa nje" (mst. 7). Mtume alimwambia Tito kwamba, mzee "asiwe na lawama…mtu apendaye mema, mwenye kiasi, mwadilifu, mtakatifu na mwenye nidhamu" (Tito 1:7-8).

Barani Afrika, wachungaji wanaheshimiwa sana. Wanawagusa watu moja kwa moja na kwa njia isiyo moja kwa moja. Wanawashawishi moja kwa moja kwa maneno yao - kwa kile wanachosema. Wanawagusa kwa njia isiyo ya moja kwa moja na maisha yao - kwa kile wanachofanya. Wanachofanya wachungaji mara nyingi huwa na ushawishi zaidi kuliko kile wanachosema. Wakati mmoja kuna mshirika aliyemwambia mchungaji wake, "Unachofanya kinatoa sauti kubwa sana kiasi kwamba siwezi kusikia unachosema." Kwa hiyo kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufanye kuishi maisha ya utakatifu kuwa mojawapo ya vipaumbele vyako muhimu.

## KIPAUMBELE CHA USIMAMIZI WA MUDA

Wapentekoste wanathamini hali ya upekee na kujieleza katika ibada zao. Wanathamini Roho kuongoza na kuingilia kati, si vitu vinavyosomwa kama liturjia. Maadili haya ni mazuri, na hayapaswi kamwe kuachwa. Lakini, mchungaji wa Kipentekoste hapaswi kamwe kuvitumia hivyo kama kisingizio cha matumizi mabaya ya muda. Kama ulivyo msimamizi wa fedha ambazo Mungu ameweka mikononi mwako, wewe pia ni msimamizi wa muda ambao Mungu amekupa. Kwa hivyo lazima ujitoe kuwa msimamizi mzuri wa muda.

Wachungaji wengine hawana nidhamu na muda wao, na wana mazoea ya kuchelewa kufika kwenye ahadi za kukutana na watu. Hawa wachungaji wanaweka mfumo mbaya kwa makanisa wanayoongoza. Tabia yao ya kutojali

inapunguza uaminifu wao kwa watu. Inakuwa sehemu ya utamaduni wa kanisa kitaasisi na kuzuia maendeleo yake.

Kwa upande mwingine, usimamizi mzuri wa muda utakuwezesha kuliongoza kanisa kwa ufanisi zaidi. Utaweza kutenga muda kwa ajili ya masomo, shughuli za utawala, kutembelea, ushauri nasaha, na masuala ya familia. Udhibiti mzuri wa muda ni pamoja na kutayarisha ratiba ya shughuli kama vile kuweka malengo ya kila siku, kutengeneza orodha inayoweza kutekelezeka ya mambo ya kufanya, kuweka kipaumbele kwa kazi kulingana na umuhimu na uharaka, na kuweka kikomo cha muda wa kukamilisha kila kazi.

---

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ukusudie jinsi unavyoishi maisha yako na kuendesha huduma yako. Lazima uweke vipaumbele vya kibinafsi kwa makusudi. Basi, inabidi ukaishi kulingana na vipaumbele hivyo. Ikiwa utafanya mambo haya, utabarikiwa, na watu unaowaongoza pia watabarikiwa.

~ Sura 7 ~

# Vipaumbele vya Familia

Mchungaji wa kanisa moja kubwa katika jiji moja la Afrika Mashariki aliwashirikisha watu hadithi ya kuhuzunisha ya babu yake mzaa mama. Kwa miaka kadhaa, babu yake alikuwa mchungaji wa kanisa la Kipentekoste. Lakini siku ikafika ambapo aliiacha familia yake na imani yake na kujitwalia wake watatu. Kwa sababu ya kushindwa huko kunakosikitisha, hakuna hata mmoja wa watoto wake aliyemfuata Bwana, isipokuwa mke wa huyo mchungaji. Huyu mchungaji akatoa ushuhuda kwamba, “Mimi ni zao la uaminifu wa mama yangu. Yeye ndiye aliyenishawishi nimfuate Bwana.” Leo, mchungaji huyu anajulikana kwa mafundisho yake na kuhubiri juu ya mambo ya familia.

Ukweli wa kusikitisha ni kwamba hata wachungaji wa Kipentekoste wakati mwingine wanahangaika katika ndoa zao na watoto wao. Kwa sababu hii, lazima waweke kipaumbele cha juu sana katika kukuza uhusiano wao na familia zao. Kwa mchungaji, kufanikiwa katika maisha yake ya nyumbani ni kufanikiwa mno; kushindwa ni kushindwa kabisa. Sura mbili zilizopita zilishughulikia huduma ya mchungaji wa Kipentekoste na vipaumbele vya kibinafsi. Sura hii itashughulikia vipaumbele vyao kifamilia.

## MAHUSIANO KATIKA FAMILIA

Biblia inazungumza kuhusu uhusiano wa mchungaji na familia yake. Paulo aliandika hivi kuhusu mchungaji, "Imempasa kuisimamia nyumba yake mwenyewe vema na kuona kwamba watoto wake wanamtii, na afanye hivyo kwa namna inayostahili heshima kamili." Kisha akauliza swali linalojijibu lenyewe: "Ikiwa mtu yeyote hajui kuisimamia familia yake mwenyewe, atawezaje kulitunza kanisa la Mungu?" (1 Tim. 3:4-5). Maagizo mbalimbali ya Biblia kwa waume, wake, na watoto yanahusu pia nyumba ya mchungaji (rej. Mwa. 2:24; Mk. 10:6-9; 1 Kor. 11:3; Efe. 5:22-33; 6: 1-4; Kol. 3:18-21; 1 Pet. 3:1-7).

### Utaratibu Wa Kibiblia

Kama mchungaji wa Kipentekoste, maisha yako ya nyumbani lazima yaende kwa mujibu wa Maandiko. Katika tamaduni zinapopinga Maandiko, ni lazima sikuzote wewe ukubaliane na Maandiko, ukihakikisha kwamba jinsi unavyofanya wewe na mwanandoa mwenzako na watoto wako vinalingana na mafundisho ya Neno la Mungu.

Kwa mfano, tamaduni nyingi za Kiafrika humwona mume kuwa mtawala wa familia asiyepingwa. Neno lake, hata kama halieleweki vizuri, halipaswi kutiliwa shaka. Lakini Yesu alionyesha aina tofauti ya uongozi. Akizungumza juu yake mwenyewe, alitangaza na kusema, "Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mk. 10:45).

Hivyo, Bwana alionyesha aina ya uongozi anaoutarajia kutoka kwako kama mume Mkristo. Uongozi wako katika familia unapaswa kufafanuliwa kwa unyenyekevu na kujali bila ubinafsi kwa mke wako na watoto. Paulo alifafanua mada hii ya uongozi wa utumishi, akiwahimiza waume, "Wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Efe. 5:25).

Paulo alieleza jinsi nyumba ya Kikristo inavyopaswa kuwa, kama ifuatavyo: "Kwa maana mume ni kichwa cha mke, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa, mwili wake, naye ni mwokozi wake" (Efe. 5:23). Katika sehemu nyingine, mtume aliandika hivi: "Enyi waume, wapendeni wake zenu na msiwe wakali kwao. Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika kila jambo, kwa maana hilo humpendeza Bwana. Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa" (Kol. 3:19-21). Katika mazingira hayo yenye utaratibu mzuri, ndoa yenu inaweza kukua na watoto wenu waweza kusitawi.

**Kunyenyekeana**

Biblia inafundisha kwamba uhusiano kati ya mume na mke lazima uwe wa kunyenyekeana. Paulo aliandika kwamba waume na wake wanapaswa "kunyenyekeana kwa kumcha Kristo" (Efe. 5:21). Ingawa mume ndiye kichwa cha mke, yeye kama Yesu anapaswa kujinyenyekeza kwa uamuzi wake na kumtumikia mwenzake kwa unyenyekevu. Na huyo mwingine anapaswa afanye vivyo hivyo. Badala ya jambo hilo kushusha hadhi yako kama mchungaji, huduma ya unyenyekevu ya aina hiyo kwa familia itaongeza heshima yako katika kanisa na jamii.

**Upendo na Heshima**

Zaidi ya hayo, uhusiano wako na familia yako unapaswa kuonyeshwa kwa upendo na kuheshimiana. Paulo aliwasihi waume, "Wapendeni wake zenu, kama Kristo alivyolipenda kanisa na kujitoa kwa ajili yake" (Efe. 5:25). Baadaye aliongeza, "Kila mmoja wenu ampende mke wake kama anavyojipenda mwenyewe, na mke na amheshimu mume wake" (mst. 33). Kinyume chake pia ni kweli; mke lazima ampende mumewe, na mume amheshimu mke wake. Kwa kufanya mambo haya, familia ya wachungaji itakuwa kielelezo kwa wengine.

**Uhalisia**

Zaidi ya hayo, uhusiano wako na familia yako lazima uwe na sifa ya uhalisia. Hii ina maana kwamba lazima uwe mtu yule yule nyumbani kama ulivyo mbele ya watu. Lazima uonyeshe nia ya dhati katika kile kinachotokea katika maisha ya mwenzi wako na watoto. Wakiwa nyumbani, watoto lazima wasikie sauti ya baba au mama yao, si sauti ya mhubiri ambaye yuko mbali na uhalisia wa maisha yao.

## CHANGAMOTO KWA WACHUNGAJI WA KIKE

Neno kwa wachungaji wa kike na familia zao linafaa hapa. Wachungaji wanawake walioolewa barani Afrika wanajikuta katika nafasi ya kipekee na yenye changamoto. Mungu amewaita kuongoza kanisa. Ila pia wanapokuwa nyumbani, amewaita kuwaheshimu waume zao na kujinyenyekeza chini ya mamlaka yao. Hii inaweza kuwa hali ngumu kudhibiti.

Zaidi, tamaduni nyingi za Kiafrika zinapinga uongozi wa kike. Ila - na Mungu ashukuriwe - katika maeneo mengi mtazamo huu unabadilika. Kwa sababu hiyo, baadhi ya washirika wa kanisa wanasitasita kufuata uongozi wa mchungaji wa kike au kumruhusu kufanya kazi fulani za kichungaji.

Kwa hiyo ni muhimu sana kwamba mume wa mchungaji amuunge mkono mke wake katika huduma yake. Zipo nyakati fulani ambapo ni lazima awe tayari kujinyenyekeza na kumwunga kwa njia nyingi zinazoonekana kuwa kinyume na utamaduni uliozoeleka. Kwa mfano, nyakati fulani fulani, kwa sababu ya kazi nyingi za mke, mume anapaswa kuwa tayari kujinyenyekeza, kuwakaribisha wageni na kuwakirimu, na kusaidia kwa njia yoyote awezayo. Kwa upande mwingine, mchungaji mwanamke hapaswi kutumia kazi zake za kihuduma kama kisingizio cha kupuuza wajibu wake wa nyumbani kwa mume na watoto wake.

Hii itahitaji kiwango cha kipekee cha ukomavu na kubadilika kwa upande wa mchungaji wa kike na mumewe. Ni lazima watangulize uhusiano wao wawili zaidi ya yote, na lazima wajifunze kuwasiliana vizuri.

## KUSIMAMIA FAMILIA VIZURI

Mchungaji wa Kipentekoste si tu kwamba anatakiwa aweze kulisimamia kanisa lake ipasavyo, bali pia lazima asimamie familia yake ipasavyo. Kama tulivyo ona hapo juu, Paulo alimkumbusha Timotheo kwamba mwangalizi "lazima asimamie familia yake vema" (1 Tim. 3:4). Baadaye alimwandikia Tito hivi, "Imempasa mzee awe mtu asiye na lawama, mwaminifu kwa mkewe, mwanamume ambaye watoto wake wanaamini, wasioshitakiwa kuwa wapotovu na wasiotii" (Tito 1:6).

Wajibu huu muhimu unahusisha kuongoza, kulinda, na kutunza mke na watoto wake. Biblia inafundisha kwamba mwanamume anapaswa kuhusiana na mke wake kama Kristo anavyohusiana na kanisa (Efe. 5:25-27). Zaidi ya hayo, anapaswa kuwaangalia watoto wake kwa juhudi ile ile itokanayo na upendo ambao Baba yake wa mbinguni anao. Mtu mmoja mwenye hekima alishauri hivi: "Waongoze watoto katika njia iwapasayo kuiendea, na hata watakapokuwa wazee hawataiacha" (Mith. 22:6).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, uongozi wako wa familia yako unahusisha angalau maeneo matatu:

### Maendeleo Kiroho

Kwanza, lazima ujishughulishe na ukuaji wa kiroho wa familia yako. Kama Ayubu, lazima uongoze familia yako kwa makusudi kabisa katika mambo ya kiroho (Ayubu 1:4-5). Njia moja ya kufanya hivyo ni kwa kufanya ibada za pamoja na familia yako. Katika nyakati hizi za ibada, wafundishe watoto wako

kuomba na kusoma na kushika Maandiko kwa kichwa. Zaidi, fanya bidii watoto wako wamjue Kristo kama Mwokozi, na wabatizwe katika Roho Mtakatifu.

**Maendeleo Kibinafsi**

Pili, lazima usimamie maendeleo binafsi ya familia yako. Wewe na mwanandoa mwenzako mnapaswa kuwatengeneza watoto wenu wawe watu wakomavu, Wakristo waliojitoa, na raia wanaotii. Isitoshe, wafundishe watoto wako jinsi ya kutumia pesa kwa busara. Watoto wako wanapokua na kukomaa zaidi, waruhusu wasaidie katika usimamizi wa fedha za familia. Kwa njia hii, watajifunza kutofautisha mahitaji na matakwa, au vitu visivyokuwa mahitaji.

**Maendeleo Kijamii**

Mwisho: wewe na mwanandoa mwenzako mnapaswa kuzingatia maendeleo ya kijamii ya watoto wenu. Maisha ya nyumbani ya familia yanapaswa kuandaa mazingira sahihi kwa watoto kukua katika ufahamu wao kijamii. Lazima uwafundishe kutambua tofauti kati ya marafiki wazuri na wabaya. Wafundisheni jinsi ya kuhusiana na wengine katika ngazi mbalimbali za kijamii.

## VIPAUMBELE KUHUSU MWENZI

Biblia husema waziwazi kuhusu wajibu wa mume kwa mke wake. Bila shaka wajibu huo unamhusu mchungaji wa KiPentekoste. Kama mtu mcha Mungu, wajibu zako kwa mwanandoa mwenzako ni pamoja na hizi zifuatazo:

**Onyesha Upendo**

Paulo aliandika kwamba mume anapaswa “kumpenda mke [wake] kama Kristo alivyolipenda kanisa” (Efe. 5:25). Upendo wa Kristo kwa kanisa ulikuwa wa kujitoa dhabihu, usio na ubinafsi. Upendo wako kwa mke wako unapaswa kuwa sahihi. Unapaswa kutangaza upendo wako kwa mke wako faraghani na hadharani. Unapokuwa peke yako naye, unapaswa kumwambia mara nyingi, "Nakupenda." Unapokuwa mbele ya watu, unapaswa kuonyesha waziwazi upendo wako kwa mke wako. Kwa mfano, unaweza kutangaza kanisani, “Nimebarikiwa kwamba leo mke wangu yuko pamoja nami hapa. Ni mke wa ajabu na mama mzuri kwa watoto wetu. Ninampenda sana.”

Vitendo hivi na vingine vizuri vitakusaidia kuwa na uhusiano na mke wako na kanisa lako. Unapaswa pia kuonyesha upendo wako kwa mkeo kwa matendo yako, yaani, kwa kuzungumza naye kwa upole, kumpendelea kuliko wewe mwenyewe, na kwa kumsaidia katika majukumu yake.

**Saidia**

Jukumu la pili ambalo wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unalo kuhusu mke wako na watoto wako ni kuwajali na kuwategemeza. Petro aliwaandikia waume, "Iweni wa kujali mnapoishi na wake zenu, na muwatendee kwa heshima" (1 Pet. 3:7).

Ukiwa mwanamume Mkristo, unahitajika kumtegemeza mke wako na watoto wako kimwili kwa kuwaandalia makao, chakula, na mavazi ya kutosha. Ingawa mke wako na watoto wako wakubwa wanaweza kusaidia katika eneo hili, wewe, kama mkuu wa familia, ndiyo mwenye jukumu la kwanza.

Njia nyingine muhimu unayoweza kumsaidia mke wako ni kwa kumsaidia kutimiza wito wake wa kibinafsi katika huduma. Kauli mbiu yako inapaswa kuwa, "Ikiwa siwezi kumsaidia mke wangu kufikia uwezo wake, nitalisaidiaje kanisa langu kufanya vivyo hivyo?" Ili kufanya hivyo, utahitaji kukiri wazi kwamba Mungu ana mwito katika maisha ya mke wako, kama vile alivyo na wito kwa maisha yako. Ni lazima basi utembee naye kwa maombi na ushauri, ukimsaidia kutambua na kufuata mapenzi ya Mungu kwa maisha yake.

**Ulinzi**

Wajibu wa tatu ulio nao kuhusu mke wako ni kumlinda dhidi ya mashambulizi ya kimwili, kihisia na kiroho. Kwanza kabisa, lazima umlinde kimwili. Biblia inamwita mke "mwenzi dhaifu" katika uhusiano wa ndoa (1 Pet. 3:7). Wewe kama mwenye nguvu zaidi, unapaswa kumlinda mke wako kila wakati, ukiwa tayari kumlinda dhidi ya mashambulizi ya kimwili. Kujua hili kutamfanya ajisikie salama na mwenye kuthaminiwa.

Zaidi ya hayo, ni lazima umlinde mke wako kutokana na madhara ya kihisia. Kwa bahati mbaya, mara nyingi mke wa mchungaji ndiye anayepingwa na kukosolewa zaidi. Wakwe zake na washirika kanisani mara nyingi humkosoa yeye na watoto wake. Wengine hushindwa kuonyesha jinsi wanavyothamini yote anayofanya. Hili linaweza kumuumiza sana. Unapaswa kufahamu hali hii katika kanisa, na unapaswa kumlinda mke wako na kumpa usaidizi wa kihisia anaohitaji.

Mwisho: kwa kuwa mke wa mchungaji ndiye shabaha kuu ya Shetani, lazima umlinde kiroho. Unaweza kufanya hivyo kwa kumjengea ukuta wa maombi kumzunguka. Pia, inapobidi, lazima usimame katika pengo kati yake na adui (Eze. 22:30).

## VIPAUMBELE KWA WATOTO

Mchungaji wa Kipentekoste lazima pia awape watoto wake kipaumbele. Zaidi ya wajibu wake wa kumpenda na kumtunza mke wake, ana wajibu wa kuwapenda na kuwatunza watoto wake. Anapaswa kuwajali kama vile Baba yake wa Mbinguni anavyomjali. Anapaswa "kuwalea katika adabu na maonyo ya Bwana" (Efe. 6:4).

Kama mcha Mungu na baba Mkristo, wewe una majukumu matatu ya msingi kuhusu watoto wako:

### Kuwa Mfano wa Upendo wa Mungu

Kwanza, ni lazima uwe kielelezo cha upendo wa Mungu kwa watoto wako. Watoto hupata uelewa wao mwingi kuhusu Mungu kwa kumtazama baba yao. Ikiwa baba yao wa duniani ni mwenye fadhili na upendo, watamwona Baba yao wa Mbinguni kuwa mwenye fadhili na upendo. Ikiwa baba yao wa kidunia ni jeuri, watoto watamwona Mungu hivyo hivyo. Unapo-onyesha sifa za kiungu kama vile upendo, heshima, huduma, na uaminifu, watoto wako wataweza kukubali mafundisho na adhabu utakazotoa nyumbani. Biblia inaeleza asili ya kweli ya upendo:

"Upendo huvumilia, upendo ni mwema. Hauna wivu, haujisifu, hauna kiburi. Hauwavunjii wengine heshima, haujitafutii mambo yake wenyewe, haukasiriki upesi, hauweki kumbukumbu ya makosa. Upendo haufurahii ubaya bali hufurahi pamoja na ukweli. Daima hulinda, daima huamini, daima hutumaini, daima huvumilia. Upendo haushindwi kamwe." (1 Kor. 13:4-8)

Hiyo ndiyo aina ya upendo unaopaswa kuonekana na watoto wako.

### Waongoze Kwenda kwa Kristo

Zaidi ya kuwaonyesha upendo wa Mungu, ni lazima uwaongoze watoto wako kuwa na uhusiano binafsi na Yesu Kristo. Wakati mzuri wa kufanya hivi ni katika ibada za familia. Katika ibada hizi, unaweza kuwasilisha mpango wa wokovu kwa watoto wako. Kisha, wakati ufaao, unaweza kuomba pamoja nao ili wampokee Kristo kama Mwokozi wao. Baada ya hilo kufanyika, ni kitu muhimu kwa watoto kutangaza hadharani kumfuata Kristo kwao kwa njia ya ushuhuda na ubatizo wa maji. Unapaswa pia kutafuta fursa za kuwaongoza watoto wako katika ubatizo wa

Roho Mtakatifu. Basi, unapaswa kuwahimiza wawashirikishe rafiki zao imani waliyopokea.[1]

**Tengeneza Tabia Zao**

Unapaswa kuwa na mpango wa kutengeneza tabia ya watoto wako. Wewe na mwanandoa mwenzako mnapaswa kuwafundisha mema na mabaya na jinsi ya "kukataa kila aina ya uovu" (1 The. 5:22). Unapaswa pia kuwafundisha watoto wako kuwa wenye adabu, fadhili, na kutii mamlaka, pamoja na umuhimu wa kuwa wakweli na kufanya kazi kwa bidii. Maelekezo haya yatasaidia sana katika kuwawezesha kufanikiwa maishani.

Unaweza kufanya mambo haya kwa kuonyesha maisha matakatifu nyumbani, na kwa kuzungumza vizuri masuala ya maadili na watoto wako. Watoto wako wanapowaona wazazi wao wakitenda Kwa uadilifu na kwa unyofu, bila shaka nao watataka kukufuata. Wakati fulani utahitaji kuwaadhibu watoto wako kwa upendo ili kuwaepusha na mazoea ya kipumbavu na yenye kuumiza (Mit. 29:15).

## KUSAIDIA WANAUKOO

Lazima pia uonyeshe kuzijali familia yako na ya mwanandoa mwenzako kwa upendo. Familia hii kubwa ni pamoja na wazazi, kaka na dada, wajomba, mashangazi na hata wengine – au, wanaukoo. Paulo aliandika, "Yeyote asiyewajali na kuwatunza wa nyumbani mwake hasa, ameikana imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini." (1 Tim. 5:8)

Hata hivyo, kuna nyakati ambapo matakwa ya wanaukoo yatakuwa kinyume na Maandiko. Kwa mfano, ukoo unaweza kutaka kulazimisha mambo yasiyo ya kiBiblia kwa familia yako kama vile tohara ya kitamaduni au kumpa jina mtoto aliyezaliwa kwa taratibu za kimila. Katika matukio kama haya, kwa upendo mwingi na uthabiti kataa chochote kinachopendekezwa.

Njia nyingine ambayo ukoo unaweza kukulazimisha wewe na familia yako kufanya yasiyofaa ni kwa kuhamia nyumbani mwako kwa muda mrefu. Kwa sababu hiyo, kunakuwa na upotevu wa rasilimali za kifedha, kiakili, na kihisia za familia yako. Madai makubwa zaidi mara nyingi huwekwa kwa mke wa mchungaji. Anaweza kushinikizwa, hata kufikia hatua ya kuchoka. Katika hali

[1] Ili kupata habari zaidi kuhusu jinsi ya kufanya hivyo, tazama Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

kama hizi, kama mkuu wa nyumba, lazima uchukue udhibiti wa hali hiyo na uweke mipaka itakayosaidia.

Unapaswa kukumbuka shauri la Paulo kwa Timotheo, kama lilivyotajwa hapo juu, kwamba mtu lazima atunze watu wa jamaa yake, "hasa watu wa nyumbani mwake." Ukiwa mwanamume Mkristo, wajibu wako mkuu si kwa ukoo bali kwa mke na watoto wako. Kwa hiyo huenda ikawa lazima kumkumbusha mtu wa ukoo atakayejisikia vibaya kwamba Biblia imetoa ushauri huu kwako: "jiepusheni na kila mwamini ambaye ni mvivu na msumbufu" (2 The. 3:6), na kwamba "mtu ambaye hataki kufanya kazi asile" (mst. 10).

Badala ya kujaribu mara kwa mara kukidhi matakwa ya wanafamilia, wewe na mwenzi wako mnapaswa kuamua kwa uangalifu mtawasaidiaje. Ili kufanikiwa hapo, itabidi mkubaliane kuhusu mambo muhimu. Kwa mfano: Nani atakayeamua watakaosaidiwa kutoka pande zote? Na, msaada huo utatolewa kwa muda gani?

Lengo lako kuu kwa wanafamilia wako ni kuwa chumvi na mwanga kwao. Inawezekana ukakubaliana sana na matakwa ya utamaduni mpaka ukawa hufai katika huduma. Kwa hivyo tafuta uwiano katika kusaidia na kutokusaidia. Ila wakati wote, familia yako inapaswa kulenga kuwa mashahidi kwa washirika wako wa karibu wa familia.

---

Kama mchungaji wa Kipentekoste, Mungu amekuita uliongoze kanisa katika kutimiza utume wa Mungu. Lakini kwa kufanya hivi, hupaswi kupuuza familia yako mwenyewe. Hupaswi kamwe kufikia mahali pa kusema: "Nimeleta waliopotea kwa Kristo; lakini nimepoteza familia yangu mwenyewe."

\

## ~ Sura ya 8 ~

# Kipaumbele cha Maombi

Kama ilivyokuwa desturi yake, Musa alitoka nje ya kambi hadi hema la mkutano ili kuomba. Kila wakati watu walipomwona akifanya hivyo, waliacha walichokuwa wakifanya na kutazama hadi alipoingia ndani ya hema. Musa alipokuwa ndani ya hema akiomba, nguzo ya wingu ingeshuka na kutulia mlangoni pake. Watu walipoona hivyo, walistaajabu, wakainama na kumwabudu Mungu. Walitiwa moyo, wakijua kwamba kiongozi wao alizungumza na Mungu mara nyingi. Zoezi hilo la Musa lilimgusa zaidi kijana msaidizi wake, Yoshua. Mara nyingi alimfuata Musa kwenye hema, na angekaa huko muda mrefu baada ya Musa kuondoka. Alitaka sana kuwa kama mshauri wake (linganisha Kut. 33:8 -11).

Hakuna kitu kinachoinua kusanyiko kama mchungaji anayeomba. Ibilisi haogopi digrii zetu za kitaaluma. Wala haogopi bajeti zetu kubwa za kanisa au majengo yetu ya fahari. Lakini anaogopa sana maombi yetu. Yeye na majeshi yake hutetemeka wakati watu wa Mungu wanapopiga magoti kuomba maombi yaliyo na upako na kujaa imani. Ikiwa mchungaji wa Kipentekoste hafanikiwi katika jambo lingine lolote, bora afanye vyema katika maombi.

## MTINDO WA MAISHA YA MAOMBI

Martin Luther aliyekuwa Mtengeneza Kanisa wa Kiprotestanti, aliwahi kusema, "Kuwa Mkristo bila maombi ni kitu kisichowezekana, kama ambavyo haiwezekani kuwa hai pasipo kupumua." Kilicho kweli kwa kila aaminiye ni kweli maradufu kwa mchungaji wa Kipentekoste. Mtu hawezi kuhudumu kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste bila mtindo wa maisha wa maombi ya kujitoa. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwamba inawabidi "kumwomba Mungu siku zote, wala wasikate tamaa" (Lk. 18:1).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima Yesu awe mfano wako. Maisha yote ya Bwana na huduma yake vilijawa na maombi, na kufunikwa kwa maombi. Luka anaandika kwamba "Mara nyingi Yesu aliondoka akaenda mahali pasipokuwa na watu na kusali" (Lk. 5:16). Wakati mmoja, "alitoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha akimwomba Mungu" (6:12). Katika tukio lingine, aliwachukua Petro, Yohana, na Yakobo na "kupanda mlimani kuomba" (9:28). Kwa kweli, Yesu aliomba kila alipopata nafasi. Ili uweze kuwaongoza watu wa Mungu, wewe pia kama Yesu, lazima uwe mwanamume au mwanamke anayeomba daima. Hakuna anayeweza kuhudumu katika nguvu za Roho bila kuwa na tabia ya maombi ya kudumu.

Kupitia maombi, unajitayarisha kwa huduma. Unapongoja katika maombi, unamkaribia Mungu (Yakobo 4:8; taz. Ebr. 10:22). Zaidi ya hayo, unapata nguvu za kiroho unazohitaji ili kuishi kwa ajili ya Kristo, na nguvu unayohitaji ili kutekeleza huduma yako kwa ufanisi (Isa. 40:31; Zab. 40:1-3).

Biblia inahimiza, "Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili" (Gal. 5:16). Ili kufanya hivyo utahitaji kuishi daima katika ushirika na Mungu. Ushirika huo hupatikana kwa njia ya maombi. Wakati wa misimu ya maombi, Roho atazungumza nawe na kukutia moyo na kukupa maelekezo. Maombi yaliyotiwa mafuta na Roho yatakutayarisha zaidi kwa vita vya kiroho (Efe. 6:12, 18).

## HUDUMA YA MAOMBI

Pamoja na kuendeleza maisha yako ya maombi ya kibinafsi, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uone maombi kama njia ya kuwahudumia wengine. Kuna njia tatu unazoweza kuwahudumia wengine kupitia maombi.

**Kuhudumu Kupitia Maombi Binafsi, Faraghani**

Kwanza, unaweza kuhudumia wengine kupitia maombi ya faragha. Yesu aliita aina hii ya maombi kuwa ni maombi ya siri. Alifundisha hivi: “Wewe unaposali, ingia ndani ya chumba chako, funga mlango na umwombe Baba yako asiyeonekana” (Mt. 6:6). Huko mahali pa siri, lazima utumie wakati kuombea mahitaji ya wengine. Unapoomba, unaweza kumwomba Mungu kwa ujasiri, ukijua kwamba Mungu anaona kazi yako ya upendo na kwamba atajibu maombi yako. Katika kifungu hichohicho, Yesu aliahidi hivi: “Baba yako, aonaye sirini, atakupa thawabu.” Nyakati zako za maombi ya siri zinaweza kuwa za aina tatu:

*1. Maombi ya kuabudu*. Kwanza, unapaswa kuomba kwa kuabudu. Yaani, unapaswa kutumia muda katika maombi kumkaribia Mungu. Hiyo itaimarisha uhusiano wako na Bwana. Unapoomba katika Roho Mtakatifu, imani yako itajengwa, na kudumishwa katika upendo wa Mungu (Yuda mst. 20-21; taz. Rum. 5:5). Kutoka kwa uhusiano huu na Mungu utaweza kutimiza huduma yako kwa mafanikio.[1]

*2. Maombezi*. Kama ilivyotajwa, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unapaswa kutumia muda mbele ya Mungu kumwomba kwa ajili ya mahitaji ya wengine - hasa kwa ajili ya mahitaji ya walio washirika wa kanisa lako. Yesu mara nyingi aliwaombea wanafunzi wake (Yoh. 17:9). Kwa mfano, aliwaombea ili imani yao iendelee kuwa na nguvu (Lk. 22:32). Zaidi, aliomba Mungu awalinde (Yoh. 17:11-12, 15), na kwamba wawe na furaha (mst. 13). Pia aliomba ili watakaswe (mst. 17-19) na kwamba wadumu katika umoja (mst. 21-23).

Vivyo hivyo, mtume Paulo aliendelea kuomba kwa ajili ya watu wa Mungu. Aliwaandikia waamini huko Rumi na kuwaambia hivi: “Ninawakumbuka daima katika sala zangu” (Rum. 1:9-10). Aliwaambia Waefeso, “sijaacha kutoa shukrani kwa ajili yenu, nikiwakumbuka katika sala zangu” (Efe. 1:16; taz. Kol. 1:9). Kama wachungaji wa Kipentekoste lazima tufuate mifano ya Yesu na Paulo na kutumia muda mwingi katika maombi, kuwaombea wengine.

*3. Maombi pamoja na kufunga*. Mwisho: wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kuomba mara kwa mara pamoja na kufunga. Katika mfumo wa kiroho, maombi na kufunga vitakusaidia kuingiza roho yako katika

[1] Kwa habari zaidi kuhusu kumkaribia Mungu, tazama Sura ya 15: “Tabia Imara ya Ibada Binafsi.”

maelewano na Roho wa Mungu. Unapotumia muda katika maombi na kufunga, mwili wako utaletwa chini, na roho yako itakuwa tayari kutambua kwa uwazi zaidi sauti ya Roho (taz. Gal. 5:16-17).

### Kuhudumu Kupitia Maombi ya Mtu kwa Mtu

Zaidi ya hayo, mara nyingi utaitwa kuhudumu katika maombi ya mtu kwa mtu. Maombi ya mtu kwa mtu hutokea unapoomba kwa ajili ya mtu uliye naye. Aina hii ya maombi mara nyingi hutokea wakati wa maombi mbele ya kanisa. Inaweza pia kutokea katika nyumba au hospitali wakati wa ziara ya kichungaji. Au inaweza hata kufanyika sokoni wakati wa kufanya uinjilisti. Wakati mwingine, maombi kama hayo yanahusisha kuwekea watu mikono au kuwatia mafuta (rej. Mdo 19:6; Yakobo 5:14). Na ni kuomba kwa imani wakati wote (Yakobo 5:15).

Mifano minne ya maombi ya mtu kwa mtu ni kuomba na watu ili waokolewe, kuomba na watu ili wapone, kuomba na watu ili wafunguliwe toka vifungo vya kipepo, na kuomba na watu ili wajazwe Roho Mtakatifu. Ni lazima uwe na uzoefu katika kila moja ya maeneo haya ya huduma. Vyovyote vile, ni lazima uonyeshe kwamba unaliamini Neno la Mungu, utamke maneno ya imani na yenye kutia moyo, na uonyeshe kuwajali kweli wale unaowaombea.[2]

### Kuhudumu kwa Maombi Hadharani (au Mbele za Watu)

Wakati fulani utaitwa kufanya maombi hadharani. Kuna wachungaji wachache wanao-ongoza maombi ya kichungaji kanisani kila Jumapili asubuhi. Vile vile, mchungaji wa Kipentekoste mara nyingi huitwa kuomba mbele ya watu wengi kama vile mazishi na harusi. Unapoombwa kufanya hivyo katika matukio kama haya, omba kwa heshima na neema. Lakini, usiombe hadharani ili kujionyesha au kujitukuza. Wakati wote omba kwa kumaanisha. Yesu alionya hivi: “Mnaposali, msiwe kama wanafiki, kwa maana wao hupenda kusali sala ndefu hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu” (Mt. 6:5).

---

[2] Kwa habari zaidi kuhusu kuombea watu binafsi, tazama Sura ya 20: “Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho”; Sura ya 21: “Kuhudumu Katika Nguvu za Roho”; na Sura ya 22: “Kujihusisha Katika Vita vya Kiroho.” Pia, tazama kitabu (tafsiri), *Huduma Yenye Nguvu: Uhudumu Katika Nguvu na Upako wa Roho Mtakatifu,* cha Denzil R. Miller, kinachotoa ushauri kuhusu kuombea watu kuponywa, kujazwa na Roho, na kukombolewa kutoka vifungo vya kipepo. Hiki kitabu kinaweza kupakuliwa bila malipo katika tovuti ya www.DecadeofPentecost.org.

## KULIONGOZA KANISA KATIKA MAOMBI

Mchungaji wa Kipentekoste hapaswi akuze tu maisha yake binafsi ya maombi, ila pia ni vizuri ajenge huduma ya maombi yenye nguvu katika kanisa pale anapofanya huduma.

### Kuhubiri na Kufundisha Kuhusu Maombi

Jambo moja muhimu kwa ajili ya kukuza huduma ya maombi yenye nguvu katika kanisa ni kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu yake. Kwa kufanya hivi, utakuwa unafuata tena mfano wa Yesu, ambaye mwenyewe alifundisha sana juu ya somo la maombi (rej. Lk. 18:1; Mt. 6:5-15).

Unaweza kuwatia moyo Wakristo kuomba kwa kuwashirikisha shuhuda jinsi ambavyo Mungu amejibu maombi siku zilizopita. Shuhuda hizo zinaweza kutolewa katika Biblia, kutoka historia, au kutoka maishani. Ni vizuri uwe na muda zaidi kufundisha masomo ya vitendo juu ya faida za maombi, na jinsi ya kuomba.[3]

### Kuonyesha Mfano wa Maombi

Usifundishe tu kuhusu maombi. Waonyeshe waamini jinsi ya kuomba. Tena, hivi ndivyo Yesu alivyofundisha wanafunzi wake. Hakuwafundisha tu kwa maneno, aliwaonyesha kwa maisha yake. Alitoa kielelezo cha maisha ya maombi mbele yao. Wanafunzi wa Yesu waliona jinsi alivyoenenda katika ushirika wa mara kwa mara na Baba Yake wa Mbinguni. Wakati mmoja, baada ya kumwangalia akiomba, walimwambia hivi: “Bwana, tufundishe hata sisi kuomba, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake” (Lk. 11:1). Kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kuishi maisha ya maombi mpaka washirika wako wakuulize, “Mchungaji, tufundishe sisi kuomba, kama vile Yesu alivyowafundisha wanafunzi Wake.”

---

[3] Mihutasari ya kuhubiri na kufundisha juu ya maombi inaweza kupatikana katika kitabu kiitwacho, *Interceding for the Nations: 100 Sermon Outlines on Missional Prayer*, ambacho kinaweza kupakuliwa bila malipo katika tovuti ya www.DecadeofPentecost.org.

**Kuandaa Maombi**

Tena, ni vizuri uliandae kanisa lako kwa ajili ya maombi. Unaweza kufanya hivyo kwa kuunda vikundi vya maombi na kwa kupanga matukio ya maombi kama ifuatavyo:

Kuunda vikundi vya maombi. Utataka kuhimiza uundwaji wa vikundi maalum vya maombi katika kanisa. Vikundi hivi vinaweza kuundwa kama visaidizi vya idara zilizopo kama ile ya wanaume, ya wanawake, ya vijana na nyingine. Pia, vinaweza kuundwa ili kushughulikia mahitaji fulani katika kanisa, jumuiya, taifa, au ulimwengu. Mahitaji haya yanaweza kuwa ya kijamii au kiroho, ya ndani au ya kimataifa. Kwa mfano, washirika wengine wanaweza kutaka kuombea uamsho katika kanisa, huku wengine wakitaka kuombea amani nchini. Mahitaji mengine mengi yanaweza kutambuliwa, yenye kuhitaji maombi.

Kupanga matukio ya maombi. Tena utahitaji kuingiza matukio mengi ya maombi kwenye kalenda ya shughuli za kanisa. Bila shaka utataka kupanga ibada za kawaida za maombi endelevu kwa kanisa, kama vile mkutano wa maombi ya katikati ya wiki. Pia utataka kupanga matukio maalum ya maombi kama vile mifungo au wiki za maombi maalum.

Kwa mfano, mchungaji mmoja wa Kipentekoste alipanga wiki ya maombi na kufunga mara mbili kila mwaka mwezi wa Januari na wa Julai. Katika kujiandaa kwa ajili ya matukio haya, aliwahimiza washirika kukusanya maombi kutoka kwa wanafamilia wao, marafiki, majirani, na wafanyakazi wenzao. Baada ya kufanya hivyo walipaswa kuandika hayo maombi kwenye fomu maalum zilizotayarishwa na kugawanywa kwa washirika ili yaweze kuombewa wakati wa mikutano ya maombi ya asubuhi na jioni. Kanisa hilo pamoja na jamii lilipokea baraka kubwa kupitia jambo hilo.

Makanisa mengi ya Kipentekoste hupanga mfululizo wa mikutano ya maombi kuelekea Jumapili ya Pentekoste kila mwaka. (Jumapili ya Pentekoste huja majuma saba baada ya Jumapili ya Pasaka.) Katika mikutano hii maalum, washirika humwita Mungu kumimina Roho Wake juu ya kanisa. Pia wanaomba kwamba wakati wa sherehe zao za Pentekoste Wakristo wengi watiwe nguvu na Roho Mtakatifu (Mdo. 1:8; 2:4). Na wanaomba kwamba wengi wamjie Bwana kama ilivyotokea siku ya Pentekoste ya kwanza (2:41).

Unaweza pia kutaka kupanga maombi ya kufunga ya pamoja kila mwaka yenye kuwashirikisha watumishi wa kanisa na viongozi. Tafuta maelekezo toka kwa Bwana kuhusu maombi ambayo inakupasa kuyaratibu kwa ajili ya kanisa.

**Kuombea Utume wa Mungu**

Mkazo mmoja wa maombi unapaswa kuwepo katika kila kanisa la Kipentekoste barani Afrika. Mchungaji wa Kipentekoste lazima ahakikishe kwamba kanisa lake linaomba mara kwa mara kwa ajili ya maendeleo ya utume wa Mungu duniani. Hili lilikuwa ombi la Yesu, na halipaswi kupuuzwa (Mt. 9:37-38). Kwa hiyo unapaswa kuliongoza kanisa lako katika maombi ya kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya ufalme wa Mungu katika jumuiya yako, taifa, bara na ulimwengu. Unapaswa kuwaongoza katika maombi kwa ajili ya wamishenari waliotumwa na kanisa lako la kitaifa, pamoja na wale wanaosaidiwa na kanisa lako la mahali pamoja. Na unapaswa kuomba mara kwa mara kwa ajili ya maelfu ya makundi ya watu duniani ambao hawajafikiwa.[4]

## KUONGOZA MKUTANO WA MAOMBI

Mchungaji wa Kipentekoste lazima ajue jinsi ya kuendesha vizuri mkutano wa maombi. Yafuatayo ni maelekezo yanayoweza kufuatwa kwa ajili ya kuongoza mkutano wa maombi wenye ufanisi.

**Panga Mapema**

Kama ilivyo kwa tukio lolote muhimu kanisani, utahitaji kupanga mapema ili kuwa na mkutano wa maombi wenye ufanisi. Utahitaji kuchagua wakati na mahali pa mkutano. Utahitaji pia kuamua madhumuni ya mkutano wa maombi na kwamba mkazo wake utakuwa nini. Na utahitaji kutengeneza orodha ya vitu vya kuombewa katika huo mkutano. Unaweza pia kuhitaji kukusanya taarifa muhimu kuhusu hayo mahitaji ya maombi. Kisha utawashirikisha washirika kwa wakati ufaao katika mkutano wa maombi.

**Tunza Muda – Usipoteze Lengo (Mwelekeo)**

Unapoongoza mkutano wa maombi, utahitaji kujali muda na kutopoteza lengo. Yaani, anza na kumaliza mkutano wa maombi kwa muda uliopangwa. Watu wengine wana shughuli nyingi, na watathamini jinsi unavyoheshimu wakati wao.

[4] Taarifa kuhusu vikundi vya watu ambao hawajafikiwa duniani zinaweza kupatikana kwenye tovuti ya www.JoshuaProject.net.

Matokeo yake, utakuwepo uwezekano mkubwa wao kuhudhuria mikutano ya maombi.

Zaidi ya hayo, unapoongoza mkutano wa maombi, unapaswa kujali mwelekeo. Maana yake ni kwamba hutaruhusu mkutano wa maombi kuingiliwa na chochote na kuyumbishwa. Ibada fupi na muda mfupi wa kuimba vinafaa mwanzoni mwa mkutano wa maombi. Halafu sehemu kubwa ya mkutano iwe ni maombi.

**Uwe Wazi kwa Utendaji na Uongozi wa Roho**

Ingawa mkutano wa maombi unapaswa kupangwa vizuri na ratiba kuzingatiwa, kiongozi wa mkutano anapaswa kuwa wazi kila wakati kwa maongozi ya Roho Mtakatifu. Anapaswa kuwahimiza watu kuomba katika Roho (Rum. 8:26-27; 1 Kor. 14:15: Efe. 6:18) na kufunguka kwa uongozi wa Roho na madhihirisho ya karama za kiroho (1 Kor 14:26).

## MFANO WA MKUTANO WA MAOMBI

Mtu anaweza kuuliza, "Mkutano wa Kipentekoste wa maombi ukoje?" Jibu la swali hili linapatikana katika Biblia. Kitabu cha Matendo ya Mitume kinatupa mfano wa mkutano wa kawaida wa maombi katika kanisa la kwanza. Mkutano huu wa maombi ulifanyika mara baada ya Siku ya Pentekoste.

Kanisa lilikuwa likipitia mateso makubwa. Viongozi wa Kiyahudi waliwakamata Petro na Yohana. Kisha wakawatisha na kuwaamuru waache kuhubiri katika jina la Yesu. Walipowaachia wale mitume wawili waende zao, walirudi kanisani na kueleza yaliyowapata. Wakristo walianza kuomba. Maombi yao na matokeo ya maombi yao yameandikwa katika Matendo 4:23-31. Kutoka kwa mkutano huu wa maombi, tunajifunza masomo matatu muhimu kuhusu jinsi tunavyopaswa kuendesha mikutano yetu ya maombi leo.

**Namna ya Kuomba Kwetu**

Kwanza, tunajifunza kuhusu namna ya kuomba kwetu, au tunavyopaswa kuomba. Biblia inasema juu ya Wakristo hao kwamba, "walipaza sauti zao pamoja katika kumwomba Mungu" (Mdo. 4:24). Hivyo, maombi yao yalikuwa ya bidii ("walipaza sauti zao") na ya umoja ("kwa pamoja"). Tunapokusanyika ili kuomba, sisi pia tunapaswa kumtafuta Mungu kwa bidii, na lazima tuombe kwa umoja. Kwa kuongezea, maombi yetu yanapaswa kutolewa kwa imani (Mk. 11:24). Wale

walioomba siku hiyo huko Yerusalemu walitarajia kabisa Mungu asikie na kujibu maombi yao. Na sisi leo inapaswa kuwa hivyo.

**Yaliyomo Katika Maombi Yetu**

Kisha, tunajifunza kuhusu yaliyomo katika sala zetu, au kile tunachopaswa kuomba. Wakristo hao wenzetu hawakufikiri matatizo yao, ingawa walikuwa na mengi. Badala yake walielekeza mawazo yao kwenye uwezo na ukuu wa Mungu (Mdo. 4:24-25). Na waliomba mapenzi ya Mungu yatimizwe (mst. 26-28). Zaidi ya hayo walimwomba Mungu awatie nguvu na kuwapa ujasiri wa kutangaza injili, hata katikati ya mateso (mst. 29-30). Kwa kumwomba Mungu "kunyosha mkono wake," walikuwa wakimwambia ashuke na nguvu za Roho wake (linganisha Eze. 37:1; Lk. 11:20 pamoja na Mt. 12:28; Mdo. 11:21).

**Matokeo ya Maombi Yetu**

Mwisho: tunajifunza tunachoweza kutarajia kutokea tukiomba. Ikiwa tutaomba kama wale waamini wa kwanza, sisi pia tunaweza kutarajia Mungu kufanya uwepo wake ujulikane katika mikutano yetu ya maombi. Biblia inasema, "Baada ya kusali, mahali walipokuwapo pakitikiswa. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri" (Mdo. 4:31). Ikiwa tutasali kama wao, tunaweza kutazamia Mungu ajibu sala zetu kama vile alivyojibu sala zao. Tunaweza kumtarajia atujaze na Roho Mtakatifu na kututia nguvu kama mashahidi wa Kristo kwa waliopotea.

~ Sehemu ya 3 ~

# Anavyoviamini Mchungaji wa Kipentekoste

~ Sura ya 9 ~

# Anaiamini Biblia

Kwenye ukuta wa mbele wa jengo la makao makuu ya taasisi ya Africa's Hope huko Springfield, Missouri, Marekani, kuna ramani kubwa ya Afrika. Juu ya hiyo ramani kuna mchoro wa mwanamume Mwafrika akiwa amenyoosha mkono wake mbele yake. Katika mkono wa mtu huyo kuna Biblia. Anahubiri injili. Picha hii inawakilisha maelfu ya wahubiri wa Kipentekoste kote barani Afrika ambao wanatangaza Neno la Mungu kwa uaminifu kwa wote watakaosikia. Inawakilisha uhusiano maalum wa mchungaji wa Kipentekoste na Biblia yake.

Biblia ni kama kitabu kingine chochote ulimwenguni. Ingawa inahusiana kwa usahihi na historia, ni zaidi ya kitabu cha historia. Ingawa inafundisha tabia nzuri, ni zaidi ya kitabu cha maadili. Wanafalsafa hustaajabia undani wa dhana zake, lakini Biblia si kitabu cha falsafa. Biblia ina "maneno halisi ya Mungu" (Rum. 3:2). Inafunua hali ya dhambi ya wanadamu, na inaonyesha njia ya wokovu kupitia Kristo. Sura hii itachunguza uhusiano maalum wa mchungaji wa Kipentekoste kwa Biblia kama Neno la Mungu.

## JINSI MCHUNGAJI WA PENTEKOSTE ANAVYOIONA BIBLIA

Wachungaji wa Kipentekoste wanaiheshimu sana Biblia. Wanaamini kuwa ni ujumbe wa Mungu kwa wanadamu—Neno la milele la Mungu. Kwa mchungaji wa Kipentekoste, Biblia hutumika kama msingi wa huduma na matendo yote. Kifungu cha 1 cha "Tamko la Imani la Umoja wa Assemblies Of God Duniani

(World Assemblies of God Fellowship)," chenye kichwa hiki cha habari: "Uvuvio wa Maandiko," kinaeleza kwa kifupi jinsi mchungaji wa Kipentekoste anavyoiona Biblia: "Maandiko, Agano la Kale na Agano Jipya, yamevuviwa na pumzi ya Mungu neno kwa neno, na ni ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu, kanuni isiyoweza kukosea, yenye mamlaka kuhusu imani na mwenendo (2 Tim. 3:15-17; 1 The. 2:13; 2 Pet. 1:21)."[1] Ili kuelewa vizuri maana ya kauli hii, hebu tuigawanye katika sehemu zake nne:

**Uvuvio wa Pumzi ya Mungu Neno kwa Neno**

Kwanza, mchungaji wa Kipentekoste anaamini kwamba "Maandiko, Agano la Kale na Agano Jipya, yamevuviwa na pumzi ya Mungu neno kwa neno." Tunaposema kwamba Maandiko yamevuviwa na pumzi ya Mungu neno kwa neno, maana yake ni kwamba Mungu, kwa uweza, ukuu na enzi Yake, alitulia juu ya manabii na mitume wa kale, akiwaongoza kwa njia isiyo ya kawaida kuandika mawazo na dhana alizochagua. Paulo alithibitisha ukweli huu alipoandika, "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu" (2 Tim. 3:16). Petro alieleza kwa undani zaidi mchakato huu usio wa kawaida, kama ifuatavyo: "Zaidi ya yote, mnapaswa kufahamu kwamba hakuna unabii wowote katika Maandiko uliokuja kwa tafsiri ya mwandishi ya mambo. Maana unabii haukuletwa kamwe kwa mapenzi ya mwanadamu, bali manabii walinena yaliyotoka kwa Mungu, ingawa ni wanadamu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Pet. 1:20-21).

Tunaposema kwamba Biblia imevuviwa neno kwa neno kwa maongozi ya Mungu, tunamaanisha kwamba uvuvio huo unafika mpaka kwenye kila neno la mistari husika. Mungu hakuongoza tu mawazo ya Maandiko, alisimamia mchakato wa uandishi, akichagua maneno yenyewe yaliyotumika kuonyesha kilichotakiwa. Yesu alithibitisha ukweli huu aliposema, "Ni rahisi zaidi mbingu na dunia kutoweka kuliko hata yodi au nukta moja ya torati" (Lk. 16:17). Kwa hiyo, uvuvio wa maneno unamaanisha kwamba kila neno katika Maandiko limeongozwa na Roho Mtakatifu. Liko pale kwa sababu Mungu alitaka liwepo.

Kwa kuwa Biblia imevuviwa, ni sahihi kuitwa Neno la Mungu. Nayo inajisema yenyewe kuwa ni "Neno la Mungu" au "Neno la Bwana" zaidi ya mara arobaini.

---

[1] Tazama Nyongeza 1: "Tamko la Ukiri wa Imani la Ushirika wa Assemblies of God Duniani."

### Ufunuo wa Mungu

Vile vile mchungaji wa Kipentekoste anaamini kwamba Biblia ni "ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu." Maana yake ni kwamba Mungu amefunua mapenzi yake kwa wanadamu kupitia maneno ya Maandiko. Alivuvia Biblia ili watu wamjue Yeye, kazi Zake, na njia Zake. Kwa kutupa Biblia, Mungu amejionyesha kuwa Mungu mwenye kujifunua. Biblia ni uthibitisho kwamba Mungu anataka wanaume na wanawake wote kila mahali wamjue Yeye na mpango Wake wa wokovu.

### Isiyo na Makosa

Zaidi ya hayo, mchungaji wa Kipentekoste anaamini kwamba Biblia haina makosa. Maana yake ni kwamba haina makosa. Kwa kuwa maneno ya Maandiko yamevuviwa kwa pumzi ya Mungu, dhana zake ni kweli na kauli zake ni sahihi. Mtunga Zaburi alitangaza hivi: "Neno la Bwana halina dosari" (Zab. 18:30). Yesu alithibitisha ukweli huo aliposema, "Mbingu na dunia zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe" (Mt. 24:35).

Ni muhimu mchungaji wa Kipentekoste aelewe kwamba tunapozungumza kuhusu Biblia kutokuwa na makosa, hatusemi kuhusu tafsiri yoyote ya Biblia. Tunayataja Maandiko kama yalivyoonekana katika maandishi yake ya asili. Watafsiri wa Biblia hujitahidi kuhakikisha kwamba wanatafsiri kwa usahihi maandishi hayo. Lakini kwa sababu wao ni wanadamu, ni jambo lisiloepukika kwamba makosa hufanywa. Ila makosa haya ni madogo sana. Leo, tunaweza kuwa na hakika kwamba Biblia zetu zinaonyesha kwa usahihi maneno ya Mungu kama yalivyofunuliwa kwa walioiandika hapo kwanza.

### Ndiyo Kanuni na Mamlaka ya Imani na Mwenendo

Mwisho: Mchungaji wa Kipentekoste anaamini kwamba Biblia ndiyo "kanuni yenye mamlaka ya imani na mwenendo" kwa ajili ya mwamini. Biblia inamwambia mwanamume au mwanamke wa Mungu kile wanachopaswa kuamini na jinsi wanavyopaswa kuishi. Kwa sababu Biblia ni Neno la Mungu, ina mamlaka. Hii ina maana kwamba mafundisho yake lazima yaaminiwe, na amri zake lazima zifuatwe. Mfalme Daudi alielewa ukweli huu. Aliliita Neno la Mungu "taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu" (Zab. 119:105).

## JINSI MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE ANAVYOHUSIANA NA BIBLIA

Je, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuchukuliaje Biblia? Je, anapaswa kuwa na mtazamo na maoni gani kuhusu Maandiko? Kwa kuamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu kweli, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuiendea Biblia akiwa na mitazamo mitatu.

### Kwa Heshima Takatifu

Kwa sababu maneno ya Maandiko hutiririka kutoka moyoni mwa Mungu mtakatifu, Biblia yenyewe ni takatifu. Na kwa sababu Biblia ni takatifu, mchungaji wa Kipentekoste lazima aichukue kwa heshima ya juu zaidi. Ni lazima aheshimu Neno la Mungu na kulitendea kwa heshima takatifu. Paulo aliwapongeza Wakristo wa Thesalonike kwa mtazamo huo, "Mlipolipokea neno la Mungu,…" (1 The. 2:13). Kwa sababu mchungaji wa Kipentekoste anaiheshimu Biblia kama maneno halisi ya Mungu, ataepuka kupotosha mafundisho yake kwa kujaribu kuifanya iseme kile ambacho yeye anataka iseme. Petro anaonya kwamba wale wanaofanya hivi wanafanya "kwa uharibifu wao wenyewe" (2 Pet. 3:16).

### Kwa Upendo wa Kina

Sio tu kwamba mchungaji wa Kipentekoste lazima aheshimu Biblia, ni lazima awe na upendo wa dhati kwa mafundisho yake. Mwandishi wa Zaburi ya 119 anaonyesha upendo huo kwa Neno la Mungu. Ikiwa na mistari 176, Zaburi hii ndiyo sura ndefu zaidi katika Biblia. Ni maombi marefu kwa Mungu.

Katika sala hiyo nzuri, mwandishi anaonyesha tena na tena upendo wake kwa Neno la Mungu. Kwa mfano, anamwambia Mungu, "Ninapendezwa na amri zako kwa sababu ninazipenda" (mst. 47). Naye anamkumbusha Mungu jinsi ambavyo maneno Yake yameathiri maisha yake: "Nafsi yangu imechoka kwa kutamani sheria zako nyakati zote….Sheria zako ndizo furaha yangu; ni washauri wangu" (mst. 20, 24). Kama Mtunga Zaburi, mchungaji wa Kipentekoste lazima asitawishe mapenzi ya dhati kwa Neno la Mungu.

### Kujiamini kwa Uhakika

Zaidi ya hayo, kwa sababu mchungaji wa Kipentekoste anaamini kweli kwamba Biblia ina pumzi ya Mungu, anaikaribia kwa ujasiri mkubwa. Anajua kwamba anaweza kuamini matamshi yake, na kuzitumaini ahadi zake. Kwa sababu mchungaji wa Kipentekoste anaiamini Biblia kikamilifu, kama Ibrahimu,

anasadiki kabisa kwamba kile ambacho Mungu ameahidi atafanya hakika (Rum. 4:21).

Mchungaji wa Kipentekoste haamini tu kwamba Biblia ni kweli, anaelewa kwamba ina nguvu. Ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu (Yoh. 1:1-3). Biblia yenyewe inasema hivi, "Neno la Mungu li hai na lina nguvu. [Ni] kali kuliko upanga wowote ukatao kuwili" (Ebr. 4:12). Paulo alieleza injili kama "nguvu ya Mungu iletayo wokovu" (Rum. 1:16). Vifungu hivi na vingine vingi vinazungumza juu ya nguvu ya Neno la Mungu. Kwa mfano, akizungumza kupitia nabii Isaya, Mungu alisema hivi kuhusu Neno Lake, "Kama vile mvua na theluji zishukavyo kutoka mbinguni, na hazirudi tena pasipo kuinywesha nchi, na kuifanya kuchipua na kusitawi,…ndivyo lilivyo neno langu linalotoka kinywani mwangu: Halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu na kutimiza kusudi nililolituma" (Isa. 55:10-11).

Kwa kuongezea, Biblia hutuambia kwamba Neno la Mungu huonyesha njia (Zab. 119:105), huokoa nafsi (Yak. 1:21), hutokeza imani (Rum. 10:17), huzalisha upya (1 Pet. 1:23), hutakasa (Yoh. 17:17), hujenga (Mdo. 20:32), huponya na kuokoa (Zab. 107:20), husafisha (Yoh. 15:3), hufanikisha (Yos. 1:8), huleta shangwe (Yer. 15:16), na mengine mengi sana. Kwa sababu ya kweli hizi zenye nguvu, mchungaji wa Kipentekoste ana imani kubwa katika Neno la Mungu.

## WAJIBU WA MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE KUHUSU BIBLIA

Kama mchungaji wa Kipentekoste unazo wajibu fulani kwa Neno la Mungu. Ni sita, kama ifuatavyo:

### Kuijua Biblia

Kwanza, lazima uwe na maarifa mapana ya Maandiko. Hakuna kinachomstahilisha mchungaji wa Kipentekoste kwa ajili ya huduma zaidi ya ujuzi kamili wa Biblia. Na hakuna kitu kinachomnyima sifa kama kuwa na ujuzi duni, wa juujuu wa Maandiko. Kwa hiyo ni lazima ujitoe na kujitahidi katika maisha yako yote kuelewa Maandiko. Unaweza kufanya hivyo kwa njia tatu:

*1. Kusoma kila siku.* Unaweza kupata ujuzi wa Neno la Mungu kwa kusoma Biblia kila siku. Kwa hiyo unapaswa kukuza nidhamu ya usomaji wa Maandiko.[2] Unaweza kukamilisha Biblia katika mwaka mmoja kwa kusoma wastani wa

[2] Kwa zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 15: "Tabia Imara ya Ibada Binafsi."

dakika kumi na tano tu kwa siku. Ikiwa utafuata mazoezi haya, siku baada ya siku, ujuzi wako wa Biblia utaongezeka.

*2. Kujifunza Biblia kwa mpangilio.* Unaweza kuongeza ujuzi wako wa Maandiko kupitia kujifunza Biblia kwa mpangilio. Biblia inazungumza juu ya desturi hii miongoni mwa waamini wa Kiyahudi huko Beroya. Inasema, "Waliupokea ujumbe [wa injili] kwa hamu kubwa na wakayachunguza Maandiko kila siku waone kama yale aliyosema Paulo ni kweli" (Mdo. 17:11). Lingekuwa jambo la hekima kuiga mazoea ya watu wa Beroya ya kulichunguza Neno la Mungu kwa umakini.

Ni vizuri pia utamani kujenga maktaba binafsi ya rejea ili kukusaidia katika kujifunza Maandiko kwako. Maktaba hii inapaswa kuhusisha vitabu vya marejeo vya Biblia kama vile kamusi ya Biblia, vitabu vya mafafanuzi ya Biblia, na vingine vinavyotoa mafundisho maalum kuhusu Biblia. Ni vizuri maktaba yako ijumuishe Biblia nzuri za kujifunzia. Biblia bora kabisa ya Kipentekoste kwa ajili ya mafunzo na rejea ni ile ijulikanayo kama Biblia Ya Uzima Tele, itolewayo na Kanisa la Tanzania Assemblies of God kwa kushirikiana na Chama cha Biblia Tanzania.[3]

Ikiwezekana, ni vizuri umalize masomo katika shule ya Biblia ya Kipentekoste. Hii itaongeza sana ujuzi wako wa Maandiko na huduma. Assemblies of God barani Afrika ina taasisi nyingi za mafunzo ya watumishi katika bara zima. Taasisi hizi ni pamoja na shule za watu kukaa, na za kutwa. Angalau shule moja ya Biblia ya Assemblies of God inaweza kupatikana karibu kila nchi ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Bonde la Bahari ya Hindi. Shule hizi hutoa mafunzo kwa watumishi wa Assemblies of God na wa madhehebu mengine.[4]

*3. Kushika Maandiko kwa kichwa (au kuyaweka moyoni).* Unapaswa pia kushika Maandiko kwa kichwa ukifuata mpangilio fulani. Lengo zuri ni kushika kwa kichwa andiko angalau moja jipya au fungu la maandiko kwa wiki. Pia, ni kitu kizuri kushika kwa kichwa fungu lolote la Maandiko unalotaka kufundisha au

---

[3] Ili kupata Biblia hii kwa Kiswahili, wasiliana na Idara ya Uanafunzi na Maandiko ya Tanzania Assemblies of God kupitia Mkurugenzi wake.

[4] Orodha ya shule za Biblia za Assemblies of God barani Afrika inaweza kupatikana katika tovuti ya Africa Theological Training Service (ATTS) katika https://africaatts.org/.

kuhubiri. Zoezi hili litakupa uhuru zaidi katika mahubiri yako. Pia litaongeza sana akiba yako ya maandiko uliyojifunza na kuyashika kwa kichwa au kwa moyo.

### Kuishi kwa Viwango Vyake

Pili: Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uishi kulingana na viwango vya Biblia. Haitoshi tu kujua Biblia inafundisha nini. Ni lazima uruhusu mafundisho yake yatengeneze maisha na huduma yako. Biblia inahimiza hivi: "Msisikilize neno tu, na hivyo kujidanganya wenyewe. Fanyeni linachosema" (Yak. 1:22; taz. Rum. 2:13). Lazima uweze kuomba kwa uaminifu pamoja na Mtunga Zaburi, "Nimeichagua njia ya uaminifu; nimeweka moyo wangu kwenye sheria zako. Nimezishika sana sheria zako, Bwana" (Zab. 119:30-31).

### Kulitumia kwa Usahihi Neno la Kweli

Tatu: Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe tayari kulitumia "neno la kweli" kwa usahihi au kihalali (2 Tim. 2:15). Kwa sababu unaamini kuwa Biblia ni Neno la Mungu la milele kwa wanadamu, lazima uepuke jaribu lolote la kugeuza Maandiko kwa makusudi ili kuendana na mawazo yako mwenyewe. Ni vema kutii onyo la Petro kwamba ujihadhari na "watu wasiojua na wasio na msimamo thabiti wanaopotosha Maandiko kwa uharibifu wao wenyewe na uharibifu wa wengine" (2 Pet. 3:16). Na lazima utii kwa uangalifu amri ya Maandiko ya "kufundisha yale yanayofaa kwa ajili ya uzima" (Tito 2:1).

### Ili Kuendeleza Utume Wake kwa Uaminifu

Nne: Jitoe kuelewa kwa uwazi na kuendeleza utume wa Mungu kwa bidii kama unavyofunuliwa katika Maandiko. Biblia inafunua kwamba Mungu ni Mungu anayefanya umishenari na kwamba anafanya kazi ili kutimiza utume Wake duniani. Huu utume wakati mwingine unajulikana kama *missio Dei*. Mungu yuko katika utume wa kukomboa na kuwaita kwake watu kutoka katika kila kabila, lugha na taifa duniani (Uf. 5:9).[5]

Kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uliongoze kanisa lako kujiunga na Mungu katika utume huo (Mt. 24:14). Ili kufanya hivi, lazima uelewe

---

[5] Kwa mengi zaidi kuhusu utume wa Mungu, tazama kitabu cha Africa's Hope katika mfululizo wa Masomo ya Ugunduzi kiitwacho, *Theolojia ya Kibiblia ya Umisheni*, cha Paul York.

kwa uwazi kile Biblia inachofundisha kuhusu utume wa Mungu. Na lazima ujitoe kuliongoza kanisa lako kufanya sehemu yake katika kutimiza utume huo.

**Kuhubiri na Kufundisha Neno**

Tano: Wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu kwa uaminifu kwa watu wako. Kwa kufanya hivi, utawasaidia "kukua katika neema na maarifa ya [Bwana]" (2 Pet. 3:18). Na utahakikisha kwamba watu wa Mungu "wamewezeshwa kikamilifu kwa ajili ya kila kazi njema" (2 Tim. 3:17). Hii ndiyo sababu ya Paulo kumhimiza Timotheo, mwanawe katika imani kama ifuatavyo: "Lihubiri neno; uwe tayari wakati ufaao na usiofaa; sahihisha, kemea, na kuhimiza kwa uvumilivu mwingi na mafundisho makini" (2 Tim. 4:2).

Mchungaji wa Kipentekoste anayefundisha Neno la Mungu kwa uaminifu atapata thawabu (Mt. 24:45-47). Anayeshindwa kutimiza wajibu huu atahukumiwa vikali (Yak. 3:1).

**Ili Kutetea kwa Uthabiti Ukweli Unaoufunua**

Hatimaye, kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uwe tayari kutetea ukweli uliofunuliwa katika Maandiko. Kama Paulo, lazima utengwe "kwa ajili ya ulinzi wa injili" (Flp. 1:16). Katika maneno ya mtume, ni lazima "ushike kwa uthabiti ujumbe wa kuaminiwa kama ulivyofundishwa, ili [wewe] upate kuwatia moyo wengine kwa mafundisho yenye uzima na kuwakataa wanaopingana nayo" (Tito 1:9).

Ukizingatia hilo, ni lazima uliangalie kwa bidii kundi la Mungu ili kuwalinda watakatifu dhidi ya walimu wa uongo na mafundisho ya uongo (Mdo. 20:28-31). Unaweza kufanya hivyo kwa kufundisha mafundisho ya kweli ya Biblia kwa kanisa, kwa uaminifu. Na unaweza kulinda kundi kwa kufichua na kupinga ukengeufu aina yoyote ukitumia kweli ya Neno la Mungu.[6]

---

Mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kujulikana kama mwanamume au mwanamke wa Kitabu. Ni lazima aamini kwamba Biblia imeongozwa na Roho wa Mungu. Kwa sababu hiyo, anapaswa kuithamini Biblia na kuiheshimu sana.

[6] Kwa habari zaidi kuhusu kulinda kundi, tazama Sura ya 27: "Kulilinda Kundi."

Wanapaswa kujua Neno la Mungu na kufundisha kwa bidii na kuhubiri maagizo yake kwa watu wa Mungu.

~ Sura ya 10 ~

# Husimamia Ukweli wa Kipentekoste

Mchungaji katika bara la Afrika lazima aimarishe kwa uaminifu ukweli wa Kipentekoste katika kanisa analolichunga. Ili kufanya hivyo, ni lazima kuelewa ukweli wa Biblia unaofafanua Upentekoste kama vuguvugu. Na lazima aweze kutetea ukweli huu.

Suala hilo ni zaidi ya uwezo wa kushinda mjadala wa kitheolojia. Ni pamoja na kutimizwa kwa Agizo Kuu kwa ufanisi. Jinsi mtu anavyoiona kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya waamini itaathiri sana jinsi anavyotafuta kutimiza agizo la Kristo la kufanya mataifa yote kuwa wanafunzi (Mt. 28:18-20). Bila ufahamu dhahiri wa kazi ya kutia nguvu ya Roho Mtakatifu, utimizo wa Utume Mkuu hautawezekana.

Hebu fikiria mkasi usiokuwa na mkono wa pili. Hata kama utakuwa na makali kiasi gani, hauna maana. Lakini zile sehemu mbili zinapokuwa zimeungana, mkasi huwa chombo cha thamani. Ndivyo ilivyo kwa mafundisho ya Biblia kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu. Iwapo mtu anasisitiza tu kazi ya Roho Mtakatifu ya kuzaa upya (kama inavyoelezwa katika barua za Paulo), na kuacha kusisitiza kazi Yake ya kutia nguvu (kama inavyoelezwa katika kitabu cha Matendo), utendaji wa Roho

katika maisha ya waamini hupungua, na kazi ya ufalme huharibika. Ila, sehemu hizo zote mbili zinapounganishwa, ufahamu kamili zaidi wa kazi ya Roho hujitokeza. Matokeo yake, watu wa Mungu hufanikiwa kutimiza yale aliyokusudia Roho wa Mungu. Na wanawezeshwa kuendeleza ufalme wa Mungu kwa ufanisi zaidi duniani.

Sura hii inahusu wajibu wa mchungaji wa Kipentekoste kushikilia ukweli wa Kipentekoste katika kanisa. Kwa ukweli wa Kipentekoste tunamaanisha yale mafundisho ya Biblia na matendo yaliyosisitizwa kipekee na wasomi wa Kipentekoste. Kweli hizi zinahusu mtu na kazi ya Roho katika maisha ya waaminio.

Ikiwa vuguvugu la Kipentekoste barani Afrika litahifadhi ari yake ya uinjilisti na utume, wachungaji wa Kipentekoste lazima waendeleze kwa uaminifu mafundisho na utendaji wa Kipentekoste katika makanisa yao. Wakishindwa katika hilo, vuguvugu litayumba na kufifia, kama ilivyokuwa kwa nyingine huko nyuma. Makanisa yao yanaweza kubaki na sura za Upentekoste kwa nje; ila baadaye yatapoteza uhai wao wa kiroho na bidii ya kufanya utume. Watakuwa kanisa lingine la kihistoria lenye kumbukumbu tukufu kuhusu siku za zamani ila yasiyo na nguvu katika siku za leo (2 Tim. 3:5).

## KUELEWA MSINGI

Wasomi wa Kipentekoste wanatazama Maandiko yote kama msingi wa mafundisho yao. Hata hivyo, chanzo chao cha kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu kuwezesha waamini ni kitabu cha Matendo ya Mitume katika Agano Jipya. Humo wanapata maongozi na uelewa kuhusu jinsi Roho Mtakatifu anavyojaza, kutia nguvu, na kuwatumia watu kwa ajili ya huduma ya ufalme.

Kitheolojia, kitu kinachotofautisha usomi wa Kipentekoste na usomi usio wa Kipentekoste ni jinsi kila msomi anavyokitazama kitabu cha Matendo. Asiye Mpentekoste anasoma Matendo kama kitabu chenye historia takatifu. Kwao, hicho kitabu kinasimulia hadithi iliyovuviwa na Mungu ya jinsi Kanisa lilivyoanza katika Yerusalemu ya karne ya kwanza na kisha kuenea katika Dola ya Rumi. Kwa wale wasio Wapentekoste, kitabu cha Matendo hutazamwa kama historia tu, kinachosimulia mambo yaliyotukia wakati huo na pale katika karne ya kwanza .

Lakini Wapentekoste wanakitazama kitabu cha Matendo kwa njia tofauti sana. Wanakubaliana na wengine kwamba kitabu hicho kinasimulia kwa usahihi historia ya Kanisa la kwanza. Lakini, wanaona kitabu hicho kuwa zaidi ya historia

takatifu. Wapentekoste wanaamini kwamba Luka aliandika kitabu cha Matendo ili kulipatia Kanisa mfano wa kudumu jinsi linavyopaswa kuishi hadi Kristo atakaporudi. Hivyo Matendo hutupatia kielelezo cha kudumu cha jinsi Wakristo wanavyopaswa kuishi na kuhudumu hapa na sasa. Kutokana na kitabu cha Matendo tunajifunza kwamba Kanisa lipo ili kutoa ushuhuda wa Kristo kwa nguvu za Roho Mtakatifu nyumbani na mpaka miisho ya dunia (Mdo. 1:8).

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaeleza zaidi jinsi wanafunzi wa kwanza wa Kristo walivyobatizwa katika Roho Mtakatifu, na jinsi uzoefu huo ulivyobadilisha maisha na huduma zao kwa kiasi kikubwa. Kinaonyesha kwamba Kanisa linatimiza utume wake kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kwa ishara za ajabu zinazofuata (5:12-16; 6:8; 15:12). Katika Matendo ya Mitume, Roho anaita, anawezesha na kutuma watumishi wa Kristo kwa mataifa ili kutangaza ujumbe wa wokovu kwa ujasiri. Wanapotii, Roho huwaelekeza kimkakati katika njia yao. Kazi yao ya umishenari inaambatana na kumiminiwa kwa nguvu kwa Roho Mtakatifu (2:4; 4:31).

Basi, shughuli ya kimishenari ya Roho Mtakatifu katika Matendo inampa mchungaji wa Kipentekoste picha ya wazi jinsi kanisa la Kipentekoste linavyopaswa kuonekana leo.

## KUENDELEZA "UPEKEE" WA KIPENTEKOSTE

Wapentekoste wanasisitiza kwamba kitabu cha Matendo ya Mitume hulipa Kanisa muundo wa kudumu wa jinsi mtu anavyompokea Roho Mtakatifu. Ubatizo wa Roho hupokelewa baada ya kuzaliwa upya. Na kitendo hicho huambatana na ishara ya kunena kwa lugha kama anavyowezesha Roho. Hebu tupitie kwa ufupi mafundisho haya pekee ya Kipentekoste.

### Mafundisho Kwamba Huja Baada Ya

Fundisho hili linakaza kwamba ubatizo katika Roho Mtakatifu ni tukio "tofauti na linalofuata baada ya kuzaliwa upya."[1] Wasio Wapentekoste wanaona kwamba, kuzaliwa mara ya pili na ubatizo wa Roho ni pande mbili za ujuzi huo huo wa wokovu. Lakini Wapentekoste wanayaona kama mambo mawili tofauti.

[1] Kutoka Tamko la Imani la Umoja wa Assemblies of God Duniani (WAGF), Namba 9: "Ubatizo Katika Roho Mtakatifu" (tazama Nyongeza ya 2).

Wapentekoste hutoa mfano wa ukweli huu kama unavyo-onekana wazi katika matukio matatu ya kitabu cha Matendo:

*1. Roho kupokelewa huko Samaria (Mdo. 8:4-17).* Katika habari hii, Filipo alishuka kwenda Samaria, akamhubiri Kristo. Watu walisikiliza kwa makini maneno yake, wakaamini ujumbe huo, wakakombolewa kutoka utumwa wa mapepo, wakafurahi sana na kubatizwa kwa maji (mst. 5-8, 12). Hata hivyo, Petro na Yohana walipofika siku kadhaa baadaye na kuweka mikono yao juu yao ndipo walipopokea Roho Mtakatifu (mist. 14-17).

*2. Sauli (Paulo) kumpokea Roho (Mdo. 9:1-19).* Sauli alikutana na Yesu njiani akielekea Dameski. Wakati huo, alimwamini Yesu na kumwita "Bwana" mara mbili (mst. 5; 22:8-10). Baadaye aliandika, "Hakuna awezaye kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu" (1 Kor. 12:3). Sauli mara moja alijisalimisha kwa Kristo na kutii amri ya Bwana wake mpya ya kuingia mjini (mst. 6-9). Huko, alikutana na Anania, aliyemwita "ndugu Sauli" (mst. 17; 22:13). Siku tatu baadaye, Anania alipomwekea mikono, Sauli alimpokea Roho Mtakatifu (mst. 17-18).

*3. Kupokelewa kwa Roho na wanafunzi kumi na wawili huko Efeso (Mdo. 19:1-7).* Inaonekana kwamba hawa ndugu walikuwa washirika wa kanisa lililokuwa linaanza huko Efeso (18:27). Andiko linawaita "wanafunzi" (mst. 1). Walikuwa wameamini ujumbe wa Yohana Mbatizaji kuhusu Bwana Yesu, na walikuwa wameweka imani yao katika Kristo ili kuokolewa. Basi, Paulo akawabatiza kwa maji (mst. 5). Baada ya hayo yote ndipo "Paulo aliweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri" (mst. 6).

Katika hayo matukio yote matatu, kulikuwa na kipindi dhahiri kati ya kuokoka kwa watu na kubatizwa kwao katika Roho Mtakatifu. Zaidi ya hayo, kusudi la kutia nguvu la ubatizo wa Roho linahitaji kuwe na kutenganishwa kwa hayo matukio mawili (Mdo. 1:8).

**Mafundisho Kuhusu Ushahidi wa Lugha**

Zaidi, Wapentekoste wanafundisha kwamba ubatizo katika Roho Mtakatifu "hupokelewa kwa imani, na huambatana na udhihirisho wa kunena kwa lugha

kama vile Roho anavyowezesha kutamka kama ushahidi wa kwanza."[2] Kama ilivyo kwa fundisho lililotangulia, Wapentekoste hupata fundisho lao la lugha kama ushahidi wa kujazwa Roho kutokana na kujifunza na kufuata kitabu cha Matendo.

Kitabu cha Matendo kinasimulia mara tano juu ya watu kujazwa au kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Katika matukio matatu kati ya hayo, andiko linasema wazi kabisa kwamba wale wanaompokea Roho walinena kwa lugha kama matokeo ya wao kujazwa na Roho. Tukio la kwanza lilitokea Siku ya Pentekoste wakati wanafunzi wapatao 120 "wakajazwa na Roho Mtakatifu na wakaanza kusema kwa lugha nyingine kama Roho alivyowawezesha" (Mdo. 2:4). Tukio la pili lilikuwa katika nyumba ya Kornelio mjini Kaisaria, jiji lililokuwa pwani. Biblia inasema kwamba wale waliohudhuria "walishangazwa kwamba zawadi ya Roho Mtakatifu ilikuwa imemiminwa hata juu ya Mataifa. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha na wakimsifu Mungu" (10:45-46). Tukio la tatu lilikuwa katika mji wa Efeso, ambapo Paulo alikutana na wanafunzi kumi na wawili. Biblia inasema, "Paulo alipoweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri" (19:6).

Katika matukio mawili yaliyosalia ya watu kujazwa na Roho Mtakatifu mwanzoni katika Matendo, kifungu kinadokeza sana kwamba waliopokea kipawa cha Roho walinena kwa lugha. Katika tukio la kwanza, waamini wapya huko Samaria walipokea Roho wakati mitume, Petro na Yohana, walipoweka mikono juu yao (Mdo. 8:17). Ingawa Luka hasemi waziwazi kwamba walinena kwa lugha, andiko hilo linafunua kwamba jambo fulani la kushangaza sana na lenye kusadikisha lilitokea. Simoni Mchawi alivutiwa sana mpaka akaomba kununua zawadi hiyo. Wasomi wa Biblia wanakubali kwamba ishara aliyoiona Simoni ilikuwa ni hao waamini wapya wakinena kwa lugha, kwa kuwa ndiyo ishara pekee ya kupokelewa Roho inayotajwa mahali pengine katika Matendo.

Tukio la mwisho la mtu kujazwa Roho katika Matendo ya Mitume ni pale mwanafunzi aitwaye Anania alipomwekea mikono Sauli wa Tarso na kuomba pamoja naye ili ajazwe na Roho (Mdo. 9:17-18). Ingawa andiko halisemi Sauli alinena kwa lugha wakati huo, Paulo mwenyewe alishuhudia baadaye kwamba

---

[2] Kutoka Tamko la Imani la Umoja wa Assemblies of God Duniani (WAGF), Namba 9: "Ubatizo Katika Roho Mtakatifu" (tazama Nyongeza ya 2).

aliomba kwa lugha mara nyingi (1 Kor. 14:18). Inaelekea kwamba alianza kunena kwa lugha katika wakati huo.

Kwa sababu hizi na nyinginezo, wasomi wa Kipentekoste wanasisitiza kwamba mtu yeyote anayetafuta kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu anapaswa kutarajia kunena kwa lugha anapojazwa kwa mara ya kwanza.

## KUTANGAZA "INJILI KAMILI"

Njia moja ya mchungaji wa Kipentekoste kufanikiwa katika kukuza ukweli wa Kipentekoste kanisani kwake ni kwa kukazia mara kwa mara "Injili Kamili" katika mafundisho na mahubiri yake. Neno Injili Kamili linataja kuhusu dhana ya kitheolojia iliyoshikiliwa na Wapentekoste siku za kwanza za wimbi la Upentekoste. Wazo hili pia linajulikana kama "Injili ya Miraba Minne." Viongozi wa Kipentekoste wa mwanzoni waliikuza ili kusaidia kusisitiza kile walichoamini kuwa ujumbe mkuu wa Kanisa.

Nguzo nne za Injili Kamili zimefupishwa katika kauli nne fupi: Yesu anaokoa; Yesu anaponya; Yesu anabatiza kwa Roho Mtakatifu; na Yesu anarudi tena. Wapentekoste wa zamani waliona kwamba mafundisho haya manne muhimu yalikuwa yakipuuzwa na makanisa, na yalihitaji kusisitizwa. Nguvu kuu ya kielelezo hiki ni kwamba inamweka Yesu katikati ya mahubiri na mafundisho yetu. Wakati huu ambapo makanisa mengi ya Kipentekoste kote barani Afrika yanaonekana kuwa yamepotea njia, ingekuwa vyema kwa Wapentekoste kurudi kwenye mikazo hii minne, kama ifuatavyo:

### Yesu Anaokoa

Nguzo ya kwanza ya Injili Kamili ni ukweli kwamba Yesu anaokoa. Yeye pekee ndiye Mwana wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu (Yoh. 20:31; 1 Yoh. 4:14). Basi, Wapentekoste wanaamini kwamba tumaini pekee la mwanadamu la wokovu ni kupitia damu iliyomwagika msalabani ya Yesu (Mdo. 4:12; Kol. 1:20). Kila mchungaji wa kweli wa Kipentekoste atahubiri mara kwa mara juu ya msalaba wa Kristo, akiwaita watu "kutubu na kuamini habari njema!" (Mk. 1:15).

### Yesu Anaponya

Nguzo ya pili ya Injili Kamili ni ukweli kwamba Yesu anaponya. Wapentekoste wanaamini kwamba ahadi ya uponyaji wa kiungu iko ndani kabisa mwa injili. Wanaamini kwamba wokovu kutoka dhambini na ukombozi kutoka magonjwa umetolewa katika Upatanisho. Kwa hiyo, uponyaji ni fursa ya waamini

wote (Isa. 53:4-5; Mt. 8:16-17). Kwa sababu hii, wanatangaza kwa ujasiri, "Yesu Kristo ni yeye yule jana na leo na hata milele" (Ebr. 13:8). Kama vile alivyookoa na kuponya watu katika Biblia, anaokoa na kuponya watu hata leo.

**Yesu Anabatiza kwa Roho Mtakatifu**

Nguzo ya tatu ya Injili Kamili ni ukweli kwamba Yesu anabatiza waaminio katika Roho Mtakatifu, akiwatia nguvu kama mashahidi wake kwa waliopotea (Mdo. 1:8). Wapentekoste wanatangaza kwa ujasiri kwamba waamini wote wana haki na wanapaswa kutafuta kwa bidii kubatizwa katika Roho Mtakatifu kulingana na amri ya Kristo (mst. 4-5; taz. Lk. 24:49).

Kama tulivyo-ona hapo juu, uzoefu huu ni tofauti na kuzaliwa upya, na unathibitishwa na ushahidi wa kimwili wa kunena kwa lugha kama Roho wa Mungu awezeshavyo kutamka (Mdo. 2:4). Kila mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuhubiri mara kwa mara juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na aombe na watu wake ili wajazwe.[3]

**Yesu Anakuja Tena**

Nguzo ya nne ya Injili Kamili ni ukweli kwamba Yesu anakuja tena. Yesu aliahidi kwamba angerudi kutoka mbinguni kuchukua watu wake ili wawe pamoja naye (Yoh. 14:3). Wakati wa kuja kwake, wafu katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha, wale ambao bado wako hai watanyakuliwa pamoja nao ili kumlaki Bwana (1 The. 4:16-17; 1 Kor. 15:51-52). Hili ndilo tumaini lenye baraka la Kanisa (Tito 2:13).

Wale wanaomjua Kristo kama Mwokozi wao, na wanaishi maisha ya utii na uaminifu, wanapokea ujumbe wa kuja kwa Kristo kwa furaha. Lakini, wale wanaomkataa Kristo, wanapokea kwa hofu. Mchungaji wa Kipentekoste lazima atangaze ujumbe wa kuja kwa Kristo kwa watu wote kwa ujasiri, akiwataka kuachana na dhambi zote na mambo ya kidunia na kufuata maisha ya utakatifu. Kujua kwamba Kristo anakuja karibuni kunawatia moyo Wakristo wa Kipentekoste kufanya kazi ili kuona watu waliopotea wakija kwa Kristo.

---

[3] Kwa habari zaidi kuhusu kuomba na waamini ili wajazwe na Roho, tazama Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

## HUDUMA YA PENTEKOSTE

Mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima anaelewa kwamba maisha na huduma ya Kipentekoste ni asili ya kushikilia kweli ya Kipentekoste. Anaelewa kwamba imani ya watu haipaswi kamwe "kutegemea hekima ya kibinadamu, bali uweza wa Mungu" (1 Kor. 2:4-5). Imani sahihi inapaswa kusababisha uzoefu sahihi, na imani sahihi na uzoefu unapaswa kusababisha utendaji sahihi. Hebu tuangalie mifano mitano ya maisha na huduma ya Kipentekoste vyenye kutokana na kuambatana na ukweli wa Kipentekoste:

### Kuishi Maisha ya Kujaa Roho

Maisha ya kujaa Roho ni matokeo ya mtu kukubali na kupokea ukweli wa Kipentekoste. Unapohubiri na kuomba pamoja na watu wako ili wajazwe na Roho, Roho wa Mungu ataanza kufanya kazi kwa nguvu maishani mwao. Ataanza kuwafinyanga ili wawe watenda kazi wafaao kwa ajili ya Kristo. Basi, tumia vyema hali hii kuwaongoza watu waishi maisha ya kujazwa na Roho.[4]

### Maombi Yanayoongozwa na Roho

Kuhubiri na kufundisha ukweli wa Kipentekoste kutoka kwenye mimbari kutapelekea maombi yanayoongozwa na Roho katika kanisa. Unapowaongoza washirika wako katika maisha yaliyojazwa na Roho, na kuwafundisha jinsi ya kuomba katika Roho, tabia zao za maombi zitabadilika. Wataanza kuomba maombi yenye nguvu, yanayoongozwa na Roho. Paulo alizungumza kuhusu maombi aina hiyo katika Warumi 8:26-27 (fananisha na 1 Kor. 14:14-15; Efe. 6:18).[5]

### Shahidi Mwenye Nguvu

Yesu aliahidi, "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu" (Mdo. 1:8). Watu wanapojazwa na Roho na kuelekezwa kwenye mavuno, wataanza kushuhudia kwa bidii na nguvu zaidi kuliko hapo awali. Hapa tena ni vizuri utumie hilo vizuri zaidi kwa kuwaongoza watu katika kushuhudia, kupanda makanisa, na shughuli nyingine za uinjilisti.

---

[4] Kitabu, *In Step With the Spirit,* cha Denzil R. Miller, kinapatikana bila malipo kutoka tovuti ya DecadeofPentecost.org.

[5] Kujua zaidi juu ya kufundisha washirika wa kanisa jinsi ya kuomba, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi."

### Karama za Kiroho

Mafundisho kuhusu uaminifu kwa ukweli wa Kipentekoste katika kanisa pia yatahimiza udhihirisho wa karama za kiroho. Kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kuhimiza mazoezi haya katika kanisa kwa kufundisha juu ya hilo somo.[6] Tena, unapaswa kuruhusu muda wa udhihirisho wa karama katika huduma za kanisa. Unaweza kukuza zaidi utendaji wa karama za kiroho kwa kumruhusu Roho kufanya kazi ndani yako na kupitia kwako. Utendaji kazi wa karama za kiroho katika kanisa utasababisha watu wengi zaidi kuokolewa, kuponywa, na kujazwa na Roho.

### Maono ya Umisheni

Hatimaye, unapofundisha ukweli wa Kipentekoste kwa uaminifu kwa watu wako, maono ya umisheni yataundwa katika kanisa. Washirika wa kanisa wanapojazwa na Roho na kufundishwa kuhusu wajibu wao wa kufanya wanafunzi wa mataifa yote, mioyo yao itachomwa na shauku ya wokovu kwa watu kila mahali. Ni lazima basi uendeleze maono hayo kwa kutengeneza mpango thabiti wa umisheni kanisani.

---

Kanisa la Kipentekoste leo linatazama kanisa katika kitabu cha Matendo kama kielelezo chake cha huduma na utendaji uliotiwa mafuta na Roho. Linaongozwa na msukumo mkuu wa umishenari wa Kanisa la kwanza na kuchota kutoka humo mkakati wenye nguvu wa kuwafikia waliopotea kwa injili. Katika siku hizi za mwisho kabla ya kurudi kwa Yesu, wachungaji wa Kipentekoste lazima wawe Wapentekoste kweli katika imani, uzoefu, na utendaji. Na lazima wafundishe watu wao kuwa sawa.

---

[6] Tazama Nyongeza ya 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

~ Sura ya 11 ~

# Hukuza Utendaji na Uzoefu wa Kipentekoste

Mchungaji mmoja wa Kipentekoste mwenye hekima aliwahi kusema, “Ni jambo moja kuwa mhubiri wa Kipentekoste; ni jambo lingine kabisa kuwa mhubiri wa Pentekoste.” Jambo muhimu ambalo mchungaji alikuwa akitoa ni kwamba mhubiri anaweza kuwa Mpentekoste kwa jina bila kuwa Mpentekoste kimatendo. Mchungaji anaweza kujitambulisha kwa dhati na dhehebu la Kipentekoste wakati huo huo akipuuza uzoefu na utendaji wa Kipentekoste. Hata hivyo, mchungaji wa kweli wa Kipentekoste ataendeleza kwa uaminifu uzoefu na utendaji wa Kipentekoste katika kanisa analoongoza.

Katika sura iliyopita, tulichunguza wajibu wa mchungaji wa Kipentekoste kushikilia ukweli wa Kipentekoste. Katika sura hii, tutajadili wajibu wake wa kukuza uzoefu na utendaji wa Kipentekoste.

## HUENDELEZA UZOEFU WA PENTEKOSTE

Wapentekoste ulimwenguni pote wanashikilia kwamba, ingawa kumwamini Mungu ni muhimu, hii pekee haitoshi. Mara nyingi wao huelekeza kwenye

maneno ya Yakobo: “Wewe unaamini kwamba kuna Mungu mmoja. Vizuri! Hata pepo huamini hivyo na kutetemeka” (Yakobo 2:19).

Wapentekoste wanafundisha kwamba, zaidi tu ya imani katika Mungu, ni lazima mtu afurahie uhusiano Naye wa kibinafsi. Uhusiano huo unaanzishwa na kudumishwa kupitia uzoefu wa kibinafsi na Mungu. Matatu katika hayo matukio muhimu ni kuzaliwa upya, ubatizo wa Roho, na ushirika wa kila siku na Kristo. Hebu tuangalie kwa karibu zaidi kila moja ya matukio haya matatu na jinsi wewe, kama mchungaji wa Kipentekoste, unavyopaswa kukuza uzoefu huu katika kanisa ambalo Kristo amekuweka kuliongoza.

**Kuzaliwa Upya**

Kwanza, ni lazima ukazie hitaji la kuzaliwa mara ya pili katika kuhubiri na kufundisha kwako. Lazima utake kwamba kila mshirika wa kanisa awe amezaliwa kweli kutoka juu. Na lazima uhakikishe kwamba kila mtu anayehudhuria kanisa lako anapata changamoto kuhusu kumpokea Kristo kama Mwokozi. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya na Nikodemo. Alimpa changamoto hiyo kiongozi wa kidini, kwamba, “Lazima uzaliwe mara ya pili” (Yoh. 3:7). Maneno haya ya Yesu yanapaswa kuwa midomoni mwako mara kwa mara unapofundisha na kuhubiri.

Kuzaliwa mara ya pili ni “kuzaliwa na Mungu” (Yoh. 1:13; taz. 3:5, 8). Mtu huzaliwa na Mungu anapokuja kwa Kristo kwa unyenyekevu, kumkiri Yeye kama Bwana na Mwokozi, kutubu dhambi zake, na kuweka tumaini lake lote Kwake kwa ajili ya msamaha na utakaso. Wakati huo, uongofu wa kiroho unaobadilisha maisha hutokea. Kristo anaingia katika maisha, na Roho Mtakatifu anawabadilisha kutoka ndani kwenda nje. Paulo aliandika hivi: “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya” (2 Kor. 5:17, maelezo ya pembeni).

**Ubatizo wa Roho**

Pamoja na kuwaongoza watu katika kuzaliwa upya, kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste lazima uwape changamoto wale wote wanaompokea Kristo kama Mwokozi, wabatizwe upesi katika Roho Mtakatifu. Hii ilikuwa ni kawaida katika Kanisa la kwanza. Mitume wa Yerusalemu waliposikia kwamba watu wanaokolewa huko Samaria, wakawatuma Petro na Yohana mara moja kuomba pamoja nao ili wampokee Roho Mtakatifu (Mdo. 8:14-17). Miaka mingi baadaye, Paulo alipofika Efeso, swali la kwanza aliloliuliza wanafunzi huko lilikuwa hili: “Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?” (Mdo. 19:2). Mtume

alipogundua kwamba hawakumpokea Roho Mtakatifu, mara moja aliweka mikono juu yao, na "Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri" (mst. 6).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufuate mfano wa mitume na ufanye bidii kuhakikisha kwamba kila Mkristo mpya anabatizwa mara moja katika Roho Mtakatifu. Lazima uhakikishe zaidi kwamba kila mtu anayempokea Roho ana ufahamu wazi wa kwa nini Mungu huwabatiza waumini katika Roho Mtakatifu. Anawapa Roho wake ili kuwatia nguvu kama mashahidi wa Kristo (Mdo. 1:8). Kwa hiyo utataka kuwapa changamoto waamini wapya waliobatizwa kwa Roho kushirikisha habari za Kristo kwa ujasiri na familia zao na marafiki.

Ili kukuza kanisa la kitume kwa kweli lililowezeshwa na Roho, utahitaji kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu ya hitaji la kila mwamini kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Mafundisho yako juu ya ubatizo wa Roho yanapaswa kujibu kwa uwazi maswali matatu: (1) Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni nini? (2) Kwa nini kila mwamini lazima abatizwe katika Roho Mtakatifu? na (3) Mtu anawezaje kumpokea Roho Mtakatifu?[1]

Zaidi ya hayo, utahitaji kuwapa washirika kanisani nafasi za mara kwa mara za kujazwa au kujazwa tena na Roho Mtakatifu. Hii ina maana kwamba utahitaji kutengeneza nafasi katika ibada za kanisa kwa washirika kumtafuta Mungu na kumwomba Roho Mtakatifu (rej. Lk. 11:13). Kwa kuongezea, utahitaji kukuza kwa uangalifu mazingira katika ibada za kanisa ambapo watu wanaweza kumpokea Roho kwa urahisi. Hali kama hiyo itaingiza uwepo dhahiri wa Mungu na hali ya imani yenye matarajio katika mioyo ya watu wa Mungu.[2]

### Ushirika na Mungu Kila Siku

Hatimaye, lazima uhakikishe kwamba washirika wa kanisa lako wanaishi katika ushirika wa kila siku na Kristo. Yesu alitaja tendo hili kama kukaa, au kukaa ndani ya Kristo (Yoh. 15:4-7). Paulo analiita kutembea "katika Roho" (Gal. 5:25).

---

[1] Kwa muhtasari wa mahubiri juu ya mada hii, ona kitabu, *Kuitangaza Pentekoste: Mihutasari 100 ya Mahubiri Kuhusu Nguvu za Roho Mtakatifu,* Mahubiri Namba 2: "Ubatizo Katika Roho Mtakatifu." Kitabu hiki kinapatikana katika mfumo wa kielektroniki (PDF) kwenye tovuti ya www.DecadeofPentecost.org.

[2] Kwa habari zaidi juu ya kuwatayarisha waamini kumpokea Roho Mtakatifu, ona kitabu, *Mobilizing for Mission,* Sura ya 7: "Jinsi ya Kuhubiri Juu ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu." Kinapatikana bila gharama kwenye tovuti ya www.DecadeofPentecost.org.

Kwa hiyo ni lazima uwafundishe watu kwamba haitoshi tu kuzaliwa mara ya pili, au hata kujazwa na Roho. Wakristo lazima wajitolee wenyewe kuishi katika ushirika na Kristo usiovunjika kwa njia ya Roho Mtakatifu (rej. Yoh. 14:16-18, 23; 1 Yoh. 1:3).

- Kupitia Neno ni lazima uwafundishe watu wa Mungu kwa mfano wa maisha yako pia jinsi ya kufanya yafuatayo:
- "Kuenenda katika Roho" (Gal. 5:25).
- "Kuishi kwa kufuatana na Roho" kwa kutia "nia zao katika mapenzi ya Roho" (Rum. 8:5-6).
- Kumkaribisha Roho wa Mungu atembee nao kama Mtetezi, Msaidizi na Mfariji (Yoh. 14:16).
- "Kuomba katika Roho kila wakati kwa kila namna ya sala na maombi" (Efe. 6:18; taz. Rum. 8:26; Yuda 20).
- Kumtegemea Roho Mtakatifu kuangaza akili zao na kuchochea mioyo yao wanapotafakari Maandiko (Yoh. 16:13).
- Kuzaa na kukuza matunda ya kiroho katika maisha yao (Gal. 5:22-23).

Ili kutimiza hayo, utahitaji kuwafundisha watu wa Mungu kwa bidii kile ambacho Maandiko yanasema kuhusu maisha yanayotiwa nguvu na Roho. Utahitaji pia kuonyesha kwa vitendo hayo katika maisha yako mwenyewe na huduma.

## HUENDELEZA UTENDAJI WA PENTEKOSTE

Pamoja na kuwaongoza watu wa Mungu katika uzoefu wa Kipentekoste, wewe, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwaongoze kwenye utendaji wa kweli wa Kipentekoste. Ili kufanya hivi, ni lazima uwe tayari kukuza tabia kumi za msingi za Kipentekoste katika kanisa lako, zifuatazo:

### Mahubiri Yenye Upako

Kwanza, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima utafute upako wa kutangaza Neno la Mungu. Upako ni uwepo dhahiri wa Mungu ambao huja kutulia juu ya mfuasi aliyejazwa na Roho, kumwezesha kuhudumu kwa nguvu na ufanisi zaidi. Katika kutafuta upako, utakuwa unafuata mfano wa Yesu na mitume. Yesu alisema hivi juu ya mahubiri yake mwenyewe, "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kutangaza habari njema" (Lk. 4:18). Mitume pia walihubiri katika upako wa Roho Mtakatifu (Mdo. 2:14-18; 4:8; 13:8-12).

Jihakikishie upako wa Roho kwa kumkaribisha aje juu yako unapohudumu Neno la Mungu. Kisha, atakapokuja, itikia kwa imani na kutangaza Neno la Mungu kwa ujasiri (Mdo. 4:31). Yesu ameahidi kuthibitisha mahubiri ya Neno yaliyotiwa mafuta kwa ishara za miujiza (Mk 16:15-18).

**Kuombea Wagonjwa**

Pili, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitoe kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka, ukimwamini Mungu kwa ajili ya uponyaji wa kimungu. Yesu aliwatuma wanafunzi wake kumi na wawili na kuwapa amri hii: "Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo. Mmepokea bure; toeni bure" (Mt. 10:8). Yakobo aliwaagiza viongozi wa kanisa hivi, "Je, kuna yeyote kati yenu aliye mgonjwa? Na awaite wazee wa kanisa wamwombee na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kuomba kwa imani kutamponya mgonjwa; Bwana atamwinua" (Yakobo 5:14-15).[3]

**Kushiriki Katika Umisheni**

Tatu, kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uhakikishe kwamba utume unabakia kuwa kwenye nafasi ya juu katika mipango ya kanisa lako. Shauku katika ushiriki wa utume ndio kiini kikuu cha kuwa Mpentekoste kweli. Yesu alijiunga na utume wa Pentekoste alipowaambia wanafunzi wake, "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Mdo. 1:8). Kanisa haliwezi kujiita kuwa la Kipentekoste kwa uhalali na wakati huo huo likiepuka kufanya umisheni. Kwa hiyo, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unawajibika kuanzisha mpango hai wa umisheni kanisani.

Ili kufanya hivyo, utahitaji kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu ya utume wa Mungu. Utume wa Mungu ni mpango wake wa kukomboa na kuwaita kwake watu kutoka kila lugha, kabila, na taifa duniani kabla ya kurudi kwa Yesu (rej. Mt. 24:14; Uf. 5:9). Lazima uhakikishe kwamba kila mshiriki wa kanisa anaelewa wajibu wake wa kushiriki katika kutimiza utume wa Mungu.

---

[3] Kwa ufahamu zaidi juu ya mada hii, tazama kitabu cha kiada cha Mfululizo wa Masomo ya Ugunduzi wa Africa's Hope kiitwacho, *Power Ministry: How to Minister in the Spirit's Power,* Sura ya 11: "Jinsi ya Kuponya Wagonjwa."

Utahitaji pia kuandaa fursa kwa washirika wa kanisa kujihusisha kibinafsi katika umisheni. Unaweza kufanya hivi kwa kuwaongoza kwenda safari fupi fupi za umisheni, mikutano ya hadhara, uinjilisti mitaani, na huduma zingine zinazofanana na hizo. Zaidi ya hayo, utataka kupanga matukio ya mara kwa mara ya kuhamasisha umisheni ambapo washiriki wanahimizwa kutoa ahadi zao za kifedha ili kuunga mkono mpango wa umisheni wa kanisa. Kila kanisa la Kipentekoste linapaswa kuwa na wamishenari linalowaunga mkono kihuduma na kuwategemeza kwa fedha na maombi yao.[4]

**Wito wa Mungu**

Nne, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima utilie mkazo wito wa Mungu katika huduma. Wito wa Mungu ni kuwachagua na kuwaita watu kwake na kwa makusudi yake. Yesu, ambaye mwenyewe alitumwa na Mungu, sasa anawaita na kuwatuma wengine kwenda kwenye mavuno (Mt. 4:19; Yoh. 20:21). Aliwaambia wanafunzi wake, "Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi na kuwaweka ili mwende mkazae matunda" (Yoh. 15:16).

Kama kanisa la Kipentekoste litapanuka (kama Mungu anavyokusudia), lazima wapanda makanisa mapya waongezeke na kusambaa, pamoja na wachungaji, wamishenari, wainjilisti, na wahudumu wengine wa injili wa kudumu. Hawa lazima watoke katika makanisa yetu ya Kipentekoste. Basi ni lazima uwatie moyo watu wako kusikiliza wito wa Mungu. Na anapozungumza nao kama alivyofanya kwa nabii wa kale, wanapaswa kujibu, "Mimi hapa. Nitume mimi!" (Isa. 6:8).[5]

**Vita vya Kiroho**

Tano, kama mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika, lazima uwe tayari kushiriki katika vita vya kiroho. Ni lazima wakati wote uwe tayari kukabiliana na kuzishinda nguvu za pepo zinapojidhihirisha. Ndivyo Yesu na mitume

---

[4] Kwa habari zaidi juu ya mada hii, tazama Sura ya 40: "Kutengeneza Mpango wa Utume wa Kanisa la Mahali Pamoja."

[5] Ili kupata habari zaidi juu ya wito wa Mungu katika huduma, tazama Sura ya 1: "Mtu wa Uzoefu." Muhtasari wa mahubiri kumi na mawili juu ya wito wa Mungu unaweza kupatikana katika kitabu, *Kumtangaza Kristo kwa Mataifa: Jumbe 100 Kuhusu Utume Unaowezeshwa na Roho Mtakatifu,* Sehemu ya 5: "Wito wa Mungu." Muhtasari huu unapatikana katika mfumo wa kielektroniki kwenye tovuti ya www.DecadeofPentecost.org.

walivyofanya (Mk 1:21-28; Mdo 16:16-18). Lazima uwaandae washirika wako kufanya vivyo hivyo.[6]

## Ibada Zenye Uhai

Sita, lazima uhakikishe kwamba kanisa lako linafanya ibada iliyochangamka, yenye uvuvio wa Roho. Ibada kama hiyo ni alama ya Kipentekoste. Wapentekoste wanajulikana kwa ibada zao zilizo huru na za wazi. Huduma zao ni pamoja na kuimba kwa mwamko, kupiga makofi, kucheza, na kuinua mikono. Hata hivyo, haitoshi kwamba ibada ya kanisa lako iwe yenye msisimko. Ni lazima iwe na upako. Na lazima iwe ya kweli. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba, "Mungu ni roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli" (Yoh. 4:24). Paulo aliongeza, "Palipo na Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru" (2 Kor. 3:17).

Wakati wa ibada, unapaswa kuhimiza kila anayeabudu kuelekeza mawazo yake kwa Mungu na ukuu Wake. Na unapaswa kuwafundisha watu wa Mungu kufungua mioyo yao kwa mtembeo wa Roho wa Mungu.[7]

## Ushuhuda Binafsi

Saba, unapaswa kuwahimiza washirika wa kanisa lako kuwashirikisha wengine ushuhuda wao. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa tayari kila wakati kusimulia habari ya kile Mungu alichofanya katika maisha yao ambacho Mungu amefanya maishani mwao (1 Pet. 3:15). Biblia inashauri hivi: "Waliokombolewa na BWANA wasimulie habari zao" (Zab. 107:2).

Ushuhuda ndio kiini cha maana ya kuwa shahidi wa Kristo. Ni njia rahisi lakini yenye nguvu kwa waamini kushirikisha injili kwa waliopotea. Kwa hiyo himiza zoezi hilo miongoni mwa washirika wa kanisa. Pia ni vizuri utoe nafasi katika ibada kanisani kwa watu wa Mungu kutoa shuhuda jinsi Roho anavyofanya kazi katika maisha yao.

---

[6] Kwa ufahamu zaidi juu ya mada hii, tazama Sura ya 22: "Kujihusisha Katika Vita vya Kiroho." Tazama pia kitabu cha Mfululizo wa Masomo ya Ugunduzi wa Africa's Hope, *Power Ministry: How to Minister in the Spirit's Power,* Sura ya 12: "Kutoa Pepo."

[7] Kwa habari zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 18: "Kuliongoza Kanisa Katika Kuabudu."

**Karama za Kiroho**

Nane, kama mchungaji wa Kipentekoste, ni lazima utilie mkazo utendaji wa Roho katika ibada za kanisa, unaodhihirisha karama za kiroho. Hii ilikuwa kawaida katika Kanisa la kwanza, na inapaswa kuwa desturi ya kila kanisa la Kipentekoste leo (kama katika Mdo. 11:28-30; 13:1-2; 21:10-14). Katika 1Wakorintho 12:8-10, Paulo anazungumza kuhusu karama tisa za kiroho:

"Mtu mmoja kwa Roho hupewa ujumbe wa hekima, na mwingine ujumbe wa maarifa katika Roho yeye yule, na mwingine imani katika Roho huyohuyo, na mwingine karama za kuponya katika Roho huyo mmoja, na mwingine miujiza. na mwingine unabii, na mwingine kupambanua roho, na mwingine kunena kwa lugha, na mwingine tafsiri za lugha. Hayo yote ni kazi ya Roho huyo huyo mmoja, naye humgawia kila mtu kama apendavyo yeye mwenyewe."[8]

Unapowafundisha watu kuhudumu katika karama hizi, kanisa litajengwa, Mungu atatukuzwa, na ufalme wake utakuzwa.

Lakini ni vizuri ujue kwamba udhihirisho wa karama za kiroho hauji tu. Lazima kuwe na shauku ya karama, na udhihirisho wake utiwe moyo (1 Kor. 12:31; 14:1). Basi tamani udhihirisho wa karama za kiroho katika maisha yako mwenyewe, na uhimize udhihirisho wake katika maisha ya wengine. Unaweza kufanya hivyo kwa kufundisha na kuhubiri juu ya somo hilo. Unapaswa pia kuwa mfano wa matumizi sahihi ya zawadi hizo. Unaweza pia kuhimiza udhihirisho wa karama za kiroho kwa kutoa nafasi katika ibada za kanisa (14:26) na kwa kulinda dhidi ya matumizi mabaya (14:39-40).[9]

**Kufanya Maombezi**

Tisa, lazima uliongoze kanisa lako katika kufanya maombezi ya kujitoa. Kama kanisa la kitabu cha Matendo, kanisa la Kipentekoste katika Afrika leo lazima lijitoe kwa maombi (Mdo. 1:14; 4:23-32; 12:5; 13:2). Kama vile Yesu alivyowafundisha wanafunzi wake jinsi ya kuomba, lazima uwafundishe watu wako vivyo hivyo (Lk. 11:1-13). Unaweza kufanya hivi kwa kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu ya maombi, na kwa kuonyesha kwa uaminifu

---

[8] Tazama Nyongeza ya 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

[9] Kwa habari zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 21: "Kuhudumu Katika Nguvu za Roho."

maisha ya maombi mbele ya kanisa. Watu wanapomtazama mchungaji wao akiomba, wao pia watatiwa moyo kuomba (Lk. 11:1; Kut. 33:10).10

**Maisha Matakatifu**

Mwisho: Wewe kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, tamani washirika wa kanisa waishi maisha matakatifu, ya kumheshimu Mungu (1 Yoh. 2:6). Kuishi maisha matakatifu ni agizo la Maandiko na ni desturi ya waamini wa kweli wa Kipentekoste duniani kote (1 Pet. 1:16). Kama vile jina Mkristo linavyodokeza, wafuasi wa Kristo wanapaswa kujitahidi kuwa kama Yeye. Ni lazima wawe watakatifu kwa sababu Mungu wanayemwakilisha ni mtakatifu. Paulo aliwahimiza Wakristo wa Filipi kuwa "wasio na lawama na safi, watoto wa Mungu wasio na hatia katika kizazi kilichopotoka na chenye ukaidi" (Flp. 2:15).

Kwa hiyo ni lazima uwaonyeshe watu wako jinsi ya kuishi maisha kama ya Kristo. Ili kufanya hivyo, utahitaji kufundisha na kuhubiri mara kwa mara juu ya takwa la Wakristo kuishi maisha matakatifu na safi. Lazima uwaonyeshe watu mfano jinsi maisha kama hayo yalivyo. Paulo aliwakumbusha waamini wa Filipi kwamba, "Ninyi ni mashahidi, na Mungu pia, jinsi tulivyokuwa watakatifu, wenye haki na wasio na lawama miongoni mwenu mlioamini" (1 The. 2:10). Alizidi kuwahimiza waamini, "Fuateni mfano wangu, kama mimi ninavyoufuata mfano wa Kristo" (1 Kor. 11:1). Ni lazima uweze kusema maneno hayo hayo kwa washirika wa kanisa lako.

---

Upentekoste wa kweli hauwezi kamwe kupunguzwa na kuwa orodha ya imani na taratibu za kidini, bila kujali jinsi imani hizo zinavyoweza kuwa halisi. Kwa asili yake, Upentekoste ni njia ya maisha inayotaka kujiunganisha na uzoefu na desturi za waamini wa karne ya kwanza kama ilivyoelezwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume na maandiko ya mitume. Kwa hiyo kila mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na lengo la kuliongoza kanisa lake katika uzoefu na utendaji halisi wa Kipentekoste.

[10]Kwa habari zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi."

# ~ Sura ya 12 ~

# Anathamini Urithi wa Kipentekoste

Leila McKinney alikuwa mishenari wa kwanza wa Kipentekoste kwa watoto katika Afrika. Alijazwa na Roho katika siku za mwanzo za Umwagiko wa Roho wa Mtaa wa Azusa huko Los Angeles, California, Marekani, kati ya 1906 hadi 1908. Shauku ya umisheni ilijaa na kuambatana na uamsho huo, na Leila pamoja na shangazi yake Julia Hutchins na wengine, walichochewa kwenda Afrika kuhubiri injili. Leila aliandika katika gazeti la The Apostolic Faith lililochapishwa na shirika hilo la umisheni kwamba, “Niko tayari kumwamini hadi Afrika. Najua Bwana anataka niende huko. Ninataka kuwashuhudia watu na kuwafundisha watoto kuhusu Bwana aliyebarikiwa, na kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Niko tayari kuwaacha wapendwa wangu wote kwa ajili Yake.” Hadithi ya Leila McKinney ni moja tu ya mamilioni ya hadithi zinazoambatana na uamsho wa Kipentekoste barani Afrika.

Ni muhimu mchungaji Mwafrika wa Kipentekoste aelewe na kufahamu jinsi ujumbe wa Pentekoste ulivyokuja na kufika katika bara hili. Mchungaji mmoja Mwafrika alisema hivi wakati fulani, “Ikiwa hatujui tulikotoka, hatujui sisi ni akina nani, au tunakoelekea. Tunapokuwa hatuelewi maisha yetu ya zamani, sisi

ni kama mashua bila tanga. Tunakuwa na hatari ya kupeperuka bila malengo, bila mwelekeo au kusudi wazi. Lakini, tunapojua tulikotoka na kwa nini tuko hapa, tunaweza kusonga mbele kwa ujasiri katika siku zijazo."

Sura hii itajibu maswali kadhaa muhimu kuhusu mwanzo wa Upentekoste barani Afrika, kama: Nini chimbuko la vuguvugu la Upentekoste wa kisasa? Upentekoste ulikuja Afrika lini na kwa jinsi gani? Pentekoste ilieneaje katika bara zima? Je, kanisa la Kipentekoste barani Afrika linakabili changamoto gani leo? Ni nini mustakabali wa Upentekoste katika Afrika?

## MWANZO WA HARAKATI

Mwishoni mwa Desemba 1900, katika shule ndogo ya Biblia huko Topeka, Jimbo la Kansas, Marekani, Charles Fox Parham aliwapa wanafunzi wake kazi ya kufanya utafiti. Aliwaambia wachunguze Maandiko ili kugundua "ushahidi wa Biblia" wa ubatizo katika Roho Mtakatifu. Baada ya muda wa kusoma kwa kina, wanafunzi waliwasilisha matokeo yao kwa Parham. Walikuwa wamehitimisha kwamba ushahidi wa kibiblia wa ubatizo wa Roho ulikuwa kunena kwa lugha kama Roho anavyowezesha mtu kutamka.

Kisha walianza mkutano wa maombi ambao uliendelea kwa siku kadhaa. Mara baada ya saa sita usiku mnamo Januari 1, 1901, Roho Mtakatifu alikuja kwa nguvu juu ya mwanamke aliyeitwa Agnes Ozman. Kimuujiza, alianza kunena kwa lugha kama Roho alivyomwezesha kutamka. Baada ya siku chache, wengine wengi, pamoja na Parham, walibatizwa katika Roho Mtakatifu, ikithibitishwa na kunena kwa lugha. Kama matokeo ya kujazwa na Roho, Parham na wanafunzi wake walianza kuhubiri injili kwa nguvu nyingi na mamlaka, sawa na waamini katika kitabu cha Matendo. Mioyo yao ilishikwa na shauku kubwa ya umishenari. Parham aliamini kwamba Mungu alikuwa akimwaga Roho Wake ili kuliwezesha kanisa kufikishia mataifa habari njema za Kristo kabla ya kurudi Kwake karibuni.

Mnamo mwaka wa 1905, Parham alihamisha shule yake hadi Houston, Jimbo la Texas, Marekani, ambako aliendelea kufundisha kuhusu ubatizo katika Roho Mtakatifu. Muda si mrefu baadaye, Lucy Farrow alijiunga na harakati. Kisha alimtambulisha Parham kwa William J. Seymour, mhubiri mwenye asili ya Kiafrika aliyekuwa anahubiri kuhusu utakatifu. Seymour alisikiliza Parham akifundisha, na yeye pia aliukubali ujumbe wa Kipentekoste.

Muda mfupi baadaye, Seymour alipokea mwaliko kutoka kwa kanisa dogo la dhehebu la Holiness huko Los Angeles, California, akawe mchungaji wao.

Seymour alikubali mwaliko huo na akasafiri hadi Los Angeles. Katika mahubiri yake ya kwanza hapo kanisani, alihubiri ujumbe juu ya ubatizo katika Roho Mtakatifu na ushahidi wa kunena kwa lugha. Aliyekuwa mchungaji wa hilo kanisa, Julia Hutchins, aliukataa ujumbe huo na kumfungia Seymour asihubiri katika hicho kituo chake.

Seymour akaanza kuhubiri ujumbe wa Kipentekoste katika nyumba za baadhi ya washirika wa kanisa. Alipokuwa akihubiri na watu walipokuwa wakiomba, wengi walijazwa na Roho Mtakatifu. Umati wa watu ukawa mkubwa sana kiasi kwamba walilazimika kununua jengo kubwa la zamani la kanisa kwenye Barabara ya Azusa. Mungu aliendelea kumwaga Roho Wake, na kwa muda wa miaka mitatu, kuanzia 1906 hadi 1908, maelfu walikuja kutoka duniani kote na kujazwa na Roho Mtakatifu. Walirudi makwao wakiwa na ujumbe kwamba Pentekoste imekuja.

Wamishenari wa Kipentekoste walitoka Mtaa wa Azusa hadi mataifa zaidi ya 25 katika miaka miwili, ikiwa ni pamoja na Uchina, India, Japan, Misri, Liberia, Angola, na Afrika Kusini. Uamsho mkuu wa Mtaa wa Azusa ulihusika sana kueneza Pentekoste duniani kote kuliko kingine chochote. Leo, kiasi cha madhehebu 26 tofauti ya Kipentekoste yanaweza kufuatilia mwanzo wake hapo Azusa Street, ikiwa ni pamoja na Assemblies of God.[1]

Katika miaka hiyohiyo, Mungu alikuwa akimmiminia Roho wake mahali pengine ulimwenguni. Vituo vingine vilivyopokea umwagiko wa Pentekoste siku za mwanzoni vilikuwa Wales (1904), India (1905), Uingereza (1907), Korea (1907), Chile (1909), na kwingineko. Mungu alikuwa anatimiza ahadi aliyoitoa kwa nabii Yoeli: “Katika siku za mwisho, ... nitamimina Roho yangu juu ya wote wenye mwili” (Mdo. 2:17; taz. Yoe. 2:28).

## PENTEKOSTE YAWASILI AFRIKA

Hebu sasa tuangalie jinsi ujumbe wa Pentekoste ulivyokuja Afrika na jinsi ulivyoenea katika bara zima.

---

[1] Kwa habari zaidi kuhusu jinsi Uamsho wa Mtaa wa Azusa ulivyoigusa Afrika, tazamaa kitabu kiitwacho, *From Azusa to Africa to the Nations*, Toleo la Pili, cha Denzil R. Miller, kinachopatikana bila malipo katika tovuti ya www.DecadeofPentecost.org.

**Pentekoste Inakuja Afrika**

Wamishenari wa kwanza wa Kipentekoste waliotoka Marekani hadi Afrika walitokea kituo cha Azusa na kuja moja kwa moja. Walifika Liberia mwaka wa 1907. Kundi lao lilikuwa pamoja na Lucy Farrow, JW na Julia Hutchins, mpwa wao, Leila McKinney, na baadaye mwaka huo, Edward McCauley. Jumla ya wanaume, wanawake na watoto wao wapatao kumi na wawili walitoka Azusa hadi Liberia mwaka huo katika vikundi viwili. Katika muda wa majuma machache, saba kati yao walikufa kwa malaria au homa ya kuhara. Hata hivyo, watu wengi wa Liberia walimjia Bwana Yesu na kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Kanisa la kudumu la kwanza la Kipentekoste barani Afrika lilipandwa mjini Monrovia mwaka wa 1907. Vile vile, wamishenari kutoka Azusa walisafiri hadi Afrika Kusini na Angola.

Mungu pia alitumia wenyeji Waafrika kueneza ujumbe wa Kipentekoste. Hadithi mbili za kusisimua ni za Elias Letwaba wa Afrika Kusini na William Wadé Harris wa Liberia. Wapendwa hawa walisaidia kuanzisha harakati ambazo ziligusa mataifa kadhaa ya Afrika Kusini na Magharibi mwa Afrika, na kusababisha mamia ya maelfu kuja kwa Kristo.

Elias Letwaba (1870-1959) ameitwa mhubiri wa Kipentekoste mwenye ushawishi mkubwa zaidi katika historia ya Afrika Kusini. Mnamo mwaka wa 1870, Elias alipokuwa angali tumboni, mama yake alipokea maono kutoka kwa Mungu. Roho alimwambia kwamba siku moja Mungu atamtumia mwanawe kama chombo chake kuanzisha makanisa mengi. Hivyo, Letwaba alikua akiwa na njaa kubwa ya kumjua Mungu na kutumiwa naye.

Mnamo 1908, alikutana na John G. Lake, mishenari wa Kimarekani, ambaye kabla ya kwenda Afrika Kusini, alikuwa amepokea Roho Mtakatifu katika huduma ya Charles Parham. Lake pia alikuwa amehudhuria Uamsho wa Mtaa wa Azusa huko Los Angeles. Letwaba na Lake walisafiri pamoja katika huduma hadi 1913, wakati Lake aliporudi Marekani.

Kama Mungu alivyomfunulia mama yake, Letwaba akawa mhubiri na mwalimu wa Kipentekoste mwenye nguvu, akiwaongoza wengi katika wokovu na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Aliona maelfu wakiponywa na maelfu wengine kuokolewa katika huduma yake huko Afrika Kusini na Rhodesia (Zimbabwe). Letwaba alishirikiana na Apostolic Faith Mission nchini Afrika Kusini. Alianzisha Shule ya Biblia ya Patmo, seminari ya kwanza ya Afrika Kusini iliyoendeshwa na watu weusi. Letwaba alihubiri bila kuchoka hadi kifo chake mwaka 1959.

William Wadé Harris (1860-1929) alitumiwa na Mungu kueneza injili kote Afrika Magharibi. Ameitwa “mwinjilisti mwenye mafanikio zaidi barani Afrika.” Wakati wa miaka yake ya utu uzima, alishirikiana na makanisa ya Methodist na Episcopal nchini Liberia. Aliishi Monrovia wakati wamishenari wa Mtaa wa Azusa wakiwa huko. Wengine wanaamini kwamba wamishenari hao Wamarekani Weusi walikuwa chanzo cha theolojia ya Kipentekoste ya Harris.

Harris alishuhudia kwamba malaika Gabrieli alimtokea katika maono akimwambia kwamba wengi watakuja kwa Kristo kupitia huduma yake ya kinabii. Kufuatia maono hayo, Harris alisafiri kila mahali katika nchi za Liberia, Côte d'Ivoire, Ghana, na Sierra Leone, akiwaambia watu waache dhambi zao na kumgeukia Kristo. Alihudumu katika nguvu za Roho, akitoa pepo, akiponya wagonjwa, na kunena kwa lugha. Alisisitiza zaidi kwamba watu waache uchawi wao, wamwamini Yesu, na wasubiri Wazungu waje na Biblia zao ili kuwafundisha Neno la Mungu. Inakadiriwa kuwa zaidi ya watu laki moja walipata wokovu kupitia huduma yake.

Letwaba na Harris ni mifano miwili tu ya maelfu ya wachungaji, wainjilisti, walimu na wamishenari Waafrika ambao wamehubiri Injili Kamili katika Afrika, wakitangaza kwamba Yesu anaokoa, anaponya, anabatiza katika Roho Mtakatifu, na atarudi hivi karibuni.

## Pentekoste Yaenea Kote Afrika

Hadithi ya kuenea kwa Pentekoste barani Afrika kupitia Assemblies of God (AG) ni simulizi la Roho akifanya kazi kupitia kwa wamishenari kutoka nchi za Magharibi na wahudumu wa Kiafrika ili kupanda kanisa Afrika. Ingawa AG ni moja tu ya makanisa mengi ya Kipentekoste barani humu, Mungu ametumia harakati hiyo kwa nguvu kueneza ujumbe wa Kristo. Hebu tutazame mbili kati ya simulizi hizo nyingi.

*Liberia.* Mnamo 1908, Jasper Klabioh Toe aliomba hivi, "Ikiwa kuna Mungu muumbaji, naomba msaada nimpate." Mungu alizungumza na Toe, akimwambia “tembea hadi baharini.” Wakati huo huo, Roho alikuwa akishughulika na mishenari wa Marekani, John Moore Perkins. Perkins alikuwa amebatizwa katika Roho Mtakatifu alipokuwa akihudhuria uamsho wa Kipentekoste huko Toronto, Kanada. Baadaye, Mungu alimwelekeza kupeleka ujumbe wa Kristo Liberia.

Akiwa anasafiri kando ya pwani ya Liberia, Perkins alisikia Roho akimwambia aende pwani mahali fulani. Nahodha wa meli alimuonya, "Hapa si

mahali salama." Perkins hata hivyo alisisitiza kwamba aachwe hapo. Basi, yeye na timu yake walishuka hapo mahali ambapo Roho alikuwa amemwongoza Toe. Ilikuwa Siku ya Krismasi mwaka wa 1908. Perkins alimshirikisha Toe injili, ambaye alimpokea Kristo mara moja. Kazi ambayo Toe na Perkins walianza ilikua mpaka ikawa Liberia Assemblies of God. Leo, hilo kanisa ndilo kundi kubwa zaidi la Kipentekoste katika hiyo nchi.

*Nigeria.* Mapema miaka ya 1930, Augustine Ehurieiwe Wogu wa Port-Harcourt, Nigeria, alipata nakala ya Pentecostal Evangel, gazeti lililochapishwa na Assemblies of God, Marekani. Wogu alivutiwa na kile alichosoma katika gazeti hilo kuhusu uponyaji wa kimungu na ubatizo katika Roho Mtakatifu. Alianza kuwaombea wagonjwa na kuwaongoza watu katika ubatizo wa Roho kwa sababu hiyo. Kanisa alilokuwa akihudhuria lilipokataa kupokea mafundisho yake ya Kipentekoste, Wogu na wengine wachache waliondoka na kuanzisha kanisa huru la Kipentekoste waliloliita Kanisa la Yesu Kristo.

Miaka kadhaa baadaye, mnamo 1939, Wogu alikutana na wamishenari wa AG ya Marekani huko Port Harcourt. Walikuwa wamekuja Nigeria kuchunguza uwezekano wa AG kuanza kazi huko. Wogu aliwaomba watume wamishenari kumsaidia. Shirika lilikubali na kutuma timu iliyoongozwa na W. Lloyd Shirer kufanya kazi na Wogu. Walikubali kuliita kanisa hilo Assemblies of God Nigeria. Leo, ndilo kanisa kubwa zaidi la kitaifa la AG barani Afrika lenye waumini na wafuasi zaidi ya milioni tatu.

Hizi ni hadithi mbili tu kati ya mamia ya hadithi ambazo zinaweza kusimuliwa. Wanasaidia hata hivyo, kuwasilisha hadithi ya jinsi Roho wa Mungu alivyoenea kote Afrika kupitia ushirikiano wa Waafrika na wale ambao Roho aliwatuma Afrika. Hadithi nyingine zingeweza kusimuliwa jinsi moto wa Pentekoste ulivyowashwa katika mashirika mengine ya makanisa katika bara zima, kama vile Kanisa la Pentekoste nchini Ghana na Kanisa la Wanaoamini Injili Kamili nchini Ethiopia.

*Africa Assemblies of God.* Wakati ujumbe wa Kipentekoste ulipofika Liberia mwaka wa 1906, hapakuwa na makanisa ya Kipentekoste au waamini popote barani Afrika. Hata hivyo, Mungu alikuwa anaanza kumimina Roho wake barani. Ukuaji wa Assemblies of God ni mfano mzuri wa jinsi ambavyo Mungu amebariki bara hili. Kufikia mwaka wa 1948, Assemblies of God Afrika ilikuwa imeongezeka na kufikia waamini 40,000, wakikutana katika makanisa yapatayo 700 katika mataifa 11 ya Afrika.

Mnamo mwaka wa 1989, AG iliunda Africa Assemblies of God Alliance (AAGA) au Umoja Wa Makanisa Ya Assemblies Of God Barani Afrika, uliojumuisha makanisa ya kitaifa kutoka bara zima. Mwaka uliofuata, AAGA ilizindua mkazo wao wa “Miaka Kumi Ya Mavuno”, kuanzia mwaka wa 1991 hadi 2000. Mkazo huo ulikuwa katika upandaji kanisa unaowezeshwa na Roho Mtakatifu na umisheni. Katika miaka hiyo kumi kanisa lilikua kutoka wafuasi milioni 2.1 wanaokutana katika makanisa 11,688 katika nchi 31, hadi wafuasi milioni 6.3 waliokutana katika makanisa 24,019 katika nchi 39. Kasi iliyopatikana wakati wa Miaka Kumi Ya Mavuno iliendelea hadi kipindi kilichofuata. Kufikia mwaka wa 2010, Assemblies of God barani Afrika ilikuwa imeongezeka hadi wafuasi milioni 16.6 waliokuwa wanakutana katika makanisa 67,827.

Mnamo Januari 2010, AAGA ilizindua mpango wa pili wa miaka kumi, unaoitwa "Miaka Kumi Ya Pentekoste" (2010-2020). Kama ilivyokuwa kwa Miaka Kumi Ya Mavuno, mpango huu ulisisitiza upandaji wa makanisa na umisheni. Lengo la ziada lilikuwa kuona washirika milioni 10 wa kanisa wakibatizwa katika Roho Mtakatifu na kuhamasishwa kama mashahidi waliotiwa nguvu na Roho. Kufikia mwisho wa 2019, Assemblies of God barani Afrika iliongezeka hadi wafuasi milioni 18.7 wanaokutana katika makanisa 87,741 eneo la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Bonde la Bahari ya Hindi.

Mnamo Januari 2021, AAGA ilizindua mkazo wa tatu unaoitwa "Miaka Kumi Ya Uamsho." Katika kipindi hiki, kanisa linaendelea na mkazo wake juu ya uinjilisti, ubatizo wa Roho, upandaji kanisa, na umisheni. Kitu cha kipekee katika Miaka Kumi Ya Uamsho ni kwamba Assemblies of God Afrika inalenga Afrika Kaskazini, kwa lengo la kuanzisha harakati za upandaji makanisa zinazowezeshwa na Roho katika eneo hili ambalo hapo awali lilikuwa limepuuzwa.

## MATOKEO YA PENTEKOSTE

Upentekoste umebadilisha sura ya kanisa la Kiafrika kwa njia nyingi. Ukuaji wake umekuwa wa kushangaza. Mnamo mwaka wa 2015, kitabu kinachojulikana kama Encyclopedia ya Utafiti ya Oxford kiliripoti kwamba kulikuwa na Wapentekoste (Wapya) milioni 202 katika Afrika, wakiwa asilimia 35 (%) ya idadi ya Wakristo katika bara na asilimia 17 (%) ya jumla ya wakazi wake. Katika viwango tofauti, karibu kila madhehebu ya Kiafrika yameathiriwa. Makanisa mengi ya kimapokeo yamekubali ishara za nje za Upentekoste kama vile kuimba kwa furaha, ibada ya kujieleza, na maombi ya bidii na msisimko. Wengi

wamekubali hata baadhi ya mambo ya msingi zaidi ya Upentekoste kama vile kuzaliwa mara ya pili, kunena kwa lugha, na huduma katika nguvu na uwezo.

Ukristo wa Kipentekoste pia umegusa utamaduni mpana wa Afrika. Njia moja ambayo wamefanya hivi ni kupitia jambo linalojulikana kama "ukombozi na kuinuliwa." Wakati watu wanapo-okoka na kujitoa kabisa, maisha yao yanabadilishwa, na "wanainuliwa" kutoka katika dhambi na unyonge wao. Matokeo yake, wanakuwa watu bora na wananchi wenye tija zaidi. Wanaanza kutendea familia zao kwa upendo na heshima, na hivyo kutokeza watoto wenye mafanikio zaidi. Zaidi ya hayo, mara nyingi Wakristo waliojiweka wakfu hufuatia elimu ya juu zaidi, kufanya kazi kwa bidii zaidi, kupata kazi bora zaidi, na kutafuta kufuata utimilifu wa kifedha. Mara nyingi hufikiwa na huruma na kuwajali wale wanaotatizika na maisha. Zaidi ya hayo, baadhi ya Wakristo wa Kipentekoste wanapeleka maadili yao katika uwanja wa kisiasa na kuleta mabadiliko huko. Vitendo hivi na vingine vingi vinachangia kuwepo kwa jamii bora. Ingawa si Wakristo wote wa Kipentekoste wanaoishi kulingana na maadili ya Kristo katika jamii, wale wanaojitahidi kufanya hivyo wanaleta matokeo chanya.

## KUELEKEA SIKU ZIJAZO

Kanisa la Kipentekoste la leo barani Afrika liko kwenye njia panda. Linapotafakari maisha yake ya zamani, linaweza kujivunia mafanikio mengi, kama tulivyo-ona katika sura hii. Hata hivyo, jinsi Upentekoste wa Kiafrika unavyokabili siku zijazo, kuna changamoto nyingi zinazoukabili. Tatu kati ya changamoto hizo ni tishio la mafundisho potofu, kudumaa kiroho, na ubinafsi.

Kama itikio, wewe mchungaji wa Kipentekoste ungefanya vyema kujiuliza maswali matatu ya uchunguzi:

- Je, nitaendelea kuwa mwaminifu kwa Maandiko, au nitaliongoza kanisa langu kwenye mafundisho ya makosa?
- Je, nitaliongoza kanisa langu kwenye uamsho halisi wa Kipentekoste, au nitaliruhusu lizame katika hali ya kudumaa kiroho, likiwa na “namna ya utauwa huku wakikana nguvu zake”? (2 Tim. 3:5).
- Je, nitawaongoza watu wangu kutafuta waliopotea katika uwezo wa Roho Mtakatifu, au nitawaongoza katika harakati zisizo na maana, za ubinafsi, za ustawi na baraka za kibinafsi?

Mustakabali wa kanisa la Kipentekoste barani Afrika unategemea sana jinsi wewe na maelfu ya wachungaji wengine wa Kipentekoste mtakavyojibu maswali hayo.

Ikiwa wachungaji wote wa Kipentekoste barani humu watajitolea kwa moyo wote kuwa waaminifu kwa urithi wao wa Kipentekoste na kubaki Wapentekoste wa kweli katika mafundisho, uzoefu, na utendaji, wakati ujao ni mzuri. Lakini, wakiamua kuacha urithi wao na kuwa kama wale walio karibu nao, mustakabali wa Upentekoste barani Afrika uko hatarini. Kwa hiyo ni muhimu kwamba wachungaji wa Kipentekoste kote barani Afrika wafuate kwa bidii mifano ya kiungu ya mababu zao.

Urithi huu wa Kipentekoste ni amana takatifu. Uamsho wa kweli wa Kipentekoste ndio tumaini kuu la mwisho la ulimwengu. Ikiwa zawadi ya Pentekoste inatunzwa na kuchochewa kuwa moto, inaweza kulipuka na kuwa moto mkali, unaoenea kutoka Afrika hadi kwa mataifa ya ulimwengu. Lakini ikiwa imepuuzwa au kutumiwa vibaya, inaweza kupepesuka na kufa. Kwa hiyo, wachungaji wa Kipentekoste kote barani Afrika wanapaswa kuzingatia maneno ya Paulo kwa Timotheo, Mpentekoste mwenzake na mchungaji wa kanisa la Efeso, yafuatayo: "Nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako uliyoipata kwa kuwekewa mikono yangu. " (2 Tim. 1:5). Paulo aliongeza, "Ilinde ile amana nzuri uliyokabidhiwa, ilinde kwa msaada wa Roho Mtakatifu aliyeko ndani yetu" (mst. 14).

Kama wachungaji wa Kipentekoste barani Afrika, sisi pia lazima tuthamini na kuchochea zawadi ya Mungu ambayo imefikishwa kwetu na watangulizi wetu wa Kipentekoste. Na kama wao, lazima tuhifadhi kwa uaminifu kile ambacho tumekabidhiwa na Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu na kututia nguvu.

~ Sehemu ya 4 ~

# Maisha Binafsi ya Mchungaji wa Kipentekoste

## ~ Sura ya 13 ~

# Maisha Yanayosimamiwa Vizuri

Mchungaji mmoja kijana aliketi kwenye meza yake, huku ameshika kichwa chake. Mahitaji ya huduma ya kichungaji yalikuwa yanazidi kuwa mengi kuliko uwezo wake wa kuvumilia. Alikuwa akifikiria kuacha huduma na kurudi kwenye kazi yake ya kuajiriwa. Jambo ambalo mchungaji huyu kijana hakutambua ni kwamba, hakuwa peke yake katika mawazo yake hayo. Kotekote barani Afrika, mamia ya wachungaji wa Kipentekoste wanajikuta katika hali kama hiyo. Wanahisi hawawezi kuendelea kukabiliana na shinikizo nyingi za huduma.

Sababu moja ambayo wachungaji hawa wanahisi kulemewa sana ni kwamba hawajajifunza kusimamia maisha yao vizuri. Wanaishi maisha yasiyosimamiwa vizuri hivi kwamba kila changamoto mpya huwapata bila kutegemewa, na kuwakosesha usawa.

Ingawa ni jambo lisilowezekana kwa mchungaji wa Kipentekoste kufikiri kwamba anaweza kuepuka mashinikizo yote ya maisha na huduma, si jambo lisilowezekana kwao kuamini kwamba wanaweza kukabiliana na changamoto hizi ipasavyo. Sura hii itatoa ushauri wa jinsi wewe, kama mchungaji wa Kipentekoste, unaweza kufikia maisha yenye kusimamiwa vizuri.

## UMUHIMU WA MAISHA YALIYOSIMAMIWA VIZURI

Jina moja la kibiblia la mchungaji ni mwangalizi (1 Tim. 3:1-2). Paulo aliwaagiza wazee wa Efeso, "Jilindeni nafsi zenu, na lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake" (Mdo. 20:28). Kama mwangalizi, mchungaji "anaisimamia nyumba ya Mungu" (Tito 1:7). Basi, mchungaji wa Kipentekoste anabeba jukumu la kusimamia vyema mambo ya kanisa la mahali pamoja. Hata hivyo, kabla yeye hajaweza kusimamia kanisa kwa mafanikio, lazima kwanza aweze kusimamia maisha yake mwenyewe vizuri.

### Maisha Yanayosimamiwa Vizuri

Maisha yenye kusimamiwa vizuri hayana mfadhaiko, wala hayajasongwa na vurugu na machafuko yasiyo ya lazima. Maisha yenye kusimamiwa vizuri yatakupa ujasiri unaohitaji ili uendelee katika huduma. Yatakuruhusu kuwa na tija zaidi - kufanya mengi kwa juhudi ndogo. Na yatakusaidia kukabiliana vyema na dharura za maisha. Hebu tuangalie vipengele vinne vya maisha yanayosimamiwa vizuri:

*1. Kusudi.* Maisha yenye kusimamiwa vizuri ni maisha yenye kusudi lililo wazi na lenye kueleweka. Paulo alitaja kusudi la Mungu kama "mapenzi Yake mema, ya kumpendeza, na makamilifu" (Rum. 12:2). Kadiri unavyoelewa kwa uwazi zaidi kusudi la Mungu kwa maisha yako, ndivyo utakavyokuwa na matokeo zaidi katika kupanga maisha yako kuzunguka kusudi hilo.

Kwa ujumla, wewe, kama mchungaji wa Kipentekoste - kama kila mfuasi mwingine wa Kristo - unaishi ili kumtukuza Mungu na kufanya mapenzi yake. Ingawa unaweza kuukubali ukweli huu, hupaswi kuishia hapa. Ni lazima ujitahidi kujua mapenzi kamili ya Mungu kwa maisha yako. Ni lazima utafute kuelewa kwa nini Mungu amekuweka katika hilo kanisa lako kwa wakati huu. Ni lazima umtafute Mungu katika maombi ukimuuliza, "Bwana, kwa nini umenileta mahali hapa?" Pia, "Unataka nitimize nini hapa kwa ajili ya utukufu Wako?"

*2. Kipaumbele.* Ukishaelewa kwa uwazi kusudi la Mungu la wewe kuwa katika kanisa fulani ulilokoko kwa wakati huo, unaweza kuanza kuunda vipaumbele vyako vya kibinafsi na vya huduma. Vipaumbele vyako ni vile vitu unavyoona kuwa muhimu zaidi. Ni maswala ambayo unazingatia sehemu kubwa ya wakati wako na nguvu. Kristo alizungumza juu ya vipaumbele vya maisha yake aliposema, "Sikushuka kutoka mbinguni ili kufanya mapenzi yangu, bali kuyafanya mapenzi yake aliyenituma" (Yoh. 6:38).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, unaweza kutumia ufahamu wako wa mapenzi ya Mungu kukuongoza katika kufanya huduma yako na maamuzi ya maisha. Unaweza kuuliza hivi kuhusu kila mbadala unaojitokeza na unaowezekana, "Shughuli hii inanisaidiaje kutimiza kusudi la Mungu kwa maisha yangu?" Shughuli yoyote inayoendeleza kusudi la Mungu inapaswa kukumbatiwa. Shughuli yoyote ambayo haiendelezi kusudi la Mungu inapaswa kuepukwa au kukomeshwa.[1]

*3. Uwiano.* Zaidi ya hayo, maisha yaliyosimamiwa vizuri ni maisha yenye uwiano (au mlingano). Maisha yenye mlingano ni yale yanayopanga wakati na nishati inayofaa kwa kila shughuli muhimu ya maisha. Mtu anayejaribu kuvuka kijito akitumia gogo la mti ulioanguka lazima atunze uwiano wake kwa makini. Ikiwa atalalia sana kushoto au kulia, ataanguka ndani ya maji. Ndivyo ilivyo kwa mchungaji wa Kipentekoste. Ikiwa ataweka fikira zake zote kwenye sehemu moja au mbili tu za maisha au huduma, yuko katika hatari ya kukosa uwiano na kushindwa katika sehemu nyingine muhimu.

Kwa mfano, wewe kama mchungaji unaweza kutumia muda mwingi kuwahudumia washirika wa kanisa mpaka ukapuuza familia yako mwenyewe. Au unaweza kujitoa sana kwa maandalizi ya mahubiri kiasi cha kupuuza maombi au kuwafikia waliopotea. Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima ujitahidi kudumisha usawa katika nyanja mbalimbali za maisha, kama vile

- uwiano kati ya unayofanya na jinsi ulivyo,
- uwiano kati ya kazi na mapumziko,
- uwiano kati ya huduma na familia,
- uwiano kati ya kujali wengine na wewe mwenyewe kujijali.

Maneno ya Yesu kwa Mafarisayo yanafaa hapa. Aliwapa changamoto juu ya wao kukazia zaka kupita kiasi, huku wakipuuza mambo mengine muhimu zaidi. Alisema, "Mngefanya hayo ya mwisho bila kuacha yale ya kwanza" (Lk. 11:42).

*4. Mwelekeo.* Mwisho ni kwamba: kwa mchungaji wa Kipentekoste, maisha yanayosimamiwa vizuri ni maisha yanayoongozwa na Roho wa Mungu. Kadiri

[1] Kwa habari zaidi kuhusu vipaumbele vya huduma na vya kibinafsi vya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 5: "Vipaumbele vya Kihuduma," na Sura ya 6: "Vipaumbele vya Kibinafsi."

unavyofuata mwongozo wa Roho Mtakatifu kwa ukaribu zaidi, ndivyo maisha yako yatakavyokuwa yenye mpangilio zaidi.

Paulo aliwatia moyo waamini wa Galatia, kama ifuatavyo: "Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili" (Gal. 5:16). Kisha akaorodhesha "matendo ya mwili" kadhaa. Fikiria jinsi kila moja ya matendo haya yanavyoweza kutajwa kuwa tunda la maisha yasiyosimamiwa vizuri au yasiyo na nidhamu: "uasherati, uchafu na ufisadi; ibada ya sanamu na uchawi; chuki, fitina, wivu, hasira, ubinafsi, fitina, mafarakano na husuda; ulevi, karamu zisizo na kiasi, na mengineyo" (Gal. 5:19-21).

Kwa upande mwingine, kuongozwa na Roho Mtakatifu ni kuishi maisha yaliyo chini ya Mungu. Maisha kama hayo hutafuta kusitawisha "tunda la Roho." Paulo anabainisha tunda hili kuwa "upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi" (Gal. 5:22-23). Fikiria jinsi kila moja ya sifa hizi nzuri inaweza kutajwa kuwa ubora wa maisha yaliyosimamiwa vizuri. Zinazalishwa kwa kubaki ndani ya Kristo (Yoh. 15:5) na kutembea katika Roho (Gal. 5:24-25).

**Mfano Wetu wa Maisha Yanayosimamiwa Vizuri**

Yesu ndiye kielelezo chetu kikamilifu cha mtu aliyeishi maisha yenye kusimamiwa vizuri. Yesu aliishi maisha Yake kwa kuendana na ajenda ya Baba Yake, na Alikwenda sambamba na ratiba ya Baba Yake. Kwa sababu hii, Aliweza kudumu katika kuzingatia utume wake. Ona jinsi maisha ya Yesu yanavyodhihirisha sifa nne zilizotajwa hapo juu za maisha yanayosimamiwa vizuri.

- *Kusudi.* Yesu alijua kusudi lake la kuja, na alidumisha uaminifu kwa utume Wake wa maisha. Ndiyo maana huduma yake ilipokaribia mwisho, aliweza kumwomba Baba yake akisema, "Nimekuletea utukufu duniani kwa kuimaliza kazi uliyonipa niifanye" (Yoh. 17:4).
- *Kipaumbele.* Siku zote Yesu alitanguliza mambo ya kwanza. Kwa mfano, Alitanguliza kudumisha uhusiano thabiti na Baba Yake. Marko aliandika hivi juu yake, "Asubuhi na mapema, kungali giza, Yesu aliamka, akatoka nyumbani, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba" (Mk. 1:35).
- *Uwiano.* Yesu aliishi maisha yenye uwiano kabisa. Alioanisha jinsi alivyo na utendaji Wake, akifanya kazi na kupumzika (Mk. 6:31-32). Kwa kuwa Aliishi maisha yenye uwiano, hakuwahi kuwa na fadhaa wala

hakuwahi kuharakishwa. Siku zote alikuwa mahali sahihi kwa wakati sahihi akifanya jambo sahihi.

- *Mwelekeo.* Yesu aliishi maisha yake chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Alikuwa amejaa Roho (Lk. 4:18-19), na siku zote alifanya kama Roho alivyomwelekeza (Mt. 4:1; Lk. 4:1). Alisema hivi juu yake mwenyewe, “Mwana hawezi kufanya neno peke yake; aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akilifanya, kwa maana yote ayatendayo Baba, Mwana pia ayafanya” (Yoh. 5:19).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima lengo lako liwe kufuata mfano wa Yesu (1 Yoh. 2:6).

### Faida Za Maisha Yanayosimamiwa Vizuri

Ingawa kufikia maisha yenye kusimamiwa vizuri kunahitaji juhudi, kwa mchungaji wa Kipentekoste ni juhudi inayofaa. Mchungaji anayesimamia maisha yake vizuri atapata tija kubwa katika huduma. Kwa sababu wakati wake unasimamiwa vizuri, anaweza kufanya mengi kwa juhudi kidogo.

Zaidi ya hayo, maisha yenye kusimamiwa vizuri huleta amani na utulivu akilini. Usimamizi mzuri wa maisha hupelekea kuwa na utaratibu, na utaratibu hupelekea kuwepo amani. Katika maisha yake yote, Yesu alionyesha utulivu wa akili usiokuwa wa kawaida. Wakati wengine walipohofu, Yeye alibaki mtulivu. Kwa mfano: wanafunzi Wake walipoingia kwenye dhoruba, Yeye alilala kwa amani nyuma ya mashua (Mt. 8:23-27). Mengi kama hayo yalimpata Paulo katika safari yake ya kwenda Rumi (Mdo. 27:27-38).

Maisha yenye kusimamiwa vizuri pia husababisha maisha marefu zaidi katika huduma. Maisha yasiyosimamiwa vizuri husababisha mfadhaiko, na mfadhaiko husababisha uchovu. Lakini maisha yenye kusimamiwa vizuri husababisha amani, ambayo huchangia uvumilivu zaidi katika huduma.

## MAMBO MATATU YA MAISHA YENYE KUSIMAMIWA VIZURI

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uweze kusimamia vyema maeneo matatu ya maisha na huduma, kama ifuatavyo:

### Kusimamia Fedha

Kwanza, lazima ujifunze kusimamia fedha zako binafsi vizuri. Unaweza kuanza mchakato huu kwa kujikumbusha kwamba kila kitu ulicho nacho mwisho wa siku ni mali ya Mungu (Zab. 24:1; 1 Kor. 4:7). Ni lazima utambue kwamba

wewe ni msimamizi tu wa mali ya Mungu, na siku moja utatoa hesabu kwake kuhusu jinsi ulivyoshughulika na fedha zako (Lk. 16:2).

Mpango mzuri wa usimamizi wa fedha ni kugawanya mapato yako katika makundi makubwa matatu: Kwanza, unamtolea Mungu; kisha unaweka kwa ajili ya siku za baadaye; na mwisho, unatumia busara kwa mahitaji ya sasa. Hebu tuangalie kwa karibu zaidi hizo sehemu tatu za usimamizi wa fedha kiungu.

*1. Kwanza, unamtolea Mungu.* Kama mchungaji wa Kipentekoste, kutoa kwa ukarimu ni hatua yako ya kwanza katika kufikia ustawi wa kifedha. Maandiko yanatufahamisha mara kwa mara kwamba malimbuko ya kila kitu tunachopokea ni ya Mungu (ling. Kut. 13:1; 34:26; Law. 2:14; Mit. 3:9). Hivyo, mahali pa kuanzia katika kusimamia fedha zako ni kutoa zaka na sadaka zako kwa Mungu kwa uaminifu. Tena ni vizuri utimize ahadi nyingine zozote za kifedha ulizoweka Kwake au kwa kanisa Lake, kama vile umisheni na ahadi kwa ajili ya ujenzi. Mungu anaahidi kuwabariki kwa wingi wale walio wakarimu kwake (Mal 3:10-11; Lk 6:38).

*2. Kisha, unahifadhi kwa siku zijazo.* Baada ya kumtolea Mungu, ni vizuri uweke akiba kwa ajili ya mahitaji ya siku zijazo na ya dharura. Unaweza kufanya hivyo kwa kuweka kiasi fulani cha pesa kwenye akaunti ya akiba kila wiki. Akaunti hii inapokua, inaweza kutumika kama usalama kwa dharura, na inaweza kuwa chanzo cha pesa kwa ununuzi wa vitu vikubwa.

*3. Mwisho: tumia kwa busara.* Kinachobaki baada ya kumtolea Mungu na kuweka akiba kinaweza kutumiwa kutosheleza mahitaji endelevu ya familia kama vile chakula, nyumba, na mahitaji mengine. Kwa sababu pesa hizi pia ni za Mungu, lazima uzitumie kwa busara. Njia bora ya kufanya hivyo ni kutengeneza bajeti inayoweza kutekelezeka, au mpango wa kifedha. Mpango huu utatumika kama mwongozo wa matumizi, na utasaidia kufanya ununuzi wako kuwa wenye uwiano. Fedha zinazosimamiwa vizuri zitasaidia kuleta amani na utulivu katika nyumba yako. Na zitakusaidia wewe na familia yako kufikia malengo yenu.

### Kutawala Muda

Pili, katika kuishi maisha yanayosimamiwa vizuri, lazima ujifunze kutawala muda wako. Kwa sababu ya athari za kitamaduni, wachungaji wengi wa Kiafrika wanaona usimamizi wa muda kuwa changamoto. Lakini, wakati ni rasilimali ya thamani sana kwa mtu. Ingawa tunaweza kurejesha pesa zilizopotea, hatuwezi

kamwe kurudisha wakati uliopotea. Biblia inatuhimiza kuukomboa wakati kwa kutumia vyema kila fursa (Efe. 5:15-16; Kol. 4:5).

Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, sawa na unavyotakiwa kujifunza kupanga bajeti ya pesa zako, lazima pia ujifunze kupanga wakati wako. Ni lazima ujifunze kutenga muda kwa ajili ya familia, kazi, starehe, kusoma, maombi, kutembelea washirika, na shughuli nyingine muhimu. Jukumu hili litahitaji wewe utengeneze ratiba ya mambo ya kufanya, kupanga shughuli, kuwa na taratibu za kila siku na za kila wiki, na kuepuka kuahirisha mambo.

**Kujijali Mwenyewe**

Tatu, katika kutafuta maisha yenye kusimamiwa vizuri, lazima ujifunze jinsi ya kujijali. Kujijali ni kujitahidi kukidhi mahitaji yetu binafsi ya kiroho, kihisia, na kimwili. Tunafanya hivyo, si kwa sababu za ubinafsi, bali kwa sababu za kiungu. Tunajijali wenyewe ili tuweze kumtumikia Mungu na wengine vizuri zaidi.

Mungu alipowaumba wanadamu, aliwaumba wakiwa na roho, nafsi, na mwili (1 The. 5:23). Roho ni ile sehemu ya mtu yenye mawasiliano na Mungu. Nafsi ni sehemu inayofikiri, kuhisi na kuchagua. Mwili ni sehemu muhimu katika mwanadamu. Ni nyumba ambayo nafsi na roho zetu hukaa. Kujitunza kunahusisha kujali hizo zote tatu.

Unaweza kutunza roho na nafsi yako kwa kufanya matendo ya kiroho ya kutafakari Neno, ibada, maombi, na kufunga.2 Zaidi ya hayo, lazima uendelee kutoa mawazo, hisia, na mapenzi yako na kukubali kwamba Kristo ni Bwana. Biblia inatuagiza hivi: “Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuyajaribu na kuyathibitisha mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu” (Rum. 12:2). Biblia inatufundisha zaidi jinsi tunavyopaswa kudhibiti maisha yetu ya mawazo:

> “Mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo sawa, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye kupendeza, ikiwa ni kitu kilicho bora au cho chote chenye kustahili sifa—yatafakarini hayo.” (Flp. 4:8)

Kutunza miili yetu ni muhimu kwa sababu miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Kwa hiyo tunapaswa kumheshimu Mungu kwa miili yetu (1 Kor. 6:19-20). Mwili wenye afya hutuwezesha kutimiza vyema wito wa Mungu maishani mwetu. Hutuwezesha sisi kuishi maisha kwa ukamilifu (Yoh. 10:10). Kwa hiyo,

tunapaswa kuijali miili yetu kwa kula vizuri, kuwa na kawaida ya kufanya mazoezi, kulala vya kutosha, na kufanyiwa uchunguzi wa kiafya mara kwa mara.

## KUTAFUTA MAISHA YENYE KUSIMAMIWA VIZURI

Huenda unauliza, “Ninawezaje, kama mchungaji wa Kipentekoste, kutafuta maisha yenye kusimamiwa vizuri?”

### Amua

Unaanza safari yako ya kupata maisha yenye kusimamiwa vizuri kwa uamuzi. Yesu alisimulia hadithi ya Mwana Mpotevu. Katika hadithi hii, mwana mpotevu alidai sehemu ya urithi kutoka kwa baba yake, na kuondoka nyumbani. Punde, kwa sababu ya maisha yake ya anasa na starehe, kijana huyo alijikuta shambani akilisha nguruwe. Hapo alirudiwa na fahamu zake na kusema hivi moyoni mwake: “Nitaondoka na kurudi kwa baba yangu na kumwambia: ‘Baba, nimekosa juu ya mbingu na wewe mwenyewe. Sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako’ ” (Lk. 15:18-19). Kwa uamuzi huo, aliamka na kuanza safari ya kurudi nyumbani.

Ni sawa na kutafuta maisha yenye kusimamiwa vizuri. Safari yako ya maisha yenye tija zaidi lazima ianze kwa uamuzi thabiti. Ni lazima uangalie hali yako ya sasa na utambue kwamba kuna njia bora ya kuishi na kuhudumu. Kisha unapaswa kujiambia, "Nitasimama na kufuata mtindo wa maisha wenye matokeo zaidi."

### Tengeneza Mpango

Ingawa uamuzi wa kufuata maisha yenye kusimamiwa vizuri ni muhimu, hautoshi. Uamuzi wako lazima ufuatwe na mpango unaotekelezeka. Mpango huu utahusisha hatua tatu, kama ifuatavyo:

*1. Kujitathmini.* Unaanza safari yako ya maisha yenye kusimamiwa vizuri kwa kujitathmini. Katika tathmini hii ya kibinafsi, utachunguza mtindo wako wa maisha wa sasa ili kubaini ni wapi unahitaji kuboreshwa. Unaweza kufanya hivyo kwa kujibu kwa uaminifu maswali kama haya:

- Je, ninafanya vizuri kiasi gani katika kusimamia fedha zangu?
- Je, ninafanya vyema kiasi gani katika kusimamia muda wangu?
- Je, ninafanya vizuri kiasi gani katika kutunza roho, nafsi, na mwili wangu?
- Ninawezaje kufanya vizuri zaidi katika kila moja ya maeneo haya?

Jibu maswali haya kwa uangalifu, na uandike majibu yako kwenye daftari.

*2. Kuweka malengo.* Mara tu unapogundua maeneo ambayo unahitaji uboreshaji, weka malengo yako ya kibinafsi ya maendeleo. Unaweza kufanya hivyo kwa kuuliza na kujibu kwa uangalifu maswali yafuatayo:

- Ninataka kuboresha ujuzi wangu wa kusimamia fedha kwa kiasi gani?
- Ningependa kuboresha ujuzi wangu wa usimamizi wa wakati kwa njia gani?
- Ningependa kuboresha ujuzi wangu katika kutunza roho, nafsi, na mwili wangu kwa njia gani?

Hapa tena, andika majibu yako kwenye daftari lako. Andika kitu halisi.

*3. Kutengeneza mpango.* Mara baada ya kuweka malengo yako, ni vizuri kutengeneza mpango wa kufikia malengo haya. Zingatia suala moja au mawili tu kwa wakati mmoja, na utengeneze mpango wa kufikia kila lengo. Katika mpango wako, utataka kutambulisha hatua mahususi unazoweza kuchukua ili kufikia malengo yako. Kwa mfano, unaweza kutaka kuboresha ujuzi wako wa kifedha kwa kuendeleza na kufuata bajeti ya familia. Au, unaweza kutaka kuboresha ujuzi wako wa kudhibiti muda kwa kutengeneza orodha ya mambo ya kufanya kila asubuhi, na kisha kutumia orodha hii kuongoza shughuli zako za siku.

**Ingiza Kwenye Matendo**

Baada ya kutengeneza mpango wako, lazima uchukue hatua. Lazima uanze kutekeleza mpango wako. Kuwa na subira; shikamana na mpango wako. Kisha, mwishoni mwa miezi mitatu hadi sita, tathmini maendeleo yako. Tambua ni wapi umefanya vizuri na wapi hujafanya vizuri. Kisha, rekebisha mpango na kurudia mchakato. Unaweza kutaka kuendelea kufanyia kazi malengo yale yale, au unaweza kuchagua kufanyia kazi malengo mengine.

---

Kufikia maisha yaliyosimamiwa vizuri ni mchakato unaodumu maisha yako yote. Ni lengo linalostahili kufuatwa, na litaleta baraka nyingi katika maisha ya mchungaji wa Kipentekoste.

# ~ Sura ya 14 ~

# Mahusiano Mazuri Yanayofaa

Mtaalamu wa Sheria ya Musa alimwendea Yesu na kumuuliza swali. Akauliza, "Mwalimu, ni amri ipi iliyo kuu katika Torati?" Bila kusita, Yesu akamjibu, " 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili yako yote. Hii ndiyo amri kuu na ya kwanza. Na ya pili inafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako' " (Mt. 22:36-39). Hivyo, kulingana na Yesu, mahusiano ndiyo kiini cha maana ya kumtumikia Mungu.

Ukristo ni zaidi ya dini; ni uhusiano wa kibinafsi na Mungu kupitia Yesu Kristo. Si suala la kushikilia tu imani fulani au kufuata taratibu fulani. Ni suala la kumpenda Mungu na wengine. Hili jambo la uhusiano wa upendo na Mungu na watu hutofautisha Ukristo na dini zingine.

Huduma ya kichungaji lazima ifanyike kwa karibu. Kama isivyowezekana kwa mchungaji kuchunga kondoo wake akiwa mbali, mchungaji wa Kipentekoste naye hawezi kutunza watu wake akiwa mbali. Ili kufanikiwa katika huduma, mchungaji wa Kipentekoste lazima aelewe umuhimu wa kujenga mahusiano imara na yenye afya. Na lazima ajue jinsi mahusiano hayo yanavyoendelezwa na kudumishwa.

## KUELEWA MAHUSIANO

Mahusiano ni miunganiko baina yetu. Ni jinsi tunavyohusiana sisi kwa sisi. Uhusiano unaweza kuwa wa karibu au wa mbali, wenye nguvu au dhaifu, wa kina au wa juu juu, wenye afya au wenye uharibifu. Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujue jinsi ya kujenga uhusiano mzuri na wanafamilia, washirika wa kanisa, marafiki, na wachungaji wengine. Na lazima uweze kuwafundisha wengine kufanya vivyo hivyo.

Mahusiano yenye afya huwaruhusu watu wa Mungu kuishi pamoja kwa maelewano. Hubariki watu na kuwajenga. Huwasaidia kujisikia salama, kuheshimiwa, na kukubalika. Mahusiano yenye afya pia huwaleta watu wa Mungu pamoja katika shughuli yenye matokeo. Husababisha kanisa kustawi na kuwa na nguvu. Kwa upande mwingine, mahusiano yasiyofaa husababisha watu kuingia katika mabishano na chuki. Mahusiano kama haya husababisha kanisa kuwa dhaifu na kutofanya kazi.

Kwa hiyo, Paulo aliwahimiza Wakristo wa kwanza wasitawishe uhusiano mzuri kati yao. Aliwaandikia Wakristo wa Efeso hivi: “Fanyeni bidii kuuhifadhi umoja wa Roho kupitia kifungo cha amani” (Efe. 4:3). Aliwashauri waamini huko Rumi, “Ishini kwa umoja ninyi kwa ninyi. Msiwe na kiburi, bali iweni tayari kushirikiana na watu wa hali ya chini” (Rum. 12:16). Paulo alielewa kwamba mahusiano mazuri yanaunda msingi wa huduma yenye ufanisi ndani na nje ya kusanyiko.

## AINA ZA MAHUSIANO

Kama mchungaji wa Kipentekoste, ni muhimu kuwa na ufahamu wa aina mbalimbali, au viwango, vya mahusiano unayokutana nayo maishani. Uelewa huu utakusaidia kuamua vyema mahusiano yapi unapaswa kuwekeza kwa uzito zaidi.

### Uhusiano wa Msingi

Uhusiano wako muhimu zaidi maishani ni uhusiano wako na Mungu. Mahusiano mengine yote lazima yajengwe kwenye uhusiano huu wa msingi. Kwa hiyo ni lazima utangulize uhusiano wako na Mungu. Ikiwa uhusiano huu utakuwa sawa, mahusiano mengine yote yatafuata. Kinyume chake pia ni kweli, kwamba ukiharibu au kuboronga kwenye uhusiano huu, mahusiano mengine yote yataathiriwa vibaya.

Uhusiano wako na Mungu lazima uwe wa upendo wa kina (Mt. 22:37). Upendo huu kwa Mungu utajidhihirisha katika utii wa kujitoa kwa amri Zake (Yoh. 14:15, 21) na kwa kuwajali wengine kwa upendo (Yoh. 15:12).

**Mahusiano ya Familia**

Uhusiano mwingine muhimu baada ya uhusiano wako na Mungu ni uhusiano wako na mwenzi wako. Biblia inasema kwamba Mungu amewafanya mume na mke kuwa mwili mmoja (Mwanzo 2:24). Kwa hiyo ni lazima mume ampende mke wake kama anavyoupenda mwili wake mwenyewe, kama Kristo anavyolipenda kanisa. Na mke lazima amheshimu mumewe na kunyenyekea chini ya mamlaka yake nyumbani (Efe. 5:21-33). Kwa hiyo wewe na mwenzi wako lazima mthamini uhusiano huu kuliko mahusiano mengine yote ya kibinadamu. Na lazima uwekeze muda wa kutosha na juhudi katika kuimarisha uhusiano huu.

Uhusiano wa tatu ulio muhimu sana ni ule baina yako na watoto wako. Ni lazima uwapende watoto wako sana, na lazima uwalee kwa upole na vizuri. Biblia inasema kwamba wazazi wanapaswa kuwalea watoto wao katika mafundisho ya Bwana (Efe. 6:4). Kwa hivyo, hupaswi kamwe kupuuza watoto wako - hata katika kutekeleza majukumu yako ya kichungaji. Badala yake, ni vizuri utenge wakati ili kuunda urafiki na kila mmoja wao. Hii itazalisha hali ya urafiki wa upendo ndani ya nyumba. Mazingira haya yatakuruhusu kuendelea na kazi yako kwa amani, na itaongeza tija yako katika huduma. Pia itatumika kama ushuhuda kwa kanisa na jamii. Muhimu zaidi: lazima utafute kuwaongoza watoto wako kuingia katika uhusiano wa kibinafsi na Kristo. Na lazima uhakikishe kwamba kila mtoto amejazwa na Roho Mtakatifu.

Kwa kuongezea, lazima ukuze uhusiano wenye upendo kwa ukoo wenu. Unapaswa kuonyesha upendo na heshima ifaayo ya Kikristo kwa wazazi wako, ndugu na dada zako, binamu zako, na wanafamilia wengine. Lakini, weka weka vitu vyote katika utaratibu stahiki. Haupaswi kamwe kupendelea wanaukoo wako kuliko mwenzi wako na watoto wako. Paulo alimwandikia Timotheo, “Yeyote asiyewatunza watu wa jamaa yake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini” (1 Tim. 5:8).[1]

[1] Kwa habari zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 7: “Vipaumbele vya Familia.”

**Mahusiano ya Kihuduma**

Pamoja na mahusiano yako na Mungu na wanafamilia yako, kama mchungaji wa Kipentekoste lazima utunze vizuri na kukuza kwa makini mahusiano yako ya kihuduma. Mahusiano haya yanawahusisha wale unaowahudumia na wale unaohudumu nao. Hujumuisha washirika wa kanisa lako, jamii yako, na dhehebu lako au kanisa la kitaifa. Kila moja ya mahusiano haya ni ya kipekee, na kila uhusiano unapaswa kushughulikiwa kitofauti kidogo. Kufanikiwa kwako au kutofanikiwa kwako katika huduma kwa sehemu kubwa kutategemea jinsi unavyoendesha na kusimamia mahusiano haya.

Zaidi ya hayo utahitaji kujenga uhusiano thabiti wa kibinafsi na kitaaluma na wachungaji na walei wa kanisa lako. Yesu alipowachagua mitume kumi na wawili, aliwatuma kuhubiri na kutoa pepo. Lakini kwanza, aliwaita wakae pamoja Naye (Mk. 3:13-15). Bwana wetu alijua kwamba kiunganisho atakachojenga pamoja nao kwa kuwa pamoja kingetumika kama msingi wa huduma yao wakiwa mbali. Ndivyo ilivyo kwa kanisa unaloliongoza. Jinsi utakavyohusiana na watenda kazi wako katika huduma na walei utakuwa ndiyo msingi wa huduma zote katika kanisa la mahali pamoja.[2]

**Mahusiano Matatu Yenye Hatari**

Kuna mahusiano yanayoambatana na hatari kiasi fulani. Matatu kati ya hayo ni uhusiano wako na dunia, uhusiano wako na watu wa jinsia tofauti, na chaguo lako la marafiki wa karibu. Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima upitie kila moja ya mahusiano haya kwa uangalifu sana.

*1. Uhusiano na dunia.* Lazima uwe macho katika uhusiano wako na dunia. Dunia ina mifumo mingi inayotawaliwa na Shetani na wenye kumtumikia (1 Yoh. 5:19). Yesu aliwaambia wanafunzi wake hivi, “Ninyi si wa ulimwengu, ila mimi nimewachagua ninyi kutoka ulimwenguni” (Yoh. 15:19). Biblia inaeleza kwamba, ingawa mfuasi wa Kristo ni lazima aishi duniani, hapaswi kujihusisha na mambo yake (1 Kor. 7:31). Asiweke mapenzi yake na moyo katika mambo ya dunia (1 Yoh. 2:15). Wala asifananishe maisha yake na njia za dunia (Rum. 12:2).

*2. Uhusiano na watu wa jinsia nyingine*. Tena, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uangalie sana uhusiano wako na watu wa jinsia nyingine.

---

[2] Kwa habari zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 5: “Vipaumbele vya Kihuduma.”

Wachungaji wengine hawakuweka mipaka kwenye uhusiano huu na kupelekea kuanguka katika fedheha na kuleta aibu kwa kazi ya Mungu. Paulo alimwonya Timotheo hivi, "Zikimbie tamaa mbaya za ujanani, ukafuate uadilifu" (2 Tim. 2:22). Alizidi kumuasa mwanae katika imani hivi: "[Watendee] wanawake wazee kama mama zako, na wanawake vijana kama dada zako, kwa usafi kabisa" (1 Tim. 5:2).

Ni lazima uhusiane na watu wa jinsia tofauti kwa heshima kubwa na staha. Kamwe hupaswi kuwa peke yako na mtu wa jinsia tofauti, isipokuwa mkeo (au mumeo). Linda pia mawazo na fikra zako. Kila tendo la zinaa huanza katika mawazo ya mtu. Kwa hiyo, usiruhusu kamwe mawazo yako yaondoke kwa mwenzi wako na kuelekea kwa mtu mwingine (Mt. 5:28). Biblia inaonya hivi: "Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo, kwa maana kila ufanyalo hutoka ndani yake" (Mit. 4:23).

*3. Marafiki unaochagua*. Jinsi mtu anavyochagua rafiki zake huweza kuleta baraka kubwa au madhara makubwa katika maisha yake. Basi, tumia hekima katika kuchagua marafiki zako. Biblia inatuambia, "Wenye haki huchagua rafiki zao kwa uangalifu, bali njia ya waovu huwapotosha" (Mit. 12:26). Paulo anaongeza, "Msidanganyike: Marafiki wabaya huharibu tabia njema" (1 Kor. 15:33). Ukiwa mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kutengeneza urafiki wenye nguvu na wale tu ambao watakuhimiza umkaribie Mungu na kuishi maisha yanayompendeza.

## SIFA ZA MAHUSIANO YANAYOFAA

Waafrika wanatambua kuwa ubora wa maisha ya mtu hutegemea kwa kiasi kikubwa ubora wa mahusiano yake. Je, nini vigezo vichache ambavyo mchungaji wa Kipentekoste anaweza kutumia ili kumwongoza kujenga na kudumisha mahusiano mazuri katika familia, kanisa na jamii? Kama mchungaji wa Kipentekoste, uhusiano wako unapaswa kuonyesha sifa tano zifuatazo:

### Upendo

Sifa ya kwanza ambayo lazima iwepo katika uhusiano wako na wengine ni upendo wa kujitoa. Ni lazima umpende mwenzi wako, watoto wako, na watu wa Mungu sawa na Kristo anavyokupenda wewe. Yesu aliwaamuru wanafunzi wake kwa kusema, "Kama vile nilivyowapenda ninyi, pendaneni vivyo hivyo" (Yoh. 13:34). Alikuwa akiwaambia kwamba upendo usio na ubinafsi lazima utawale uhusiano wao na wengine. Yesu alikuwa tayari kuutoa uhai wake kwa ajili yao.

Basi nao inabidi wawe tayari kutoa maisha yao kwa ajili ya wengine (Yoh. 15:12-13). Hivyo Petro anatuhimiza, “Mpendane kwa dhati, kutoka moyoni” (1 Pet. 1:22).

**Mawasiliano Yaliyo Wazi**

Tabia ya pili yenye kuonyesha uhusiano wako na wengine ni mawasiliano wazi, na ya dhati. Paulo aliwashauri Wakristo wa Efeso waseme kweli katika upendo. Hiyo ingepelekea ukuaji na kukomaa kama mwili wa Kristo (Efe. 4:15). Tena, aliwaonya waamini wa Kolosai kama ifuatavyo: “Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi ya kumjibu kila mtu” (Kol. 4:6).

Ukiwa mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kupima kwa uangalifu maneno yako kabla ya kusema, ukikumbuka yasemavyo Maandiko: “Walindao midomo huhifadhi maisha yao, bali wao wanenao bila kufikiri wataangamia” (Mithali 13:3). Mawasiliano yako na wengine yanapaswa yaonyeshe urafiki, kujiamini, na unyofu. Maneno yako yanapaswa kuwa ya wazi bila kuwa mkali, na uaminifu bila kuwa mbaya. Na lazima ujifunze kusikiliza kwa karibu kile kinachosemwa na wengine. Biblia inashauri kwamba, “Kujibu kabla ya kusikiliza — ni upumbavu na aibu” (Mit. 18:13).

**Kuaminiana Pande Zote**

Sifa ya tatu ambayo inapaswa kuonyesha uhusiano wako na familia yako na hata washirika wa kanisani mwako ni kuaminiana kwa kila upande husika. Tendo hilo ni imani watu waliyo nao baina yao, au wao kwa wao. Ni wote kuamini kwamba kila anayehusika katika uhusiano husika atakuwa mkweli, na kwamba amejitolea kuujenga uhusiano huo. Ili hali ya kuaminiana iwepo, wahusika wote katika uhusiano lazima waonyeshe kujitoa kila mmoja kwa mwingine.

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uhakikishe kuwa unatumainika na watu. Watu lazima wajisikie salama karibu na mchungaji wao. Ni lazima wajisikie salama kumweleza siri zao za ndani kabisa. Na lazima wajue kwamba mchungaji wao hatamwambia mtu mwingine hizo siri.

**Heshima**

Sifa ya nne inayotakiwa kuwepo katika uhusiano wako na wengine ni kuheshimiana. Heshima ni mtazamo wa hali ya juu na kujali ambako mtu anakuwa nao kuhusu hisia, haki, na utu wa wengine. Petro aliwahimiza Wakristo,

"Onyesheni heshima ifaayo kwa kila mtu" (1 Pet. 2:17). Wake wanapaswa kuwaheshimu waume zao na waume wanapaswa kuwaheshimu wake zao. Watoto wanapaswa kuwaheshimu wazazi wao, na wazazi wanapaswa kuwaheshimu watoto wao. Washirika wa kanisa wanapaswa kumheshimu mchungaji wao, na mchungaji wao lazima awaheshimu.

Kwa sababu watu wote wana sura ya Muumba wao, lazima kumthamini kila mtu bila kujali rangi, kabila, au hadhi yake kijamii. Paulo aliwahimiza Wakristo wa Rumi kama ifuatavyo: "jitoleeni na kuheshimiana ninyi kwa ninyi" na tena, "kila mmoja amheshimu mwingine kuliko yeye mwenyewe" (Rum. 12:10). Akazidi kusema hivi: "Ishini kwa amani ninyi kwa ninyi. Msijivune, bali muwe tayari kushirikiana na watu wa hali ya chini. Msijiinue" (mst. 16).

**Unyenyekevu**

Hatimaye, uhusiano wako na wengine unapaswa kuonyeshwa kwa unyenyekevu. Unyenyekevu ni kinyume cha kiburi na kujionyesha. Ni kuwa huru na majivuno na kujiona. Unyenyekevu ni uwezo wa mtu kujiona kama Mungu anavyomwona. Yaani, mtu mnyenyekevu anaweza kujiona jinsi alivyo. Unyenyekevu ni udhihirisho wa upendo wa kweli. Paulo aliandika, "Upendo… haujisifu, haujivuni. hauwavunji wengine heshima, hautafuti mambo yake binafsi" (1 Kor. 13:4-5).

Kiburi hufunga mlango wa mahusiano ya ndani sana, yenye maana na ya kudumu. Unyenyekevu hufungua hiyo milango kwa upana (Rum. 12:16). Kama mchungaji mnyenyekevu, utakuwa mtu wa watu. Utafikiwa. Badala ya kujenga kuta kati yako na watu, utajenga madaraja.

## KUDUMISHA MAHUSIANO MAZURI YANAYOFAA

Yafuatayo ni mazoea matatu ambayo yatakusaidia kujenga na kudumisha mahusiano mazuri yanayofaa, yanayomletea Mungu heshima, pamoja na wengine:

**Kusudia**

Kwanza, lazima ukusudie kujenga na kudumisha uhusiano mzuri na wanafamilia wako, washirika wa kanisa, na wenzako katika huduma. Chukua hatua na utafute mahusiano haya kikamilifu. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya. Alichagua kutembea kati ya watu. Alichukua muda kuwasikiliza na kusikia kilio chao. Maadui zake waliona hili, na wakamshtaki kuwa "rafiki wa watoza ushuru na wenye dhambi" (Mt. 11:19). Kama mchungaji wa Kipentekoste, ni lazima

ujitahidi kuwa kama Yesu na kutafuta kwa bidii kujenga mahusiano imara na wengine.

**Kuza Mahusiano**

Zaidi ya hayo, lazima ufanye bidii ili kukuza uhusiano mzuri. Ni lazima uwe tayari kuwekeza muda na juhudi zinazohitajika ili kujenga vifungo imara vya kudumu na familia yako, washirika wa kanisa lako, na wenzako katika huduma. Ili kufanya hivyo, utahitaji kutumia muda pamoja nao, kusikiliza habari wanazosimulia, kucheka na vichekesho vyao, na kulia kuhusu maumivu ya moyo na kushindwa kwao (Rum. 12:15). Ikiwa utafanya hivyo, baada ya muda, kufungamana kwa nguvu kutokana na upendo kutakuwepo kati yako na watu wako.

**Samehe**

Pia, kama unataka kujenga na kudumisha uhusiano thabiti na wa kudumu na wengine, lazima ujifunze kuomba msamaha na kuutoa pia. Huwezi kuepuka kuudhi watu na watu kukuudhi wewe. Kutokuelewana kutatokea na kutakuwa na wewe kuumizwa kihisia, na hata wewe utaumiza. Ili mahusiano yahifadhiwe, msamaha ni lazima.

Msamaha una pande mbili. Upande mmoja ni wa yule anayeomba msamaha, aliyekosea. Upande wa pili ni wa yule aliyekosewa, kutoa msamaha. Lazima uwe tayari kufanya yote mawili (Mt. 5:22-26). Lazima uwe mwepesi wa kuomba msamaha pale unapokosea. Na lazima uwe tayari kutoa msamaha pale mtu anapokuomba. Msamaha huwaweka huru mkosaji na aliyekosewa. Hufungua mlango wa upatanisho na kufanya njia ya mahusiano yaliyovunjika kurekebishwa.

---

Huduma yenye ufanisi imejengwa juu ya mahusiano imara na yenye afya. Mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima atawekeza sana katika kujenga mahusiano haya.

## ~ Sura ya 15 ~

# Tabia Imara ya Ibada Binafsi

Nayahesabu yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu Bwana wangu" (Flp. 3:8). Haya ni maneno ya mtume Paulo. Huyu anaaminika kuwa mishenari mkuu zaidi aliyepata kuishi, baada ya Yesu. Alihubiri kwa nguvu, akafanya miujiza, na akapanda makanisa katika Dola yote ya Rumi. Mungu alimtumia kufungua mlango wa wokovu kwa Wasiokuwa Wayahudi (Mdo. 14:27). Hata hivyo, katika hayo yote, alihisi kwamba mafanikio Yake makubwa zaidi maishani yalikuwa ni kumjua Yesu tu. Ombi lake la kudumu lilikuwa, "Nataka kumjua Kristo" (Flp. 3:10).

Kama Paulo, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste ni kiongozi. Kwa hivyo, una majukumu mengi. Umeitwa kuwalea na kuwakuza waamini wawe wanafunzi na kuendeleza ufalme wa Mungu duniani. Vyote hivyo ni kazi kubwa, na lazima uzitekeleze kwa uaminifu. Hata hivyo, kama unataka kwenda mbali katika huduma, kama Paulo, lazima utangulize uhusiano wako na Kristo. Ni lazima ujitoe kumjua Kristo na kujifunza daima kuishi katika ushirika pamoja Naye.

Ili kufanya hivyo, utahitaji kuendeleza tabia imara ya ibada binafsi. Hakuna kiasi chochote cha kazi, bidii au ufanisi, kitakachofidia ukosefu wa ushirika na

Bwana. Sura hii itashughulikia tabia ya kuabudu kibinafsi ya mchungaji wa Kipentekoste.

## TABIA YA IBADA BINAFSI

Tutaanza uchunguzi wetu wa tabia ya ibada binafsi kwa ufafanuzi kidogo.

### Kuelewa Maana Yake

Tabia ni kitu ambacho mtu hufanya mara kwa mara. Ni kitu kinachojirudia, ambacho ni kama kawaida. Kama mtu anayepiga mswaki kila asubuhi, mazoea husitawishwa kwa kurudia-rudia kitu. Mwanzoni, mtu anapaswa kujikumbusha mwenyewe haja ya kufanya shughuli hiyo. Na wakati mwingine anapaswa kujisukuma kufanya hivyo. Ila baada ya muda, shughuli hiyo inakuwa kitu cha kawaida.

Tabia ya ibada binafsi ni nini? Tabia ya ibada binafsi ni desturi ya Kikristo ya kutumia muda kila siku wa kushirikiana na Kristo. Ni muda ambao mtumishi mwaminifu wa Kristo hutenga kila siku ili kukuza uhusiano wake na Mungu. Ni tabia kwa sababu, baada ya muda, inakuwa kawaida ya maisha. Ni ibada kwa sababu kusudi lake ni kukuza uhusiano wa mtu na Mungu na kuongeza kujitoa kwake na kwa utume Wake.

### Faida Za Ibada Binafsi

Ukikuza na kudumisha kwa uaminifu tabia ya ibada binafsi, faida nyingi zitakuja katika maisha yako na huduma. Hebu tuangalie faida nne kati ya hizo.

*1. Kumjua Kristo.* Faida ya kwanza ni kwamba itakufanya ukue katika uhusiano wako na Kristo. Mwandishi wa Waebrania anatuhimiza, “Tumkaribie Mungu kwa unyofu wa moyo” (Ebr. 10:22). Yakobo anaongezea: “Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi” (Yakobo 4:8). Unapoomba na kutafakari Maandiko, utaingia Patakatifu pa Patakatifu (Ebr. 10:19). Hapo katika uwepo wa Mungu, wewe kama Musa wa kale, utajikuta ukiwasiliana na Mungu “uso kwa uso, kama mtu asemavyo na rafiki” (Kut. 33:11).

*2. Kutambua mapenzi ya Mungu.* Faida ya pili ni kwamba utakuja kuelewa vyema mapenzi ya Mungu kwa maisha yako. Unaposali, kusoma Neno la Mungu, na kutumia mafundisho yake maishani mwako, akili yako itabadilika. Hili likitokea, “utaweza kupima na kuthibitisha mapenzi ya Mungu ni nini—mapenzi yake mema, ya kumpendeza na ukamilifu” (Rum. 12:2).

*3. Kukuza uelewa wa kibiblia kuhusu dunia.* Faida ya tatu ni kwamba zoezi hilo litakusaidia kukuza mtazamo wa Kibiblia kuhusu dunia. Unapochunguza Maandiko kwa maombi, utaanza kuuona ulimwengu jinsi Mungu anavyouona. Utaanza kuelewa mpango Wake kwa wanadamu. Na utaweza kutambua nafasi yako katika kutimiza mpango huo.

*4. Kuenenda sambamba na Roho.* Faida ya nne ni kwamba utajifunza kuishi katika ushirika wa karibu na Roho Mtakatifu (2 Kor. 13:14). Paulo aliwahimiza Wakristo “kuenenda katika Roho” (Gal. 5:25). Alizidi kuwashauri hivi: “Endeleeni kujazwa Roho Mtakatifu” (Tafsiri halisi ya Waefeso 5:18). Katika mazingira ya ibada, Roho Mtakatifu atajulisha nguvu na uwepo wake. Ni kama umeme unaotoka kwenye chnzo hadi kwenye taa. Mradi waya imeunganishwa kwenye kishikio cha taa, balbu hutoa mwanga. Lakini kukitokea kizuizi chochote, umeme huacha kupita na taa inaacha kutoa nuru. Kupitia tabia ya uaminifu ya ibada binafsi, utadumu ukiwa umeunganishwa kwenye chanzo cha umeme. Unaweza kudumu ukiwa umejaa Roho wa Mungu.

## VIPAUMBELE NA MAMBO YA KUFANYA KATIKA IBADA BINAFSI

Maswali mawili yanazuka: “Je, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unawezaje kusitawisha mazoea ya ibada binafsi?” Na pia, “Unapaswa kufanya nini ili kufaidika zaidi na zoezi hilo?”

### Mambo Matatu Muhimu

Ili kuanzisha tabia hii imara ya ibada binafsi, utahitaji kushughulikia masuala matatu yanayohusiana:

*1. Vipaumbele.* Hatua yako ya kwanza katika kuunda tabia ya ibada ni kuamua vipaumbele vyako. Kipaumbele ni kitu ambacho mtu huona kuwa muhimu zaidi. Ni jambo ambalo yeye hufanya kwanza. Ni lazima uamue kwamba uhusiano wako na Mungu ndio jambo kuu. Na lazima uone tabia hii ya ibada ni njia ya kuimarisha uhusiano huo. Ili kufanya hivyo, utahitaji kujilinda dhidi ya kile kinachoitwa "uvamizi wa dharura." Yaani, usiruhusu shughuli nyingi za haraka za maisha zizuie mazoea hayo yaliyo muhimu zaidi.

Kama mchungaji mwenye shughuli nyingi, unakutana na mahitaji mengi ya dharura kila siku, majukumu ambayo yanadai wakati wako mara kwa mara. Ingawa huwezi kuyapuuza, inakubidi ujifunze kuyaweka katika mpangilio

unaofaa. Unapaswa kulinda uhusiano wako na Mungu. Na ni vizuri uhusiano huo uwe wa kwanza kwenye orodha yako ya vipaumbele. Hivyo ndivyo Yesu alivyofanya. Hakuruhusu majukumu Yake mengi kumzuia kuwa na ushirika na Baba Yake wa Mbinguni. Biblia inatuambia kwamba "mara nyingi aliondoka akaenda mahali pasipokuwa na watu na kusali" (Lk. 5:16). Alitambua kwamba alihitaji huo muda wa kuwa peke yake na Baba Yake ili kutegemezwa katika huduma.

Kisa cha Mariamu na Martha kinaonyesha zaidi jambo hili. Mariamu alitanguliza kuketi miguuni pa Yesu na kumsikiliza akifundisha. Lakini Martha alikengeushwa na kazi yote iliyohitaji kufanywa. Yesu alimwambia Martha, "Wewe unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya mambo mengi, lakini yanahitajika machache — au moja tu. Mariamu amechagua lililo bora zaidi, wala halitaondolewa kwake" (Lk. 10:41-42). Martha alikuwa amekengeushwa na haraka kumvamia. Lakini Mariamu alikuwa ametanguliza jambo bora zaidi, yaani ushirika na Bwana. Kila mchungaji wa Kipentekoste lazima ajifunze kufanya vivyo hivyo.

Unaweza kujaribiwa kusema, "Siwezi kusoma Biblia na kuomba leo. Nina mambo mengi na ya haraka sana ya kufanya." Ila, kama unasema hivi leo, na kesho, na siku inayofuata, utajikuta umetumbukia katika mfumo ambao huwezi kuuepuka kirahisi. Lakini ikiwa utaona wakati wako wa ibada ya kila siku kuwa sawa na miadi yako na Mungu, na kama utatimiza hilo kwa uaminifu, njaa yako ya kutaka kuwa na Mungu itakua na kuongezeka. Utakuwa unausogelea wakati wako wa ibada kwa furaha.

*2. Kusimamia muda.* Suala la pili ambalo mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kulifanya kwa habari ya kukuza tabia ya ibada binafsi ni usimamizi wa wakati. Kusimamia wakati ni utaratibu wa kupanga ratiba ya kila siku ili kuhakikisha kwamba muda sahihi umetengwa kwa ajili ya kila shughuli ya siku. Wachungaji wenye ufanisi wanaelewa kwamba muda ni zawadi kutoka kwa Mungu, na wanapaswa kuusimamia vizuri. Katika kupanga siku yako, lazima uhakikishe kuwa unatenga wakati wa kutosha kwa ajili ya ibada binafsi.[1]

Mchungaji mmoja mkomavu alizungumza jinsi alivyopanga wakati wake wa ibada. Alisema hivi: "Niliweka wakati kila asubuhi kwa ajili ya kuabudu kibinafsi,

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu mchungaji wa Kipentekoste na usimamizi wa wakati, tazama Sura ya 13: "Maisha Yanayosimamiwa Vizuri."

na kujifunza Biblia, na kuwajulisha watu wangu hiyo ratiba. Ikitokea kwamba mtu fulani anapiga simu wakati huo na kuniambia, 'Nataka kukuona,' inabidi angoje mpaka nimalize ibada yangu. Nikimaliza, natoka na kukutana naye. Ni kweli kwamba zipo dharura ambazo lazima nizishughulikie. Ila, hizo ni tofauti. Kanuni ni kwamba ninatoa kipaumbele kwa ule muda wangu ninaokuwa mbele za Mungu."

*3. Nidhamu*. Suala la tatu katika kukuza tabia imara ya ibada binafsi ni nidhamu binafsi. Kuna faida gani ikiwa mchungaji wa Kipentekoste anaweka vipaumbele na kupanga wakati wake kisha kukosa nidhamu binafsi inayohitajika ili kutekeleza mpango wake? Kwa hiyo ni lazima uwe na nidhamu ili kutunza miadi yako na Mungu kila siku. Kama mchungaji, huna mtu wa kukuambia, "Ni wakati wa kuomba. Ni wakati wa kusoma Biblia." Kwa hiyo, lazima uwe na nidhamu. Paulo alimwambia Timotheo kwamba mwangalizi, au mchungaji, lazima awe na kiasi (1 Tim. 3:2). Zaidi, alifundisha kwamba kujitawala au kiasi ni tunda la Roho Mtakatifu (Gal. 5:23).

### Mambo Mawili Yanayofanyika Katika Ibada Binafsi

Kama tulivyokwisha onyesha katika sura hii, mambo mawili makuu ya ibada binafsi ni maombi na kujifunza Biblia. Hebu tuyaangalie kwa karibu zaidi.

*1. Maombi ya kuabudu.* Mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kujumuisha maombi ya kuabudu katika nyakati zake za ibada binafsi. Maombi haya ni tofauti na dua au maombezi. Katika maombi ya kuabudu, mtafutaji anamwomba Bwana kukutana na hitaji katika maisha yake mwenyewe. Katika maombezi, yeye huombea mahitaji ya wengine. Pia, katika maombi ya ibada binafsi, mhusika hujikabidhi kwa Mungu, akitafuta kumkaribia. Daudi aliomba maombi aina hiyo aliposema: "Nionyeshe njia zako, Bwana, unifundishe mapito yako" (Zab. 25:4).

Maombi haya pia yanajumuisha nyakati za kuimba, kuabudu, na kumshukuru Mungu. Kuna wakati ambapo yanajumuisha toba, kama Daudi alivyo-omba, "Nimekutenda dhambi wewe peke yako, na kufanya yaliyo maovu machoni pako. …Unitakase kwa hisopo, nami nitakuwa safi; unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji" (Zab. 51:4, 7). Neno la Mungu linaahidi, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yoh. 1:9).

Katika nyakati zako za ibada, ni vizuri kuombea familia yako, ili wawe na afya njema ya kimwili na kiroho. Pia utataka kuliombea kanisa lako, ili Roho

Mtakatifu atie nguvu na kuelekeza mambo yake, na kwamba wote walio sehemu ya kanisa wajazwe na Roho. Vilevile ni vema kuombea kanisa liwe na afya njema na kwamba karama na tunda la Roho viwepo kanisani.

*2. Kujifunza Biblia.* Nyakati zako za ibada zijumuishe kujifunza Biblia. Ila ni vizuri ukaelewa tofauti kati ya ibada na kujifunza Biblia kitaaluma. Kusoma Biblia kitaalamu ni somo ambalo mchungaji hufanya ili kujitayarisha kwa ajili ya huduma. Aina hii ya kujifunza Biblia hutokea anapojifunza Biblia ili kuandaa mahubiri au somo la Biblia. Kwa mchungaji wa Kipentekoste, kujifunza Biblia kitaalamu ni muhimu. Lakini hupaswi kujifunza Biblia hivyo wakati unapofanya ibada yako binafsi.

Kusoma Biblia kwa kuabudu hutokea unaposoma Biblia kwa ajili ya ukuaji wa binafsi kiroho. Lengo lako si kutayarisha mahubiri bali kuelewa vyema Neno la Mungu, na kuruhusu maneno ya Mungu yatengeneze maisha yako. Kusudi la kujifunza Biblia hivi ni kukutana na Mungu katika Neno Lake. Kusudi ni kumjua Mungu zaidi, kumkaribia Kristo, na kumtumikia kikamilifu zaidi. Ayubu alizungumza kuhusu mwitikio wake wa ibada kwa Maandiko aliposema, "Sikuacha maagizo ya midomo yake; Nimeyatunza maneno ya kinywa chake kuliko riziki yangu ya kila siku" (Ayubu 23:12).

Wengine wamependekeza hatua nne katika kujifunza Biblia kwenye ibada binafsi. Hatua ya kwanza ni kusoma kifungu husika polepole na kwa kufikiria. Hatua ya pili ni kutafakari kifungu husika, kuuliza maswali kama vile, "Mungu ananiambia nini kupitia kifungu hiki? na "Ninapaswa kuitikiaje ujumbe wa Mungu katika kifungu hiki?" Hatua ya tatu ni kuomba, "Bwana, unataka nifanye nini?" Na hatua ya mwisho ni kutii yale ambayo Mungu amesema katika Neno lake na kuweka kanuni zake katika matendo.

## MAONI ZAIDI KUHUSU IBADA BINAFSI

Kwa kumalizia, hebu tuangalie maarifa matatu ya ziada kuhusu jinsi unavyoweza kuimarisha tabia yako ya ibada binafsi na kuimarisha uhusiano wako na Mungu.

### Kutumia Sala ya Bwana

Mara kwa mara, utapenda kutumia Sala ya Bwana kuwa mwongozo katika nyakati za ibada yako binafsi. Sala hii inapatikana katika Mathayo 6:9-13. Yesu aliwapa wanafunzi Wake kama kielelezo cha maombi yenye matokeo. Kwa

kutumia maombi haya kama mwongozo, muda wako wa ibada binafsi utakwenda kama ifuatavyo:

1. *Anza na sifa:* "Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe" (mst. 9). Tumia dakika chache kuimba na kumwabudu Mungu. Msifu kwa vile alivyo, na umshukuru kwa yote aliyofanya.
2. *Omba mapenzi yake yatimizwe:* "Ufalme wako uje, Mapenzi yako yafanyike duniani kama huko mbinguni" (mst. 10). Omba ufalme wa Mungu uje katika maisha ya watu. Omba watu wazaliwe mara ya pili na kuanza kumfuata Kristo (Yoh. 3:3-8). Omba waponywe na kukombolewa kutoka kwenye kufungwa na mapepo (Mt. 12:28; Lk. 11:20). Waombee wajazwe na Roho Mtakatifu (Mk. 9:1; Mdo. 1:3-8). Na omba ili Yesu aje upesi (Lk. 22:18; Uf. 12:10; 22:20).
3. *Msihi Mungu:* "Utupe leo mkate wetu wa kila siku" (mst. 11). Mwombe Mungu akutimizie mahitaji yako yote "kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake katika Kristo Yesu" (Flp. 4:19). Omba kwa ajili ya mahitaji ya wengine.
4. *Omba msamaha na kuutoa:* "Na utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe wadeni wetu" (mst. 12). Jinyenyekeze mbele za Mungu, ukiomba msamaha wake na kutoa msamaha kwa wengine.
5. *Omba mwongozo na ulinzi wa Mungu:* "Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu" (mst. 13). Mwombe Mungu akupe mwongozo katika maisha na huduma yako na ulinzi wake kinyume na shetani na majeshi yake ya pepo wabaya.

**Maombi Endelevu**

Pamoja na kudumisha muda wa kila siku wa ibada binafsi, mchungaji wa Kipentekoste lazima ajifunze "kuomba bila kukoma" (1 Thes. 5:17). Bila shaka hii haimaanishi kwamba unapaswa kubaki kwenye maombi siku nzima kila siku. Ina maana kwamba hupaswi kamwe kuacha kuomba. Unapaswa kujifunza kuishi katika hali endelevu ya ushirika na Mungu. Unapoendelea na shughuli zako za kila siku, sala inapaswa kuwa midomoni mwako daima (Zab. 34:1; Ebr. 13:15). Zoezi hili litaimarishwa ikiwa siku yako itaanza na wakati wa ibada binafsi kama ilivyoelezwa hapo juu. Maombi bila kukoma ni muhimu ili kuishi maisha sambamba na Roho wa Mungu (Gal. 5:25).

**Kuandika Vitu**

Hatimaye, ni mazoezi mazuri kwa mchungaji wa Kipentekoste kuweka shajara ya maombi ya kila siku. Jarida la maombi ni daftari ambalo mchungaji

huweka kumbukumbu ya kile kinachotokea wakati wa ibada yake binafsi. Katika jarida hili, unarekodi maombi ambayo umemwomba Mungu, pamoja na majibu ya Mungu kwa maombi hayo. Unapotazama uaminifu wa Mungu katika kujibu sala zako, imani yako itaimarishwa.

Pia utataka kuandika maneno au hisia zozote unazoweza kupokea kutoka kwa Roho Mtakatifu. Maoni haya yanaweza kutumika baadaye kama miongozo, kukusaidia kutambua mwelekeo wa Mungu kwa maisha na huduma yako. Kwa kuongezea, unaweza kutaka kuandika maarifa yoyote unayopokea unaposoma Biblia. Baadhi ya maarifa haya yanaweza baadaye kukuzwa kuwa ujumbe kwa ajili ya kusanyiko. Mara kwa mara utataka kuhakiki yale uliyoandika katika shajara yako, ukimwomba Mungu kutia moyoni mwako mambo hayo anayotaka uyakumbuke.

---

Kwa mchungaji wa Kipentekoste, tabia ya ibada binafsi ya kila siku si hiari; ni jambo la lazima. Tabia kama hiyo itaboresha sana maisha na huduma yake kwa njia nyingi. Itatoa mwongozo na nguvu za kiroho, vitu vinavyohitajika ili kutimiza mwito wa Mungu maishani mwao.

## ~ Sehemu ya 5 ~

# Huduma ya Mchungaji wa Kipentekoste Mbele ya Watu

~ Sura ya 16 ~

# Mahubiri Yenye Upako wa Roho

Mchungaji mmoja asiye Mpentekoste alitilia shaka ukweli wa ubatizo katika Roho Mtakatifu. Mara nyingi alionyesha mashaka yake juu ya uzoefu huo. Kisha siku moja alipokuwa akisoma Matendo 2 na kutafakari juu ya matukio ya Siku ya Pentekoste, aliomba na kupokea uzoefu wa Kipentekoste. Baadaye alishuhudia, "Kwa muda mfupi tangu nimpokee Roho Mtakatifu, mahubiri yangu yametoa matokeo zaidi kuliko miaka yangu yote ya awali ya kuhubiri!"

Kihistoria, mahubiri yenye nguvu, yaliyotiwa mafuta na Roho yamekuwa alama ya huduma ya Kipentekoste. Tangu mwanzo wa karne ya ishirini, harakati ya Kipentekoste imetokeza jeshi kubwa la wahubiri waliowezeshwa na Roho Mtakatifu, wakitangaza kwa bidii ujumbe wa wokovu kwa mataifa.

Sura hii itashughulikia mada ya mahubiri ya Kipentekoste. Itazingatia nafasi ya Roho Mtakatifu katika kumtia mafuta mhubiri. Pia itatoa mapendekezo kuhusu maandalizi na utoaji wa mahubiri.

## MAHUBIRI YA PENTEKOSTE

Yesu aliwaamuru wanafunzi wake, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa viumbe vyote" (Mk. 16:15). Kuhubiri ni kutangaza Neno la Mungu kwa bidii ili kuwashawishi watu wamfuate Kristo na kufanya mapenzi

yake. Ni mada kuu katika Agano Jipya ambapo maneno kuhubiri au kutangaza hutokea karibu mara 150. Uwezo wa kuhubiri jumbe zenye upako wa Roho ni wajibu wa msingi wa kila mchungaji wa Kipentekoste.

**Mfano wa Kitabu cha Matendo**

Wapentekoste wanaamini kwamba kuhubiri kwa mitume na wengine katika kitabu cha Matendo kunakusudiwa kuwa kielelezo kwa wahubiri wa leo. Katika Matendo, Luka anaandika yaliyomo katika mahubiri kadhaa yaliyohubiriwa na mitume na wahubiri wengine (kwa mfano, Petro: Mdo. 2:14-40; 3:12-26; 10:28-47; Stefano: Mdo. 7:1-53; Paulo: Mdo. 13:16-41; 17:22-31). Sehemu kubwa ya nafasi anayotoa Luka kwa mahubiri haya katika Matendo ya Mitume huonyesha umuhimu anaoweka juu yake. Alitaka wasomaji wake wajue jinsi mitume walivyohubiri ili nao wafanye vivyo hivyo.

Uchunguzi wa makini wa mahubiri katika Matendo ya Mitume unaonyesha angalau vipengele vitano muhimu vya mahubiri ya mitume.

1. *Kiini alikuwa Yesu.* Utu na kazi ya Kristo ni kiini cha kila ujumbe unaohubiriwa katika Matendo. Wahubiri wa Agano Jipya walitangaza mara kwa mara kwamba Yesu alikuwa utimilifu wa unabii wa Agano la Kale, na kwamba alikuwa njia pekee ya wokovu (taz. Mdo. 2:22-24, 30-32; 3:13-20; 4:10-12); 5:30-31; 8:5; na mengine).
2. *Maandiko yalirejelewa*. Wahubiri katika kitabu cha Matendo mara kwa mara walifanya rejea kwa Maandiko kuunga mkono madai yao (taz. Mdo. 2:17-21; 3:22-23; 4:11, 25-26; na mengine).
3. *Yalitiwa mafuta na Roho Mtakatifu.* Wahubiri katika Matendo ya Mitume walijazwa, na hivyo kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu (taz. Mdo. 2:4, 14; 4:8; na mengine).
4. *Uthibitisho usio wa kawaida.* Katika Matendo ya Mitume, utangazaji wa injili mara nyingi uliambatana na ishara na maajabu ya kuthibitisha (rej. Mdo. 3:1-8; 8:4-7; 14:8-10; na mengine).
5. *Wito wa toba na imani.* Wahubiri katika kitabu cha Matendo kwa kawaida walihitimisha mahubiri yao kwa mwito wa toba na imani (rej. Mdo. 2:38; 3:19; 8:22; na mengine).

Sifa hizi hizi zinapaswa kuwa kiini cha mahubiri ya Kipentekoste katika Afrika leo. Ungefanya vyema kukariri orodha hii na kuitumia kama kiwango cha kutathmini huduma yako ya kuhubiri.

## UPAKO WA ROHO MTAKATIFU

Katika Agano la Kale, manabii, makuhani, na wafalme walipakwa mafuta walipoingizwa kazini (kama vile Kut. 28:41; 1 Sam. 9:16; 16:11-13; 1 Waf. 1:34; 19:16). Upako huu ulitumika kama ishara ya wito wao, na ulionyesha mamlaka waliyopewa na Mungu ya kufanya kazi katika ofisi zao. Ilionyesha zaidi uwepo wa Roho wa Mungu juu yao ili kuwawezesha kufanya kazi za huduma yao (Isa. 61:1-2).

Kama ilivyoelezwa hapo juu, kipengele kimoja cha mahubiri katika kitabu cha Matendo ni kwamba wahubiri walitiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Hebu tuangalie kwa karibu zaidi wazo hili.

### Huduma ya Yesu Yenye Upako

Yesu alianza huduma yake kwa kutangaza kwamba, "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kutangaza habari njema" (Lk. 4:18). Kwa hali hiyo, alielezea jambo hilo kuwa ni Roho kuwa juu yake. Alitumia neno hili kuelezea utendaji kazi wenye nguvu wa Roho Mtakatifu ndani na kupitia Kwake, na kumwezesha Yeye kutekeleza huduma Yake kama Masiya.

### Huduma ya Mitume Yenye Upako

Ndivyo ilivyotokea kwa wale wanafunzi 120 siku ile ya Pentekoste. Kwanza, Roho alikuja juu yao (Mdo. 2:3). Kisha, akawajaza. Na hatimaye, Alianza kunena kupitia kwao (mst. 4, 14). Haya yote yalitokea katika utimizo wa ahadi ya Yesu katika Matendo 1:8, kama ifuatavyo: "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu… hata mwisho wa nchi."

Hivyo, kupakwa mafuta ni kujazwa na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Kama vile Roho alivyokuja juu ya Yesu na wanafunzi wa kwanza, akiwatia mafuta kwa ajili ya huduma, Roho atakuja juu ya mfuasi aliyejitoa leo, akimtia mafuta kwa ajili ya huduma.

### Upako Unaelezwa

Upako ni utendaji wenye nguvu wa Roho Mtakatifu ndani, juu, na kupitia kwa watu binafsi ambao wamejitoa kikamilifu kwa Mungu. Ni uwepo dhahiri wa Mungu ambao huja kutulia juu ya mfuasi aliyejazwa na Roho, kumwezesha kuhudumu kwa nguvu na ufanisi zaidi.

Katika kitabu cha Matendo, maneno kujazwa na kujazwa na Roho Mtakatifu hutumiwa wakati m wingine kuelezea upako wa Roho. Neno hili, kujazwa na Roho Mtakatifu, linaeleza kuja kwa Roho juu ya mtu, kujazwa na kumtia mtu mafuta ili kutenda na kusema kwa nguvu na mamlaka (Mdo. 4:8, 31; 13:9-12). Neno hili kujaa Roho Mtakatifu, linaeleza hali inayoendelea ya kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu (Mdo. 6:3, 5; 7:55). Huu unaweza kuwa "upako uliobaki" unaonenwa na Yohana (1 Yoh. 2:27). Upako unabaki juu yetu kadiri tunavyobaki ndani ya Kristo (Yoh. 15:4-7). Kutengana na dhambi ni sharti muhimu kwa upako kuendelea kubaki (Yoh. 14:15-16). Upako huu lazima uwe kipaumbele katika maisha ya kila mchungaji wa Kipentekoste.

## Mahubiri Yenye Upako

Mahubiri yaliyovuviwa hayapaswi kuchanganywa na ufasaha tu, haiba ya asili, au uwezo wa kusisimua hisia. Wala hayapaswi kuchanganywa na utoaji wa mahubiri kwa mhemuko. Ingawa mahubiri yaliyotiwa mafuta na Roho yanaweza kuonyesha hayo yote, ni zaidi ya hayo. Mahubiri yaliyotiwa mafuta na Roho ni mahubiri yenye Roho. Ni aina ya mahubiri kwa mifano iliyo-onyeshwa na Yesu na mitume.

Luka anaonyesha ukweli huu katika habari ya Apolo. Anaeleza kama ifuatavyo: "Apolo…alikuwa mtu mwenye elimu, mwenye ujuzi kamili wa Maandiko. Alikuwa amefundishwa njia ya Bwana, naye alinena kwa bidii nyingi na kufundisha juu ya Yesu kwa usahihi" (Mdo. 18:24-25). Kwa hiyo Apolo alikuwa mhubiri mwenye ufasaha na mwenye uwezo kiakili. Lakini, "alijua ubatizo wa Yohana tu" (mst. 25). Hakuwa na ujuzi wa Pentekoste. Ila baada ya Prisila na Akila "kumfafanulia njia ya Mungu kwa ubora zaidi," yaonekana alijazwa na Roho Mtakatifu. Ndipo akasafiri hadi Akaya ambako alikuwa "msaada mkubwa kwa wale walioamini kwa neema" (mst. 27).

Yesu alisema juu ya mahubiri na mafundisho yake yaliyotiwa mafuta, "Maneno niliyowaambia — yamejaa Roho na uzima" (Yoh. 6:63). Biblia inaeleza hivi kuhusu mahubiri ya mitume: "Mitume wakaendelea kushuhudia ufufuo wa Bwana Yesu kwa nguvu nyingi. Na neema ya Mungu ilifanya kazi kwa uwezo ndani yao wote" (Mdo. 4:33). Maneno yale - neema ya Mungu ilifanya kazi kwa nguvu sana ndani yao wote - yanaeleza vizuri sana upako wa Roho Mtakatifu. Katika Matendo ya Mitume, upako wa Roho juu ya mhubiri uliwaathiri sana wale waliosikiliza (Mdo. 2:4, 14 na 1 Kor. 2:4; Mdo. 2:37 na 1 Kor. 2:5).

Paulo alizungumza juu ya mahubiri yake mwenyewe yaliyotiwa mafuta na Roho katika nyaraka zake. Aliwakumbusha waamini wa Korintho jinsi alivyowahubiria injili mara ya kwanza. Aliandika hivi: "Ujumbe wangu na mahubiri yangu havikuwa kwa maneno ya hekima na ya kuvutia, bali kwa onyesho la nguvu za Roho" (1 Kor. 2:4-5). Alieleza huduma yake kwa waamini katika Warumi: "Kwa nguvu za ishara na maajabu, kwa nguvu ya Roho wa Mungu…nimeihubiri Injili ya Kristo kwa utimilifu" (Rum. 15:19). Aliwakumbusha waamini wa Thesalonike, "Injili yetu iliwajia si kwa maneno tu, bali pia kwa nguvu, na Roho Mtakatifu na usadikisho wa kina" (1 Thes. 1:5).

Roho Mtakatifu yuko tayari kutia mafuta mahubiri yetu leo kama vile alivyomtia mafuta Yesu na mitume katika karne ya kwanza. Lakini, nini chanzo cha upako, na unapatikanaje?

## ASILI YA UPAKO

Ili kuweza kuhubiri kwa upako wa Roho, mchungaji wa Kipentekoste lazima aelewe chanzo. Chanzo cha upako ni uwepo unaokaa ndani na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Ni Roho ndani, na juu ya mhubiri (Yoh. 14:17; Mdo. 1:8). Nguvu hizi za Roho Mtakatifu hupokelewa pale mtu anapobatizwa na kujazwa na Roho Mtakatifu (Mdo. 2:4). Upako unabaki pale mtu anapotembea "katika hatua na Roho" (Gal. 5:25). Ukweli huu unaonyeshwa katika huduma za Yesu na mitume.

### Chanzo cha Upako wa Yesu

Yesu alithibitisha kwamba chanzo cha upako wake ni Roho wa Bwana (Lk. 4:18). Ingawa alikuwa Mwana wa Mungu kweli aliyefanyika mwili, alichagua kujiondolea uweza wake wa kiungu na mapendeleo na kutekeleza huduma yake katika nguvu za Roho (Flp. 2:5-8). Hivyo huduma ya Yesu iliyotiwa mafuta na Roho ingetumika kuwa kielelezo kwa wote ambao wangemfuata.

Yesu hakuanza huduma yake hadi alipotiwa mafuta kwa Roho mara ya kwanza. Yeye kubatizwa na Roho kulifanyika mara baada ya Yohana kumbatiza katika maji. Biblia inasema, "Naye [Yesu] alipokuwa akiomba, mbingu zilifunguliwa na Roho Mtakatifu akashuka juu yake katika umbo kama hua" (Lk. 3:21-22). Kisha Yesu "alianza huduma yake" (mst. 23). Alianza kutembea na kuhudumu katika nguvu za Roho (Lk. 4:1, 14). Alitangaza na kusema, "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kutangaza habari njema" (Lk. 4:18). Baadaye, watu walipomsikia Yesu akisema, "walishangazwa na maneno ya

neema yaliyotoka midomoni mwake" (mst. 22). Nao walishangaa "kwa sababu maneno yake yalikuwa na mamlaka" (mst. 32; taz. Mt. 7:28 -29).

**Chanzo cha Upako wa Mitume**

Kama vile Roho Mtakatifu alivyokuwa chanzo cha huduma ya Yesu iliyotiwa mafuta, Yeye pia alikuwa chanzo cha huduma ya mitume iliyotiwa mafuta. Kama Yesu, mitume walibatizwa kwanza katika Roho Mtakatifu. Kisha wakaanza kuhubiri kwa nguvu.

Labda Petro ndiye mfano bora zaidi wa nguvu hii ya kiroho. Kabla ya Pentekoste, aliogopa kumkiri Yesu kwa kijakazi (Mt. 26:69-72). Lakini mara tu alipojazwa na Roho Mtakatifu, alihubiri kwa nguvu, na maneno yake yaliwagusa sana wasikilizaji wake (Mdo. 2:37). Matokeo yake: watu elfu tatu walikuja kwa Kristo. Hali hii inarudiwa mara kadhaa katika Matendo (4:8, 31-33).

Upako uleule uliokuwa juu ya Yesu na mitume ukiwawezesha kuhubiri kwa nguvu unapatikana kwetu leo.

## KUPATA UPAKO

Maswali yanaibuka, "Je, mtu anawezaje kweli kupata upako wa Roho Mtakatifu leo? Je, upako unapokelewaje? Je, unaonyeshwaje katika huduma? Unaweza kudumishwaje?"

**Kupokea Upako**

Upako unapokelewa leo kama vile ulivyopokelewa na Yesu na wanafunzi wa kwanza. Hupokelewa mwanzoni mtu anapobatizwa katika Roho Mtakatifu. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Yesu alipokea Roho Mtakatifu wakati wa ubatizo wake. Kisha akaanza kuhudumu kwa nguvu. Ndivyo ilivyokuwa kwa wanafunzi. Walipokea Roho mara ya kwanza siku ya Pentekoste, na kama Yesu, wao pia walianza kuhudumu kwa nguvu.

Yesu alitoa maagizo ya wazi kuhusu jinsi mtu anavyoweza kupokea Roho. Aliwaambia wanafunzi wake, "Baba yenu aliye mbinguni [atawapa] Roho Mtakatifu wale wamwombao!" (Lk. 11:13). Alieleza, "Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa mlango. Kwa maana kila aombaye hupokea; atafutaye huona; naye abishaye, mlango utafunguliwa" (mst.

9-10). Hivyo Roho hupokelewa kwa kuomba kwa imani (mst. 9), kupokea kwa imani (mst. 10 na Mk. 11:24), na kunena kwa imani (Mdo. 2:4).[1]

**Kudhihirisha Upako**

Upako unaopokelewa wakati wa ubatizo wa Roho unadhihirika katika huduma hasa kupitia utendaji wa karama za kiroho. Kweli mahubiri yaliyotiwa mafuta na Roho ni onyesho la karama ya unabii. Ni matamko yaliyo-ongozwa na Roho, na kuvuviwa na Roho. Mahubiri yaliyotiwa mafuta kwa Roho ni pamoja na udhihirisho wa karama za ufunuo kama vile neno la maarifa na neno la hekima. Kwa kuongezea, mahubiri yaliyotiwa mafuta na Roho mara nyingi huambatana na udhihirisho wa karama ya nguvu, kama ilivyotokea kwa Paulo huko Listra (Mdo. 14:8-10).[2]

Unaweza kupata upako kwa kuomba, na kuitikia kwa imani uwepo wa Roho Mtakatifu. Unapoingia katika mimbari, unapaswa kuomba na kusema, "Ee Roho Mtakatifu, njoo sasa unitie mafuta kuhudumu Neno lako." Basi, nenda kwa imani, ukiamini kwamba Mungu amesikia maombi yako. Mara unapohisi uwepo wa Roho, itikia kwa imani, jitoe kwa uongozi wake na kumwamini awezeshe na kutia nguvu mahubiri yako.

**Kudumisha Upako**

Upako unadumishwa kwa kuishi na kutembea katika Roho (Gal. 5:25). Kutembea katika ujazo wa Roho ni maisha ya kujinyenyekeza na kumtii Mungu na utume Wake. Maombi pamoja na kuomba katika Roho, ni kipengele muhimu cha kudumisha upako (Rum. 8:26-27; 1 Thes. 5:17).

## KUJIANDAA NA KUHUBIRI KATIKA UPAKO

Mchungaji yeyote wa Kipentekoste mwenye nia ya kuwa mhubiri aliyefanikiwa na kutiwa mafuta na Roho, atahitaji kujishughulisha mwenyewe katika kujiandaa na kuhubiri. Ni lazima ahakikishe kwamba Roho Mtakatifu yuko naye, akimpaka mafuta na kuongoza kila shughuli.

---

[1] Mengi zaidi yanasemwa kuhusu kupokea Roho Mtakatifu katika Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

[2] Tazama Nyongeza 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

**Maandalizi Mahubiri**

Kutazama kwa karibu mahubiri katika Matendo ya Mitume kunaonyesha kweli mbili muhimu: jumbe za mitume zilijaa Maandiko, na kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Wahubiri katika Matendo walionyesha ufahamu mpana wa Maandiko. Mara nyingi walinukuu Maandiko katika jumbe zao. Kwa mfano, mahubiri ya Petro ya Siku ya Pentekoste yana maandiko manne kutoka Agano la Kale (ling. Mdo. 2:16-21, 25-28, 31, 34-35). Vile vile, ujumbe wa Stefano kwa Baraza la Wazee Viongozi wa Kiyahudi (Sanhedrin) una maandiko nane (ling. Mdo. 7:3, 6-7, 28, 32-35, 37, 40, 42-43, 49). Mahubiri mengine katika Matendo ya Mitume yanafuata mtindo huo. Wahubiri hawa wa kwanza walielewa Maandiko, na walijenga jumbe zao katika uelewa wao huo.

Wachungaji wa Kipentekoste wa Afrika ya leo lazima wafanye vivyo hivyo. Kama wenzetu, yaani mitume, ni lazima tujenge mahubiri yetu kwenye uthabiti katika Maandiko. Ili kufanya hivyo, ni lazima tujitoe na kujifunza Biblia kwa nidhamu na bidii kubwa. Ni lazima tutoe wakati wa kutosha kila juma kwa ajili ya usomaji wa Biblia kwa uzito na kutayarisha mahubiri. Tunapojiandaa, tunapaswa kumwangalia Roho Mtakatifu ili atie mafuta na kuhuisha mawazo yetu, tukitambua kwamba upako wa Roho Mtakatifu haukatazi maandalizi; badala yake huyaimarisha na kuyatia nguvu zaidi.

Pia katika Matendo wahubiri waliomba kwa matarajio ya kujazwa na kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Mara kwa mara, kitabu cha Matendo huunganisha kuja kwa Roho Mtakatifu na maombi. Kwa mfano, wanafunzi walikuwa kwenye maombi kabla ya kushuka kwa Roho ile Siku ya Pentekoste (Mdo. 1:14; 2:1-4). Waamini wa Yerusalemu walikuwa wakiomba kabla ya umwagiko wa pili wa Roho katika mji huo (Mdo. 4:23-31). Paulo na Anania walikuwa wakiomba kabla ya Paulo kujazwa na Roho (Mdo. 9:5, 10-15). Mifano zaidi inaweza kutajwa.

Sisi wachungaji wa Kipentekoste tunaotaka Roho Mtakatifu atie mafuta mahubiri yetu lazima tujitoe kuomba. Maombi kama haya ya kujitoa yatahakikisha upako wa Roho, yakigusa sana na kwa kina maudhui na utoaji wa mahubiri yetu.

**Kutolewa kwa Mahubiri**

Lengo la utoaji wa mahubiri si kuwavutia wasikilizaji bali kuongeza uelewa wa ujumbe kwa watu. Kila linalosemwa au kufanywa linapaswa kulenga kuwaelekeza watu wakutane na Mungu. Mbinu au tabia zozote zinazochangia

lengo hili zinapaswa kuendelezwa. Zozote zinazosumbua na kuchepuka kutoka kwenye lengo hilo zinapaswa kuachwa.

Basi kama wahubiri wa Kipentekoste, mwenendo wetu unapaswa kuwa wa kweli na usioathiriwa na ubovu wowote. Tunapaswa kuepuka kunong'ona, kupiga kelele, kutanga-tanga madhabahuni pasipo mwelekeo, na kupepesa mikono bila utaratibu na mpango. Ishara zetu zinapaswa kuwa za kawaida na zisizo za kuigiza au kujifanya. Vitendo vyetu madhabahuni vinapaswa kuibuka kwa kawaida kutoka ndani na kuongozwa na Roho na yaliyomo katika ujumbe. Ikiwa tutajihusisha na ujumbe tunaohubiri kiakili na kihisia, ishara zinazofaa zitajitokeza na kufuata kama sehemu yetu ya kawaida.

Kuita watu madhabahuni katika kumalizia mahubiri ni muhimu sana. Wakati wa hatua hii muhimu ya mahubiri, ni muhimu kwa mhubiri kuongozwa na Roho Mtakatifu. Huo mwito si wakati wa kutambulisha mawazo mapya katika ujumbe. Mhubiri lazima abakie kwenye lengo lake, wala asichepuke kwenda pembeni. Badala yake, ni vizuri abakie kwenye hoja yake na kutoa maelekezo ya wazi kuhusu kile anachotaka watu wafanye kama itikio lao kwa mahubiri.

---

Wachungaji wa Kipentekoste ni wa kipekee miongoni mwa wahubiri kwa kuwa tunathamini na kutafuta upako wa Roho Mtakatifu katika mahubiri yetu. Kwa kufanya hivi, tunatafuta kufuata mfano wa Yesu na wahubiri wa Agano Jipya. Maombi yetu ya kudumu yanapaswa kuwa hivi: “Bwana, nijaze na kunitia mafuta kwa ajili ya huduma”.

~ Sura ya 17 ~

# Kufundisha kwa Ufanisi

Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa" (Hosea 4:6). Maneno haya ya Mungu yalisemwa kupitia nabii Hosea kwa makuhani wa Israeli. Kwa sababu viongozi hao wa kiroho hawakuwafundisha watu wa Mungu ukweli, waliamini uongo. Kwa sababu hiyo, walikuwa wametangatanga katika dhambi. Nabii huyo alieleza hali yao yenye kuhuzunisha kwa kusema hivi: "Hakuna uaminifu, hakuna upendo, hakuna kumtambua Mungu katika nchi. Kuna laana tu, na kusema uongo, na kuua, na kuiba na uzinzi" (mst. 1-2).

Cha kusikitisha ni kwamba Wakristo wengi wa Kipentekoste kote barani Afrika wanajikuta katika hali kama hiyo. Hawana ufahamu mzuri wa Neno la Mungu. Kwa hiyo, kukua kwao kiroho kumeathirika, na wamedumaa. Kwa sababu hiyo, wamekuwa mawindo rahisi kwa walimu wa uongo. Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uhakikishe kwamba hali kama hiyo haipo katika kanisa lolote ambalo umeitwa kuchunga.

## WAJIBU WA MCHUNGAJI

Kila mchungaji wa Kipentekoste anabeba jukumu la kipekee la kulisha kundi la Mungu. Katika mkutano wake wa mwisho na wachungaji wa kanisa la Efeso, Paulo aliwahimiza kwamba, "Jilindeni nafsi zenu, na lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake" (Mdo. 20:28). Kisha

akawaamuru wachungaji hao, “Iweni wachungaji wa kanisa la Mungu [au, lisheni kundi], ambalo alilinunua kwa damu yake mwenyewe.” Paulo alijua kwamba kwa kuwafundisha watu wa Mungu Neno la Mungu, wachungaji wa Efeso wangewasaidia kuimarika kiroho. Hilo lingewatayarisha kupingana na “mbwa-mwitu wakali” ambao wangeingia kanisani karibuni ili kupotosha ukweli, na kutafuta kuwavuta watu mbali na Kristo (mst. 29-30).

Basi, kufundisha ndicho kitu muhimu katika maana ya kuwa mchungaji wa Kipentekoste. Paulo aliandika kuhusu karama tano za huduma ambazo Kristo ametoa kwa kanisa, kama ifuatavyo: “Vivyo hivyo Kristo mwenyewe alitoa mitume, na manabii, na wainjilisti, na wachungaji, na waalimu, ili kuwatayarisha watu wake kwa kazi ya huduma, ili mwili wa Kristo ujengwe” (Efe. 4:11-12).

Katika fungu hili la Maandiko, angalia jinsi Paulo anavyounganisha karama mbili za huduma za mwisho kuwa moja. Kwa sababu hiyo, wasomi fulani wameitaja karama hiyo kuwa “mchungaji aliye mwalimu.” Ni hivi: Ili mtu awe mchungaji, ni lazima pia awe mwalimu. Mungu anapomwita mchungaji, humpa pia karama ya kufundisha.

Ili kuwatunza kondoo ifaavyo, ni lazima uweze kuwalisha watu wa Mungu ifaavyo, kuwalisha Neno la Mungu. Biblia inalifananisha Neno la Mungu na vyakula vyenye lishe kama vile mkate (Mt. 4:4), maziwa (1 Pet. 2:2), na chakula kigumu (Ebr. 5:12-14). Mchungaji yeyote ambaye anashindwa kuwalisha watu wake Neno la Mungu ni mchungaji asiye mwaminifu, na Mungu atawawajibisha kwa kushindwa hapo (Yak. 3:1; Eze. 34:16).

Ila, kama utawafundisha watu Neno la Mungu kwa uaminifu, utaheshimiwa na Mungu (Mt. 24:45-47). La maana zaidi ni kwamba, watu wa Mungu wataimarishwa. “Hawatakuwa tena watoto wachanga, wakitupwa huku na huku na mawimbi, na kupeperushwa huku na huku na kila upepo wa mafundisho, na kwa hila na ujanja wa watu katika hila zao za udanganyifu. Badala yake, wakisema kweli katika upendo, watakua katika kila namna mwili mkomavu wake yeye aliye kichwa, yaani, Kristo” (Efe. 4:14-15).

**Kufanya Wanafunzi**

Yesu aliliamuru Kanisa Lake hivi, “Nendeni mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi” (Mt. 28:19). Alichosema ni kwamba wanapaswa kufanya kwa wengine yale ambayo alikuwa amefanya kwao. Yesu alitembea pamoja na wanafunzi Wake, aliwafundisha kweli, na kuwaonyesha jinsi ya kuishi. Kama

wachungaji wa Kipentekoste, lazima tufanye vivyo hivyo na washirika wa kanisa letu. Haitoshi kupata waongofu tu, lazima tutengeneze wanafunzi. Mwanafunzi ni mfuasi wa Kristo aliyejitoa kwake. Yeye ni mwenye kuketi miguuni pa Yesu na kujifunza kutoka Kwake. Si lazima tuwaite watu wamfuate Kristo tu, bali pia ni lazima "tuwafundishe kutii" amri zake zote (mst. 20).

**Kuhubiri na Kufundisha**

Wachungaji wengi wa Kipentekoste barani Afrika wanajiona kuwa wahubiri, lakini hawajioni kuwa walimu. Ila wewe kama mchungaji, Mungu amekuita kuwa yote mawili. Lazima uwe mhubiri stadi na mwalimu mzuri wakati huo huo. Ili kuelewa vizuri nafasi yako kama mwalimu wa watu wa Mungu, unahitaji kujua tofauti kati ya kuhubiri na kufundisha.

Biblia inatofautisha waziwazi kati ya kazi hizi mbili. Kwa mfano, Biblia inasema kwamba Yesu "alizunguka Galilaya, *akifundisha* katika masinagogi yao, na *kuhubiri* habari njema ya ufalme" (Mt. 4:23, maneno mepesi kuonyesha msisitizo). Tunaambiwa hivi kuhusu Paulo na Barnaba: "wakabaki Antiokia, ambapo wao na wengine wengi *walifundisha na kuhubiri* neno la Bwana" (Mdo. 15:35, maneno mepesi kuonyesha msisitizo). Paulo alimsihi Timotheo, mchungaji wa kanisa la Efeso hivi, "Hata nitakapokuja, fanya bidii katika kusoma Maandiko hadharani, *na kuhubiri na kufundisha*" (1 Tim. 4:13, maneno mepesi kuonyesha msisitizo). Kuna tofauti gani basi kati ya kuhubiri na kufundisha?

Kihalisia, kuhubiri ni kutangaza Injili mbele ya watu kwa nia ya kuwaita waje kumwamini Kristo. Kufundisha ni kueleza maana ya kuishi kwa ajili ya Kristo. Kuhubiri ni kutangaza; kufundisha ni kufafanua au kutoa maelezo. Kuhubiri ni kutoa tangazo, kufundisha ni kufanya wanafunzi. Mhubiri anawaita watu watangatangao waje kwenye imani katika Kristo; mwalimu anawaeleza njia za Bwana. Kusudi la mwalimu ni kuwaonyesha watu wa Mungu jinsi ya kumtumikia kikamilifu zaidi. Kama mchungaji-mwalimu, lazima uwafafanulie watu wa Mungu Maandiko kwa uangalifu. Ni lazima uwape taarifa na uelewa hitajika ili kutekeleza kwa vitendo neno ambalo wamesikia.

**Kufuata Mfano wa Yesu**

Ukiwa mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitahidi kufuata mfano wa Yesu, mwalimu mkuu kuliko wote, aliyepata kuishi. Yesu mara nyingi alijiita "Mwalimu" (Mt. 26:18; Yoh. 13:13-14). Wengine walifanya vivyo hivyo (kwa mfano, Mt. 8:19; 12:38; Lk. 10:25; Yoh. 11:28). Injili mara nyingi huzungumza

juu ya huduma ya kufundisha ya Yesu (kwa mfano, Mk. 1:21-22; Lk. 4:31-32). Na vifungu virefu vya Maandiko vimetengwa, vyenye mafundisho Yake. Vifungu hivyo ni pamoja na Mahubiri ya Mlimani (Mt. 5-7), Mafundisho ya Mlima wa Mizeituni (Mt. 24-25), na Hotuba aliyoitoa Chumba cha Juu (Yoh. 14-16). Kama Yesu alichukulia huduma Yake ya kufundisha kwa uzito sana, sisi leo pia tunapaswa kuichukulia kwa uzito.

Mengi yangeweza kusemwa kuhusu jinsi Yesu alivyotimiza huduma Yake ya kufundisha. Vitabu vimeandikwa kuhusu njia zake za kufundisha. Mambo matatu kuhusu mtindo Wake wa kufundisha yanastahili kutajwa.

*1. Alifundisha kwa mamlaka*. Biblia inasema hivi juu ya Yesu: “Umati ulishangazwa na mafundisho yake, kwa sababu alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye mamlaka, si kama walimu wa sheria” (Mk. 1:22). Yesu alifundisha kwa mamlaka kwa sababu alikuwa ametumwa na Mungu, na kwa sababu alinena maneno ambayo Mungu alikuwa amempa. Alishuhudia na kusema, “Sifanyi neno kwa nafsi yangu ila nanena yale ambayo Baba amenifundisha” (Yoh. 8:28). Ili kufundisha kwa mamlaka kama Yesu, wewe pia lazima ufundishe Neno la Mungu kwa uaminifu.

*2. Alifundisha kwa upendo*. Yesu aliwapenda sana wale aliowafundisha. Ukweli ni kwamba mafundisho yake yalikuwa upendo Wake kwa watu. Wakati mmoja Yesu alikutana na umati mkubwa wa watu waliochoka na wenye njaa. Alipowaona, “akawahurumia, kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji.” Kisha, kwa upendo wake mkuu kwao, “akaanza kuwafundisha mambo mengi” (Mk. 6:34). Baadaye angewalisha chakula cha kimwili (mst. 35-44). Lakini kwanza, alihudumia mahitaji yao makuu zaidi kwa kuwalisha Neno la Mungu.

Wakati mwingine, Yesu alikutana na wanafunzi wake katika chumba cha juu. Biblia inasema, “Yesu alijua kwamba saa imefika ya yeye kuondoka katika ulimwengu huu na kwenda kwa Baba. Akiwa amewapenda watu wake katika ulimwengu, aliwapenda mpaka mwisho” (Yoh. 13:1). Tena, kwa sababu ya upendo Wake mwingi kwao na kwa wale ambao wao nao wangewaongoza baadaye, aliwafundisha somo lenye nguvu juu ya uongozi wa kitumishi (mst. 2-17).

Katika nyakati hizo zote mbili, upendo wa Yesu kwa watu ulimchochea kuwafundisha. Vivyo hivyo, kama mchungaji wa Kipentekoste lazima uwapende wale ambao umeitwa kuwaongoza. Na upendo huu unapaswa kukusukuma

kuwafundisha Neno la Mungu kwa uaminifu. Bila upendo wa namna hiyo kwa watu wako, maneno yako yanaweza kuwa "shaba iliayo au upatu uvumao" (1 Kor. 13:1).

*3. Alifundisha katika nguvu za Roho.* Yesu aliwahi kuwaeleza wanafunzi wake asili ya huduma Yake ya kufundisha. Alisema hivi: "Maneno niliyowaambia, yamejaa Roho na uzima" (Yoh. 6:63). Maneno ya Yesu yalikuwa yamejaa Roho na uzima kwa sababu Yeye mwenyewe alikuwa amejaa Roho na uzima. Alianza huduma yake kwa kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu (Lk. 3:21-22; 4:18-19). Kisha alitekeleza huduma yake ya kufundisha kwa nguvu za Roho (Lk. 4:14-15).

Yesu alifundisha, si kwa maneno tu, bali pia kwa madhihirisho ya nguvu za Roho (Lk. 5:17). Maneno yake yalikuwa yamejaa nguvu za Roho kiasi kwamba, hata alipokuwa akifundisha, mapepo yalipaza sauti na kusema, "Una nini nasi, Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Nakujua wewe ni nani - Mtakatifu wa Mungu! (Mk. 1:24). Yesu akamtoa yule pepo. Watu wakamaka na kusema, "Ni nini hiki? Mafundisho mapya — na yenye mamlaka! Anaamuru hata pepo wachafu nao wanamtii" (mst. 27).

Yesu aliambukiza huduma yake ya kufundisha kwa wanafunzi wake (Mt. 28:19-20). Kwa kumtazama, walijifunza jinsi ya kufundisha wengine. Kama wachungaji wa Kipentekoste, lazima tufanye vivyo hivyo. Ni lazima tutafute kuiga huduma ya kufundisha ya Yesu.

## MCHUNGAJI KAMA MWALIMU MKUU

Kama mchungaji, unapaswa kujiona kama "mwalimu mkuu" katika kanisa ulilotwa kuliongoza. Yaani, si lazima wewe tu uwe mwalimu stadi wa Neno, lazima ufundishe wengine kwa bidii kufanya vivyo hivyo. Hivi ndivyo Yesu na mitume walivyofanya. Kama mwalimu mkuu, una majukumu matatu ya msingi: (1) lazima ukuze huduma yako ya kufundisha; (2) lazima ukuze stadi za wengine za kufundisha; na (3) lazima uweke mipango ya huduma ya kufundisha kanisani. Hebu tuangalie kila moja ya majukumu haya:

### Kujiendeleza

Kwanza, kama mwalimu mkuu kanisani, jitahidi kuboresha huduma yako ya kufundisha. Paulo alimwandikia Timotheo akisema kwamba mwangalizi, au mchungaji, lazima "aweze kufundisha" (1 Tim. 3:2). Au, kama tafsiri moja inavyosema, mchungaji lazima awe "stadi katika kufundisha." Katika barua yake

kwa Wakristo huko Rumi, Paulo alisema kwamba wale waliopewa karama ya kufundisha lazima watumie karama hii kwa uaminifu (Rum. 12:6-8). Maana yake hapo ni kwamba, wanapaswa kujitahidi kwa bidii kukuza ustadi wao wa kuwa waalimu. Ingawa uwezo wa kufundisha hutolewa kama karama ya kiroho, ni lazima ukuzwe na kuendelezwa kwa mafunzo. Ukiwa mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe mwanafunzi wa Neno la Mungu maisha yako yote. Na lazima ufanye bidii kukuza ustadi wako wa kufundisha (2 Tim. 2:15).

Kuna mtu aliyeona kwamba kufundisha ni zaidi ya kuzungumza, na kujifunza ni zaidi ya kusikiliza. Lengo kuu la kufundisha ni kuleta mabadiliko katika maisha ya wanafunzi. Hivyo, ufundishaji wenye matokeo unahusisha matumizi ya mara kwa mara ya kweli zinazofundishwa. Kwa kutambua hili, hatupaswi kamwe kuridhika na kujua kwamba wanafunzi wetu wamesikia tu maneno yetu. Tunapaswa kuridhika tu tunapoona maisha yao yakibadilishwa. Kwa hiyo, hatupaswi kueleza maana ya Neno la Mungu tu, bali tunapaswa kuwasaidia waamini kutumia kweli za Maandiko katika maisha yao.

Zaidi ya hayo, kama wachungaji wa Kipentekoste, lazima tuelewe kwamba mara nyingi tunafundisha zaidi kwa matendo yetu kuliko tunavyofanya kwa maneno yetu. Paulo alielewa ukweli huu. Hivyo aliwatia moyo Wakristo wa Korintho kwa kuwaambia, "Fuateni mfano wangu, kama mimi ninavyoufuata mfano wa Kristo" (1 Kor. 11:1). Yesu alikuwa akitumia kanuni hiyohiyo alipowaambia wanafunzi wake, "Mwanafunzi hawi juu ya mwalimu, bali kila aliyefundishwa atafanana na mwalimu wake" (Lk. 6:40). Kwa hiyo, kama mifano kwa kanisa, ni lazima tutie katika vitendo yale tunayowafundisha wengine.

### Kuendeleza Wengine

Pili, kama mwalimu mkuu kanisani, lazima ufanye kazi kukuza ufundi wa kufundisha wa viongozi wengine wa kanisa. Kadiri kanisa linavyokua na kukomaa, viongozi watahitajika kuongoza huduma zinazoibuka. Ili kuongoza vizuri, kila mmoja atahitaji kukuza ustadi fulani wa kimsingi wa kufundisha. Lazima uhakikishe kwamba kila kiongozi mpya anapata mafunzo anayohitaji ili kuongoza vyema.

Katika kufanya hivi, lazima uwafundishe viongozi walei jinsi ya kusoma na kutafsiri Biblia kwa usahihi. Na lazima uwaonyeshe jinsi ya kutayarisha na kufundisha Neno la Mungu kwa wengine. Ukifanya mambo hayo, daima kanisa litakuwa na akiba ya waalimu wenye uwezo. Ukishindwa kuwafundisha viongozi

walei jinsi ya kufundisha, huduma ya uanafunzi kanisani itayumba na maendeleo ya kiroho ya Wakristo yata-athirika.

## KULIPANGA KANISA ILI KUFUNDISHA

Hatimaye, kama mwalimu mkuu, lazima uwe mtetezi mkuu wa elimu ya Kikristo. Lazima upange kwa uangalifu na kukuza huduma za mafundisho ya kanisa kwa uangalifu. Tena, ni vizuri uhakikishe kwamba huduma za kufundisha za kanisa zinahusisha kila mtu wa kila umri katika kusanyiko. Mipango na ratiba za mafunzo katika kanisa zinapaswa kuwa pamoja na zifuatazo:

### Shule ya Jumapili

Hakuna mpango wa mafunzo katika kanisa wenye uwezo mkubwa kuliko Shule ya Jumapili. Shule ya Jumapili ndiyo huduma pekee katika kanisa inayomfikia kila mtu wa kila umri katika kusanyiko. Kwa hiyo ni lazima ufanye kazi kuhakikisha kwamba kanisa unaloongoza lina Shule ya Jumapili iliyopangiliwa vizuri na yenye kuungwa mkono kiasi cha kutosha. Tena hakikisha kwamba Idara ya Shule ya Jumapili inaongozwa na mtu anayestahili. Kwa sababu ya umuhimu mkubwa wa huduma hii, unapaswa kushiriki kikamilifu katika hii shule. Na lazima ufuatilie shughuli zake kila wakati na ujitahidi kuboresha ufanisi wake.[1]

### Seli, Mikusanyiko ya Nyumba kwa Nyumba au Ushemasi

Seli au vikundi vya nyumba kwa nyumba au shemasi ni njia nyingine nzuri ya mafunzo ya watu kuwa wanafunzi. Vikundi hivi hukutana kila wiki katika nyumba za washirika wa kanisa waliochaguliwa kwa ajili ya ushirika, maombi, na kujifunza Biblia. Kama mwalimu mkuu, lazima uhakikishe kwamba kila kikundi cha nyumbani kinaongozwa na kiongozi mwaminifu, aliyefundishwa vizuri. Muda unapaswa kupangwa katika kila mkutano wa vikundi vidogo kwa ajili ya majadiliano ya wazi juu ya mada iliyochaguliwa ya kibiblia. Wewe au mtu uliyemkabidhi jukumu, anapaswa kufuatilia kwa karibu kile kinachofundishwa

---

[1] Mfululizo wa Africa's Hope ujulikanao kama *Living the Truth* ni mtaala wa Shule ya Jumapili ya watu wazima unaowapitisha wanafunzi katika Biblia nzima katika muda wa miaka saba. Unapatikana bure kwa ajili ya kupakuliwa kwenye tovuti ya https://africaatts.org/resources/.

katika kila kikundi kidogo. Unaweza kutaka kuandaa masomo rasmi kwa ajili ya kufundishwa katika vikundi.[2]

**Huduma za Idara**

Huduma za idara kanisani zinapaswa kutazamwa kama njia za mafunzo ya uanafunzi. Idara hizo ni pamoja na Ushirika Wa Wanaume, Ushirika Wa Wanawake, Ushirika Wa Vijana, Huduma Kwa Watoto na nyinginezo. Masomo ya Biblia yanayofaa yanatakiwa kufundishwa kila wakati ambapo kimoja katika vikundi hivi kinakutana.

**Shule ya Huduma**

Kila mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kufikiria kuanzisha Shule ya Huduma katika kanisa lake. Shule ya Huduma ni shule inayolenga "kuwatayarisha watakatifu kwa ajili ya kazi za huduma" (Efe. 4:12). Kusudi lake ni kuwafundisha wafanyakazi kwa ajili ya huduma katika kanisa la mahali pamoja. Katika shule hii, mchungaji hufundisha masomo yanayohusu mambo ya kimatendo zaidi kama vile kuhubiri, kufundisha, maombi, kuleta watu kwa Yesu, jinsi ya kupanda kanisa, stadi za uongozi, na zaidi. Mafunzo hayo yatasaidia kuhakikisha kwamba kanisa linakuwa na akiba ya kuaminika ya watenda kazi waliofuzu.

Kanisa linapokua na kufanikiwa, unaweza kuhitaji kukasimu sehemu ya majukumu yako ya kufundisha kwa wengine. Lakini kama mwalimu mkuu wa kanisa, ni vizuri kila mara uendelee kushiriki kikamilifu katika mafundisho ya kanisa na huduma za kufanya watu kuwa wanafunzi.

---

Yesu alimwuliza Petro mara tatu, "Simoni, mwana wa Yohana, wanipenda?" Na Petro akajibu mara tatu, "Naam, Bwana, unajua kwamba nakupenda." Kila mara Yesu alijibu, "Lisha wana-kondoo wangu," au "Lisha kondoo wangu." (Yoh. 21:15-18). Kama Petro alimpenda Yesu kwelikweli, angefanya yale ambayo Bwana wake alikuwa amemwamuru na kulilisha kundi la Mungu kwa uaminifu.

Leo, Yesu anawauliza wachungaji wa Kipentekoste kote barani Afrika swali lile lile: "Je, wanipenda?" Naye anatoa amri ile ile aliyompa Petro: "Lisha kondoo

---

[2] Mfululizo wa Africa's Hope wa masomo yajulikanayho kama *Roots of Faith* ni mtaala wa mada za kujifunza Biblia unaopatikana katika tovuti ya https://africaatts.org/resources/. Unaweza kupakuliwa bila malipo.

wangu." Kama uthibitisho wa upendo wao, Yesu anawaamuru wachungaji hao kuchukulia kwa uzito jukumu lao walilopewa na Mungu la kutunza watu wa Mungu kwa kuwafundisha Neno la Mungu kwa uaminifu.

~ Sura ya 18 ~

# Kuliongoza Kanisa Katika Kuabudu

Katika nchi moja ya Afrika ya Kati, mwanafunzi kijana alipangiwa kutumika chini ya kasisi mzee. Mchungaji alimwomba mwanafunzi huyo aliongoze kanisa katika ibada Jumapili iliyofuata asubuhi. Lakini huyo kijana hakufurahi. Alitamani huyo mchungaji mzee amtake kuhubiri. Alijisikia kwamba kuongoza ibada kulikuwa chini ya hadhi yake kama mchungaji. Tena, kwa sababu alikuwa amejazwa na Roho katika shule ya Biblia, hakuona haja ya kusali au kujiandaa vyovyote vile kwa ajili hiyo.

Kama ilivyotarajiwa, chini ya uongozi wake Jumapili asubuhi, ibada haikuenda vizuri. Kama yule mchungaji mzee asingeingilia kati kwa ustadi na ujuzi wake, ibada ile ingekuwa janga. Tangu wakati huo, mchungaji amekuwa akichagua viongozi wake wa ibada kwa uangalifu sana. Sasa anaruhusu watu wakomavu tu, waliozoezwa vizuri kuhudumu wakiwa viongozi wa ibada.

Kuongoza kanisa katika ibada ya kweli ni kazi ya kiroho sana. Inahitaji ujuzi, maandalizi, na usikivu wa kiroho. Mfalme Daudi alielewa hili. Hivyo alihitaji wale walio-ongoza watu katika sifa na ibada wachaguliwe kutoka miongoni mwa Walawi tu (taz. 1 Nya. 15:16). Ingawa mchungaji anaweza kuchagua wengine

kuongoza kanisa katika ibada, hawezi kamwe kuachilia wajibu wake ili kuhakikisha kwamba kanisa linafanya ibada ya kiBiblia, inayo-ongozwa na Roho.

## KIINI CHA IBADA YA KWELI

Katika Biblia, maneno ya Kiebrania na Kiyunani yanayozungumzia kuabudu yana maana ya kusujudu na kutoa heshima kwa Mungu. Yanatoa wazo la kuonyesha shukrani Kwake kwa unyenyekevu, na kumwinua kwa ajili ya utakatifu, utukufu, na uwezo Wake (Isa. 6:1-3; Uf. 7:11-12).

### Kuabudu Katika Roho na Kweli

Yesu alidhihirisha kiini cha ibada ya kweli alipomwambia mwanamke Msamaria hivi, "Wakati unakuja, na tayari upo, ambapo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na kweli, kwa maana hao ndio waabuduji Baba anaowatafuta. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli" (Yoh. 4:23-24). Katika mistari hii, Yesu alifunua kweli nne muhimu kuhusu ibada ya kweli.

1. Mungu ni Roho. Kwa kuwa ni roho, Mungu hazuiliwi na wakati au mahali. Basi anaweza kuabudiwa wakati wowote na mahali popote.
2. Mungu anatafuta waabuduji wa kweli. Anatafuta watu ambao watamsujudia kutoka ndani kabisa ya mioyo yao kuliko kwa nje na kwa mazoea na desturi (taz. Mk. 12:33).
3. Ibada ya kweli lazima ifanywe katika Roho na kweli. Kwa kuwa Mungu ni Roho, wale wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho. Kwa kuwa Yeye ni kweli kabisa, lazima wamwabudu kulingana na ukweli kama ulivyofunuliwa katika Maandiko.
4. Wakati ni sasa. Wakati wa kumwabudu Mungu katika Roho na kweli ni sasa.

Ibada ni tendo takatifu la kuitikia ipasavyo uwepo wa Mungu, kama walivyofanya wazee ishirini na wanne katika Ufunuo 4. Wakistaajabishwa na kuwapo kwa Kristo, "wanaanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na kumwabudu" (mst. 10). Watu wa Mungu wanapoabudu, Yeye hudhihirisha uwepo Wake zaidi katikati yao, akiwachochea kumwabudu hata zaidi.

### Matarajio ya Kipentekoste

Kama mchungaji wa Kipentekoste, ni muhimu uelewe asili ya kipekee ya ibada ya Kipentekoste. Ibada ya Kipentekoste ni ya kipekee kwa kuwa inasisitiza kukutana kibinafsi na Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Kwa hiyo

Wapentekoste wanaingia katika ibada wakiwa na matarajio tofauti kuliko wengi wasio Wapentekoste. Watu wengi wasio Wapentekoste huingia kwenye ibada wakiwa na lengo la kutimiza wajibu wa kidini au kutekeleza taratibu mbalimbali za kidini. Lakini Mpentekoste wa kweli anaingia katika ibada akiwa na lengo tofauti. Kusudi lake ni kukutana na Kristo aliye hai, na kama matokeo ya tukio hilo, kubadilishwa na Roho wa Mungu (2 Kor. 3:17-18).

Mabadiliko haya yanaweza kuwa madogo au makubwa, yasiyokuwa wazi au yenye kuwa wazi sana. Mabadiliko yasiyokuwa wazi yanaweza kuwa kama ifuatavyo: mwamini anapokutana na Kristo katika ibada, anapata nguvu mpya na furaha katika kumtumikia. Mabadiliko yaliyo wazi yanaweza kuwa mwabuduji anakutana na Kristo aliyefufuka na kuponywa kimuujiza au kubatizwa katika Roho Mtakatifu.

Mabadiliko hayo yanakuja kwa njia mbili: kwa Roho na kwa kweli (rej. Yoh. 4:23). Waabuduji wanapomkaribia Mungu, Yeye hudhihirisha uwepo Wake. Wanapokutana na kuitikia kwa imani uwepo dhahiri wa Mungu (kuabudu katika Roho) wanabadilishwa na kuwa mfano wa Kristo (2 Kor. 3:17-18). Zaidi ya hayo, wanapoitikia kwa imani Neno lililotangazwa (kuabudu katika ukweli), wanabadilishwa hata zaidi.

## KULIANDAA KANISA KWA AJILI YA IBADA

Kama mchungaji, ni jukumu lako kuliandaa kanisa kumwabudu Mungu katika kweli. Lazima uhakikishe kwamba watu wanajua jinsi ya kumwabudu katika Roho na kweli. Lazima uhakikishe zaidi kwamba watu wanatenda ibada kama hiyo. Unaweza kukamilisha hili kwa njia tatu.

### Kufundisha Kuhusu Kuabudu

Kwanza, unaweza kufundisha kanisa kile Biblia inachosema kuhusu ibada. Unaweza kufanya hivi kupitia mahubiri, mawaidha, na mfululizo wa mafundisho. Mojawapo ya njia bora zaidi ambayo mchungaji wa Kipentekoste anaweza kuwafundisha watu wake jinsi ya kumwabudu Mungu katika Roho na kweli ni kuwaonyesha. Ni lazima watu wamwone mchungaji wao akimwabudu Mungu kwa bidii. Mchungaji mkomavu wakati fulani aliagiza kikundi cha wachungaji wanafunzi kwa kuwaambia hivi, “Ikiwa utamwabudu Mungu kwa uaminifu, watu wako watakufuata, na wao pia watamsujudia.”

Zaidi ya hayo, ni lazima uwaonyeshe watu jinsi ya kumwabudu Mungu kwa maisha yako. Unaweza kufanya hivi kwa kuishi mtindo wa maisha ya utakatifu na kwa kuwa njia ya baraka za Roho kwa wengine.

**Kwa Kufuatilia Huduma za Ibada**

Pili, katika jukumu lako kama mwangalizi, lazima ufuatilie kwa maombi huduma hiyo ya kuabudu ili kuhakikisha kwamba watu wanaongozwa kumwabudu Mungu kikwelikweli katika Roho na kweli. Tamani kila kitu katika huduma ya kanisa kifanywe "kwa njia ifaayo na ya utaratibu" (1 Kor. 14:40). Yaani hakikisha kwamba ibada inafanywa kwa njia ambayo inamtukuza Mungu kweli na kuwavuta watu karibu na Kristo (1 Kor. 10:31).

**Kwa Kuilea Timu ya Kuabudu**

Njia ya tatu unayoweza kuhakikisha kwamba kanisa linamwabudu Mungu katika Roho na kweli ni kwa kuishauri kwa upendo timu ya sifa na kuabudu ya kanisa. Lazima uwafundishe kwamba jukumu lao ni kuongoza kusanyiko katika kusifu na kuabudu kunako-ongozwa na Roho kweli kweli. Kwa hiyo ni lazima utumie muda pamoja nao, ukiwafundisha jinsi ya kumwabudu Mungu kikweli, na kuwaonyesha jinsi ya kuwaongoza wengine katika ibada ya kweli.

Zaidi ya hayo, lazima uombe mara kwa mara pamoja na wanatimu hiyo, ukihakikisha kwamba wamejazwa na Roho Mtakatifu na kwamba wanajua jinsi ya kufuata mwongozo wa Roho. Unapaswa pia kuhakikisha kwamba timu inachagua nyimbo ambazo ni za kiroho na za kimaandiko. Kama mchungaji, lazima uhifadhi haki ya kuidhinisha mapema nyimbo zote mpya kabla ya kutumika katika ibada yoyote.

Zaidi ya hayo, kama mchungaji wa kanisa lazima ukumbuke kwamba, baada ya Roho mwenyewe, wewe ndiye unayefuata kama kiongozi mkuu wa ibada kanisani. Hii haimaanishi kwamba utasimama mbele ya kusanyiko ukiwaongoza watu katika kusifu na kuabudu. Lakini maana yake ni kwamba lazima uendelee kusimamia huduma wakati wote. Timu ya kuabudu lazima ielewe kwamba wewe kama mchungaji unaweza kuchukua hatua na kusimamia huduma wakati wowote. Hili linapotokea, timu ya kuabudu lazima ikuachie wewe huduma mara moja.

Wakati ibada halisi katika Roho na kweli inapofanyika, baraka zenye nguvu huja kwa kanisa: Mungu hutukuzwa, uwepo wa Roho unadhihirika, na mwili wa Kristo unaimarishwa.

## KULIONGOZA KANISA KATIKA IBADA

Mchungaji wa Kipentekoste ambaye anaelewa kweli hizi atakuwa na shauku ya kuliongoza kanisa lake katika ibada inayoongozwa na Roho. Hii ina maana kwamba, wakati wa ibada, lazima uendelee kuwa makini kusikilliza sauti ya Roho, na lazima uwe mwepesi kufuata maongozi Yake. Kama Musa kule jangwani, ni lazima uwe tayari kuliongoza kanisa liende wakati wingu linaposogea, na kusimama wakati wingu linaposimama (taz. Kut. 40:34-38).

### Kuhimiza Ushiriki

Kama kiongozi wa kiroho kanisani, unapaswa kuhimiza kila mtu anayehudhuria ashiriki kikamilifu katika ibada. Wahimize waonyeshe sifa zao kwa Mungu kwa kuinua mikono yao, kuimba, kupiga kelele, kushuhudia, kupiga makofi, kucheza, kupiga magoti, au kitu kingine chochote kimaandiko ambacho ni kuabudu. Zaidi, unapaswa kuwafundisha watu kwamba wanamwabudu Mungu wanapotoa zaka na sadaka zao. Kwa kufanya hivi, wanamheshimu Mungu kwa mali zao na malimbuko ya mavuno yao (Mithali 3:9).

### Kwa Kuandaa na Kuendeleza Kwaya

Zaidi ya hayo, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuhimiza maendeleo ya kwaya na vikundi vya muziki ili kuhudumu kanisani na huduma za uinjilisti. Kila kikundi au kwaya lazima wakati wote ibaki kuwa inayofaa kwa mchungaji au mhudumu wa muziki. Basi, unapaswa kushirikiana na vikundi vya uimbaji sawa na jinsi unavyofanya kazi na timu ya sifa na kuabudu, ukiwafundisha tofauti kati ya kufanya kwa ajili ya watu na huduma ya kweli katika Roho.

### Kukuza Karama za Kiroho

Kama kiongozi wa kiroho wa kanisa, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuhamasisha matumizi ya karama za kiroho katika ibada. Hili lilikuwa ni jambo la kawaida katika kanisa la Agano Jipya, na linapaswa kuwa jambo la kawaida katika ibada za leo (taz. Mdo. 11:27-28; 13:2).

Paulo alihimiza kanisa la Korintho hivi: "takeni sana karama za Roho" (1 Kor. 14:1). Akaendelea kusema, "Mkutanikapo pamoja, kila mmoja wenu ana wimbo, au neno la mafundisho, na ufunuo, na lugha, au tafsiri ya lugha" (1 Kor. 14:26). Kwa hiyo, kama mchungaji, unapaswa kufundisha kanisa kuhusu karama za kiroho. Na unapaswa kutoa nafasi kwa udhihirisho wake katika ibada za kanisa.

Wakati huo huo, jilinde kinyume cha matumizi mabaya ya karama hizo za kiroho (1 Kor. 14:26-33).[1]

**Nafasi ya Muziki**

Muziki na uimbaji huwa na nafasi muhimu katika ibada. Mtunga Zaburi anawahimiza watu wa Mungu, "Mwimbieni Bwana kwa furaha, enyi wenye haki; ni vizuri wanyofu kumsifu. Msifuni Bwana kwa kinubi; mpigieni muziki kwa kinubi chenye nyuzi kumi. Mwimbieni wimbo mpya; cheza kwa ustadi, pigeni kelele za furaha" (Zab. 33:1-3).

Kwa mujibu wa Paulo, muziki na uimbaji hufanya kazi kama nne katika ibada: kumtukuza Mungu, kumshukuru, kufundisha ukweli wa maandiko, na kuwaonya waamini kumwishia Yeye. Mtume alikazia yale mawili ya kwanza katika barua yake kwa kanisa la Efeso, kama ifuatavyo: "Mwimbieni Bwana kutoka moyoni mwenu, mkimshukuru Mungu Baba sikuzote kwa kila jambo" (Efe. 5:19-20). Alikazia yale mawili ya pili katika barua yake kwa Wakolosai, kama ifuatavyo: "Mfundishane na kuonyana kwa hekima yote kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi zitokazo kwa Roho" (Kol. 3:16).

**Onyo Muhimu**

Onyo muhimu linafaa hapa. Watu mara nyingi huvutiwa na makanisa ya Kipentekoste kwa sababu ya uimbaji wao uliochangamka. Hii ni nzuri, na unapaswa kuhimiza hilo. Lakini pia, usiruhusu kamwe kanisa lipeleke "moto wa kigeni" mbele za Bwana (Law. 10:1). Yaani, hakikisha kwamba kuimba na kucheza havifanyiki maonyesho ya kimwili badala ya mwitikio wa mioyo iliyotakaswa kwa Roho wa Mungu. Kwa hiyo, wewe kama mchungaji hupaswi kamwe kuruhusu muziki uwe wa sauti kubwa na wenye msukosuko kiasi cha kufunika ibada ya kweli itokayo moyoni. Kumbuka huu ushauri wa Paulo: "Mtu yeyote asijisifu mbele za Mungu" (1 Kor. 1:29, tafsiri halisi). Mungu kamwe asije kusema kuhusu kanisa lenu, "Ondoeni kelele za nyimbo zenu! Sitasikiliza sauti ya vinubi vyenu" (Amosi 5:23).

## CHANGAMOTO MBILI KATIKA KUABUDU

Afrika ni bara kubwa lenye kujumuisha zaidi ya makabila elfu 3 (3,000) yenye kuzungumza zaidi ya lugha elfu 2 na mia moja (2,100). Kwa hiyo, si jambo la

[1] Tazama Nyongeza ya 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

ajabu kwa kusanyiko la Kipentekoste barani Afrika kuwa na watu kutoka makabila mbalimbali. Isitoshe, kila kusanyiko lina vikundi vya umri mbalimbali. Hizi tofauti huonekana kwa mikazo tofauti katika uimbaji, muziki na mitindo ya kuabudu. Pasipo matumizi ya hekima, hali hiyo inaweza kuwa chanzo cha machafuko katika mikusanyiko. Badala ya kukuza umoja kanisani, ibada za kanisa zinaweza kuwa chanzo cha mgawanyiko.

Changamoto mbili zinazotokana na utofauti huu ni kutoelewana kuhusu mitindo ya kuabudu na changamoto ya kutumia lugha nyingi katika ibada. Kama mchungaji, lazima ushughulikie kwa hekima kila moja ya changamoto hizi.

**Mitindo ya Muziki na Jinsi ya Kuabudu**

Makanisa mengi ya Kipentekoste barani Afrika huwaingiza washirika katika hali ya kutoelewana kuhusu mitindo ya muziki na jinsi ya kuabudu. Kwa mfano, vijana wa kanisa wanaweza kupendelea mtindo wa kuabudu wenye sauti kubwa, wa vitendo zaidi, huku washirika wazee wakipendelea mtindo tulivu, uliotulia zaidi. Mmoja anapendelea nyimbo za kisasa huku mwingine akipendelea nyimbo za kitamaduni. Kama mchungaji, lazima utumie hekima kuu katika kushughulikia suala hili. Na lazima uweze kutofautisha kati ya mtindo na uhalisia katika ibada.

Mtindo unahusu matakwa ya mtu binafsi kuhusu aina za nje za ibada; uhalisia huzungumza juu ya ukweli wake wa ndani. Kuabudu ni kumwabudu Mungu kwa moyo wote (taz. Mk. 7:6-7). Ukweli ni kwamba Mkristo anaweza kumwabudu Mungu kihalisia kwa kutumia mitindo mbalimbali. Aina ya mtindo anaotumia mtu kuabudu si kitu, ikiwa kuabudu kunafanyika katika Roho na katika kweli. Mungu huukubali. Kama ibada haijafanywa katika Roho na kweli, inakataliwa. Basi, wafundishe watu kuheshimu anachopenda mtu mwingine katika ibada. Unapaswa "kujitahidi kufanya mambo yanayosababisha amani na kujengana" (Rum. 14:19).

Mchungaji mwenye hekima atawafundisha washirika wazee kushangilia wanapoona vijana wakimwabudu Mungu kwa namna inayoweka wazi mioyo yao kwa Mungu na kuwasogeza karibu naye. Kwa sababu ya kuwapenda vijana, wote wanapaswa kuwa tayari kujiunga nao katika ibada yao kwa Mungu. Vivyo hivyo, lazima kuwafundisha vijana kuheshimu mahitaji na vinavyopendwa na kutakiwa na wazee wao, na kuungana nao kwa moyo wote katika ibada yao. Pia utahitaji kuwafundisha vijana kupenda na kuthamini nyimbo za kale katika imani, ambazo ni nzuri na zenye kuheshimika mno.

Mchungaji wa Kipentekoste mwenye busara atahakikisha kwamba ibada za kanisa zina mchanganyiko wa nyimbo mpya na za zamani, za kisasa, za kienyeji, na za kitamaduni. Atakumbuka kwamba jambo la maana ni kila mwamini akutane na Roho wa Mungu katika ibada na waonyeshe kwa unyofu kujitoa kwao kwa udhati kwa Kristo.

**Lugha Mbalimbali**

Kama ilivyotajwa hapo juu, makanisa mengi ya Kipentekoste katika bara la Afrika yanahudhuriwa na watu wanaozungumza lugha tofauti. Suala hili linaleta changamoto kubwa kwa mchungaji wa Kipentekoste. Kanisa likichagua kuendesha ibada zake katika lugha kuu ya mahali hapo - huku likipuuza zingine zote - kuna hatari ya kuwatenga watu kutoka lugha zingine. Lakini kama linatumia lugha nyingi katika ibada, kanisa linaelekea kwenye hatari ya kuleta kutoridhika miongoni mwa waamini wa kawaida. Kwa hiyo lazima kusimamia hali hii kwa hekima. Lazima uhakikishe kwamba huduma za ibada za kanisa zinavutia watu wa utamaduni katika eneo uliopo, na wakati huo huo, kuwavuta na kuwafanya wengine kutoka utamaduni mwingine wajisikie kukaribishwa.

Utahitaji kumtafuta Mungu na hekima yake katika kushughulikia suala hili. Wewe na timu yako ya uongozi mtahitaji kushughulikia masuala kama haya yafuatayo, kwa maombi sana:

- Ni lugha gani kuu itakayotumiwa katika ibada kanisani?
- Lugha gani nyingine zitatumika? Lugha hizi zitatumika lini na katika mazingira gani?
- Matangazo, maombi ya watu wote na mahubiri yatatafsiriwa katika lugha gani?
- Lugha gani zitatumika katika kuimba? Lugha hizi zitatumika wakati gani na vipi?
- Ni makundi gani ya lugha katika kanisa yanapuuzwa kwa sasa? Tunaweza kuwasaidiaje wajisikie kwamba wamejumuishwa?

Ingawa kila kusanyiko litalazimika kutafuta njia yake kushughulikia suala hili, kanuni fulani zinatumika. Kwa mfano, katika kupanga ibada, unapaswa kutamani kuhakikisha kwamba kila mtu anayehudhuria ibada anajisikia kukaribishwa na kuhusishwa. Lengo lingine ni kwamba wote wanaohudhuria wapate kujengwa. Kwa kuongezea, huduma za ibada zinapaswa kuwa na umoja badala ya kugawanya mkutano. Kuzingatia kanuni hizi kutasaidia kuhakikisha kwamba maamuzi sahihi yanafanywa.

Baadhi ya makanisa ya mijini, kama yanayoitwa ya kimataifa, yatataka kuendesha huduma zao katika lugha ya Kizungu inayotumika katika nchi husika. Makanisa mengine yatataka kutumia lugha ya Kiafrika inayotumika katika hiyo kanda. Baadhi watataka kutafsiri ibada nzima. Wengine watatafsiri mahubiri tu. Bado wengine wanaweza kutaka kutekeleza huduma mbalimbali huku kila huduma ikiendeshwa katika lugha tofauti. Vyovyote kanisa lako litakavyoamua kufanya, lengo lako lazima liwe kuhakikisha kwamba kila mtu anayehudhuria ibada anajisikia kuheshimiwa na kuhusishwa.

---

Jukumu la msingi la kila mchungaji wa Kipentekoste ni kuliongoza kanisa lake katika ibada ya kweli, yenye kuvuviwa na Roho. Anaweza kufanya hivi kwa kuwafundisha watu maana ya kumwabudu Mungu kweli katika Roho na kweli, na kwa kuiga maisha yake mwenyewe jinsi maisha ya kweli ya kuabudu yanavyoonekana.

~ Sura ya 19 ~

# Kuliongoza Kanisa Katika Uamsho wa Kipentekoste

Mtu fulani alieleza kumwagwa kwa Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste kuwa uamsho wa kwanza wa Kanisa. Siku hiyo ndipo Mungu alipomwaga Roho Wake kwa mara ya kwanza juu ya Kanisa, akilijaza uhai na kulitia nguvu ili litimize utume Wake duniani. Harakati za Kipentekoste za kisasa zinapata jina na utambulisho wake kutokana na kile kilichotokea siku hiyo.

Kuwa Mpentekoste maana yake ni mtu anayeshikilia uzoefu na madhumuni ya Pentekoste. Uzoefu wa Pentekoste ni uzoefu wa kiroho wenye nguvu ambao Biblia inaeleza kama ubatizo, au kuzamishwa, katika Roho Mtakatifu (Lk. 3:16; Mdo. 1:5). Kusudi la Pentekoste ni kutiwa nguvu kwa ushuhuda nyumbani na hata miisho ya dunia (Mdo. 1:8).

Tofauti na makanisa yasiyo ya Kipentekoste, kanisa la Kipentekoste haliwezi kusimama kwenye kusudi lake na wito bila umwagiko wa Roho Mtakatifu mara kwa mara. Kama ambavyo mwili hufa ukiacha kupumua, kanisa la Kipentekoste litakufa likiacha kupumua katika Roho wa Mungu. Yaani, ili liwe la Kipentekoste kweli lazima kanisa lipate uamsho wa Kipentekoste. Yesu alieleza hivi, “Roho hutia uzima; mwili haufai kitu” (Yoh. 6:63). Sura hii itatazama jinsi ambavyo

wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unavyoweza kuliongoza kanisa lako kwenye uamsho wa aina hiyo.

## FAHAMU UAMSHO

Kabla ya mchungaji wa Kipentekoste kuliongoza kanisa lake kwenye uamsho, ni lazima ajue vizuri uamsho wa Agano Jipya unavyoonekana. Lakini kwa bahati mbaya, wachungaji wengi wa Kipentekoste wana mawazo potofu kuhusu uamsho. Wazo walilo nalo kuhusu uamsho halitokani na Maandiko, bali hutoka katika utamaduni na desturi za kanisa. Matokeo yake ni kwamba, wanaona uamsho kuwa ni kanisa lililojaa watu wanaoimba kwa furaha, wakicheza na kumsifu Mungu. Au wanauona uamsho kama tendo la Mungu akimimina baraka za kimwili na ustawi juu ya watu wake. Ingawa baadhi ya vipengele hivi vinaweza kuendana na uamsho, havielezi uamsho wa kweli kama unavyo-onyeshwa katika kitabu cha Matendo.

Ingawa neno uamsho halipatikani katika Agano Jipya, dhana ya kufanywa upya kiroho inapatikana (taz. Mdo. 3:19). Uamsho unahusu maisha mapya na humaanisha kurejeshewa ufahamu, hamasa, na nguvu. Kinachoitwa uamsho na Agano la Kale (Zab. 85:6; Hab. 3:2) kinaelezwa na Agano Jipya kuwa ni kumwagwa kwa Roho (Mdo. 2:17-18). Katika sura mbili za kwanza za Matendo, Biblia inabainisha mambo matatu muhimu ya uamsho wa Agano Jipya:

- Kwanza, watu wa Mungu wanabatizwa, na hivyo kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu (Mdo. 1:8; 2:1-4).
- Kisha, watu wa Mungu wanaanza kumtangaza Kristo kwa ujasiri kwa wasiomjua, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Mdo. 2:14-40; 4:31).
- Hatimaye, watu waliopotea wanatubu, wanamwamini Kristo, na kuokolewa (Mdo. 2:41, 47; 5:12-16).

Matokeo mengine ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kama ilivyoelezwa katika kitabu cha Matendo ni uponyaji wa kimiujiza, ishara, na maajabu (Mdo. 2:43; 5:12-16). Maajabu haya mara nyingi husababisha furaha kuu, mikusanyiko iliyo hai ya kanisa, na ukuaji wa kanisa. Pia, vipengele vitatu muhimu vinasalia kama kiini cha uamsho wa kweli wa Kipentekoste, ambavyo ni: uwezeshaji kiroho, ushuhuda wenye nguvu, na watu wanaokuja kwa Kristo. Kama kimoja katika hivyo vipengele vitatu hakipo, uamsho wa kweli wa Kipentekoste haujatokea.

## MFANO WA KIBIBLIA

Hebu tupanue kidogo ufafanuzi wetu wa uamsho kwa kuangalia kwa karibu zaidi kile kilichotokea Siku ya Pentekoste. Uchunguzi makini wa Matendo 2 unaonyesha mambo saba muhimu ya uamsho halisi wa Agano Jipya.

### Watu Humtafuta Mungu

Jambo la kwanza muhimu la uamsho halisi wa Agano Jipya ni kwamba watu wa Mungu watafute uso wake katika maombi. Biblia inatuambia kwamba, kabla ya kumwagwa kwa Roho siku ya Pentekoste, wanafunzi 120 "walidumu sikuzote katika hekalu, wakimsifu Mungu" (Lk. 24:53). Pia inasema kwamba "wote walikusanyika pamoja bila kukosa" (Mdo. 1:14). Kitabu cha Matendo mara kwa mara huunganisha maombi na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Maana yake ni wazi: Ikiwa kanisa linataka kupata uamsho wa Kipentekoste, washirika lazima wamtafute Mungu kwa bidii katika maombi.

### Mungu Humwaga Roho Wake

Kipengele cha pili cha uamsho wa Agano Jipya ni kumwagwa kwa Roho wa Mungu. Siku ya Pentekoste, kwa kujibu maombi ya watu wake, Mungu kwa neema alimimina Roho wake juu ya Kanisa. Ilifanyika hivi:

"Ilipofika siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Ghafla, sauti kama ya upepo mkali ilitoka mbinguni, ikaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Wakaona kama ndimi za moto zilizogawanyika na kutua juu ya kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowawezesha" (Mdo. 2:1-4).

### Waamini Humpokea Roho

Kipengele cha tatu cha uamsho wa Agano Jipya ni kwamba waamini hujazwa na Roho Mtakatifu. Ni jambo moja kwa Mungu kumwaga Roho wake; ni jambo lingine kabisa kwa watu wake kumpokea Roho. Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu hakuja tu juu ya kila mmoja wao, bali "wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine kama Roho alivyowawezesha" (Mdo. 2:4). Wanafunzi walibatizwa kwa Roho Mtakatifu kama Yesu alivyoahidi (Mdo. 1:4-5). Wakati huo, walipokea uwezo wa kuwa mashahidi wa Kristo nyumbani na hata miisho ya dunia (Mdo. 1:8). Watu wa Mungu wakipokea Roho huashiria mwanzo wa uamsho wa kweli wa Kipentekoste.

**Watu wa Nje Huona Yanayotokea**

Jambo la nne la uamsho katika Agano Jipya ni kwamba watu wa nje watambue kile ambacho Mungu anafanya kati ya watu wake. Siku ya Pentekoste, wale walioshuhudia kuja kwa Roho juu ya wanafunzi na kusikiliza walipokuwa wakizungumza katika lugha ambazo hawajajifunza "walishangaa na kufadhaika." Wakaanza kuulizana, "Hii ina maana gani?" (Mdo. 2:12).

**Injili Hutangazwa**

Kipengele cha tano cha uamsho halisi wa Agano Jipya ni injili kutangazwa kwa ujasiri, kwa uvuvio wa Roho. Hiki ndicho kilichotokea siku ya Pentekoste. Baada ya Petro kujazwa na Roho Mtakatifu, alisimama na kutangaza injili kwa ujasiri kwa umati uliokusanyika. Aliwaambia habari za Yesu na akawaita kutubu na kuamini (Mdo. 2:14-40). Wote waliojazwa na Roho waliungana na Petro kumshuhudia Kristo (mst. 47).

**Watu Wengi Huokolewa**

Kipengele cha sita cha uamsho wa Agano Jipya ni kwamba wengi hupokea injili na kuokolewa. Siku ya Pentekoste, kwa sababu ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu na tangazo la Injili lililofanywa na Petro kwa upako, wengi walitubu na kumjia Bwana. Biblia inasema kwamba wasikilizaji 'walichomwa mioyoni' na kumlilia Petro, "Tufanye nini? Petro akajibu, 'Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu. Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu' " (Mdo. 2:37-38). Matokeo yake, watu elfu 3 (3,000) waliokolewa, wakabatizwa kwa maji, na kuongezwa kanisani (mst. 41). Katika siku zilizofuata, "Bwana alizidisha idadi yao kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa" (mst. 47).

**Kanisa Hupanuka**

Kipengele cha saba cha uamsho wa Agano Jipya ni kupanuka kwa kanisa. Kufuatia Pentekoste na kumiminiwa kwingine kwa Roho katika kitabu chote cha Matendo, kanisa liliendelea kukua kiidadi na kupanuka kijiografia (taz. Mdo. 2:47; 4:31-35; 5:12-16; 9:31).

Mambo mengine makubwa ya uamsho yaliyofunuliwa katika Matendo 2 ni kujitoa kusoma Maandiko, maombi, na kupendana. Mungu alipofanya maajabu katikati yao, watu waliishi katika utakatifu. Uwepo wa Roho wa Mungu ulizidi

kuumba ndani ya mioyo yao roho ya ukarimu. Mambo haya yote yalisababisha kukua kwa kanisa (Mdo. 2:41, 47; 4:4; 5:14).

Kwa kifupi, uamsho wa kweli wa Kipentekoste hutokea wakati watu wanapoamini ujumbe unaomhusu Yesu, wanapojazwa na Roho, na kisha kwenda kuwashirikisha wengine habari njema. Basi, wale wanaopokea injili huokolewa na kujazwa na Roho Mtakatifu. Kisha, wao wenyewe wanakuwa watangazaji waaminifu wa injili na wenye bidii. Mchakato huu unaporudiwa tena na tena, uamsho unaenea na kufika mbali sana.

## NAFASI YA MCHUNGAJI

Kama mchungaji wa Kipentekoste, wewe ndiye ufunguo wa uamsho katika kanisa lako la mahali pamoja. Unaweza kuwa njia inayowezesha mtiririko wa Roho au bwawa linalozuia mtiririko wake. Chochote unachofanya - au kushindwa kufanya - kinaweza kuamua kama kanisa lako linapitia uamsho au la. Zaidi ya hayo, kama kiongozi wa kiroho wa kanisa, utaamua kwa kiasi kikubwa jinsi kanisa lako linavyoitikia kuja kwa umwagiko wa Roho. Lazima uchukue jukumu hili la ajabu kwa umakini.

Kwa kawaida, uamsho wa Kipentekoste huanza na shauku katika moyo wa mchungaji. Hii shauku ya mtembeo wa Roho itamtia moyo kumtafuta Mungu kwa bidii kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya kanisa. Basi, mchungaji lazima afikishe hamu hii ya uamsho ndani ya mioyo ya watu wa Mungu. Unaweza kufanya hivyo kwa kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu ya hii mada.

Zaidi, unaweza kujenga hamu kama hiyo katika mioyo ya watu wako kwa kuwaongoza katika maombi ya uamsho kwa bidii. Akizungumza juu ya Roho Mtakatifu, Yesu aliwaambia wanafunzi wake hivi, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa mlango” (Lk. 11:9; taz. mst. 13). Tafsiri halisi ya maneno ya Yesu ingesomeka hivi: “Nawaambia, Endeleeni kuomba, nanyi mtapewa. Endeleeni kutafuta, nanyi mtapata. Endeleeni kubisha hodi, na mtafunguliwa mlango.” Maana yake ni wazi: Maadamu tunaendelea kumwomba Roho, tutaendelea kupokea kutoka kwa Mungu. Lakini tukiacha kuomba, tutaacha kupokea. Kwa hiyo moto wa uamsho wa Kipentekoste lazima uchochewe kwa maombi ya kudumu.

Tena wewe kama mchungaji, lazima uwaonyeshe watu wako jinsi ya kuomba kwa imani. Lazima uwaongoze kuamini kwamba, wakimtafuta Mungu kwa uaminifu, atatimiza ahadi yake ya kutuma ufufuo (Mk. 11:24). Utataka kuendelea

kuwakumbusha watu kuhusu tangazo la kinabii la Petro: "Katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamimina Roho yangu juu ya *watu wote*" (Mdo. 2:17, Maneno mepesi kwa msisitizo). Washirika wa kanisa wanapokubali ahadi hii, watatiwa moyo kuamini ahadi ya Yesu kwamba Baba wa Mbinguni "atawapa Roho Mtakatifu wale wamwombao!" (Lk. 11:13).

Kanisa linapofuata uamsho wa Kipentekoste, inabidi wakati huo huo lifuatilie utume wa Kipentekoste. Haya yalikuwa maagizo ya Yesu ya wazi katika Matendo 1:8. Kwanza, aliahidi uamsho: "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu." Wakati huo huo, aliagiza umisheni, hivi: "Nanyi mtakuwa mashahidi wangu… hadi mwisho wa nchi."

Kwa hiyo wewe kama mchungaji, kazi ya kuwaongoza waamini katika ubatizo wa Roho ili kujiandaa kwa ajili ya ushuhuda unaowezeshwa na Roho lazima ibaki kuwa kipaumbele chako kikubwa kimoja. Unapaswa kukumbuka kwamba sababu moja ya msingi ya Mungu kukuweka katika kanisa lako ni ili uweze kuinua wanafunzi wengine waliotiwa nguvu na Roho ambao anaweza kuwatumia kujenga ufalme wake (Efe. 4:11-12).

## KUHIMIZA UAMSHO WA PENTEKOSTE

Wiki chache baada ya umwagiko wa Roho Siku ya Pentekoste huko Yerusalemu, Maandiko yanasimulia juu ya Roho kushuka tena huko Samaria, karibu kilomita 50 (maili 30) kaskazini mwa Yerusalemu (Mdo. 8:1-25). Uamsho huu uliongozwa na Filipo mwinjilisti kwa msaada wa mitume Petro na Yohana. Kwa kutazama matendo ya watu hawa, tunagundua njia saba za kuhimiza uamsho katika kanisa.

### Jazwa Roho

Njia ya kwanza ambayo wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unayoweza kuitumia kuhimiza uamsho katika kanisa lako ni kwa kumtafuta Mungu kwa bidii ili wewe binafsi ujazwe au ujazwe tena na Roho Mtakatifu. Filipo alikuwa mmoja wa wale "mashemasi" saba waliojazwa na Roho katika kanisa la Yerusalemu (Mdo. 6:3-5). Yaelekea alijazwa na Roho siku ya Pentekoste au punde baada ya hapo. Alipofukuzwa mjini kwa sababu ya mateso, alibaki amejaa Roho Mtakatifu. Alipofika Samaria, alihudumu katika nguvu za Roho, akasababisha uamsho mkuu huko.

Yeye pamoja na mitume Petro na Yohana, walioshuka kutoka Yerusalemu kumsaidia (8:14-17), waliweza kuhamasisha uamsho huko Samaria kwa sababu

wao wenyewe walikuwa wamejaa Roho Mtakatifu. Hivyo, uamsho wa Kipentekoste huanza na wewe mchungaji, na viongozi wengine wa kanisa kujazwa au kujazwa tena na Roho Mtakatifu.[1]

**Onyesha Imani Thabiti**

Njia ya pili unayoweza kuhimiza uamsho katika kanisa ni kutumia imani thabiti. Filipo alipofika Samaria, alitenda kwa imani. Matokeo yakawa Mungu kummjalia miujiza ili kuthibitisha ujumbe aliohubiri, na wengi wakavutwa kwenda kwa Bwana (Mdo. 8:5-8).

Kama Filipo, wewe pia utahitaji kuamini kwamba uamsho unawezekana. Lazima uwe na hakika kabisa kwamba Mungu anaweza kufanya yale aliyoahidi (taz. Rum. 4:18-21). Na utahitaji kufuatilia kwa ujasiri ahadi za Mungu ukiwa na uhakika kamili kwamba uamsho unakuja. Ukifanya hivi, imani yako itaambukiza. Washirika wako wanapomwona mchungaji wao akitenda kwa imani ya kijasiri, wao pia watatiwa moyo kumwamini Mungu ili uamsho uje.

**Mtangaze Kristo**

Njia ya tatu ya kuliongoza kanisa lako katika uamsho wa Kipentekoste ni kutangaza injili ya Kristo kwa uaminifu. Biblia inatuambia, "Filipo akashuka mpaka mji mmoja katika Samaria, na huko akamhubiri Kristo" (Mdo. 8:5). Hii lilikuwa kawaida kwa Wakristo katika kitabu chote cha Matendo. Popote walipokwenda, waliwaambia watu juu ya Yesu (fananisha Mdo. 2:22; 3:13; 4:2, 33; 9:22; 16:31). Ikiwa unataka kupata uzoefu wa uamsho halisi wa Agano Jipya katika kanisa lako, lazima ufanye kama Filipo na mitume. Unapaswa kumtangaza Kristo kwa uaminifu mkubwa, kwa wote. Na lazima uwafundishe watu wako kufanya vivyo hivyo.[2]

**Ombea Wagonjwa**

Nne, unaweza kuliongoza kanisa lako kwenye uamsho wa kweli wa Agano Jipya kwa kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka kwa uaminifu, ukimtarajia Mungu kulithibitisha Neno Lake kwa njia isiyo ya kawaida kwa ishara za miujiza. Huko Samaria, "umati ulipomsikia Filipo na kuziona ishara alizozifanya, wote

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu ujuzi wa mchungaji wa Kipentekoste na Roho, tazama Sura ya 1: "Mtu wa Uzoefu."

[2] Kwa habari zaidi kuhusu kuhubiri, tazama Sura ya 16: "Mahubiri Yenye Upako wa Roho."

walisikiliza kwa makini maneno yake" (Mdo. 8:6). Ishara hizi na miujiza zilihusisha ukombozi wenye nguvu na uponyaji wa kimuujiza. Matokeo yake yakawa furaha kuu kuja kwa watu, wengi wakaokolewa, na uamsho ukaingia mjini.[3]

**Kazia Ubatizo wa Roho**

Njia ya tano unayoweza kutumia kuhimiza uamsho wa Kipentekoste katika kanisa lako ni kusisitiza mara kwa mara hitaji la washirika kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Mitume huko Yerusalemu waliposikia kwamba Wasamaria wamepokea injili, mara moja wakawatuma Petro na Yohana ili waombe pamoja nao, wampokee Roho Mtakatifu (Mdo. 8:14-17). Mchungaji yeyote wa Kipentekoste ambaye anataka kanisa lake lipate uamsho wa kweli wa Kipentekoste lazima afanye vivyo hivyo. Ni lazima kufundisha na kuhubiri mara kwa mara juu ya ubatizo wa Roho. Na ni lazima kuomba pamoja na watu wao ili wampokee Roho Mtakatifu. Hii itasaidia kuandaa kanisa kushiriki kikamilifu katika uamsho na kueneza injili kwa waliopotea.[4]

**Ongoza Katika Ushuhudiaji**

Njia ya sita unayoweza kuhimiza uamsho halisi wa Kipentekoste ni kuliongoza kanisa lako katika kuwashuhudia waliopotea. Filipo alizindua uamsho wa Samaria kupitia ushuhuda wa kijasiri uliowezeshwa na Roho kwa watu waliopotea wa Samaria. Kwa kufanya hivi, akawa mfano kwa kanisa. Tunajua Wakristo wapya huko Samaria walifuata mfano wake katika kushuhudia, maana, baada ya muda mfupi, "kanisa lote katika Uyahudi, Galilaya, na Samaria likafurahia wakati wa amani na kuimarishwa. Wakiishi katika kicho cha Bwana na kuhimizwa na Roho Mtakatifu, idadi ikaongezeka" (Mdo. 9:31).

Ikiwa wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unataka uamsho wa kweli wa kiroho katika kanisa lako, utahitaji kufuata mfano wa Filipo. Hupaswi tu

[3] Kwa habari zaidi kuhusu huduma katika nguvu isiyo ya kawaida, tazama kitabu cha Discovery Series kinachoitwa, *Power Ministry: How to Minister in the Spirit's Power*, cha Denzil R. Miller.

[4] Ili kupata habari zaidi juu ya kuomba na waamini ili wampokee Roho, tazama Sura ya 11: "Hukuza Utendaji na Uzoefu wa Kipentekoste" na Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

kuwaambia watu wako washuhudie, lazima uwe kielelezo cha kusudi la kweli la uamsho wa Kipentekoste kwa wewe mwenyewe kuwa mshuhudiaji.[5]

**Dumu Katika Maombi**

Mwisho: unaweza kuliongoza kanisa lako katika uamsho wa Kipentekoste kwa kulionyesha kanisa jinsi ya kuomba, kama tulivyotazama mapema katika sura hii. Wakati mitume Petro na Yohana walipofika Samaria, "waliwaombea waamini wapya huko ili wampokee Roho Mtakatifu" (Mdo. 8:15). Ukitaka kuona uamsho wa kweli wa Kipentekoste ukitokea kanisani kwako, wewe pia lazima uwaongoze watu katika maombi. Na lazima udumu katika maombi hadi jibu lije, ukikumbuka maneno ya Paulo, "Tena tusichoke katika kutenda mema, maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho" (Gal. 6:9)[6]

---

Ili kubaki kuwa shahidi muhimu katika jamii na duniani, kila kanisa la Kipentekoste lazima lipate umwagiko wa Roho Mtakatifu mara kwa mara. Mchungaji wa Kipentekoste lazima aongoze katika jitihada hiyo. Ni lazima awe kielelezo kwa kutafuta uamsho kwa bidii, na kuwafundisha watu kufanya vivyo hivyo. Wanaweza kutiwa moyo na ahadi ya Mungu kwa Yoeli iliyonukuliwa na Petro Siku ya Pentekoste:

> "Siku za mwisho, asema Mungu, nitawamiminia watu wote Roho yangu. Wana wenu na binti zenu watatabiri, vijana wenu wataona maono, wazee wenu wataota ndoto. Hata juu ya watumishi wangu, wanaume kwa wanawake, nitawamiminia Roho yangu siku zile, nao watatabiri." (Mdo. 2:17-18)

---

[5] Kwa maelezo zaidi juu ya kuliongoza kanisa katika uinjilisti unaowezeshwa na Roho, tazama Sura ya 36: "Kuelewa Mkakati wa Agano Jipya" na Sura ya 37: "Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti."

[6] Kwa habari zaidi juu ya kuliongoza kanisa katika maombi, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi."

~ Sura ya 20 ~

# Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho

Yesu alikuwa karibu kurudi mbinguni. Kazi aliyokuwa ameianza angelliachia Kanisa Lake. Katika kujitayarisha kuondoka, aliwakusanya wanafunzi Wake juu ya kilele cha mlima nje ya Yerusalemu. Hapo akawapa amri ya mwisho na ahadi ya mwisho.

Amri yake ilikuwa hii: "Msiondoke Yerusalemu, bali ingojeni zawadi ambayo Baba yangu aliahidi…Kwa maana Yohana alibatiza kwa maji, lakini baada ya siku chache ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu" (Mdo. 1:4-5). Ahadi yake ilikuwa hii: "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na Uyahudi wote, na Samaria, hata mwisho wa nchi" (mst. 8). Katika kutoa maagizo haya, Yesu alikuwa analihamasisha Kanisa Lake changa ili kutimiza utume aliokuwa amewapa.

Vivyo hivyo, kila mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika lazima ahamasishe kanisa lake kushiriki katika utume wa ukombozi wa Kristo. Kama Yesu, lazima wahakikishe kwamba watu wao wamebatizwa katika Roho Mtakatifu na kutiwa nguvu kama mashahidi wa Kristo kwa waliopotea. Hakuna

kanisa lililo tayari kushiriki kikamilifu katika utume wa Mungu hadi viongozi na washiriki wake wapokee uwezo huu ulioahidiwa kutoka juu (Lk. 24:49). Sura hii itashughulikia suala hili muhimu. Itakusaidia kujitayarisha kuwaongoza washirika wako katika ubatizo wa Roho.

## UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NI NINI?

Ubatizo katika Roho Mtakatifu (wakati mwingine hujulikana kama ubatizo wa Roho) ni ujuzi wenye nguvu wa kubadilisha maisha. Ni kukutana na Mungu kwa ndani ambapo Roho wake huja juu ya mfuasi wa Yesu, akiwavisha na kuwajaza uwepo na nguvu zake. Ubatizo katika Roho Mtakatifu ndio ulifanyika kwa wanafunzi 120 siku ya Pentekoste. Biblia inaeleza yaliyotokea kwao kama ifuatavyo:

> "Ilipofika siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Ghafla, sauti kama ya upepo mkali ikatoka mbinguni, ikaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Wakaona kama ndimi za moto zilizogawanyika na kutua juu ya kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowawezesha." (Mdo. 2:1-4)

Fikiri kilichowapata wanafunzi wakati huo. Kwanza, Roho Mtakatifu alikuja juu yao, kama ambavyo Yesu alikuwa ametabiri katika Matendo 1:8. Kisha, Roho aliingia ndani yao, akiwajaza kwa nguvu na uwepo Wake mkuu. Matokeo yake yakawa walianza kunena kwa lugha kama Roho alivyowawezesha. Mwisho, walianza kushuhudia kwa nguvu na kwa mafanikio ya ajabu (Mdo. 2:14-41). Mtindo huu uliendelea katika kitabu chote cha Matendo. Na tunaweza kutarajia mambo kuendelea hivyo hata leo.

Hayo yakiwa mawazoni mwetu, hebu tuthibitishe mambo matatu kuhusu ubatizo wa Roho.

*1. Ni ujuzi wenye nguvu.* Yesu aliuelezea ubatizo wa Roho kuwa ni "kuvikwa uwezo utokao juu" (Lk. 24:49). Aliahidi kwamba, "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu" (Mdo. 1:8). Mtu anapojazwa na Roho, anakutana na nguvu kuu za Mungu.

*2. Ni ahadi kwa waamini wote.* Yesu alisema kwamba Baba wa Mbinguni angemtoa Roho Mtakatifu bure kwa mtoto wake yeyote ambaye angemwomba kwa imani (Lk. 11:13; Mk. 11:24). Katika mahubiri yake ya Pentekoste, Petro alisema hivi kuhusu tukio hilo, "Hii ahadi ni kwa ajili yenu na watoto wenu na

kwa wote walio mbali — kwa wale wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita" (Mdo. 2:39).

*3. Ni agizo toka kwa Mungu.* Yesu aliwaamuru wanafunzi wake, "Msiondoke Yerusalemu, bali ingojeeni zawadi ambayo Baba yangu aliahidi" (Mdo. 1:4). Vivyo hivyo, Paulo aliwaagiza waamini wa Efeso "wajazwe na Roho" (Efe. 5:18). Kwa sababu kila Mkristo ameagizwa kuwa shahidi wa Kristo, kila Mkristo lazima awezeshwe na Roho Mtakatifu (Lk. 24:48-49; Mdo. 1:8; 5:32).

Ubatizo wa Roho humwezesha zaidi Mkristo kuishi maisha yanayompendeza Mungu (Gal. 5:16). Inaongeza uwezo wake wa kuomba (Rum. 8:26-27). Na kwa ubatizo wa Roho huja uwezekano mkubwa zaidi kwa mtu huyo kutumiwa katika madhihirisho ya karama za kiroho (1 Kor. 12:7-10). Zaidi ya hayo, uzoefu huo husababisha usikivu mkubwa zaidi kwa mambo ya Mungu (Yoh. 16:8; 1 Kor. 2:12), uwezekano wa kuelewa zaidi kiroho (Yoh. 3:8; 1 Kor. 2:14), kupokea kwa undani zaidi uwezo wa kumpenda Mungu (Rum. 5:5), na kujitolea zaidi kwa kazi yake (Mdo. 4:20; 5:29). Kila Mkristo anahitaji kubatizwa katika Roho Mtakatifu.

## KUHAMASISHA UBATIZO KATIKA ROHO

Kama hiyo ni kweli, mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste atajibidisha sana kuwatia moyo na kuwaongoza washirika wake kubatizwa katika Roho. Zifuatazo ni mbinu tano unazoweza kutumia kuwatia moyo na kuwasaidia watu wako kubatizwa katika Roho Mtakatifu.

*1. Wasaidie kuelewa.* Kwanza, unaweza kuwatia moyo watu wako wajazwe na Roho kwa kuwasaidia kuelewa asili, kusudi, na umuhimu wa jambo hilo. Unaweza kufanya hivyo kwa kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu ya somo hilo. Waamini wanapokuwa na uelewa zaidi kuhusu Roho Mtakatifu, watakuwa tayari kumwitikia na kujazwa.[1]

*2. Ingiza hamu.* Akizungumzia Roho Mtakatifu, Yesu alisema, "Yeyote aliye na kiu na aje kwangu anywe" (Yoh. 7:37). Katika tukio lingine aliahidi hivi, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa" (Mt. 5:6). Hivyo, kuwa na njaa na kiu ya Mungu ni sharti muhimu kwa ajili ya kupokea Roho Mtakatifu.

---

[1] Kitabu *Kuitangaza Pentekoste: Muhtasari wa Mahubiri 100 juu ya Nguvu za Roho Mtakatifu,* kinaweza kupakuliwa bila malipo kutoka tovuti ya www.DecadeofHarvest.org.

Kwa kujua hili, utataka kuwaingizia watu wako hamu ya kutiwa nguvu na Roho wa Mungu. Njia moja unayoweza kufanya hivi ni kwa kuwasaidia kujua jinsi ambavyo kujazwa na Roho kutabariki maisha yao. Baraka hizi ni pamoja na uwezo wa kushuhudia, kutembea karibu zaidi na Kristo, msaada katika maombi, ushindi juu ya majaribu, na mengi zaidi.

Tena, unaweza kujenga hamu ya Roho katika mioyo ya watu kwa kuwa wazi unapoishi maisha ya kujazwa na Roho mbele yao. Waamini wanapotazama karama za Roho na tunda la Roho vikionyeshwa katika maisha ya mchungaji wao, hamu ya kujazwa na Roho itazaliwa mioyoni mwao.

*3. Hamasisha imani.* Akizungumza kuhusu Roho kwa mara nyingine tena, Yesu alisema, "Yeyote aniaminiye mimi ... kutoka ndani yake itatiririka mito ya maji yaliyo hai" (Yoh. 7:38). Paulo alieleza hivi: “Kwa imani tunapokea ahadi ya Roho” (Gal. 3:14). Kwa kuwa Roho hupokelewa kwa imani, ni wazi kwamba itakuwa vizuri kuwatayarisha watu wako kumpokea Roho kwa kujenga imani yao katika ahadi za Mungu.

Kwa mfano, unaweza kuwakumbusha maneno ya Kristo katika Luka 11. Hapo, Yesu aliahidi, “Nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa.… Kwa maana *kila aombaye hupokea*…” (mst. 9-10; taz. mst. 13, maneno mepesi kusisitiza). Onyesha kwamba kila mtu katika kifungu hiki maana yake ni kila aliye mtoto wa Mungu – ambao ni pamoja na wao. Ahadi nyingine unazoweza kuwashirikisha zinapatikana katika Marko 11:24 na Matendo 2:39. Kwa kuongeza, unaweza kujenga imani ya watu kwa kuwashirikisha shuhuda za wale ambao Mungu amewajaza na Roho na kuwatumia kwa utukufu Wake.

*4. Kuza mazingira.* Njia nyingine muhimu unayoweza kuwasaidia watu wako wajazwe na Roho ni kwa kukuza mazingira yanayofaa katika ibada za kanisa. Ubatizo wa Roho unapokelewa vyema zaidi katika mazingira ambayo imani iko juu na uwepo wa Roho ni wenye nguvu. Imani inaweza kusemwa kuwa ya juu wakati watu wa Mungu wanatazamia kwa hamu sana mtembeo wa Roho. Wanatazamia Mungu kutimiza ahadi zake mara moja. Uwepo wa Roho unaweza kusemwa kuwa wenye nguvu wakati watu wanaona ukaribu wa ajabu wa Mungu. Kama Yakobo, wanaweza kushuhudia na kusema, “Hakika Bwana yuko mahali hapa” (Mwa. 28:16).

Kumbuka, Siku ya Pentekoste Roho Mtakatifu alipajaza mahali hapo kwanza. Kisha akawajaza watu (Mdo. 2:3-4). Kwanza, Uwepo unasikika; ndipo Roho

hupokelewa. Uwepo wa Roho unaweza kukuzwa kupitia maombi ya dhati, utii kwa Neno, ibada ya upako, na uwazi kwa Roho.

*5. Kutoa nafasi*. Mwisho, ikiwa unatarajia kuona washirika wako wakibatizwa katika Roho Mtakatifu, utahitaji kuwapa fursa za mara kwa mara za kupokea. Maombi kwa ajili ya Roho lazima yawe tukio la kawaida katika mikusanyiko ya ibada ya kanisa lako. Zaidi ya hayo, lazima uite watu kufika madhabahuni mara kwa mara na kuwaalika kujazwa na Roho.

Katika kupanga ibada za kanisa lako, lazima uruhusu muda wa kutosha mwishoni mwa ibada kwa ajili ya maombi madhabahuni. Hii inaweza kumaanisha kwamba utahitaji kufupisha ibada na muda wa kuhubiri. Zaidi ya hayo, utataka kuwafundisha watenda kazi wa madhabahuni jinsi ya kuwaongoza wanaotafuta ubatizo wa Roho kuupata. Kwa kuongezea, unaweza kutaka kutenga mikutano kadha wa kadha ya maombi na ya seli za nyumbani ili kuona waamini wakiwezeshwa na Roho.

## KUOMBA PAMOJA NA WAAMINI ILI KUPOKEA

Umetoa mahubiri yako, na waamini wamejiandaa ili wajazwe na Roho. Nini kifuatacho? Unawezaje kuwaongoza kwa ufanisi zaidi watafutaji hawa ili waingie kwenye kubatizwa katika Roho?

Kwanza, ni muhimu kuwa na ufahamu wa mwelekeo wa kiroho unaokaribia kutokea katika maisha ya waamini hawa wanapojazwa na Roho. Kama ilivyokuwa Siku ya Pentekoste, Roho atakuja juu yao kwanza (Mdo. 2:3). Kisha ataingia ndani yao, akiwajaza nguvu na uwepo wake (mst. 4a). Mwishowe, Roho atatiririka kutoka kwao kwa lugha inayotoka na kuongozwa na Roho (mst. 4b). Unapaswa kuangalia mienendo hii ya kiroho kutokea kwa waamini wanapobatizwa katika Roho Mtakatifu.

Unapaswa kukumbuka ukweli kwamba, katika mchakato mzima, watafutaji watahitaji kutenda kwa imani shupavu (Gal. 3:2, 5, 14). Kumbuka, ni imani itakayotayarisha mioyo yao kupokea Roho; ni imani itakayoleta uwepo wake; na ni imani itakayoachilia nguvu za Roho kwa maneno yaliyovuviwa. Tukikumbuka hayo, hebu tuangalie jinsi ambavyo wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unavyoweza kuwaongoza watafutaji kufikia ubatizo wa Roho.

**Hatua Tatu za Imani**

Katika Luka 11:9-13, Yesu anawafundisha wanafunzi wake jinsi wanavyoweza kuomba na kupokea Roho Mtakatifu. Mistari hii, pamoja na yaliyotokea kwa wale 120 siku ya Pentekoste (Mdo. 2:1-4), hutoa hatua tatu katika kumpokea Roho Mtakatifu. Hatua hizi tatu ni kuomba kwa imani, kupokea kwa imani, na kunena kwa imani. Hivi ndivyo unavyoweza kuwaongoza watafutaji kupiga hatua hizi tatu za imani.

*Hatua ya 1: Kuomba kwa imani.* Kwanza, waongoze watafutaji kumwomba Roho. Kumbuka ahadi ya Yesu: "*Ombeni* nanyi mtapewa" (Lk. 11:9, Maneno mepesi kukazia). Pia, mwongoze mwenye dhambi katika maombi ya toba, huku unawahimiza watafutaji kuomba ili kujazwa na Roho Mtakatifu. Waagize kwamba wanapoomba, wanapaswa kuamini kabisa kwamba Mungu anasikia maombi yao na kwamba anatenda ili kujibu maombi yao. Sala inaweza kuwa kama ifuatavyo, na watafutaji kuirudia neno kwa neno:

"Bwana, nimekuja kujazwa na Roho Mtakatifu… Uliahidi kwamba ningepokea nguvu Roho atakapokuja juu yangu… Nahitaji nguvu hiyo niwe shahidi wako… Pia uliahidi kwamba kila aombaye hupokea… ninaomba; kwa hiyo, natazamia kupokea… Nikipokea, nitanena kwa imani… sitaogopa… nitaanza kunena kwa lugha kama Roho Wako atakavyonipa kutamka… Roho Mtakatifu, nishukie sasa."

Mara baada ya kuomba, wahakikishie hao waombaji kwamba Mungu amesikia maombi yao, na kwamba wakati huo yuko tayari kuwajaza na Roho Mtakatifu. Wahimize kuwa makini juu ya ujio wa Roho juu yao. Wawe makini kuhisi uwepo wake. Unaweza kutaka kuchukua muda mfupi kumwabudu Bwana pamoja nao, ukiitikia ujio wa Roho.

*Hatua ya 2: Kupokea kwa imani.* Sasa, waongoze watafutaji kupiga hatua yao ya imani. Yesu alisema, "Kila aombaye *hupokea*" (Lk. 11:10, maneno mepesi kukazia). Yesu anazungumza juu ya kupokea kwa vitendo badala ya kupokea tu. Useme, "Kila aombaye lazima anyooshe mkono kupokea." Yesu alituambia jinsi hili linavyofanyika. Ni kwa tendo la imani. Alisema hivi: "Lolote mtakaloomba katika sala, aminini kwamba mnalipokea, nalo litakuwa lenu" (Mk. 11:24).

Ili kuwaongoza watafutaji katika hatua yao ya imani, waambie kuinua mikono yao juu, na kwa imani ombeni sala hii nyepesi: "Bwana, sasa hivi, katika jina la Yesu, ninampokea Roho Mtakatifu." Maombi haya yatawapa mazingira yaliyo

dhahiri ambapo wanaweza kuachilia imani yao ili kupokea Roho. Wakati huo, wanapaswa "kuamini kwamba wamepokea!" Mara tu wanapoamini, Roho ataingia ndani kwa kasi na kuwajaza. Waambie wajisikie uwepo wa Roho kwa ndani kabisa.

*Hatua ya 3: Kunena kwa imani*. Sasa, wahimize watafutaji kutenda kwa imani na kuanza kusema kwa ujasiri - si kutoka mawazoni mwao, lakini kutoka ndani kabisa, kutoka kwenye kuhisi ndani yao (Yoh. 7:38). Wanapojisalimisha kwa Roho anayetiririka ndani na anayepitia ndani yao, wataanza kunena maneno ambayo hawaelewi (Mdo. 2:4; 10:46; 19:6). Kuzungumza kwao kunaweza kulinganishwa na hatua ya imani ya Petro wakati, katika kutii amri ya Yesu, alitoka kwenye mashua na kuanza kutembea juu ya maji. Hatua yake ya ujasiri ya imani ilisababisha muujiza (Mk 14:28-29). Kwao pia itakuwa hivyo! Wahimize wasiogope bali washirikiane kikamilifu na Roho kwa kuendelea kunena kwa imani.

### Kunena kwa Lugha

Inaweza kusaidia hapa tena kusema kidogo kuhusu kunena kwa lugha, kwa kuwa hili mara nyingi ni jambo jipya na labda geni kwa wale ambao hawajawahi kulipitia. Ni muhimu kuelewa kwamba, mwamini aliyejazwa na Roho anaponena kwa lugha, maneno wanayozungumza hayatoki akilini mwao, kama katika usemi wa kawaida. Maneno yanatoka ndani kabisa, kutoka rohoni mwao. Yesu alisema, "Yeye aniaminiye mimi, kama vile Maandiko yalivyosema, 'Mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake' " (Yoh. 7:38, tafsiri halisi). Paulo alisema, "Yeyote anenaye kwa lugha hasemi na watu bali na Mungu. Hakika, hakuna anaye-elewa kinachosemwa; hutamka mafumbo katika Roho" (1 Kor. 14:2). Wakumbushe watafutaji kwamba kuzungumza kwao hakutakuwa kwa kulazimishwa. Utakuwa mtiririko wa asili wa maneno yasiyo ya kawaida. Wanapaswa kuruhusu jambo hilo litendeke tu, na kushirikiana na Roho kusema kwa ujasiri na kwa imani.

### Ushauri Baada ya Maombi

Ni muhimu ushauri baada ya maombi utolewe kwa watafutaji. Ikiwa wamejazwa na Roho, utatoa ushauri wa aina moja; na kama hawajajazwa, utatolewa ushauri wa aina nyingine.

Kwa watafutaji waliojazwa na Roho na kunena kwa lugha, wape ushauri huu: kumpokea Roho si mwisho; bali ni njia ya kufikia malengo makubwa zaidi. Kusudi la wao kupokea Roho ni ili wapate nguvu za kuishi kwa ajili ya Mungu na

kuwa mashahidi wa Kristo wenye kuwezeshwa na Roho. Pia utataka kuwatia moyo kutumia muda kila siku kuomba katika Roho, yaani kuomba kwa lugha. Zoezi hili litawaimarisha kiroho, na litawakumbusha uwepo wa Roho ndani yao (1 Kor. 14:4).

Kwa wale ambao hawakujazwa kwa wakati huu, wape ushauri huu: wasivunjike moyo. Wahakikishie kwamba ahadi ya Yesu bado ni ya kweli: "Ombeni nanyi mtapewa" (Lk. 11:9). Waambie kwamba wanapaswa kuendelea kuomba, kutafuta, na kubisha, kama Yesu alivyofundisha. Wanapofanya hivyo, wanapaswa kukumbuka ahadi ya Yesu: "Kila aombaye *hupokea*" (mst. 10, maneno mepesi kukazia). Unaweza kuwauliza kama wanataka kuomba tena. Ikiwa watafanya hivyo, rudia utaratibu wa pale juu, ukiwatia moyo kutenda kwa imani ya ujasiri.

## KUHAMASISHA WALE WANAOPOKEA

Kama mchungaji wa Kipentekoste, hupaswi kamwe kupoteza sababu ya msingi ya Yesu kubatiza wafuasi wake katika Roho Mtakatifu. Anawabatiza ili kuwatia nguvu kama mashahidi wake (Mdo. 1:8). Kwa hivyo unapaswa kuwatia moyo wale ambao wamejazwa na Roho kuanza mara moja kushuhudia familia zao na marafiki zao. Unapaswa pia kuwaongoza katika uinjilisti kwa ujasiri, upandaji kanisa, na kufanya umisheni. Ndivyo Yesu na mitume walivyofanya katika Injili na katika Matendo.[2]

Mara tu Yesu alipotiwa mafuta (au kubatizwa) na Roho Mtakatifu, alianza kuhudumu kwa nguvu (Lk. 3:22-23; 4:8; 14, 18-19; 5:17). Baada ya kupokea Roho siku ya Pentekoste, Petro alisimama pamoja na wanafunzi na kuhubiri kwa nguvu kiasi kwamba watu elfu tatu walimjia Bwana (Mdo. 2:14-41). Wale waliokuja kwa Kristo pia walishuhudia kwa nguvu. Kwa sababu ya ushuhuda wao, "Bwana alizidisha idadi yao kila siku kwa waliokuwa wakiokolewa" (mst. 47). Siku chache baadaye, Mungu alipomimina tena Roho Wake juu ya wanafunzi huko Yerusalemu, "wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri" (4:31). Mtindo huu uliendelea katika kitabu chote cha Matendo, na unapaswa kuendelea katika makanisa yetu ya Kipentekoste leo.

[2] Kwa habari zaidi kuhusu mada hizi, tazama Sura ya 37: "Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti" na Sura ya 39: "Kupanda Makanisa Mapya."

~ Sura ya 21 ~

# Kuhudumu Katika Nguvu za Roho

Ndugu Henry na Ruth mkewe walikuwa wakitumika kama wamishenari kwa watu wanaoabudu sanamu wa kijiji cha Glofaken kusini-mashariki mwa Liberia. Kwa muda mrefu, Henry alikuwa akiwahimiza watu kuacha sanamu zao na kumgeukia Yesu, lakini ni wachache walioitikia.

Siku moja, chifu wa kijiji na wazee wake walimtembelea Henry. Chifu alimwambia Henry, "Umekuwa ukituhimiza tuache sanamu za mababu zetu na kumgeukia Mungu wako. Unasema Mungu wenu ana nguvu kuliko sanamu zetu, lakini hatujashuhudia nguvu za huyu Mungu mnayejisifia. Ukiweza kutuonyesha uwezo wake, tutafikiria kuacha masanamu yetu ili kumfuata Yeye."

Henry alijua kwamba chifu hakuwa akimpa changamoto tu; alikuwa akimpinga Mungu! Kwa hiyo Henry aliomba akisema, "Bwana, onyesha uwezo Wako kwa watu wa Glofaken." Mungu alijibu maombi ya Henry, na upesi alianza kuonyesha uwezo wake kupitia huduma ya Henry.

Asubuhi moja, mtoto wa chifu alimwomba Henry aombe ili Mungu amwondolee giza lililokuwa limemfunika machoni na kumzuia asione vizuri. Henry aliweka mikono juu yake huyo na kusali, akimwomba Mungu muujiza. Mungu alijibu maombi yake mara moja, na mtoto wa jicho akatoweka!

Baada ya hapo, Mungu aliendelea kufanya miujiza kati ya watu wa Glofaken. Wakati mmoja Mungu alizungumza na Henry akimwambia aweke mikono juu ya mwanamke aliyekufa ambaye alikuwa karibu kuzikwa. Kwa mshangao, macho ya mwanamke huyo yalifunguliwa, na maisha yake yakarudishwa. Kwa sababu ya miujiza hiyo na mingine, yule chifu na wazee wake walimgeukia Mungu na kumwamini Yesu, pamoja na watu wengine wengi wa kijiji cha Glofaken. Kanisa lenye nguvu lililojazwa na Roho lilianzishwa.

Katika Agizo Lake Kuu, Yesu aliamuru Kanisa Lake, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa viumbe vyote. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, lakini asiyeamini atahukumiwa." Kwenye hiyo amri aliongeza ahadi ifuatayo: "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka kwa mikono yao; na wanywapo sumu ya kufisha, haitawadhuru hata kidogo; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya" (Mk. 16:15-18). Katika historia yote ya Kanisa, watu wamemwamini Yesu waliposikia habari njema na kushuhudia hayo madhihirisho ya nguvu za Roho.

Sura hii itatazama umuhimu wa mchungaji wa Kipentekoste kuhudumu katika nguvu za Roho. Katika kufanya hivi, itaangalia karama za udhihirisho zilizoorodheshwa katika 1Wakorintho 12:8-10, pamoja na kusudi lake katika huduma. Itatoa miongozo ya kibiblia kwa ajili ya matumizi na utendaji kazi wa karama za kiroho katika kanisa.

## HUDUMA KATIKA NGUVU ZA ROHO

Kila mchungaji wa Kipentekoste lazima ajue jinsi ya kuhudumu katika nguvu za Roho, huku ishara zikifuatana na mahubiri yake. Huduma kama hiyo ilikuwa kawaida katika Agano Jipya, na inasalia kuwa kawaida katika huduma hata leo.

Huduma ya nguvu asili yake iko katika Roho wa Mungu. Kwa hiyo ipo kama ishara kwamba yeyote anayetaka kuhudumu katika nguvu za Roho lazima ajazwe na Roho Mtakatifu. Yesu alielewa hili. Ndiyo maana kabla ya kupaa mbinguni, aliwaachia wanafunzi Wake amri hii ya mwisho: "Msiondoke Yerusalemu, bali ingojeni zawadi ambayo Baba yangu aliahidi, ambayo mmenisikia nikisema juu yake. Kwa maana Yohana alibatiza kwa maji, lakini baada ya siku chache ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu" (Mdo. 1:4-5). Kisha Yesu akawaahidi, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi

mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (mst. 8).

Cha kusikitisha ni kwamba wachungaji wengi barani Afrika siku hizi hawajapokea uwezesho wa Roho. Na kwa sababu hawajajazwa na Roho Mtakatifu, hawaoni madhihirisho ya nguvu za Roho katika huduma zao. Hii inasikitisha. Ikiwa hujajazwa Roho Mtakatifu, inakubidi kumtafuta Mungu hadi uwe "umevikwa uwezo utokao juu" (Lk. 24:49). Mungu atakujaza kwa Roho na kukutia nguvu kwa ajili ya huduma, kama alivyofanya kwa wale wanafunzi wa kwanza Siku ya Pentekoste (Mdo. 2:1-4).[1]

Zaidi ya hayo, kuna wachungaji wa Kipentekoste ambao, ingawa wamejazwa na Roho, wanapata uzoefu mdogo wa nguvu za Roho katika huduma zao. Wengi wa wachungaji hawa wanafikiri kusudi pekee la kujazwa na Roho Mtakatifu ni kuwawezesha kunena kwa lugha. Wao ni kama mwindaji wa kijiji ambaye husafisha bunduki yake kila asubuhi, anapiga risasi chache hewani, na kuiweka kando, na kutarajia mke wake kupika nyama nzuri. Wanafanya kelele nyingi, lakini wanatimiza mambo kidogo sana.

Ingawa kunena kwa lugha ni dhihirisho muhimu la Roho, sio kusudi kuu la kujazwa na Roho. Kusudi la msingi la kujazwa na Roho ni kutiwa nguvu kwa ajili ya huduma (Mdo. 1:8). Kama wachungaji wa Kipentekoste, lazima tupige hatua zaidi tu ya kunena kwa lugha hadi kufikia kwenye huduma iliyotiwa nguvu na Roho. Ni lazima tujifunze kuhudumu katika nguvu za Roho zikiambatana na ishara na maajabu. Huduma kama hiyo italeta baraka kwa watu wa Mungu na kuwavuta wenye dhambi kwa Yesu.

## MIFANO YA HUDUMA ILIYOWEZESHWA NA ROHO

Mchungaji wa Kipentekoste anaweza kujifunza vyema jinsi ya kuhudumu katika nguvu za Roho kwa kujifunza na kuiga huduma ya Yesu katika injili, na ya wanafunzi wa kwanza katika kitabu cha Matendo.

### Huduma ya Yesu

Ingawa Yesu alikuwa Mungu kweli aliyedhihirishwa katika mwili, alichagua kutimiza huduma Yake kama mwanadamu aliyejaa Roho Mtakatifu. Biblia

---

[1] Kwa habari zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 2: "Mtu wa Roho" na Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

inasema "alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akazaliwa katika sura ya wanadamu" (Flp. 2:7). Hivyo Yesu akawa mfano wetu mkuu wa huduma iliyotiwa nguvu na Roho.

Karne nyingi kabla ya kuja kwa Kristo, Isaya alitabiri kwamba Masihi angetimiza wito wake kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Isa. 61:1-2). Katika utimizo wa unabii wa Isaya, Yesu alianza huduma Yake duniani kwa kutangaza, "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kutangaza habari njema" (Lk. 4:18). Petro alisema hivi kuhusu huduma ya Yesu iliyowezeshwa na Roho: "Mungu alimtia mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu na nguvu, naye akazunguka huko na huko akitenda mema na kuponya wote waliokuwa chini ya nguvu za Ibilisi, kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye" (Mdo. 10:10; 38). Mistari hii na mingine katika Agano Jipya inaonyesha kwamba Yesu alifanya huduma yake katika uwezo wa Roho Mtakatifu (ona Lk. 4:1, 14; 5:17). Miujiza, ishara, na maajabu yaliyoambatana na huduma ya Yesu ilisaidia kuwashawishi watu kumfuata (ona Mt. 4:23-25; 9:35-36; Yoh. 2:11).

Uamuzi wa hiari wa Bwana wetu kutegemea nguvu za Roho katika huduma hutupa sisi mfano mkuu. Kama Yesu, ni lazima tutiwe nguvu na Roho Mtakatifu, na kama Yeye, ni lazima tutangaze habari njema kwa wote kwa ujasiri. Wakati huo huo, ni lazima tumwamini Mungu kuthibitisha neno lililotangazwa kwa ishara na maajabu yanayofanywa kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

**Huduma za Mitume**

Pamoja na huduma ya Yesu, huduma za mitume na wanafunzi wengine katika kitabu cha Matendo hutoa mifano bora ya huduma katika nguvu za Roho. Wanafunzi hawa wa kwanza walijifunza kuhudumu katika nguvu za Roho kwa kutazama na kuiga huduma ya Yesu iliyotiwa nguvu na Roho. Karibu kila muujiza ambao wanafunzi walifanya katika kitabu cha Matendo una mizizi yake katika muujiza uliofanywa na Yesu katika injili.

Mitume walifuata mfano wa Yesu wa kujazwa na Roho. Walijua kwamba, kabla ya kuhudumu kama alivyofanya, walihitaji kutiwa nguvu na Roho, kama yeye alivyokuwa. Na kama Yesu, walihakikisha kwamba wote waliokuja kwa Kristo walitiwa nguvu na Roho Mtakatifu na kuhamasishwa kwa ajili ya huduma iliyotiwa nguvu na Roho (tazama Mdo. 2:38-39; 8:14-17; 9:17; 19:1-7).

Mifano hii inatufundisha kwamba huduma ya kweli ya Agano Jipya ni zaidi ya asili, ujuzi, na uwezo. Inahitaji kutiwa nguvu za kiroho, ambazo huja kwa

kujazwa na Roho Mtakatifu. Chini ya upako wa Roho Mtakatifu, Yesu na mitume walitangaza ujumbe wa wokovu kwa ishara zilizofuata.

## MAHALI PA ISHARA NA MAAJABU

Basi, nini kazi ya ishara na maajabu katika huduma ya injili siku hizi? Ishara, maajabu, na miujiza huonyesha huruma yenye upendo ya Mungu kwa wanadamu walioanguka. Huonyesha kwamba injili ina uwezo wa kubadilisha maisha. Sawa na alama za barabarani, hizo huwaelekeza watu kwa Yesu kama Mponyaji, Mkombozi, na Mwokozi. Yohana anatuambia, "Umati mkubwa wa watu ulimfuata [Yesu] kwa sababu waliona ishara alizofanya kwa kuponya wagonjwa" (Yoh. 6:2 ; ona pia Yoh. 20:30-31; Mdo. 3:1-10). Mungu anataka jambo hilo hilo litokee katika huduma zetu leo.

Yesu pia alitangaza kwamba milango ya kuzimu, inayoendeshwa na nguvu za mapepo, haitalishinda Kanisa Lake linaloendelea (Mt. 16:18). Alitoa pepo ili kuwaweka huru walio-onewa, na kudhihirisha utawala wa ufalme wake juu ya ufalme wa ibilisi (Mt. 12:28-29; Lk 11:20-22). Yesu ametoa nguvu na mamlaka yanayolingana kwa wote, na kwa wale wote watakaompokea Roho wake na kujinyenyekeza chini ya mamlaka yake (Mt. 10:1; Mk. 3:14-15; Lk. 9:1-2; Mdo. 1:8).

Zaidi ya hayo, mchungaji wa Kipentekoste lazima atambue kwamba nguvu za Roho zinapatikana kwa kila mshirika wa kanisa lake (Mdo. 2:39). Mungu anataka kuwajaza kila mmoja wao na Roho wake Mtakatifu, kuwatia nguvu kwa ajili ya ushuhuda, na kuwapa karama mbalimbali za Roho. Anafanya hivi "kwa manufaa ya wote" kanisani (1 Kor. 12:7) na kwa ajili ya kuendeleza ufalme Wake duniani (ona Mk. 16:20).[2]

## KARAMA ZA KIROHO

Nguvu ya Roho Mtakatifu iliyopokelewa wakati wa ubatizo wa Roho inatolewa katika huduma hasa kupitia madhihirisho ya karama za kiroho. Katika 1Wakorintho 12:8-10, Paulo anazungumza kuhusu karama tisa za Roho zinazopaswa kufanya kazi katika kila kanisa. Karama hizi tisa nyakati zingine hutajwa kama karama za udhihirisho, kwa kuwa, katika mstari wa 7, Paulo anazitaja kuwa "udhihirisho wa Roho." Karama hizi zimefafanuliwa kuwa ni

---

[2] Unaweza kujua zaidi kuhusu kuwaongoza washirika wa kanisa kujazwa na Roho katika Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

upako usio wa kawaida unaotolewa na Roho Mtakatifu kupitia wanafunzi waliojazwa na Roho ili kutimiza mapenzi ya Baba. Karama tisa za udhihirisho zinaweza kugawanywa katika makundi matatu: Kundi la kwanza ni karama za ufunuo, nazo ni neno la maarifa, neno la hekima, na kupambanua roho. Kundi la pili ni karama za kinabii, nazo ni unabii, aina mbalimbali za lugha, na tafsiri za lugha. Kundi la tatu ni karama za nguvu, nazo ni karama za uponyaji, imani, na matendo ya miujiza. Mara nyingi karama za nguvu ndizo hutumika kudhihirisha ishara na maajabu.[3]

**Kusudi la Karama za Kiroho**

Roho hutoa karama kwa sababu tatu: Kwanza, Yeye huzitoa ili kulijenga, au kuliimarisha, kanisa la mahali (1 Kor. 12:7; 14:12, 26). Kwa sababu ya kuimarishwa, kanisa linaweza kuwatayarisha kwa ufanisi zaidi washirika wake kwa ajili ya huduma (Efe. 4:11-12).

Pili, Roho hutoa karama ili kuwezesha kanisa kueneza injili na kuwafikia waliopotea kwa mafanikio zaidi. Kazi hii ya karama za kiroho imeonyeshwa katika kitabu cha Matendo ambapo karama zinaonyeshwa kuwa mstari wa mbele wa uinjilisti na umisheni.

Mwisho: Roho Mtakatifu hutoa karama za kiroho ili kuwezesha kanisa kukuza na kupanda makanisa mengine yanayowezeshwa na Roho. Ni rahisi kuanzisha kanisa mahali ambapo injili inahubiriwa kwa ishara na maajabu kuliko mahali ambapo hakuna maonyesho ya nguvu za Mungu. Kisa cha Henry na Ruth mwanzoni mwa sura hii kinathibitisha ukweli huu.

**Matumizi ya Karama za Kiroho**

Nguvu za kiroho ni muhimu kwa utendaji mzuri wa kanisa. Lakini, zinaweza kutumiwa vibaya. Kama vile afisa wa serikali anavyoweza kutumia vibaya mamlaka ya kisiasa, Mkristo wa Kipentekoste anaweza kutumia vibaya nguvu za kiroho. Ili kulinda dhidi ya hili, katika 1 Wakorintho sura ya 12 hadi ya 14 Paulo aliweka miongozo fulani kwa ajili ya matumizi sahihi ya karama za kiroho kanisani.

---

[3] Kwa orodha kamili ya karama hizi pamoja na ufafanuzi na madhumuni yake, tazama Nyongeza ya 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

Katika sura ya 13, mtume anasema kwamba karama za kiroho zinapaswa kueleweka kuwa ni madhihirisho ya upendo wa Mungu kupitia aaminiye. Kujali kwa upendo na kutamani ustawi wa wengine lazima kuwe kanuni kiongozi katika kila udhihirisho wa Roho.

Kisha, katika sura ya 14, Paulo anaweka kanuni maalum chache kwa ajili ya udhihirisho sahihi wa karama za kiroho katika kusanyiko la mahali pamoja, hasa karama za unabii, lugha, na tafsiri za lugha. Anasema kwamba matamko ya kinabii kamwe hayapaswi kusababisha machafuko katika kanisa. Yanafaa kutumika kuwatia nguvu watu wa Mungu, kuwatia moyo, na kuwafariji (mst. 3). Zaidi ya hayo, karama ya unabii inapaswa kila wakati itumiwe kwa utaratibu (mst. 27-32). Na mwisho, utoaji na yaliyomo katika matamko ya kinabii vinapaswa "kupimwa kwa uangalifu" kabla ya kupokelewa kwamba yametoka kwa Mungu (mst. 29).

Siku za leo katika bara la Afrika, karama za kinabii zinatumiwa vibaya, na hata karama za nguvu pia. Manabii wa uongo na mitume wa uongo wamegeuza uponyaji na miujiza kuwa biashara ya kutengeneza faida. Hawa watumishi fisadi bila aibu wanauza ishara na maajabu yao ya uongo kwa watu rahisi kudanganyika wanaotafuta suluhu la matatizo yao. Lakini ukisoma katika Maandiko yote, hakuna popote ambapo muujiza uliuzwa kwa mtu.

Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uhakikishe kwamba kanisa lako halifuati hizo tabia ambazo hazimletei Mungu utukufu na zenye kuonyesha kutomcha Yeye. Wewe unapaswa kumwamini Mungu kwa unyenyekevu kwamba atafanya ishara na maajabu kupitia huduma yako. Na unapaswa kufanya hivi bila kuguswa na majaribu ya kufanya biashara na miujiza ya Mungu. Yesu aliwaamuru wanafunzi wake, “Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo.” Kisha akaongeza, “Mmepokea bure; toeni bure” (Mt. 10:8). Mchungaji wa Kipentekoste mcha Mungu atakumbuka daima kwamba karama za kiroho si zake kuzitumia aonavyo vema au kwa faida yake. Badala yake, ni karama za Roho Mtakatifu na zinapaswa kutumiwa tu “kama apendavyo yeye” (1 Kor. 12:11).

Unaweza kutathmini madhihirisho ya karama za kiroho katika kanisa kwa kuuliza maswali yafuatayo:

*1. Je, udhihirisho huo unalingana na Neno la Mungu?* Ikiwa haupatani na mafundisho ya wazi ya Maandiko, unapaswa kukataliwa. Roho wa Mungu hatapingana na Neno la Mungu kamwe.

*2. Je, udhihirisho wa karama unamtukuza Mungu?* Karama za kiroho hazipewi ili kumwinua mtumishi. Zimetolewa ili kumtukuza Mungu na kuwaelekeza watu kwa Yesu (Mt. 15:31; Mk. 2:12). Ikiwa udhihirisho wa karama ya kiroho unaelekea kumwinua mtu ye yote isipokuwa Mungu, unapaswa kutiliwa shaka (Yoh. 16:13-15; 1 Kor. 1:29).

*3. Je, udhihirisho huo unalijenga kanisa?* Karama za kiroho zinatolewa ili kulijenga kanisa. Ikiwa udhihirisho unasababisha kuchanganyikiwa au kudhoofisha imani ya watu katika Kristo, ni lazima kukataliwa.

*4. Je, udhihirisho huo unasaidia kuendeleza utume wa Mungu?* Karama za kiroho ni zana zenye nguvu za uinjilisti na upandaji kanisa. Kwa hiyo, wale wanaotumiwa katika karama wanapaswa kuwa mashahidi wa Kristo wenye ufanisi. Ikiwa udhihirisho wa Roho unaelekea kuvuruga au kuwageuza watu mbali na utume wa Mungu, ni lazima uzuiliwe.

**Kuhamasisha Karama za Kiroho**

Ingawa wewe kama mchungaji wa Kipentekoste inabidi ujilinde dhidi ya matumizi mabaya ya karama za kiroho katika kanisa lako, hili lisiwe jambo lako kuu. Kitu kikubwa kwako kiwe ni kuhimiza udhihirisho wa karama. Kamwe usikubali kuridhika na majadiliano tu ya ishara na maajabu. Tetea ufanyaji kazi wake mara kwa mara katika kanisa na popote. Unaweza kufanya hivyo kwa njia nne.

Kwanza, unapaswa kuwafundisha washirika wako kuhusu jinsi upendo wa Mungu unavyojali watu wote, na jinsi anavyotaka kunyoosha mkono Wake wa neema kuwaokoa, kuwabariki, na kuwaponya. Zaidi, utahitaji kuwafundisha washirika jinsi Mungu anavyotaka kuwatumia katika huduma iliyotiwa nguvu na Roho, na jinsi wao wenyewe wanavyoweza kutumika katika kudhihirisha karama za kiroho.

Pili, lazima uwe mfano wa huduma iliyotiwa nguvu na Roho mbele ya watu. Njia bora ya kuwatia moyo washirika wako kutumia karama za kiroho ni kuwaonyesha jinsi inavyotumika. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya na wanafunzi wake. Aliwaonyesha jinsi ya kuhudumu katika nguvu za Roho kwa kumtoa pepo mtu aliyekuwa amepagawa (Lk. 8:26-39), kwa kumponya mwanamke mgonjwa na kumfufua msichana aliyekuwa amekufa (mst. 40-56). Kisha "akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu na kuponya wagonjwa" (9:2). Kwa hiyo inabidi umruhusu Mungu akujaze na kukujaza tena na tena nguvu za Roho Mtakatifu.

Kisha, lazima umwamini Yeye akutumie kuonyesha karama za kiroho katika maisha yako mwenyewe na huduma.

Tatu, wahimize washirika wako kuitikia maongozi ya Roho Mtakatifu na kutenda kwa imani ili kudhihirisha karama za kiroho. Lazima pia utoe fursa kwa watu kutumia karama wakati wa ibada na uinjilisti.

Mwisho, himiza udhihirisho wa karama za kiroho katika kanisa kwa kutafuta kukuza mazingira yanayofaa katika ibada za kanisa. Mazingira kama hayo huonyeshwa kwa uwepo dhahiri wa Mungu na imani tarajia. Mungu hudhihirisha uwepo wake wakati watu wake wanapomfungulia mioyo yao kwa sifa na ibada ya kweli. Imani inayotarajia hutengenezwa pale watu wa Mungu wanapohimizwa kufikia na kumtarajia Mungu kudhihirisha uwepo wake "kwa ishara, na maajabu, na miujiza ya namna nyingi, na kwa karama za Roho Mtakatifu zinazotolewa sawasawa na mapenzi yake" (Ebr. 2:4).

---

Mchungaji wa kweli wa Kipentekoste atajitahidi kuwa mwanamume au mwanamke wa Roho. Atafanya lengo lake liwe kujifunza kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu kwa ishara na maajabu vinavyoambatana na huduma hiyo, na atawafundisha watu wake kufanya vivyo hivyo.

## ~ Sura ya 22 ~

# Kujihusisha Katika Vita vya Kiroho

Yesu alielewa kwamba yuko katika pambano kubwa la kiroho na Shetani na majeshi yake. Kuna wakati alitoa pepo kutoka kwa mtu aliyekuwa kipofu na bubu. Watu walitazama kwa mshangao huku mtu huyo akianza kuona na kuongea. Wengine waliuliza, "Je, huyu anaweza kuwa Mwana wa Daudi?" Wengine walinong'ona wakisema, "Huyu anatoa pepo kwa kumtumia Beelzebuli, mkuu wa pepo" (Mt. 12:22-24).

Yesu akijua mawazo yao, aliwaambia, "Kila ufalme ukifitinika juu yake wenyewe, utaharibika, na kila mji au nyumba iliyofitinika juu yake haitasimama. Ikiwa ninatoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi Ufalme wa Mungu umekuja juu yenu." Akaongeza, "Mtu anawezaje kuingia katika nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuchukua mali yake bila kwanza kumfunga huyo mwenye nguvu? Ndipo atakapoweza kuteka nyara nyumba yake" (Mt. 12:25-29).

Ndivyo ilivyo leo; sisi nasi tunahusika katika mapambano hayo makubwa dhidi ya nguvu za giza na uovu. Kabla ya kuwaweka watu huru kutoka makucha ya dhambi na Shetani, inabidi mara nyingi tushiriki katika vita vya kiroho. Ni lazima kwanza tumfunge huyo mwenye nguvu. Ndipo tutaweza kupora nyumba

yake. Sura hii itatazama hitaji la mchungaji wa Kipentekoste kuwa na uwezo katika changamoto na kuzishinda roho za kishetani.

## KUELEWA VITA VYA KIROHO

Kabla Yesu hajarudi mbinguni, aliliachia Kanisa Lake Agizo Kuu, kama ifuatavyo: “Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi” (Mt. 28:19, 20). Yesu aliwaamuru wafuasi wake kuwa waaminifu. Kitabu cha Matendo ni habari ya jinsi wanafunzi wa kwanza wa Kristo walivyoanza kutimiza hilo agizo lake kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

Agizo Kuu bado linafanya kazi hadi leo, na litaendelea kutumika “mpaka mwisho wa nyakati” (mst. 20). Ili kutekeleza agizo hili kwa ufanisi, Kanisa na uongozi wake lazima wajue jinsi ya kukabiliana na kumshinda Shetani na majeshi yake.

### Ukweli Kuhusu Vita vya Kiroho

Vita vya kiroho ni kitu halisi. Kuna adui wa kweli, na kuna vita vya kweli vya kiroho ambavyo sisi kama wachungaji wa Kipentekoste lazima tupigane na kushinda. Katika barua yake kwa Waefeso, Paulo alizungumza kuhusu vita hivi vya kiroho kama ifuatavyo:

> "Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." (Efe. 6:12)

Mtume huyo alieleza zaidi jinsi ambavyo watumishi wa Kristo wamepewa silaha za kiroho zenye nguvu za kutumiwa katika vita hivi dhidi ya uovu. Alisema hivi: “Silaha tunazopigana nazo si silaha za kidunia. Hapana. Zina uwezo wa kiungu wa kubomoa ngome” (2 Kor. 10:4).

Mamilioni kote barani Afrika hawajapokea ushuhuda wa kutosha wa injili. Watu hawa wanaishi katika sehemu zinazotawaliwa na mifumo ya kidini inayopinga kuenea kwa Ukristo. Mifumo hii inasimamiwa na watawala wa kishetani wenye nguvu, ambao nao wanatawaliwa na Shetani, “mkuu wa mapepo” (Mk 3:22; tazama pia 1 Yoh. 5:19). Ili kuwakomboa watu hawa, mtu mwenye nguvu itabidi afungwe na kufukuzwa (Mt. 12:28-29). Basi, ikiwa Kanisa linataka kutimiza utume wa Kristo kwa mafanikio, ni lazima lijifunze kutembea katika

nguvu za Roho Mtakatifu. Na ni lazima kujua jinsi ya kushiriki na kuzishinda nguvu za giza.

Yesu aliwafundisha wanafunzi Wake kusali kama ifuatavyo: "Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, duniani kama huko mbinguni" (Mt. 6:10). Kuna wakati mmoja aliwaambia, "Kweli nawaambieni, baadhi ya watu wanaosimama hapa hawataonja kifo kabla ya kuona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu" (Mk. 9:1). Yesu alikuwa akimaanisha Siku ya Pentekoste, wakati ambapo wanafunzi Wake wange "vikwa uwezo utokao juu" (Lk. 24:49; Mdo. 2:4).

Leo, ufalme wa Mungu unakuja kwa nguvu kila wakati mtu anapookolewa, kuponywa, kukombolewa, au kujazwa na Roho Mtakatifu. Mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuwaongoza watu wake kuomba mara kwa mara ili ufalme wa Mungu uje kwa nguvu.

**Chanzo cha Vita vya Kiroho**

Vita vya kiroho ni pambano kati ya wema na ubaya, kati ya kitakatifu na kiovu. Katika kipindi hiki, ni pambano linaloendelea kati ya Shetani na mapepo yake na Kanisa la kweli la Mungu.

Ibilisi amekusanya rasilimali zake zote ili kuhujumu utume wa Mungu wa ukombozi kwa mataifa. Yeye ni muuaji na mwongo na anatafuta "kuiba, kuua na kuharibu" (Yoh. 8:44; 10:10). Yeye na mapepo yake wanafanya kazi ya kupofusha akili za watu wasijue ukweli wa Injili (2 Kor. 4:3-4). Kwa kuwa anamchukia Mungu, shetani anataka kumpiga na kumdhuru. Hata hivyo, anajua hawezi kumuumiza Mungu. Kwa hiyo anatafuta kuwatesa na kuwaangamiza wale ambao Mungu anawapenda, yaani jamii ya wanadamu.

Yesu alitangaza kwamba ufalme wa Mungu umekuja (Mk. 1:14-15; Lk. 8:1, 9:11). Alitangaza kwa ujasiri kwamba amekuja kupindua ufalme wa Shetani na kusimamisha utawala wa Mungu duniani. Ujumbe wa ufalme wa Mungu ulikuwa kiini cha mahubiri ya wanafunzi wa Kristo pia (rej. Mdo. 8:12; 19:8). Yesu aliwatuma kutangaza ufalme wa Mungu na kuonyesha uwezo wake juu ya "nguvu zote za yule adui" (Lk. 10:19; taz. Mt. 10:7; Lk. 9:1-2; 10:8- 9).[1]

---

[1] Ili kupata mengi zaidi kuhusu ujio wa ufalme wa Mungu, tazama kitabu cha Mfululizo wa Africa's Hope kiitwacho, *Ufalme wa Mungu: Maelezo ya Kipentekoste,* cha Denzil R. Miller.

## KUJIANDAA KWA VITA VYA KIROHO

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwe tayari kila wakati kuzipinga na kuzishinda roho za kishetani. Na lazima uwafundishe washirika wa kanisa lako kufanya vivyo hivyo. Zifuatazo ni njia chache unazoweza kutumia kujiandaa kwa ajili ya vita vya kiroho:

### Jazwa Roho Mtakatifu

Kwanza, hakikisha kwamba umejazwa na Roho Mtakatifu (Mdo. 2:4; 4:31) na kwamba sasa hivi unatembea na kuishi kwa kufuata agizo hili: "enendeni katika Roho" (Gal. 5:25). Yesu mwenyewe alijazwa na Roho (Lk. 3:21-22), na aliishi na kuhudumu katika nguvu za Roho (Lk. 4:18-19; Mdo. 10:38). Yesu alishuhudia kwamba aliwafukuza pepo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Mt. 12:28). Ikiwa tunataka kushiriki kwa mafanikio katika vita vya kiroho, sisi pia lazima tuwezeshwe na Roho Mtakatifu.

### Tambua Alichotimiza Kristo

Kisha, katika kujitayarisha kwa vita vya kiroho, lazima utambue yote ambayo Kristo alitimiza pale Kalvari. Pale alilipa gharama ya ukombozi wa wanadamu (Isa. 53:6; 1 Yoh. 2:2). Aliharibu kabisa utawala wa shetani juu ya ulimwengu (Yoh. 12:31). Biblia inatuambia kwamba Kristo "alizivua milki na enzi, na kuzifanya maonyesho mbele ya wote, akishangilia kwa ushindi wa msalaba" (Kol. 2:15).

Sasa, kwa sababu ya kazi kuu ya Kristo pale Kalvari, Shetani na mapepo yake ni maadui walioshindwa (Ebr. 2:14-15). Tukitembea katika Roho na kujinyenyekeza kikamilifu kwa Kristo na mapenzi yake, atatupa nguvu na mamlaka tunayohitaji kumshinda Shetani na mapepo yake.

### Kumbuka Wewe Ni Nani Ndani ya Kristo

Tena katika kujitayarisha kwa vita vya kiroho, unapaswa kujikumbusha wewe ni nani katika Kristo. Ingawa unaishi hapa duniani, wewe kama mtoto wa Mungu ni raia wa mbinguni (Flp. 3:20). Ikiwa utakumbuka ukweli huu, na kuchagua kuishi kama mtoto wa kweli wa mbinguni, Bwana anakupa rasilimali zote, mamlaka, na nguvu za ulimwengu huo. Kadiri unavyojifunza kufikiria na kutenda kama raia wa ufalme wa Mungu ndivyo utakavyokuwa tayari kutangaza zaidi injili ya ufalme kwa wanadamu waliopotea, na ndivyo utakavyokuwa na uwezo zaidi wa kupigana vita katika ulimwengu wa kiroho.

## Vaa Silaha Kamili za Mungu

Halafu, Paulo anawasihi wapiganaji wa kiroho “wawe hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake” (Efe. 6:10). Njia moja tunayoweza kufanya hivyo ni kwa kuvaa silaha zote za Mungu. Kisha, siku ya uovu itakapokuja, tutaweza kusimama imara dhidi ya adui (mst. 11, 13).

Kisha Paulo anataja silaha saba za kiroho zenye nguvu, ambazo Kristo amewapa watumishi wake. Pia anatoa maelezo kidogo jinsi kila silaha inavyoweza kutumika kupigana katika vita vya kiroho (Efe. 6:13-18). Hebu tuangalie kwa karibu zaidi silaha hizi saba za kiroho.

*1. Mkanda wa ukweli*. Kwanza, ni lazima tujivike “mkanda wa ukweli” (Efe. 6:14). Kujifunga mshipi wa ukweli kunamaanisha mambo mawili: kujizatiti kwa ukweli wa Neno la Mungu (Yoh. 17:17). Pia, ni lazima tujifunike huo ukweli, yaani, uaminifu na kuwa waadilifu kabisa. Kwa silaha hii tutaweza kukabiliana na uongo wa shetani (Yoh. 8:44).

*2. Bapa la haki kifuani*. Ni lazima tujitayarishe kwa vita vya kiroho kwa kuvaa “dirii ya haki kifuani” (Efe. 6:14). Tunafanya hivyo kwa kuhakikisha kwamba tuko katika uhusiano sahihi na Mungu, na kwamba tunaishi katika ushirika na Yesu Kristo, ambao haujakatika au kuvunjika (Yoh. 15:5). Kwa sababu ya uhusiano huo, tunawezeshwa kuishi maisha safi na matakatifu (Tito 2:11-12).

*3. Miguu iliyo tayari*. Tatu, ni lazima tujizatiti kwa “utayari” (Efe. 6:15). Kwa maneno mengine, ni lazima tuwe macho kila mara dhidi ya mashambulizi ya adui (1 Pet. 5:8). Utayari huu unatolewa kwa kusikia na kutii injili. Pia, tukiwa wachungaji waaminifu wa kundi la Mungu, lazima tuwatayarishe watu wa Mungu kwa ajili ya mashambulizi ya adui, kama Paulo alivyofanya kwa wazee wa Efeso (Mdo. 20:28-31).

*4. Ngao ya imani*. Nne, ni lazima tuchukue “ngao ya imani” (Efe. 6:16). Tunaweza kutumia silaha hii ya kiroho kama ulinzi dhidi ya “mishale yote yenye moto ya yule mwovu” (mst. 16). Mishale hii yenye moto ni pamoja na majaribu mbalimbali ya shetani kama vile mawazo na tamaa zisizo takatifu na vishawishi vya kuasi amri za Mungu. Imani yetu hujengwa kwa kusikiliza na kusoma Neno la Mungu (Rum. 10:17) na kwa kuomba katika Roho Mtakatifu (Yuda mst. 20).

*5. Kofia ya wokovu*. Silaha ya tano tuliyo nayo ni “chapeo ya wokovu” (Efe. 6:17). Wokovu huu - si wokovu toka dhambi na kuzimu tu - bali ni ukombozi

wowote kutoka kwa Mungu - kama vile kukombolewa kutoka pepo waovu, hatari, magonjwa, na kifo.

*6. Upanga wa Roho.* Sita, ni lazima tuchukue "upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu" (Efe. 6:17). Neno la Mungu ni mojawapo ya silaha za kiroho za mchungaji wa Kipentekoste. Tunaweza kujizatiti kwa Neno la Mungu kwa kujifunza kwa bidii na kushika Maandiko kwa kichwa na kuyaweka moyoni (Zab. 119:11). Zaidi ya hayo, ni lazima tulitangaze Neno la Mungu kwa uaminifu kwa wote watakaosikiliza (2 Tim. 4:2).[2]

Neno la Mungu linaweza kutumika vitani kama silaha ya kushambulia na ya kujikinga. Linaweza kutumika kama silaha ya kushambulia katika maombi, na vile vile linapohubiriwa na kufundishwa katika upako wa Roho. Na linaweza kutumika kama silaha ya kujikinga ili kukabiliana na mashambulizi ya Shetani, kama Yesu alivyofanya nyikani (Lk. 4:1-13).

"Neno la Mungu" lililotajwa katika kifungu hiki linaweza pia kuwa neno la rhema (yaani kwa ajili yako binafsi) ambalo mfuasi wa Kristo anaweza kupokea kutoka kwa Roho. Huu unaweza kuwa mstari fulani wa Biblia ambao Bwana anaupa msisitizo wa kipekee kwenye moyo wa mtu. Au unaweza kuwa ufunuo kutoka kwa Mungu ili kukidhi hitaji maalum, kama vile neno la maarifa au neno la hekima (1 Kor. 12:8).

*7. Kuomba katika Roho.* Mwisho, ni lazima tuchukue silaha ya maombi katika Roho. Sala kama hiyo ni silaha yenye nguvu ya kiroho. Kwa hiyo Paulo anawahimiza waamini "kuomba katika Roho kila wakati kwa kila aina ya sala na maombi" (Efe. 6:18). Maana yake ni kwamba, mara nyingi tunapaswa kumruhusu Roho Mtakatifu kuvuvia na kuelekeza maombi yetu. Aina hii ya maombi inahusisha maombezi katika lugha (1 Kor. 14:14; taz. Rum. 8:26).

## Silaha Zingine Saba za Kiroho

Biblia inazungumza juu ya silaha saba za ziada zenye nguvu, ambazo mchungaji wa Kipentekoste anaweza kutumia kumshinda adui:

*1. Silaha ya mfungo.* Inapotumiwa pamoja na maombi, kufunga ni silaha yenye nguvu ya kiroho (Mk. 9:29).

---

[2] Kwa maelezo zaidi kuhusu uhusiano wa mchungaji wa Kipentekoste na Biblia, tazama Sura ya 9: "Anaiamini Biblia."

*2. Silaha ya kusifu*. Nguvu kuu za kiroho huzalishwa kupitia sifa yenye upako wa Roho. Watu wa Mungu wanapomsifu, kuta zinaanguka (Yoshua 6:16-20), majeshi yanashindwa (2 Nya. 20:1-26), na milango ya gereza inafunguliwa (Mdo. 16:25-26).

*3. Silaha ya upendo.* Upendo wa kweli una nguvu ya ajabu katika kuwaelekeza wanaume na wanawake kwa Kristo (Rum. 5:5). Wengine ambao hawawezi kuguswa kwa hoja zetu au hata madhihirisho yetu ya nguvu, wanaweza kuvutwa wamjie Kristo kupitia maonyesho rahisi tu ya upendo wa Kikristo (12:20-21).

*4. Silaha ya kubatizwa katika Roho.* Yesu aliwaahidi wafuasi wake nguvu wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu yao (Mdo. 1:8). Alikuwa anazungumza kuhusu tukio aliloliita ubatizo katika Roho Mtakatifu (Lk. 3:16; Mdo. 1:5; 2:4).[3]

*5. Silaha za karama za Roho*. Sababu moja ya Roho hutoa karama zake kwa kanisa ni ili waamini waweze kutayarishwa kwa ajili ya vita vya kiroho (1 Kor. 12:8-10).[4]

*6. Silaha ya jina la Yesu*. Mamlaka yote ya mbinguni yanasimama nyuma ya jina la Yesu (Flp. 2:9-11). Tunapotumia jina lake kama alivyoelekeza, nguvu za kuzimu lazima ziachie (Yoh. 14:13-14; Mdo. 3:6; 9:27; 16:18).

*7. Silaha ya injili.* Paulo aliitaja injili kuwa ni "nguvu ya Mungu iletayo wokovu kwa kila aaminiye" (Rum. 1:16). Injili ni ujumbe wa wokovu katika Kristo. Ujumbe wa injili una nguvu ya kujenga imani ndani ya mioyo ya wale wanaoisikia ikihubiriwa (Rum. 10:17). Hatupaswi kushindwa kuhubiri injili kwa uaminifu kwenye kila fursa inayojitokeza (1 Kor. 9:16).

## KUSHIRIKI KATIKA VITA VYA KIROHO

Swali linazuka, "Mchungaji wa Kipentekoste (au mfuasi yeyote aliyejazwa na Roho) anawezaje kukabiliana mpaka kutoa pepo wachafu kwa mtu aliyepagawa

[3] Kwa habari zaidi kuhusu ubatizo wa Roho, tazama Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."
[4] Tazama Nyongeza ya 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

na pepo?” Hizi hapa hatua tatu unazoweza kutumia kufanya huduma ya ukombozi kwa wale waliofungwa au wanaoteswa na pepo.[5]

**Mahojiano**

Hatua ya kwanza katika kutoa ukombozi kwa waliofungwa ni mahojiano, kama hili linawezekana. Katika hatua hii, utazungumza na mtu anayehitaji ukombozi. Lengo lako ni kupata kuelewa zaidi kuhusu hali ya mtu huyo. Katika hatua hii, kupitia karama ya kupambanua roho, unaweza kugundua kuwepo wa pepo. Au pepo wanaweza kuzidiwa na uwepo wa Mungu na kujidhihirisha (Mk 1:23; 5:6-7).

Inapowezekana, unapaswa kumwongoza mhudumiwa katika sala ya toba na kuungama dhambi. Hii ni muhimu hasa wakati dhambi za mtu huyo zinahusiana kwa karibu na kufungwa kwake kiroho. Katika sala hii, mwenye kuteseka anapaswa kukana uvamizi wa kipepo na kazi za kimwili zinazoambatana nazo maishani mwake.

**Makabiliano Kihuduma**

Hatua ya pili ya mchakato wa ukombozi ni makabiliano kihuduma. Huku ndiko kupambana na nguvu za mapepo. Unapaswa kuanza shughuli kwa kuliitia jina la Yesu na kumwalika Roho Mtakatifu aje kudhihirisha uwepo na nguvu zake. Mara tu unapohisi uwepo wa Mungu, endelea kutoa (au kufukuza) pepo. Roho anavyoongoza, unaweza kutumia moja ya taratibu zifuatazo za kibiblia:

- Unaweza kuwafunga pepo kwa jina la Yesu (Mt. 16:17-19; 18:18).
- Unaweza kuamuru pepo watoke, au wamwachilie huyo wanayemtesa (Lk. 4:35).
- Unaweza kuwaamuru pepo wasimwingie tena mtu huyo (Mk. 9:25).

Wakati fulani pepo watapinga, na pambano litatokea (Lk. 8:29; 11:14). Katika hali hiyo, wewe dumu katika imani hadi ushindi utakapokuja. Ukombozi mara nyingi huambatana na maonyesho ya kimwili (Mk. 7:30; Lk. 4:33-35; 9:42). Hili linapotokea, hupaswi kutishika au kupotoshwa. Wewe endelea kutembea kwa

[5] Kuhusu changamoto na kuwashinda pepo wachafu, tazama kitabu cha Discovery Series cha Africa's Hope, *Power Ministry: How to Minister in the Spirit's Power,* Sura ya 11: “Jinsi ya Kutoa Pepo” na Sura ya 12: “Kushinda Roho za Eneo.”

nguvu za Roho Mtakatifu, uwaamuru pepo wanyamaze (Mk. 1:25), na kwa mamlaka ya jina la Yesu, uwaamuru kutoka na kubaki nje (Mk. 9:25).

**Ushauri Baada ya Maombi**

Hatua ya mwisho katika mchakato wa ukombozi ni ushauri baada ya maombi. Hatua hii ni muhimu sana kwa mtu ambaye amekuwa chini ya utawala wa mapepo. Atahitaji maombi na usaidizi wa kihisia baada ya ukombozi. Ikiwa mtu huyo hajazaliwa mara ya pili, unapaswa mara moja umwongoze kuingia katika kumwamini Kristo. Zaidi ya hayo, unapaswa kuwaongoza mara moja katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yesu alionya kuhusu kupuuza mambo haya muhimu (Mt. 12:43-45). Wewe, au mtu uliyemkabidhi, mnapaswa kudumisha mawasiliano ya karibu na mtu huyo hadi atakapokuwa huru kabisa kutoka kwa utumwa wake.

---

Kama mchungaji wa Kipentekoste, Kristo amekuagiza kushiriki katika vita vya kiroho (Mk. 16:15-16). Unaweza kumkabili shetani na majeshi yake ya pepo kwa ujasiri mkubwa, ukijua kwamba Yeye anayekaa ndani yako ni mkuu zaidi kuliko yeye aliye katika ulimwengu (1 Yoh. 4:4).

~ Sehemu ya 6 ~

# Mchungaji wa Kipentekoste Kama Mchungaji

## ~ Sura ya 23 ~

# Kuielewa Huduma ya Kichungaji

Inawezekana kabisa kwa mtu kushiriki kikamilifu katika shughuli ya kidini, na kujitolea sana kwa shughuli hiyo, na wakati huo huo asielewe kabisa kile anachofanya au hata kwa nini anakifanya. Roho aliwahi kumwelekeza Filipo kwa mtu wa Kushi aliyekuwa amejitoa na mwaminifu kabisa. Huyo mheshimiwa alikuwa akisoma Maandiko kwa bidii. Lakini hakuwa anaelewa alichokuwa akisoma (Mdo. 8:29-31). Katika wakati mwingine, Paulo alikutana na baadhi ya watu waliokuwa waaminifu na waliokuwa wamejitoa vizuri sana huko Athene. Hao watu walimwabudu "mungu asiyejulikana". Pamoja na hayo, hawakuelewa walikuwa wanamwabudu nani au kwa nini (Mdo. 17:22-23). Walihitaji maelezo.

Wachungaji wengi wa Kipentekoste barani Afrika hujikuta katika hali kama hiyo. Wanashiriki kikamilifu katika huduma ya kichungaji, na wamejitoa sana kutimiza wajibu wao kama wachungaji. Lakini kwa kweli, wanaelewa kidogo sana juu ya kile wanachofanya au kwa nini wanakifanya. Sawa na yule afisa wa Kushi, wanasihi, "Nitajuaje mtu asiponifafanulia?" Sura hii imeandikwa kujibu hitaji hili. Itaweka msingi wa ufahamu wa huduma ya kichungaji, msingi ambao juu yake huduma imara inaweza kujengwa.

## MAZINGIRA YA HUDUMA YA UCHUNGAJI

Huduma ya kichungaji hutokea katika mazingira ya kanisa la mahali. Neno la Kiyunani lililotafsiriwa kanisa katika Agano Jipya ni ekklesia, ambalo maana yake ni wale walioitwa na kutengwa. Hivyo, kanisa la mahali ni kundi la watu ambao wametengwa na Kristo kumtumikia na kumwabudu. Linaundwa na wale ambao wamezaliwa kwa Roho wa Mungu na kuoshwa katika damu ya Yesu (Yoh. 3:3-7; Mdo. 20:28).

Mambo matatu yanaweza kusemwa kuhusu Kanisa: Kwanza, Kanisa ni la Mungu. Yesu alilitaja Kanisa kama "kanisa langu" (Mt. 16:18). Paulo aliliita "nyumba ya Mungu… kanisa la Mungu aliye hai" (1 Tim. 3:15). Pili, Kanisa ni makao ya Mungu. Paulo anazungumza juu ya Kanisa kama "hekalu takatifu" ambalo "limekuwa makao ambayo Mungu anaishi kwa Roho wake" (Efe. 2:22). Na mwisho, Kanisa ni "nguzo na msingi wa kweli" (1 Tim. 3:15). Kwa maneno mengine, ni mfumo wa kiroho wenye kuunga mkono ukweli na kuudumisha. Utume mmoja mkubwa na wa msingi sana wa Kanisa ni kuhifadhi na kutangaza ukweli (Mt. 28:19; 2 Kor. 2:14). Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufahamu kikamilifu kwamba unatekeleza huduma yako katika mazingira hayo.

## DHANA YA HUDUMA

Ni muhimu pia kuelewa dhana ya kibiblia ya huduma. Maandiko yanafundisha kwamba Kristo huweka na kupanga huduma katika Kanisa ili kuliwezesha kutimiza utume wake lililopewa na Mungu. Utume wa Kanisa ni kutangaza habari njema kwa watu wote kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kabla ya kurudi upesi kwa Kristo (Mk. 16:15-16; Mdo. 1:8). Kisha, ni kuwachukua wale wanaoamini na kuwafanya kuwa wanafunzi watiifu, wakiwatengeneza wawe mfano wa Bwana wao (Mt. 28:19; Kol. 3:10).

Neno huduma limebeba zaidi dhana ya utumishi na kazi. Paulo anafafanua wazo la huduma. Katika Waefeso 4, anazungumza juu ya aina tatu za huduma.

### Huduma ya Yesu

Kwanza, Paulo anazungumza kuhusu huduma ya Yesu Masiya (Efe. 4:8-10). Kupitia kazi yake ya ukombozi msalabani (pamoja na kifo chake, kuzikwa, kufufuka, na kupaa kwa Baba), Yesu alianzisha Agano Jipya. Akiwa duniani, Kristo alihudumu kama mtume (Ebr. 3:1), nabii (Lk. 24:19), mwinjilisti (Lk. 19:10), mchungaji (Yoh. 10:11-16), na mwalimu (Yoh. 3:2; 13:13). Hivyo akawa

"jiwe kuu la pembeni" la Kanisa, akihakikisha uthabiti na kudumu kwa hiyo taasisi (Efe. 2:20).

**Huduma ya Waaminio**

Pili, Paulo anazungumza kuhusu huduma ya waaminio (Efe. 4:11-16). Yesu alikabidhi huduma yake kwa Kanisa. Kwa hiyo, huduma yoyote katika Kanisa ni mwendelezo wa huduma Yake. Lengo la huduma ni kila mshiriki wa kanisa kuwa mkomavu "na kufikia kipimo cha utu uzima na utimilifu wa Kristo" (Efe. 4:13). Wale ambao wamekomaa wanapaswa kugeuka na kuwaimarisha wengine, na kusababisha kanisa zima kukua na kustawi.

**Huduma za Uongozi**

Tatu, Paulo anajadili huduma za uongozi ambazo Kristo alitoa kwa Kanisa. Anaandika hivi: "Kristo mwenyewe alitoa mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu" (Efe. 4:11). Kimsingi, majukumu hayo ya kihuduma hayapaswi kutazamwa kuwa ni vyeo, kama wengi wanavyofanya. Afadhali zifikiriwe kama kazi za huduma. Sio vyeo ili viongozi watawale juu ya kanisa. Badala yake, ni kazi zinazotolewa kwa viongozi watumishi ili "kuwatayarisha watu [wa Mungu] kwa ajili ya kazi za huduma" (Efe. 4:12), kama ifuatavyo:

- Utendaji wa kitume: Mtume hutumikia Kanisa na makusudi ya Mungu kwa kuendeleza ufalme wa Mungu katika maeneo ambayo hayajafikiwa na miongoni mwa watu ambao hawajafikiwa, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu - na kwa kuwatayarisha wengine kufanya vivyo hivyo.
- Utendaji wa kinabii: Nabii hutumikia Kanisa na makusudi ya Mungu kwa kunena jumbe kutoka kwa Mungu katika uwezo wa Roho Mtakatifu - na kwa kuwatayarisha wengine kufanya vivyo hivyo.
- Utendaji wa kiinjilisti: Mwinjilisti hutumikia Kanisa na makusudi ya Mungu kwa kutangaza injili kwa waliopotea katika uwezo wa Roho Mtakatifu - na kwa kuwatayarisha wengine kufanya vivyo hivyo.
- Utendaji wa kichungaji: Mchungaji hutumikia Kanisa na makusudi ya Mungu kwa kuwahudumia watu wa Mungu katika nguvu za Roho Mtakatifu - na kwa kuwatayarisha wengine kufanya vivyo hivyo.
- Utendaji wa kufundisha: Mwalimu hutumikia Kanisa na makusudi ya Mungu kwa kufundisha Neno la Mungu katika nguvu za Roho Mtakatifu, na kwa kuwatayarisha wengine kufanya vivyo hivyo.

Mara nyingi, hizi kazi za huduma huingiliana, na watu wanafanya kazi nyingi. Kwa mfano, mtu mmoja anaweza kufanya kazi kama mtume na nabii kwa wakati

mmoja. Mwingine anaweza kufanya kazi kama mwalimu na mwinjilisti, na kadhalika. Kama ilivyotajwa hapo juu, Yesu alitenda katika huduma zote hizo tano, kama na mtume Paulo alivyofanya. Kwa maneno yake ya mstari wa 11, Paulo anaonekana kuunganisha majukumu ya mchungaji na mwalimu katika huduma moja ya mchungaji mwalimu.

Katika mfumo huu, Paulo anajitambulisha kama "mtumishi wa Yesu Kristo, aliyeitwa kuwa mtume" (Rum. 1:1; taz. Tito 1:1). Vivyo hivyo, Petro anajitambulisha kama "mtumishi na mtume wa Yesu Kristo" (2 Pet. 1:1). Angalia jinsi hao wote wawili walivyojitangaza kuwa watumishi. Hivyo tu ndipo wangeweza kuwa mitume wa kweli. Inapaswa kuwa vivyo hivyo leo kwa yeyote anayehudumu katika mojawapo ya zile huduma tano za uongozi. Zaidi ya yote, wanapaswa kujiona kuwa watumishi wa Mungu na wa watu wake (rej. Yoh. 21:15-17; 1 Pet. 5:2-4).

Hizi "karama tano zitokanazo na kupaa kwa Kristo" hutumika zaidi kama maonyesho ya mamlaka ya Kristo ndani ya Kanisa. Kusudi ni kuliongoza Kanisa kufikia malengo ya kimungu. Paulo alifundisha kwamba huduma hizi zina kazi mbili: kupanda na kumwagilia maji (1 Kor. 3:6). Huduma za upandaji zinaweza kuwashirikisha mitume na wainjilisti. Huduma za kumwagilia maji zinaweza kuwashirikisha manabii, wachungaji, na waalimu. Ushirikiano kati ya wapandaji na wanaomwagilia maji huhakikisha kuendelea kwa kazi ya Mungu.

**Huduma za Utumishi**

Pamoja na huduma za uongozi, Mungu ameweka huduma fulani za utumishi katika Kanisa. Huduma hizi ni pamoja na wazee, mashemasi, na mashemasi wa kike (cf. Mdo. 6:1-6; 14:23; 1 Tim. 3:1-10). Neno mzee kwa Kiebrania ni zaqen , lenye maana ya mtu mwenye ujuzi, mzoefu na mwenye mamlaka (Hes. 11:16). Neno mzee kwa Kiyunani ni presbyteros, ambalo lina maana sawa na lile tulilotaja hapo juu. Mzee katika kanisa ni yule aliye na mamlaka ya kuhudumu kama mwangalizi (episkopos kwa Kiyunani) (Mdo. 20:17, 28). Hivyo, mchungaji ni mzee na mwangalizi (Mdo. 20:17, 28; 1 Tim. 3:1-2; Tito 1:5-7). Ili kuliongoza kanisa ipasavyo, mchungaji wa Kipentekoste lazima awe amekomaa kiroho, na lazima awe na ujuzi kamili wa Neno la Mungu (1 Tim. 3:6; 2 Tim. 4:2).

Neno shemasi kwa Kiyunani ni diakonos, ambalo linamaanisha "mtu anayetumikia." Katika Matendo 6, wanaume saba waliojazwa na Roho walichaguliwa kuhudumia meza ili mitume waweze "kujitoa wenyewe kwa

maombi na huduma ya neno" (Mdo. 6:2-4). Wawili kati ya hao - Stefano na Filipo - wakawa mashahidi wenye nguvu sana kwa ajili ya Kristo. Katika Warumi 16:1, Paulo alimtambulisha Fibi kama shemasi wa kike wa kanisa la Rumi.

## KAZI YA MCHUNGAJI

Neno la kibiblia "mchungaji" linatokana na neno poimēn ambalo ni la Kiyunani. Maana yake hasa ni "mchunga mifugo." Kama mchungaji, jukumu lako ni kuchunga kundi la Mungu (Mdo. 20:28). Na kama mchungaji, unafaa kutumika kama kiongozi, mshauri, na mlinzi wa watu wa Mungu (1 Pet. 5:1-4).

### Majukumu ya Kichungaji

Miongoni mwa majukumu yako ya kichungaji ni kulitunza kundi (Yoh. 21:15-17; 1 Pet. 5:2-3), kuimarisha mwili (Efe. 4:11-12), kushauri watu wa Mungu (1 Tim. 5:14), na kuwachunga kondoo (Mdo. 20:28). Majukumu mengine ni pamoja na kuhubiri (2 Tim. 4:2), kufundisha (1 Tim. 3:2; Tito 2:1), kuongoza (Ebr. 13:17), kusimamia (Mdo. 20:28), kufanya wanafunzi (Mt. 28:19), kuwafikia waliopotea (2 Tim. 4:5), na kuhamasisha kanisa kwa ajili ya umisheni (Mdo. 13:1-4).[1]

Katika siku za mwanzo za Kanisa, mara tu baada ya Siku ya Pentekoste, mitume walichukua nafasi ya wachungaji. Waliliongoza Kanisa kama Yesu alivyokuwa amewaongoza, wakisisitiza kile alichokuwa amesisitiza. Misisitizo yao mingi imefunuliwa katika maelezo ya Luka kuhusu Kanisa katika Matendo 2:38-47.

Hayo maandiko ya ajabu, pamoja na mistari inayotangulia, yanafunua mikazo kumi ya mitume kuhusu uchungaji. Kama mchungaji wa Kipentekoste, itakuwa hekima kufuata mfano wa mitume, ukiruhusu mikazo hii kumi kutumika kama vitu vya kuiga katika huduma yako mwenyewe leo.

*1. Kutangaza injili.* Akiwa amewezeshwa upya na Roho Mtakatifu, Petro alisimama na kutangaza injili kwa ujasiri. Katika mahubiri yake Siku ya Pentekoste, yeye alikazia kifo na ufufuo wa Kristo (Mdo. 2:23-24, 32; taz. 1 Kor. 15:1-4). Alihitimisha ujumbe wake kwa kuwaita watu watubu na kuiamini Injili (Mdo. 2:36-40). Msisitizo huu uliendelea katika Matendo ya Mitume yote

---

[1] Kwa habari zaidi juu ya majukumu ya mchungaji wa Kipentekoste, ona Sura ya 23-27.

(fananisha 3:19; 20:21; 26:20). Vivyo hivyo, utangazaji wa injili unapaswa kuwa kiini cha huduma yako leo ya kichungaji.[2]

*2. Kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu.* Petro pia alisisitiza haja ya kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu (Mdo. 2:38-39; taz. 2:17-18). Wale wanaompokea Kristo wapewe mara moja nafasi ya kujazwa na Roho Mtakatifu. Sawa na kutangazwa kwa injili, msisitizo huu uliendelea kote katika Matendo (8:14-17; 9:17-18; 10:44-46; 19:1-7). Kama mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika, lazima ufanye vivyo hivyo. Unapaswa kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa lengo la kuona kila mshirika akiwezeshwa kuwa shahidi wa kuwafikia waliopotea (1:8).[3]

*3. Kufundisha neno la Mungu.* Zaidi ya hayo, Luka anatuambia kwamba waamini wa Yerusalemu "walijitoa wenyewe kwa mafundisho ya mitume" (Mdo. 2:42). Kwa hiyo mitume walikazia kufundisha Neno la Mungu. Miaka mingi baadaye, Paulo angeshuhudia, "Mnajua ya kuwa sikusita kuhubiri neno lo lote ambalo lingekuwa la manufaa kwenu, bali nimewafundisha hadharani na nyumba kwa nyumba" (20:20). Hii ilikuwa ni njia ya Paulo ya kufanya kazi popote alipokwenda (fan. 11:26-26; 15:35; 28:31). Wewe pia unapaswa kuhakikisha kwamba Neno la Mungu linafundishwa kwa usahihi, kwa uwazi, na kwa upana katika kanisa ambalo Mungu amekuita uliongoze.[4]

*4. Kuadhimisha ibada maalum.* Kwa kutii amri za Yesu (Mt. 28:19-20; Lk. 22:19), mitume walisisitiza ubatizo wa maji na Ushirika Mtakatifu (Mdo 2:38-41). Ubatizo wa maji hushuhudia ujuzi wa mwamini wa kuzaliwa upya. Ushirika Mtakatifu hushuhudia uhusiano wao na Kristo, unaoendelea. Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uhakikishe kwamba ibada hizi mbili muhimu zinasimamiwa na kuendeshwa kanisani kwa uaminifu.[5]

*5. Kuongoza katika maombi.* Mitume walikazia sana maombi. Luka anatuambia kwamba watu "walijitoa wenyewe… kwa maombi" (Mdo. 2:42). Sala

---

[2] Kwa habari zaidi kuhusu huduma ya kuhubiri ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 16: "Mahubiri Yenye Upako wa Roho."

[3] Kwa habari zaidi kuhusu kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu, tazama Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

[4] Kwa habari zaidi kuhusu huduma ya kufundisha ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 17: "Kufundisha kwa Ufanisi."

[5] Kwa habari zaidi juu ya zile ibada maalum, tazama Sura ya 42: "Kuendesha Meza ya Bwana, Kuweka Wakfu, na Kuingiza Kazini."

ya kujitoa hutengeneza msingi wa uchaji na ushuhuda binafsi wa mwamini. Pia huhakikisha uwepo na nguvu za Roho katika kanisa na katika maisha ya waaminio (rej. 4:31). Kama mchungaji wa Kipentekoste, wewe pia lazima uwaongoze watu katika maombi kwa njia ya mafundisho na kwa mfano wako binafsi.[6]

*6. Kutarajia ishara na maajabu.* Mitume walifanya bidii sana kwa ajili ya dhihirisho la uwepo wa Mungu na nguvu Zake katika kanisa. Luka anaandika hivi: "Kila mtu akastaajabia maajabu na ishara nyingi zilizofanywa na mitume" (Mdo. 2:43). Madhihirisho ya uwepo na nguvu za Mungu yanapaswa pia kubainisha huduma yako kama mchungaji wa Kipentekoste leo.[7]

*7. Kukuza umoja.* Mitume pia walikuza umoja katika mwili. Luka anaandika, "Waamini wote walikuwa pamoja na kuwa na vitu vyote shirika" (Mdo. 2:44). Umoja wa watu unaozungumziwa hapa, ulikuwa zaidi ya kimwili. Walikuwa na umoja wa moyo na kusudi ambao ulisukuma kanisa mbele katika utume.

*8. Kuhimiza ukarimu.* Zaidi ya hayo, mitume walikuza ukarimu. Matokeo yake, washiriki wa kanisa "wakauza mashamba na mali ili wawagawie wale waliohitaji" (Mdo. 2:45). Ukarimu kama huo ulitokana na uhusiano wa upendo kati yao wenyewe na upendo kwa Mungu wao. Kama mitume, wewe pia lazima uwaongoze watu wako katika kutoa kwa ukarimu kwa kazi ya Mungu.

*9. Kujipanga kwa ajili ya ibada.* Luka anaandika, "Kila siku waliendelea kukutana hekaluni….wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote" (Mdo. 2:46-47). Mitume walijua jinsi ilivyokuwa muhimu watu wakutane kwa ajili ya ibada, mafunzo na kutiana moyo.[8]

*10. Kuhamasisha ushuhudiaji.* Mwisho, mitume walikazia ushuhudiaji binafsi. Waliwahamasisha watu kwa ajili ya utume, wakiwatia moyo kushirikisha wengine ujumbe wa Kristo. Kwa hiyo, "Bwana akawazidishia idadi kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa" (Mdo. 2:47).[9]

---

[6] Kwa maelezo zaidi kuhusu mchungaji wa Kipentekoste na maombi, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi."

[7] Kwa maelezo zaidi juu ya huduma katika nguvu zisizo za kawaida, tazama Sura ya 21: "Kuhudumu Katika Nguvu za Roho."

[8] Kwa maelezo zaidi juu ya kuliongoza kanisa katika ibada, ona Sura ya 18: "Kuliongoza Kanisa Katika Kuabudu."

[9] Kwa habari zaidi juu ya kuhamasisha kanisa kwa ajili ya ushuhudiaji, tazama Sura ya 37: "Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti."

Hii mikazo kumi ya mitume katika kanisa la Yerusalemu inaweza kutumika kama mifano kwako leo wewe kama mchungaji wa Kipentekoste. Itakusaidia kuiunganisha huduma yako na huduma ya Yesu na mitume. Na itasaidia kuhakikisha kwamba kanisa unalochunga linakuwa nguvu ya kiroho katika jumuiya yako mwenyewe na katika ulimwengu.

**Hamasa za Kichungaji na Uwajibikaji**

Kama mchungaji wa Kipentekoste, unachofanya ni muhimu; na kwa nini unakifanya ni muhimu zaidi. Petro aliandika kuhusu motisha zinazofaa kwa kazi ya uchungaji (1 Pet. 5:2-3). Wachungaji hawapaswi kufanya kazi zao kwa kutimiza tu wajibu, au kwa ajili ya faida ya kifedha, au kwa kutamani kutawala watu. Wanapaswa kuwajali watu wa Mungu kikweli na kuwatumikia kwa upendo. Wale wachungaji wanaohudumu kwa nia njema watapokea tuzo. Petro anawatia moyo wachungaji waaminifu kwa ahadi kwamba: "... Mchungaji Mkuu atakapotokea, mtapokea taji ya utukufu isiyonyauka kamwe" (taz. mst. 4).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, hupaswi kusahau kamwe kwamba siku moja utasimama mbele ya Kristo kutoa hesabu ya jinsi ulivyotimiliza wito wako. Paulo anatuambia, "Imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja wetu apokee ijara yake kwa mambo aliyotenda alipokuwa katika mwili, kwamba ni mema au mabaya" (2 Kor. 5:10). Mchungaji mwaminifu atapata thawabu (Mt. 25:23); mchungaji asiye mwaminifu atawajibishwa (mst. 26).

Katika Maandiko yote, wachungaji wanaoshindwa kutunza watu wa Mungu wanahukumiwa. Kwa mfano, Mungu alisema kupitia Yeremia kama ifuatavyo: "Ole wao wachungaji wanaoharibu na kuwatawanya kondoo wa malisho yangu!…Kwa sababu mmetawanya kundi langu na kuwafukuza, wala hamkuwatunza, nitawaadhibu ninyi kwa uovu mlioufanya" (Yer. 23:1-2; taz. Eze. 34:1-10).

## UWEZESHAJI KWA AJILI YA HUDUMA

Huduma ya kichungaji ni shughuli nzito ya kiroho, na ya kina kirefu. Ili kuwafikia waliopotea kwa ufanisi na kuwaandaa watakatifu, mchungaji wa Kipentekoste lazima ajifunze kutegemea rasilimali zinazotolewa na Mungu.

Huduma ya kichungaji inahusisha vita vya kiroho vinavyotakiwa kupiganwa kwa silaha za kiroho (Efe. 6:12; 2 Kor. 10:4-5).[10]

Moja ya silaha hizi za kiroho ni nguvu uliyopokea ulipobatizwa katika Roho Mtakatifu. Kabla ya kurudi mbinguni, Yesu aliwaamuru wanafunzi wake kubaki Yerusalemu ili kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu (Mdo. 1:4-8). Hawakupaswa kuanza huduma zao mpaka "mtakapovikwa uwezo utokao juu" (Lk. 24:49). Walipokea nguvu hizo siku ya Pentekoste wakati ambapo "wote walijazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine kama Roho alivyowawezesha" (Mdo. 2:4). Kama mitume, huwezi kutimiza wajibu wako kama mchungaji ipasavyo bila kuwezeshwa na Mungu. Na kama wao, lazima uhakikishe kwamba kila mtu anayekuja kwa Kristo anabatizwa upesi sana katika Roho Mtakatifu na kutiwa nguvu kama shahidi wa Kristo.[11]

---

[10] Kwa habari zaidi kuhusu vita vya kiroho, tazama Sura ya 22: "Kujihusisha Katika Vita vya Kiroho."

[11] Kwa habari zaidi juu ya kuwaongoza waamini wapya katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, ona Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

~ Sura ya 24 ~

# Kuwatunza Kondoo

Wakati mmoja Mafarisayo fulani walimlaumu Yesu kwa kushirikiana na watu waliopotea. Walinung'unika wakisema "Mtu huyu huwakaribisha wenye dhambi, na hata anakula nao!" Aliposikia maneno yao, Yesu akawauliza, "Hebu tuseme mmoja wenu ana kondoo mia, na mmoja akapotea. Itakuwaje?" Kisha akawaambia hadithi ya mchunga mifugo mmoja aliyegundua kondoo wake mmoja amepotea. Mchungaji yule mwaminifu aliwaacha wale tisini na kenda kondeni na kuanza kumtafuta yule kondoo mmoja aliyepotea. Alipompata, alimweka mabegani mwake na kumpeleka nyumbani. Alipokuwa akiingia kijijini kwao, aliwaita rafiki zake na majirani, na kusema, "Furahini pamoja nami, kwa maana nimempata kondoo wangu aliyepotea!" (fan. Lk. 15:4-6).

Kabla Daudi hajawa mfalme na mtunga-zaburi, alikuwa mchungaji, akichunga kondoo za baba yake. Katika shughuli yake hiyo, alijifunza kumpenda kila kondoo mmoja-mmoja. Alikuja kuelewa kwamba Mungu alimpenda na kumtunza kama yeye alivyowatunza kondoo wake. Aliandika na kusema, "Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji tulivu huniongoza, huniburudisha nafsi yangu" (Zab. 23:1-2).

Yesu alijipa mwenyewe cheo cha Mchungaji. Alisema hivi: "Mimi ndimi mchungaji mwema. Nawajua kondoo wangu na kondoo wangu wananijua ... nami

nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo wangu" (Yoh. 10:14-15). Mwandishi wa Waebrania anamwita Yesu “Mchungaji mkuu wa kondoo” (Ebr. 13:20). Kondoo wake ni wale waliochagua kumfuata. Yesu anaendelea kusema kwamba Yeye ndiye mmiliki wa kondoo. Tofauti na mtu wa kuajiriwa, ambaye hukimbia mbwa mwitu atakapokuja kuwaangamiza kondoo, mchungaji wa kweli atasimama imara kuwatetea. Yuko tayari hata kuutoa uhai wake kwa ajili yao.

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima Yesu awe kielelezo chako. Ni lazima uwachunge watu wa Mungu kama ambavyo Yesu mwenyewe angewachunga kama angekuwa hapa katika mwili. Sura hii itatazama wajibu wa mchungaji wa Kipentekoste katika kuchunga kundi la Mungu.

## MOYO WA KICHUNGAJI

Kama wachungao kundi la Mungu, wachungaji wa Kipentekoste lazima wawe na huruma, waaminifu, na wanaotegemewa.

### Mwenye Huruma

Akizungumza kuhusu Mungu, Isaya aliandika hivi: “Hulichunga kundi lake kama mchungaji: Huwakusanya wana-kondoo mikononi mwake na kuwachukua karibu na moyo wake” (Isa. 40:11). Kama Bwana wao, wachungaji wa kweli wa Kipentekoste nao wana huruma. Wanawapenda watu kwa dhati. Na ni pamoja na wale walio ndani na walio nje ya kanisa. Yesu alionyesha upendo wake kwa watu. Biblia inasema hivi juu yake: “Alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wametaabika na wanyonge, kama kondoo wasio na mchungaji” (Mt. 9:36). Vivyo hivyo, lazima uwapende kweli watu ambao Mungu amekuita uwatumikie.

### Mwaminifu

Zaidi ya hayo, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujithibitishe kuwa mwaminifu. Lazima uwe tayari kuacha yote na kumfuata Bwana wako kikamilifu (Mt. 19:21; Mk. 8:34-35). Kristo amewaweka watu wake mikononi mwako kama amana takatifu. Kwa hivyo ni lazima uweke kando kwa hiari uhuru haki zako binafsi. Na lazima uwatumikie kwa uaminifu wale ambao Kristo amewaweka katika uangalizi wako. Paulo aliandika kuhusu wahudumu wa injili, “Inatakiwa wale waliokabidhiwa wawe waaminifu” (1 Kor. 4:2).

**Mwenye Kutegemewa**

Mwisho: ili kulichunga kundi la Mungu kwa uaminifu ni lazima uwe mtu unayetegemewa. Usiwe kama mtu wa kuajiriwa, ambaye inapotokea taabu, huwaacha kondoo na kukimbia (Yoh. 10:12-13). Badala yake, uwe thabiti na anayetegemewa. Wote wawili: Mungu aliyekuita, na watu unaowatumikia, lazima waweze kukutegemea, wakijua kwamba chochote kitakachokuja, unaweza kutazamiwa kusimama na kutimiza wajibu wako.

## KAZI YA MCHUNGAJI

Kama mchungaji wa Mungu, kila mchungaji wa Kipentekoste anabeba majukumu mawili mazito: kuwatunza kondoo na kuliandaa kanisa kuwa jumuiya inayojali. Hebu tuyatazame hayo majukumu mawili.

**Kuwatunza Kondoo**

Kwanza, ni lazima kuwachunga kondoo. Ili kufanya hivyo, utahitaji kutimiza angalau majukumu sita:

*1. Kulisha kondoo*. Ujumbe wa Yesu kwa Petro ulikuwa, "[Ikiwa unanipenda]…utawalisha kondoo wangu" (Yoh. 21:17). Mungu aliwaahidi Israeli, "Nitawapa ninyi wachungaji waupendezao moyo wangu, watakaowaongoza [au kuwalisha] kwa maarifa na ufahamu" (Yer. 3:15). Vivyo hivyo lazima ulishe watu wa Mungu. Unapaswa kuwafundisha Neno la Mungu kwa uaminifu. Tendo hili litawafanya watu wakue na kuwa imara katika imani. Pia itasababisha kanisa kujengwa na kukomaa katika Kristo (Efe. 4:11-16). Bila shaka hiyo ndiyo sababu moja iliyomfanya Paulo kumtia moyo Timotheo kama ifuatavyo: "lihubiri neno; kuwa tayari wakati unaofaa na usiofaa; onya, kemea, na kuhimiza kwa uvumilivu mwingi na mafundisho makini" (2 Tim. 4:2).

Si lazima tu uhubiri na kufundisha Neno la Mungu kwa uaminifu wewe mwenyewe, lazima pia uanzishe mpango wa kufundisha wa kina katika kanisa. Ni lazima uhakikishe kwamba Biblia inafundishwa kwa utaratibu kwa watu wa rika zote — watoto, vijana, na watu wazima.[1]

*2. Kulilinda kundi.* Paulo aliwahimiza wazee wa Efeso hivi: "Jilindeni nafsi zenu, na lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa

[1] Kwa maelezo zaidi juu ya wajibu wa mchungaji wa Kipentekoste katika kufundisha Neno la Mungu, tazama Sura ya 17: "Kufundisha kwa Ufanisi."

waangalizi juu yake" (Mdo. 20:28). Kisha akawaonya, "Najua kwamba baada ya mimi kuondoka, mbwa-mwitu wakali wataingia kati yenu na wasilihurumie kundi. Hata katika hesabu yenu wenyewe watainuka watu na kupotosha kweli ili kuwavuta wanafunzi wawafuate. Kwa hiyo jihadharini!" (Mst. 29-31).

Kwa hiyo ni lazima uwe macho dhidi ya manabii wa uongo na walimu wa uongo wanaotaka kuliteka kanisa. Ni lazima uwatambue hawa "mbwa-mwitu waliovaa mavazi ya kondoo" na kuwakabili kwa ujasiri. Ikibidi, kwa kushirikiana na uongozi wa kanisa, wafukuze kutoka katika kusanyiko. Fanya vivyo hivyo na wanaoendelea kusumbua na wenye kusababisha mgawanyiko katika kanisa (Rum. 16:17).

Zaidi ya hayo, ni lazima uwalinde watu wa Mungu dhidi ya mafundisho ya uongo na walimu wa uongo kwa kuwaonyesha ukweli. Hivyo hawatakuwa "tena watoto wachanga, wakitupwa huku na huku na mawimbi, na kupeperushwa huku na huku na kila upepo wa mafundisho na kwa hila za watu katika udanganyifu wao." Badala yake, "watakua katika kila jambo na kuwa mwili uliokomaa wake yeye aliye kichwa, yaani, Kristo" (Efe. 4:14-15).[2]

*3. Kuwafikia wanaoumia.* Yesu aliwafikia watu walioumizwa kwa huruma sana (Mt. 9:36; 15:32-38). Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufanye vivyo hivyo. Ni lazima uwafikie walio dhaifu kwa upendo, wanyonge na wanaoteseka walio kanisani mwako na katika jumuiya. Hii inaweza kuhusisha wajane na walio yatima (Yakobo 1:27). Vile vile inaweza kuhusisha wagonjwa, maskini, walio gerezani, na wengine wenye uhitaji (Mt. 25:38). Yesu anatutia moyo, "Amin, nawaambia, lo lote mtakalomfanyia mmoja wa hao ndugu zangu walio wadogo, mmefanya kwa ajili yangu" (Mst. 40).

Utahitaji pia kutembelea walio wagonjwa majumbani mwao, waliokata tamaa, waliorudi nyuma, au wanaosumbuliwa na mapepo. Huko, utawahudumia kulingana na mahitaji yao. Unapaswa pia kuwatembelea washirika wa kanisa waliolazwa hospitalini au kufungwa gerezani. Chukua muda wa kuomba nao na kuwatia moyo. Unaweza pia kupanga saa maalum za ofisi ambapo unapokea watu wenye matatizo au mahitaji ya ushauri. Huko, utasikiliza matatizo yao kwa

[2] Kwa habari zaidi juu ya kulinda kanisa, tazama Sura ya 27: "Kulilinda Kundi."

makini, utaomba nao, na kuwasaidia kupata ufumbuzi wa mambo yao kutoka katika Neno la Mungu.[3]

*4. Kuimarisha wanyonge.* Katika kila kusanyiko kuna wale walio dhaifu kiroho. Kwa sababu hii, mwendo wao na Bwana hauwi imara. Wengine, kwa sababu ya kutokomaa kiroho, au kwa sababu nyinginezo, wako katika hatari ya kupeperushwa, waondoke kwa Bwana. Unapaswa kuwa macho kila wakati kwa wale walio katika hali hii hatari. Unapaswa kutafuta njia za kuwatia moyo na kuwatia nguvu katika kutembea kwao na Bwana. Njia moja ya kufanya hivyo ni kumpa Mkristo mwenye nguvu wajibu wa kufanya urafiki na kuwatia moyo. Njia nyingine ni kuhakikisha kwamba wamejazwa na Roho Mtakatifu. Roho atakuwa msaidizi kwao, mfariji, na kiongozi.[4]

*5. Kutafuta waliopotea.* Yesu alishuhudia kwamba alikuja "kutafuta na kuokoa waliopotea" (Lk. 19:10). Aliwaagiza wanafunzi wake kufanya vivyo hivyo (Mk. 16:15-16; Lk. 14:23). Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufuate mfano wa Bwana. Lazima uwashuhudie waliopotea, na uwaongoze watu wako kufanya vivyo hivyo. Zaidi ya hayo, ni vizuri kanisa lako liwe na mpango kwa ajili ya uinjilisti unaowezeshwa na Roho, upandaji makanisa, na umisheni.

Kwa hiyo utahitaji kuhubiri na kufundisha mara kwa mara juu ya hitaji la watu kumjua Kristo kama Mwokozi. Na ni vizuri uwakumbushe watu wa Mungu mara kwa mara wajibu wao wa kuwafikishia Injili waliopotea. Unapaswa pia kuanzisha utaratibu na mipango ya kuhamasisha na kuandaa watu kwa ajili ya ushuhudiaji. Mtu mmoja amesema, "Njia bora ya mchungaji kuwatia moyo watu wake kushuhudia ni yeye mwenyewe kuwa mshuhudiaji." Watu wanapomwona mchungaji wao akiwaleta waliopotea kwa Kristo mpaka kuwafikisha kanisani, watatiwa moyo kufanya vivyo hivyo.[5]

*6. Kuwaadibisha waliokwenda kombo.* Nidhamu ni sehemu muhimu ya kutunza kondoo. Ni njia iliyowekwa kibiblia ya kuwarudisha zizini waliopotea. Washirika walioasi wanapofanya dhambi, lazima waonywe. Ikiwa watatubu, ndugu husika watakuwa wamerejeshwa kwa Kristo. Wakikataa kutubu, inabidi

---

[3] Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma ya ushauri ya mchungaji wa Kipentekoste, tazama Sura ya 26: "Kuwashauri Watu wa Mungu."

[4] Kwa maelezo zaidi juu ya kuwaongoza washirika wa kanisa katika utimilifu wa Roho, tazama Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

[5] Kwa habari zaidi kuhusu kuwafikia waliopotea, tazama Sura ya 37: "Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti" na Sura ya 39: "Kupanda Makanisa Mapya."

waadhibiwe (Mt. 18:15-17). Hayo yatafanikisha mambo mawili: Kutumika kumshtua na kumwamsha aliyerudi nyuma, na kuwaonya wengine katika kanisa.

Kumbuka, siku zote lengo la adhabu ni ukombozi. Lazima adhabu itolewe kwa roho ya unyenyekevu na upendo. Paulo aliandika hivi, “Ikiwa mtu amenaswa katika uovu, ninyi mnaoishi kwa Roho mnapaswa kumrejesha mtu huyo kwa upole. Bali jiangalieni wenyewe, msije nanyi mkajaribiwa pia” (Gal. 6:1).

**Kuunda Jumuiya Inayojali**

Kama mchungaji wa Kipentekoste, si lazima wewe peke yako tu uwajali watu, lakini kama ilivyosemekana hapo juu, lihimize kanisa kufanya vivyo hivyo. Jitahidi kukuza kanisa lako kuwa jumuiya inayojali kweli. Kuwa jumuiya inayojali humaanisha kwamba mioyo ya washirika imejawa na huruma kwa ajili ya wanaoumia. Kwa kuwa wamejawa na upendo wa Mungu, itakuwa kawaida kuwafikia wale walio na uhitaji. Wanapomwona ndugu au dada anayeumia, wanaitikia mara moja kwa huruma. Ndivyo Yesu alivyofanya alipokutana na mtu mwenye ukoma. Yule mtu akamwambia Yesu, “Ukipenda waweza kunitakasa.” Biblia inatuambia, “Yesu akijawa na huruma, akaunyosha mkono wake akamgusa mtu huyo. 'Niko tayari,' alisema. ‘Takasika!’ ” (Mk. 1:40-42 , maelezo ya pembeni ya mstari husika).

Njia moja ya kuwafanya watu wa Mungu kuwa jumuiya inayojali ni kuhakikisha kwamba wamejazwa na Roho Mtakatifu na kwamba Roho anafanya kazi kwa nguvu katika maisha yao. Upendo ni tunda la Roho (Gal. 5:22). Biblia inasema, “Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa mioyoni mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu tuliyepewa” (Rum. 5:5). Pia, watu wanapotazama huruma inayoonyeshwa katika maisha ya mchungaji wao, watakuwa na huruma pia.

Kwa kadiri ya hali halisi, na jinsi Roho anavyoongoza, utataka kuliongoza kanisa kuanzisha mpango wa kuonyesha huruma za watu. Ni pamoja na kulisha wenye njaa, kusaidia upatikanaji makazi, na mipango mingine.[6]

## WAJIBU WA MCHUNGAJI

Kama tulivyokwisha ona, ni vizuri wachungaji wa Kipentekoste wajione kama mawakili, au walezi, wa kanisa la Kristo. Hawapaswi kusahau kamwe kwamba kanisa si mali yao; ni mali ya Yesu. Kama wasimamizi wa kanisa Lake,

---

[6] Hili limejadiliwa kwa undani zaidi katika Sura ya 38: "Kutumikia Jumuiya."

wanawajibika Kwake. Ni lazima watekeleze wajibu wao kwa uaminifu, kwani siku moja Kristo atakaporudi watatoa hesabu jinsi walivyosimamia mali yake (Lk. 12:42-43; 1 Kor. 4:2).

Wale wachungaji wanaojijali wenyewe kwa ubinafsi na kupuuza kundi watahukumiwa vikali. Katika Agano la Kale na Agano Jipya, Biblia inashutumu vikali wachungaji kama hao. Ezekieli alitabiri hivi juu ya wachungaji waliojinenepesha kwa gharama ya kondoo: "Hukumtia nguvu aliye dhaifu, wala kumponya mgonjwa, wala kumfunga aliyejeruhiwa; Hukuwarudisha wala kuwatafuta waliopotea" (Eze. 34:4). Kisha, akizungumza kupitia kwa nabii, Mungu alitangaza, "Mimi ni juu ya wachungaji na nitawafanya watoe hesabu kuhusu kundi langu" (mst. 10). Mahali pengine Mungu aliwasema wachungaji wa Israeli kama ifuatavyo: "Kwa kuwa mmetawanya kundi langu, na kuwafukuza, wala hamkuwajali, nitawaadhibu kwa ajili ya uovu mlioutenda" (Yer. 23:23). Mungu aliwaagiza wachungaji wa Israeli kuwa waangalifu sana.

Katika Agano Jipya, Yakobo anaonya hivi, "Wengi wenu msiwe waalimu ndugu zangu, kwa maana mnajua kwamba sisi tufundishao tutahukumiwa zaidi" (Yak. 3:1). Petro anaandika kuhusu manabii na walimu wa uwongo, "Wataingiza kwa siri mafundisho mapotofu yenye uharibifu, hata wakimkana Bwana aliye Mkuu, aliyewanunua, wakijiletea uharibifu upesi" (2 Pet. 2:1).

Ingawa Mungu atawahukumu wachungaji wasio waaminifu, Yeye atawapa kwa ukarimu mkubwa thawabu wale wanaowatunza kondoo kwa uaminifu. Yesu akasema, "Ni nani basi yule mtumishi mwaminifu na mwenye busara, ambaye bwana - mkubwa amemweka juu ya watumishi katika nyumba yake ili awape watu chakula kwa wakati wake? Itakuwa heri kwa mtumishi yule ambaye bwana wake atakaporudi, atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambia, atamweka juu ya mali yake yote" (Mt. 24:45).

Akiwaandikia wazee wa makanisa, Petro alionya hivi: "Iweni wachungaji wa kundi la Mungu lililo chini ya uangalizi wenu, na kuwalinda, si kwa sababu ni lazima, bali kwa kuwa mko tayari, kama Mungu apendavyo; si kutafuta faida ya dhuluma, bali kutumika kwa bidii. Si kwa kujifanya mabwana juu ya hao waliowekwa chini yenu, bali kuwa vielelezo kwa kundi" (1 Pet. 5:2-3). Kisha akawatia moyo, akisema, "Na Mchungaji Mkuu atakapotokea, mtaipokea taji ya utukufu ambayo haitakauka kamwe" (mst. 4).

---

Kumtumikia Kristo kama mchungaji wa kundi lake ni heshima na wajibu mtakatifu. Wachungaji wanaotimiza wajibu wao kwa uaminifu wanaweza kutazama siku zijazo kwa furaha na matarajio makubwa. Siku moja watasikia maneno ya Bwana wao akisema, “Vema, mtumishi mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu kwa machache; Nitakuweka juu ya mambo mengi. Njoo ushiriki furaha ya bwana wako!” (Mt. 25:21).

## ~ Sura ya 25 ~

# Kuuimarisha Mwili

Mhubiri mashuhuri aliendesha mkutano mkubwa wa uinjilisti katika nchi moja ya Afrika ya Kati. Makumi elfu walihudhuria mkutano huo, na maelfu waliitikia mwaliko wa kumpokea Kristo kama Mwokozi. Kulikuwa na furaha kubwa katika jiji hilo ambako mkutano ulifanywa.

Miaka mitatu baadaye, ufuatiliaji wa matokeo ulifanyika. Iligunduliwa kwamba, kati ya maelfu waliokiri imani wakati wa mkutano husika, ni wachache tu waliobakia makanisani. Aliposikia hivyo, kiongozi mmoja wa kanisa alijibu, "Moyo wangu ulisikitishwa na taarifa hiyo. Ndani ya roho yangu nilihisi kwamba kanisa la Afrika lazima litazame tena mbinu za uanafunzi za Yesu. Kanisa la Kipentekoste katika Afrika lazima lielewe kwamba kutangaza injili kamili ni pamoja na mafunzo ya uanafunzi."

Kanisa la Kipentekoste barani Afrika linajulikana sana kwa mafanikio yake ya uinjilisti. Kwa sasa, ni vizuri lijulikane kwa mipango yake ya uanafunzi. Uinjilisti na uanafunzi vinakwenda pamoja. Si lazima mchungaji wa Kipentekoste ajishughulishe mwenyewe na jambo la kukuza kanisa tu. Ni vizuri kujitoa kwa ajili ya kuuimarisha mwili (kanisa). Sura hii itatazama baadhi ya njia ambazo wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unaweza kuimarisha mwili wa Kristo.

## WAJIBU WA MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE

Wajibu mkuu wa kila mchungaji ni kujenga na kuimarisha kanisa analoliongoza. Basi, kila mchungaji wa Kipentekoste lazima awe na lengo la kulifanya kanisa kuwa na nguvu zaidi kuliko wakati walipolipokea. Njia ya msingi ambayo mchungaji anaweza kufikia lengo hili ni kupitia mafunzo ya uanafunzi. Kazi hii ndiyo kiini cha Agizo Kuu, ambapo Yesu aliwaagiza wafuasi Wake kwa kusema, "Nendeni mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (Mt. 28:19). Alikuwa akiwaambia wawafanyie wengine yale aliyowafanyia wao. Kama Yeye, walipaswa kutumia na kuwekeza muda na nguvu zao katika kujenga timu ambayo ingegusa mataifa. Paulo alikazia mkakati huu wa Yesu alipomwagiza mwanafunzi wake Timotheo kama ifuatavyo, "Mambo uliyonisikia nikisema mbele ya mashahidi wengi, yakabidhi kwa watu wenye kutegemeka ambao nao watastahili kufundisha wengine" (2 Tim. 2:2).

### Kuimarisha Kanisa

Paulo alichukulia kwa uzito sana amri ya Yesu ya kufanya watu kuwa wanafunzi. Sehemu kubwa ya huduma yake ya kitume ilitolewa mahsusi kuimarisha makanisa aliyokuwa amepanda. Hii ndiyo sababu aliwateua wachungaji katika makanisa (Mdo. 14:23), akatembelea tena makanisa aliyoyapanda (15:41), na kuwaandikia barua za ufuatiliaji akiwafundisha njia za Bwana. Paulo alishuhudia zaidi kwamba Bwana alikuwa amempa mamlaka yake ya kitume ya kujenga makanisa (2 Kor. 10:8; 13:10). Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uangalie huduma yako kwa usahihi. Ni lazima ujione kama kiongozi mtengeneza wanafunzi katika kanisa ambalo Kristo amekupa kuliongoza.

Katika barua yake kwa Wakristo wa Efeso, Paulo alisema kwamba Kristo alitoa wachungaji (pamoja na karama nyingine nne za huduma) ili kuimarisha mwili wa Kristo (Efe. 4:11-16). Katika mistari hii, mtume anabainisha kwamba jukumu la msingi la hao watumishi ni "kuwatayarisha watu [wa Kristo] kwa ajili ya kazi za huduma" (mst. 12). Wanapaswa kufanya hivyo "ili mwili wa Kristo ujengwe, mpaka sisi sote … tuwe watu wazima" (mst. 12-13). Kisha, Paulo alieleza kwamba kanisa hatimaye litakua "hata kuwa mwili mkomavu katika kila namna yake yeye aliye kichwa, yaani, Kristo" (mst. 15).

Kwa hivyo kufanya wanafunzi ni kitu muhimu kwa afya ya kanisa lolote. Ikiwa uongozi wa kanisa utashindwa kufanya watu kuwa wanafunzi, juhudi zao nyingi katika uinjilisti na upandaji makanisa zitakuwa bure.

**Kuelewa Utaratibu**

Ili kuelewa vyema mchakato wa kufanya wanafunzi, ni muhimu kwamba tuelewe maneno yanayotumika. Hebu tuangalie maneno matatu kati ya hayo:

*1. Mwanafunzi.* Mwanafunzi ni mtu aliyejitoa. Ni yule anayekaa miguuni mwa mwalimu mkuu akipokea maneno yake kwa umakini mkubwa. Kama mwanafunzi, yeye hujifunza kazi kwa kumwiga fundi stadi. Mwanafunzi wa Kristo ni mtu aliyekabidhi maisha yake kwa Yesu Kristo na anamfuata kila siku, akijifunza kutoka Kwake, na kufuatilia utume Wake.

*2. Uanafunzi.* Uanafunzi ni mchakato wa kuwa kama Yesu kwa kipindi cha maisha yote. Huanza pale mtu anapokabidhi maisha yake kwa Kristo na kuendelea hadi kifo. Dhana ya ufuasi ni mada kuu ya Agano Jipya. Wakati neno Mkristo linaonekana mara tatu tu katika Matendo ya Mitume, na neno muamini kutokea mara 35 katika Injili na Matendo, neno mwanafunzi linatokea mara 289 katika Injili na mara 13 katika Matendo.

Ufuasi unahitaji kujitoa kwa Kristo na utume Wake. Yesu alionya umati uliomfuata, “Yeyote asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata hawezi kuwa mfuasi wangu” (Lk. 14:27). Aliwaambia kwamba walitakiwa kuhesabu gharama kabla ya kuwa wanafunzi Wake. Alionya hivi: “Wale kati yenu wasioacha kila kitu mlicho nacho hawawezi kuwa wanafunzi wangu” (mst. 33).

*3. Mfanya wanafunzi.* Mfanya wanafunzi ni yule aliyejitolea kutii amri ya Kristo ya “kufanya wanafunzi kutoka katika mataifa yote” (Mt. 28:19). Yeye ni mfuasi mkomavu wa Yesu Kristo ambaye amejitolea kumfuata Bwana wake kikamilifu na kuwaongoza wengine kufanya vivyo hivyo. Wachungaji wa Kipentekoste wenye ufanisi wanaelewa kwamba kazi yao si kuongoza watu kuongoka tu. Kazi yao ni kuwakuza waamini kuwa wanafunzi waliojitoa kikamilifu wa Kristo.

## NJIA ZA KUIMARISHA KANISA

Kristo hakukusudia kamwe kazi ya ufalme wa Mungu ifanywe na watumishi waliofundishwa huduma peke yao. Alitoa karama tano za huduma kwa Kanisa ili kutoa mafunzo kwa Wakristo wa kawaida wafanye huduma kila siku katika

maisha ya ufalme na utumishi. Kusudi la mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji, na waalimu ni kuwakuza Wakristo kuwa wanaovuna roho, na kisha kuwafundisha jinsi ya kutunzana wao kwa wao, na kila mmoja kukuzwa katika kumtumikia Kristo kwa ufanisi (Efe. 4:11-16).

Kwa hiyo kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufundishe kwamba kila mfuasi wa Kristo ameitwa na kutiwa nguvu kushiriki kuendeleza ufalme wa Mungu duniani. Ingawa ni wachache walioitwa kuwa mitume, kila mmoja ameitwa kushiriki katika umisheni. Ingawa ni wachache walioitwa kuwa manabii, kila mmoja ameitwa kusimamia kilicho kizuri na sahihi. Ingawa ni wachache walioitwa kuwa wainjilisti, kila mmoja ameitwa kuwashirikisha wengine imani. Ingawa ni wachache walioitwa kuwa walimu, kila mmoja ameitwa kuwafundisha wengine jinsi ya kumtumikia Kristo. Ingawa ni wachache walioitwa kuwa wachungaji, kila mmoja ameitwa kuwajali wengine kwa upendo. Kazi yako wewe kama mchungaji ni kufundisha mambo haya kwa watu wa Mungu na kuendeleza mpango wenye uhakika kwa ajili ya mafunzo ya ufuasi kanisani.

Hebu tuangalie mbinu sita unazoweza kutumia kuimarisha kanisa lako.

**Kuonyesha Uanafunzi Ili Kuigwa**

Kwanza, unaweza kuimarisha kanisa kwa kuiga maana ya kuwa mfuasi halisi wa Kristo. Kwa maisha yako mwenyewe, unaweza kuonyesha jinsi mfuasi wa kweli anavyoonekana. Washirika wa kanisa wanapotazama maisha ya mchungaji wao, watatiwa moyo kuishi vivyo hivyo. Wao pia watataka kuwa wanafunzi wa Kristo. Matokeo ni kwamba kanisa litakuwa na nguvu na kufanikiwa, na ufalme wa Mungu utasonga mbele.

Mkakati huu wa ufuasi ni muhimu, hasa katika kuanzisha makanisa mapya kwenye sehemu ambazo hazizafikiwa na Injili. Katika hali hizi, Wakristo wapya hawajui hata kidogo maana ya kuishi kwa ajili ya Kristo. Mifano pekee waliyo nayo ya maisha ya Kikristo ni mfumo wa maisha ya mchungaji na familia yake. Kama Paulo, ni lazima uwe tayari kuwaambia watu, “Fuateni mfano wangu, kama na mimi ninavyofuata mfano wa Kristo” (1 Kor. 11:1).

**Kuhubiri na Kufundisha**

Pili, unaweza kuimarisha mwili kupitia mahubiri ya kimkakati na kufundisha Neno la Mungu kwa mpangilio. Kuhubiri Neno la Mungu kimkakati ni kuandaa na kuhubiri jumbe za kibiblia kwa lengo lililo wazi. Ili kufanya hivyo, lazima kwanza uamue, kupitia maombi na kutafakari Neno, mwelekeo ambao Roho

Mtakatifu analiongoza kanisa. Unapokaa katika maombi, Roho Mtakatifu atazungumza na moyo wako, akisema, “Njia ni hii; ifuateni” (Isa. 30:21).[1]

Mara tu unapotambua mwelekeo wa Mungu kwa ajili ya kanisa, anza kutayarisha na kuhubiri mahubiri yanayolenga kulielekeza kanisa katika mwelekeo huo. Wakati huo huo, hakikisha kwamba "mapenzi yote ya Mungu" - yaani, Neno kamili la Mungu - yanafundishwa kanisani (Mdo. 20:27). Uzoefu huu utahakikisha kwamba watu wa Mungu wanaelewa Neno la Mungu na mapenzi yake kwa ajili ya maisha yao.[2]

Zaidi ya hayo, mafundisho na mahubiri yako lazima yawe na jumbe za mara kwa mara kuhusu utume wa Mungu pamoja na wajibu wa kanisa kushiriki katika utume huo. Utume wa Mungu ambao wakati mwingine huitwa *missio Dei*, ni mpango wa milele wa Mungu wa kukomboa na kuwaita kwake watu kutoka kila kabila, lugha, na taifa duniani (Uf. 5:9; 7:9). Yesu alisisitiza wajibu wa Kanisa katika kutimiza utume wa Mungu katika Agizo Kuu (Mt. 28:18-20; Mk. 16:15-18; Lk. 24:46-49; Yoh. 20:21-22; Mdo. 1:8).

**Kuwawezesha Washirika**

Tatu, unaweza kuimarisha mwili kwa kuhakikisha kwamba washirika wa kanisa lako wamewezeshwa kwa ajili ya huduma. Hii ni pamoja na uwezeshaji wa kiroho na kisaikolojia.

*Uwezeshaji kiroho*. Lazima ujitahidi kuona kwamba kila mshirika wa kanisa ametiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Hii ilikuwa amri ya mwisho ya Yesu kwa Kanisa. Muda mfupi tu kabla hajapaa mbinguni, Yesu aliwaamuru wanafunzi wake hivi: “Msiondoke Yerusalemu, bali ingojeni zawadi ambayo Baba yangu aliahidi, ambayo mmenisikia nikizungumza juu yake. Kwa maana Yohana alibatiza kwa maji, lakini baada ya siku chache ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu” (Mdo. 1:4-5). Kisha Yesu akawapa wanafunzi Wake ahadi ya kushangaza: “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na Uyahudi wote, na

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 15: “Tabia Imara ya Ibada Binafsi.”

[2] Kwa habari zaidi kuhusu mada hii, tazama Sura ya 16: “Mahubiri Yenye Upako wa Roho” na Sura ya 17: “Kufundisha kwa Ufanisi.” Mitaala ya uanafunzi inayoitwa *Living the Truth* na *Roots of Faith* inaweza kupakuliwa bila malipo kwenye tovuti ya https://africaatts.org/resources/.

Samaria, hata mwisho wa nchi" (mst. 8). Wanafunzi walitii amri ya Kristo, na Yesu alitimiza ahadi yake. Biblia inatuambia hivi,

> "Ilipofika siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Ghafla, sauti kama ya upepo mkali ikatoka mbinguni, ikajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Wakaona kama ndimi za moto zilizogawanyika na kutua juu ya kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowawezesha." (Mdo. 2:1-4)

Uwezeshaji huu wa kimungu ndio ufunguo wa uinjilisti wenye ufanisi na umisheni katika kanisa. Kwa hiyo ni lazima uhubiri mara kwa mara juu ya mada hii na kuomba pamoja na watu wako ili wajazwe Roho Mtakatifu.[3] Wafundishe zaidi jinsi ya kuishi na kutembea katika nguvu za Roho. Na uwatie moyo kukuza tunda la Roho na kudhihirisha karama za Roho katika maisha na huduma zao (Gal. 5:22-23; 1 Kor. 12:8-10).[4]

*Uwezeshaji kisaikolojia*. Kama mchungaji, lazima pia uhakikishe kwamba washirika wa kanisa lako wamewezeshwa kisaikolojia kwa ajili ya huduma. Washirika wanawezeshwa kisaikolojia wanapoamini kuwa mlango uko wazi kwao kushiriki katika huduma za kanisa. Wamepewa uhakika kwamba wanaweza kufaulu katika huduma waliyochagua. Kama mchungaji wa Kipentekoste, ni kazi yako kuingizaa imani kama hiyo kwa watu.

Ukifanya hivyo, washirika wa kanisani watahimizwa kujitoa kwa ajili ya huduma. Ila ukishindwa kufanya hivi, watasita kujitoa. Basi epuka kuonyesha kwamba wewe tu katika kanisa ndiye unastahili kufanya huduma. Badala yake, sisitiza kwamba kuna nafasi ya kila mtu kufanya huduma. Ingiza katika mioyo ya watu uhakikisho kwamba wanaweza kuhudumu kwa ajili ya Kristo ipasavyo.

---

[3] Kitabu, *Kuitangaza Pentekoste: Mihutasari 100 ya Mahubiri Kuhusu Nguvu za Roho Mtakatifu*, kinaweza kupakuliwa bila malipo kutoka tovuti ya www.DecadeofPentecost.org. Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuomba pamoja na waamini ili kupokea Roho, tazama Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

[4] Kwa ufafanuzi wa karama za kiroho, ona Nyongeza ya 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

**Kuhamasisha Watenda Kazi**

Baada ya watu kuwezeshwa, ni vizuri wahamasishwe kwa ajili ya huduma. Hii ni njia ya nne ya kuimarisha kanisa. Mchakato wa kuhamasisha watenda kazi ni pamoja na shughuli zifuatazo:

*Kutambua hitaji.* Unaanza mchakato wa uhamasishaji kwa kutambua hitaji unalotaka kushughulikia. Je, kanisa linataka kuzindua huduma mpya ya watoto, kupanda kanisa jipya, kuboresha ibada za kanisa, au kukamilisha kazi nyingine? Lazima uanze mchakato wa uhamasishaji kwa kufafanua vizuri na kwa uwazi kile unachotaka kuona kikikamilishwa.

*Kutengeneza fursa za huduma*. Ni lazima uamue ni nafasi zipi zinafaa kutengenezwa ili kuhudumu katika huduma mpya. Unapaswa kutayarisha maelezo ya kuongoza majukumu kwa kila nafasi mpya. Maelezo hayo yaonyeshe sifa za kazi hiyo na majukumu yake atakayeshikilia nafasi hiyo.

*Kuomba*. Muda wote huo, unapaswa kumwomba Bwana wa Mavuno, awatume na kuwaibua watumishi wanaohitajika (Lk. 10:2).

*Kushirikisha maono*. Kwa wakati ufaao, unatakiwa kushirikisha maono hayo kwa kanisa. Waambie watu kuhusu hizo huduma mpya, ukieleza jinsi zitakavyobariki kanisa.

*Kupata watendaji.* Lazima uombe watu wa kujitolea. Sema wazi hiyo huduma itahusisha nini. Pengine uchague watu fulani ambao unadhani wanaweza kufanya kazi vizuri na kuwaagiza waombe kuhusu kujitoa. Pia tafuta kulinganisha vipawa vya mtu na mahitaji ya huduma husika.

*Mafunzo*. Andaa mpango wa mafunzo kwa wale wanaojitolea.

*Ingiza kazini.* Ukishachagua watendaji wapya, na kuwafundisha ipasavyo, waweke kwenye nafasi zao. Sasa wasiliana na hao watumishi wapya, fuatilia maendeleo yao na kuwatia moyo katika kazi. Vile vile, kanisa linapaswa kuwapa hao wafanyakazi vifaa wanavyohitaji ili kutimiza wajibu wao.

**Mafunzo kwa Ajili ya Huduma**

Kama ilivyotajwa hapo juu, unapohamasisha washirika kwa ajili ya huduma, unapaswa kuwa tayari kutoa mafunzo kwa wale wanaojitolea. Watu wana uwezekano mkubwa wa kujitolea ikiwa wanajua wataandaliwa kwa ajili ya kazi hiyo. Mafunzo pia yataongeza sana uwezekano wao kufaulu. Mafunzo haya

yanaweza kufanywa katika semina maalum au kupitia mafunzo kazini. Mafunzo yajumuishe kwa nini kufanya kinachofanywa, na jinsi ya kufanya kazi husika. Watumishi wapya ni vizuri wafundishwe kwa nini huduma ipo na inataka kutimiza nini. Ni lazima pia wafundishwe jinsi ya kufanya kazi vizuri zaidi. Mchungaji anaweza hata kufikiri kuhusu kuanzisha Shule ya Huduma kanisani.5

**Kuwashauri Wanao-onyesha Kutaka Kutumika**

Njia ya mwisho unayoweza kuimarisha mwili ni kwa kutambua na kuwashauri kwa uangalifu wale wanaoonyesha kutaka kutumika. Kama mchungaji, wajali washirika wale wenye kuonyesha bidii ya kipekee kwa kazi ya Mungu. Huenda ukahisi mkono wa Mungu juu ya watu hawa. Hili likitokea, ni vizuri kuanzisha mahusiano nao ya ushauri, kama vile Yesu alivyofanya na wanafunzi Wake. Kisha tumia muda wa kutosha na hao watu kibinafsi, ukiomba pamoja nao na kuwaalika wajiunge nawe katika kazi fulani fulani kihuduma.

Kuna ambao wameona kwamba njia ya Yesu ya uanafunzi ilikuwa na mambo matatu: Kwanza, Yesu aliwahudumia wengine huku wanafunzi Wake wakitazama. Wakati fulani alikuwa akiwachukua kando na kuwaeleza kile alichokuwa amefanya na kwa nini alifanya hivyo. Pili, wanafunzi walihudumu huku Yesu akitazama. Kisha angetathmini kazi yao. Mwisho, Yesu aliwatuma wanafunzi kuhudumu peke yao na kuzalisha wanafunzi wengine kama Yeye alivyowakuza. Aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu ili kuwatia nguvu na kuwawezesha katika huduma.

Baadhi ya wale unaowalea wanaweza kujisikia kuitwa katika huduma. Hili likitokea, utataka kusitawisha wito huo. Na utataka kuwaongoza katika mchakato wa uthibitisho wa huduma.

---

Biblia inafundisha kwamba kanisa “hukua na kujijenga katika upendo, *kila sehemu* ifanyapo kazi yake” (Efe. 4:16, maneno mepesi kukazia). Njia bora ya mchungaji wa Kipentekoste kuimarisha kanisa ni kuendeleza mpango imara wa ufuasi unaolenga kuwageuza waamini kuwa wanafunzi na wanafunzi kuwa wahudumu wa injili wenye ufanisi.

[5] Huduma hii inazungumziwa katika Sura ya 17: “Kufundisha kwa Ufanisi.”

## ~ Sura ya 26 ~

# Kuwashauri Watu wa Mungu

Mshirika mmoja wa kanisa anafikiria talaka baada ya miaka mingi katika uhusiano wa kikatili. Mjane mchanga anapambana na kufiwa na mume wake. Mama mmoja anakabiliana na majibu ya uchunguzi wa saratani. Wazazi waliofadhaika wanajaribu kumdhibiti mtoto wao wa kiume chipukizi, ambaye ameasi. Haya ni baadhi ya masuala mengi sana yanayowakabili washirika wa makanisa yetu ya Kipentekoste kote barani Afrika. Ongeza kwenye hiyo orodha wale wanaopambana na uonevu wa mapepo, umaskini uliokithiri, ukosefu wa ajira, tabia za ulevi, na mengine mengi.

Mungu aliumba wanaume na wanawake kwa mfano wake mwenyewe. Aliwaumba Adamu na Hawa wakiwa wazima kabisa katika mwili, akili, na roho. Walikuwa "kazi bora zaidi ya Mungu," wakiishi kwa uwiano kamili pamoja Naye na wenyewe kwa wenyewe. Lakini walipokosa, uhusiano wao na Mungu na baina yao wenyewe uliathirika (Mwanzo 3:6-24; Rum. 5:12). Hali ya kuharibikiwa na mateso vikawa sehemu ya hali ya mwanadamu.

Ushauri wa kichungaji ndio kitovu cha huduma ya kichungaji. Kristo ameliita Kanisa lake kuwa jumuiya yenye upendo, inayojali. Anataka pawe mahali ambapo watu wa Mungu wanashirikiana Naye na Roho Mtakatifu kuleta uponyaji na utimilifu kwa watu waliovunjika. Kanisa linapaswa kuwa mahali ambapo

waliopotea wanaweza kupata mabadiliko, upatanisho, na tumaini (2 Kor. 5:18-19). Mungu amemuagiza mchungaji wa Kipentekoste kuhakikisha kwamba kazi hii inatekelezwa.

Sura hii itaangazia huduma ya ushauri ya mchungaji wa Kipentekoste katika Afrika. Itajadili sifa stahiki za ushauri wa kichungaji na kuweka msingi wa kibiblia kwa ajili yake. Itatazama zaidi nafasi ya Roho Mtakatifu katika ushauri. Hatimaye, itajadili kwa ufupi aina, kanuni, na maadili ya ushauri wa kichungaji.

## MCHUNGAJI KAMA MSHAURI

Kristo anamwita kila mchungaji wa Kipentekoste kutekeleza agizo la utume la Kanisa. Amemtoa kwa Kanisa ili kuwafinyanga waamini kuwa wanafunzi wanaofaa (Efe. 4:11-12). Zaidi ya kuhubiri, kufundisha, na kuongoza, Kristo ameweka juu ya mchungaji jukumu la kutoa ushauri wa kiungu na msaada kwa washiriki wanaotafuta kumfuata Kristo kikamilifu.

### Mchungaji wa Kundi la Mungu

Huduma Yake ilipokaribia kufikia mwisho hapa duniani, Yesu alimwagiza Petro hivi, "Tunza kondoo wangu" (Yoh. 21:16). Katika hotuba yake ya kuwaaga wazee wa kanisa la Efeso, Paulo alikazia hitaji la wachungaji "kulilinda… kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi wake." Walipaswa kuwa "wachungaji wa kanisa la Mungu, ambalo alilinunua kwa damu yake mwenyewe" (Mdo. 20:28). Vivyo hivyo, Petro aliwataka wazee wa kanisa wawe "wachungaji wa kundi la Mungu" (1 Pet. 5:2). Walipaswa kuwaganga kondoo walioumizwa, wanaotaabika, na waliojeruhiwa.

Wito wa mchungaji wa Kipentekoste kama mshauri si swala la hiari bali ni jukumu la kiungu. Wakati washirika wa kanisa (na wakati mwingine, wasio washirika) wanapopambana na masuala ya kihisia, kijamii, na kiroho, wanapaswa kuwa na uwezo wa kumgeukia mchungaji wao kwa usaidizi. Kama vile mchungaji anavyowalisha, kuwaongoza, na kuwalinda kondoo wake, wachungaji wa Kipentekoste lazima wawajali wale ambao Kristo amewaweka chini yao.

### Uhusiano Maalum

Ikilinganishwa na wataalamu wengine wa afya ya akili, huduma ya ushauri nasaha ya mchungaji ni ya kipekee. Mara nyingi, watu huwachukulia wachungaji kama wawakilishi wa Mungu. Wanawaona kuwa waliotiwa mafuta na kutayarishwa kama vyombo katika mchakato wa uponyaji. Tofauti na wataalamu

wengine wa afya ya akili, lengo la mchungaji ni kuona watu wa Mungu “wakikua katika neema na maarifa ya Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo” (2 Pet. 3:18).

Zaidi ya hayo, wachungaji wana uhusiano imara na wenye kuaminika baina yao na washirika wao. Wanahusika katika maeneo mbalimbali ya maisha ya washirika wao, ikiwa ni pamoja na matatizo yao, hatua muhimu, na mafanikio. Wao huombwa kusimamia sherehe za ndoa, kuweka watoto wakfu, na mazishi. Kwa sababu ya uhusiano huu wa kipekee, washirika wanaweza kumshirikisha mchungaji wao kwa urahisi zaidi maumivu yao bila hofu ya kupuuzwa.

Tena, wachungaji wanafikiwa kwa urahisi zaidi kuliko wataalamu wengine wa afya ya akili. Jamii nyingi hazina washauri wenye ujuzi. Hata wakiwepo, huduma zao mara nyingi ni za gharama kubwa. Tumaini pekee la watu ni mchungaji. Na kama Bwana wao, wachungaji wanasukumwa na huruma kwa "wanaonyanyaswa na wasiojiweza" (Mt. 9:36). Wanaona ushauri kuwa fursa ya kushirikisha upendo wa Mungu kwa wanaoumizwa.

## Ushauri wa Kichungaji

Kote barani Afrika leo, matukio ya ushauri nasaha yanazidi kuongezeka. Kila mmoja hutafuta kukabiliana na hali ngumu maishani. Na kila njia inategemea mtazamo fulani wa dunia na imani. Miongoni mwake kuna mtazamo wa kidunia, kuiona dunia kwa mtazamo wa jadi wa Kiafrika, na kuiona dunia kwa mtazamo wa Kikristo.

Ushauri wa kisaikolojia wa kidunia ni wa kisayansi na mbinu, na mara nyingi hukataa ukweli wa Maandiko. Mbinu hii hutumia mtindo na matibabu mbalimbali kutibu matatizo ya kiakili, kihisia na kitabia. Katika baadhi ya nchi za Kiafrika, mbinu za matibabu za asili za Kiafrika pia zinatambuliwa na kuruhusiwa kufanya kazi pamoja na aina za matibabu za kimagharibi. Mbinu hizi za kimila zinatokana na mtazamo wa Kiafrika wa dunia wenye kuhusisha maisha na uwezo na imani katika nguvu za kiroho zisizoonekana.

Mtazamo wa mchungaji wa Kipentekoste katika ushauri hutofautiana na mtazamo wa kidunia au wa utamaduni wa Kiafrika. Mtazamo wa mchungaji wa Kipentekoste msingi wake ni katika Biblia, wenye kumpa Kristo nafasi muhimu, na wenye kuongozwa na Roho. Basi, ushauri wa kichungaji umejikita katika mamlaka ya Maandiko. Huo unashikilia kwamba Biblia ni Neno la Mungu na kwamba “linafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa

kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki" (2 Tim. 3:16). Kwa kuwa ni Neno la Mungu, Biblia ina majibu ya matatizo yote ya maisha.

## MISINGI YA KIBIBLIA YA USHAURI WA KICHUNGAJI

Mchungaji wa Kipentekoste anaamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililofunuliwa. Kwa hiyo, ni mwongozo wa uhakika wa ushauri. Kama hakuna chombo kingine cha uchunguzi, Biblia inaweka wazi siri za ndani za moyo wa mtu (Ebr. 4:12). Inashughulika na mizizi ya kuharibika kwa wanadamu, na kumwonyesha Yesu Kristo kuwa suluhisho la matatizo yote ya kibinadamu.

Hii ina maana kwamba wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kujitosheleza na kweli zinazopatikana katika Neno la Mungu. Unapaswa kuruhusu ukweli huu kukuongoza zaidi katika huduma yako ya ushauri. Ukichagua kuazima kutoka katika nadharia za kidunia ili kuongeza ujuzi wako wa ushauri, hakikisha kwamba nadharia hizi zinakubaliana na ukweli wa Biblia na maadili ya Kikristo.[1]

### Viongozi wa Agano la Kale

Agano la Kale lina mifano mingi ya viongozi wanaotoa ushauri wa kiungu. Kwa mfano: Musa alitumia muda mwingi sana akiwaamua na kuwashauri watu wa Mungu. Kuna wakati aliwashauri katika makundi makubwa. Nyakati zingine alimshauri mmojammoja au wawili tu kwa mara moja (Kut. 18:13-27). Ila, wakati ulifika ambapo Musa mwenyewe alihitaji ushauri. Mzee Yethro aliyekuwa baba mkwe wake, aliona kwamba analemewa na kazi zake. Basi alimshauri Musa achague watu wenye uwezo wa kumsaidia. Musa alifuata ushauri wa Yethro na kazi ikafanikiwa.

Daudi ni mfano mwingine wa mshauri wa kiungu. Aliwashauri watu katika Zaburi zake. Humo, anatoa mikakati mingi bora ya kushughulikia maswala ya maisha. Hayo hayo yanaweza kusemwa kuhusu Sulemani katika Mithali na manabii katika maandiko yao.

### Huduma ya Yesu

Yesu mwenyewe alikuwa mshauri. Isaya anamwita "Mshauri wa Ajabu" (Isa. 9:6). Mara nyingi alitoa shauri kwa watu waliotatizika katika masuala ya kiroho. Mifano mitatu maarufu ni ushauri kwa Nikodemo (Yoh. 3:1-21), kwa Zakayo (Lk.

---

[1] Kwa mengi zaidi kuhusu uhusiano wa mchungaji wa Kipentekoste na Biblia, tazama Sura ya 9: "Anaiamini Biblia."

19:1-9), na mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi (Yoh. 8:1-11). Yesu alisema, “Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele” (Yoh. 10:10).

Kuna nyakati ambapo Yesu aliwahudumia wale waliokuwa na matatizo ya kihisia na ya moyoni. Mariamu na Martha walipofiwa na kaka yao Lazaro, Yesu alikuja kwao. Alionyesha huruma na kutembea pamoja nao katika huzuni yao (Yoh. 11:17-44). Usiku kabla ya kusulubishwa, Yesu alitumia muda mwingi na wanafunzi wake kuwatayarisha kwa ajili ya jaribu lililokuwa linakuja (Yoh. 14-16).

Huduma ya ushauri ya Yesu iliwagusa watu wa nyanja mbalimbali. Iligusa watu waliosoma na wasiosoma, wenye kujua kuandika na wasiojua, wenye haki na wasiokuwa haki, wasafi na waliotakaswa, na wasio safi na watu wa kawaida, matajiri na maskini, wanaume, wanawake, na watoto. Upendo wa Yesu kwa watu ulimsukuma kuvuka vikwazo vyote vya kiuchumi, kijamii na kitamaduni ili kutimiza utume wake wa kutafuta na kuokoa waliopotea (Lk. 19:10).

**Huduma ya Paulo**

Sehemu za barua za Paulo zinaweza kusomwa kama vipindi vya ushauri. Zinaonyesha hangaiko la kichungaji la mtume kwa watu wa Mungu. Ndani yake, anawashauri wale wanaokabiliana na masuala ya maisha. Kwa mfano: aliwaandikia waamini huko Filipi akiwaambia, “Msihangaike juu ya jambo lolote.” Kama wataomba, wangepata amani ya Mungu (Flp. 4:6-7). Mfano mwingine wa huduma ya ushauri ya Paulo ni jinsi alivyomshughulikia Timotheo mwanafunzi wake, ili kumsaidia kushughulika hali yake ya kutojiamini kibinafsi na kuhusu kujistahi na kujijali (2 Tim. 1:3-14; 2:15).

Katika barua yake kwa Wakristo wa Korintho, mtume alizungumzia mitazamo na tabia fulani mbaya ambazo zilikuwa zikitishia kuharibu kanisa huko. Katika barua yake kwa Filemoni, mtume huyo anatafuta kurekebisha uhusiano uliovunjika kati ya Filemoni na Onesimo, mtumwa wake aliyetoroka, ambaye kwa wakati huo alikuwa ndugu. Ukipitia barua za Paulo kwa kina, utaona kwamba njia yake ya ushauri ilikuwa ya Kristo, iliyoongozwa na Roho, ya kufundisha, ya kutia moyo, kuunga mkono, upatanisho, na wakati mwingine ya majadiliano na utoaji hoja.

## NAFASI YA ROHO MTAKATIFU KATIKA USHAURI

Kama mchungaji wa Kipentekoste, una mshirika mkubwa katika huduma yako ya ushauri. Mshirika huyo ni Roho Mtakatifu. Hupaswi kushindwa

kumtegemea Yeye. Waza kuhusu mwanajeshi anayekwenda vitani bila silaha yake. Anaweza kujua sheria zote na mbinu za kushiriki na mikakati ya vita, lakini bila silaha yake, matokeo yatakuwa mabaya. Vile vile ni upumbavu kwa mchungaji wa Kipentekoste kujitosa katika vita vya kiroho bila nguvu za Roho Mtakatifu.

**Msaidizi**

Mara nne Yesu alimtaja Roho Mtakatifu kuwa *Paraclete*, neno ambalo maana yake ni "Msaidizi" au "Mshauri" katika lugha ya Kiyunani (Yoh. 14:16, 26; 15:26; 16:7). Kama Mshauri wetu wa mbinguni, Roho Mtakatifu anasimama akiwa tayari kutusaidia katika kila hatua ya safari ya ushauri. Akikaribishwa, ataongoza, ataimarisha, na kumsaidia anayefanya ushauri. Naye atamsaidia anayeshauriwa kukabiliana na maumivu na mapambano yake (Yoh. 14:1; 16:8).

Mara nyingi ushauri huhusisha vita vya kiroho (Efe. 6:12). Ni Roho wa Mungu pekee aliye na nguvu za kutosha "kuwaganga waliovunjika moyo" na "kuwatangazia wafungwa uhuru wao" (Isa. 61:1; taz. Lk. 4:17-18). Kwa hiyo Biblia inatuhimiza kuwa "hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake" (Efe. 6:10).

Maombi kwa uaminifu, yaliyojaa imani, ni sehemu muhimu ya mchakato wa ushauri. Roho Mtakatifu atasaidia katika eneo hili. Biblia inasema, "Roho hutusaidia udhaifu wetu. Hatujui tunapaswa kuomba nini, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkika" (Rum. 8:26). Yesu alisema kwamba Baba wa Mbinguni angempa Roho Mtakatifu yeyote ambaye angemwomba (Lk. 11:9-10, 13).[2]

Yesu ndiye kielelezo kamili kwa mshauri wa Kipentekoste. Biblia inasema kwamba alitiwa mafuta na Roho Mtakatifu ili "kuwaponya wote waliokuwa chini ya nguvu za Ibilisi" (Mdo. 10:38). Kupitia upako huo, alitangaza habari njema kwa maskini, alitangaza kufunguliwa kwa wafungwa, na kuwaweka huru waliokandamizwa (Lk. 4:18). Paulo ni mfano mwingine bora wa kuigwa kama mshauri wa Kipentekoste. Licha ya elimu yake kubwa na mafanikio, alitegemea nguvu za Roho Mtakatifu (1 Kor. 2:4-5). Vivyo hivyo, mchungaji wa Kipentekoste anahitaji msaada wa Roho Mtakatifu ili kuwa mshauri mzuri.

---

[2] Kwa habari zaidi juu ya kuwasaidia waamini kupokea Roho Mtakatifu, tazama Sura ya 20: "Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho."

### Anayefunua Ukweli

Zaidi, Yesu alifundisha kwamba Roho Mtakatifu ndiye mwenye kufunua ukweli wote (Yoh. 16:13). Atatusaidia kuelewa na kufasiri Neno la Mungu. Pia atatupatia ufahamu katika mawazo ya Mungu na mawazo ya wale tunaowashauri (1 Kor. 2:11-12). Hii ni muhimu kwa sababu tabia ya mtu imeguswa na mawazo yake na tafsiri anazoweka juu ya matukio ya maisha. Mtu anayeamini kuwa mabaya yanayozunguka maisha yake ni kutokana na nguvu za uovu na mababu wenye hasira atafanya kwa mwelekeo huo. Roho Mtakatifu atawasaidia kujua ukweli ambao utawaweka huru (Yoh. 8:32).

### Mtoa Zawadi

Matatizo ya afya ya akili ni tofauti, magumu, na yanahusiana na utamaduni. Huhusisha vipengele vya asili na vya kiroho. Kwa hiyo karama za Roho Mtakatifu ni muhimu kwa mchakato wa ushauri (1 Kor. 12:8-10). Kupitia karama za ufunuo, Roho Mtakatifu anaweza kumpa mshauri wa Kipentekoste ufahamu kuhusu mahitaji ya anayeshauriwa. Kupitia karama ya kupambanua roho, Roho anaweza kufichua uwepo na utendaji wa roho za kishetani. Na, kupitia karama za kinabii, mshauri anaweza kusema maneno yaliyovuviwa ya matumaini na uponyaji. Kwa hiyo mchungaji wa Kipentekoste lazima adumu akiwa amejaa Roho Mtakatifu, na kuwa makini na kazi Yake katika kila hatua ya ushauri.[3]

## AINA ZA USHAURI WA KICHUNGAJI

Mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuwa tayari kutoa aina zifuatazo za ushauri:

### Ushauri wa Kiroho

Ushauri wa kiroho unazingatia uhusiano kati ya anayeshauriwa, na Mungu, na mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yake. Hapa, jambo kuu la mchungaji wa Kipentekoste ni kwamba anayeshauriwa afikishwe kwenye uhusiano hai kati yake na Kristo. Lingine muhimu ni kwamba uhusiano huo uwe na afya na unaokua. Masuala mengine yanayohusiana na ushauri ni pamoja na yafuatayo:

---

[3] Kwa maelezo zaidi kuhusu karama za kiroho, tazama Nyongeza ya 2: “Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10.”

- Ufahamu wa mtu huyo kuhusu Mungu kama Baba mwenye upendo na anayejali
- Uelewa wa mtu huyo juu ya maana ya kweli na asili ya wokovu
- Mwenendo unaoendelea wa mtu huyo na Kristo
- Ukombozi kutoka vifungo na hitaji la uponyaji wa ndani
- Kupatanisha maadili ya Kikristo na maisha ya kila siku.

Katika mazingira ya Kiafrika, mwenye kushauri anaweza kuhitaji kushughulika na jitihada za yule anayeshauriwa kuchanganya desturi zake za zamani za Kiislamu na mwendo wa Kikristo. Mazoea haya yanaweza kuwa ni pamoja na matumizi ya hirizi au mazindiko ili kujihakikishia ulinzi juu ya laana na nguvu za giza.

**Ushauri wa Ndoa na Familia**

Ushauri wa ndoa na familia unalenga kukuza maadili ya Kikristo na kuishi kiungu katika familia za washirika. Ushauri wa aina hii unaweza kujumuisha ushauri wa mtu binafsi au kikundi katika semina. Yafuatayo yanahusika:

- Ushauri kabla ya ndoa kwa wawili wanaopanga kuoana
- Ushauri wa kuboresha ndoa kwa wanandoa wanaotaka kuimarisha uhusiano kati yao
- Ushauri wa ndoa kwa wanandoa wanaopitia changamoto katika ndoa zao
- Ushauri kwa wazazi Wakristo
- Ushauri wa kikundi cha familia kusaidia wanafamilia ambao wanatatizika na uhusiano baina ya watu
- Ushauri unaohusiana na mila za kiukoo kama vile ndoa, kuzaa, kifo, na mazishi.

**Ushauri wa Kusaidia Katika Mgogoro**

Ushauri wa usaidizi na wa dharura unalenga kuwasaidia watu kupitia matukio yanayoleta usumbufu na vurugu maishani. Matukio hayo ni pamoja na haya:

- Ugonjwa usiopona au kifo cha mpendwa
- Ukame, njaa, magonjwa ya milipuko na majanga ya asili
- Kuathirika na uhalifu au unyanyasaji
- Ukosefu wa ajira na umaskini.

Katika nyakati hizi ngumu, washirika wanaweza kuhitaji mtu atakayewasikiliza wanaposhughulikia maumivu yao. Ikiwa mchungaji hana jinsi

ya kukabiliana na hali za hatari katika maisha kama vile kujiua na mfadhaiko mkubwa, anapaswa kumpeleka mgonjwa kwa mshauri aliyehitimu.

**Ushauri kwa Ajili ya Ukuaji**

Ushauri wa ukuaji unalenga kuwawezesha watu kufanikiwa maishani. Lengo lake ni kuwasaidia kuamua juu ya njia iliyo bora zaidi. Zaburi na Mithali hutoa maneno mengi ya hekima na ushauri (km. Zab. 32:8; Mit. 15:22).

## KANUNI ZA USHAURI

Tukiangalia vizuri ule mkutano wa Yesu na yule mwanamke Msamaria katika Yohana 4, zinaonyeshwa kanuni nne muhimu za ushauri ambazo mchungaji wa Kipentekoste atataka kutumia.

**Kujenga Kuaminika**

Yesu alianza mchakato wa ushauri kwa kujenga kuaminika kati yake na yule mwanamke. Alionyesha kuheshimu pasipo kuhukumu, na upendo bila masharti, na kukubalika. Alizidi kumfikia kwa kuvuka mipaka ya kitamaduni iliyokuwepo (Yoh. 4:7-9, 17-18).

**Kusikiliza Kikamilifu**

Yesu alitaka kujua hali ya mwanamke huyo kwa kuuliza maswali ya kiuchunguzi. Kisha akasikiliza kwa makini alichokisema yule mwanamke na kumjibu ipasavyo. Majibu yake yaliwasilisha kwa uwazi uelewa Wake wa mahitaji yake ya kina ya kiroho. Yesu alizidi kupingana na ule upofu katika kufikiri kwa huyo mwanamke, uliokuwa ukimzuia kuukubali ukweli na kupata uhuru ndani yake (Yoh. 4:9-16, 21-24).

**Kusema Ukweli Katika Upendo**

Ilipobidi, Yesu alikabili makosa ya yule mwanamke kwa ukweli na kumpinga kwa matamko ya ukweli (Yoh. 4:16-18; taz. Efe. 4:15).

**Kubaki Kwenye Mada**

Katika mchakato mzima, Yesu alidumu na kusimama kwenye lengo lake la kumsaidia huyo mwanamke kugundua kusudi lake la kweli la kuishi (Yoh. 4:10, 13-14, 16-18, 21-24). Mwanamke huyo alikubali dhambi yake na kukiri kuwa Yesu ndiye Masiya. Kisha alikimbia kuwaambia wengine juu yake (Yoh. 4:28-29).

## MAADILI YA USHAURI

Kama wawakilishi wa Kristo na walezi wa watu wake, wachungaji wa Kipentekoste lazima wawe wanaume na wanawake waadilifu. Unapaswa kuzingatia masuala yafuatayo ya kimaadili katika ushauri nasaha. Kuzingatia kanuni hizi kutakulinda wewe na yule anayeshauriwa.

**Elewa Mapungufu ya Mtu**

Lazima uwe mwaminifu kuhusu uwezo wako na mapungufu katika ushauri nasaha, na usijaribu kuvuka mipaka hii. Katika nchi zingine, washauri wa kitaalamu hutakiwa kuthibitishwa na bodi maalum.

**Uwe Tayari Kutuma kwa Wengine**

Lazima ujue unapofikia kikomo chako. Kama hujafundishwa au hujahitimu kutoa ushauri katika maeneo fulani maalum, ni vizuri uwe tayari kuwaelekeza washirika wako kwa washauri wa Kikristo walioidhinishwa. Ushauri unapofikia mahali pa mahusiano tegemezi baina yako na yule unayemshauri, uwe tayari kumtuma kwa mshauri mwingine. Na hata wakati anayeshauriwa hafaidiki tena na ushauri wako.

**Uadilifu wa Kijinsia**

Kama mchungaji, unapaswa kuchukua tahadhari maalum unaposhauri watu wa jinsia tofauti. Ikiwa mvuto wa kihisia unaanza kukua kati yako na anayeshauriwa, vikao vya ushauri vinapaswa kukomeshwa na mtu huyo apelekwe kwa mshauri mwingine.

**Usiri**

Habari yoyote utakayoshirikishwa katika ushauri inapaswa kuheshimiwa na kutunzwa, na kamwe isisemwe kwa wengine.

---

Kama mchungaji wa Kipentekoste, hupaswi kamwe kuacha wajibu wako wa kutumika kama mshauri kwa watu wa Mungu. Unapokuwa na Yesu Kristo kama kielelezo chako, na Roho Mtakatifu kama msaidizi wako, lazima uikubali kwa shauku huduma hii muhimu.

## ~ Sura ya 27 ~

# Kulilinda Kundi

Katika historia, viongozi waovu wametenda uhalifu usioelezeka dhidi ya wanadamu. Uhalifu huu ni pamoja na mauaji ya halaiki, mauaji ya kikabila, na vita visivyo vya haki. Wengine wana hatia ya kutekeleza vitendo hivi vya kikatili; wengine wana hatia ya kutofanya lolote kuzuia hayo. Inasikitisha kwamba Afrika imekuwa na mchango wake katika ukatili huo. Kanuni ya ulimwengu mzima ya utawala bora ni kwamba kila taifa linabeba jukumu la kuwalinda watu wake dhidi ya watenda maovu. Ndivyo ilivyo kwa Kanisa. Linabeba jukumu la kuwalinda watu wa Mungu dhidi ya mashambulizi ya shetani na majeshi yake ya kishetani.

Yesu alionya juu ya manabii wa uongo, ambao alisema, "wanakuja kwenu wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali." Alishauri, "Kwa matunda yao mtawatambua" (Mt.7:15-16). Paulo alitoa onyo kama hilo kwa wazee wa Efeso. Aliwaambia, "Mbwa-mwitu wakali wataingia kati yenu na hawatalihurumia kundi. Hata miongoni mwenu wenyewe watainuka watu na kupotosha kweli ili kuwavuta wanafunzi wawafuate. Kwa hiyo jihadharini!" (Mdo. 20:29-31).

Sura hii itatazama jukumu zito la mchungaji wa Kipentekoste la kulinda kundi la Mungu dhidi ya mawakala hawa wa Shetani. Itajibu maswali haya: "Biblia

inasema nini kuhusu kazi ya mchungaji wa Kipentekoste kulinda kundi?" na "Je, anatekelezaje jukumu hili?"

## ASILI NA THAMANI YA KUNDI

Biblia inatumia picha ya mchungaji na kondoo kueleza uhusiano kati ya mchungaji na watu wake. Ili kuelewa vyema wajibu wa mchungaji wa Kipentekoste kwa kusanyiko lake, ni vizuri kuelewa asili na thamani ya kondoo.

### Asili ya Kondoo

Mchungaji mmoja alilalamika akisema, "Kuongoza watu wangu ni kama kuchunga paka!" Kuchunga paka ni kitu kisichowezekana. Wao ni wakaidi na wanakataa kufuata mwelekeo unaotaka. Si hivyo kwa kondoo. Kondoo ni watiifu. Wako tayari kumfuata mchungaji popote anapowaongoza. Hili ni jambo jema. Hata hivyo, sifa hii ya tabia inaleta hatari kwa kondoo. Kwa ujinga wao, wakati mwingine wao humfuata mtu mbaya. Kwa hivyo wanahitaji utunzaji na ulinzi.

Wakristo wa kweli hujitiisha kwa hiari kwa Mchungaji Mwema. Wako tayari kumfuata popote atakapowaongoza (Yoh. 10:27). Lakini, Wakristo fulani hawajakomaa, na kama kondoo nyakati fulani huchanganyikiwa kati ya mbwa-mwitu wa kiroho na wachungaji wa kweli. Wanawafuata wale ambao si watu wa Mungu wa kweli kwa upofu wao.

Zaidi ya hayo, kondoo hawana ulinzi wa asili. Kwa sababu hii, wako hatarini na wanahitaji mchungaji wa kuwalinda. Na wana mwelekeo wa kutangatanga mbali na usalama wa kundi na uangalizi wa mchungaji. Hii inapotokea, wanakuwa mawindo rahisi kwa wanyama wawindaji. Ndivyo ilivyo kwa Wakristo wengi. Wana mwelekeo wa kutangatanga mbali na uangalizi wa mchungaji wao na usalama wa kanisa. Wanahitaji utunzaji na ulinzi wa mchungaji wa kweli.

### Thamani ya Kondoo

Katika nyakati za Biblia, kondoo walikuwa na thamani kubwa kwa mchungaji. Mara nyingi walikuwa chanzo kikuu cha riziki ya familia. Walikuwa ndiyo nyama ya kuliwa, na walitoa maziwa ili kunywewa, sufu kwa ajili ya mavazi, na ngozi kwa ajili ya makazi na madhumuni mengine. Wakristo wana thamani kubwa zaidi kwa Mchungaji Mwema. Hii ni kweli kwa angalau sababu mbili:

Kwanza, Wakristo ni wa thamani kwa Kristo kwa sababu ya bei kubwa aliyolipa kwa ajili ya ukombozi wao. Yesu alisema hivi juu yake mwenyewe,

"Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo" (Yoh. 10:11). Petro anatukumbusha thamani yetu kwa Kristo: "Kwa maana mnajua ya kuwa mlikombolewa, si kwa vitu viharibikavyo kama fedha au dhahabu,… bali kwa damu ya thamani ya Kristo" (1 Pet. 1:18-19).

Zaidi ya hayo, Wakristo ni wa thamani kwa Kristo kwa sababu ya uhusiano wao maalum Kwake. Kuna wakati walikuwa "wametengwa na Kristo, wametengwa na uraia wa Israeli, na wageni kwa maagano ya ahadi, bila tumaini na bila Mungu katika ulimwengu." Lakini sasa "wameletwa karibu kwa damu ya Kristo" (Efe. 2:12-13). Petro anatukumbusha kwamba watu wa Mungu ni "watu waliochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, milki ya pekee ya Mungu" (1 Pet. 2:9). Kama kundi lililochaguliwa na Mungu, watu wake wanastahili uangalizi wa pekee.

## VITISHO DHIDI YA KUNDI

Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uwe macho kila wakati ili kuwalinda watu wako kutokana na tishio la manabii wa uongo na walimu wa uongo.

### Kuwatambua Manabii Waongo na Waalimu Waongo

Nabii wa uongo ni mtu yeyote anayedai kusema kwa niaba ya Mungu, ingawa ukweli ni kwamba anasema kwa jina lake mwenyewe au kwa jina la mungu wa uongo au roho ya kishetani (Yer. 23:16). Biblia inaonya kwamba Mungu yuko kinyume cha manabii hao wa uongo, na kwamba hawapaswi kuruhusiwa kukaa kati ya watu wa Mungu (Eze. 13:9). Yesu alionya kwamba manabii wa uongo wakati mwingine hata "hufanya ishara kubwa na miujiza" na kwamba wanatishia "kuwapoteza, ikiwezekana, hata wateule " (Mt. 24:24). Paulo aliwaita "mbwa-mwitu wakali" ambao "wanapotosha kweli ili kuwavuta wanafunzi wawafuate" (Mdo. 20:29-30). Aliandika kwamba wanafundisha hadithi na kusema kile ambacho watu wanataka kusikia (2 Tim. 4:3 -4).

Walimu wa uongo ni sawa na manabii wa uongo. Ingawa nabii wa uongo anajifanya kusema kwa niaba ya Mungu, mwalimu wa uongo anapotosha Neno la Mungu bila kujali ili kusema jambo tofauti na maana yake. Mara nyingi hufanya hivyo kwa faida ya kibinafsi (Tito 1:11). Biblia inasema kwamba watu hawa ni wajinga na wasio imara na kwamba wanayapotosha Maandiko kwa uharibifu wao wenyewe (2 Pet. 3:16).

Kuna njia mbili za kutambua manabii wa uongo na walimu wa uongo katika kanisa leo.

*1. Kwa kutazama maisha yao.* Yesu aliwafundisha wanafunzi wake akisema, “Jihadharini na manabii wa uongo. Wanawajia wamevaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali. Kwa matunda yao mtawatambua” (Mt. 7:15-16). Wanajifanya kuwa wasivyokuwa. Wanavaa na kuishi kama watakatifu; wanatumia maneno yote ya kisasa ya kidini, na wanaomba sala zenye kuvutia. Wengine wanaweza hata kufanya miujiza mikubwa. Kwa nje, wanaonekana kuwa watakatifu na wametiwa mafuta. Lakini kwa ndani wao ni wanyang'anyi, waongo, na wazinzi. Matunda ya maisha yao binafsi yanadhihirisha unafiki wao. Hakuna mtu anayeishi maisha yasiyomcha Mungu ambaye ni nabii wa kweli wa Mungu.

Yesu aliwapa changamoto walimu wa uongo wa siku zake: “Ole wenu… wanafiki! Ninyi mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, ambayo kwa nje yanaonekana kuwa mazuri, lakini ndani yamejaa mifupa ya wafu na kila kitu kichafu.… Kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, lakini ndani mmejaa unafiki na uovu.” (Mt. 23:27-28). Waasi hawa wanakataa kutii mamlaka ya Mungu na ya Kanisa.

*2. Kwa kuzingatia nia na mbinu zao.* Njia ya pili ya kutambua manabii wa uongo na walimu wa uongo katika kanisa ni kwa kuzingatia mbinu zao, na yanayowasukuma. Kusudi kuu la nabii wa uongo ni kuendeleza masilahi yake ya binafsi. Ili kufanya hivyo, wanapotosha Neno la Mungu bila kujali. Mara nyingi huondoa maana na kuitumia nje ya mazingira husika, wakizitafsiri kuendana na ajenda zao wenyewe. Kusudi lao ni "kuwavuta wanafunzi wawafuate" (Mdo. 20:30). Wanajali kidogo sana kuhusu wokovu wa wafuasi wao au kukua katika Kristo. Wanajali zaidi faida na utukufu wao binafsi.

**Mafundisho ya Uongo Barani Afrika**

Cha kusikitisha ni kwamba katika makanisa mengi ya Kipentekoste barani Afrika, mafundisho ya uongo na unabii wa uongo ni vitu vinavyo-onekana siku hizi kuwa mambo ya kisasa. Mafundisho haya yanaahidi baraka huku yakipuuza hitaji la imani ya kujitoa na toba kutoka dhambini. Wakizingatia zaidi mahitaji ya watu ya muda, wanapuuza ukuaji wao wa kiroho na ukuaji katika neema. Kwa kufanya hivi, wanashindwa kuwaleta waliopotea kwa Kristo na kuwatayarisha watakatifu kwa ajili ya umilele (Mk. 8:36). Biblia inaonya vikali dhidi ya mafundisho hayo (1 Tim. 4:1).

Mafundisho mawili ya uongo yameenea hasa barani Afrika:

*1. Injili ya mafanikio.* Mafundisho ya kwanza ni ile inayoitwa "injili ya mafanikio." Injili ya mafanikio ni fundisho kwamba waamini wote wana haki ya agano kupokea baraka za afya, mali, na mafanikio. Baraka hizi zaweza kupatikana kupitia imani, ukiri, na kwa kupanda “mbegu kwa imani.”

Ingawa ni kweli kwamba Mungu huwabariki wale wanaomfuata kwa uaminifu, injili ya mafanikio sio injili ambayo Yesu na mitume walihubiri. Yesu aliwaamuru watu, “Tubuni na kuamini habari njema!” (Mk. 1:15). Petro alisema, “Tubuni… mkamrudie Mungu, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa toka kwa Bwana” (Mdo. 3:19). Paulo alionya, “Zamani Mungu alijifanya kama haoni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu” (Mdo. 17:30).

Kanisa la kweli la Kipentekoste lazima likatae injili ya mafanikio kwa sababu ina ubinafsi, badala ya kumzingatia Kristo. Inalenga zaidi tamaa za watu za kimwili badala ya utume wa Mungu wa ukombozi. Mkazo wa injili ya mafanikio ni baraka badala ya huduma. Ni injili potofu ambayo ina madhara kwa Wakristo. Onyo la Paulo kwa Wakristo wa Galatia linafaa hapa: “Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita kuishi katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine — ambayo kwa hakika si Injili hata kidogo… Lakini hata ikiwa sisi au malaika kutoka mbinguni atawahubiri injili tofauti na ile tuliyowahubiria, na wapate laana ya Mungu! (Gal. 1:6-8).

*2. Kuchanganya Ukristo na desturi za kimila (syncretism).* Kitendo kingine cha uharibifu katika makanisa ya Kipentekoste Afrika ni kule kuchanganya mambo ya Kikristo na desturi za kimila (*syncretism*). Huu ni mchanganyiko wa imani ya Kikristo na vipengele vya dini za jadi za Kiafrika. Manabii wa uongo na waalimu wa uongo wakati mwingine hutumia mkakati huu katika kujaribu kuvutia watu wengi zaidi kwenye kanisa lao. Mifano mingi ya hilo inaweza kupatikana kote barani Afrika. Huko Afrika Magharibi, mifano ni pamoja na

- sadaka ya nabii
- sadaka ya ukombozi
- sadaka ya tambiko
- uuzaji na matumizi yasiyo ya kimaandiko ya mafuta ya upako
- kuuza na kutumia maji matakatifu
- uuzaji na utumiaji wa asali na maziwa
- uuzaji wa picha za “mtu wa Mungu”

- matumizi ya ufagio mtakatifu (kuwafagilia mbali maadui zako)
- matumizi ya matope kutoka Bahari ya Chumvi
- matumizi ya maji kutoka Mto Yordani
- kulipia ili kukutana na kushauriwa na nabii.

Matendo hayo ni jaribio la "kufanya kuwa ya Kikristo" desturi za dini za kienyeji. Ni kuhusu pesa na ahadi ya baraka na ulinzi kwa wale wanaozikubali. Ni lazima kukataliwa na kupingwa kwa kukazia "ujumbe wa kweli wa Injili" (Kol. 1:5-6).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, hupaswi kusahau kamwe kwamba mikononi mwako umeshika hatima za milele za wale unaowahudumia. Basi ni lazima ufikirie kwa makini kile unachofanya na kufundisha. Ukishindwa kufundisha ukweli na kukubali kufundisha uongo, watu watapotoshwa, kanisa litaharibika, na wewe utahukumiwa na Mungu.

**Matokeo ya Mafundisho ya Uongo na Unabii wa Uongo**

Mafundisho ya uongo hudhuru kanisa kwa namna tano:

*1. Mafundisho ya uongo yanahimiza kutomcha Mungu.* Ukweli huwatakasa na kuwahamasisha Wakristo kuishi maisha ya kiungu (Yoh. 17:17). Lakini mafundisho ya uongo huharibu akili na moyo, na yanahimiza uasherati (1 Kor. 15:33).

*2. Mafundisho ya uongo huzaa viongozi wasiomcha Mungu*. Kweli huzaa viongozi watumishi wa Mungu, lakini, mafundisho ya uongo hutokeza viongozi wasiomcha Mungu, madikteta. Kiongozi wa kweli wa Kikristo "lazima ashike kwa uthabiti neno la tumaini kama lilivyofundishwa, ili apate kuwatia moyo wengine kwa mafundisho yenye uzima, na kuwakanusha wapingao" (Tito 1:9).

*3. Mafundisho ya uongo huwafanya watu kuwa watumwa.* Ukweli huwaweka watu huru (Yoh. 8:32). Lakini uzushi huwafanya watu kuwa watumwa (Gal. 4:9). Paulo aliwahimiza Wagalatia, "Kristo alituweka huru ili tuwe huru. Basi simameni imara, wala msijiache tena kulemewa na kongwa la utumwa" (Gal. 5:1).

*4. Mafundisho ya uongo huzaa Wakristo dhaifu*. Wakristo wanaofundishwa mafundisho ya uongo na uzushi hawakui katika neema. Wanabaki kuwa watoto wachanga kiroho. Hata kama kanisa linakua kwa idadi, linabaki dhaifu na halifanyi kazi.

*5. Mafundisho ya uongo hupelekea hukumu na uharibifu*. Biblia inazungumza juu ya "watu wasio na ujuzi na wasio imara, wanaopotosha… Maandiko, kwa uharibifu wao wenyewe" (2 Pet. 3:16).

## KULINDA KUNDI

Ukiwa mchungaji wa kundi la Mungu, unapaswa kuwachunga kondoo wakati wote. Inabidi hata uwe tayari kuutoa uhai wako kwa ajili yao (Yoh. 10:11; taz. 1 Sam. 17:34-35). Zifuatazo ni njia tano za wewe kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, kutumia kuwalinda watu wa Mungu:

### Kuwaombea Kondoo

Kwanza, lazima upige magoti mara kwa mara mbele ya Baba kwa niaba ya kusanyiko. Kwa kufanya hivi, utapokea kutoka Kwake nguvu na hekima unayohitaji ili kutunza na kulinda kundi. Tena, maombi yako yatahakikisha kwamba mkono wa ulinzi wa Mungu unabaki juu ya watu wake.

### Kutumia Utambuzi Kiroho

Pili, lazima utumie utambuzi wa kiroho. Biblia inaonya kuhusu "roho zidanganyazo na mambo yanayofundishwa na mashetani" (1 Tim. 4:1). Basi unapaswa kumwomba Mungu karama ya kupambanua roho ili kukusaidia kufunua fundisho lolote au udhihirisho wowote wa kiroho ambao hautoki kwa Mungu. Hii karama ya kiroho itakuwezesha kujua kama mtu kanisani anatenda mambo kwa ushawishi wa Roho Mtakatifu au roho ya kishetani.[1]

### Kufundisha Mafundisho Sahihi

Tatu, ni lazima uhubiri na kufundisha kwa uaminifu mafundisho yenye uzima (2 Tim. 4:2; Tito 1:9). Hii itaimarisha kondoo na kuwakinga dhidi ya mafundisho ya uongo. Itasaidia kuwaweka kwenye njia ya usafi (Zab. 119:9-11).

### Kuwatambua na Kuwafichua Manabii wa Uongo na Walimu wa Uongo

Nne, ni lazima ulitahadharishe kanisa kuhusu manabii wa uongo na waalimu wa uongo. Biblia inazungumza juu ya njia tatu za kuwatambua mbwa-mwitu hao waliovaa mavazi ya kondoo.

---

[1]Kwa maelezo zaidi kuhusu karama za kiroho, tazama Nyongeza ya 2: "Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10."

*1. Unabii wao hautimii.* Ikiwa unabii wao hautatimia, hawajasikia kutoka kwa Mungu. Ni manabii wa uongo (Yer. 28:9).

*2. Wanawaelekeza watu kwenda mbali na ukweli.* Hata kama unabii wao utatimia, ikiwa wanawaelekeza watu mbali na ujumbe wa kweli wa injili, wao ni manabii wa uongo (Kum. 13:1-3; Gal. 1:6-9).

*3. Wanaishi maisha machafu.* Hata kama unabii wao utatimia, na hata wakiweza kufanya ishara za ajabu, kama wanaishi maisha yasiyo ya kumcha Mungu, wao ni manabii wa uongo (2 Pet. 2:10-15). Yesu alionya, "Kwa matunda yao mtawatambua" (Mt. 7:15-16; taz. mst. 22-23).

Kama mchungaji mwaminifu, lazima uwalinde kondoo dhidi ya wanyama wanaowinda wanyama wengine, na kama Bwana anavyofanya na wewe, lazima uwaongoze kwenye njia zilizo sawa (Zab. 23:3).

**Fichua Mafundisho ya Uongo**

Mwisho: ni lazima ulinde kundi la Mungu kwa kutambua na kusahihisha mafundisho ya uongo na unabii wa uongo katika kanisa. Paulo aliandika, "Msiudharau unabii." Lakini akaongeza upesi hivi: "Lakini jaribuni unabii wote; lishikeni lililo jema, kataeni kila aina ya ubaya" (1 Thes. 5:20-22). Kwa hiyo, ukiwa mchungaji wa kundi la Mungu, utahitaji kuendelea kufahamu mambo yanayofundishwa katika kanisa. Kuna njia tatu za kufanya hivyo, nazo ni:

*1. Kufuatilia kinachofundishwa.* Mafundisho ya uongo wakati mwingine yanaweza kuingia kanisani kupitia vikundi vidogo au masomo ya Biblia. Msimamizi wa kikundi huanza kufundisha kitu ambacho amesikia au kusoma mahali. Baada ya muda mfupi, uzushi unasambaa katika kanisa lote. Kwa hiyo, lazima ufuatilie kwa karibu kile kinachofundishwa katika madarasa ya shule ya Jumapili, madarasa ya ubatizo, vikundi vidogo au ushemasi, ushirika wa nyumbani, na vikundi vingine ili kuhakikisha kwamba ukweli unafundishwa.

*2. Kufahamu watu wanachosikiliza*. Siku hizi angani kumejaa mafundisho na mahubiri ya kila aina. Watu wetu wanasikiliza sana vyombo vya habari. Ingawa wahubiri wengi wa vyombo vya habari wanaeneza habari njema kwa uaminifu, wengine wanafundisha makosa. Ni lazima ufahamu kile watu wanachosikiliza ili uweze kuwaelekeza kwenye ukweli wa Neno la Mungu.

*3. Kuwa "mlinzi wa lango."* Kama mchungaji, lazima usimame kama mlinzi wa lango la kanisa lako. Yaani ni lazima uwe mwangalifu unamruhusu nani

kuzungumza na kusanyiko. Si kitu kwamba mhubiri husika ni maarufu au mwenye mvuto. Kama tabia yake si njema kimaadili, au kama amekengeuka kutoka kwenye ukweli, usimruhusu kwenye mimbari yako.

---

Mchungaji wa Kipentekoste mwenye kulilinda kundi la Mungu kwa uaminifu ataleta baraka kwa kanisa na kwake mwenyewe. Kondoo watasitawi chini ya ulinzi wa mchungaji wao, na watakuwa wanafunzi wakomavu wa Kristo. Mchungaji pia atabarikiwa. Atapokea thawabu kwa uradhi wa kujua kwamba wamekuwa watumishi wazuri na waaminifu.

Petro alisema hivi kuhusu thawabu ya mchungaji mwaminifu: "Iweni wachungaji wa kundi la Mungu lililo chini ya uangalizi wenu, mkililinda — si kwa sababu ni lazima, bali kwa sababu mna nia, kama Mungu anavyowataka ninyi; si kwa kutafuta faida ya dhuluma, bali kutumika kwa moyo na bidii. Msiwatawale wale waliowekwa chini yenu, bali muwe vielelezo kwa kundi. Na Mchungaji Mkuu atakapotokea, mtaipokea taji ya utukufu ambayo haitakauka kamwe" (1 Pet. 5:2-4).

## ~ Sehemu ya 7 ~

# Mchungaji wa Kipentekoste Kama Kiongozi

## ~ Sura ya 28 ~

# Uongozi wa Kipentekoste

Paulo na kikundi chake cha wamishenari waliondoka Galatia wakielekea magharibi hadi mkoa wa Asia. Lakini, Roho Mtakatifu aliwazuia kuendelea upande huo. Basi, wakaamua kusafiri kuelekea kaskazini hadi mkoa wa Bithinia. Huko pia Roho akawazuia. Hivyo, kwa mara nyingine tena, waligeukia upande wa magharibi. Mwishowe walifika Troa, jiji lililo pwani ya kaskazini-magharibi ya Bahari ya Aegea. Huko, jambo lisilo la kawaida lilitokea.

Wakati wa usiku, Roho Mtakatifu alimpa Paulo maono. Katika maono hayo, mtume aliona mtu kutoka Makedonia amesimama na kumsihi, "Vuka uje Makedonia utusaidie" (Mdo. 16:6). Paulo aliposhirikisha timu yake hayo maono, wote walikubali kwamba yalikuwa yametoka kwa Bwana. Luka anaeleza: "Baada ya Paulo kuona maono hayo, tulijitayarisha mara moja kuondoka kwenda Makedonia, tukiamua kwamba Mungu ametuita tuwahubirie Injili" (mst. 10). (Mifano mingine ya Paulo akiongozwa na Roho inapatikana katika Mdo. 13:1-5, 15:28, na 20:22.)

Paulo ni mfano mzuri wa kiongozi wa Kipentekoste. Aliwaongoza wengine kwa kumruhusu Roho Mtakatifu amwongoze yeye kwanza. Kwa kufanya hivyo, alikuwa akifuata mfano wa Yesu, ambaye yeye mwenyewe alihudumu chini ya upako na uongozi wa Roho Mtakatifu (Lk. 4:1; Yoh. 5:19; Mdo. 10:38).

Sura hii itatazama uongozi wa Kipentekoste. Itatoa mifano ya uongozi kulingana na mbinu za Yesu na mitume. Kwanza, itafafanua maana ya kuwa kiongozi wa Kipentekoste. Kisha, itatazama baadhi ya sifa na shughuli za viongozi halisi wa Kipentekoste.

## KUFAFANUA UONGOZI WA PENTEKOSTE

Ingawa ni kweli kwamba wachungaji wa Kipentekoste hutumia njia nyingi za uongozi kama wachungaji wasio Wapentekoste, kuna tofauti muhimu. Mtazamo wa mchungaji wa Kipentekoste kwa uongozi unachangiwa sana na uzoefu wake na Roho. Uelewa wao wa kipekee wa jinsi Roho anavyofanya kazi katika maisha yao na maisha ya wengine huathiri sana jinsi wanavyoongoza.

Kiongozi wa Kipentekoste ni mtu aliyechaguliwa na Mungu, ambaye amejazwa na Roho na anayetafuta hekima na mwongozo wa Roho kwa umakini mkubwa. Lengo lake ni kushawishi kundi maalum la watu wa Mungu ili kutimiza kwa uaminifu na kwa ufanisi jukumu lao lililowekwa na Mungu katika kuendeleza utume Wake duniani. Hebu tugawanye hiyo tafsiri katika sehemu nne.

### Ameitwa na Mungu

Kwanza, kiongozi wa kweli wa Kipentekoste ameitwa na Mungu kuwaongoza watu wake. Kwa sababu hii, anajitambulisha kwa ukaribu na Paulo, aliyejieleza kuwa "mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume na kutengwa kwa ajili ya Injili ya Mungu" (Rum. 1:1).

### Amejaa Roho

Kisha, kiongozi wa Kipentekoste amejazwa na Roho na anatafuta kuishi maisha yake "kwa kufuata hatua za Roho" (Gal. 5:25). Huchukulia kwa uzito sana amri ya Kristo kwamba "kaeni humu mjini hata mvikwe uwezo utokao juu" (Lk. 24:49), na maagizo ya Paulo kuhusu "kujazwa na Roho" (Efe. 5:18).

### Anafuta Mwongozo wa Mungu

Tatu, kiongozi wa Kipentekoste hutafuta mwongozo wa Roho kwa bidii katika yote anayofanya. Anaelewa kwamba wajibu wake mkuu ni kutekeleza mapenzi ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika Maandiko na Roho Mtakatifu. Basi, kiongozi wa kweli wa Kipentekoste atatumia muda mwingi katika kujifunza Biblia na katika maombi.

**Ana Ushawishi Watu wa Mungu**

Mwisho, kiongozi wa Kipentekoste hutafuta kushawishi kundi maalum la watu wa Mungu - kama vile kanisa la kitaifa au la mahali pamoja - ili kutimiza kwa uaminifu na kwa ufanisi jukumu lake lililowekwa na Mungu katika kuendeleza utume wa Mungu duniani.

## SIFA ZA KIONGOZI WA KIPENTEKOSTE

Ni nini kinachomfanya mtu kuwa kiongozi wa Kipentekoste? Kwa ufupi tu, kiongozi halisi wa Kipentekoste lazima azaliwe kwa Roho, ajazwe na Roho, na aweze kuwaongoza wengine akienenda na kuwezeshwa na Roho. Lazima aweze kutambua sauti ya Roho na kuwa na ujuzi katika huduma ya karama za kiroho. Lazima aelewe na kujitoa kwa utume wa Mungu. Na ni lazima awe tayari kutoa maisha yake kwa ajili ya Kristo, ikiwa hilo litahitajika.

Kama kiongozi wa Kipentekoste, maisha na huduma yako inapaswa kuwa na sifa sita muhimu, zifuatazo:

**Uadilifu**

Zaidi ya yote, ni lazima ujitahidi kuishi maisha ya utauwa, yanayomheshimu Kristo. Katika kazi ya Mungu, hakuna kitu muhimu zaidi ya hicho. Lakini cha kusikitisha ni kwamba, makanisa na mashirika mengi ya Kipentekoste yamevamiwa na watu mafisadi ambao, kwa sababu ya haiba zao zenye nguvu, wamepata umashuhuri katika harakati hiyo. Hawa "mbwa mwitu waliovaa ngozi ya kondoo" huleta aibu kwa kanisa (Mt. 7:15).

Biblia inazungumza kuhusu watu hao wasiomcha Mungu. Kwa mfano, Paulo aliwaonya wazee wa Efeso kuhusu "mbwa-mwitu wakali" ambao wangeingia na kuliharibu kundi la Mungu (Mdo. 20:29). Katika ujumbe huo huo, aliwakumbusha jinsi yeye alivyowaongoza kwa uadilifu. Alisema, "Sikutamani fedha, wala dhahabu, wala mavazi ya mtu" (Mdo. 20:33). Vivyo hivyo, aliwakumbusha Wathesalonike juu ya mwenendo wake wa kumcha Mungu kati yao, akisema, "Ninyi ni mashahidi, na Mungu pia, jinsi tulivyokuwa watakatifu, wenye haki, na wasio na lawama miongoni mwenu mlioamini" (1 The. 2:10). Paulo hakuongoza kwa mamlaka na kuhudumu kwa nguvu tu bali aliishi kwa uadilifu wa kimungu. Ni lazima tufanye vivyo hivyo leo.

**Uelewa**

Tena, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uelewe waziwazi wajibu wako uliopewa na Mungu. Ni lazima umtumikie Kristo na kanisa lake kwa uaminifu kwa kuwaongoza watu wa Mungu kuendeleza utume wake katika nguvu za Roho Mtakatifu. Unaweza kupata ufahamu huu kutoka vyanzo viwili: Neno la Mungu na Roho wa Mungu. Kwa kujifunza Maandiko kwa uaminifu, utakuja kuelewa utume wa Mungu wa kukomboa mataifa. Kwa kuomba na kuwa makini kuisikiliza sauti ya Mungu, utakuja kuelewa jukumu lako la kipekee katika kutimiza utume huo.

Yesu alielewa wazi nafasi yake katika mpango wa Mungu wa ukombozi. Mara nyingi alizungumza juu ya utume Wake (Mk. 10:45; Yoh. 6:38; 18:37). Alitangaza hivi: "Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea" (Lk. 19:10). Vivyo hivyo, Paulo alielewa jukumu lake la pekee katika kazi ya Mungu. Aliandika hivi: "Mimi niliwekwa niwe mhubiri na mtume … na mwalimu mwaminifu na wa kweli kwa Mataifa" (1 Tim. 2:7).

Kupitia maombi ya kila siku na kujifunza Biblia, wewe, sawa na Yesu na Paulo, unaweza kupata ufahamu mkubwa zaidi wa utume wa Mungu, na jukumu lako binafsi katika kuutimiza.[1]

**Kujitoa**

Vile vile kama kiongozi wa Kipentekoste, hupaswi tu kuelewa utume wa Mungu, lazima ujitolee kikamilifu kufanya sehemu yako ili kutimiza utume huo. Utume wa Mungu, ambao wakati mwingine hujulikana kama *missio Dei*, ni kusudi Lake na kazi yake ulimwenguni kuhusiana na wanadamu walioanguka. Anafanya kazi kupitia Kanisa Lake kuwaita watu kutoka katika kila kabila, lugha, na taifa duniani (Uf. 5:9; 7:9).

Ingawa mawazo ya watu wengine yanaweza kutangatanga kutoka kwenye huo utume, umakini wako lazima ubaki kwenye kufanya mapenzi ya Mungu. Mawazo na matendo yako yote lazima yaende kwenye mwelekeo wa utume wa Mungu. Kama kiongozi wa Kipentekoste, lazima uielewe ile picha kubwa zaidi - mpango wa Mungu wa ukombozi kwa mataifa. Lazima uelewe zaidi mahali

---

[1] Kwa habari zaidi kuhusu utume wa Mungu, tazama kitabu cha Discovery Series cha Africa's Hope kinachoitwa, *Theolojia ya Kibiblia ya Umisheni,* cha Paul York.

ambapo kanisa lako linaungana kwenye mpango huo mkuu. Kisha, lazima ulielekeze kanisa lako kwenda huko kwa uthabiti.[2]

**Upako**

Nne, kama kiongozi wa Kipentekoste lazima uthamini upako wa Roho, na ujitahidi kudumisha mguso wa Roho maishani mwako kupitia maombi ya kujitoa, maisha matakatifu, na huduma ya unyenyekevu. Ni lazima umtegemee sana Roho Mtakatifu akupake mafuta, akuwezeshe, na kukuongoza katika huduma. Lazima uchukue kwa uzito maneno ya Mwalimu alipowaaga wanafunzi wake, na kuwaamuru wasianze huduma zao hadi watiwe nguvu na Roho Mtakatifu (Mdo. 1:4-5; taz. Lk. 24:49).

**Unyenyekevu**

Tano, kama kiongozi wa kweli wa Kipentekoste, lazima ujione wewe ni mtumishi wa Mungu na watu wake. Ni lazima utake kufuata kielelezo cha Bwana wako, ambaye alijinyenyekeza na kuwa mtumishi, mpaka akafa msalabani (Flp. 2:7-8). Na unapaswa kukumbuka maneno ya Yesu: "Yeyote anayetaka kuwa mkubwa kati yenu lazima awe mtumishi wenu, na yeyote anayetaka kuwa wa kwanza lazima awe mtumwa wa wote. Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mk. 10:43-45).

Uongozi wa aina hii unajulikana kama uongozi wa kitumishi. Kinyume chake ni kwamba, kiongozi anayejiinua na kutaka kuwanyonya watu wa Mungu hawezi kamwe kuitwa kiongozi wa kweli wa Kipentekoste. Badala yake ni "mbwa-mwitu waliovaa mavazi ya kondoo" (Mt. 7:15-16; Mdo. 20:29-30). Biblia inatuambia, "Usijihusishe na watu kama hao" (2 Tim. 3:5).[3]

**Ustadi**

Hatimaye, kama kiongozi wa kweli wa Kipentekoste, lazima ujitahidi kupata ustadi. Lazima uelewe kwamba, ingawa kuwa mtu mzuri ni muhimu, haitoshi. Waafrika wanajulikana kwa kuwa wema, wanyenyekevu, na wakarimu. Lakini, ili kuwa kiongozi mzuri, kukuza ujuzi fulani ni muhimu. Stadi hizi ni pamoja na

---

[2] Kwa maelezo zaidi juu ya kuliongoza kanisa katika utume wa Mungu, tazama Sura ya 31: "Uongozi wa Kimisheni."

[3] Kwa ufahamu zaidi juu ya uongozi wa mtumishi, tazama Sura ya 29: "Uongozi wa Kitumishi."

uwezo wa kufundisha, kushirikisha maono, kutia moyo na kuwahimiza wengine, na kupanga kazi.

Zaidi ya hayo, lazima uelewe kwamba mwisho wa siku, uwezo wa uongozi unatoka kwa Mungu. Paulo alifahamu jambo hili kwa uwazi. Aliwaeleza Wakorintho hivi: "Si kwamba tunaweza katika nafsi zetu kujidai cho chote, bali uweza wetu watoka kwa Mungu. Naye ametuwezesha kuwa wahudumu… wa Roho" (2 Kor. 3:5-6). Kama kiongozi wa Kipentekoste, ni lazima kila mara umtazame Mungu kwa ajili ya uwezo huo.

## SHUGHULI ZA KIONGOZI WA PENTEKOSTE

Mchungaji wa Kipentekoste lazima asiwe kama mchungaji aliyeonekana akikimbia nyuma ya kusanyiko lake akipaza sauti, "Ningojeni! Mimi ndiye kiongozi wenu!" Inabidi yeye awatangulie watu, akiwahimiza kumfuata. Ni lazima wawe kama Yesu, aliyewaita wanafunzi wake, "Njooni, mnifuate, nami nitawafanya wavuvi wa watu." Biblia inatuambia, "Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata" (Mk. 1:17-18).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, Kristo amekuteua wewe kuanzisha mpango na mikakati iliyoongozwa na Roho Mtakatifu kanisani. Ni lazima basi uwatie moyo watu wa Mungu kukufuata katika kazi. Wakati huo huo, kama kiongozi mcha Mungu, lazima uwe mfuasi aliyejitoa. Unapaswa kumfuata Roho wa Mungu kwa uaminifu. Nawe unapaswa kunyenyekea chini ya wale ambao Roho amewaweka juu yako. Ni lazima uliongoze kanisa lako ili kutimiza utume wa Mungu kwa njia tatu muhimu.

### Ushirikishwaji Maono

Kwanza, lazima uwaongoze watu wako kwa kushirikisha maono ya mustakabali unaopendelewa wa kanisa. Kwa maneno mengine, ni lazima uwasaidie wawazie wakati ujao mzuri ambao Mungu amepanga kwa ajili yao. Kisha, lazima uwashawishi wapige hatua kuelekea huko. Unafanya hivyo kwa maneno yako, matendo yako, na mitazamo yako, yaani, kwa kile unachosema, unachofanya, na jinsi unavyojionyesha kwa watu.

Maono yako yenye kuongozwa na Roho wa Mungu yanapaswa kuwaka mno ndani yako kiasi cha kutoweza kuyaacha. Matokeo ni kwamba, utazungumza kila wakati juu ya maono. Shauku yako itatiririka toka maishani mwako na kugusa watu, na kuwafanya kushiriki katika hayo maono. Kama kiongozi halisi wa Kipentekoste, hupaswi kamwe kukuza maono yako binafsi ya siku zijazo. Ni

vizuri uendeleze maono ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika Neno Lake na kwa Roho Wake.

Biblia inatuambia, "Pasipo mafunuo watu huacha kujizuia" (Mit. 29:18). Au, kama tafsiri moja inavyosema, "Pasipo maono ya kiunabii watu huvunjika moyo." Kukata tamaa kama hiyo mara nyingi husababisha kujimaliza nguvu, kupungua, na hatimaye kuharibikiwa. Lakini maono yenye kuwasilishwa vizuri yatawafanya watu kuelewa mambo matano:

- Wao ni nani. Ni watu wa kimishenari wa Mungu waliotiwa nguvu na Roho, walioagizwa na Kristo kutimiza agizo Lake duniani.
- Wapi wanapaswa kwenda. Wanapaswa kutembea pamoja ili kutimiza utume wa Mungu kwa kuwashuhudia waliopotea, kuanzisha makanisa mapya, na kushiriki katika kutuma wamishenari kwa mataifa mengine.
- Wanapaswa kufanya nini. Ni lazima watiwe nguvu na Roho wa Mungu na kujitoa kufanya sehemu yao katika kutimiza utume Wake.
- Jinsi wanavyopaswa kufanya. Mchungaji lazima aeleze mpango maalum au utaratibu wa jinsi ya kukamilisha kazi. Kisha awaonyeshe watu jinsi wanavyoweza kushiriki katika kazi hiyo.
- Jinsi wanavyopaswa kuanza. Mchungaji wa Kipentekoste anayefaa atawapa kazi mmoja mmoja ili kuwasaidia kuanza vyema.

Cha kusikitisha ni kwamba ndoto nyingi mchungaji alizopewa na Mungu hufia moyoni mwake. Usiruhusu hilo kutokea. Shirikisha maono kwa uaminifu, yanayohusu mustakabali unaopendelewa wa kanisa. Simama kwa uthabiti na kuwaambia watu kwa ujasiri, "Njia ni hii, ipiteni" (Isa. 30:21).[4]

### Kusimamia

Kati ya kugundua mahali Mungu anapotaka kanisa lako liwe na kufika hapo, kuna njia ambayo lazima uipitie. Kama mwakilishi wa Mungu, lazima uliongoze kanisa katika njia hiyo. Usitoe tu maono ya wakati ujao unaopendelewa na Mungu, lazima pia usimamie kutimizwa kwa maono hayo.

Hivi ndivyo Yesu alivyofanya. Aligawa maono, kisha akatekeleza mkakati wa kutimiza maono hayo. Mkakati wake ulikuwa ni kuwaita watu upande Wake, kuwafundisha, kuwaagiza, kuwawezesha, na kisha kuwatuma kazini. Kama

---

[4] Kwa habari zaidi kuhusu ushirikishaji maono, tazama Sura ya 30: "Uongozi Wenye Maono."

kiongozi wa Kipentekoste, lazima ufanye vivyo hivyo. Unaweza kufanya hivi kupitia mpango unao-ongozwa na Roho Mtakatifu, uhamasishaji, na usimamizi.

Basi, kama mchungaji wa Kipentekoste, hutakiwi kuwatia tu moyo watu wako, unatakiwa kusimamia kazi pia (1 Tim. 3:1-2; Tito 1:7). Kama mwangalizi, unatakiwa kulipanga kanisa kwa ajili ya utume unaowezeshwa na Roho. Lazima kusimamia mbinu na shughuli zinazohitajika ili kutekeleza mpango wenyewe. Hizo shughuli ni pamoja na kuajiri, kupanga, mafunzo, na kuwaingiza kazini watendakazi. Katika haya yote, ni lazima umtazame Roho Mtakatifu atoe ufahamu na mwelekeo.

**Ni Endelevu**

Mwisho ni kwamba, kama kiongozi wa watu wa Mungu, unabeba jukumu la kupanua na kuendeleza maono ya kimishenari ya kanisa. Njia moja ya kufanya hivyo ni kwa kuzaa viongozi wengine wa Kipentekoste wenye maono. Hili lisipofanyika, maono yatakufa, na ule utume utashindwa. Inasikitisha kwamba huduma nyingi sana zilizowekwa na Mungu zimekufa pamoja na waanzilishi wake kwa sababu hao wahusika walishindwa kuwekeza maono ya kutosha ndani ya wengine.

Lakini Yesu alikuwa na bidii ya kurithisha maono Yake kwa wengine. Mara baada ya kuanza huduma Yake, alianza kuita wanafunzi. Biblia inasema, "Akaweka watu kumi na wawili ili wawe pamoja naye na kwamba awatume kuhubiri" (Mk. 3:14; taz. 1:16-17; 2:13-14; 3:13-19). Watu hawa wangeendeleza kazi baada ya Yeye kuondoka. Kwa hiyo aliwazoeza, akawatia nguvu, na kuwatuma waende "kufanya wanafunzi katika mataifa yote" (Mt. 28:19). Kwa maneno mengine, Yesu alitarajia wengine wawafanyie wengine yale aliyokuwa amewafanyia.

Paulo alifuata mfano wa Yesu. Hakutekeleza huduma Yake ya umishenari peke yake, bali alikaribisha na wengine kujiunga naye. Kisha akawashauri na kuwazoeza, kama vile Yesu alivyofanya na wanafunzi wake. Miongoni mwa wanafunzi wa Paulo ni Yohana Marko, Timotheo, Tito, Luka na wengine. Paulo alimwagiza Timotheo kuwafanyia wengine kama yeye alivyokuwa amemfanyia. Alimwandikia hivi mtoto wake katika imani, "Mambo uliyonisikia nikisema, wakabidhi watu wenye kutegemeka ambao nao watafaa kuwafundisha wengine" (2 Tim. 2:2). Ikiwa tunataka kuendeleza maono ndani ya wengine, ni lazima tufuate nyayo za Yesu na Paulo.

Paulo aliwaonya hivi waamini wa Thesalonike, “Ninyi wenyewe mnajua jinsi iwapasavyo kufuata mfano wetu.” Akatoa sababu hii: “tulijitoa wenyewe kuwa kielelezo ili muige” (2 The. 3:7, 9). Ikiwa tunataka kweli kuendeleza leo maono ya utume wa Kipentekoste, ni lazima tuwe watu ambao wengine watataka kutuiga, kama Paulo alivyokuwa. Yaani, tunapaswa kuwa watu wa heshima, uadilifu, na maono.

---

Kama kiongozi wa kanisa la mahali pamoja, aliyeteuliwa na Mungu, ni vizuri uwe bora kadiri iwezekanavyo. Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, fanya bidii kukuza ujuzi wa uongozi unaohitajika ili kutimiza jukumu hili.

~ Sura ya 29 ~

# Uongozi wa Kitumishi

Siku moja kundi la wanafunzi wa Yesu lilimwendea na swali. Waliuliza hivi: "Ni nani aliye mkuu zaidi katika ufalme wa mbinguni?" (Mt. 18:1). Wanafunzi hawa walikuwa wakibishana kuhusu hilo jambo wao kwa wao (fan. Mt. 20:20-28; Mk. 9:33-37; 10:35-45; Lk. 22:24-27). Baadhi yao walikuwa na tamaa kubwa na walitaka kuwa viongozi kati ya wanafunzi.

Akijua mioyo yao, Yesu alimwita mtoto mdogo aje na kusimama katikati yao. Kisha akawaambia wanafunzi wake, "Kweli nawaambieni, msipobadilika na kuwa kama watoto wadogo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. Kwa hiyo ye yote atakayejishusha kama mtoto huyu ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni" (Mt. 18:3-4). Wakati mwingine, Yesu alieleza hivi: "Mnajua ya kuwa watawala wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Haitakuwa hivyo kwenu. Lakini, yeyote anayetaka kuwa mkubwa kati yenu lazima awe mtumishi wenu, na yeyote anayetaka kuwa wa kwanza lazima awe mtumwa wenu" (Mt. 20:25-27).

Yesu alikuwa anazungumza kuhusu aina ya uongozi ambao angeuhitaji katika Kanisa Lake jipya alilokuwa analiunda. Viongozi katika Kanisa Lake walitarajiwa kuongoza kwa namna tofauti kuliko viongozi wa ulimwengu. Badala ya kutumikiwa, viongozi hawa wapya wangewatumikia wengine. Badala ya

kuwatawala watu, wangewatunza kwa upendo wale waliowaongoza. Uongozi wa aina hii umejulikana kuwa uongozi wa kitumishi. Ni aina ya uongozi ambao Mungu anadai leo kwa wachungaji wa Kipentekoste katika Afrika.

## UONGOZI WA KITUMISHI WAFAFANULIWA

Uongozi ni uwezo wa kushawishi watu kutenda kwa njia fulani au kuelekea upande fulani. Kwa mchungaji wa Kipentekoste, uongozi ni uwezo aliopewa na Mungu wa kuwashawishi watu wa Mungu kutafuta ufalme wa Mungu kwanza (Mt. 6:33). Ni uwezo wa kuwatia moyo watu wa Mungu watimize wajibu wao walioagizwa na Mungu katika kuendeleza utume wa Mungu duniani.

Kama viongozi wote, viongozi watumishi wanahusika na utume. Lakini pia viongozi wa kitumishi wanajali ukuaji na ustawi wa watu wanaowaongoza. Wanatumikia watu wa Mungu kwa unyenyekevu na huruma, na kujitahidi kushawishi kupitia upendo badala ya kulazimisha.

Mawazo ya kiongozi mtumishi ni kinyume cha "mawazo ya kiongozi" ambayo mara nyingi huonekana katika Afrika. Mkuu asiyemcha Mungu hutawala kwa vitisho; kiongozi mtumishi huongoza kwa upendo na huruma. Mtemi anadai utii; kiongozi mtumishi anahamasisha kujiamini. Mtemi huwanyonya watu; kiongozi mtumishi anatafuta kuwabariki.

Yesu angeweza kutawala akiwa mtemi; lakini alichagua kuongoza kama mtumishi (Mt. 20:28). Wakati wowote, Yesu angeweza kuamuru majeshi ya malaika kutekeleza mapenzi yake (Mt. 26:53). Lakini alichagua kujinyenyekeza na kujisalimisha kwa mapenzi ya Baba yake (Mt. 26:39, 42). Sadaka yake msalabani ni mfano mkuu wa maana ya kuwa kiongozi mtumishi. Kama Bwana wao, wachungaji wa kweli wa Kipentekoste ni viongozi watumishi. Badala ya kuwadhulumu wafuasi wao, wanawatumikia kwa furaha na upendo.

Ufalme wa Mungu umefafanuliwa kuwa “ufalme uliogeuka.” Hii ni kwa sababu uongozi katika ufalme wa Mungu hufanya kazi tofauti na uongozi katika mfumo wa ulimwengu. Katika mashirika ya kidunia, kiongozi anatarajiwa kuwa juu. Yeye huwadhibiti wengine na hupokea utukufu na marupurupu mengi. Lakini katika ufalme wa Mungu, kiongozi ndiye yuko chini. Anajitahidi kuwatumikia na kuwabariki wengine.

## TABIA ZA KIONGOZI MTUMISHI

Sifa sita zinatakiwa kuwepo kwa mchungaji yeyote wa Kipentekoste ambaye anataka kuwa kiongozi mtumishi.

**Unyenyekevu**

Kwanza, kama kiongozi mtumishi, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuongoza kwa unyenyekevu. Asipoteze muda kutafuta kutambuliwa kibinafsi, au mamlaka. Badala yake, afuate mfano wa Yohana Mbatizaji, aliyesema hivi kumhusu Yesu, "Lazima yeye aongezeke, mimi nipungue" (Yoh. 3:30). Na lazima wakumbuke maneno ya Mungu aliye mlezi wao: "Aliye mkubwa miongoni mwenu atakuwa mtumishi wenu. Kwa maana wale wajikwezao watashushwa, na wale wajinyenyekezao watakwezwa" (Mt. 23:11-12).

Kuna tabia isiyokuwa nzuri miongoni mwa baadhi ya wachungaji wa Kiafrika kujidai na vyeo vya juu. Yesu alionya dhidi ya tabia hii. Aliwaambia wanafunzi wake, "Ninyi msiitwe Rabi, kwa maana mnaye Mwalimu mmoja, na ninyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu yeyote duniani 'baba,' kwa maana mnaye Baba mmoja, naye yuko mbinguni. Wala ninyi msiitwe waalimu, kwa maana mnaye Mwalimu mmoja, ndiye Masiya. Aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu" (Mt. 23:8-11). Wanaume na wanawake wenye akili ndogo mara nyingi hutafuta vyeo vikubwa. Lakini, viongozi wakuu wa kweli wanaridhika kuonekana kama watumishi wa Kristo.

Usiku kabla ya Yesu kusulubishwa alikutana na wanafunzi wake katika chumba cha juu huko Yerusalemu. Hapo akawafundisha somo juu ya uongozi wa kitumishi. Baada ya kumaliza mlo wa Pasaka, Mwokozi aliinuka, akavua vazi Lake la juu na kujifunga taulo kiunoni Mwake. Kisha akajaza maji kwenye beseni na kuanza kusafisha miguu ya wanafunzi wake. Alipomaliza, aliwauliza, "Je, mnaelewa nilichowafanyia?"

Yesu akawaeleza hivi: "Ninyi mnaniita 'Mwalimu' na 'Bwana,' na kweli, ndivyo nilivyo. Sasa kwa kuwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, nanyi pia mnapaswa kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Nimewawekea kielelezo, ili mfanye kama mimi nilivyowatendea" (Yoh. 13:13-15). Yesu alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake kwamba viongozi wakuu katika ufalme wake ni wale wanaochukua nafasi ya mtumishi mdogo kabisa katika nyumba.

Basi wewe kama mchungaji wa Kipentekoste ni lazima kupinga kwa nguvu zote mvuto wa uharibifu wa mamlaka na kiburi. Kama kiongozi mtumishi wa

kweli, hupaswi kamwe kutafuta kuwanyonya watu wa Mungu. Badala yake, tafuta kuwatumikia na kuwabariki.

**Huruma**

Pili, kama kiongozi mtumishi wa kweli, mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuwahurumia wale alioitwa kuwaongoza. Kuhurumia mtu ni kujitambulisha naye kwa karibu na kushiriki hisia zake, maumivu na furaha. Biblia inasema kwamba Yesu ndiye Kuhani wetu Mkuu ambaye anaweza "kuchukuliana na udhaifu wetu" (Ebr. 4:15). Aliwahurumia Mariamu na Martha alipolia nao pale kaburini kwa Lazaro (Yoh. 11:35). Wewe kama Yesu lazima ujifunze "kufurahi pamoja na wale wanaofurahi" na "kuomboleza pamoja na wale wanaoomboleza" (Rum. 12:15).

**Uwazi**

Tatu, kama kiongozi mtumishi, mchungaji wa Kipentekoste lazima ajitahidi kuwa wazi katika shughuli zake na watu. Hii ina maana kwamba hatajaribu kuficha utu wake jinsi alivyo, kwa wengine. Hajifanyi kuwa jinsi asivyokuwa. Paulo aliwakumbusha Wakorintho juu ya uwazi wake mwenyewe. Aliandika hivi: "Katika uhusiano wetu nanyi, tumeishi mbele yenu sisi wenyewe kwa unyofu wa kiungu" (2 Kor. 1:12). Baadaye aliongeza, "Tumesema nanyi kwa uhuru, enyi Wakorintho, na kuwafungulia mioyo yetu" (2 Kor. 6:11).

Uwazi kama huo utafungua njia za mawasiliano kati yako na washirika wa kanisa lako. Watu wataanza kukuona kama mtu mwaminifu, anayeaminika. Matokeo yake ni kwamba watahimizwa kukuamini. Na watafurahi kufuata uongozi wako.

**Kuamini**

Kama kiongozi mtumishi, mchungaji wa Kipentekoste atawaamini watu wa Mungu. Anaamini kwamba Roho Mtakatifu yule yule anayekaa ndani yake atawatia nguvu, kuwaongoza, na kukaa na washirika wao. Kwa sababu hii, mchungaji wa Kipentekoste anaweza kuwaamini watu wa Mungu, na yuko tayari kuwashirikisha huduma. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya na wanafunzi wake kumi na wawili (Yoh. 20:21). Na ndivyo Paulo alivyofanya na Timotheo (2 Tim. 2:2). Badala ya kujaribu kufanya kazi kumi, mchungaji anayefaa atawawezesha washiriki kumi kufanya kazi hizo.

Kwa hiyo, kama kiongozi mtumishi mwaminifu, ni lazima uzingatie karama za Mungu ndani ya wengine. Na lazima uwe na wakati wa kuwa pamoja nao, kuwawezesha na kuwazoeza kufanya kazi hiyo. Viongozi hawa wanaochipukia wanapokua katika uelewa na uwezo wao, utataka kuwakabidhi majukumu zaidi na zaidi. Na lazima uwape mamlaka watakayohitaji ili kutimiza majukumu yao mapya kwa ufanisi.

Kiongozi mkuu hatishwi na mafanikio ya wengine. Furaha yake kuu inakuja kutokana na kuwainua wengine ambao watashiriki katika kutimiza umisheni.

**Mawasiliano**

Kama kiongozi mtumishi, mchungaji wa Kipentekoste lazima ajifunze kuwasiliana vizuri na wale anaowaongoza. Mawasiliano mazuri ni kuzungumza kwa hekima na kusikiliza kwa uangalifu. Biblia inasema hivi, "Maneno yenu yawe yamejaa neema siku zote, yakikolea munyu" (Kol. 4:6). Pia inatuelekeza kuwa "wepesi [au tayari] kusikiliza" (Yakobo 1:19). Kwa hiyo, kama kiongozi mzuri wa kitumishi, lazima uwekeze muda na nguvu nyingi ili kuwa mzungumzaji mzuri.

**Upako**

Hatimaye, kama kiongozi mtumishi, mchungaji wa Kipentekoste lazima atafute upako wa Roho Mtakatifu. Ni lazima ahakikishe kwamba viongozi wengine katika kusanyiko wanafanya vivyo hivyo. Upako unapokelewa mtu anapobatizwa katika Roho Mtakatifu kama walivyobatizwa wanafunzi siku ya Pentekoste (Mdo. 2:4). Nao hudumishwa kwa kutembea katika Roho (Gal. 5:25).

Yesu ndiye mfano mkuu wa jinsi uongozi wa mtumishi aliyetiwa mafuta na Roho unavyoonekana. Alipokuwa akianza huduma yake, alitamka kwamba Roho Mtakatifu alimtia mafuta ili kuwatumikia wengine kwa kuhudumia mahitaji yao (Lk. 4:18-19). Petro alieleza huduma ya kitumishi ya Yesu hivi: "Mungu alimtia mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu na nguvu, naye akazunguka huko na huko, akitenda mema na kuponya wote waliokuwa chini ya nguvu za Ibilisi, kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye" (Mdo. 10:38).

Sisi pia kama Yesu hatupaswi kamwe kujaribu kufanya kazi ya Mungu kwa nguvu au uwezo wetu wenyewe. Badala yake, tunapaswa kutegemea nguvu na upako wa Roho (Lk. 24:49; Mdo. 1:8).

## MIFANO YA UONGOZI WA KITUMISHI

Biblia ina mifano mingi ya uongozi wa kitumishi. Tuangalie mifano minne kati ya hiyo. Miwili inapatikana katika Agano la Kale, na miwili inapatikana katika Agano Jipya.

**Musa: Huduma Iliyokasimiwa**

Musa ni mfano mzuri wa kiongozi mtumishi ambaye alikuwa mnyenyekevu kiasi cha kuwagawia wengine huduma. Mungu alimpa Musa mamlaka makubwa kwa kumchagua kuwaongoza watu wake (Kut. 3:1-10). Mara nyingi Mungu alizungumza na Musa "uso kwa uso, kama mtu asemavyo na rafiki" (33:11). Na Mungu alimtumia Musa kufanya ishara kubwa na maajabu kati ya watu (4:21; Mdo. 7:36). Pamoja na hayo, Musa hakuwa na kiburi. Ila alichagua kuwaongoza watu wa Mungu kwa unyenyekevu mkubwa (Hes. 12:3).

Biblia inasimulia habari jinsi baba mkwe wa Musa alivyomshauri kufanya kazi yake (Kut. 18:13-27). Yethro alipomwona Musa akifanya kazi yote mwenyewe, alimshauri mkwewe hivi: "Ufanyalo si jema….Kazi hii ni nzito kwako; huwezi kuwashughulikia peke yako" (mst. 17-18). Musa alifuata shauri la Yethro na kuwagawia watu wanaoaminika kazi nyingi. Kwa sababu hiyo, Musa alipata kutulia, kazi ikafanikiwa, na watu wakabarikiwa.

**Daudi: Aliwapandisha Wengine**

Mfano mwingine mzuri wa kiongozi mtumishi ni Mfalme Daudi. Mungu alimtaja kuwa "mtu anayeupendeza moyo wangu" (Mdo. 13:22; taz. 1 Sam.13:14). Kwa kuwa Daudi alikuwa salama katika cheo chake kama mfalme na akiwa mtumishi wa watu wa Mungu, aliweza kutumia wakati na nguvu zake kuwajenga wengine.

Akiwa kiongozi mtumishi mnyenyekevu, Daudi hakuogopa mafanikio ya watu wengine kama Sauli, mtangulizi wake. Kwa ujasiri na ushupavu mwingi, Daudi alijizungushia wale ambao matendo yao yalishindana na yake (1 Nya. 11:10-47). Naye aliwaheshimu wale waliotumika chini yake, akiwatia moyo wafanikiwe (mst. 17-19, 25). Mungu alitumia utayari wa Daudi kuwaendeleza wengine kumhakikishia mafanikio yake na kuwabariki wale waliotumika chini yake.

**Paulo: Mwalimu Mcha Mungu**

Mfano wa tatu wa kiongozi mtumishi mnyenyekevu ni mtume Paulo. Ingawa Mungu alimchagua kuwa mtume, alijiona kuwa mtumishi tu wa Kristo (Rum. 1:1; Tito 1:1). Paulo wakati fulani alijieleza kuwa "mdogo zaidi kati ya mitume" (1 Kor. 15:9). Yeye alifundishwa na Barnaba (Mdo. 9:26-27; 11:25-26). Kwa upande wake, aliwashauri wengine kwa bidii. Barua zake zinaonyesha jinsi alivyojitahidi daima kuwajenga wengine.

Mafanikio mawili makubwa ya Paulo yalikuwa Timotheo na Tito. Alimshauri Timotheo (Mdo. 16:1-5), na baada ya muda alimwamini "mwanawe katika imani" kuliongoza kanisa la Efeso (1 Tim. 1:2-3). Pia alimshauri Tito na kumteua kuongoza makanisa ya Krete (Tito 1:5). Ikiwa mtume huyo hangetia juhudi ya kuwashauri Timotheo, Tito, na wengine, mvuto wake na kazi yake vingalipungua sana.

**Yesu Kristo: Mfano Mkuu**

Bwana Yesu Kristo anasimama kama mfano mkuu wa uongozi wa kitumishi. Alifundisha kwamba viongozi wa kweli wa ufalme huwatumikia wengine bila ubinafsi (Lk. 22:24-27). Kisha, alionyesha dhana hii katika maisha na huduma Yake mwenyewe. Akizungumza juu yake mwenyewe, Yesu alisema, "Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mk. 10:45). Paulo alielezea mtindo wa uongozi wa kitumishi wa Yesu kama ifuatavyo:

"Katika uhusiano wenu ninyi kwa ninyi, iweni na nia moja kama Kristo Yesu... alijifanya kuwa si kitu kwa kutwaa asili ya mtumwa, aliyefanywa kwa sura ya kibinadamu. Naye alipoonekana ana sura ya mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." (Flp. 2:5-8)

> Hivyo, Paulo aliwahimiza Wakristo wote, pamoja na viongozi Wakristo, "Msifanye neno lo lote kwa kushindana kwa ubinafsi, wala kwa majivuno ya bure. Bali kwa unyenyekevu, wathaminini wengine kuliko ninyi wenyewe, bila kuangalia faida zenu wenyewe, bali kila mmoja wenu aangalie mambo ya wengine" (Flp. 2:3-4).

## MAENEO YA UONGOZI WA KITUMISHI

Mtazamo wa uongozi wa kitumishi lazima ujidhihirishe katika maeneo matatu ya maisha na huduma ya mchungaji wa Kipentekoste: nyumbani, kanisani, na katika jamii.

### Uongozi wa Kitumishi Nyumbani

Kama mchungaji wa Kipentekoste, eneo lako la kwanza la uongozi wa kitumishi ni nyumbani kwako. Kabla ya kutumikia kusanyiko lako, ni lazima umtumikie mwenzi wako na watoto wako kwa uaminifu. Paulo alisema hivi kuhusu mwangalizi, au mchungaji, "Imempasa kuisimamia nyumba yake mwenyewe vema na kuona kwamba watoto wake wanamtii, na afanye hivyo kwa namna inayostahili heshima kamili" (1 Tim. 3:4). Kisha Paulo akaongeza, "Ikiwa mtu hajui kuisimamia familia yake mwenyewe, atawezaje kulitunza [kulisimamia] kanisa la Mungu?" (Mst. 5).

Kwa hiyo, kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufahamu kwamba eneo lako la kwanza la uongozi wa kitumishi ni familia yako. Lazima uwe tayari kunyenyekea na kumtumikia mwenzi wako na watoto wako vizuri. Kwa namna fulani, familia yako ndiyo "kanisa lako la kwanza," na kanisa unaloongoza ni "kanisa la ziada". Mtazamo unaotumia kuhudumia familia yako bila shaka utakuwa ni mtazamo unaotumika pia kutumikia kanisa lako. Lazima uwe kiongozi wa kitumishi kwa wote wawili.

### Uongozi wa Kitumishi Kanisani

Eneo lako la pili la uongozi wa kitumishi ni kanisa. Unapaswa kujiona kama zawadi ya Kristo kwa kanisa (Efe. 4:11-12). Zaidi ya hayo, lazima utambue kwamba Kristo amekuita kuwachunga watu wa Mungu. Petro aliwaandikia wazee hivi: "Iweni wachungaji wa kundi la Mungu lililo chini ya uangalizi wenu, mkiwalinda, si kwa sababu ni lazima, bali kwa sababu mko tayari, kama Mungu apendavyo; si kutafuta faida ya dhuluma, bali kwa bidii kutumika; si kwa kujifanya mabwana juu ya hao waliowekwa chini yenu, bali kuwa vielelezo kwa kundi" (1 Pet. 5:2-3).

Ukiwa kiongozi mtumishi wa kweli, yakupasa kulichunga kundi la Mungu kwa kuwalisha Neno la Mungu, kwa kuwatia nguvu walio dhaifu na wanyonge, na kwa kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka. Ni lazima pia uwalinde kondoo dhidi ya wanyama wanaokula wengine (Mdo. 20:28-31). Zaidi ya hayo, lazima

uwe kielelezo cha utumishi wa kiungu kwa kuwaonyesha watu wa Mungu jinsi ya kujaliana, na kwa kuwahimiza kufanya vivyo hivyo.[1]

**Uongozi wa Kitumishi Katika Jamii**

Kama mchungaji wa Kipentekoste, eneo lako la tatu la uongozi wa kitumishi ni jamii yako. Kwa hiyo unapaswa kujiona, si tu kama mchungaji wa familia yako na kanisa unalolichunga, bali kama mchungaji wa kijiji au hiyo jamii unakoishi. Yesu alifundisha kwamba tunapaswa kuwa "chumvi ya dunia" na "nuru ya ulimwengu" (Mt. 5:13-16). Basi, ni lazima ujihusishe kwa karibu na watu wa jumuiya yako: waombee, watumikie, na uwashirikishe kwa uaminifu upendo wa Kristo.2

---

Yesu aliweka kiwango cha uongozi wa kitumishi katika Kanisa. Aliwaambia wanafunzi Wake, "Kwa maana hata Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia kwa ajili ya wengi" (Mk. 10:45). Mchungaji wa Kipentekoste lazima afuate nyayo za Bwana wake. Na anapaswa kukumbuka maneno yake: "Yeyote anayetaka kuwa wa kwanza lazima awe wa mwisho, na mtumishi wa wote" (9:35).

[1] Ili kupata habari zaidi kuhusu kuchunga watu wa Mungu, ona Sura ya 24: "Kuwatunza Kondoo" na Sura ya 27: "Kulilinda Kundi."

[2]Kwa mengi zaidi kuhusu kutunza jumuiya watu, tazama Sura ya 38: "Kutumikia Jumuiya."

~ Sura ya 30 ~

# Uongozi Wenye Maono

Baada ya maombi mengi na kujikagua katika nafsi yake, Mchungaji Imanueli alihisi kwamba Mungu alikuwa akimwita aondoke katika kanisa lake la starehe katika mji mkuu na kuihamisha familia yake katika eneo la ndani lenye misitu minene ya nchi. Huko, alipaswa kuanzisha shughuli ya upandaji kanisa. Huyo mchungaji anakumbuka, “Lilikuwa jimbo ambalo halijahubiriwa sana katika nchi yangu, lakini huko ndiko Mungu alitaka mimi na familia yangu twende.” Alikuwa na hakika kwamba Mungu ameweka maono hayo moyoni mwake.

Roho Mtakatifu alimwelekeza Mchungaji Imanueli kwenye kijiji fulani. Ijapokuwa eneo hilo lilikuwa limewekwa kimkakati, lilijulikana kuwa limezama katika uchawi. Tangu kufika kwao, mchungaji na mkewe walipokea vitisho kutoka kwa waganga wa kienyeji. Hata hivyo, hao wawili walivumilia, wakitangaza injili kwa uaminifu kwa wote ambao wangesikiliza. Watu waliokolewa na kujazwa na Roho, na kanisa lilianza kukua na kukomaa.

Mchungaji Imanueli mara nyingi alishirikisha maono yake ya kuanzisha shughuli za upandaji kanisa zinazowezeshwa na Roho kwa washirika wake. Baada ya muda wengine walianza kupata maono hayo, na muda si mrefu baadaye viongozi wakaanza kujitokeza, ambao Mchungaji Imanueli aliwazoeza kwa ajili

ya huduma. Mara nyingi aliwachukua viongozi hawa wanaojitokeza kufanya uinjilisti na kuanzisha makanisa katika eneo jirani. Kwa miaka mingi, walianzisha makanisa mengi. Hata waliwazaa wamishenari na kuwatuma kupanda makanisa kati ya makabila ambayo hayajafikiwa upande wa kaskazini.

Leo, kanisa la Mchungaji Imanueli linastawi. Watu wamekubali kusudi lao na wamejitambulisha na maono ya mchungaji wao kiasi kwamba wanaendelea kupanda makanisa mapya katika eneo hilo. Kweli, mchungaji Imanueli anadhihirisha maana ya kuwa kiongozi mwenye maono.

Ili kuliongoza kanisa katika utume wenye ufanisi, mchungaji wa Kipentekoste lazima aelewe waziwazi kusudi la Mungu kwa kanisa. Ni lazima pia awe na maono yaliyo wazi ya jinsi kanisa lake linavyopaswa kushiriki katika kutimiza kusudi hilo. Mchungaji anapoweka wazi maono ya mahali kanisa linapotakiwa kwenda, watu wanatiwa moyo kufuata. Anaposhindwa kutoa maono hayo, kanisa linayumba (taz. Mithali 29:18). Sura hii itajadili umuhimu wa maono katika kuongoza kundi la waamini wa mahali pamoja.

## UONGOZI WENYE MAONO WAFAFANULIWA

Kiongozi au mchungaji mwenye maono ni mtu anayewaongoza watu wa Mungu kutoka pale walipo hadi pale Mungu anapotaka wawe. Viongozi hawa wenye kuongozwa na Roho wanaweza kuona mbele zaidi mpaka katika siku zijazo. Wana uwezo wa kutathmini kwa usahihi hali ya sasa ya kanisa, kuelewa nguvu na udhaifu wake. Na wanaweza kuona kile ambacho kanisa linaweza kuwa na linavyopaswa kuwa. Wana uwezo zaidi wa kupanga njia kwa kanisa kufikia malengo yake yaliyotolewa kwao na Mungu. Na mwisho: kiongozi wa Kipentekoste mwenye maono anaweza kulitia moyo kanisa kusonga mbele kwa ujasiri katika kutimiza malengo hayo.

## TABIA ZA VIONGOZI WENYE MAONO

Hebu tuangalie sifa nane za viongozi wenye maono kama zilivyofunuliwa katika Maandiko.

### Kuongozwa na Roho

Kwanza, kiongozi mwenye maono ya kweli anaongozwa na Roho. Kabla ya mchungaji wa Kipentekoste kuliongoza kanisa lake kwenda katika makusudi ya Mungu, lazima yeye mwenyewe ajazwe na Roho Mtakatifu na aweze kufuata

uongozi wake (taz. Gal. 5:25). Hao ni lazima wawe tayari kuacha mipango yao wenyewe ili kufuata mipango ya Mungu kwa bidii.

**Amejaa Imani**

Pili, viongozi wenye maono wamejaa imani. Wana uwezo wa kumwamini Mungu na kumwamini katika magumu na hali mbaya (Ebr. 11:1-37).

**Ni Halisi**

Tatu, viongozi wenye maono wanatoa kielelezo cha kweli kwa kanisa kufuata (Flp. 3:17). Wana rekodi ya uaminifu ya huduma iliyothibitishwa, ambayo inathibitisha haki yao ya kuongoza kanisa. Kwa kweli wanaiga jinsi Mungu anavyotarajia kanisa liitikie maono waliyopewa na Mungu.

**Huzingatia Siku Zijazo**

Nne, viongozi wenye maono wanazingatia siku zijazo. Akili zao hazibakii kwenye mambo ya jana, bali kuhusu fursa za kesho. Paulo alitoa mfano wa tabia hii aliposhuhudia na kusema hivi: "Natenda neno moja: nikiyasahau yaliyo nyuma, nayachuchumilia yaliyo mbele" (Flp. 3:13).

**Kinabii na Kivitendo**

Tano, viongozi wenye maono, ni wa kinabii na kivitendo kwa wakati mmoja. Ni wa kinabii kwa sababu wanaona kile kinachoweza kutimizwa. Wao ni wa vitendo kwa sababu wanatambua kile kinachohitajika kufanywa ili kufikia lengo. Huku akifikiria siku zijazo, kiongozi mwenye maono lazima aweze kuliongoza kanisa kivitendo kuvuka changamoto za sasa.

**Wa Kuaminika**

Sita, viongozi wenye maono wanaaminika. Wana rekodi iliyothibitishwa ya kuaminika katika siku za nyuma. Kwa sababu hiyo, watu wa Mungu wako tayari kuwafuata wakati ujao.

**Mwenye Ushawishi**

Saba, viongozi wenye maono wana ushawishi. Wana uwezo waliopewa na Mungu wa kuwatia moyo wengine kutenda. Wana vipawa na ujuzi unaohitajika ili kugusa vyema mitazamo, uchaguzi, na matendo ya wengine.

### Ni Jasiri

Mwisho: viongozi wenye maono ni jasiri. Wana ujasiri wa kutosha kutembea katika siku zijazo zisizo na uhakika. Mchungaji Imanueli alipoachana na starehe za mji mkuu, hakujua ni nini kilikuwa mbele yake. Lakini, kwa ujasiri aliiongoza familia yake kusikojulikana, huku akimtumaini Mungu kutosheleza mahitaji yao.

## MIFANO YA VIONGOZI WENYE MAONO

Kwa namna nyingi, Biblia ni habari kuhusu wanaume na wanawake ambao Mungu aliwainua na kuwatia mafuta kuwa viongozi wa maono. Viongozi hawa wanaonyesha sifa za uongozi zilizotajwa hapo juu. Wafuatao sita ni mifano ya viongozi hao.

### Ibrahimu: Maono Yaliyojaa Imani

Ibrahimu alikuwa kiongozi mwenye maono yaliyojaa imani. Kwa imani alitazama wakati ujao na kuona "mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu" (Ebr. 11:10). Kisha, kwa imani aliongoza familia yake hadi nchi isiyojulikana, akiamini kwamba Mungu angetimiza ahadi yake kwake (Ebr. 11:8). Kwa kufanya hivi, akawa "baba wa wote waaminio" (Rum. 4:11).

### Yusufu: Ufahamu wa Kinabii

Yusufu aliongoza kupitia ufahamu wa kinabii. Mungu alimpa ufahamu wa maana ya ndoto ya Farao (Mwa. 41:15-24). Kisha Yusufu alimpa mfalme ushauri wa kivitendo jinsi anavyopaswa kuitikia habari hizo za kinabii (mst. 25-36). Kwa hiyo, wengi waliokolewa na njaa. Farao aliona Roho wa Mungu ndani ya Yusufu na kumpandisha cheo hadi nafasi ya juu katika uongozi, mkuu wa pili baada ya Farao mwenyewe (mst. 37-44).

### Yoshua na Kalebu: Maono ya Ujasiri

Maono ya ujasiri ya Yoshua na Kalebu yaliwawezesha kusonga mbele kwa imani wakati wengine walipokuwa wanaondoka kwa hofu (Hes. 14:6-9). Badala ya kusalimu amri kwa woga wao, Yoshua na Kalebu waliamua kuweka imani yao katika Mungu. Watu walipokataa kufuata mwongozo wao, wao walidumu kuwa waaminifu kwa ahadi yao na kudumisha hai maono yao kwa miaka arobaini, wakitayarisha kizazi kilichofuata kiingie katika Nchi ya Ahadi.

**Nehemia: Nia Moja**

Nehemia aliwaongoza watu wa Mungu kujenga upya kuta za Yerusalemu kwa nia moja. Alifanya hivyo mbele ya upinzani mkubwa. Aliimarishwa na maono yake ya kile ambacho kingetimizwa kama watu wa Mungu wangeendelea kushikilia kazi waliyopewa na Mungu.

**Hagai: Mtazamo wa Kutokuwa na Ubinafsi**

Mtazamo wa Hagai usio na ubinafsi uliwachochea watu wa Mungu waache mahangaiko yao ya ubinafsi na kutanguliza kazi ya Mungu. Aliwataka waache kuwekeza rasilimali zao zote kwenye kujenga nyumba zao wenyewe. Badala yake, walipaswa kuwekeza kwenye kujenga nyumba ya Mungu. Nabii huyo aliwaambia watu wa Mungu kwamba, ikiwa wangetembea pamoja wakiwa na kusudi moja kwa umoja, kazi ingekamilika.

**Yesu: Mfano Wetu Mkuu**

Bwana wetu Yesu Kristo ndiye mfano mkuu wa kiongozi mwenye maono. Alielewa vizuri alikuja kwa nini, alikuwa anakwenda wapi, na alichopaswa kufanya ili kufika huko. Yeye ndiye kielelezo kamili cha mtu aliyeona njia ya kwenda mbele kisha akajitoa kikamilifu kuifuata njia hiyo (rej. Ebr. 12:2). Kisha akawatafuta, akawafundisha na kuwahimiza wengine kujiunga Naye katika kazi hiyo.

**Paulo: Maono ya Kimisheni**

Baada ya Yesu, Paulo alifuata, akiwa kiongozi mkuu wa kimishenari. Paulo alisukumwa na maono ya mbinguni kupeleka injili kwa mataifa. Aliwashirikisha wengine hayo maono yake, na akawapa mfumo wa kujiongeza kwa ajili ya uinjilisti, upandaji kanisa, na umisheni. Kuelekea mwisho wa huduma yake, Paulo aliweza kushuhudia hivi: “Mimi sikuyaasi maono yale kutoka mbinguni” (Mdo. 26:19).

## HATUA ZA KUFUATA KATIKA UONGOZI HUO

Ili kuwa kiongozi mwenye maono ya kweli, utahitaji kuelewa mambo ya msingi na hatua za kufuata katika uongozi. Na utahitaji kufahamu wazi jinsi uongozi wenye maono unavyoonekana katika utendaji halisi.

**Dhamira na Maono**

Kwa kuanza, lazima uelewe uhusiano kati ya utume na maono. Katika ufalme wa Mungu, maono hukua nje ya utume, na si kinyume chake. Utume wa Kanisa tayari umeamuliwa na Mungu. Utume wa Mungu, ambao wakati mwingine huitwa *missio Dei*, ni kuwakomboa na kuwaita kwake watu kutoka katika kila kabila, lugha, na taifa duniani kabla Kristo hajarudi. Yesu alisema hivi katika Agizo Lake Kuu: "Nendeni mkafanye wanafunzi wa mataifa yote, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi" (Mt. 28:18-20; linganisha Mk. 16:15-18; Lk. 24:49; Yoh. 20:21; Mdo. 1:8). Kanisa lipo ili kutimiza utume wa Mungu.[1]

Kristo ameagiza kila mchungaji wa Kipentekoste na kanisa kushiriki kikamilifu katika utume wake. Ameagiza kwamba kila kanisa liwe kanisa la kimishenari. Kwa hivyo, lazima lishiriki kikamilifu katika uinjilisti, kufanya wanafunzi na upandaji wa makanisa. Tena, kila kanisa la Kipentekoste lazima likuze maono ya kuzaa na kutuma wamishenari na watenda kazi wengine wa Kikristo. Ni lazima wewe ujitolee zaidi kuwasaidia watenda kazi hawa kwa maombi na fedha.[2]

Maono yanazungumza juu ya mtazamo wa kusanyiko ulioongozwa na Roho kuhusu jukumu lao katika kutimiza utume wa Mungu. Ni unabii kwa asili, ukizingatia kazi ambazo si za leo tu bali pia fursa za kesho. Maono hujaza pengo kati ya jinsi kanisa lilivyo leo na jinsi Mungu anavyolitaka liwe kesho. Ni picha ya kiakili yenye kuongozwa na Roho ya kile ambacho kanisa, kwa msaada wa Mungu, linaweza kuwa.

Wewe na kanisa unaloliongoza unapoanza kukumbatia utume wa Mungu, Mungu atakupa maono ya kile anachotaka utimize. Maono haya yenye kuongozwa na Mungu daima yataendana na utume wa Mungu, kama ilivyoelezwa hapo juu. Hii ndiyo sababu ni muhimu sana kuwa na ufahamu dhahiri wa utume wa Mungu na jinsi utume huo unavyohusiana na madhumuni ya utume ya kanisa la mahali pamoja. Utume huleta maono, na maono huleta malengo, nayo malengo huleta hatua.

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu maono ya umisheni, tazama Sura ya 31: "Uongozi wa Kimisheni."

[2] Kwa maelezo zaidi juu ya kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya umisheni, tazama Sura ya 40: "Kutengeneza Mpango wa Utume wa Kanisa la Mahali Pamoja."

**Kukuza Maono**

Kama ambavyo shamba linapaswa kulimwa ili kutoa mazao mazuri, maono nayo yanapaswa kusitawishwa ili kutoa mavuno ya mikakati inayo-ongozwa na Roho ya Mungu. Unaweza kusitawisha maono katika moyo wako mwenyewe na katika kanisa unalochunga kwa kutumia mbinu tatu zifuatazo:

*1. Usomaji wa Biblia wa kutafakari.* Kwanza, unaweza kusitawisha maono moyoni mwako kupitia usomaji wa Biblia wa kutafakari. Unaweza kusoma katika hali ya maombi habari za viongozi wakuu katika Maandiko ambao Mungu aliwatumia kuendeleza ufalme wake. Wakati unaposoma, jiulize maswali yafuatayo:

- Je, ni maono gani ambayo Mungu aliweka katika moyo wa huyu kiongozi?
- Je, kiongozi huyu alipataje kujua hayo maono?
- Je, alifanyaje ili kutimiza hayo maono?
- Mungu ananiambia nini kupitia habari hii?

Andika majibu yako katika daftari na uyatafakari moyoni mwako katika hali ya maombi. Baada ya muda, unaweza kutaka kujenga mahubiri kutokana na mawazo haya na kushirikisha kusanyiko lako. Kwa njia hii, wewe na watu wako mnaweza kukua pamoja katika ufahamu wenu wa utume wa Mungu na jukumu la kanisa lenu katika kutimiza utume huo.

*2. Kumngoja Mungu.* Pili, unaweza kusitawisha maono moyoni mwako kwa kumngojea Mungu katika sala. Anza kwa kumkaribia kwa njia ya shukrani ya dhati na sifa (Yakobo 4:8). Mara unapohisi uwepo wa Mungu, omba hivi, "Bwana, nionyeshe mapenzi yako. Nionyeshe moyo wako." Basi unapaswa kukaa mbele za Mungu, ukiomba katika Roho na kusikiliza sauti yake (Rum. 8:26-27; Efe. 6:18).

Unapoomba hivyo, zingatia mawazo au hisia na madhihirisho ambayo Roho Mtakatifu anaweka ndani ya moyo au akili yako. Baada ya muda, maarifa machache katika haya yatakua ya kuvutia zaidi na zaidi. Mwisho, yanaweza kukua na kuwa mzigo. Pamoja na mzigo utakuja ufahamu wa kina kwamba Mungu analiongoza kanisa katika mwelekeo fulani (Isa. 30:21). Pia utataka kuliongoza kusanyiko kuingia katika nyakati za kutafuta mwongozo kutoka kwa Mungu.

*3. Kuzingatia haja.* Mwishoni unaweza kusitawisha maono kwa kutazama mahitaji ya watu katika jumuiya yako au mahali pengine palipochaguliwa katika

hali ya maombi (taz. Yoh. 4:35). Unapotazama, mwombe Mungu ufahamu, ukisema hivi: "Bwana, nisaidie kuona ng'ambo ya mwonekano wa mahitaji ya ndani ya watu" (taz. 2 Kor. 4:18). Omba zaidi kama ifuatavyo: "Bwana, ni mahitaji gani kati ya haya unayotaka kanisa letu lishughulikie?" Baada ya kuomba, tulia na usikilize majibu ya Mungu.

**Nafasi ya Roho Mtakatifu**

Tunaishi katika siku za mwisho, wakati ambao Mungu anamimina Roho wake juu ya watu wote (Mdo. 2:17-18). Mungu ametupa Roho wake ili atutie nguvu na kutuongoza katika kazi. Kama kiongozi wa kweli wa Kipentekoste, unapaswa kudumu katika kutegemea uongozi wa Roho kila wakati. Ingawa mbinu za kisasa za uongozi na mikakati ya ukuaji wa kanisa ina nafasi yake, kamwe usitegemee sana mbinu hizi zilizobuniwa kibinadamu. Kama kiongozi wa kiroho mwenye maono, kila wakati tafuta mwongozo wa Roho na kufuata uongozi Wake, ukikumbuka maneno haya ya nabii, " 'Si kwa uwezo wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu,' asema Bwana Mwenyezi" (Zek. 4:6).

**Kuyatangaza Maono**

Ingawa maono ya mtu binafsi ni muhimu, haitoshi kwako kuwa na maono na kuyabakiza kwako mwenyewe. Lazima uweze kuwasilisha maono hayo kwa kanisa. Na lazima ufanye hivyo kwa njia ambayo itawatia moyo na kuwaimarisha watu wa Mungu kufuata. Utaratibu huu unajulikana kama kushirikisha maono. Sehemu kubwa ya kazi ya Yesu pamoja na wanafunzi wake ilihusisha kushirikisha maono. Alikuwa akishiriki nao maono Yake kila mara na kuwapa changamoto wamfuate. Vivyo hivyo, ni muhimu na wewe uwasilishe maono yako kwa kanisa na kuwataka washirika kufuata mfano wako, kama na wewe unavyofuata mfano wa Kristo (1 Kor. 11:1).

Ili hili litokee, maono lazima yahamasishe mawazo ya watu. Ni lazima yawe yenye changamoto na yanayoweza kufikiwa. Yaani, maono yasiwe makubwa kiasi cha kuwashinda watu. Wala yasiwe madogo kiasi cha kutowasisimua watu na kuwatia moyo. Maono yakiwa makubwa sana watu washindwe kufahamu, mchungaji lazima ayagawe kwa kuweka malengo ya muda mfupi na ya muda mrefu yanayoweza kufikiwa.

Wakati mwingine ni busara kushirikisha maono kwa hatua. Kwanza, unaweza kutaka kumshirikisha mwenzi wako maono hayo, au kikundi cha marafiki zako wa karibu, na viongozi wanaoaminika. Kisha jadili, ombea, na pata ushuhuda

kutoka kwa Roho kwamba endelea. Baada ya hapo, utataka kushirikisha maono hayo kwa halmashauri ya kanisa na watenda kazi, nao wapate nafasi ya kujiunganisha nayo. Unahitaji timu ili kutekeleza maono. Basi ni muhimu kwa washirika wote wa timu ya uongozi wawe kwenye bodi.

Wakati ukifika wa kushirikisha kanisa hayo maono, ni vizuri upange "Jumapili Ya Maono." Tukio hili litakupa jukwaa la kueleza kwa uwazi maono hayo kwa watu. Basi itakubidi uzungumze mara kwa mara kuhusu maono hayo pamoja na kuhubiri juu yake. Mbinu hii itasaidia kupandikiza maono katika mioyo ya watu.

Zaidi, fanya juhudi kuhakikisha kwamba kanisa zima linatembea pamoja ili kutimiza maono. Mhimize kila mtu atoe, aende, afanye kazi, atumikie, na kujitoa ili kuona maono yanatimizwa. Unapoendelea unaweza kuamua kuwaita watu fulani kutoa ushuhuda kuhusu jinsi maono hayo yanavyotimizwa. Shuhuda hizi zitasaidia kuwatia moyo watu na kuliweka kanisa kwenye mstari.

**Kushinda Vikwazo**

Usishangae utekelezaji wa maono ukijaribiwa. Kanisa lolote linalotafuta kufuata maono ya Mungu litakumbana na vikwazo na upinzani wa kishetani. Paulo aliwaandikia Wakristo wa Thesalonike, na kuwaeleza hivi: "Kwa maana tulitaka kuja kwenu…lakini Shetani alizuia njia yetu" (1 Thes. 2:18).

Upinzani kama huo kamwe hauwezi kuzuia kabisa maendeleo ya kanisa. Lakini itakuwa muhimu kwako na kanisa kushika kwa uthabiti maono hayo. Ukiendelea kuzingatia maono ambayo Mungu amekupa, atayatimiza. Yesu aliahidi, "Nitalijenga kanisa langu, na milango ya kuzimu haitalishinda" (Mt. 16:18)

Katika kisa kilichosimuliwa mwanzoni mwa sura hii, Mchungaji Imanueli alikuwa mwaminifu kwa maono ambayo Mungu alimpa. Kwa utii na imani, alistahimili mpaka maono hayo yalipotimia. Inaweza kuwa kweli kwako pia. Utakapogundua maono ya Mungu kwa ajili ya kanisa lako, na ukipitia nyakati za shida, wewe pia unaweza kuona utimilifu wa maono yako. Unaweza kudai ahadi ya Mungu kwa Habakuki kwa ujasiri: "Kwa maana ufunuo wa maono unangoja wakati ulioamriwa… Ujapokawia, ungojee; hakika utakuja wala hautakawia" (Hab. 2:3).

~ Sura ya 31 ~

# Uongozi wa Kimisheni

Siku moja Yesu alikuwa akitembea kando ya Bahari ya Galilaya. Huko, alikutana na Petro na Andrea wakitupa nyavu zao baharini. Akawaambia wamfuate naye atawafanya kuwa wavuvi wa watu. Biblia inasema, "Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata" (Mk. 1:16-18). Kwa kawaida watu huvutiwa na viongozi wenye hisia kali za utume. Husukumwa kuwafuata kihisia, kama vile Petro na Andrea walivyochochewa kumfuata Yesu.

Sura hii itazingatia nafasi ya mchungaji wa Kipentekoste kama kiongozi wa umisheni. Itatazama wajibu wake wa kuongoza kanisa lake kutumikia utume wa Mungu duniani. Itajadili zaidi jinsi mchungaji anavyoweza kuwatia moyo wengine kumfuata katika jambo hili kuu.

## MCHUNGAJI MISHENARI

Yesu mwenyewe alikuwa kiongozi wa kimishenari, na anamwita mchungaji wa Kipentekoste kuwa hivyo hivyo. Anatafuta wanaume na wanawake wenye roho yenye uharaka, ya kujitoa, na yenye imani ili kuwaongoza watu wake katika umisheni (rej. 2 Nya. 16:9).

**Sifa Muhimu**

Viongozi wa kimishenari wanajua wanakokwenda, na wanajua jinsi wanavyokusudia kufika huko. Kwa sababu hiyo, wana uwezo wa kuhamasisha wengine kujiunga nao katika hiyo safari. Wachungaji wa kimishenari wana sifa tatu muhimu:

*1. Kuelewa*. Wachungaji wa kimishenari wanaelewa utume wa Mungu. Wanatambua kwamba Mungu ni Mungu mishenari na kwamba yuko katika utume wa kukomboa na kuwaita kwake watu kutoka katika kila taifa duniani (Mt. 24:14; Uf. 5:9; 7:9). Dhana hii inajulikana kama *missio Dei*, neno la Kilatini linalomaanisha "utume wa Mungu." Mchungaji wa kimishenari anaelewa kwamba kanisa lipo ili kutimiza utume wa Mungu duniani. Tena anaelewa zaidi kwamba moja ya majukumu yake ya msingi kama mchungaji ni kuhamasisha kanisa kutimiza utume wa Mungu.[1]

*2. Kujitoa.* Zaidi ya kuelewa utume wa Mungu, mchungaji wa Kipentekoste lazima ajitoe kuliongoza kanisa lake kushiriki kikamilifu katika kutimiza utume huo, kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Anapaswa kuwa tayari kufanya chochote kinachohitajika kutekeleza jukumu hili kubwa.

*3. Ustadi.* Hatimaye, mchungaji wa Kipentekoste lazima ajitoe katika kukuza mitazamo na ujuzi unaohitajika ili kuhamasisha kanisa kutekeleza utume wa Mungu. Mchungaji wa kweli wa Kipentekoste anatambua kwamba, mwisho wa siku, uwezo wake katika huduma unatoka kwa Mungu kupitia nguvu za Roho Mtakatifu (Mdo. 1:8; 2 Kor. 3:5-6).

**Mfano wa Yesu**

Yesu alikuwa kiongozi wa kimishenari. Alielewa wazi kwa nini alikuja duniani. Alitangaza hivi: “Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea” (Lk. 19:10). Katika sehemu nyingine, alitangaza hivi: “Nimeshuka kutoka mbinguni, si kufanya mapenzi yangu, bali kuyafanya mapenzi yake aliyenituma” (Yoh. 6:38). Yesu aliitaja utume wake kuwa ni “chakula” chake (Yoh. 4:34). Kama vile chakula kinavyotia nguvu na kuulisha mwili, Yesu alitiwa

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu utume wa Mungu, tazama kitabu cha kiada cha Discovery Series cha Africa's Hope kiitwacho, *Theolojia ya Kibiblia ya Umisheni,* cha Paul York.

nguvu na kulishwa kwa kufanya mapenzi ya Baba Yake. Mwishowe, ahadi hii ilimpeleka msalabani (Mt. 20:28).

Kabla ya kurudi mbinguni, Yesu alikabidhi utume na huduma Yake kwa Kanisa Lake. Aliwaambia wanafunzi wake, "Kama vile Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawatuma ninyi" (Yoh. 20:21). Kama vile Yesu alivyopata utume wake katika mapenzi ya Baba yake, mchungaji wa Kipentekoste hupata utume wake katika mapenzi ya Kristo. Na kama vile kujitoa kwa Yesu kufanya mapenzi ya Baba Yake kulivyomtia nguvu katika utume Wake, ndivyo na mchungaji wa Kipentekoste anavyoimarishwa katika utume wake (Mt. 26:36-44; Mt. 28:19-20; Yoh. 14:16)

**Kufanyika Kabla ya Kufanya**

Kama mchungaji wa Kipentekoste ni muhimu uelewe kwamba uongozi wa kimishenari ni kuwa kuliko kutenda. Kumbuka, Yesu alimwahidi hivi Petro na Andrea, "Nifuateni, nami *nitawafanya* kuwa wavuvi wa watu" (Mk. 1:17, maneno mepesi kusisitiza). Kwa kumfuata Yesu na kujazwa na Roho wake, hali halisi ya wanafunzi ingebadilishwa. Wangekuwa kama Mwalimu wao (Lk. 6:40; Mdo. 4:13).

Sio tu kwamba Roho angewawezesha kuhudumu kwa nguvu, angewapa shauku ya Kristo kwa ajili ya mavuno. Roho Mtakatifu angewabadilisha kiasi kwamba nia zao zote, matamanio, na vipaji vingekuwa chini ya ubwana wa Kristo. Wangeungana na Kristo katika kutimiza utume wa Mungu wa ukombozi. Ujuzi wenye nguvu wa kiroho, unaojulikana kama ubatizo katika Roho Mtakatifu, ungetengeneza msingi wa uongozi wao wa kimishenari wa siku zijazo (Lk. 3:16; Mdo. 1:4-5).[2]

Hayo yanaweza kutupata hata sisi leo. Kama tutaruhusu Roho wa Mungu atujaze na kufanya kazi ndani yetu, atatugeuza tufanane na Kristo (rej. 2 Kor. 3:18). Naye atatupa shauku ile ile ya mavuno kama iliyokuwa ndani ya Yesu.

**Kuwa Mishenari**

Bwana Yesu aliwaita wanaume na wanawake wamfuate na kuendeleza kazi aliyokuwa ameanza. Kisha aliwekeza muda na nguvu zake katika kuwafundisha

---

[2] Kwa habari zaidi juu ya kubatizwa katika Roho Mtakatifu, ona Sura ya 10, 11, na 20.

na kuwatengeneza kuwa viongozi wa kimishenari. Njia moja aliyotumia Yesu kufanya hivyo ilikuwa kwa kuwatuma katika safari fupifupi za umisheni. Aliwaelekeza, akawapa vitendea kazi, kisha akawatuma (Lk. 9:1-6; 10:1-16). Waliporudi, aliwaambia kuhusu kazi yao (10:17-20).

Wanafunzi kumi na wawili wa Yesu hawakuzaliwa wakiwa viongozi. Wala kwa asili hawakuwa na nia ya utume. Walikuwa watu wa kazi za kawaida. Lakini, walikuwa tayari kuweka maisha yao mikononi mwa Yesu ili kutengenezwa naye. Kupitia maisha na mafundisho Yake, Yesu aliwapa maono yake ya kimataifa. Aliwaagiza hivi: "Nendeni mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (Mt. 28:19). Zaidi, alisisitiza kwamba ni vizuri watiwe nguvu na Roho Mtakatifu, kama vile Yeye alivyokuwa (Lk. 4:18-19; Mdo. 1:8).

Katika mojawapo ya mikutano ya awali ya Petro na Bwana, alijionyesha kuwa kiongozi anayeweza kutengenezwa. Alimsihi Yesu akisema, "Ondoka kwangu, Bwana; Mimi ni mtu mwenye dhambi!" (Lk. 5:8). Petro alihisi kutostahili kwa jinsi alivyokuwa. Lakini, Yesu alijua uwezo wa Petro. Kwa hiyo akamjibu Petro na kumwambia, "Usiogope; tangu sasa utavua watu" (mst. 10). Petro alipokuwa akitembea na Yesu, aligeuzwa kuwa kiongozi wa kimishenari mwenye nguvu tunayesoma habari zake katika kitabu cha Matendo.

Biblia inasema, "Yesu aliweka mitume kumi na wawili ili wawe pamoja naye na kwamba awatume kuhubiri" (Mk. 3:14). Kwa kutumia wakati pamoja na Yesu, kusikiliza mafundisho Yake, na kutazama matendo yake, wanafunzi wakawa kama Bwana wao. Yesu aliwafinyanga wawe viongozi wa kimisheni, kila mmoja kwa njia ya kipekee, kwa kazi ya kipekee. Kwa sababu alifanya hivyo, Kanisa alilolianzisha linaendelea hadi leo. Kama wachungaji wa Kipentekoste, tungetumia muda na viongozi wamishenari tarajiwa ambao ni wazuri. Tunapomfuata Yesu kwa ukaribu, na kushirikiana na wengine wanaofanya hivyo hivyo, tutabadilishwa.

Tumeshapewa fimbo ya uongozi. Inatupasa sisi nasi tujitahidi kuwa viongozi wa kimishenari wa kweli. Sawa na Yesu na mitume, ni lazima tufanye kazi kuwaendeleza wengine. Paulo alimwandikia Timotheo hivi: "Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. Na mambo yale uliyonisikia nikisema mbele ya mashahidi wengi, uwakabidhi watu wa kutegemewa, watakaofaa pia kuwafundisha wengine" (2 Tim. 2:2).

## THAMANI YA UTUME

Hatua ya kimishenari huinuka kutokana na shauku ya utume. Shauku ni hamu kubwa ya kufikia kitu muhimu. Mtunga Zaburi alizungumza juu ya nia ya Mungu kwa Mwanawe - na kwa mataifa. Baba alimwambia Mwana hivi: “Uniombe, nami nitafanya mataifa kuwa urithi wako, miisho ya dunia kuwa milki yako” (Zab. 2:8). Kama watoto wa Mungu, tunaweza kuungana na Mwana katika sala hii ya umisheni. Kufanya hivi kutajenga ndani yetu hamu kubwa ya kuona marafiki na majirani zetu wakija kwa Yesu. Wakati huo huo, itajenga ndani yetu shauku ya kuona mataifa yakifikiwa na habari njema ya wokovu katika Kristo.

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufanye nia ya Mungu kuwa yako hata wewe. Hivyo ndivyo Abrahamu alivyofanya. Ingawa alikuwa mzee na hana mtoto, Mungu alimwambia, “Tazama mbinguni na uzihesabu nyota….Ndivyo utakavyokuwa uzao wako” (Mwa. 15:5). Ibrahimu aliamini ahadi ya Mungu na kushiriki matarajio yake. Kwa sababu ya utii wake, akawa baba wa wote waaminio (Rum. 4:11). Mwombe Mungu akupe shauku yake kwa mataifa. Kisha ruhusu shauku hii ikusukume kuhamasisha kanisa lako kushiriki katika utume wa Mungu.

## HATUA YA UMISHENI

Ingawa shauku ya utume ni muhimu, yenyewe tu haitoshi. Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufanye kazi ili kubadili shauku kuwa halisi. Paulo ni mfano wa ukweli huu. Alikuwa na shauku ya kuona watu wa mataifa mengine wakimgeukia Kristo (Mdo. 22:21; Rum. 10:1). Tamaa hii ilimlazimisha kufanya kazi bila kuchoka kwa ajili ya wokovu wao. Alishuhudia, “Nilifanya kazi kwa bidii zaidi kuliko wao wote — wala si mimi, bali ni neema ya Mungu iliyokuwa pamoja nami” (1 Kor. 15:10). Vivyo hivyo, wewe pia lazima ugeuze matarajio yako ya kimishenari kuwa hatua ya utume. Lazima ujitahidi kukuza kanisa lako kuwa kanisa la kimishenari kweli.

### Kuweka Maono ya Umisheni

Wajibu mkubwa wa kila mchungaji wa Kipentekoste ni kuingiza shauku kwa ajili ya waliopotea katika mioyo ya watu wa Mungu. Ni lazima watu watambue upotevu wa wale walio nje ya kuta za kanisa lao. Ni lazima pia wahisi upotevu wa watu hao ambao hawajafikiwa, wanaoishi katika maeneo ambayo hayajafikiwa kotekote barani Afrika na duniani kote. Ili hili lifanyike, utahitaji kuhubiri, kufundisha, na kuonyesha mfano wa umisheni mbele ya kusanyiko lako. Na

utahitaji kuvumilia hadi kila mshirika wa kanisa aelewe wajibu wake wa kushiriki katika *missio Dei*.

Maono ya umisheni hutiwa ndani ya mioyo ya watu wa Mungu kwa njia mbili: kwa Roho wa Mungu na kwa Neno la Mungu. Nguvu ya Roho na neno kutoka kwa Bwana la wakati ufaao ndiyo vilivyobadili mtazamo wa Petro kuhusu Mataifa (Mdo. 10:9-16, 19-20). Kama kiongozi wa kimishenari, lazima uhakikishe kwamba nguvu sahihi ipo katika kanisa lako. Lazima uhakikishe kwamba Roho anatembea kwa nguvu katika huduma zako, na lazima ujitahidi kuona kwamba kila mshirika amejazwa Roho kweli. Muda wote huo ni vizuri uwaeleze watu kwa nini Roho wa Mungu anatembea. Roho wa Mungu wa kimishenari huwatayarisha kushiriki katika utume wa Mungu.

Wakati huo huo, lazima uwafundishe watu kile Biblia inachosema kuhusu utume wa Mungu. Na lazima uwaonyeshe jinsi wanavyopaswa kuitikia kwa Roho na Neno. Ni lazima wajitoe kuombea waliopotea kwa bidii, kutoa kwa ukarimu katika umisheni, na kushirikisha habari njema kwa uaminifu na wale walio karibu nao. Hatimaye, lazima uwape changamoto ya kujitoa kwa utume wa Mungu.

Kama kiongozi wa kweli wa kimishenari, lazima uliongoze kanisa lako litoke kujifikiria hadi kuwafikiria watu wengine, kutoka kuzingatia matakwa yao wenyewe na mahitaji yao hadi kuzingatia mahitaji ya dunia iliyopotea inayowazunguka. Safari hii ya utume itahitaji hisia kali ya kukusudia kwa upande wako. Pia itahitaji ufanye marekebisho katika mpango na mabadiliko ya kanisa lako katika madhumuni na yaliyomo ya mikutano yako.

**Kushirikisha Hadithi za Wamishenari**

Njia moja iliyothibitishwa inayoweza kukuza kanisa lenye nia ya umisheni ni kushirikisha watu wako hadithi za umisheni. Unaweza kufanya hivi kwa kujumuisha hadithi hizi katika mahubiri na mafundisho yako. Nyingi ya hadithi hizo zinapatikana katika Biblia. Hadithi ya Yesu ndiyo hadithi kuu ya umishenari iliyowahi kusimuliwa. Na kitabu cha Matendo kimejaa hadithi za kusisimua za kimishenari. Unaweza pia kukusanya hadithi kwa kusoma vitabu vya wamishenari na kwa kuwasikiliza wamishenari wakizungumza. Kwa kuongezea, hupaswi kusita kushirikisha kusanyiko lako hadithi zako mwenyewe za umishenari.

**Kupanga Huduma za Umisheni**

Pia utataka mara kwa mara kuwapangia wamishenari fursa za kuzungumza na kanisa lako. Unaweza kuwaalika waje kwa huduma maalum ya umisheni au

wikiendi ya uhamasishaji wa umisheni. Wamishenari wanapokuja, hupaswi kusahau kulipia gharama zao za usafiri. Na utapenda kutoa nafasi kwa kusanyiko kushiriki katika huduma ya mishenari husika kwa kupokea sadaka ya ukarimu kwa ajili yao. Kanisa pia linapaswa kufikiria kumtegemeza mmishenari kwa muda endelevu.[3]

**Kuunda "Mizunguko ya Mafanikio"**

Njia nyingine nzuri ya kuingiza maono ya umisheni katika mioyo ya watu ni kupitia "mizunguko ya mafanikio." Wazo hili linatokana na hadithi ya Daudi. Kabla ya kuwa mfalme wa Israeli, aliongoza kampeni ndogo ndogo za kijeshi zilizofaulu. Watu walimheshimu Daudi, wakisema, "Wewe ndiwe uliyewaongoza Israeli katika vita vyao" (2 Sam. 5:2). Au, "Ni wewe uliyewaongoza na kuwaleta Israeli." Maneno "kuongozwa na kuletwa" huzungumzia mizunguko ya mafanikio, na kupendekeza wazo la kuongoza shughuli za umisheni za muda mfupi zinazoweza kufikiwa. Kila mafanikio yatawatia moyo watu kuweka malengo makubwa zaidi.

Kwa mfano, mwanzoni unaweza kupanga kampeni ya "Ombea Majirani Zako". Pata majina ya majirani na elekeza kanisa liwaombee. Watu wanapoanza kuonja mafanikio, watatiwa moyo kwenda nje ya kuta za kanisa. Mafanikio madogo yatafungua mioyo yao kuwa wamishenari zaidi. Watahimizwa kuwafikia watu zaidi ya wao wenyewe katika mizunguko ya mafanikio inayoongezeka.

Mafanikio haya yanaweza kusababisha kuongezeka kwa ufadhili na mafunzo ya umisheni. Baada ya muda, kanisa linaweza kupeleka timu za umisheni wa muda mfupi katika miji na vijiji vingine kwa ajili ya uinjilisti na kampeni za upandaji kanisa. Wengine wanaweza hata kuhamasishwa kusafiri kwenda nchi zingine kusaidia wamishenari katika kazi zao, au kupanda makanisa huko. Wakati timu hizi zikitoa ripoti kwa kanisa, watu watahimizwa kushiriki zaidi katika umisheni.

## TIMU YA UMISHENI YA KANISA LA MAHALI PAMOJA

Kumbuka msemo wa kale wa Kiafrika: "Ukitaka kwenda haraka, nenda peke yako; ukitaka kwenda mbali, nendeni wengi." Utataka kuunda kamati ya umisheni

[3] Ili kujifunza zaidi kuhusu kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya umisheni, tazama Sura ya 40: "Kutengeneza Mpango wa Umisheni wa Kanisa la Mahali Pamoja."

wa ndani, au timu, ili kukusaidia katika kazi. Wanaume na wanawake hawa wenye maono watakusaidia kuhamasisha kanisa kwa ajili ya umisheni.

Kanisa la kimishenari linaweza kulinganishwa na timu ya mpira wa miguu. Hapo, mchungaji haangaliwi kama mchezaji nyota, bali kama kocha. Na timu ya misheni ni wakufunzi wake. Washirika wa kanisa si mashabiki; ni wachezaji uwanjani. Kazi ya mchungaji na timu ya umisheni ni kutafuta wachezaji, kuwafundisha, kuwatia moyo, na kuwatuma kama timu yenye kushinda.

Kabla Yesu hajawachagua wale Kumi na Wawili, alikesha usiku kucha akimwomba Mungu (Lk. 6:12). Wewe pia utataka kuchagua timu yako ya umisheni kwa maombi. Tafuta watu waliojaa imani na Roho Mtakatifu, watu wenye mtazamo na ujuzi sahihi wa kubariki kazi. Kisha kutana na timu ya umisheni mara kwa mara ili kuomba nao na kuweka mipango. Kwa pamoja, mtakuza uinjilisti wa kanisa, upandaji kanisa, na mpango wa umisheni. Utaweka vipaumbele vya kimkakati na kukuza bajeti ya umisheni ya kanisa.

---

Yesu alipokuwa karibu kurudi mbinguni, aliliachia Kanisa Lake amri ya mwisho na ahadi ya mwisho. Amri yake ilikuwa hii: “Msiondoke Yerusalemu, bali ingojeeni ile zawadi ambayo Baba yangu aliahidi, ambayo mmenisikia nikisema juu yake. Kwa maana Yohana alibatiza kwa maji, lakini baada ya siku chache ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu” (Mdo. 1:4-5). Ahadi yake ilikuwa hii: “Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (mst. 8).

Kwa maneno haya, Yesu alikuwa akiwakumbusha wanafunzi Wake kwamba ujuzi ambao ungewatokea karibuni Siku ya Pentekoste ungehusiana kwa karibu na utume Wake wa kuwakomboa mataifa. Kwa hiyo, kuwa Mpentekoste maana yake ni kuwa mishenari. Basi, ili mtu awe mchungaji wa kweli wa Kipentekoste lazima awe kiongozi wa kimishenari mwenye bidii. Kama kiongozi wa kimishenari, mchungaji wa Kipentekoste ameteuliwa na Kristo kuliongoza kanisa Lake katika utume unaowezeshwa na Roho, nyumbani hadi miisho ya dunia.

~ Sehemu ya 8 ~

# Mchungaji wa Kipentekoste Kama Msimamizi

~ Sura ya 32 ~

# Kutunza na Kusimamia Taarifa, Fedha, na Mali

Yesu alisimulia kisa cha mtu tajiri ambaye aligundua kwamba msimamizi wake wa mali alikuwa akifuja mali yake. Alimwita huyo meneja asiye mwaminifu na kumtaka atoe hesabu ya jinsi alivyoshughulikia biashara ya mwajiri wake (Lk. 16:1-2).

Biblia inafundisha kwamba kila mfuasi wa Kristo ni msimamizi wa mali ya Mungu. Hiyo ni kwa sababu kila kitu anachomiliki ni mali ya Mungu (Zab. 24:1; Yakobo 1:17). Biblia inafundisha zaidi kwamba siku moja Mungu atataka kila Mkristo atoe hesabu ya jinsi alivyosimamia mali ya Mungu. Paulo anaonya, “Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja wetu apokee ijara yake kwa mambo aliyotenda wakati alipokuwa katika mwili, kwamba ni mema au mabaya” (2 Kor. 5:10).

Kanuni hii hii inatumika kwa mchungaji wa Kipentekoste. Ni lazima akumbuke ukweli kwamba kanisa analoliongoza ni la Kristo. Yeye ni msimamizi tu wa kanisa la Kristo, na siku moja atamjibu kwa jinsi alivyosimamia mali zake.

## MCHUNGAJI WA KIPENTEKOSTE AKIWA MENEJA

Paulo aliwaandikia Wakristo wa Korintho, akisema, “Sasa imewapasa wale waliokabidhiwa [mali] wawe waaminifu” (1 Kor. 4:2). Kama mwangalizi aliyeteuliwa na Mungu mwenye kanisa, mchungaji wa Kipentekoste lazima asimamie nyumba ya Mungu kwa uaminifu na kwa njia ipasayo. Hii inajumuisha mambo ya kiroho na ya kimwili ya kusanyiko. Mchungaji lazima aangalie kwa makini roho za watu. Wakati huo huo, anapaswa kusimamia kwa uaminifu shughuli za kanisa. Hii ni pamoja na taarifa za kanisa, fedha na mali.

Pamoja na karama za mitume, manabii, waalimu, miujiza, na nyingine, Mungu amelipa kanisa karama ya “maongozi,” au, kama tafsiri zingine zinavyosema, karama ya “kusimamia,” ili kusaidia kuujenga mwili. ya Kristo (1 Kor. 12:28). Paulo aliandika kwamba “mwangalizi huisimamia nyumba ya Mungu” (Tito 1:7). Hivyo ni wajibu wa mchungaji kulisimamia vyema kanisa la Mungu. Paulo alimwambia Tito kwamba, pamoja na mambo mengine, mwangalizi lazima awe “mkamilifu… mwadilifu… na mwenye nidhamu” (mst. 8). Kila moja ya sifa hizi ni sifa za meneja mzuri.

Ingawa masuala ya kiutawala yatakayojadiliwa katika sura hii yanaweza kuonekana kuwa ya kawaida kwa wengine na kuwa mbali na wito wa mchungaji wa Kipentekoste, ni muhimu sana. Jinsi mchungaji anavyoshughulikia masuala haya yaweza kuathiri sana huduma yake ya kichungaji. Wachungaji wa Kipentekoste ambao wanashindwa kushughulikia vizuri mambo ya kawaida ya kanisa wanaweza kujiondoa wenyewe katika kushughulikia mambo yake ya kiroho. Petro alionya, “Kila mmoja wenu na atumie kipawa chochote alichopokea kuwahudumia wengine, kama mawakili waaminifu wa neema ya Mungu katika namna zake mbalimbali” (1 Pet. 4:10).

Ingawa kanisa ni zaidi ya biashara, ni kama biashara. Kwa kiasi kikubwa, mafanikio ya biashara yoyote hutegemea jinsi inavyopangwa na kusimamiwa vizuri. Wengine wamepinga hoja hii na kusema kwamba kwa kuwa kanisa ni kitu hai wala si shirika, halihitaji mfumo wa shirika. Huo ni nusu tu ya ukweli. Ni kweli kwamba kanisa, kama mwili wa Kristo, ni kitu hai. Lakini, si kweli kwamba halihitaji taratibu za kishirika. Ukweli ni kwamba kila kilicho hai kwa asili kimepangiliwa sana. Kwa mfano, katika mwili wa mwanadamu, kichwa kina mahali pake, kama vile mwili, mikono, miguu, na kadhalika.

Shirika linamaanisha utaratibu, na juhudi za umoja. Fenicha iliyojaa kwenye gari la kubebea mizigo inaweza kuwa yenye thamani, lakini haitumiki sana hadi itakapopakuliwa kutoka kwenye hilo gari na kuwekwa ndani ya nyumba kwa mpangilio mzuri. Vivyo hivyo, ili kanisa lifikie uwezo wake kamili, linahitaji kupangiliwa kwa uangalifu.

Kila mchungaji wa Kipentekoste lazima ajitahidi kukuza ujuzi wake wa utawala, uongozi na usimamizi. Na kila kanisa linapaswa kuwa na mifumo iliyopangiliwa ili kuongoza mambo yake ya shughuli. Kadiri kanisa linavyoendelea na kukua, muundo wake wa shirika utakuwa mgumu zaidi na mifumo yake ya kutunza kumbukumbu kuwa yenye kina zaidi. Majukumu matatu ya usimamizi ya kila mchungaji wa Kipentekoste ni (1) kutunza kumbukumbu za kanisa, (2) kusimamia fedha za kanisa, na (3) kuhifadhi mali za kanisa. Sehemu iliyobaki ya sura hii itashughulikia majukumu haya ya kichungaji.

## KUTUNZA KUMBUKUMBU ZA KANISA

Mchungaji wa Kipentekoste anayefaa atawekeza muda na nguvu zinazohitajika ili kutunza taarifa sahihi za kanisa. Hizo taarifa zilizoandikwa zitamnufaisha mchungaji na kanisa kwa njia kama nne za muhimu.

Kwanza, mfumo mzuri wa kutunza kumbukumbu utamwezesha mchungaji kupata taarifa muhimu inapohitajika. Na kwa sababu taarifa zimetunzwa vyema, zitakuwa za kuaminika.

Pili, taarifa zilizotunzwa vizuri zinaweza kumsaidia mchungaji kusimamia na kulinda mali za kanisa. Zinaweza pia kutumika kama uthibitisho wa kisheria wa umiliki wa kanisa na shughuli za kifedha. Kwa mfano, kama mtu atapinga umiliki wa ardhi ya kanisa, mchungaji ataweza kutoa hati ya mali hiyo haraka na kuthibitisha ukweli wake.

Tatu, kumbukumbu nzuri humpa mchungaji wa Kipentekoste habari muhimu anazohitaji kufanya maamuzi ya busara kuhusu mustakabali wa kanisa. Kwa mfano, kwa kuchunguza taarifa ya mahudhurio ya miaka iliyopita, mchungaji anaweza kuelekeza ukuaji wa kanisa katika siku zijazo. Habari hii inaweza kusaidia uongozi kufanya maamuzi juu ya ujenzi wa siku zijazo na mahitaji ya wafanyakazi. Kwa njia hiyo hiyo, kwa kuchunguza jinsi ndoa nyingi zilivyofungwa miaka iliyopita, mchungaji anaweza kukadiria ni ndoa ngapi atakazofunga mwaka ujao. Kwa hivyo anaweza kutumia taarifa kutoka zamani kutabiri mwelekeo wa siku zijazo.

Nne, kumbukumbu nzuri humpa mchungaji na kanisa muunganiko na siku za zamani. Husaidia kumjulisha mchungaji na washirika juu ya yale yaliyowatangulia. Kumbukumbu hii ya kihistoria itawasaidia kuthamini watangulizi wao, na itawapa hisia ya kuwa na mali na kudumu.

**Kanuni za Usimamizi Bora wa Kumbukumbu**

Wakati utafika ambapo kila mchungaji ataombwa kukabidhi hatamu za uongozi kwa atakayemrithi. Mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste atalitayarisha kanisa kwa ajili ya tukio hili lisiloepukika. Njia moja anayoweza kufanya hivyo ni kwa kuweka kumbukumbu sahihi za kanisa. Hapa kuna kanuni tano za utunzaji mzuri wa kumbukumbu.

1. Usahihi. Kumbukumbu zote na hati lazima ziwe sahihi. Lazima ziwakilishe taarifa ya kweli ya kile kilichotokea.
2. Zilizopangiliwa. Kumbukumbu za kanisa zinapaswa kupangwa vizuri. Lazima zipangwe kwa mujibu wa mantiki, na hivyo kusababisha ufikiwaji bora wa habari inapohitajika.
3. Kwa wakati. Kumbukumbu za sasa lazima zihifadhiwe kwa namna ya kisasa. Shughuli zote za kifedha zinapaswa kutumwa mara moja. Matukio mengine, kama vile kuwekwa wakfu kwa watoto, ubatizo, na arusi, zapaswa kurekodiwa kwa wakati muafaka.
4. Zilizokamilika. Kumbukumbu za kanisa lazima ziwe kamili. Mambo yote muhimu kuhusu tukio au shughuli yanapaswa kurekodiwa.
5. Usalama. Kumbukumbu zote lazima ziwekwe mahali salama, dhidi ya wezi na hali mbaya ya hewa.

**Miniti Sahihi**

Mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuhakikisha kwamba mihutasari sahihi ya mikutano yote rasmi ya kanisa inatunzwa. Hii ni pamoja na mikutano ya baraza ya kila mwezi, mikutano mikuu ya kila mwaka kanisa, na mikutano maalum ya shughuli inayoitishwa. Miniti za kila mkutano zinapaswa kuhifadhiwa na katibu aliyeteuliwa na kuwasilishwa kwenye mkutano unaofuata ili kuidhinishwa. Baada ya kuidhinishwa, zinapaswa kutiwa sahihi na katibu na mchungaji na kuwekwa kwenye faili za kanisa kwa ajili ya marejeo ya baadaye.

**Daftari la Matukio**

Kila mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kuwa na daftari la matukio ya kikanisa. Daftari hilo litakuwa na kumbukumbu ya washirika wa kanisa, ubatizo

wa maji, harusi, kuwekwa wakfu kwa watoto, na mahudhurio ya kanisa, kama ifuatavyo:

Washirika wa kanisa. Daftari la matukio ya kanisa linapaswa liwe na orodha ya washirika wa kanisa. Majina kamili ya wanachama wote wapya yanapaswa kuongezwa kwenye orodha watakapopokelewa rasmi kama washirika. Orodha hiyo pia inapaswa kuwa na tarehe ya kupokelewa na maoni mengine yoyote muhimu kuhusu kupokelewa kwao. Wakati mshirika yeyote anapokufa au kuondoka kanisani, matukio haya yanapaswa kuzingatiwa. Ni vizuri kutoa cheti cha uanachama au kadi kwa wanachama wapya kama sehemu ya sherehe zao za mapokezi. Nakala zinapaswa kuwekwa kwenye faili za kanisa.

Ubatizo wa maji. Daftari la matukio vile vile linapaswa kuwa na orodha ya wale wanaobatizwa katika maji, pamoja na tarehe ya ubatizo wao na umri wao wanapobatizwa. Cheti cha ubatizo kinapaswa kutolewa kwa kila mhusika.

Harusi. Daftari la matukio ya kanisa linatakiwa kuwa na kumbukumbu ya wote waliofunga ndoa kanisani. Hii kumbukumbu inapaswa kujumuisha tarehe ya harusi na majina kamili ya bwana na bibi arusi. Pia kuwe na jina la msajili anayefunga hiyo harusi pamoja na orodha ya wengine wote walioshiriki rasmi katika hafla hiyo. Mchungaji pia anaweza kutaka kurekodi tarehe ambayo wanandoa walitangaza rasmi uchumba wao kwa kusanyiko. Kufuatia sherehe ya harusi, cheti cha ndoa kinapaswa kutolewa kwa wanandoa. Mchungaji lazima azingatie sheria zote za kiserikali kuhusu ndoa.

Kuwekwa wakfu watoto. Mchungaji wa Kipentekoste anapaswa pia kusajili watoto wote wanaowekwa wakfu hapo kanisani. Ingawa makanisa ya Kipentekoste hayabatizi watoto wachanga, yanaweka watoto wakfu. Hana kumtoa Samweli mtoto wake ni mfano mzuri wa desturi hii (1 Sam. 1:21-28). Baada ya sherehe ya kuwekwa wakfu, ni vizuri mchungaji aandike jina kamili la mtoto katika daftari ya matukio, pamoja na tarehe ya kuzaliwa kwa mtoto, mahali mtoto alipozaliwa, na tarehe ya huko kuwekwa wakfu. Vile vile, hayo maelezo yanapaswa kuwa na majina ya wazazi, anwani ya wazazi na namba za mawasiliano, na maelezo mengine yoyote yanayofaa, na ya muhimu. Mchungaji anapaswa kutoa cheti cha mtoto kuwekwa wakfu kwa wazazi.

Mahudhurio kanisani. Mchungaji pia anapaswa kufuatilia mahudhurio ya kila wiki ya kanisa. Kumbukumbu hizi zinapaswa kuonyesha tarehe na idadi ya watu wanaohudhuria kila darasa la Shule ya Jumapili, ibada ya Jumapili asubuhi, ibada

ya Jumapili jioni, pamoja na ibada zozote za watoto, vijana na katikati ya juma. Kumbukumbu hizi zinapaswa kuhifadhiwa na mchungaji au katibu wa kanisa.

**Kumbukumbu ya Mahubiri**

Mbali na kumbukumbu za kanisa, unaweza kutaka kuweka kumbukumbu binafsi ya mahubiri unayohubiri. Kila wakati unapotoa mahubiri, kufundisha somo, au kuzungumza hadharani katika kongamano lolote, ni vizuri uandike tukio hilo katika daftari la mahubiri. Kila unapofanya hivyo, weka tarehe, tukio na mahali mahubiri yalipotolewa. Ni vizuri pia kuhusisha Maandiko yaliyotumiwa, pamoja na kichwa cha ujumbe. Unaweza pia kutaka kuongezea habari za itikio la watu kwa ujumbe. Kumbukumbu hii itakusaidia kufuatilia ujumbe wako, na hata kutathmini ratiba yako ya kuhubiri. Unaweza pia kuweka jumbe zako mahali salama kwa ajili ya marejeo ya wakati ujao.

## KUSIMAMIA FEDHA ZA KANISA

Pia mchungaji wa Kipentekoste ni vizuri ahakikishe kwamba kumbukumbu sahihi na za wakati zinawekwa za shughuli zote za kifedha zinazohusiana na kanisa. Utaratibu huu utahakikisha kwamba fedha za kanisa zinashughulikiwa ipasavyo kila wakati. Pia itasaidia kumlinda mchungaji na viongozi wa kanisa dhidi ya mashtaka ya kutumia vibaya fedha za kanisa.

**Kupokea na Kushughulikia Sadaka**

Makanisa mengi ya Kipentekoste barani Afrika yanategemezwa kupitia zaka na matoleo yanayopokelewa wakati wa ibada zao za Jumapili asubuhi. Ingawa matoleo haya yanaweza kupokelewa kulingana na desturi za kanisa la mahali, mchungaji lazima ahakikishe kwamba kila utoaji unashughulikiwa kwa uaminifu na uwazi kabisa.

Ili kufanya hivyo, atahitaji kuhakikisha kwamba matoleo yanakusanywa kila mara na kuhesabiwa na viongozi waaminifu wa kanisa, wawili au zaidi. Baada ya kuhesabu matoleo, hao hao viongozi wanapaswa kujaza fomu ya matoleo. Kwenye hiyo fomu panapaswa kuwepo mahali pa kujaza tarehe ya siku husika, aina ya/za matoleo yaliyopokelewa, na majina na sahihi za waliohesabu. Fomu hiyo pia inapaswa kuwa na mistari mbalimbali ya kuandika kila aina ya matoleo yaliyopokelewa. Kwa mfano, mstari mmoja uandikwe "zaka," mwingine uitwe "sadaka za kawaida," mwingine "fedha za ujenzi," mwingine "umisheni," na kadhalika. Wahesabuji wanapaswa kuhakikisha kuwa kiasi chote cha matoleo yaliyopokelewa kimewekwa katika nafasi yake sahihi.

Fomu hizi za matoleo zinapaswa ziwe na nakala: moja iende kwa mweka hazina wa kanisa na nyingine iende kwa mchungaji. Kisha mweka hazina atahesabu tena pesa na kuingiza kila kiasi kilichopokelewa kwenye kitabu kiitwacho leja ya kanisa katika nafasi yake stahiki. Kisha ataweka pesa benki. (Ikiwezekana, kila kanisa linapaswa kuwa na akaunti ya benki. Hili lisipowezekana, fedha zinapaswa kuwekwa kwenye kabati iliyo salama, iliyofungwa, au sanduku/kasha imara.) Mweka hazina anapaswa kuhifadhi risiti yenye kuonyesha fedha imewekwa benki kwa ajili ya kumbukumbu za kanisa.

**Kutunza Kumbukumbu za Fedha**

Kumbukumbu za uhasibu zinaweza kuwekwa kwenye kitabu cha leja au kwenye kompyuta. Kompyuta ikitumiwa, lingekuwa jambo la hekima kuchapisha taarifa kila juma ili kuweka kwenye faili, kwa kuwa nyakati zingine kompyuta hukwama au kukataa kazi. Wakati wowote pesa inapopokelewa au kutolewa, shughuli hiyo inarekodiwa kwenye stakabadhi ya pesa taslimu. Kisha, hiyo stakabadhi hupewa mweka hazina wa kanisa ambaye huirekodi kwenye daftari ya fedha.

Kila mchungaji wa Kipentekoste lazima ajifunze kusoma na kuchambua kitabu cha kumbukumbu ya fedha. Ustadi huu utamwezesha kufuatilia shughuli za kifedha za kanisa na kujua ni kiasi gani cha pesa kinapatikana katika kila mfuko wakati wowote. Kitendo hiki kitamwezesha mchungaji na viongozi wa kanisa kufanya maamuzi ya busara ya kifedha. Na itasaidia kuhakikisha kwamba kumbukumbu za fedha za kanisa zinashughulikiwa vyema.

**Kutoa na Kutumia Fedha za Kanisa**

Sadaka yoyote inayotolewa kwa kanisa inapaswa kutumika kwa kusudi la kutolewa kwake tu. Ni kinyume cha maadili kuchukua fedha zilizotolewa kwa ajili ya mfuko wa ujenzi na kuzitumia kumnunulia mchungaji gari. Wakati wowote pesa inapotolewa au kuhamishwa kutoka kwa mtu mmoja au mpango hadi kwingine, lazima risiti itolewe kwa mweka hazina kwa ajili ya utaratibu sahihi wa kihasibu. Stakabadhi zote zinapaswa kuhifadhiwa katika faili za hesabu za kanisa.

**Taarifa za Fedha**

Mwishoni mwa kila mwezi, mweka hazina wa kanisa anapaswa kuandaa taarifa ya fedha kwa ajili ya mchungaji na halmashauri ya kanisa. Hii taarifa itawapa uongozi wa kanisa kumbukumbu sahihi ya mapato na matumizi kwa mwezi uliopita. Hii itawasaidia kufanya maamuzi ya busara kuhusu fedha za

kanisa. Pamoja na taarifa za fedha za kila mwezi, mweka hazina wa kanisa anapaswa kutoa taarifa ya fedha ya mwaka na kuiwasilisha kwa mchungaji na halmashauri ya kanisa. Mchungaji na halmashauri wataitoa taarifa ya fedha ya kila mwaka kwa washirika wa kanisa katika mkutano mkuu wa kila mwaka.

**Bajeti**

Ni muhimu kwamba mchungaji wa Kipentekoste ajue jinsi ya kuandaa na kufuata bajeti ya kila mwaka ya kanisa. Zoezi hili litawasaidia kusimamia vyema fedha za kanisa. Bajeti ni mpango wa kifedha. Ni makadirio ya mapato ya kanisa kwa mwaka unaokuja na mpango wa jinsi ya kutumia mapato hayo. Bajeti nzuri itahusisha umisheni na vipaumbele vya kanisa. Kwa mfano, ikiwa kanisa linatanguliza umisheni na upandaji wa kanisa jipya mahali, bajeti inapaswa kuonyesha kipaumbele hicho. Kwa njia hii, bajeti inaweza kutazamwa kama hati ya kimkakati ya utume.

Kutayarisha bajeti ya kanisa kunamhitaji mchungaji na halmashauri ya kanisa watazame shughuli za kifedha za kanisa kwa miaka iliyopita. Kisha, kwa kutumia habari hiyo, wanaweza kufanya maamuzi ya kimkakati kuhusu jinsi kanisa litakavyogawanya fedha zake katika mwaka ujao. Zoezi hili litasaidia kuhakikisha kuwa fedha za kanisa hazipotei kwa vitu vidogo, huku vitu muhimu zaidi vikiachwa bila kufadhiliwa.

Bajeti ina sehemu kuu mbili: makadirio ya mapato na makadirio ya gharama na matumizi kwa mwaka unaokuja. Mapato tarajiwa ni pamoja na zaka, matoleo maalum, na vyanzo vingine. Gharama na matumizi tarajiwa ni pamoja na matumizi yasiyobadilika (kama vile mishahara, malipo ya pango, na huduma) na matumizi yanayobadilika (kama vile vifaa vya ofisi, vifaa vya shule ya Jumapili, matangazo na matengenezo ya jengo). Kanisa linapaswa pia kupanga bajeti kwa ajili ya matumizi yasiyotarajiwa na ya dharura. Mwanzoni, kuandaa bajeti kutakuwa kugumu. Lakini baada ya miaka miwili au mitatu ya kufuatilia kwa uaminifu mapato na matumizi ya kanisa, mchakato wa kupanga bajeti utakuwa rahisi zaidi. Kisha itakuwa nyenzo kuu kwa ajili ya utendaji mzuri wa kanisa.

## KUTUNZA MALI ZA KANISA

Pia, kama msimamizi wa mali za Mungu, mchungaji wa Kipentekoste lazima ahakikishe kwamba mali za kanisa zinatunzwa vizuri. Mali hizi ni pamoja na hati muhimu za kanisa pamoja na jengo la kanisa, uwanja, na mali zingine.

**Kuhifadhi Nyaraka za Kisheria**

Mchungaji lazima ahakikishe kwamba hati za kisheria za kanisa zimewekwa kwa utaratibu na kuhifadhiwa mahali salama. Ikiwezekana, hati hizi ziwekwe kwenye sefu au kwenye sanduku la amana la usalama kwenye benki. Orodha ya vitu katika sanduku la amana ya usalama inapaswa kuwekwa kwenye faili za kanisa.

**Kutunza Mali za Kanisa**

Mchungaji wa Kipentekoste pia anawajibika kuona kwamba jengo la kanisa linatunzwa vizuri, na viwanja pia. Anaweza kutaka kuteua kamati ya matengenezo na misingi ya kusimamia jukumu hili. Kamati hii itahakikisha kwamba mali za kanisa hutunzwa inavyostahili nyumba ya Mungu. Sakafu na misingi vifagiliwe vizuri na kutokuwa na uchafu. Kuta zipakwe rangi na kusafishwa. Madirisha yawe katika hali ya usafi na katika hali nzuri. Fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya eneo zinapaswa kuwa sehemu ya matumizi ya bajeti ya kanisa.

Na vyombo na vifaa vya kanisa pia. Vyombo vya kanisa, kama vile mimbari, viti, madawati, fanicha za ofisi, na vyombo vya muziki vinapaswa kuwekwa katika hali ya usafi. Wakati matengenezo yanahitajika, yanapaswa kufanywa kwa wakati muafaka.

## ~ Sura ya 33 ~

# Kuhamasisha Viongozi Walei

Barani Afrika, si jambo la ajabu kuona watoto wakicheza soka katika viwanja wazi. Wengine hucheza na mpira halisi. Wengine, katika mazingira ya vijijini zaidi, hucheza na mpira wa kujitengenezea nyumbani kwa mifuko ya plastiki iliyofungwa kwenye mpira na kufungwa kwa nyuzi. Ni furaha iliyoje kuwaona wakikimbia, wakicheka, na kujitoa vilivyo kwa ajili ya timu zao.

Watoto wengine wamebahatika kucheza kwenye timu ya jamii. Huko, wanajifunza maadili ya kazi ya pamoja na kucheza kwa haki. Washiriki wa timu hujifunza kwamba kila mchezaji ni muhimu na wa thamani kwa timu. Ili timu ifanikiwe ni lazima kila mchezaji atoe chake kilicho bora. Hata katika kushindwa, kila mtu huvuta pamoja ili kutiana moyo. Watoto hujifunza kuwa mafanikio ya timu yanaamuliwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo wa wachezaji. Hii inajumuisha wote waliopo uwanjani na wale wa pembeni. Kanisa linaweza kujifunza mengi kutoka kwa timu ya soka inayosimamiwa vyema.

Kuna mtu aliwahi kuelezea soka la kulipwa kuwa ni watu ishirini na wawili wanaohitaji mapumziko, wakitazamwa na wengine elfu kumi ambao wanahitaji mazoezi! Cha kusikitisha ni kwamba, hali hii inaeleza makanisa mengi ya Kipentekoste leo barani Afrika. Ingawa washirika wachache ndio wanaobeba mzigo mkubwa wa huduma na kuchoka mno, wengi katika kusanyiko huchangia kidogo sana. Makanisa haya yamekuwa "uwanja wa michezo" ambapo wachezaji

wachache hushangiliwa na watazamaji wengi. Hali hii isiyofaa na isiyo ya kibiblia inalemaza ufanisi wa kanisa katika kutimiza utume wa Mungu. Ili kanisa lolote listawi, ni lazima mchungaji ajifunze kuhamasisha walei kwa ajili ya huduma ya ufalme.

Sura hii itaangazia changamoto hii. Kwanza, itaweka msingi wa kibiblia kuhusu uongozi wa kanisa. Kisha, itatoa ushauri unaoweza kufuatwa na wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, katika kuhamasisha walei kwa ajili ya huduma kanisani na katika jumuiya.

## KINACHOSEMWA NA BIBLIA

Tangu mwanzo wa Kanisa, mitume waliona haja ya kuhamasisha kila mtu kwa ajili ya huduma iliyowezeshwa na Roho. Yesu aliahidi hivi: “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8). Hii haikuwa kwa mitume tu. Ilikuwa kwa kila Mkristo, watumishi na wasiokuwa watumishi pia. Mpango wa Yesu kwa Kanisa ulikuwa kila mshirika ajazwe na Roho na kila mmoja ashiriki katika kutimiza utume wa Mungu.

### Kanisa la Kwanza

Mara tu baada ya kumwagwa kwa Roho siku ya Pentekoste, kanisa la kwanza lilianza kujipanga kwa ajili ya uinjilisti na uanafunzi. Biblia inasema, “Walidumu katika fundisho la mitume na katika ushirika” (Mdo. 2:42). Kisha inaongeza, “Kila siku waliendelea kukutana pamoja katika nyua za hekalu … wakimsifu Mungu na kufurahia kibali cha watu wote. Bwana akawazidisha kila siku wale waliokuwa wakiokolewa” (mst. 46-47). Viongozi walihitajika kutunza hivi vikundi vya nyumbani vilivyokuwa vinaibuka haraka. Bila shaka mitume walianza kuwaingiza baadhi ya waamini hao wapya katika shughuli za uongozi na huduma.

Kanisa lilipokua na kustawi, wengine walianza kujiunga na timu ya uongozi. Wanaume na wanawake hawa walitumikia chini ya mitume na kuwasaidia katika kazi yao. Leo, tunawaita watu hawa mashemasi. Mitume waliweka masharti kwamba viongozi hawa walei walihitaji kujazwa na Roho na hekima. Kazi yao ingekuwa kuandaa mpango wa kulisha wajane wa Kiyunani waliomfuata Bwana (Mdo. 6:1-7). Bila shaka, madaraka ya hao wanaume yalibadilika kadiri mahitaji

mengine yalivyotokea. Angalau wawili kati yao, Stefano na Filipo, wakawa watangazaji hodari wa injili.

Miaka mingi baadaye, baada ya taasisi ya kanisa kukua, kupangwa na kuendelea, Paulo aliwaeleza Waefeso muundo wa uongozi wa kanisa. Kanisa lilipaswa kuongozwa na mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu (Efe. 4:11). Lakini viongozi hawa hawakupaswa kufanya huduma peke yao. Kazi yao ilikuwa "kuwatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kazi za utumishi" (mst. 12). Walipaswa kuzaa viongozi walei wa kuwasaidia katika kazi hiyo. Kwa kufanya hivyo, kanisa lingekuwa na nguvu na ufanisi (mst. 11-16).

**Ukuhani Utume wa Waamini Wote**

Biblia inafundisha "ukuhani wa waamini wote." Maana yake ni kwamba kila mfuasi wa Kristo ni kuhani mbele za Mungu. Kama kuhani, ana haki ya kusoma na kufasiri Maandiko na kushirikisha neema ya Mungu kwa wengine (1 Pet. 2:5, 9). Tena Biblia inafundisha kuhusu "unabii wa waamini wote." Hii ina maana kwamba, kutokana na kuzaliwa mara ya pili na kujazwa na Roho Mtakatifu, kila mwamini amekuwa sehemu ya jumuiya ya kinabii ya Mungu ya siku za mwisho (Hes. 11:29; Yoe. 2:28-29; Mdo. 2:17-18). Kwa kuwapa Roho wake, Mungu amewatia nguvu kuwa mashahidi wa Kristo "katika Yerusalemu, na Uyahudi wote, na Samaria, hata mwisho wa nchi" (Mdo. 1:8).

Siku ya Pentekoste, Petro alianza mahubiri yake kwa kutangaza kwamba, "Hili [kumwagwa kwa Roho Mtakatifu] ndilo lililonenwa na nabii Yoeli: 'Siku za mwisho, asema Mungu, nitawamiminia watu wote Roho yangu. Wana wenu na binti zenu watatabiri' " (Mdo. 2:16-17). Petro alimaliza mahubiri yake kwa kuwaamuru watu hivi: "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu. Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Kisha Petro alitoa ahadi ya kushangaza: "Hii ahadi ni kwa ajili yenu na watoto wenu na kwa wote walio mbali — kwa wale wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita" (mst. 38-39). Petro alikuwa akisema kwamba siku ilikuwa imefika ambapo watu wote wa Mungu wangemtumikia wakiwa wahudumu waliotiwa nguvu na Roho.

Kutiwa nguvu na Roho kwa njia hiyo kunawawezesha watu wote, bila kujali jinsi walivyo wanyenyekevu au kutengwa, wazungumze na kuhudumu kwa ajili ya Kristo. Mchungaji wa Kipentekoste lazima atambue ukweli huu, na lazima awatie moyo watu wake kujazwa na nguvu za Roho na kuwa washirika hai katika huduma ya kanisa.

## UHITAJI WA VIONGOZI WALEI

Ili kanisa listawi na kukua kama Mungu anavyokusudia, lazima liwe na uongozi thabiti wa kichungaji. Ni lazima pia wawepo viongozi walei walio thabiti.

Changamoto kubwa inayokabili makanisa mengi ya Kipentekoste barani Afrika leo ni kwamba washirika wengi hawajajitosheleza katika uanafunzi. Hili limedhoofisha kanisa sana. Kwa sababu watu hawajafanya kazi kiasi cha kutosha, wachungaji wanafanya kazi zinazopaswa kufanywa na wengine. Kwa sababu hiyo, mara nyingi wachungaji wanajishughulisha sana na kazi ndogo ndogo kiasi kwamba hawana wakati wala nguvu za kutekeleza kazi zile kubwa kwa ufanisi.

Hadithi ya Yethro na Musa inadhihirisha jambo hili (Kut. 18:13-26). Musa alikuwa amewaongoza wana wa Israeli kutoka utumwani Misri. Sasa, walikuwa wanakuja kwake ili kusuluhisha kutokuelewana kwao. Walikuja wengi kiasi kwamba Musa aliketi akiwaamua tangu asubuhi hadi jioni. Hii iliendelea kila siku. Baada ya muda, Musa alichoka.

Yethro, mkwewe Musa, alipoona yaliyokuwa yakitendeka, alimshauri Musa, "Ufanyalo si jema….Kazi hii ni nzito kwako; huwezi kuifanya peke yako" (mst. 17-18). Kisha Yethro akamwambia Musa, "Chagua wanaume wenye uwezo kutoka kwa watu wote… na kuwaweka kuwa maofisa…. Uwaamuru wawe waamuzi wa watu nyakati zote, lakini waambie wakuletee kila jambo gumu…. Wakushirikishe " (mst. 21-22). Musa alifuata ushauri wa Yethro. Matokeo yake ni kwamba watu walihudumiwa vyema na Musa akapata pumziko.

Kama mchungaji wa Kipentekoste mwenye busara, lazima ufanye vivyo hivyo. Ni lazima uchague wanaume na wanawake wanaomcha Mungu ili wakusaidie katika kazi hiyo. Basi inabidi uwafundishe na kuwapanga kutekeleza kazi zao. Ukifanya hivyo, utakuwa huru na kazi za kila siku za kanisa. Na utaweza kuzingatia kazi ambazo wewe tu ndiye uwezaye kuzifanya. Na kanisa litakua na kustawi.

### Mabadiliko ya Kuzingatia

Ili hayo yafanyike, itabidi kuwe na mabadiliko katika mwelekeo. Ni lazima wewe uache kujiona kuwa ndiye mchezaji nyota kwenye timu na kujiona kama kocha. Kazi yako sio kufunga mabao, bali ni kuwafundisha watu jinsi ya kufunga mabao. Kazi yako si kushauri watu wote, lakini kuona kwamba watu wote wanapokea ushauri wa hekima (Kut. 18:21-22). Kazi yako si kulisha wajane wote

wa Kiyunani pekee yako, bali kuona kwamba wajane wote wa Kiyunani wanalishwa ipasavyo (Mdo. 6:1-3). Yaani, kama mchungaji, kazi yako ni "kuwatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kazi za huduma" (Efe. 4:11-12). Tangu unapoanza huduma yako katika kanisa lolote, anza kuandaa washirika kwa ajili ya huduma. Timu ya uongozi ya walei ya kanisa itatokea miongoni mwa watakaofundishwa.

**Kuhamasisha Viongozi Walei**

Kama mchungaji, lazima uwatambue, uwafundishe na kuwaingiza hao viongozi walei katika huduma. Unapaswa kuwaona washirika wa kanisa lako kama timu yenye watu walio na karama tofauti na ujuzi mbalimbali unaoweza kuhamasishwa kwa ajili ya huduma ya ufalme. Ili timu ifanikiwe, lazima kila mchezaji acheze sehemu yake. Kiongozi mlei ni mtu yeyote ambaye amechukua uongozi wa huduma yoyote katika kanisa. Hao ni mashemasi, wazee walei, wasimamizi na waalimu wa shule ya Jumapili, viongozi wa vikundi mbalimbali, viongozi wa huduma ya wanaume na wanawake, viongozi wa vijana, wakurugenzi wa huduma ya watoto, wakurugenzi wa kwaya, viongozi wa timu za sifa na ibada, wanakamati ya umisheni, na wengine.

## SIFA ZA VIONGOZI WALEI

Ingawa kila mshiriki wa kanisa ameitwa kuhudumu, si wote waliofuzu. Ili kutumika kama kiongozi katika kanisa, maisha ya mtu lazima yaendane na kiwango kilichowekwa katika Neno la Mungu. Paulo alisema hivi kuhusu mashemasi, "Ni lazima wajaribiwe kwanza; na ikiwa hakuna neno juu yao, na watumike" (1 Tim. 3:10).

Mitume katika kitabu cha Matendo waliweka sifa mbili za msingi kwa viongozi walei: lazima wawe "wamejaa Roho na hekima" (Mdo. 6:3). Katika 1 Timotheo sura ya 3 na Tito sura ya 1, Paulo anaorodhesha sifa za viongozi wa kanisa. Ingawa sifa nyingi hizi zinahusiana na wachungaji na wazee, bado zinafaa kuzingatiwa kama sifa za nafasi yoyote ya uongozi katika kanisa.

Kutokana na orodha hizi, tunapata mambo matano ya kuzingatiwa wakati wa kuteua viongozi kanisani. Hayo mambo matano ni (1) maadili, (2) uzoefu wao wa kiroho, (3) tabia zao, (4) mwenendo wao wa kila siku, na (5) ushuhuda wao katika jamii. Mchungaji anapaswa kuteua viongozi wale tu waliojazwa Roho, watauwa, waliojitoa, wanaofundishika, na walio tayari kutumika chini ya mchungaji kama viongozi walei.

## MAFUNZO YA WALEI, NA KUWAINGIZA KAZINI

Sawa na jinsi ambavyo kocha hutafuta waliofuzu ili kucheza kwenye timu yake, wewe pia kama kiongozi kanisani aliyeteuliwa na Mungu, lazima utafute watu waliofuzu ili kuongoza huduma za kanisa. Kama hakuna viongozi wenye sifa, wewe wafundishe na kuwatayarisha. Yesu alifanya hivyo na wanafunzi Wake, na Paulo alifanya hivyo na Timotheo, Tito, na wengine. Hebu tuangalie sehemu hizi mbili za kuhamasisha viongozi walei kanisani: kuwapata watendaji na kufundisha viongozi.

### Kuwapata Watendaji na Kuwaingiza Kazini

Mchakato wa kupata watendaji unahitaji mjadala na mazungumzo ya kina baina ya viongozi walioko wa kanisa. Pia yanahitajika maombi mengi ili kutafuta maongozi ya Mungu. Ndivyo Yesu alivyofanya. Katika huduma Yake yote, aliendelea kutafuta mwongozo wa Baba Yake (Lk. 5:16). Kwa mfano, kabla ya kuwachagua wanafunzi wake kumi na wawili, Yesu "alitoka akaenda mlimani kuomba, akakesha usiku kucha akimwomba Mungu" (6:12).

Mara tu unapopokea maelekezo kutoka kwa Bwana, ni vizuri uamue ni watendakazi gani watahitajika kukamilisha kazi. Kisha shirikisha maono hayo kwa kusanyiko na kuanza kuomba watu wajitolee. Unapoomba watu wa kujitolea, ni muhimu kuahidi kwamba yatakuwepo mafunzo kwa kazi hiyo. Hii itahimiza watu wengi zaidi kuitikia. Mara nyingi viongozi wazuri huibuka kutoka kwa wale wanaojitolea kwa huduma. Mara kwa mara jiulize hivi: "Ni nani katika kundi hili ana uwezo wa uongozi?" Pengine itabidi kuwaona watu fulani kibinafsi na kuzungumza nao kuhusu kupokea majukumu fulani ya uongozi.

### Kuendeleza Viongozi

Mara tu viongozi watarajiwa watakapotambuliwa, lazima waendelezwe. Huu ni wajibu wa kila mchungaji wa Kipentekoste. Kama ilivyokwisha elezwa, Paulo alionyesha kwamba kazi ya mchungaji ilikuwa "kuwatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kazi za huduma, ili mwili wa Kristo ujengwe" (Efe. 4:12). Unaweza kufanya hivyo kwa njia tatu:

*1. Mafunzo kazini.* Aina hii ya mafunzo ya uongozi hujulikana pia kama mafunzo kwa kuiga, au ya vitendo. Mchungaji humkabidhi kiongozi mtarajiwa kwa kiongozi mwenye uzoefu. Kiongozi mwenye uzoefu anamchukua kiongozi

mpya na kumwingiza katika utendaji chini yake na kumfundisha jinsi ya kuongoza huduma fulani.

*2. Semina*. Ni vizuri ufanye semina za mara kwa mara, warsha, au faragha kwa ajili ya kuwafundisha viongozi wapya.

*3. Ushauri*. Unaweza kutaka kuwashauri kibinafsi wale wanaoonyesha aina fulani ya kupiga hatua. Ili kufanya hivi utahitaji kuwa na muda na viongozi hao ili kuwafundisha kuhusu huduma. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya na wanafunzi wake (Yoh. 3:22). Alikuza uhusiano pamoja nao, akimimina maisha yake ndani yao. Baada ya muda, walifanana naye zaidi na zaidi (Mdo. 4:13). Yesu alieleza hivi: "Kila mtu ambaye amefundishwa kikamilifu atakuwa kama mwalimu wake" (Lk. 6:40).

## KUENDELEZA ROHO YA TIMU

Ili kanisa lifanye vizuri, ni lazima kuwe na hali ya umoja na kusudi moja kati ya watu. Watu lazima wajisikie kuwa ni sehemu ya kitu kikubwa kuliko wao wenyewe. Ni lazima waamini kwamba kanisa lao ni sehemu ya utume mkuu wa Mungu wa ukombozi, na kwamba lipo ili kutekeleza jukumu muhimu katika kutimiza utume huo.

Hii ni kweli hasa kwa viongozi walei. Ili wafanye vizuri zaidi, lazima wajisikie kuwa wao ni sehemu muhimu ya timu. Lazima wahisi kwamba wanatembea pamoja na wenzao wenye nia moja ili kufikia mwisho mzuri. Kama mchungaji, lazima ufanye bidii ili kukuza roho ya timu kama hiyo miongoni mwa viongozi.

### Unda Maono ya Pamoja

Kama mchungaji wa kanisa, wewe ndiye mlinzi na mkuzaji mkuu wa maono ya kanisa. Ni juu yako kukuza maono ya kawaida katika mioyo ya timu ya uongozi wa kanisa. Maono yanapaswa kuwa na mvuto wa kutosha kwa watu kutaka kuyafuata. Maono ya Yesu yalikuwa yenye mvuto sana kiasi cha kuwasukuma Petro, Andrea, Yakobo, na Yohana kuacha kila kitu ili kumfuata (Mt. 4:18-22).

Vivyo hivyo, lazima uweze kuwasilisha maono kwa uwazi na kwa ushawishi. Ukimrudia nabii wa kale, lazima uweze kusema, "Hii ndiyo njia; tuenende ndani

yake" (ling. Isa. 30:21). Kama mkondo wa mto mkubwa, maono haya ya kawaida yatamsukuma kila mtu katika mwelekeo sawa.[1]

**Unda Hali ya Urafiki**

Mbali na kukuza maono ya kawaida miongoni mwa viongozi walei, lazima utafute kujenga hali ya urafiki miongoni mwao. Ili watu wafanye kazi vizuri pamoja ni lazima wapendane kwa dhati na kufurahia kuwa pamoja. Biblia inatuambia kwamba sababu moja ya Yesu kuchagua mitume kumi na wawili ilikuwa "ili wawe pamoja naye" (Mk. 3:14). Na inawezekana kuongezea haya yafuatayo: Aliwachagua ili wawe pamoja. Wale Kumi na Wawili walipotumia muda pamoja na Yesu, na wao kwa wao, walizidi kupendana. Pamoja, wakawa jeshi lenye nguvu duniani.

Vivyo hivyo, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitahidi kusababisha hali za urafiki kati yako, wafanyakazi wako, na viongozi wako walei. Hii inaweza kufanyika tu kwa kutumia muda bora pamoja. Muda unaweza kutumika pamoja kwa njia tatu muhimu:

*1. Muda wa pamoja katika maombi.* Kwanza, wewe na timu yako ya uongozi wa walei mnapaswa kutumia muda pamoja katika maombi. Weka wakati unaofaa kila wiki wakati wewe na viongozi wako walei mnapoweza kukusanyika pamoja kwa maombi. Nyakati hizi za maombi lazima ziwe na lengo moja. Ingawa muda unaweza kutumika kuombea mahitaji binafsi, muda mwingi utumike kuombea maono na huduma za kanisa.

*2. Wakati wa pamoja katika huduma*. Kisha, wewe na viongozi wako walei lazima mwe na muda kuwa pamoja katika huduma. Kila Jumapili asubuhi kabla ya ibada kuanza, ikusanye pamoja timu ya uongozi kwa ajili ya maombi na wakumbushe kwamba mnafanya kazi pamoja kama timu. Njia nyingine ambayo timu ya uongozi wa walei inaweza kuhudumu pamoja ni kwa kuunda kikundi cha upandaji kanisa jipya mahali. Kila mwaka, waende pamoja ili kupanda kanisa jipya mahali penye uhitaji.

*3. Muda wa kushirikiana.* Tatu, wewe na viongozi wako walei ni vizuri muwe na muda wa ushirika pamoja. Viongozi wenu walei wanapaswa kuhimizwa

[1] Kwa maelezo zaidi juu ya ugawaji maono, tazama Sura ya 30: "Uongozi Wenye Maono."

kutembeleana nyumbani. Chakula cha pamoja kila mwezi kinaweza kusaidia sana katika kuimarisha ushirika katika familia za viongozi wako. Baada ya Yesu kukaa muda mwingi na wanafunzi Wake, aliwaambia, "Siwaiti tena watumwa… Badala yake, nimewaita rafiki" (Yoh. 15:15). Vivyo hivyo, wewe na viongozi wako walei mnafaa kuwa marafiki.

---

Ili kanisa listawi, ni lazima liwe na msingi imara wa viongozi walei waliojitoa kuendeleza utume na maono ya kanisa. Basi mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima, ataweka kujenga timu imara ya walei viongozi kama mojawapo ya malengo yake makuu katika huduma. Yeye atawekeza kimakusudi muda na nguvu katika kutambua, kuingiza kazini, na kuendeleza viongozi walei ili kuhudumu pamoja nao katika kuuendeleza ufalme wa Mungu.

~ Sura ya 34 ~

# Kuongoza Kanisa Katika Idara

Mtoto hukua tumboni mwa mama yake. Kila siku mwili wake unakuwa imara zaidi na zaidi. Wakati wa kutungwa mimba, mwanadamu mpya ametengenezwa na seli moja tu iliyorutubishwa. Na kwa kushangaza, muundo wake wa maumbile tayari unakuwa umekamilika. Ndani ya masaa 24, yai huanza kugawanyika haraka katika seli nyingi. Katika wiki tatu, seli za kwanza za mwili zinakuwa zimeundwa. Mwishoni mwa miezi mitatu ya kwanza, ingawa mtoto ana urefu wa sentimeta 10 tu (inchi nne), viunganisho na viungo vyake vyote vipo. Lakini, ili mtoto awe mtu anayefanya kazi kikamilifu, na aweze kuishi nje ya tumbo la uzazi la mama yake, viungo vyake vitahitaji kukua. Baada ya miezi sita zaidi, mtoto yuko tayari kuzaliwa. Huyu ndiye mtoto wa thamani ambaye mama na baba watamshika mikononi mwao hivi karibuni. Haishangazi kwamba Daudi alishangilia na kusema, ″Nimeumbwa kwa jinsi ya kutisha na ya ajabu!″ (Zab. 139:14).

Kanisa jipya linaweza kulinganishwa na yai jipya lililorutubishwa. Tayari ni kanisa kamilifu; lakini, mifumo fulani itahitajika kabla ya kuwa kikundi cha waamini kinachofaa, kinachofanya kazi kwa ukamilifu. Baadhi ya mifumo hii inajulikana kama idara za kanisa. Sura hii itajadili nafasi ya mchungaji wa Kipentekoste katika kutekeleza, kuendeleza, na kusimamia idara hizi.

KUSUDI NA KAZI ZA IDARA ZA KANISA

Idara za kanisa ni huduma za kusanyiko la mahali pamoja zilizoundwa kushughulikia mahitaji maalum katika mwili. Kusudi lake ni kuwezesha kanisa kutekeleza kwa ufanisi zaidi utume wake wa kuwafikia waliopotea na kuwakuza wanafunzi katika sura ya Kristo. Idara za kanisa zinaweza kutazamwa zaidi kama nguzo zinazounga mkono muundo wa huduma za kanisa, zinaozidi kupanuka. Idara mpya zinapoongezwa, uwezo wa kanisa kuhudumu unapanuliwa.

**Madhumuni ya Idara**

Ili kuelewa vizuri madhumuni na kazi ya idara za kanisa, mchungaji wa Kipentekoste lazima kwanza aelewe utume wa Kanisa. Kanisa lipo ili kutekeleza Agizo Kuu na kutimiza Amri Kuu ya Kristo. Agizo Kuu ni agizo la Kristo kwamba "nendeni mkafanye wanafunzi katika mataifa yote" (Mt. 28:19). Amri Kuu ni agizo la Bwana la "kumpenda Bwana Mungu ... kwa moyo ... wote na kwa roho ... yote na kwa akili ... zote" na "kumpenda jirani ... kama nafsi yako" (Mt. 22:37-39).

Majukumu haya makubwa hayawezi kutekelezwa na mchungaji peke yake, au hata watumishi wa kanisa walioajiriwa. Kazi inahitaji mikono mingi ili ifanyike. Idara za kanisa zipo ili kuwezesha kanisa kutimiza kwa ufanisi zaidi agizo lake la kujenga ufalme wa Mungu duniani.

**Kazi Saba za Idara**

Idara za kanisa huliwezesha kutekeleza vyema kazi kuu saba za huduma:

*1. Kuwafikia waliopotea*. Kwanza, idara zipo ili kusaidia kanisa kutimiza amri ya Kristo ya kwenda "ulimwenguni mwote kuhubiri Injili kwa viumbe vyote" (Mk. 16:15). Kila idara katika kanisa lazima ifanye sehemu yake kuliwezesha kanisa kuifanya kazi hiyo muhimu. Idara zinapaswa kuwahimiza washirika wao kuwashirikisha wengine habari njema na kuwatia moyo kushiriki katika uinjilisti na mipango ya umisheni ya kanisa.

*2. Kufanya watu kuwa wanafunzi.* Zaidi ya hayo, Yesu aliagiza Kanisa lifanye watu kuwa "wanafunzi kutoka kwa mataifa yote… na kuwafundisha kuyashika yote niliyoamuru" (Mt. 28:19-20). Kufundisha ndicho chombo kikuu cha kufanya watu kuwa wanafunzi. Maelekezo ya hatua kwa hatua ni muhimu kwa ukuaji wa kiroho wa watu wa Mungu na maendeleo ya kanisa. Idara husaidia kutimiza kusudi hili.

*3. Kuhimiza ibada.* Kanisa pia lipo ili kuwa mahali ambapo watu wa Mungu wanaweza kukusanyika na kumwabudu Mungu “katika Roho na kweli” (Yoh. 4:23). Idara ya sifa na muziki iliyopangwa vizuri inaweza kusaidia kuhakikisha kwamba ibada hiyo inafanyika kwa ufanisi.

*4. Kukuza maombi.* Zaidi ya hayo, Kanisa lipo ili kutia moyo na kuwafundisha watu wa Mungu kuomba (Mdo. 2:42). Yesu alisema, “Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote” (Mk. 11:17). Kanisa la mahali pamoja linapaswa kuwa mahali ambapo Wakristo wanapaza sauti zao kwa pamoja na kumwita Mungu, wakimtarajia kujibu maombi yao (Mt. 18:19-20; Mdo. 4:24). Idara husaidia kanisa kutimiza wajibu huo. Kila wakati idara ya kanisa inapokutana, inapaswa kusisitiza maombi sana na kuonyesha umuhimu wake.

*5. Kutoa ushirika.* Zaidi ya hayo, Kanisa lipo ili kukuza ushirika miongoni mwa ndugu na dada katika Kristo. Idara husaidia kanisa kufikia lengo hili. Watu wa Mungu wanapokusanyika katika mikutano ya idara, wanakuwa na upendo kati yao. Kwa hiyo, kwa kawaida wanapaswa kusaidiana na kujaliana. Nguvu hii hutumika kuunganisha na kuimarisha mwili. Pia husaidia kuvutia watu wapya kuja kanisani.

*6. Kuhamasisha utume.* Tena, kanisa lipo ili kutimiza utume wa Mungu. Lipo ili kupeleka habari njema kuhusu Kristo kwa “kila kabila na lugha na jamaa na taifa” kabla hajarudi kutoka mbinguni (Mt. 24:14; Uf. 5:9). Idara husaidia kanisa kujikusanya kwa ajili ya uinjilisti, upandaji kanisa, na umisheni.

*7. Kuendeleza viongozi.* Hatimaye, Yesu aliagiza Kanisa kuwafundisha viongozi. Aliwaamuru wanafunzi wake kwenda kufanya wengine kuwa wanafunzi (Mt. 28:19). Alipopaa mbinguni, alitoa karama za huduma kwa Kanisa “ili kuwatayarisha watu wake kwa ajili ya kazi za huduma, ili mwili wa Kristo ujengwe” (Efe. 4:11). Paulo alimwagiza Timotheo hivi: “Mambo uliyonisikia nikisema mbele ya mashahidi wengi uwakabidhi watu wanaotegemewa ambao watastahili kuwafundisha wengine pia” (2 Tim. 2:2). Idara husaidia kanisa kutekeleza kazi hii kwa ufanisi zaidi.

## KUUNDA IDARA ZA KANISA

Kanisa linapoendelea na kukua, wewe na timu yako ya uongozi mtahitaji baada ya maombi mengi, kuweka muundo wake wa huduma. Wewe anza kwa kuanzisha idara moja au mbili. Kisha, kama Roho anavyokuongoza, anzisha idara na mipango mingine. Idara zinazowezekana ni pamoja na zifuatazo:

**Elimu ya Kikristo**

Idara ya Elimu ya Kikristo ni kitengo kikuu cha mafunzo cha kanisa. Idara hii ipo ili kuwafanya waamini kuwa wanafunzi kwa kuwafundisha Neno la Mungu na kwa kutumia kanuni zake katika maisha yao. Katika makanisa mengi ya Kipentekoste, Shule ya Jumapili [au Shule ya Uanafunzi na Maandiko] ndiyo kitovu cha Idara ya Elimu ya Kikristo na huduma ya msingi kanisani ya kufanya wanafunzi. Kwa kweli ndiyo idara pekee katika kanisa inayohudumia kila rika, kuanzia watoto wadogo hadi wazee.

Kwa hiyo mchungaji wa Kipentekoste lazima aweke kipaumbele katika kuendeleza idara hii. Ni lazima iwe mojawapo ya idara za kwanza ambazo huanzishwa na kanisa jipya. Kanisa linaweza pia kutaka kuanzisha vikundi [au seli au shemasi] vya nyumbani ambapo watu wanafundishwa Neno la Mungu. Zaidi ya hayo, kila idara lazima ihusike katika elimu ya Kikristo kwa kiwango fulani.[1]

**Idara ya Wanawake**

Idara ya Huduma kwa Wanawake mara nyingi ni moja ya idara zenye nguvu zaidi katika kanisa la Pentekoste. Kusudi lake ni kuwafikia wanawake kwa ajili ya Kristo na kuwapa fursa za ushirika na huduma. Kupitia huduma hii, wanawake wanahimizwa kuwafikia wanafamilia wao, marafiki, na majirani na kuwavuta wamjie Kristo. Wanawake pia wanahimizwa kujihusisha katika kufanya watu kuwa wanafunzi, upandaji kanisa, umisheni, na huduma zingine.

**Idara ya Wanaume**

Idara ya Huduma kwa Wanaume ipo ili kuwafikia wanaume kwa ajili ya Kristo, kuwapa ushirika wa Kikristo, na kutoa changamoto ya kuwa viongozi katika nyumba zao na jamii. Zaidi, ipo ili kuhamasisha wanaume kwa ajili ya huduma yenye kuwezeshwa na nguvu na Roho. Kupitia huduma hii, wanaume

---

[1] Africa's Hope (wenye kutoa kitabu hiki) wametengeneza nyenzo mbili zenye nguvu za ufuasi kwa makanisa ya Kipentekoste barani Afrika. Mfululizo wa kwanza ni wa *Living the Truth*, mtaala wa Shule ya Jumapili ambao huwapitisha wanafunzi katika Biblia nzima kwa muda wa miaka saba. Nyingine ni mfululizo unaoitwa *Roots of Faith*. Huu ni mtaala wa mada unaoshughulikia masuala muhimu yanayohusu maisha ya Kikristo, kama vile "Hatua za Kwanza: Maisha Yako Mapya Katika Kristo," "Mafundisho ya Biblia," "Maisha Katika Roho," na mengine. Mfululizo huu hutolewa katika lugha kadhaa za Kiafrika. Unaweza kujua zaidi kuhusu nyenzo hizi kwenye tovuti hii: https://africaatts.org/resources/.

wana changamoto ya kujihusisha katika uinjilisti, upandaji kanisa, na shughuli nyingine kubwa za utume wa kanisa.

**Idara ya Vijana**

Kusudi la Idara ya Huduma kwa Vijana ni kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo na kuwakuza kuwa Wakristo waliokomaa, waliojazwa na Roho. Ipo ili kuwafundisha kuishi maisha ya utauwa, kumheshimu Kristo, na kuwahamasisha kwa ajili ya huduma yenye maana kwa vijana wengine.

**Idara ya Watoto**

Idara ya Huduma kwa Watoto inalenga kuwafikia watoto kwa ajili ya Kristo, kuwaongoza katika maisha yaliyojazwa na Roho, na kuwakuza katika njia za Bwana. Haikusudiwi kuchukua nafasi ya juhudi za wazazi bali kuwa kama nyongeza (Mit. 22:6). Upeo wa huduma hii ni pamoja na Kanisa la Watoto na huduma zingine za kuwawezesha watoto kama vile vilabu vya wavulana na wasichana.

**Idara ya Kusifu, Kuabudu na Muziki**

Kusudi la Idara ya Kusifu, Kuabudu na Muziki ni kusajili na kuendeleza wanamuziki, viongozi wa kuabudu, na wanakwaya ambao wataongoza kusanyiko katika ibada iliyovuviwa na Roho (Yoh. 4:23). Idara hii pia inafanya kazi na Kamati ya Umisheni katika kufanya uinjilisti na kufikia watu, na upandaji kanisa. Wahusika katika timu ya sifa na kuabudu lazima waombe pamoja mara kwa mara, na lazima wafundishwe jinsi ya kuitikia mtembeo na uwepo wa Roho na kuhudumu katika uwezo Wake.[2]

**Idara ya Maombi**

Idara ya Huduma ya Maombi iliyopangwa vizuri ni sehemu muhimu ya kila kanisa la Kipentekoste. Huduma hii inatoa msaada wa kiroho kwa kanisa kwa kuwaombea wachungaji na washirika wake. Pia huwaombea watu ambao hawajaokoka kote barani Afrika, na duniani kote. Huduma hii inaweza kufuata mbinu kadhaa, kama vile mikutano ya maombi ya kawaida, mikutano ya maombi

[2] Huduma ya kuabudu ya kanisa imejadiliwa kwa undani zaidi katika Sura ya 18: "Kuongoza Kanisa Katika Ibada."

ya kufunga, maombi ya kutembea, timu za maombi, na huduma ya waombaji binafsi wenye kufanya maombi ya vita.[3]

### Idara ya Umisheni

Idara ya Umisheni imepewa jukumu la kuliweka kanisa kwenye kueneza injili kwa watu wote kila mahali. Majukumu yake ni pamoja na kupanga na kutekeleza matukio ya kiinjilisti na umisheni, na shughuli ya upandaji kanisa. Matukio ya uinjilisti yanaweza kujumuisha mikutano ya uamsho, mikutano ya nje viwanjani, kampeni za kushuhudia nyumba kwa nyumba, ugawaji vipeperushi, na mbinu zingine za kibunifu za uinjilisti.[4]

Zaidi ya hayo, idara ina jukumu la kuendeleza na kukuza mpango wa umisheni wa kanisa. Kupitia mpango huu muhimu, kanisa linahamasishwa kusaidia wamishenari kwa maombi na fedha zao. Huduma hufanya hivyo kwa kuwafundisha watu kuhusu utume wa Mungu na kuwaweka wamishenari wazi kwa watu. Baadhi ya makanisa yatataka kuwa na idara tofauti za uinjilisti, upandaji makanisa, na idara za umisheni.[5]

### Idara ya Kuonyesha Huruma Watu

Yesu alijali mahitaji ya kimwili ya watu. Kanisa la kweli la Kipentekoste litafanya vivyo hivyo. Yakobo aliandika, “Dini anayoikubali Mungu Baba yetu kuwa safi na isiyo na dosari ni hii, kuwatunza yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na kuchafuliwa na dunia” (Yak. 1:27). Kupitia Huduma yake ya Huruma, kanisa la Kipentekoste hunyoosha mkono wa Kristo kwa watu wenye uhitaji na wanaoumia.[6]

### Idara ya Wanaume Ambao Hawajaoa

Kupitia Huduma ya Watu Wazima Wasio na Wake, wanaume wa Kikristo wanawezeshwa kukua na kuimarika katika imani yao na kukumbatia jukumu katika uhai wa kanisa. Huduma hii husaidia kanisa kutambua thamani ya kuwa na

---

[3] Kwa habari zaidi kuhusu huduma ya maombi ya kanisa, tazama Sura ya 8: “Kipaumbele cha Maombi.”

[4] Kwa habari zaidi juu ya kuhamasisha kanisa kwa ajili ya uinjilisti, tazama Sura ya 37: “Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti.”

[5] Kwa maelezo zaidi juu ya kuendeleza mpango wa umisheni wa kanisa, tazama Sura ya 40: “Kutengeneza Mpango wa Utume wa Kanisa la Mahali Pamoja.”

[6] Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma ya kuonyesha huruma kwa wahitaji, tazama Sura ya 38: “Kutumikia Jumuiya.”

watu wazima wasio na wenzi kushiriki katika shughuli za kanisa. Inatafuta kugusa rasilimali nyingi za kikundi hiki ambacho mara nyingi hupuuzwa.

### Idara ya Wanafunzi Wanaosoma Vyuo Vikuu

Ikiwa kanisa lako liko karibu na chuo kikuu au chuo cha aina yoyote, ni vizuri, katika hali ya maombi, kuzindua Huduma ya Wanafunzi wa Vyuo. Kusudi la huduma hii ni kufikia chuo cha aina yoyote au chuo kikuu, kutafuta kuwaleta wanafunzi kwa Kristo. Basi, huduma hii itawafundisha na kuhamasisha wanafunzi hawa kuwafikia wanafunzi wenzao zaidi na injili. Ikiwa kanisa lako la kitaifa lina idara ya huduma ya chuo kikuu, ni vizuri kufanya kazi na idara hiyo kwa karibu.[7]

### Vyombo vya Habari na Teknolojia

Idara ya Vyombo vya Habari na Teknolojia inashughulikia masuala yote ya teknolojia kwa kanisa. Inatunza, kuendesha, na kuangalia vyombo vya kanisa vya kupaza sauti, na video. Zaidi, hutengeneza na kuendeleza tovuti ya kanisa na uwepo wa mitandao ya kijamii. Idara hii pia ina jukumu la kuandaa huduma na matukio ya kanisa kupitia vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na mtandao.

### Ukarimu

Madhumuni ya Idara ya Ukarimu ni kuwakaribisha na kuwasaidia wale wanaohudhuria shughuli za kanisa. Hii idara inajitahidi kujenga mazingira ya uchangamfu na kukubalika kwa wote. Inawakaribisha wanaohudhuria ibada, inaelekeza wageni mahali pa kuketi, inasambaza nyenzo, na kukusanya matoleo. Pia inatazama hali ya usalama, inashughulikia vielelezo, na kuweka utaratibu katika kanisa.

### Jengo na Viwanja

Idara ya Ujenzi na Viwanja inawajibika na matengenezo ya mali za kanisa. Inahakikisha kwamba majengo yanatunzwa na kuwekwa katika hali ya usafi, viwanja vinatunzwa vizuri, kila kitu kinaangaliwa vizuri na kuwekwa katika hali nzuri kwa kukarabatiwa ipasavyo.

---

[7] Nyenzo za kuendeleza huduma kwa wanafunzi wa chuo zinaweza kupatikana kwenye Mtandao katika https://chialpha.com/resources/.

KUENDELEZA IDARA

Swali linazuka, ″Mchungaji wa Kipentekoste anawezaje kuendeleza idara na huduma mpya katika kanisa?″ Bila shaka, haiwezekani kuanza idara zote zilizotajwa hapo juu kwa mara moja. Badala yake, idara mpya zinapaswa kuanzishwa kwa maombi na mkakati mkubwa. Kuanzisha idara mpya lazima kutazamwe kama mchakato unaoendelea hatua kwa hatua, zinazochukua miaka mingi.

Mara nyingi, kuanzisha idara au huduma mpya huhusisha hatua ya ujasiri ya imani kwa upande wa mchungaji na halmashauri ya kanisa. Lazima waone hitaji, wajisikie kuongozwa na Roho, kisha wachukue hatua kwa imani ili kuzindua huduma mpya.

**Kuanzisha Mchakato**

Wewe na halmashauri yako ya kanisa mnapaswa kuanza mchakato kwa kumtafuta Mungu. Unapaswa kuomba hivi: "Bwana, ni huduma gani mpya zinazohitajika sana kanisani wakati huu?" Kisha unaweza kutayarisha orodha fupi ya idara na huduma hizo unazo-ona Roho anakuongoza zianze. Baada ya kutayarisha orodha hiyo, ipe kipaumbele, ukiamua ni idara gani itaanzishwa kwanza, ifuate ipi, na kadhalika.

Kisha, elekeza uwezo wako na fikra zako kwa kutazama idara iliyoko mwanzo kwenye orodha yako ya kipaumbele. Unapaswa kukutana na timu yako ya uongozi na kujadili yafuatayo:

- Je, tuchukue hatua gani ili kuanzisha idara hii mpya?
- Ni rasilimali gani zitahitajika?
- Nani ataongoza na kuhudumia mpango huo?
- Ianze lini?

Andika maamuzi yako na kuendelea kuyaombea. Kisha, kwa wakati unaofaa, unaweza kuanza kutekeleza mkakati wako. Anza polepole, kwa kutumia rasilimali zilizopo. Kwa mfano, kama unataka kuanzisha idara mpya ya Shule ya Jumapili, anza na madarasa matatu tu: watu wazima, vijana, na watoto. Itakuwa vizuri kumteua mtu wa kuhudumu kama msimamizi wa Shule ya Jumapili, au unaweza kutaka kuhudumu katika nafasi hiyo wewe mwenyewe, angalau kwa kuanza. Huduma inapokua, anzisha madarasa mengine mapya na kuteua viongozi wapya.

**Kuchagua Viongozi**

Siri ya mafanikio ya idara yoyote mpya ni viongozi waliochaguliwa vizuri na kufundishwa ipasavyo. Wakati wa kuchagua viongozi, tafuta watu wenye uwezo wa kuongoza, wale unaoweza kuwaendeleza mpaka kufikia kuwa viongozi. Watu hawa wanapaswa kuwa "wamejaa Roho na hekima" (Mdo. 6:3). Zaidi ya hayo, lazima wawe wamejaa imani, na lazima wayashike kikamilifu na kuyaunga mkono maono ya kanisa.

**Kuwafundisha Watendaji**

Mara nyingi, viongozi wenye ujuzi hawapatikani. Kwa hiyo, mchungaji mwenye ufanisi atakuwa akiendeleza viongozi wapya wakati wote. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya. Alichagua watu kumi na wawili ambao angewakuza kuwa mitume, baada ya maombi (Lk. 6:12-13). Ingawa walikuwa watu wa kawaida, Yesu aliona uwezo wa uongozi ndani yao. Aliwaambia, "Njooni, mnifuate… nami nitawatuma kuwa wavuvi wa watu" (Mt. 4:19). Walipomfuata, aliwakuza na kuwaendeleza kuwa viongozi wakuu.

Wakati wa kuingiza viongozi wapya wa idara kazini, ni muhimu kwamba utoe ahadi ya mafunzo. Waambie watu, "Tutatembea pembeni yako na kukufundisha jinsi ya kutimiza huduma yako." Hayo mafunzo ya huduma yanaweza kufanywa kwa njia kadhaa: kupitia semina, ushauri wa mtu kwa mtu, na njia zingine za ubunifu. Ikiwa kanisa litawagawa viongozi vizuri, ni vizuri mchungaji awe na kusudi la kuwafundisha uongozi.[8]

**Kuunda Roho ya Kufanya Kazi Kama Timu**

Ili huduma za idara katika kanisa zistawi, lazima ujenge hali ya uaminifu na kukusudia kushirikiana miongoni mwa viongozi na wafanyakazi. Moyo huu wa timu utawawezesha kufanya kazi pamoja na kujitoa kwa uwezo wao wote kufanya kazi zao vizuri. Unaweza kukuza moyo huu wa timu kwa kuwakumbusha mara kwa mara maono ya kanisa, na kwa kuwaonyesha jukumu muhimu wanalotekeleza katika kutimiza maono.

---

[8] Kwa maelezo zaidi kuhusu kuwafundisha watumishi kwa ajili ya huduma katika kanisa la mahali, tazama Sura ya 33: "Kuhamasisha Viongozi Walei."

Unapaswa kukutana mara kwa mara na viongozi wa idara na watumishi ili kuwatia moyo na kuwashirikisha ushindi na malengo. Unapaswa pia kuwatambua hadharani watumishi waaminifu na wenye bidii kwa mafanikio yao (Rum. 13:7).

---

Idara za kanisa zina jukumu muhimu katika kuliwezesha kanisa la Kipentekoste kutimiza Agizo Kuu la Kristo. Basi mchungaji wa Kipentekoste anayefaa atafanya kazi ya kuendeleza idara za huduma zenye nguvu katika kanisa lake.

~ Sura ya 35 ~

# Usimamizi wa Washirika wa Kanisa

Hebu fikiria shule ya umma isiyojua vizuri nani ni mwanafunzi na nani si mwanafunzi shuleni. Shule haitunzi orodha ya wahudhuriaji, na haina kumbukumbu za ufaulu wa wanafunzi. Ukweli ni kwamba shule kama hiyo isingekuwa na nafasi ya kufanikiwa. Yanaweza kusemwa mengi kama hayo kuhusu kanisa. Kanisa lisilojua vizuri nani ni mshirika na nani si mshirika, na lenye kushindwa kuzingatia maendeleo yao ya kiroho, lina nafasi ndogo ya kuwa kanisa imara.

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uhakikishe kwamba kanisa unaloongoza linasimamiwa vyema. Sehemu moja muhimu katika usimamizi ni orodha ya washirika wa kanisa. Daftari la washirika linalosimamiwa vizuri litasaidia kanisa kutimiza vema wajibu wake lililopewa na Mungu wa kutunza kondoo na kuwafikia waliopotea kwa namna ya uinjilisti. Sura hii itashughulikia wajibu wako wa kusimamia orodha ya washirika wa kanisa.

## MAADILI YA KIBIBLIA KUHUSU UANACHAMA

Ingawa Biblia haisemi moja kwa moja kuhusu ushirika rasmi wa kanisa kama inavyojulikana katika kanisa leo, inaunga mkono wazo hilo.

**Msingi wa Kibiblia wa Uanachama**

Dhana ya uanachama wa kanisa asili yake ni katika Agano la Kale. Hapo, Mungu alikuwa na uhusiano wa pekee na taifa la Israeli. Walikuwa watu Wake, naye alikuwa Mungu wao. Huko nyikani, Mungu alianzisha utaratibu wa kuwapanga watu wake. Alimwamuru Musa, "Hesabu jumuiya yote ya wana wa Israeli kwa koo zao na jamaa zao, ukimworodhesha kila mtu kwa jina, mmoja mmoja" (Hes. 1:2). Kisha Musa na Haruni walitumia sensa hiyo ili kuchagua watakaokuwa viongozi, watakaowahudumia, na kuwatetea watu wa Mungu.

Katika Agano Jipya, Stefano alizungumza juu ya Israeli kama "kusanyiko [Kiyunani: ekklesia ] jangwani." Katika Agano Jipya lote neno *ekklesia* limetafsiriwa "kanisa." Husema kuhusu kusanyiko la watu walioitwa kutoka duniani ili kumfuata Kristo na kuendeleza utume Wake duniani.

Yesu alisema, "Nitalijenga kanisa langu" (Mt. 16:18). Alianza mchakato huo kwa kuita watu wamfuate (Mt. 4:19). Kutoka katika hao wafuasi, Yesu aliteua wengine kuwa mitume (Mk 3:13-14). Mitume nao waliweka mashemasi kutumika chini yao. Walikuwa wakiandaa kanisa kwa ajili ya mafanikio. Kwa hiyo, "idadi ya wanafunzi katika Yerusalemu ikaongezeka upesi" (Mdo. 6:1-7).

Ili kanisa la mahali pamoja lifanye kazi inavyopaswa, ni muhimu kwamba kila mtu ajue mshirika ni nani, na asiyekuwa mshirika ni nani. Kanisa la kwanza lilielewa hili. Kwao kulikuwa na ufafanuzi mzuri kuhusu "walioko ndani" na "walioko nje". Kwa mfano, wakati mmoja Paulo aliagiza kanisa la Korintho kumfukuza mshirika mwenye dhambi, kumwondoa kwenye orodha ya kanisa (1 Kor. 5:5, 13). Orodha ya washirika inayosimamiwa vyema itamsaidia mchungaji wa Kipentekoste kuwaimarisha waamini na kuendeleza utume wa kanisa.

**Dhana ya Kibiblia ya Uanachama**

Lakini, mtu hapaswi kufikiria ushiriki wa kanisa kama suala la klabu ya kilimwengu au kijamii. Ni kitu zaidi ya hicho. Paulo analinganisha Kanisa na mwili wa mwanadamu, akiliita "mwili wa Kristo" (1 Kor. 12:27). Basi, kila mshirika wa Kanisa ni sehemu ya mwili wa Kristo, na "kila kiungo kwa wengine

wote" (Rum. 12:5). Kama vile mwili wa mwanadamu unavyopangwa, na kila kiungo cha mwili kina kazi maalum, ndivyo ilivyo kwa Kanisa la Kristo.

## SIFA ZA UANACHAMA

Katika Agano la Kale, Mungu aliweka viwango kwa ajili ya watu wake kuishi navyo. Viwango hivi vimejumlishwa katika Amri Kumi (Kut. 20:1-17). Vivyo hivyo, kanisa la kwanza lilipokua na kutawanyika nje ya Yerusalemu, mitume waliongozwa na Roho Mtakatifu kuweka sifa za kujumuishwa kwa Wasio Wayahudi katika kanisa (Mdo. 15:19-20, 28-29). Kama mchungaji wa kanisa la Kipentekoste, lazima wewe pia uhakikishe kwamba yeyote anayepokelewa katika kanisa kama mshirika anatimiza sifa fulani, ikiwa ni pamoja na zifuatazo:

### Kuzaliwa Mara ya Pili

Kanisa la mahali pamoja linapaswa kuwa kielelezo cha Kanisa la dunia nzima. Kanisa la duniani kote linajumuisha watu wote wa mataifa yote ambao wameweka tumaini lao kwa Yesu Kristo na kuokolewa. Ni wale tu ambao wamezaliwa kweli na Roho Mtakatifu (1 Kor. 12:13). Kwa hiyo, kabla mtu hajawa mshirika wa kanisa la mahali pamoja, lazima kwanza awe mshirika wa Kanisa la dunia nzima. Bwana mwenyewe lazima awe amewaongeza kwenye Kanisa lake (Mdo. 2:47). Basi, ili kuwa mshiriki wa kanisa la mahali pamoja, mtu lazima azaliwe mara ya pili (Yoh. 3:3-7).

### Ubatizo wa Maji

Sharti la pili la ushirika wa kanisa ni ubatizo wa maji mengi. Yesu analiamuru Kanisa lake kama ifuatavyo: "Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu" (Mt. 28:19; taz. Mdo. 2:38). Ubatizo wa maji ni ushuhuda hadharani kwamba mtu amepita kutoka mautini kuingia uzimani (Rum. 6:4).[1]

### Imani Moja

Sifa ya mwisho ya mshiriki wa kanisa ni makubaliano kamili na mafundisho na sera za kanisa (rej. 1 Kor. 1:10). Sharti hili litahakikisha kwamba kanisa

[1] Kwa mengi zaidi kuhusu ubatizo wa maji, tazama Sura ya 42: "Kuendesha Meza ya Bwana, Kuweka Wakfu, na Kuingiza Kazini."

linabaki kuwa na umoja na kuzingatia utume wake lililopewa na Mungu. Masuala haya yanapaswa kushughulikiwa katika darasa la washirika wapya.

## KUPOKEA WANACHAMA WAPYA

Kama mchungaji, lazima uhakikishe kwamba kanisa lina utaratibu uliowekwa vema wa kupokea washirika. Utaratibu huu unapaswa kuwa na vipengele vitatu:

### Kuhimiza Uanachama

Unapaswa kuwahimiza waamini wapya mara kwa mara kujiunga na kanisa. Ili kufanya hivyo, unapaswa kuchukua muda katika ibada za kanisa kueleza manufaa ya ushiriki wa kanisa na kuwaalika Wakristo wapya kujiunga. Unaweza pia kutaka kuzungumza binafsi na washirika tarajiwa. Matendo hayo yatahakikisha kwamba washirika wanaongezeka kila mara katika kanisa. (Hii inamaanisha kwamba watu wapya wanamjia Kristo kama matokeo ya uenezaji wa injili wa kanisa.[2]) Zaidi ya hayo, unapaswa kuhakikisha kwamba fomu za maombi ya uanachama zinapatikana kwa urahisi.

### Kujitayarisha kwa Uanachama

Ni muhimu kwamba kanisa lako liwe na njia za kuwatayarisha watu kwa ajili ya kuwa washirika wa kanisa. Njia moja ya kufanya hivyo ni kupitia darasa la washirika wapya. Hili linapaswa kuwa darasa linaloendelea. Linaweza kutolewa Jumapili asubuhi wakati wa saa ya shule ya Jumapili au wakati mwingine wowote unaofaa. Katika darasa hili, washirika tarajiwa watajifunza kuhusu manufaa na wajibu wa ushirika wa kanisa. Mengi ya yale yanayojadiliwa katika sura hii yanaweza kufundishwa darasani.

### Kupokea Wanachama

Baada ya kuidhinishwa na halmashauri ya kanisa, washirika wapya wanapaswa kupokelewa kanisani kwa furaha katika sherehe ya hadhara Jumapili asubuhi iliyopangwa. Wahusika wasimamishwe mbele ya kanisa. Kisha wakaribishwe hadharani kama washirika, na kuombewa. Kisha kanisa litawapa “mkono wa ushirika” (Gal. 2:9). Kwa wakati huu unapaswa kukabidhi cheti cha

---

[2] Kwa habari zaidi kuhusu kuwafikia waliopotea, tazama Sura ya 37: “Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti.”

uanachama kwa kila mshirika mpya. Kisha utaongeza majina yao kwenye orodha ya washirika wa kanisa.

Zaidi ya hayo, itakuwa vema kwa mtu fulani katika kundi la wachungaji kuwatembelea hao washirika wapya majumbani mwao. Hii itawasaidia wajue kanisa linathamini kwa kiasi gani uamuzi wao wa kujiunga. Hatimaye, unapaswa kuwaunganisha washirika wapya na huduma za kanisa, kama vile vikundi vidogo vidogo, huduma kwa wanawake, huduma kwa wanaume, kikundi cha vijana, na nyinginezo.

## WAJIBU ZA UANACHAMA

Kama mchungaji wa kanisa, lazima uhakikishe kwamba washirika wapya wanafahamishwa kuhusu wajibu na fursa za ushirika.

### Wajibu za Washirika kwa Kanisa

Uanachama huleta kuwajibika. Majukumu hayo ni pamoja na yafuatayo:

*1. Kuhudhuria ibada kanisani wakati wote.* Mwandishi wa Waebrania aliwaonya Wakristo kwamba wasipuuze kukusanyika pamoja. Bali wakusanyike mara kwa mara ili kutiana moyo. Hii ilikuwa muhimu hasa katika mtazamo wa Yesu kuja upesi (Ebr. 10:25). Vivyo hivyo, washirika wa kanisa leo wanatarajiwa kuwa waaminifu katika mahudhurio yao kanisani. Huko, watatiwa moyo, watamwabudu Mungu, wataabudu pamoja, watapata mafundisho, watatoa kwa ajili ya kazi ya Mungu, na kusitawisha uhusiano wa kudumu na Wakristo wengine waliojitoa.

*2. Kuenenda katika Roho.* Kila mshirika wa kanisa la Kipentekoste anapaswa kujitoa kwa kuenenda akiwa amejazwa na Roho (Gal. 5:25). Ikiwa bado hawajabatizwa katika Roho Mtakatifu, wanapaswa kutafuta kwa bidii ujuzi huo (Mdo. 1:4-5; Efe. 5:18). Ikiwa wamejazwa na Roho, ni lazima wajitoe kuendelea kutembea katika ujazo wa Roho (Gal. 5:16, 25).[3]

*3. Ushuhudiaji wa dhati.* Kila mshirika wa kanisa anatarajiwa kuwa shahidi wa Kristo (Mdo. 1:8). Ni lazima Kristo ashirikishwe kwa watu wa familia zao, marafiki, majirani, na wafanyakazi wenzao. Yesu anatuamuru, “Nuru yenu na

[3] Kwa zaidi kuhusu kuwaongoza waamini katika matembezi yaliyojazwa na Roho, ona Sura ya 11: “Hukuza Utendaji na Uzoefu wa Kipentekoste” na Sura ya 20: “Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho.”

iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mt. 5:16).

*4. Maisha matakatifu.* Njia moja ambayo Wakristo wa Kipentekoste humshuhudia Kristo ni kwa kuishi maisha matakatifu (1 Pet. 1:15; 2:9). Kwa kufanya hivyo, wanaonyesha upendo wao kwa Mungu. Wakati huo huo, maisha yao yanaishuhudia dunia iliyopotea maana ya kuwa mfuasi wa Kristo (Flp. 2:15).

*5. Kutoa kwa uaminifu*. Kila mshirika wa kanisa anatarajiwa kulitegemeza kanisa kwa uaminifu (1 Kor. 16:2). Kwa kutoa zaka na sadaka zao wanaimarisha mwili na kusaidia kuendeleza ufalme wa Mungu duniani. Zaidi ya hayo, kutoa kwa furaha humpendeza Mungu na kufungua mlango wa baraka zake maishani mwao (2 Kor. 9:7-8; Lk. 6:38).

*6. Huduma hai.* Zaidi ya hayo, kila mshirika anatarajiwa kupata nafasi yake ya huduma katika kanisa. Kila mshirika anapofanya sehemu yake, kanisa huwa na nguvu. Kama mchungaji, lazima ufanye bidii kuhakikisha kwamba washirika wanaelewa karama zao za kipekee na kwamba wanajitoa kutumia karama hizo kumtumikia Kristo na kanisa.

*7. Maombi ya dhati.* Alama moja ya kanisa la kweli la Kipentekoste ni maombi ya dhati. Kila mshirika anaweza kutarajiwa kuomba mara kwa mara kwa ajili ya mchungaji, kanisa, jumuiya, na washirika wengine wa kanisa. Utataka kuwahimiza wengine wajiunge na vikundi vya maombi ya maombezi vilivyoundwa kipekee.

*8. Mtazamo wa ushirika.* Hatimaye, wanachama wanatarajiwa kudumisha tabia ya ushirikiano. Mtazamo kama huo utachangia umoja wa kanisa (Efe. 4:3). Itahakikisha kwamba kanisa halibabaishwi na mabishano yasiyo na maana, bali linabaki kwenye lengo la kutimiza utume wake lililopewa na Mungu.

**Wajibu wa Kanisa kwa Washirika**

Si tu kwamba washirika wa kanisa hubeba majukumu fulani kanisani, na mchungaji na kanisa wana majukumu fulani kwa washirika. Miongoni mwa hayo majukumu ni:

*1. Kukaribishwa kwa furaha*. Kwanza, lazima uhakikishe kwamba washirika wapya wanakaribishwa kwa uchangamfu na kuingizwa kikamilifu katika uhai wa kanisa. Wengine watakuwa wamewaacha watu na mambo waliyoyazoea. Huenda wameingia katika dunia mpya wanayoijua kidogo sana. Unapaswa kuhakikisha

kwamba wanachama hawa wapya wanasaidiwa kuzoea mazingira yao mapya. Na lazima ufanye juhudi zote kuhakikisha kwamba wanajisikia wao ni washirika kweli katika familia ya Mungu.

*2. Huduma bora za kuabudu*. Pili, kama mchungaji, unawajibika kwa washirika wa kanisa, wazee na wa zamani kuwapa uzoefu unaowajenga wa ibada ya kweli. Kwa maneno mengine, ni lazima uhakikishe kwamba ibada za kanisa zimepangwa vyema na za ubora wa juu. Ili kufanikisha hilo, ni lazima ufanye kila juhudi kutayarisha na kuhubiri jumbe zinazofaa na zenye kutia moyo kibiblia. Lazima uhakikishe zaidi kwamba kila sehemu ya huduma inafanywa kwa njia ya heshima na ya kitaaluma. Hii ni pamoja na kuabudu, kutoa, matangazo, au sehemu nyingine yoyote ya huduma. Zaidi ya hayo, wewe na timu yako ya uongozi mnapaswa kuzamisha ibada za kanisa katika maombi ili kuhakikisha kwamba Roho Mtakatifu yuko kwa nguvu.[4]

*3. Uchungaji*. Zaidi ya hayo, kama mchungaji wa kundi, una wajibu wa kuona kwamba kila mshirika wa kanisa anathaminiwa na kutunzwa. Ni lazima umwige Yesu aliyejiita "mchungaji mwema… [ambaye] huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo" (Yoh. 10:11). Ni lazima uwe tayari kumtumikia hata mshirika wa hali ya chini kabisa kanisani (Lk. 15:1-7).[5]

*4. Maombi ya dhati*. Kisha kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwaombee washirika wa kanisa lako kwa uaminifu. Ingekuwa vyema kutengeneza orodha ya majina yao ili kutumika kama mwongozo wa maombi. Kisha, unaweza kutumia hiyo orodha kuomba kila siku kwa ajili ya kila mshirika. Zaidi ya hayo, wakati wao wa shida, wewe na timu yako ya uongozi mnapaswa kuwa tayari kwenda kwa wanachama wanaoumia ili kuwatia moyo na kuwaombea.[6]

*5. Mafundisho ya Biblia*. Zaidi ya hayo, kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uhakikishe kwamba washirika wa kanisa lako wanapokea mafundisho ya kweli ya Biblia. Mafundisho haya yanapaswa kuwa ya vitendo na muhimu kwa maisha yao. Yatawasaidia kukua na kukomaa. Unapaswa pia

---

[4] Kwa maelezo zaidi juu ya kupanga ibada, tazama Sura ya 18: "Kuliongoza Kanisa Katika Kuabudu."

[5] Tazama Sura ya 24: "Kuwatunza Kondoo."

[6] Kwa habari zaidi kuhusu mchungaji wa Kipentekoste na maombi, tazama Sura ya 8: "Kipaumbele cha Maombi."

kufuatilia ufundishaji katika madarasa ya shule ya Jumapili na vikundi vya mtaani ili kuhakikisha kwamba yako sawa kibiblia na yenye kujenga.[7]

*6. Ulinzi kutoka kwa manabii wa uongo.* Kama mchungaji, una wajibu zaidi wa kulichunga kundi la Mungu na kuwalinda dhidi ya manabii na walimu wa uongo (rej. Mdo. 20:28-29). Njia moja unayoweza kufanya hivyo ni kwa kuendelea kufundisha kweli za Neno la Mungu. Njia nyingine ni kuwaweka wazi manabii na waalimu wa uongo, tukionyesha makosa ya njia zao. Zaidi ya hayo, unaweza kuwalinda washirika wako dhidi ya manabii na walimu wa uongo kwa kutoruhusu hawa "mbwa-mwitu waliovaa mavazi ya kondoo" kupanda kwenye mimbari ya kanisa lako (Mt. 7:15).[8]

*7. Fursa za huduma*. Unapaswa pia kuwapa washirika wapya fursa za huduma katika kanisa. Unapaswa kuwaalika mara moja kusaidia kwa njia rahisi. Hii itasaidia kuwashikanisha na kuwaunganisha kwa kanisa. Pia itawasaidia kuelewa tangu mwanzo kwamba kumtumikia Mungu ni zaidi ya kuhudhuria matukio ya kanisa, kwamba ni pamoja na huduma kamilifu.

*8. Kufanya harusi na mazishi*. Mwisho: kama mchungaji wao, unatakiwa kutembea na washirika katika matukio makubwa katika mapito ya maisha. Unapaswa kuwapa ushauri wa ndoa na kuwafungia harusi. Unapaswa pia kuendesha mazishi na kutoa msaada na kutia moyo kwa wanafamilia wanao-omboleza.[9]

## MIKUTANO YA WANACHAMA

Mikutano ya washirika ni sehemu muhimu ya maisha ya kanisa la Kipentekoste. Katika mikutano hii, washirika hukusanyika ili kujadili shughuli za kanisa. Hapo, mchungaji na viongozi wengine hushiriki ripoti kuhusu maendeleo ya kanisa, changamoto, na mahitaji. Mikutano ya wanachama inapaswa kufanywa

---

[7] Kwa maelezo zaidi kuhusu mchungaji wa Kipentekoste kama mwalimu, tazama Sura ya 17: "Kufundisha kwa Ufanisi." Mtaala wa *Living the Truth* na *Roots of Faith* ni nyenzo bora za uanafunzi wa Kipentekoste. Zinapatikana kutoka Africa Theological Training Service (ATTS) katika https://africaatts.org/resources/.

[8] Kwa habari zaidi juu ya kulinda kanisa dhidi ya manabii wa uongo, tazama Sura ya 27: "Kulilinda Kundi."

[9] Kwa habari zaidi kuhusu kuendesha arusi na mazishi, tazama Sura ya 41: "Kufanya Harusi na Mazishi."

kila mwaka. Kwa kuongezea, mikutano maalum inaweza kupangwa kama hitaji litatokea.

Mikutano ya washirika ni wakati mzuri wa kujadili matukio yajayo na kushirikisha maono yako na kanisa. Mikutano hii pia huwapa washirika wa kanisa nafasi ya kujadili matumaini na ndoto zao kwa ajili ya kusanyiko. Utataka kufaidika zaidi na mikutano hii. Unaweza kufanya hivyo kwa kujitayarisha vyema. Unapaswa kuja kwenye mikutano hii kila wakati na ajenda iliyoandaliwa kwa uangalifu na taarifa sahihi.

Pamoja na mikutano ya washirika, utataka kukutana na timu yako ya uongozi (wazee, walei na mashemasi) angalau mara moja kwa mwezi ili kujadili masuala yanayohusiana na kanisa. Wakati wa mikutano hii, omba pamoja na timu yako ya uongozi. Kwa pamoja, mnaweza kufanya shughuli ya kanisa, kueleza maono, na kuendeleza mikakati ya ukuaji wa kanisa.

Pia utataka kukutana mara kwa mara na viongozi wa huduma ya kanisa, kama vile wale wanaoongoza idara ya shule ya Jumapili, vikundi vya nyumba kwa nyumba, huduma za wanaume na wanawake, huduma ya vijana, kamati ya umisheni, kamati ya upandaji kanisa, kamati ya uinjilisti, vikundi vya maombezi, na wengine.[10]

## KUWAADIBISHA WANACHAMA WAPOTEVU

Wakati unaweza kuja ambapo ni muhimu kumwadhibu mshirika aliyepotoka wa kanisa. Hiyo ni utekelezaji wa mamlaka ya kimaandiko ambayo kanisa linawajibika kuyatekeleza (Mt. 18:15-20; Lk. 17:3; Yoh. 20:23; 1 Kor. 5:1-5; Efe. 5:11; 1 Tim. 5:19-20). Kama mchungaji wa kanisa, hupaswi kukwepa jukumu hili. Tukio linapotokea, lazima utende kwa ujasiri na huruma, ukijua kwamba makusudi ya kuadhibu ni mawili: kutakasa kanisa (Mdo 5:9-11) na kumrejeza mkosaji (Gal. 6:1).

Wakati wewe na uongozi wa kanisa mnapoamua kwamba nidhamu ni muhimu, unapaswa kufuata utaratibu uliowekwa na Yesu katika Mathayo 18:15-20. Utaratibu huu una hatua tatu. Kwanza, mchungaji au kiongozi wa kanisa aliyeteuliwa huenda kwa mshirika aliyekosea ili kujadili mashtaka na kuwasihi watubu. Jaribio hili lisipotatua suala hilo, mshirika anaitwa kukutana na mchungaji

[10] Kwa kujua zaidi juu ya kufanya kazi na viongozi wa huduma, tazama Sura ya 33: "Kuhamasisha Viongozi Walei" na Sura ya 34: "Kuongoza Kanisa Katika Idara."

na halmashauri ya kanisa. Ikiwa mshirika mwenye dhambi bado anakataa kutubu, suala hilo hupelekwa mbele ya kusanyiko katika mkutano wa shughuli wa kanisa. Washirika hai wa kanisa tu ndio wanaoruhusiwa kuhudhuria mkutano huu. Uamuzi wa kanisa utakuwa wa mwisho. Akipatikana na hatia, mshirika aliyekosea atafukuzwa kutoka kanisani (Mt. 18:17). Walakini, katika hali zingine, hatua ndogo za kinidhamu zinaweza kufaa zaidi.

~ Sehemu ya 9 ~

# Mchungaji wa Kipentekoste Katika Umisheni

## ~ Sura ya 36 ~

# Kuelewa Mkakati wa Agano Jipya

Biblia inasimulia hadithi ya kusisimua ya utume wa Mungu unaoendelea wa kuwakomboa wanadamu waliopotea. Inaeleza zaidi jinsi anavyowaamuru wote wanaomfuata kuungana Naye katika utume Wake. Kwa hiyo, kila mchungaji wa Kipentekoste lazima ajitoe mwenyewe kufanya kazi hii muhimu sana. Ni lazima kila mmoja wetu ajiulize, “Nawezaje kuliongoza vyema kanisa langu kufanya sehemu yake katika kutimiza utume wa Mungu hapa kwetu, na kote Afrika, na duniani kote?” Jibu ni kwamba lazima tufuate mfano wa utume uliowekwa na Yesu na mitume.

Kupitia maisha na huduma Yake, Yesu alionyesha jinsi Kanisa linavyopaswa kutimiza utume wa Mungu. Mitume walielewa hilo, na kuiga kielelezo cha Yesu. Kama wachungaji wa Kipentekoste, na warithi wa utume wa Kristo, lazima tufanye vivyo hivyo. Kielelezo hiki nyakati fulani huitwa “Mkakati wa Roho wa Agano Jipya.” Sura hii itachunguza mkakati huu kwa makini. Pia itatoa mapendekezo kuhusu jinsi wewe, kama mchungaji wa Kipentekoste barani Afrika, unavyoweza kutekeleza mkakati huo katika maisha ya kanisa lako.

## KUSUDI LA UTUME LA MATENDO

Luka aliandika kitabu cha Matendo kwa madhumuni ya utume. Aliandika kuliita kanisa la wakati wake -- na hatimaye kanisa katika kila kizazi - kurudi kwenye mizizi yake ya Kipentekoste na kimishenari. Kwa kuwaambia wasomaji wake jinsi Kanisa lilivyoanza, na jinsi walivyoshinda kwa nguvu za Roho hata katikati ya mateso makali, Luka alitumaini kuwatia moyo kufanya vivyo hivyo. Hivyo Luka aliandika Matendo kuwasilisha mkakati wa kimishenari ambao utafanya kazi katika kila utamaduni na katika kila kizazi hadi Yesu atakaporudi.

Kusudi kuu la Luka katika kuandika limefunuliwa katika Matendo 1:8, ambapo Yesu anawaambia wanafunzi Wake, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi". Maneno haya ya Yesu ndiyo ufunguo wa kuelewa mfano wa umisheni kilichoonyeshwa katika Matendo. Wanatoa muundo unaorudiwa katika kitabu kizima:

*Kutiwa nguvu kwa Roho Mtakatifu*
*— daima husababisha —*
*shahidi aliyewezeshwa na Roho*.

Mtindo huu umeitwa "picha ya shahidi wa uwezeshaji" ya Luka. Picha ni muundo wa maneno, dhana, au matukio yanayorudiwa katika kitabu chote. Katika Matendo, mtindo huu unarudiwa tena na tena. Kila wakati Roho anapomiminwa, matokeo yake ni ushuhuda unaowezeshwa kwa nguvu za Roho. Hakuna ubaguzi.[1]

Ahadi ya Matendo 1:8 bado inafanya kazi kwetu hata leo. Kama wale wanafunzi wa kwanza, sisi pia tunaweza kupokea nguvu za Roho Mtakatifu anapokuja juu yetu. Na kama wao, tunaweza kuwa mashahidi wa Kristo waliotiwa nguvu na Roho nyumbani na hata miisho ya dunia.

## MKAKATI WA AGANO JIPYA

Hebu tuangalie jinsi Paulo alivyotekeleza mkakati huu wa Matendo 1:8 katika mji wa Kirumi wa Efeso (Mdo. 19:1-11). Kwa kufanya hivi, tutagundua kwamba

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu somo hili, tazama kitabu cha kiitwacho, *Acts: The Spirit of God In Missions,* cha Denzil R. Miller, kinachotolewa na Africa's Hope katika mfululizo wa Discovery Series.

mkakati wa Paulo ulikuwa ni nakala ya mkakati ambao Yesu aliutumia katika kuhamasisha Kanisa Lake. Ni mkakati ambao sisi kama wachungaji wa Kipentekoste lazima tuutumie leo katika kuhamasisha makanisa yetu kwa ajili ya uinjilisti, upandaji kanisa, na umisheni.

**Huduma Mfano Katika Efeso**

Kwa kusimulia kisa cha huduma ya Paulo huko Efeso, Luka anatoa mfano kamili wa mbinu ambayo Paulo alitumia katika kazi yake ya umishenari. Hiyo mbinu imekusudiwa kuwa mkakati wa kudumu wa upandaji kanisa na umisheni. Hebu tuangalie jinsi Paulo alivyotumia Mkakati huu wa Roho kupanda kanisa, si Efeso tu, bali katika Asia Ndogo yote.

**Umwagiko wa Roho Huko Efeso (Matendo 19:1-7)**

Paulo alifika Efeso akiwa na lengo lililokuwa wazi katika akili zake. Lengo lake lafunuliwa katika mstari wa 10, ambapo Luka anatuambia kwamba baada ya miaka miwili tu "Wayahudi wote na Wayunani waliokaa katika jimbo la Asia walisikia neno la Bwana." Lengo la Paulo lilikuwa kufikia Efeso na Asia Ndogo yote kwa ujumbe wa Kristo. Paulo pia alikuwa akifikiria mbinu iliyo wazi ya kutimiza lengo lake. Mbinu hii inakuwa wazi kupitia uchunguzi makini wa huduma yake huko Efeso katika Matendo 19:1-11. Kwa hali hiyo, hebu tuangalie kile alichofanya Paulo huko Efeso.

Paulo alipofika mjini hapo, aliwakuta wanafunzi kumi na wawili. Yawezekana hao walikuwa viongozi katika kanisa lililokuwa likianza huko Efeso (Mdo. 18:24-27). Mara Paulo akawauliza, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" (19:2). Mtume aliuliza swali hili ili kugundua kama hao wanaume walikuwa wamewezeshwa kiroho kushiriki katika utume wa kufikia kwa injili Efeso na Asia. Alikuwa akitumia mafundisho ya Yesu katika Matendo 1:4-8 (rej. Lk. 24:49).

Baada ya mazungumzo mafupi, Paulo aliweka mikono yake juu ya hao wanafunzi kumi na wawili, na "Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri" (Mdo. 19:6). Maneno, "Roho Mtakatifu akaja juu yao" hutukumbusha ahadi ya Yesu katika Matendo 1:8, ambapo alisema, "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; *nanyi mtakuwa mashahidi wangu*" (sisitizo limeongezwa). Utambuzi huu unatusaidia kuelewa kile kinachotokea katika kifungu hiki. Roho Mtakatifu 'aliwashukia' wanaume hao sawa tu na jinsi alivyokuja juu ya wanafunzi Siku ya Pentekoste, ili kuwatia nguvu

kwa ajili ya ushuhuda "katika Yerusalemu, na Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."

Mara tu Roho Mtakatifu alipowashukia na kuwajaza wale kumi na wawili wa Efeso, "walisema kwa lugha na kutabiri," kuonyesha kwamba Kristo alikuwa amewapa uwezo wa kunena kwa niaba Yake.

**Kampeni ya Efeso (Matendo 19:8-11)**

Mara baada ya watu hawa kumi na wawili kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu, Paulo alizindua kampeni yake ya uinjilisti na upandaji kanisa. Kampeni hii iliendelea kwa miaka miwili na kusababisha "Wayahudi wote na Wayunani waliokaa katika jimbo la Asia" kusikia habari njema za Kristo (mst. 10). Ni ajabu kama nini! Katika miaka miwili tu, kila mtu katika Asia — hata wale wa tamaduni mbalimbali za asili na makabila — alisikia injili. Kwa kuongezea, makanisa mengi yalipandwa. Yawezekana idadi hii ni pamoja na yale makanisa saba ya Asia yaliyotajwa katika Ufunuo sura ya 2 na ya 3.

**Mkakati wa Roho**

Luka alijumuisha hadithi ya huduma ya Paulo huko Efeso kama mfano wake kamili wa mkakati wa umishenari wa huyo mtume. Kwa kweli, inajumlisha mkakati wake wa umishenari ulioonyeshwa katika safari yake ya kwanza na ya pili ya umishenari. Ni mkakati ambao sisi kama wachungaji wa Kipentekoste, lazima tuutumie katika juhudi zetu za uinjilisti na upandaji kanisa leo. Hebu tuangalie kwa karibu zaidi huu mkakati wa Roho. Mkakati wa Paulo ulikuwa na "nguzo" tatu muhimu:

*1. Nguzo ya Kwanza: Kuwezesha.* Nguzo ya kwanza ya mkakati wa umishenari wa Paulo ilikuwa kutia nguvu. Uwezeshaji huu ulikuwa wa aina mbili. Kwanza, ilikuwa kuwezeshwa kwa mishenari mwenyewe. Kisha, uwezeshaji wa kanisa, au makanisa, yakipandwa. Hebu tuangalie kila moja ya vipengele hivi muhimu:

Paulo aliingia Efeso akiwa amejaa Roho Mtakatifu. Hivyo alihudumu kama shahidi aliyetiwa nguvu na Roho kulingana na maagizo ya Yesu katika Matendo 1:8. Ukweli kwamba aliweza kuweka mikono juu ya wanafunzi kumi na wawili akiwatia moyo wajazwe na Roho Mtakatifu inaonyesha kwamba yeye mwenyewe alikuwa amejaa Roho. Zaidi ya hayo, katika kitabu chote cha Matendo ya Mitume, Luka anatoa mifano mingi ya huduma ya Paulo iliyotiwa nguvu na Roho (kwa mfano, Mdo. 9:17-20; 13:4-5, 9-11; 14:8-10; 15:12).

Lakini, Paulo alielewa kwamba haikutosha kwake peke yake kujazwa na Roho. Alijua kwamba, ikiwa kazi itafanikiwa, kanisa la Efeso lazima pia litiwe nguvu na Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, baada ya kufika mjini, utaratibu wa kwanza wa kazi ya Paulo ulikuwa kuhakikisha kwamba waamini katika mji huo walikuwa wamebatizwa katika Roho Mtakatifu. Ndiyo maana aliwauliza wale wanafunzi kumi na wawili, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" Na ndio maana aliomba mara moja pamoja nao ili apokee Roho. Kwa hiyo, vipengele viwili muhimu vya nguzo ya kwanza ya mkakati wa kimishenari wa Paulo ni uwezeshaji wa mishenari na uwezeshaji muhimu sawa wa kanisa.

Kwa kuwezeshwa hivyo, kanisa la Efeso lingeweza kuwa kituo chenye nguvu cha shughuli ya umishenari, na kufika kila kona ya jimbo. Hivyo vipengele viwili — uwezeshaji wa mchungaji na uwezeshaji wa kanisa, lazima viwe sehemu ya mkakati wetu wa umisheni leo. Mkakati wa Paulo umeonyeshwa hapa chini:

---

**AGANO JIPYA "MKAKATI WA ROHO"**
(Matendo 19:1-11)

| **Nguzo ya 1: Kuwezesha** | **Nguzo ya 2: Shahidi** | **Nguzo ya 3: Uhamasishaji** |
|---|---|---|
| ● Ya mishenari | ● Tangazo | ● Mafunzo |
| ● Ya kanisa | ● Maonyesho | ● Kutuma |

---

*2. Nguzo ya Pili: Shahidi.* Nguzo ya pili ya mkakati wa umishenari wa Paulo ilikuwa ushuhuda. Hili linapaswa kutarajiwa, kwa kuwa ushuhuda wa ujasiri ni matokeo yanayotarajiwa ya kubatizwa katika Roho Mtakatifu (Mdo. 1:8; 4:31). Kama ilivyo kwa kuwezesha, shahidi pia ana vipengele viwili: tangazo na onyesho.

Kwanza, Paulo alitoa ushuhuda kwa Kristo kwa kutangaza injili kwa nguvu. Tangazo hili lilianza wakati wale kumi na wawili "waliposema kwa lugha na kutabiri." Kwa kutumia Matendo 1:8 kama ufunguo wetu wa kufasiri, tunaelewa kwamba unabii wao ulikuwa katika namna ya kutangaza injili kwa uwezo wa Roho kwa waliopotea, kama vile tangazo la kinabii la Petro katika Siku ya Pentekoste (2:14).

Kisha Luka anatuambia kwamba Paulo "akaingia katika sinagogi akanena humo kwa ujasiri kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu kwa kuwavutia kuhusu ufalme wa Mungu" (Mdo. 19:8). Katika Matendo, kutangaza ufalme wa Mungu ni sawa na kutangaza habari njema kuhusu Kristo (8:12; 28:23, 31). Zaidi ya kumtangaza Kristo katika masinagogi, Paulo "alifundisha… hadharani na nyumba kwa nyumba," na "aliwatangazia Wayahudi na Wayunani pia kwamba imewapasa kumgeukia Mungu katika toba na kumwamini Bwana wetu Yesu" (20:20 - 21). Ushahidi wa Paulo huko Efeso uliambatana na maonyesho ya nguvu ya ufalme kupitia ishara zilizofuata (19:11-20).

Hivyo, kama ile ya kwanza, nguzo hii ya pili ya mkakati wa Paulo wa Roho ilikuwa na vipengele viwili, utangazaji wa ujasiri wa injili na onyesho la nguvu za ufalme kupitia ishara zinazoambatana. Bila shaka, ushuhuda wa wenzake Paulo waliojazwa Roho ulijumuisha vipengele viwili vile vile, tangazo na onyesho. Vipengele hivi viwili vinapaswa kuwa sifa ya ushuhuda wa kila kanisa la Kipentekoste leo katika Afrika.

*3. Nguzo ya Tatu: Uhamasishaji.* Nguzo ya tatu ya Mkakati wa Roho wa kimishenari wa Paulo ilikuwa uhamasishaji. Mara tu kanisa lilipotiwa nguvu na Roho - na injili ilipokuwa ikihubiriwa - Paulo alianza kuhamasisha kanisa kwa ajili ya utume kieneo. Kuhamasishwa huko kunaonekana katika Matendo 19:10, kama ifuatavyo: "Hii iliendelea kwa muda wa miaka miwili, hata Wayahudi wote na Wayunani waliokaa katika jimbo la Asia walisikia neno la Bwana." Bila kuondoka Efeso, Paulo aliweza kuifikisha Injili katika jimbo lote la Asia kwa muda wa miaka miwili tu. Hili lingetimizwa tu kwa kuhamasisha wanafunzi huko Efeso.

Andiko linaonyesha kwamba Paulo alihamasisha kanisa la Efeso kwa njia mbili, mafunzo na kutuma. Kwanza, Paulo alifundisha watumishi na wapanda kanisa katika shule ya Tirano (Mdo. 19:9). Maneno ya kifungu yanaonyesha uhusiano wa sababu - na - athari kati ya mafunzo ya uongozi ya Paulo na ukweli kwamba katika miaka miwili tu kila mtu aliyeishi Asia alisikia neno la Bwana. Yawezekana mtaala wa shule ulijumuisha msisitizo mkubwa wa vitendo juu ya uinjilisti na upandaji kanisa. Kwa kuongezea, hali ya shule lazima ilikuwa imejaa uwepo wa Roho.

Utaratibu wa mafunzo wa Paulo pia unaonekana kujumuisha ushauri wa kazini. Hii inadokezwa katika Matendo 19:8-9, ambapo Paulo alijumuisha wanafunzi wapya waliojazwa na Roho katika huduma yake ya uinjilisti. Uhusiano

huu wa ushauri unathibitishwa zaidi na jinsi alivyobaki kwa ushirika wa karibu na wanafunzi wa Efeso (mst. 9; 20:1, 17-18). Inaelekea kwamba Paulo aliwashauri wanafunzi wake kuhusu mbinu zake za umishenari. Baadaye alimwandikia Timotheo huko Efeso, na kumwagiza, "Mambo uliyonisikia nikisema mbele ya mashahidi wengi, uwakabidhi watu wa kutegemewa, ambao watastahili pia kufundisha wengine" (2 Tim. 2:2).

Mara tu wanafunzi walipokuwa wamejazwa na Roho na kufundishwa — au hata walipokuwa bado wanafundishwa — Paulo aliwatuma kwenda kila kona ya jimbo kuhubiri injili na kupanda makanisa ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho. Bila shaka, walitumia mbinu ile ile ya kimishenari ya mshauri wao. Utumiaji wa mkakati huu ulisababisha kuongezeka kwa makanisa kwa uhuru katika eneo lote (Mdo. 19:10). Ni wazi pia kwamba mkakati wa Paulo ulihusisha kuwafikia watu wa makabila na tamaduni mbalimbali, kwa kuwa Luka anasema kwamba "Wayahudi na Wayunani pia" walihubiriwa.

### Mfano wa Yesu

Ni muhimu kutambua kwamba mkakati wa Paulo huko Efeso na Asia Ndogo haukuanzishwa na yeye. Alikuwa akifuata tu mfano wa Yesu alipolituma kanisa lake ulimwenguni.

Yesu aliwakusanya wanafunzi wake ili kuwafundisha na kuwatuma (Mk. 3:13-15). Katika kwenda kwao, walipaswa kuhubiri injili na kuonyesha nguvu zake kwa ishara na maajabu vilivyofuatana nao (Mk. 16:15-18). Lakini, kabla ya kufanya lolote katika hayo, walipaswa kungojea Yerusalemu kutiwa nguvu na Roho (Lk. 24:49; Mdo. 1:4-8) kama vile Yesu mwenyewe alivyokuwa amewezeshwa na Roho (Lk. 4:18-19; Mdo. 10:38). Kutiwa nguvu kwa wanafunzi kulitokea Siku ya Pentekoste na katika matukio mengine mengi katika Matendo. Paulo, katika kampeni yake ya Efeso, alikuwa akifuata tu mfano wa Yesu katika kulituma Kanisa Lake ulimwenguni.

## MASOMO YA KUJIFUNZA SIKU ZA LEO

Kama wachungaji wa Kipentekoste, tunaweza kujifunza baadhi ya masomo muhimu kutokana na uchunguzi wetu wa huduma ya Paulo iliyotiwa nguvu na Roho huko Efeso. Hebu tuangalie masomo matatu kati ya hayo:

### Wezeshwa na Roho

Kwanza, tunajifunza kwamba hatupaswi kamwe kujidai kufanya kazi ya Mungu kwa nguvu au uwezo wetu wenyewe wa kibinadamu. Ila, kama Yesu na Paulo, ni lazima tuhudumu katika nguvu na upako wa Roho Mtakatifu. Kulingana na mfano wa kitabu cha Matendo ya Mitume, huku kutiwa nguvu na Mungu kunakuja tunapobatizwa na kutiwa nguvu na Roho wa Mungu. Na hudumu tunapoenenda katika Roho kila siku.

Tunajifunza zaidi kwamba, kama makanisa yetu yanataka kuwa vituo vya uinjilisti wenye ufanisi, upandaji kanisa, na umisheni, lazima yawe na uhai wa kiroho unaohitajika ndani yake ili kufikia lengo hilo. Kwa hiyo, kama wachungaji wa Kipentekoste, shughuli yetu ya kwanza inapaswa kuwa kuona kwamba makanisa yetu yanatiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Tunaweza kufikia lengo hili kwa kuhakikisha kwamba wale wanaokuja kwa Kristo wanaongozwa mara moja kwenye kubatizwa katika Roho na kufundishwa jinsi ya kuishi maisha yaliyojaa Roho. Tena, ni lazima tuwaongoze watu hawa katika ushuhuda uliotiwa nguvu na Roho.[2]

### Tumia Mkakati wa Kibiblia

Pili, tunajifunza umuhimu wa kutumia mbinu ya Biblia, inayoongozwa na Roho katika kufanya kazi ya uinjilisti, upandaji kanisa, na umisheni. Huko Efeso, Paulo aliongozwa na mbinu kama hiyo. Ulikuwa ni mkakati uliotegemea mfano wa kiungu badala ya hekima ya kibinadamu. Paulo alikuwa akifuata tu mkakati ambao Yesu alikuwa ametumia katika kuhamasisha Kanisa Lake kwa ajili ya utume wa kimataifa.

Paulo alilenga zaidi kusambaza mikusanyiko ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho katika Asia Ndogo yote. Kila moja ya makusanyiko haya yangekuwa na maono na nguvu ya kiroho iliyohitajika ili kupanda makanisa mengine ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho. Kwa njia hii, makanisa yangeongezeka katika Asia yote, na injili ingetangazwa kwa nguvu kwa wote walioishi huko — Wayahudi na Wayunani pia.

---

[2] Kwa habari zaidi juu ya kuhimiza kanisa kumtafuta Roho, tazama Sura ya 19: “Kuongoza Kanisa Katika Uamsho wa Kipentekoste.” Kwa maelezo zaidi juu ya kuwaongoza waamini katika kutiwa nguvu na Roho, tazama Sura ya 20: “Kuwaongoza Waamini Kubatizwa Katika Roho.”

Leo, sisi kama wachungaji wa Kipentekoste lazima tufanye vivyo hivyo. Itabidi tujitahidi kuwafanya watu waokolewe. Hata hivyo, lazima tutambue kwamba uinjilisti tu hautoshi. Ni lazima tupande na kuendeleza makanisa ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho—makanisa ambayo waamini wapya wanajazwa na Roho, wamefundishwa katika njia za Kristo, wamefundishwa kuendeleza ufalme wa Mungu kwa ufanisi, na kisha kuhamasishwa na kutumwa kufanya vivyo hivyo katika maeneo ya karibu. na mbali.

**Piga Hatua kwa Kusudi**

Hatimaye, katika yote tunayofanya, lazima tutembee kwa makusudi. Shughuli nyingi za kanisa zinafanywa bila kusudi dhahiri. Mengi sana huchukuliwa. Hatuwezi kudhani kwamba watu watakuja kanisani kwetu kwa sababu tu tunafungua milango kila Jumapili. Hatuwezi kudhani kwamba watu wanazaliwa mara ya pili kwa sababu tu tunawaongoza katika "sala ya toba". Hatuwezi kudhani kwamba waamini wanawezeshwa na Roho kweli kwa sababu tu wanaonyesha udhihirisho fulani wa nje kimwili. Hatuwezi kudhani kwamba kanisa tunalolichunga limewezeshwa na Roho kwa sababu tu ni la Kipentekoste au sisi ni wa karismatiki. Hatuwezi kudhani kwamba kanisa letu litakuza maono ya kimishenari kwa bidii kwa sababu tu dhehebu letu linaamini katika mambo haya. Bali ni vizuri tuwe na wazo dhahiri la kile tunachotaka kutimiza, na ni vizuri tujue jinsi tutakavyofanya ili kutimiza lengo letu.

Pia lazima kuonyesha kila uamuzi na kila hatua tunayofanya. Ni lazima sisi binafsi tutafute uso wa Mungu kwa nia ya kujazwa (au kujazwa tena) kwa Roho Mtakatifu. Ni lazima tuhubiri injili kwa nia ya kuona waliopotea wakitubu na kuzaliwa mara ya pili kweli. Ni lazima tuombe pamoja na waamini kwa nia kwamba wawezeshwe kweli na Roho wa Mungu. Ni lazima tupande makanisa kwa nia ya kujifunza kwamba yawe makanisa ya kimishenari yanayowezeshwa na Roho.

Na wakati wote huo, lazima tupitishe kwa makusudi maono na mkakati wetu kwa viongozi ambao Mungu anawainua katika kanisa. Ni lazima basi tuhamasishe kanisa kwa nia iliyolenga ya kufikia jiji letu, nchi, eneo na mataifa kwa injili. Hivi ndivyo Yesu alivyofanya, na ndivyo Paulo alivyofikia Asia yote na injili katika muda wa miaka miwili tu. Hivi ndivyo tunapaswa kufanya leo.

# ~ Sura ya 37 ~

# Kuwafikia Waliopotea kwa Uinjilisti

Je, kuna umuhimu gani kumwongoza mtu mmoja tu kwa Kristo? Bila shaka, kwa mtu huyo mmoja ni muhimu milele. Lakini tendo hili moja la upendo wa Kikristo linaweza kuwa muhimu milele kwa wengine wengi pia, kama hadithi ifuatayo inavyoonyesha.

Edward Kimball alikuwa karani wa kawaida kwenye duka moja huko Detroit, Michigan, Marekani. Pia alikuwa mwalimu wa shule ya Jumapili katika kanisa lake. Mnamo 1854, Kimball alikutana na mvulana wa miaka kumi na saba aliyeitwa Dwight na kumuongoza amfuate Kristo. Mvulana huyo alikuja kuwa mwinjilisti mashuhuri aliyejulikana kama D.L. Moody. Moody alikuja kuwa mmoja wa wainjilisti wakuu katika historia. Moody alimshawishi F.B. Meyer kuingia katika kazi ya uinjilisti na umisheni, ambaye naye alimshawishi J. Wilbur Chapman, aliyekuja kumshawishi Billy Sunday kufanya huduma kama mwinjilisti. Yeyote ambaye amesoma historia ya kanisa la kisasa anajua kwamba watu hawa wote walikuwa wainjilisti wenye nguvu. Kwa pamoja, waliwaleta mamilioni kwa Kristo. Huo haukuwa mwisho wa hadithi.

Mhubiri mmoja aitwaye Mordekai Ham alitiwa moyo na huduma ya Billy Sunday. Kisha, mnamo mwaka wa 1934, Ham alihubiri ujumbe uliomfanya Billy Graham kutoa maisha yake kwa Kristo. Billy Graham amehubiri injili kwa watu wengi zaidi kuliko mtu mwingine yeyote katika historia. Hebu fikiria, yote haya yalitokana na mwalimu wa kawaida tu wa shule ya Jumapili kumleta mvulana mmoja wa mitaani kwa Kristo. Hadithi ya Edward Kimball inaonyesha jinsi ilivyo muhimu kwa mchungaji wa Kipentekoste kuliongoza kanisa lake katika uenezaji wa uinjilisti wenye ufanisi. Sura hii itajadili jinsi wanavyoweza kufanya hivi vizuri zaidi.

## UFAFANUZI

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ufahamu vizuri uinjilisti ni nini na jinsi unavyohusiana na upandaji kanisa na umisheni. Ingawa shughuli zote tatu hutiririka kutoka kwenye Agizo Kuu la Kristo (Mt. 28:18-20; Mk. 16:15-16), kuna tofauti muhimu.

### Uinjilisti

Uinjilisti ni kushirikisha kwa makusudi injili kwa waliopotea kwa nia ya kuwaleta kwa Kristo. Ni pamoja na kuwaambia watu kuhusu Yesu na kazi yake ya kuokoa msalabani, na kuwaita kwenye imani katika Yeye (Mdo. 16:31). Kiini cha uinjilisti ni habari ya kifo na ufufuo wa Yesu (1 Kor. 15:1-4). Uinjilisti ni zaidi ya mpango katika kanisa: ndiyo sababu ya Kanisa kuwepo. Na ni jukumu zito la kila Mkristo.

### Upandaji Kanisa

Ingawa upandaji kanisa unahusisha uinjilisti, una mengi zaidi. Upandaji kanisa unahusisha kuwapanga wale walio-okolewa katika vikundi vya waamini, yaani kanisa. Hao waamini hukusanyika mara kwa mara kwa ajili ya ushirika, maombi, na kujifunza Biblia. Viongozi wanachaguliwa ambao watawafanya hao waamini kuwa wanafunzi, wafanane na Kristo. Waamini wapya wanafundishwa jinsi ya kuacha maisha yao ya zamani ya dhambi, kuishi kulingana na Neno la Mungu, na kuwaambia wengine kuhusu Yesu.

### Umisheni

Mara nyingi umisheni hujumuisha uinjilisti na upandaji kanisa. Lakini kuna tofauti chache kubwa. Umisheni huhusisha kuwaleta waliopotea kwa Kristo na kupanda makanisa katika tamaduni mbalimbali. Inabidi wamishenari waache

makao yao, waende mahali papya, wajifunze lugha mpya, na kukubaliana na maisha katika mazingira yao mapya. Katika mazingira hayo ya "kigeni," wanawavuta waliopotea kwa Yesu na kuanzisha makanisa mapya.

Paulo ni mfano wa mishenari. Alivuka mipaka na tamaduni ili kumtangaza Kristo kwa waliopotea. Alipofanya hivyo, alianzisha makanisa na kufuatilia maendeleo yao. Ili kuhakikisha kwamba makanisa yanafanikiwa, Paulo aliteua wazee na wachungaji kuongoza makusanyiko hayo. Sehemu ya majukumu ya wachungaji ilikuwa kuongoza makanisa yao kufanya uinjilisti kwa waliopotea na wao nao kutuma wamishenari. Hili lingehakikisha kwamba kazi ya uinjilisti, upandaji kanisa, na umisheni inaendelea (rej. 1 Thes. 1:8).

## WAJIBU WA MCHUNGAJI

Paulo alimwandikia Timotheo, mwanawe katika imani na mchungaji wa kanisa la Efeso, na kumwambia "fanya kazi ya mwinjilisti" (2 Tim. 4:5). Kazi ya mwinjilisti ni kuwaleta waliopotea kwa Kristo na kuwafundisha wengine kufanya vivyo hivyo (Efe. 4:11-12). Kama mchungaji wa Kipentekoste, wewe pia unabeba jukumu hili. Lazima utengeneze mpango wa kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya uinjilisti wenye ufanisi. Mpango huu wa uhamasishaji unapaswa kuwa na mikakati mitatu: kuhamasisha, kufundisha, na kupeleka kazini.

### Kuhamasisha

Kama mchungaji wa Kipentekoste, kazi yako ya kwanza katika kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya uinjilisti ni kuingiza katika mioyo ya watu wa Mungu shauku kwa ajili ya waliopotea. Njia moja ya kufanya hivyo ni kwa kuwafundisha kile kinachosemwa na Biblia kuhusu kupotea kwa mwanadamu. Bila kuwa na uhusiano wenye kuokoa na Yesu Kristo, watu wote wamepotea milele, bila tumaini. Tumaini lao pekee katika maisha haya, na katika maisha yajayo, ni kumjua Kristo. Lazima ukazie kweli hizi za ajabu kwenye mioyo na akili za watu wako. Lazima uwakumbushe zaidi wajibu wao wa kuwashirikisha injili watu waliopotea.

Ili kukamilisha hili, utahitaji kumtegemea Roho wa Mungu aliye nguvu ya umishenari. Lazima uhakikishe kwamba washirika wa kanisa wamejazwa na Roho Mtakatifu na kutiwa nguvu kama mashahidi wa Kristo (Mdo. 1:8). Tena, lazima uhakikishe kwamba uwepo na nguvu za Roho vinaonyeshwa katika ibada za kanisa. Akipewa nafasi, Roho Mtakatifu atatembea katika mioyo ya watu, akiwafinyanga na kuwaelekeza kwenye mavuno.

**Mafundisho**

Mbinu nyingine unayoweza kutumia kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya uinjilisti ni mafundisho. Ndivyo Yesu alivyofanya. Aliwaagiza wanafunzi wake, "Njooni, mnifuate… nami nitawatuma kuwa wavuvi wa watu" (Mk. 1:17). Wanafunzi wa Yesu walipomfuata Bwana wao, kusikiliza mafundisho Yake, na kuiga mbinu Zake, wakawa watangazaji wa injili wenye nguvu sana.

Nguvu hiyo hiyo lazima itokee katika makanisa yetu ya Kipentekoste leo. Ni lazima tuwafundishe washirika wetu jinsi ya kufanya uinjilisti ili kuwafikia waliopotea kama Yesu na mitume walivyofanya. Katika kufanya hivi, ni lazima tuwafundishe jinsi ya kutembea katika Roho na kutambua sauti ya Roho anapowaelekeza katika ushuhudiaji (rej. Mdo. 8:29). Tena, kama wachungaji wa Kipentekoste, ni lazima tuwafundishe watu wetu jinsi ya kujitoa kuwa katika upako wa Roho, tukimtumaini Yeye kuwatumia wanapowaambia wengine kuhusu Kristo.

Zaidi ya hayo, ni lazima tuhakikishe kwamba watakatifu wanaelewa injili, na kwamba wana uwezo wa kuiwasilisha kwa wengine kwa uwazi. Tena ni lazima waelewe zaidi jinsi ya kuwaongoza watu kwa Yesu, wakiwaita kuja kwenye toba na imani. Njia moja ya kufanikisha hili ni kufanya warsha za kila mwaka juu ya uinjilisti unaotiwa nguvu na Roho.

**Kutuma**

Mara tu watu wa Mungu wanapokuwa wamehamasishwa na kufundishwa, ni lazima wasambazwe. Ndivyo Yesu alivyofanya. Kama sehemu ya mpango Wake wa mafunzo, aliwatuma wanafunzi Wake kuhubiri injili. Kisha waliripoti kwake ili yeye awafanyie tathmini (ling. Lk. 9:6; 10:1-20). Baadaye, huduma Yake duniani ilipokuwa karibu kumalizika, aliwatuma wanafunzi Wake kwa ajili ya ushuhuda "katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Mdo. 1:8). Kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kufanya vivyo hivyo. Unapaswa kuwa mfano wa maisha ya uinjilisti mbele ya watu wako. Unapaswa basi kuwafundisha na kuwapeleka katika huduma.

## MBINU ZA UINJILISTI

Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, hupaswi kukaa bila kufanya kitu, ukitumaini kwamba watu katika jumuiya watakuja kanisani kwako. Wala usifikirie kwamba washirika wako watakuwa mashahidi wa ghafla kwa marafiki na majirani zao. Kama mchungaji, lazima uwe mfano na kuwaongoza watu

kwenye mavuno. Tengeneza mikakati na kutekeleza mipango ya kuhamasisha kanisa kwa ajili ya uinjilisti wenye ufanisi.

Unaweza kufanya hivi kwa kutumia mbinu mbalimbali za uinjilisti. Uchaguzi wa mbinu utategemea mazingira ya jamii, walengwa, na uongozi wa Roho Mtakatifu. Hapa kuna njia chache za uinjilisti unazoweza kutumia:

**Huduma za Kawaida za Kanisa**

Uinjilisti lazima uwe muhimu sana katika ibada za kawaida za kanisa. Ni lazima wakati wote uwe makini kuhusu watu waliopotea katika ibada zako. Na lazima uwatangazie Injili kwa uaminifu. Kama Paulo, lazima uamue kuhubiri tu "Kristo, naye amesulubiwa" (1 Kor. 2:1-2). Ni huzuni iliyoje kwa mshirika kuleta rafiki aliyepotea kwenye kanisa ambalo injili haihubiriwi. Kila ujumbe unaohubiri unapaswa kuwa na maelezo ya mpango wa wokovu na mwaliko wa kuja kwa Kristo.

**Uinjilisti wa Mtu kwa Mtu**

Pamoja na kutangaza injili katika huduma za kawaida za kanisa, lazima uhakikishe kwamba washirika wa kanisa lako wanajua jinsi ya kuwashirikisha injili wale walio nje ya kanisa. Uinjilisti wa aina hii unaitwa uinjilisti binafsi. Kama mchungaji wa kanisa, utataka kuhimiza aina zifuatazo za uinjilisti wa binafsi.

*Uinjilisti wa nyumba kwa nyumba*. Katika kampeni ya kuhubiri nyumba kwa nyumba, washirika wa kanisa hufanya mazoezi kisha kutumwa kwenda nyumba kwa nyumba, wakijitambulisha kwa watu na kuwafanya watambue mzigo wa kanisa kwa ajili yao. Wajitoe kuombea mahitaji yao, na wawe tayari kushirikisha injili kwa wale wanao-onyesha kupenda.

*Uinjilisti wa urafiki.* Unapaswa pia kuandaa na kuwahimiza washirika wa kanisa kuombea wokovu wa rafiki zao. Wanapaswa kumwomba Mungu kufungua mioyo ya rafiki zao na kutoa fursa kwao kuwashirikisha injili. Kanisa linaweza kupanga "Siku ya Marafiki" ya kila mwaka wakati washirika wanahimizwa kuwaalika rafiki zao kanisani. Siku hiyo, marafiki wote watakaohudhuria wataonyeshwa heshima fulani. Kisha utahubiri ujumbe wa uinjilisti na kuwapa fursa ya kumpokea Kristo kama Mwokozi.

*Uinjilisti kwa mtindo wa maisha.* Pia utataka kuwafundisha watu kwamba, kwa kweli, uinjilisti si tukio au utaratibu bali ni mtindo wa maisha. Utataka

kuwahimiza kushuhudia kwa maisha yao na ushuhuda wa binafsi. Wanatakiwa wakati wote kuwa wazi kwa fursa za kushirikisha wengine injili katika matukio ya kila siku maishani.

**Kampeni za Uinjilisti**

Kampeni za uinjilisti (wakati fulani huitwa mikutano ya uamsho) ni njia nyingine bora ya kuwaongoza watu kwa Kristo. Kampeni ya uinjilisti inaweza kwenda kama ifuatavyo: Wewe na viongozi wako wa kanisa pangeni kampeni, na kwa wakati ufaao, muanze kuitangaza kwa kanisa na jamii. Tukio linapokaribia, kanisa linaanza kufunika hilo tukio hilo kwa maombi. Washirika wanahimizwa kualika familia zao, marafiki, na majirani kwenye mikutano. Kama mchungaji, lazima uhakikishe kwamba yule unayemwalika kuhudumu ana moyo kwa ajili ya waliopotea na ana sifa ya kuhubiri injili. Tena hakikisha kwamba mhubiri anatangaza injili kwa uaminifu katika kila huduma na kuwapa watu fursa ya kuokolewa.

**Mikutano ya Hadhara**

Pia, peleka kampeni ya uinjilisti mitaani. Andaa na kutuma timu za uinjilisti kwenye masoko au sehemu zingine ambapo idadi kubwa ya watu hukusanyika. Huko, watafanya huduma fupi lakini zenye nguvu na zinazoonekana. Ibada hizi ziwe na kuimba ili kuvutia umati, shuhuda binafsi za neema ya Mungu, na ujumbe mfupi wa injili ukifuatiwa na mwaliko wa kumpokea Kristo.

**Usambazaji wa Vipeperushi**

Njia nyingine iliyothibitishwa ya kueneza injili ni kupitia usambazaji wa vipeperushi. Unaweza kupanga siku ya kutuma watendakazi katika eneo mliloamua ili kusambaza vipeperushi vya ujumbe wa injili. Hizo traksi zinazotolewa zichaguliwe kwa uangalifu. Ni vizuri zivutie, ziwe zilizoandikwa vizuri, na zenye kuonyesha mpango wa wokovu kwa uwazi na urahisi. Vile vile ziwe na maelezo kuhusu mawasiliano, ambayo ni jina la kanisa, mahali lilipo na namba ya simu, tovuti ya kanisa na anwani za barua pepe (kama vitu hivyo vipo).

**Matembezi ya Maombi**

Matembezi ya maombi yanaweza kutumika kufungua maeneo mapya kwa ajili ya injili. Vile vile yanaweza kuwa na manufaa katika kuingiza mzigo katika mioyo ya waamini kwa ajili ya kufikia eneo fulani husika kwa ajili ya Kristo. Kanisa linaweza kupanga timu za kutembea wawili-wawili, katika mitaa

iliyochaguliwa. Wanapofanya hivyo, watamwomba Roho Mtakatifu awatangulie watenda kazi, akifungua mioyo ya wenyeji kupokea injili. Wanaweza pia kutaka kufanya vita vya kiroho, kutoa changamoto na kuwafunga pepo wanaowafunga watu katika utumwa wa kiroho na kimwili.

Vikundi vinapotembea vikiomba katika eneo au mtaa, wawe huru kutumia fursa za kuomba na watu na kuwaambia injili. Matembezi ya maombi ni njia bora ya kuandaa udongo kwa ajili ya kupanda kanisa jipya.

**Uhamasishaji Kupitia Vyombo vya Habari**

Ikiwa kanisa lako lina uwezo wa kifedha, unaweza kufikiria kutumia vyombo vya habari kueneza injili. Fursa za vyombo vya habari ni pamoja na matangazo ya redio na televisheni. Mitandao ya kijamii pia inaweza kutumika kwa ubunifu kueneza injili. Katika kupanga uhamasishaji kama huo, kumbuka kwamba, ikiwa mipango, ratiba na vipindi sio vya ubora wa hali ya juu, watu wanaweza kwenda mbali na kanisa badala ya kuwavuta wafike kanisani.

**Upandaji Kanisa**

Utafiti umeonyesha kwamba upandaji kanisa ni njia ya ufanisi zaidi ya uinjilisti. Watu wengi zaidi huja kwa Kristo katika makanisa mapya kuliko makanisa ya zamani yaliyokwisha anzishwa. Kupitia upandaji kanisa, kanisa halikui kiidadi tu, bali linaenea kijiografia.[1]

**Mbinu Nyingine Bunifu**

Funguka kwa mbinu zingine za ubunifu za uinjilisti. Wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, wakati wote uwe wazi ili kuongozwa na Roho Mtakatifu katika kuunda na kupanga mipango mipya ya kuwafikia watu.

## FURSA ZA KUFANYA UINJILISTI

Paulo aliwasihi Wakristo wa Efeso: "tumieni vizuri kila fursa" (Efe. 5:16). Kadiri hali zinavyobadilika, fursa mpya za uinjilisti zitajitokeza zenyewe. Basi wewe kama mchungaji wa Kipentekoste ni vizuri uongozwe na Roho Mtakatifu na kuwa tayari kukabiliana na mahitaji yanapotokea. Kwa mfano, tazama fursa hizi nne za kawaida:

---

[1] Upandaji kanisa unajadiliwa kwa undani zaidi katika Sura ya 39: "Kupanda Makanisa Mapya."

### Kuitikia Mambo Magumu

Misukosuko ya kijamii kama vile vita, njaa, magonjwa ya mlipuko, ukame, vimbunga, mashambulizi ya wadudu, na majanga mengine ya asili hutoa fursa kubwa kwa kanisa kushirikisha watu habari njema za Kristo. Katika nyakati hizi za shida, watu wanatafuta majibu. Basi mioyo yao inakuwa wazi zaidi kumsikia Bwana. Ujumbe wa Kikristo wa upendo hutoa tumaini kwa waliojeruhiwa na kuteseka katika mazingira kama hayo. Katika nyakati kama hizo, wewe na kanisa lako mnapaswa kuwa tayari kujitokeza na kuwafikia watu kwa upendo na huruma. Unapaswa kutafuta njia za kuwahudumia wale wanaohitaji. Unapofanya hivyo, tumia vizuri fursa zinazojitokeza za kuwashirikisha injili.

### Kufikia Jumuiya ya Waislamu

Jumuiya ya Waislamu inakua na kuenea kote barani Afrika. Uislamu wenye itikadi kali unasonga mbele kwa kasi, na unaharibu baadhi ya sehemu za bara. Waislamu wengi wamekatishwa tamaa na dini yao. Kanisa lako lazima litengeneze mikakati ya umisheni yenye uhakika na inayofaa kwa ajili ya kufanya uinjilisti kwa hao Waislamu waliokatishwa tamaa.

### Kutumia Mahusiano

Mitandao ya kifamilia kama vile wanafamilia, marafiki, majirani, na mnaofanya kazi pamoja, inaweza kutumika kama madaraja ya kawaida ya kufanya uinjilisti. Hii ni kweli hasa katika mazingira ya vijijini barani Afrika. Huko, watu wanaishi kwa ukaribu na kushirikiana katika mambo mengi. Kwa hali kama hiyo, kugeuzwa kwa kiongozi mmoja muhimu katika jamii kunaweza kusababisha wengine kuokoka katika mduara wake wa mahusiano. Uinjilisti kupitia mitandao ya uhusiano una nafasi kubwa ya mafanikio barani Afrika.

### Ubia Kimkakati

Kuunda ushirikiano wa kimkakati na makanisa na mashirika yenye nia moja na malengo yanayofanana inaweza kuwa njia nyingine nzuri ya kuwafikia waliopotea kwa injili. Hii ni kweli hasa katika kutekeleza juhudi za umisheni zinazokubaliwa na wahusika wote. Kanisa lako linaweza kushirikiana na makanisa mengine na mashirika yasiyofungamana na dhehebu lolote kutekeleza mipango maalum inayolenga kufikia sehemu fulani za jamii zilizopuuzwa, kama vile yatima, watoto wa mitaani, au waathiriwa wa majanga ya asili.

## MAMBO MUHIMU

Ingawa kunaweza kuwa na njia nyingi za uinjilisti, vipengele vitatu vya msingi lazima viwepo kila wakati kwa mchungaji wa KiPentekoste, ambavyo ni: kutangaza injili, nguvu za Roho Mtakatifu, na maombi ya dhati.

**Kutangaza Injili**

Ili kufanya uinjilisti kuwafikia waliopotea, injili lazima ihubiriwe (Mk. 16:15; 1 Kor. 9:16). Paulo alitangaza kwamba, "Kila mtu atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa" (Rum. 10:13). Kisha akauliza mfululizo wa maswali yaliyo wazi: "Basi, wanawezaje kumwita yule ambaye hawajamwamini? Na wanawezaje kumwamini yule ambaye hawajasikia habari zake? Na wanawezaje kusikia bila mtu anayewahubiria?" (mst. 14). Hakuna wokovu bila kusikia na kuamini injili. Kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kuwa tayari kila wakati kushirikisha waliopotea habari njema (Rum. 1:15-16). Na unapaswa kuwaandaa washirika wako kufanya vivyo hivyo.

**Nguvu ya Roho Mtakatifu**

Hakuna mradi wa uinjilisti unaopaswa kufanywa bila nguvu za Roho Mtakatifu. Yesu aliwaagiza hivi wanafunzi wake: "Nendeni mkafanye wanafunzi kutoka katika mataifa yote" (Mt. 28:19). Lakini kwanza, walipaswa kukaa "mjini mpaka mtakapovikwa uwezo utokao juu" (Lk. 24:49; taz. Mdo. 1:4-8). Huo mfumo wa kibiblia unaendelea hadi leo — kwanza kutia nguvu, kisha kutangaza kwa kutumia hizo nguvu.

Mtindo wa uinjilisti wa Agano Jipya unahusisha zaidi mahubiri ya upako yakiambatana na uthibitisho wa ishara na maajabu (Mt. 10:7-8; Mk. 16:17). Si lazima injili itangazwe tu, bali nguvu yake lazima idhihirishwe pia. Hii ni kweli hasa katika Afrika. Waafrika wengi wanatoka katika maisha ya kuabudu sanamu, uchawi, na ushirikina. Wanatafuta dini inayoahidi nguvu juu ya nguvu za giza.

Basi, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima, lazima ukazie ubatizo katika Roho Mtakatifu, huduma ya nguvu, na udhihirisho wa karama za kiroho katika uenezaji wa uinjilisti. Lakini, lazima uwe mwangalifu ili kuhakikisha kwamba ujumbe wa injili hauathiriwi katika utafutaji wa miujiza ya kuvutia.

**Maombi ya Dhati**

Kwa kumalizia ni vizuri kutambua kwamba kila shughuli ya uinjilisti ya kanisa inapaswa kufunikwa kwa maombi ya dhati. Maombi kama haya ni ufunguo wa mafanikio ya uinjilisti. Kila shughuli nyingine ya uinjilisti hutiririka kutokea humo. Katika maombi tunamwita Mungu awatie nguvu watakatifu, aelekeze hatua zao, atie mafuta mahubiri yao, afanye ishara na maajabu, na kufungua mioyo ya wale watakaosikia Injili itakayotangazwa (rej. Mdo. 4:29-30).

---

Uinjilisti ndio kiini cha sababu ya kuwepo kwa Kanisa. Hakuna kanisa linaloweza kujiita la Kipentekoste kweli huku likishindwa kuwafikia waliopotea kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Hivyo, kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uliongoze kanisa lako kwa ujasiri katika kuwafikia waliopotea kwa ajili ya Kristo.

~ Sura ya 38 ~

# Kutumikia Jumuiya

Mchungaji wa kanisa dogo la Kipentekoste Afrika Mashariki alisukumwa na Roho Mtakatifu kuanzisha shule ya msingi katika eneo la kanisa lake. Alishuhudia hivi: "Tulitaka tu kusaidia watoto wa jirani na elimu bora. Tulitaka kufanya sehemu yetu ili kutokomeza ujinga katika jamii yetu." Ingawa hakuwa na pesa, na hakuwa na uzoefu wa kuendesha shule, mchungaji aliamini kwamba Mungu alikuwa amesema naye. Kwa hiyo kwa imani, alisonga mbele na mpango wake.

Alipotambua kwamba shule ilihitaji kabati za kuhifadhia vifaa vya kufundishia, huyo mchungaji alitoa kabati hizo kutoka nyumbani kwake na kuzihamishia shuleni. Aliuza vitu vingine vya binafsi ili kununua madawati, vitabu, na vifaa vya ujenzi. Kisha akasonga mbele katika utendaji wa kutekeleza maono yake. Kwa sababu shule haikuwa na uwezo wa kumlipa mlinzi, alijitolea mwenyewe kuhudumu katika nafasi hiyo. Muda wote huo, alimwamini Mungu amtegemeze na kumwongoza. Hatua kwa hatua, shule ilifanikiwa na kukua.

Watu katika jamii walipomwona mchungaji akishughulika hivyo, waliguswa na maono yake na udhati wa kujali kwake kuhusu mafanikio yao. Basi walianza kuchangia fedha kusaidia shule hiyo. Baada ya muda, Mungu alitengeneza njia kwa kanisa kujenga madarasa zaidi. Madarasa haya mapya yalijengwa kulingana

na viwango vya serikali. Hivi majuzi, shule imepata ardhi ya ziada ambayo itaendeleza shule zaidi. Mchungaji alisema hivi: "Tunapanga kujenga madarasa zaidi na uwanja wa michezo kwa ajili ya watoto. Bado hatujafika mahali Mungu anapotaka tuwe, lakini Mungu ni mwaminifu, na anatusaidia kusonga mbele. Shule yetu sasa ni miongoni mwa shule bora zaidi katika eneo hili."

Katika yote waliyofanya, mchungaji na wafanyakazi wa shule walibaki kuwa waaminifu kwa agizo la Kristo la kushirikisha injili kwa waliopotea. Kwa sababu hiyo, wengi wa wanafunzi wamekuwa Wakristo. Pia, nia njema iliyotokana na shule ilifungua mioyo ya wazazi kadhaa ambao walitoa maisha yao kwa Yesu. Zaidi ya hayo, Mungu ameitumia shule hiyo kufungua mlango wa ushuhuda kwa jamii ya Kiislamu iliyo katika eneo hilo.

Huu ni mfano mmoja tu wa njia nyingi ambazo wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, unaweza kutumia kuliongoza kanisa lako katika kuonyesha kuijali jumuiya yako. Sura hii itachunguza somo hili. Itaweka msingi wa kibiblia kwa huduma kamilifu. Huduma kamili ni huduma ya Kikristo inayolenga kutumikia mtu kamili: roho, nafsi na mwili. Sura hii pia itatoa mapendekezo yanayoweza kufanyiwa kazi kuhusu jinsi kanisa lako linavyoweza kujihusisha na kuonyesha kuijali jamii.

## MAMLAKA YA KIBIBLIA

Katika mijadala ya umisheni, wakati mwingine swali huulizwa, "Ni kipi kilicho muhimu zaidi, kuhubiri injili kwa waliopotea au kuwajali wenye uhitaji?" Jibu ni kwamba, ingawa hakuna kitu muhimu zaidi kuliko kuwaongoza wenye dhambi kwa Kristo, kanisa lazima lihusishwe katika kufanya uinjilisti na uenezaji wa injili na utunzaji wa jamii. Yote hayo ni madhihirisho ya kuja kwa ufalme wa Mungu. Ingawa kanisa la Kipentekoste barani Afrika limefaulu katika kuwaongoza watu kwa Kristo na kuanzisha makanisa mapya, limekuwa na ufanisi mdogo katika kuwahudumia wanaoumia.

Kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uepuke mitego miwili. Kwanza, lazima uepuke kuhubiri injili huku ukipuuza mateso ya kimwili ya wale walio karibu nawe. Wakati huo huo, lazima uepuke kushughulikia mahitaji ya kimwili ya watu bila kuwashirikisha injili. Mtu fulani alisema, "Hatujahubiri injili kikamilifu mpaka tuonyeshe upendo wa Kristo, na hatujaonyesha upendo wa Kristo kikamilifu mpaka tunapowahubiria injili". Hebu tuchunguze kwa ukaribu zaidi kile ambacho Biblia inasema kuhusu habari hii muhimu.

**Kufuata Mfano wa Yesu**

Yesu ndiye kielelezo chetu cha huduma. Alihudumia mtu kamili: roho, nafsi, na mwili. Alipokuwa karibu kuanza huduma yake, alitaja kusudi lake. Akasema, "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa" (Lk. 4:18-19). Hivyo, huduma ya Yesu ilikuwa na alama ya kutangaza habari njema na kushughulikia mahitaji ya watu.

Kanisa katika kitabu cha Matendo ya Mitume lilifuata utaratibu uliowekwa na Yesu. Walihubiri injili, wakaponya wagonjwa, wakatoa pepo, na kuwatunza wenye uhitaji. Mfano mmoja wa wao kujali wahitaji ni jinsi walivyowajali wajane wa Kiyunani huko Yerusalemu (Mdo. 6:1). Mfano mwingine ni mwitikio wa kanisa la Antiokia kwa watakatifu waliokuwa na njaa huko Yerusalemu. Waliposikia himizo la kiunabii kutoka kwa Agabo, "wanafunzi, kwa kadiri kila mmoja alivyoweza, waliamua kutoa msaada kwa ajili ya ndugu na dada waliokuwa wakiishi Yudea. Wakafanya hivyo, wakapeleka zawadi yao kwa wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli" (Mdo. 11:29-30).

**Mamlaka Mbili Kuu**

Yesu aliliachia Kanisa Lake maagizo makuu mawili. Moja linaitwa Agizo Kuu (Mt. 28:18-20); lingine linaitwa Amri Kuu (Mt. 22:34-40). Kama mchungaji mwaminifu wa Kipentekoste, lazima uliongoze kanisa lako kutii yote mawili. Katika Agizo Kuu, Yesu ametuamuru akisema, "nendeni mkafanye wanafunzi katika mataifa yote." Katika Amri Kuu, ametuamuru kumpenda Mungu sana na kuwapenda jirani zetu kama sisi wenyewe. Katika Mfano wa Msamaria Mwema, Yesu alifundisha kwamba jirani yetu anaweza kuwa mtu yeyote tunayekutana naye anayehitaji msaada wetu — bila kujali kabila au dini. Msamaria Mwema alithibitika kuwa jirani mwema kwa kumwinua na kumsaidia yule mtu aliyejeruhiwa. Yesu anatuamuru, "Nenda ukafanye vivyo hivyo" (Lk. 10:37).

**Ushauri Mwingine wa Biblia**

Katika sehemu nyingine nyingi, Biblia inatuambia tuwajali walio na uhitaji. Kwa mfano, Yakobo anaandika, "Dini ambayo Mungu Baba yetu anaikubali kuwa safi na isiyo na dosari ni hii, kuwatunza yatima na wajane katika dhiki yao na kujilinda na kuchafuliwa na dunia" (Yakobo 1:27). Yesu alifundisha kwamba kwa kuwahudumia walio na uhitaji (yaani, wenye njaa, wenye kiu, walio uchi,

wagonjwa, wasio na makao, na wafungwa), tunamhudumia Kristo (Mt. 25:31-40). Tunapoacha kuwajali, tunakuwa tumempuuza Kristo na agizo lake kwetu (mst. 41-46). Unapohudumia mahitaji ya kimwili ya watu, hupaswi kusahau kamwe kwamba kila mmoja ana nafsi ya milele itakayoishi mbinguni au kuzimu milele. Hupaswi kukosa kuwashirikisha injili na kuwapa nafasi ya kuokoka.

## THAMANI YA KUHUDUMIA JUMUIYA

Kuna faida nyingi kwa kanisa la Pentekoste kuhudumia jamii. Hebu tuangalie mbili:

### Inampendeza Mungu

Mungu anafurahi wakati watoto Wake wanapohudumia jumuiya zao na kuwafikia walio karibu nao kwa matendo ya huruma. Tunapofanya hivyo, tunadhihirisha asili ya Mungu ya upendo na kufuata mfano wa Yesu, ambaye mara nyingi aliwaponya wote waliokuja kwake (Mt. 8:16). Katika Mahubiri yake ya Mlimani, Yesu alisema, “Mmesikia kwamba imenenwa, ‘Mpende jirani yako na umchukie adui yako’. Lakini mimi nawaambia, ‘wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni.’ Yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki” (Mt. 5:43-45). Yesu anasema tunapaswa kupenda na kutafuta kumbariki kila mtu — hata adui zetu. Tukfanya hivyo, tutakuwa kama Baba yetu wa Mbinguni, na matendo yetu yatampendeza Mungu.

### Inafungua Milango

Kuijali jamii hakumpendezi Mungu tu bali pia hujenga nia njema kati ya kanisa na jumuiya. Watu wa Mungu wanapowatendea wengine fadhili, watu huona na kuanza kulitazama kanisa kwa mtazamo mzuri. Wakati fulani Yesu alimponya kiziwi na bubu. Watu waliposikia juu ya tendo hilo la huruma, walisema kwa mshangao, "Amefanya kila kitu vizuri. ... hata huwafanya viziwi kusikia na bubu kusema" (Mk. 7:37). Watu walipoona kwamba Yesu anawajali, mioyo yao ilimgeukia. Kanisa lako linapoanza kuhudumia na kubariki jumuiya yake, watu watasema, “Hao ni watu wazuri.” Watu wa nje wanapoanza kulitazama kanisa lako vizuri, milango itafunguliwa kwa ajili ya uinjilisti.

## KUTAMBUA MAHITAJI

Huduma kwa jamii huanza kwa kutambua hitaji, kisha kupiga hatua kukidhi hitaji hilo. Zifuatazo ni njia chache kwa kanisa lako kuhudumia jumuiya yake.

### Shule za Kikristo

Shule za Kikristo ni njia iliyothibitishwa kwa kanisa kuhudumia jamii na kusambaza na kuendeleza injili. Makanisa mengi ya Kipentekoste kote barani Afrika yanabariki jumuiya zao kwa kuendesha shule. Baadhi wamezianzisha ili kushughulikia hitaji la elimu ya msingi katika eneo lililosahaulika. Wengine wameanzisha shule ili kutoa elimu mbadala ya Kikristo kwa mfumo uliopo wa elimu ya kidunia, au Kiislamu. Shule zinafaa hasa katika maeneo ambayo watu wanapinga injili. Kanisa ambalo haliwezi kuona namna ya kuanzisha shule linaweza kuanza kwa kusajili washirika wa kanisa wenye uwezo ili kutoa mafunzo ya bure kwa wanafunzi wanaohitaji usaidizi katika masomo yao (maarufu kama tuisheni).

### Miradi ya Huduma kwa Jamii

Baadhi ya makanisa ya Kipentekoste yanabariki jumuiya zao kupitia miradi ya huduma aina mbalimbali. Wanaona uhitaji katika jamii na kujipanga kulishughulikia hitaji hilo. Kwa mfano, kanisa linaweza kujitolea kupaka rangi kituo cha afya cha mtaa. Au wanaweza kutaka kurekebisha vioo vilivyovunjika katika shule ya msingi hapo mtaani. Au wanaweza kutaka kurekebisha paa inayovuja kwenye nyumba ya mjane. Katika kanisa moja, wanaume waliunda kikundi walichokiita Wasamaria wa Jumamosi. Kila Jumamosi, washirika wa kanisa walitoka ili kusaidia wajane na watu wengine wenye uhitaji kwa kazi mbalimbali. Ziko njia nyingi ambazo kanisa linaweza kutumia kutoa huduma kwa jumuiya yake kupitia miradi mbalimbali.

### Huduma ya Afya

Jamii nyingi barani Afrika hazina huduma za afya za kutosha. Ili kushughulikia hitaji hili, kanisa linaweza kutaka kujenga kituo cha afya kwa ajili ya jamii. Halafu linaweza kutumia ushawishi wake kupata wafanyakazi wa huduma ya afya kwa ajili ya hicho kituo. Unaweza kuwahimiza washirika wako kuwa watu wanaojali. Wanaweza kutafuta katika vitongoji vyao watu wenye mahitaji ya kimwili. Kisha wanaweza kuwafanyia maombi ya uponyaji, kuwafariji, na kuwapa msaada wa kifedha.

### Maji Safi

Kulingana na ukubwa wake na nguvu zake za kifedha, kanisa lako linaweza kutoa maji safi kwa jumuiya yako kwa kufadhili kisima cha maji. Au linaweza kutaka kurekebisha kisima cha zamani kisichofanya kazi.

### Kulisha na Kutunza Watoto

Utapiamlo wa watoto ni changamoto kubwa katika sehemu nyingi za Afrika. Huathiri ukuaji wa mwili na akili wa mamilioni ya watoto na vijana, na athari zake hudumu maishani. Baadhi ya makanisa ya Kipentekoste yameanzisha programu za kulisha watoto, ambapo watoto huja mara moja kwa siku kwa ajili ya kupata mlo. Wengine wameanzisha programu za utunzaji wa watoto kwa bei nafuu. Hizi huwaruhusu wazazi kwenda kazini wakijua kwamba watoto wao wanatunzwa ipasavyo. Programu kama hizo za ulishaji na malezi ya watoto hutoa fursa kwa kanisa kuwashirikisha injili wao na wazazi wao. Pia hutoa nafasi kwa kanisa kuwafundisha watoto maadili ya kimungu.

### Mipango ya Kutoa Misaada kwa Ajili ya Masomo

Watoto na vijana wengi barani Afrika wana akili na bidii sana. Lakini wazazi wao hawana uwezo wa kulipa karo zao za shule. Kanisa lako linaweza kutaka kushughulikia hitaji hilo kwa kuunda utaratibu wa ufadhili wa masomo ili kufadhili wanafunzi wanaostahili kwa kuwalipia karo za shule. Hii itawawezesha kufanikisha ndoto zao na kupata ujuzi wanaohitaji ili kujiendeleza wao na jamii kwa ujumla.

### Maendeleo ya Vijana

Vijana wa Afrika wanawakilisha mustakabali wa bara hili. Lakini cha kusikitisha ni kwamba wengi wao wanajiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya na tabia nyingine zenye uharibifu. Kanisa lako linaweza kushughulikia jambo hili kwa kuweka programu za vijana ili kutoa shughuli chanya kwa vijana. Programu hizi zinaweza kuwa pamoja na kwaya, timu za michezo, na shughuli zingine zinazofaa. Watumishi wanaweza kutumia shughuli hizo kama jukwaa la kufundisha kanuni za jinsi ya kuwa mwanaume na mwanamke mcha Mungu. Programu hizi pia zitawapa watendakazi fursa ya kufikisha injili kwa vijana na kuwaongoza kwa Kristo.

**Elimu ya Watu Wazima**

Watu wazima wengi kote barani Afrika wamekosa fursa ya elimu sahihi ya msingi au sekondari. Kanisa lako linaweza kushughulikia hitaji hili kwa kuanzisha programu za elimu ya watu wazima. Programu hizi zinaweza kuwa ni pamoja na:

*Mafunzo ya kusoma na kuandika*. Kanisa linaweza kuanzisha darasa endelevu lenye kufundisha watu wazima jinsi ya kusoma na kuandika. Kujifunza stadi hizi kutaongeza heshima kwao na kutawasaidia kupata kazi bora zaidi. Na zitaboresha maisha ya jamii nzima. Pia zitawatayarisha kusoma Biblia na vitabu vingine vya Kikristo ambavyo kanisa linaweza kutaka kuwaandalia. Kanisa linaweza pia kutaka kuanzisha darasa la kuwasaidia watu wazima kujifunza lugha ya pili kama vile Kiingereza, Kifaransa, au Kireno.

*Uboreshaji wa ndoa*. Ndoa nyingi barani Afrika hazina ubora, na kiwango cha talaka kinaongezeka. Wanandoa wanahitaji kujua kanuni za kibiblia za ndoa. Hii ni kweli ndani na nje ya kanisa. Ili kushughulikia hitaji hili, unaweza kuandaa darasa au semina ya kuimarisha ndoa na kuwakaribisha watu wote. Washirika wako wanaweza kualika rafiki zao kujiunga na hilo darasa. Hii itawasaidia kugundua kusudi la Mungu kwa ajili ya maisha yao na ndoa zao. Wakati wa darasa, injili inatakiwa kuwasilishwa, na wanandoa wanapaswa kupewa fursa ya kumpokea Kristo kama Mwokozi wao.

*Kanuni za biashara na ujasiriamali*. Ikiwezekana, kanisa lako linaweza kutaka kuanzisha darasa la kuwafundisha wanafunzi watu wazima jinsi ya kuanzisha na kujenga biashara zao wenyewe. Darasa linaweza pia kufundisha kanuni za kibiblia za biashara na uwakili, ikijumuisha umuhimu wa maadili thabiti ya kazi.

*Mbinu bora za kilimo*. Katika mazingira ya mashambani, kanisa linaweza kutaka kuanzisha darasa au kuendesha semina ya kila mwaka kuhusu mbinu bora za kilimo. Mtaalamu wa masuala ya kilimo anaweza kuombwa kufundisha semina hiyo.

**Mipango Mingine**

Hizi ni baadhi tu ya njia chache ambazo kanisa lako linaweza kutumia kuhudumia jumuiya yake. Roho Mtakatifu anaweza kukuongoza kuanzisha mipango na miradi mingine ya huduma ambayo haijatajwa hapa.

## KUHAMASISHA KANISA

Unaweza kuwa unauliza, "Ninawezaje, kama mchungaji wa Kipentekoste, kuweka mipango hii katika vitendo?" Kama kiongozi wa kanisa aliyechaguliwa na Mungu, utahitaji kuongoza. Lazima uanzishe maono, uendeleze mpango, na usimamie utekelezaji wa mpango. Ili kuunda mpango mzuri wa utekelezaji, zingatia yafuatayo:

### Angalia Haja

Yesu aliona uhitaji kwanza. Aliwaona watu waliokuwa wakiteseka karibu Naye "akawahurumia, kwa sababu walikuwa wametaabika na wanyonge, kama kondoo wasio na mchungaji" (Mt. 9:36). Kisha akatekeleza mpango. Aliwahimiza wanafunzi Wake hivi: "Kwa hiyo, mwombeni Bwana wa Mavuno apeleke watenda kazi katika shamba lake la mavuno" (mst. 38). Wakati mwingine Yesu aliwaambia, "Fumbueni macho yenu mtazame mashamba! Yameiva kwa mavuno" (Yoh. 4:35).

Kumbuka kwamba kabla ya kutekeleza mpango wako wa kushiriki katika jamii, wewe kama Yesu lazima kwanza uone hitaji. Ukishafanya hivyo, unaweza kuwasaidia washirika wa kanisa lako kufanya vivyo hivyo.

### Tambua Mapenzi ya Mungu

Mara tu unapoona mahitaji mengi katika jumuiya yako, ni vizuri umuulize Mungu hivi: "Ni mahitaji gani kati ya haya, ninayotaka kanisa letu kushughulikia?" Ikiwa utafungua moyo wako kwa Roho Mtakatifu, atakuongoza. Ataweka mzigo unaoendelea kukua juu ya moyo wako na kukuonyesha mahitaji ambayo anataka kanisa lako litimize.

### Rahisisha

Unapoanza kutengeneza mpango wa utekelezaji wa mpango wako mpya, ni muhimu kurahisisha mambo - angalau hapo mwanzoni. Kwa kawaida, utataka kuanza na mradi mdogo unaoweza kufanyika bila shida sana. Washirika wa kanisa wanapoona mafanikio ya mradi huu mdogo, watatiwa moyo kupokea miradi mikubwa na kabambe zaidi.

### Chukua Hatua

Roho anapoonyesha kwamba wakati unafaa, chukua hatua mara moja na kuanzisha programu, ukimtumaini Mungu kukuongoza hatua kwa hatua.

**Ishike Kiroho**

Unapoliongoza kanisa kujali mahitaji ya kimwili ya watu, lazima uhakikishe kwamba hupuuzi mahitaji yao ya kiroho. Kristo lazima abaki wa muhimu katika kila mpango na shughuli. Wewe na watenda kazi wako lazima muombe mara kwa mara, mkihakikisha kwamba mnabaki mmejawa na Roho Mtakatifu.

**Himiza Ushiriki Kanisa Lote**

Haupaswi kujaribu kufanya kazi peke yako. Badala yake, hamasisha washirika wa kanisa lako kushiriki. Kila mtu anaweza kushiriki kwa namna fulani. Kama mchungaji, lazima uwahimize watu kutoa kwa ukarimu kusaidia mpango huo, na lazima uwatie moyo kujitolea wakati na nguvu zao. Kama mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima, tambua karama za washirika walizopewa na Mungu, na kisha uwatie moyo kutumia karama zao kubariki kazi ya Mungu.

**Mwamini Mungu Kutoa Yanayohitajika**

Mwisho, ni vizuri umwamini Mungu kukidhi mahitaji yako. Usingoje hadi kila kitu kikae sawa ndipo uanze kuchukua hatua. Ukifanya hivi, huenda usianze. Kama alivyofanya yule mchungaji mwanzoni mwa sura hii, lazima ufanye uwezavyo na kile ulicho nacho, kisha umtumaini Mungu kufanya mengine. Ikiwa utaendelea kuwa mtii kwa Mungu na mwaminifu kwa maono ambayo amekupa, atakidhi mahitaji yako yote (Flp. 4:19).

~ Sura ya 39 ~

# Kupanda Makanisa Mapya

Charles alikuwa mwanafunzi wa huduma katika shule ya Biblia huko Afrika Mashariki. Siku moja, alimwambia mwalimu wake, “Kabla sijafa, nataka kuanzisha makanisa mia moja kati ya kabila langu.” Mzigo huu wa upandaji kanisa ulizaliwa moyoni mwake alipokuwa akisafiri na timu ya umisheni kutoka shule ya Biblia. Timu ilikuwa imeanzisha makanisa mapya kadhaa katika maeneo ya mbali, miongoni mwa makundi ya watu ambao hawajafikiwa. Wakati wa safari, Charles alijifunza mbinu chache za kivitendo za upandaji makanisa mapya.

Assemblies of God walipokuja kwa mara ya kwanza katika nchi yake, walianza kazi yao kati ya watu wake. Lakini hata baada ya miaka mingi, yalikuwepo makanisa machache tu kati yao. Alihitimu kutoka shule ya Biblia miaka kumi na sita iliyopita. Leo, Charles ameanzisha zaidi ya makanisa thelathini yeye peke yake. Kupitia ushawishi wake kama kiongozi wa dhehebu, amepanda takriban makanisa hamsini zaidi bila kujihusisha moja kwa moja, na kufikisha jumla ya makanisa mapya themanini. Sasa, Charles amelifanya upya lengo lake. Anaahidi hivi: “Ninakusudia kuanzisha makanisa mapya 200 katika miaka kumi ijayo!”

Kama ambavyo wanawake wenye afya nzuri wanavyozaa watoto, makanisa yenye afya hupanda makanisa mengine. Kila kanisa linapaswa kuwa kanisa lenye

kupanda makanisa. Sura hii itaangalia kipaumbele cha kimaandiko cha upandaji kanisa, mifano ya upandaji kanisa, kanisa kama jumuiya ya kitume, makanisa ya kimishenari yanayowezeshwa na Roho, kanuni za makanisa asilia, na njia za vitendo kwa mchungaji wa Kipentekoste kuanzisha makanisa.

## KIPAUMBELE CHA MAANDIKO

Yesu alisema, "Nitalijenga kanisa langu" (Mt. 16:18). Pia aliagiza hivi: "Nendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (28:19). Mtu fulani amesema, "Yesu hakutuagiza tupande makanisa. Alituagiza tufanye watu kuwa wanafunzi." Lakini, ona jinsi ambavyo hayo maneno Yesu yanavyohusiana. Je, mtu anawezaje kufanya watu kuwa wanafunzi bila kupanda kanisa, na mtu anawezaje kupanda kanisa la kweli bila kufanya watu kuwa wanafunzi? Kuwafikia waliopotea bila kuwaweka kanisani ni sawa na kupata mtoto na kumwacha msituni. Upandaji kanisa ni muhimu kwa kudumu kwa kazi na maendeleo ya waamini.

Mitume, wahudumu, na wafanyakazi wa kanisa katika Agano Jipya walikuwa makini kuhusu kuanzisha makanisa. Petro, Yohana, Filipo, watu toka Kipro na Kirene, Barnaba, Paulo, Yohana Marko, Sila, Luka, Timotheo, Prisila, Akila, Gayo, Aristarko, Erasto na Tito: wote hao walihusika katika upandaji makanisa. Wanaume na wanawake hawa walikuwa wakifuata amri ya Kristo ya kufanya wanafunzi, na kwa kufanya hivyo, walianzisha makanisa. Kama wachungaji wa Kipentekoste, lazima tufanye vivyo hivyo.

## MIFANO YA KUPANDA KANISA

Wakati fulani mchungaji kijana mmoja alizungumza na kiongozi wake wa jimbo kuhusu kuanzisha kanisa katika mji fulani. Kiongozi huyo akajibu, "Mungu hajaniambia nipande kanisa pale, lakini ukitaka kufanya hivyo, endelea. Ukifanikiwa, tutajua yalikuwa mapenzi ya Mungu. Ikishindikana, tutajua haikuwa hivyo." Akijisikia kuongozwa na Roho, kijana huyo alikwenda hapo na kuanzisha kanisa lake la kwanza. Tangu wakati huo, amepanda zaidi ya makanisa ishirini.

Kotekote barani Afrika, wanaume na wanawake wengi, walio na wito kutoka kwa Mungu wa kuanzisha kanisa, wamefanya vivyo hivyo. Wamefanikiwa kupanda makanisa peke yao, bila msaada mwingi kutoka nje. Hii inaweza kuitwa njia ya dharura - "kuzama au kuogelea". Ni kama baba anayemfundisha mwanawe kuogelea kwa kumtupa kwenye dimbwi lenye kina kirefu bila kumpa maagizo wala mafunzo ya awali. Ingawa makanisa mengi yameanzishwa kwa njia hii, sio

njia bora. Mpanda kanisa anathibitisha ukweli huu. Anashuhudia hivi: "Kwa hakika nilijifunza mengi kutoka kwa kanisa hilo la kwanza. Jambo moja nililojifunza ni kwamba sitaki kamwe kuanzisha kanisa lingine bila timu ya watumishi wenzangu waliojitoa."

Kielelezo cha timu ya kusaidia upandaji kanisa kina faida nyingi. Hebu fikiri: badala ya kutuma timu ya watu wawili kupanda kanisa jipya, unatuma kumi au zaidi. Timu inaweza kuwa na mchungaji na mwenzi wake, viongozi wa ibada, wanandoa wazee ili kuwepo kwa ajili ya kutoa uzoefu, na watu wa kufanya kazi na watoto na vijana. Kundi kama hilo lingetoa msaada kihisia na kifedha kwa wapanda kanisa. Mtazamo wa timu ya kusaidia upandaji kanisa inaweza kusaidia kanisa kufikia ukomavu kwa haraka zaidi. Na litakuwa kanisa ambalo lenyewe linapanda makanisa mengine upesi zaidi.

Kielelezo cha timu ya kusaidia upandaji kanisa kinaweza kuja kwa namna tofauti. Kanisa mama linaweza kuzaa kanisa tawi kwa kutuma mchungaji mshiriki na baadhi ya watu wake kwa jamii iliyo karibu. Kisha linaweza kutoa huduma na ushauri kwa kanisa jipya hadi litakapoanzishwa. Paulo na kikundi chake cha kitume cha wamishenari ni mfano bora wa timu ya kusaidia ambayo ilisafiri kwenda kwa watu ambao hawajafikiwa na kupanda makanisa katika sehemu ambapo Kristo hakuwa anajulikana.

Wengine wameunda mifumo ya kusaidia wapanda kanisa kwa mwaka mmoja au miwili wanapofanya kazi ya kupanda kanisa jipya. Baada ya hapo, usaidizi wao unapungua na hatimaye kukoma huku waamini wapya wakikuzwa na kuwa wanafunzi waliojitoa, watakaotoa zaka ili kuendeleza kazi. Mifano ya upandaji kanisa ni:

- *Uzazi:* Kanisa mama linapanda kanisa tawi kama ilivyoelezwa hapo juu.
- *Uanzishwaji:* Wapanda makanisa waanzilishi wanatumwa katika maeneo mapya ili kupanda makanisa.
- *Kuhamia:* Kundi linalohudhuria kanisa kutoka eneo la mbali au tamaduni tofauti huomba ruhusa kutoka kwa kanisa ili "kuondoka" na kuanzisha kanisa jipya.
- *Vikundi:* Vikundi vidogo vinavyokutana katika sehemu nyingine ya jiji vinapanuka na kuwa makanisa.
- *Makanisa yanayoshirikiana:* Sehemu, jimbo, au makanisa ya kitaifa hushirikiana kupanda makanisa.

- *Shule ya Biblia.* Shule za Biblia huhamasisha wanafunzi kupanda makanisa mapya.
- *Nyingine:* Njia zingine za ubunifu zinaweza kuendelezwa ili kupanda makanisa.

Njia yoyote atakayotumia mtu, upandaji kanisa si rahisi. Inahitaji kujitoa kutoka kwa mchungaji mpya, familia yake, na timu yake kuanzisha kazi mpya. Adui hapendi makanisa mapya yaanzishwe kwa sababu yanaingilia eneo lake (Mt. 12:29). Atapigana kupinga upandwaji wa kanisa na kanisa litakalo-ota hapo (Efe. 6:12). Lakini, mpanda kanisa la Kipentekoste ajue kwamba ana aliye Mkuu zaidi anayeishi ndani ili kumsaidia kushinda ushindi (1 Yoh. 4:4).

Kama mchungaji mwingine yeyote wa Kipentekoste, lazima uombe na kupanga jinsi unavyoweza kuliongoza kanisa lako kuanzisha makanisa mapya, iwe karibu, katika eneo ambalo halijafikiwa la nchi yako mwenyewe, au katika nchi nyingine barani Afrika na duniani kote.

## JUMUIYA YA KITUME

Kanisa lenye afya ni kanisa linalotoa. Kanisa lenye afya njema ni kanisa lenye mafundisho sahihi. Kanisa lenye afya ni kanisa linalofanya umisheni. Kanisa lenye afya ni kanisa linaloshuhudia. Kanisa lenye afya huzaa makanisa mengine yenye afya. Lakini kanisa moja huzaaje lingine? Je, wewe kama mchungaji wa Kipentekoste unawezaje kwenda kuanzisha kanisa lingine?

Kanisa la Antiokia ni mfano bora wa kanisa lenye afya, lililozingatia umisheni. Kanisa lilianzishwa na walei wa Kiyahudi kutoka Yerusalemu, Kipro, na Kirene ambao walishirikisha wengine imani yao kwa ujasiri, pamoja na watu wa tamaduni zingine (Mdo. 11:19-20). Walikuwa kanisa lililotiwa nguvu na Roho (mst. 21). Walikuwa na uongozi mzuri (mst. 22-26). Walikuwa kanisa linalotoa (mst. 27-30), lenye kuomba, kufunga na kumwabudu Mungu (13:2).

Hivyo, Roho Mtakatifu alipowaambia, "Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi [utume] niliyowaitia," walifanya hivyo (Mdo. 13:1-2). Kwa hiari walitoa watu wao bora zaidi waondoke kanisani kwao na kwenda kufanya kile ambacho Mungu alikuwa anawaita kufanya. Waliwatuma Barnaba na Sauli kama wapanda kanisa wa kimishenari (mst. 3-4).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, Mungu anataka kukutumia "kuwatayarisha watu wake kwa ajili ya kazi za huduma" (Efe. 4:12). Anataka kukutumia kupanda makanisa hapo karibu, katika nchi yako, na duniani kote.

Mungu amekupa njia na fursa ya kutengeneza katika kanisa lako utamaduni wa umisheni na upandaji kanisa. Unaweza kufanya hivi kwa kufundisha na kuhamasisha maombi ya kimishenari, kuabudu, uongozi, utoaji, uinjilisti, na kazi ya pamoja. Katika mazingira kama haya, Mungu atawaita na kuwawezesha watu wake kwenda nje na kuhubiri injili na kupanda makanisa mapya.

Unapaswa kuwaelekeza watu wako watoe kwa ukarimu kusaidia kazi ya Mungu, na umruhusu Mungu afanye vivyo hivyo kwako pia. Mungu anaweza kukutaka utoe washirika wako bora sana wa kanisa kufanya kazi ya kupanda kanisa. Moja ya zawadi kubwa mno unayoweza kumpa Mungu ni kuwainua watu katika karama zao walizopewa na Mungu na kisha kuwaachilia katika huduma. Barnaba alisaidia kumwinua Paulo (Mdo. 9:26-27; 11:25). Kisha alimfungua afuatilie huduma yake mwenyewe na kuendeleza timu yake ya kimishenari (15:36-41).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, jumuiya ya mitume unayoikuza katika kanisa lako itafanya kazi yenye kuvuta wengine, kama sumaku. Jumuiya ya kitume ni kundi la watu waliojikita katika kutimiza Agizo Kuu nyumbani na duniani kote. Watu wanapomwona Roho wa Mungu akitembea katika kanisa lako, watataka kuwa sehemu ya kile kinachofanyika.

Katika Matendo 6, mzozo ulitokea kuhusu kulisha baadhi ya wajane waliotelekezwa. Mitume walisuluhisha mzozo huo kwa kuteua wanaume saba waliojazwa na Roho ili kutimiza hiyo kazi. Kitendo hiki kiliwafurahisha watu ndani na nje ya kanisa. Kwa hiyo, “neno la Mungu likaenea [na] idadi ya wanafunzi katika Yerusalemu ikaongezeka kwa kasi, na idadi kubwa ya makuhani ikaitii ile imani” (mst. 7). Unapokuza kanisa lako kuwa jumuiya ya mitume yenye upendo, watu watavutwa kwa Kristo na utume Wake. Ukuaji wa kanisa na upandaji kanisa utatiririka kutoka katika mazingira kama hayo.

## MAKANISA YA WAMISHENARI YANAYOWEZESHWA NA ROHO

Kitabu cha Matendo kinasimulia hadithi ya kutia moyo ya kutiwa nguvu kwa kanisa la Yerusalemu. Roho Mtakatifu alipokuja na kuwajaza wale wanafunzi mia na ishirini (120), umati uliona jambo la ajabu. Wanafunzi walianza kunena kwa lugha kama Roho alivyowawezesha (2:1-4). Ilikuwa ni kutimizwa kwa ahadi ya Yesu katika Matendo 1:8. Kwa mshangao, umati ukawakaribia wanafunzi. Hili

lilimpa Petro nafasi nzuri ya kutangaza habari njema kwa nguvu za Roho Mtakatifu, na kusababisha watu elfu tatu (3,000) waje kwa Bwana.

Mara nyingi Mungu hutumia ishara na maajabu ili kuchochea shauku ya kusikia ujumbe wa injili. Ni vyema kutambua kwamba katika vitabu vya Injili na Matendo, miujiza mingi ilifanyika nje ya mahali pa ibada kuliko ndani. Katika Matendo, mara nyingi muujiza uliweka msingi wa kutangaza injili. Hilo lilitokea huko Yerusalemu, Petro akihusika (Mdo. 2), huko Kipro, Barnaba na Paulo wakihusika (13:4-12), huko Efeso, Paulo na Sila wakihusika (16:11-40), na katika nyakati nyingine nyingi (9:32-35; 9:36-43; 10:1-11:18; 14:1-7; 14:8-20; 19:1-20:1).

Mungu anataka wale walio nje ya kanisa waone nguvu na upendo Wake unaofanya miujiza, na wageuke kumfuata. Usiache muujiza ukapotea. Wakati wowote Mungu anapofanya muujiza, utumie kama fursa ya kuwaambia watu kuhusu Yesu.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake, “Kama vile Baba alivyonituma mimi, nami nawatuma ninyi” (Yoh. 20:21). Lakini Baba alimtumaje Yesu? Alimtuma Mwanawe kuhudumu katika nguvu za Roho. Yesu alipoanza huduma yake, alitangaza hivi: “Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa” (Lk. 4:18-19). Yesu alihudumu katika nguvu za Roho (Mdo. 10:38), na aliwatuma wanafunzi Wake kufanya vivyo hivyo (Lk. 24:46-49; Mdo. 1:8).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima uwezeshwe na Roho Mtakatifu, na lazima uendeleze kanisa lako kimakusudi liwe taasisi ya kimishenari inayowezeshwa na Roho. Tena, unapaswa kupanda makanisa ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho. Kanisa la kimishenari lililowezeshwa na Roho ndilo aina ya kanisa Yesu alilopanda. Na ndiyo aina ya kanisa tunalosoma juu yake katika kitabu cha Matendo.

Yesu alieleza kiini cha kanisa hili katika Matendo 1:8, ambapo alisema, “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi”. Kwa hivyo, kanisa la kimishenari linalowezeshwa na Roho lina sifa mbili kubwa: Washirika wake wanawezeshwa na Roho Mtakatifu, na wamejitoa kutimiza utume wa Mungu. Ni kanisa ambalo

hupanda makanisa mengine ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho, na ni kanisa ambalo limejitoa kufikia makundi ya watu ambao hawajafikiwa kote nchini na duniani kote. Tunatakiwa kuendeleza kanisa la aina hii, na ndiyo aina ya makanisa tunayopaswa kupanda.

## KANUNI ZA KANISA LA KIENYEJI

Ulimwenguni kote, kanisa la Kipentekoste limekua kwa kasi ya kushangaza. Kinachochangia ukuaji huu ni kujitoa kwake kwa kile kinachojulikana kama "kanuni za kanisa la kienyeji." Hii ni imani kwamba kila kanisa jipya lazima liweze kujitegemeza, kujitawala, na kujitangaza haraka sana. Wewe na kanisa lako mnapotoka kupanda makanisa, mnapaswa kuhakikisha kwamba yanakua na kuwa makanisa yanayoweza kujikimu, kushughulikia mambo yao wenyewe, kuwafikia waliopotea, na kuweza kupanda upesi makanisa mengine ya kimishenari yaliyowezeshwa na Roho.

Mtoto mchanga anapokuja katika familia, wazazi hushughulikia kila hitaji lake. Lakini huyo mtoto anapokua na kukomaa, wazazi humfundisha mtoto jinsi ya kujitegemea. Mtoto hufundishwa jinsi ya kuishi na, baada ya muda, anapewa jukumu zaidi na zaidi katika kujitegemea. Mwishowe mtoto anapokuwa mtu mzima, wazazi humwachilia awe mshiriki wa jamii anayejitegemea na anayechangia.

Ni kama katika kupanda kanisa jipya. Mwanzoni, kanisa mama linatumia muda mwingi na rasilimali nyingi katika kutunza kanisa tawi. Linaweza kusaidia kanisa jipya kwa uongozi, fedha, na watumishi. Lakini, hilo kanisa jipya linatarajiwa kukua na kukomaa. Kusudi ni kwamba mapema tu nalo liwe mshiriki anayejitegemea na kuchangia katika ufalme wa Mungu.

## NINI KIFUATACHO?

Pengine unajiuliza, “Nifanye nini ili kutekeleza kanuni hizi za upandaji kanisa katika huduma yangu mwenyewe na katika uhai wa kanisa langu? Ninawezaje kukuza kanisa langu kuwa chombo chenye ufanisi cha upandaji kanisa?” Fikiria kuchukua hatua zifuatazo:

### Omba

Anza na maombi ya dhati. Mwombe Mungu kwa dhati akupe maono ya upandaji kanisa. Mwambie Yesu, Bwana wa Mavuno, “Fumbua macho yangu niyatazame mashamba yaliyoiva, tayari kuvunwa” (Yoh. 4:35). Ombea jumuiya

zinazokuzunguka ambazo hazina kanisa la kimishenari lililowezeshwa na Roho (Mt. 9:38). Lakini usiishie hapo. Angalia mbali zaidi kwa watu na maeneo ambayo hayajafikiwa katika nchi yako ambako kuna ushuhuda mdogo wa Injili au hakuna kabisa. Na usisahau kutazama mataifa. Unaposali, mwulize Mungu, "Je, ungetaka tufikishe habari njema za Kristo kwa watu gani miongoni mwa hawa? Na, wapi katika maeneo haya?"

**Jitolee**

Kisha, jikabidhi mwenyewe na kanisa lako kwa Mungu na kwa utume Wake. Amua mara moja na kwa wakati wote kwamba kanisa lako litakuwa kanisa zuri katika shughuli za upandaji kanisa.

**Wekeza kwa Watu**

Mara tu unapojitoa kwa upandaji kanisa, anza kuwakuza washirika wa kanisa lako kuwa wanafunzi wa Kristo waliojitoa kikamilifu. Hubiri, fundisha, na zungumza mara kwa mara kuhusu utume wa Mungu na kuhusu agizo la Kristo la kupanda makanisa. Shirikisha maono ya upandaji kanisa kwa viongozi kanisani mwako na katika kusanyiko lako. Unapofanya hivyo, wape viongozi watarajiwa nafasi za kuhudumu na kukuza karama zao walizopewa na Mungu.

**Tengeneza Timu**

Kwa wakati ufaao, unda timu yako ya upandaji kanisa. Chagua ni nani atakayehudumu kama mchungaji wa hilo kanisa jipya. Pia, chagua wale watakaofanya kazi na mchungaji kwenye timu ya upandaji kanisa. Hakikisha kwamba kila mhusika anajua wajibu wake maalum. Pia, hakikisha kwamba wahusika katika timu yako wamewezeshwa na Roho Mtakatifu. Zaidi ya hayo, ni muhimu utengeneze timu ya usaidizi itakayosalia kanisa la nyumbani ili kuunga mkono kanisa jipya kwa kutia moyo, maombi, na fedha.

**Tengeneza Mpango**

Sasa, pamoja na timu yako, anza kutayarisha mpango mapema. Katika mpango wako, jitahidi kujibu maswali yafuatayo: "Tupande kanisa jipya lini na wapi? Nani atahusika? Tutafanya mambo gani mahususi?" Ni vizuri huo mpango wako ujumuishe bajeti inayoelezea ni kiasi gani cha pesa na vifaa gani vitahitajika na jinsi ya kupatikana kwake.

**Ingiza Kwenye Utendaji**

Mara baada ya kuomba na kukuza na kuandaa mpango wako, piga hatua haraka kutekeleza mkakati wako. Tenda kwa imani, ukiamini kwamba Roho wa Bwana atakutia nguvu na kuutia mafuta ushuhuda wako. Mwamini Mungu kuthibitisha neno unalotangaza kwa miujiza, ishara na maajabu. Watu wanapookolewa, hakikisha kwamba wao pia wamejazwa na Roho na kufundishwa mambo ya msingi ya kumtumikia Kristo. Wahamasishe mara moja wazifikie familia zao na rafiki zao.

**Tathmini**

Mwisho: mara tu unapomaliza shughuli zako za upandaji kanisa, kaa na timu yako na kwa pamoja fanyeni tathmini ya kazi iliyofanyika. Uliza maswali kama: "Nini tulichofanya vizuri? Nini kingeweza kufanyika vizuri zaidi?" Siku zote kutakuwa na mambo ambayo hayakwenda sawa, lakini usivunjike moyo. Tumia kile ulichojifunza kuimarisha shughuli yako ya upandaji kanisa, itakayofuata.

---

Kuendeleza kusanyiko lako kuwa chombo cha upandaji kanisa hakutasaidia tu kuendeleza utume wa Kristo duniani, kutaleta uamsho pia kwa kanisa. Kusanyiko lako litafurahi kwamba wao ni sehemu ya kuanzisha makanisa mapya na kuona watu wakimjia Yesu. Kila mchungaji wa Kipentekoste anapaswa kujitoa kwa furaha kuanzisha makanisa mapya.

# ~ Sura ya 40 ~

# Kutengeneza Mpango wa Utume wa Kanisa la Mahali Pamoja

Wakati ulikuwa umefika wa Yesu kudhihirisha Yeye ni nani na kwa nini alikuwa amekuja. Ili wanafunzi Wake kumi na wawili waendelee na utume Wake baada ya Yeye kuondoka, wangehitaji kuelewa kweli hizi. Alipofika mahali pa faragha nje ya jiji la Kaisaria Filipi, Yesu akaketi pamoja nao. Akawageukia, akawauliza, Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani? Wanafunzi wakajibu mmoja baada ya mwingine, "Wengine husema wewe ni Yohana Mbatizaji. Wengine wanasema Eliya. Na bado wengine hudai kwamba wewe ni Yeremia au mmoja wa manabii."

Kisha Yesu akawauliza wao moja kwa moja, "Je! Ninyi mnasema mimi ni nani?" Kwa kufunuliwa na Mungu, Petro alipaza sauti na kusema: "Wewe ndiwe Masiya, Mwana wa Mungu aliye hai!"

Yesu akamtazama Petro machoni na kujibu, "Heri wewe Simoni mwana wa Yona, kwa kuwa Baba yangu aliye mbinguni amekufunulia hili." Kisha Yesu akaongeza, "Nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, na nguvu zote za kuzimu hazitaweza kupingana nalo" (rej. Mt. 16:13-20).

Basi, Yesu aliwafunulia wanafunzi Wake Yeye ni nani: Alikuwa Masiya aliyeahidiwa, Mwana wa Mungu. Pia aliwafunulia kwa nini alikuja: alikuwa amekuja kulijenga Kanisa Lake. Alizidi kuweka wazi kwamba Kanisa alilokuwa akilijenga lingekuwa zaidi ya taasisi ya kibinadamu; ni vuguvugu iliyoagizwa na Mungu. Lingekabiliwa na upinzani mkali wa kishetani, lakini mwishowe lingeshinda.

## KUUNGANISHWA NA UTUME WA MUNGU

Kusudi kuu la Bwana wetu kwa Kanisa Lake ni kutangaza habari njema ya wokovu ndani ya Kristo kwa dunia iliyoharibika, kabla ya kurudi Kwake. Yesu alisema hivi: "Injili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; ndipo ule mwisho utakapokuja" (Mt. 24:14). Kama hii ni kweli, kila mchungaji wa Kipentekoste analazimika kuliongoza kanisa lake kushiriki kikamilifu katika utume wa Mungu. Sura hii itachunguza jinsi unavyoweza kukamilisha kazi hii kubwa ya Kanisa.

**Maandalizi Binafsi**

Kabla ya kujaribu kuunganisha kanisa lako na utume wa Mungu, lazima ujitayarishe kwa kazi hiyo. Unaweza kufanya hivyo kwa njia zifuatazo:

*1. Kuelewa utume wa Mungu.* Kwanza, lazima lengo lako liwe kupata ufahamu dhahiri wa utume wa Mungu. Basi inabidi ujue utume wa Mungu ni nini na jinsi unavyohusiana na Kanisa. Utume wa Mungu ambao wakati mwingine huitwa *missio Dei*, ndio mada inayounganisha ya Maandiko. Ni mpango wa Mungu kukomboa na kuwaita kwake watu kutoka katika kila kabila, lugha na taifa duniani (Uf. 5:9; 7:9). Ni mpango wa Mungu kwamba katika Kristo, uzao wa Ibrahimu, "watu wote wa dunia watabarikiwa" (Mwa. 12:3; 22:18; Gal. 3:16). Biblia ni hadithi ya Mungu akitenda kazi katika historia ili kutimiza huo utume.

*2. Kuelewa jukumu la kanisa*. Zaidi ya hayo, kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, lazima uelewe jukumu kuu la Kanisa katika kutimiza utume wa Mungu. Yesu aliunganisha Kanisa na utume wa Mungu alipowaagiza wafuasi wake kwa kusema, "Nendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi" (Mt. 28:19-20; taz. Mk. 16:15; Lk. 24:46-48; Yoh. 20:21; Mdo. 1:8). Amri hii ya Yesu inajulikana kama Agizo Kuu. Umisheni sio mpango wa Kanisa tu, ni kusudi la Kanisa.

*3. Kukubali wajibu wa kichungaji.* Mwisho, kama mchungaji wa kweli wa Kipentekoste, kubali wajibu wako wa kuhamasisha kanisa kushiriki katika utume wa Mungu. Ni vizuri uwe yule "mtumishi mwaminifu na mwenye busara" ambaye bwana amemtuma kutunza nyumba yake "ili kuwapa chakula kwa wakati wake" (Mt. 24:45). Kumbuka, siku moja utatoa hesabu kwa Mungu kwa jinsi ambavyo umelisimamia kanisa la Kristo (Lk. 16:2).

**Mfano wa Kibiblia**

Biblia inatupa mfano wa jinsi kanisa la kweli la Kipentekoste linavyopaswa kuonekana. Linapaswa kuwa kanisa la kimishenari. Kanisa la kimishenari ni kanisa ambalo limejitoa kuendeleza utume wa Mungu duniani. Kanisa la Antiokia ya Shamu lilikuwa kanisa kama hilo (Mdo. 11:19-20; 13:1-4). Luka anaiunganisha hiyo hadithi ya kanisa hili katika Matendo kama mfano wa kudumu wa jinsi kanisa linavyoweza kuunganika vema na utume wa Mungu. Ni mfano wa jinsi kanisa la Kipentekoste linavyopaswa kufanya kazi leo. Uchunguzi wa vifungu hivi viwili unaonyesha sifa saba za kanisa la kweli la kimishenari.

*1. Uwepo na nguvu za Roho.* Kanisa la kimishenari la kweli litathamini uwepo na nguvu za Roho Mtakatifu. Biblia inasema kuhusu kanisa la Antiokia, "Mkono wa Bwana ulikuwa pamoja nao" (Mdo. 11:21). Hii ni njia nyingine ya kusema kwamba Roho Mtakatifu alikuwa akifanya kazi kwa nguvu katikati yao (rej. 2 Waf. 3:15; Eze. 3:14). Kama matokeo ya kazi ya Roho ndani na kupitia kwa waamini wa Antiokia na mtazamo wao katika kuwapata waliopotea, "idadi kubwa ya watu waliamini na kumgeukia Bwana."

*2. Uongozi wa kumcha Mungu, uliotiwa mafuta na uliojaa imani.* Kanisa la kimishenari la kweli linaongozwa na viongozi wacha Mungu, waliotiwa mafuta na Roho, waliojaa imani kama vile Barnaba na Sauli (Mdo. 11:22-26). Biblia inasema kwamba Barnaba alikuwa "mtu mwema, amejaa Roho Mtakatifu na imani" (mst. 24). Sauli, ambaye pia aliongoza kanisa la Antiokia, naye alikuwa amejaa Roho Mtakatifu na imani (13:9; taz. 9:17-18).

*3. Mtazamo wa nje wa maono*. Ukweli ni kwamba kanisa la kimishenari linawafikia wakazi wa jiji au kijiji chake kwa makusudi. Hivi ndivyo kanisa la Antiokia lilivyofanya. Zaidi ya hayo, mawasiliano yao yalikuwa ya makabila mengi, yakiwalenga Wayahudi na Wasiokuwa Wayahudi (Mdo. 11:19-21). Kanisa la Antiokia pia lilipanda makanisa mengine katika eneo hilo (15:41). Tena walituma wamishenari kwa mataifa (13:1-4). Kisha wakakaa pamoja na wale waliowatuma (14:27).

*4. Tangazo la ujasiri*. Kanisa la kweli la kimishenari litatangaza kwa ujasiri “habari njema za Bwana Yesu Kristo” kama lilivyofanya kanisa la Antiokia (Mdo. 11:20). Kutangaza kwa ujasiri injili ilikuwa tabia ya wanafunzi katika kitabu chote cha Matendo (ling. 8:4-5; 16:30-32; 28:31).

*5. Mafunzo ya utaratibu yanayolenga utume.* Kanisa la kimishenari la kweli litawafundisha washirika wake kuhusu utume wa Mungu kwa mpangilio. Biblia inasema, “Kwa muda wa mwaka mzima Barnaba na Sauli wakakutana na kanisa na kufundisha watu wengi sana” (Mdo. 11:26). Bila shaka walifundisha mambo ya msingi ya maisha ya Kikristo. Pia, tukitazama jinsi kanisa la Antiokia lilivyofanya kazi, ni wazi kwamba walifundisha kuhusu utume wa Mungu na jinsi ambavyo Wakristo wangeweza kushiriki kikamilifu katika utume huo.

*6. Utendaji huru wa karama za kiroho.* Kanisa la kimishenari la kweli litahimiza utendaji wa karama za kiroho katika mikusanyiko yake. Kanisa la Antiokia lilihimiza udhihirisho kama huo (rej. Mdo. 11:27-28). Huko, Wakristo walimtegemea Roho wa Mungu awaongoze katika mapenzi ya Mungu. Udhihirisho wa karama ya unabii katika kanisa ulichochea kutumwa kwa Barnaba na Sauli kama wamishenari kwa Mataifa (13:2).

*7. Ukarimu unaoongozwa na Roho.* Kanisa la kimishenari la kweli ni kanisa karimu. Huko Antiokia, Wakristo walitoa kwa ukarimu ili kuendeleza kazi ya ufalme. Waliitikia unabii wa Agabo kwa kutoa msaada kwa ndugu na dada walikuwa wanaishi Uyahudi (Mdo. 11:29). Hii inatukumbusha yale yaliyotokea baada ya kushuka kwa Roho ile Siku ya Pentekoste (2:44-45).

Kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kutumia kanisa la Antiokia kama kielelezo. Unapaswa kufanya kazi ili kuhakikisha kwamba kila moja ya sifa hizi saba za kanisa la kimishenari zinakuzwa katika kanisa unaloliongoza.

## KUTEKELEZA UTUME WA MUNGU

Unaweza kuwa unauliza, “Ninawezaje kuanzisha mpango mzuri wa utume katika kanisa langu? Je, ni hatua gani za vitendo ninazoweza kuchukua ili kanisa langu lisogee kutoka mahali lilipo leo hadi mahali ambapo Mungu anataka liwe?”

Ili kufanya hivi, lazima uelewe kwamba kanisa la kimishenari la kweli haliwezi kuundwa kwa muda mfupi. Haitakuwa sawa na kuwasha swichi na mara moja "nuru ya umisheni" iwake kanisani. Kuunda maono ya kimishenari katika kusanyiko ni mchakato ambao utachukua muda na juhudi nyingi. Mpango unahitajika. Na mpango huo utahitaji kutekelezwa.

Hapa kuna mbinu tano za ufanisi unazoweza kutumia ili kuingiza maono ya kimishenari katika kanisa lako. Iwapo utatumia mbinu hizi mara kwa mara, baada ya muda kanisa lako litasogea kutoka kuwa kanisa linalozingatia mambo yake ya ndani na kujijali kibinafsi hadi kuwa kanisa linalolenga nje, la kimishenari - aina ya kanisa linalompendeza Mungu.

**Kuhubiri kwa Shauku na Bidii**

Mbinu ya kwanza unayoweza kutumia kuingiza maono ya kimishenari katika kanisa lako ni kuhubiri kwa ari na bidii. Ni lazima uhubiri mara kwa mara juu ya utume wa Mungu na wajibu wa kanisa kushiriki katika utume huo. Na lazima uruhusu shauku yako ya utume ijulikane kwa jinsi unavyowasilisha ujumbe wako. Watu wataguswa sana na kulipenda sana somo hilo kama watakavyovutiwa na hoja zako zenye mantiki. Mwishoni mwa ujumbe wako, hakikisha unawapa changamoto watu wa Mungu kujitoa kwa utume wa Mungu. Kisha toa mwito upate jibu maalum kwa ujumbe.[1]

**Maombi Yenye Lengo**

Mbinu ya pili unayoweza kutumia kuingiza maono ya umisheni katika kanisa lako ni maombi yanayolenga utume. Ni vizuri uliongoze kanisa lako mara kwa mara katika maombi kwa ajili ya mavuno (ling. Mt. 9:37-38). Unapaswa kutenga muda katika kila ibada ya Jumapili kwa ajili ya maombi ya kimishenari. Katika wakati huu, wewe au kiongozi aliyeteuliwa mtaliongoza kanisa kuomba kwa ajili ya mishenari mmoja au programu za umisheni ambazo kanisa linaunga mkono. Unapaswa pia kuomba kwa ajili ya watu na maeneo ambayo hayajafikiwa katika nchi yako na duniani kote.

Vilevile ni vizuri uwaongoze watu wako mara kwa mara katika maombi kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya kanisa. Kadiri washirika zaidi na zaidi wanavyowezeshwa na Roho wa Mungu anayetuma wamishenari, mioyo yao itajawa na shauku Yake kwa waliopotea. Na Roho atawasukuma kufanya sehemu yao katika kuwafikia watu waliopotea nyumbani na hata miisho ya dunia (Mdo. 1:8).[2]

---

[1] Kitabu, *Kumtangaza Kristo kwa Mataifa: Jumbe 100 Kuhusu Utume Unaowezeshwa na Roho Mtakatifu,* kinapatikana kutoka taasisi ya Africa's Hope, Acts 1:8 Initiative. Kinaweza kupakuliwa bila malipo kutoka tovuti ya .

[2] Kwa maelezo zaidi kuhusu mada hizi, tazama Sura ya 8: “Kipaumbele cha Maombi” na Sura ya 11: “Hukuza Utendaji na Uzoefu wa Kipentekoste.”

**Kufundisha kwa Mpangilio**

Tatu, unaweza kuingiza shauku ya umisheni katika mioyo ya watu wa Mungu kupitia mafundisho yenye mpangilio kuhusu utume wa Mungu. Ili kufanya hivyo, utahitaji kupitia Maandiko hatua kwa hatua ukiangazia jinsi ambavyo Mungu ametenda katika historia ili kutimiza utume Wake duniani. Mtazamo huu mpya wa Biblia utatengeneza katika mioyo ya watu uelewa wa wazi ulio mzuri kuhusu asili na huduma ya kimishenari ya Kanisa. Ufahamu huu utawatia moyo kushiriki kikamilifu zaidi katika utume wa Mungu.[3]

**Ushiriki Wenye Kusudi**

Njia ya nne ya kuingiza maono ya kimishenari katika watu wako ni kupanga (au kupanga upya) kanisa lako kwa ajili ya ushiriki katika utume. Ili kufanya hivi, utahitaji kutathmini kwa uangalifu kila idara na huduma za kanisa ili kuhakikisha kwamba mipango yao inaonyesha kujitoa kwa kanisa lako kwa utume wa Mungu. Wewe, pamoja na timu ya uongozi wa kanisa, mnapaswa kuuliza kila huduma katika kanisa, "Je! Mpango huu unasaidiaje kanisa letu kutimiza utume wa Mungu?" Ikiwa mpango husika hausaidii kanisa kutimiza utume wa Mungu, haupaswi kutupiliwa mbali au kurekebishwa.

**Ushirikiano wa Kimkakati**

Mbinu ya tano unayoweza kutumia ili kuingiza maono ya kimishenari katika kanisa lako ni kushirikiana kimkakati na wamishenari wanaoheshimika, na mashirika ya kimisheni. Hakuna kanisa la mahali pamoja lenye uwezo wa kutekeleza utume wa Mungu peke yake. Utume ni jambo ambalo Mwili wote wa Kristo unapaswa kufanya kwa kushirikiana pamoja. Basi, pamoja na mipango yake ya ndani ya kujieneza, lazima uliongoze kanisa lako kushirikiana na mipango ya utume ya kanisa lako la kitaifa na mashirika mengine mazuri ya umisheni. Kwa kufanya hivi, lazima uliongoze kanisa lako kuunga mkono kwa uaminifu mpango wake wa utume wa kanisa la kitaifa na wamishenari linaowaunga mkono. Washirika wa kanisa lako wanapoona yote yanayotimizwa kupitia juhudi hizi za ushirikiano, watatiwa moyo wa kushiriki hata zaidi katika utume.

---

[3] Unaweza kujifunza zaidi kuhusu utume wa Mungu katika kitabu cha Paul York kiitwacho, *Theolojia ya Kibiblia ya Umisheni,* kutoka Discovery Series ya taasisi ya Africa's Hope.

**Uhusika wa Kusanyiko**

Hatimaye, unaweza kuingiza maono ya kimishenari katika kanisa lako kwa kuwafichua washirika wako kwenye uwanja wa misheni. Hapa kuna njia tano za ufanisi unaweza kufanya hivi:

*1. Wageni wamishenari*. Njia moja unayoweza kuwaingiza washirika kwenye uwanja wa misheni ni kuwaalika wageni wamishenari kuja na kuhubiri kwenye mkutano wako. Wamishenari hawa watashirikisha kanisa maono yao ya kuwafikia waliopotea, pamoja na asili ya kazi yao katika shamba la Bwana. Watu wanapowasikiliza hao wamishenari shauku ya misheni itazaliwa mioyoni mwao. Unapomwalika mishenari kuzungumza, lazima uhakikishe kwamba kanisa lako linambariki mmishenari kwa sadaka ya ukarimu, kuweka ahadi ya kifedha ya kila mwezi, na maombi endelevu.

*2. Jumapili ya umisheni*. Njia nyingine nzuri ya kuliweka wazi kanisa lako kwa umisheni ni kwa kutenga Jumapili moja kila mwezi kama "Jumapili ya Umisheni." Siku ya Jumapili ya umisheni, wewe au mwakilishi aliyeteuliwa, mtasoma ripoti kutoka kwa wamishenari na kuwaombea. Kisha utahubiri kuhusu umisheni na kupokea sadaka ya umisheni. Mkakati huu utahakikisha kwamba kanisa lako linadumisha hazina ya umisheni iliyo nzuri, yenye afya.

*3. Makongamano ya umisheni*. Itakuwa vizuri pia kupanga kongamano la kila mwaka la umisheni kwa ajili ya kanisa. Kongamano la umisheni ni mfululizo wa huduma za kanisa zilizotengenezwa ili kulifungua kanisa kwa umisheni na kuongeza mzigo wake kuwafikia waliopotea. Wakati wa kongamano, waalike wamishenari kuhubiri na kushirikisha kanisani huduma zao. Pia wakati wa kongamano, utataka kutazama mafanikio ya umisheni ya kanisa pamoja na malengo yake kwa mwaka ujao. Zaidi ya hayo, wape changamoto watu kutoa ahadi za kila mwezi kwa mpango wa umisheni wa kanisa.

*4. Kibao cha umisheni*. Zaidi ya hayo, unaweza kulifungua kanisa kwa umisheni kwa kuandaa kibao cha umisheni kinachovutia na kukiweka mahali penye kuonekana vizuri kanisani. Kwenye ubao huu zibandikwe picha za wamishenari zikiwa na maelezo ya huduma zao. Barua toka kwa wamishenari, ramani za umisheni, na taarifa nyingine zinazohusiana na utume pia zinaweza kubandikwa.

*5. Mtoko wa kimisheni*. Njia nyingine unayoweza kulifanya kusanyiko lako kufunguka kwa umisheni ni kuwahimiza washirika wako kushiriki katika huduma

za umisheni zinazofadhiliwa na kanisa. Kwa mfano, idara ya umisheni ya kanisa inaweza kutaka kupanga kufikia eneo lililopuuzwa au kundi la kikabila katika nchi yako. Au wanaweza kutaka kufadhili mpango wa kuanzisha kanisa jipya katika eneo ambalo halijahubiriwa. Kuwekwa wazi huku kwa moja kwa moja kwa kazi ya umisheni kutaendeleza ufalme wa Mungu, kutaleta shauku ya umisheni katika mioyo ya watu, na kuwasaidia washirika kuelewa kazi ya umisheni.

## KUSAIDIA WAMISHENARI

Paulo alikumbusha kanisa la Rumi kwamba, ili wamishenari waweze kwenda na kuhubiri injili kwa waliopotea, ni lazima watumwe na watu (Rum. 10:13-15). Kwa hiyo, sehemu kubwa ya mpango wa umisheni wa kanisa lolote ni kusaidia kutuma na kuwawezesha wamishenari shambani. Njia tatu ambazo kanisa linaweza kufanya hivi ni kupitia uaminifu katika usaidizi wao kifedha, msaada unaoendelea wa maombi, na usaidizi wa kujali kimaadili, kama ifuatavyo:

### Kusaidia Kifedha kwa Uaminifu

Kwanza, kanisa lako lazima liwasaidie wamishenari wake kifedha. Paulo alikuwa anazungumza juu ya huko kutegemeza alipowapa waamini wa Korintho changamoto, kwa swali hili: “Ni nani anayekuwa askari kwa gharama yake mwenyewe?” (1 Kor. 9:7). Akawakumbusha tena, “Wale wahubirio injili wanapaswa kupokea riziki yao kutokana na injili” (1 Kor. 9:14).

Ili wamishenari wabaki shambani, ni lazima wapokee kwa uaminifu sana na endelevu usaidizi wa kifedha kutoka nyumbani. Msaada huu kwa kiasi kikubwa hutoka kwa wafadhili binafsi na makanisa ya mahali. Makanisa mengi ya mahali huwasaidia wamishenari kupitia idara ya umisheni ya kanisa lao la kitaifa. Kama mchungaji, ni lazima uhakikishe kwamba sadaka zote za umisheni zinashughulikiwa kwa uadilifu na kwamba zinatumika tu kwa madhumuni ya kutolewa kwake.

### Msaada Endelevu wa Maombi

Pili, kanisa lazima litoe msaada endelevu wa maombi kwa ajili ya wamishenari wao shambani. Mara nyingi Paulo alikumbusha makanisa kumwombea. Kwa mfano, aliwasihi Wakristo wa Thesalonike hivi: “Ndugu na dada, tuombeeni ili ujumbe wa Bwana uenee upesi na kuheshimiwa” (2 The. 3:1). Mifano mingine ya Paulo akiomba maombi kutoka kwa Wakristo ipo katika Warumi 15:30-32, Waefeso 6:19, Wakolosai 4:3-4, na 1 Wathesalonike 5:25. Kupitia sala zao, Wakristo wanaweza kuwategemeza wamishenari shambani na

kuwasaidia kupigana vita vizuri vya imani. Wakati mwingine maombi kwa ajili ya wamishenari huhusisha vita vikali vya kiroho (Efe. 6:11-18; Mt. 12:29).

**Msaada Kimaadili**

Mwisho ni kwamba: Kanisa la Kipentekoste lazima liwape wamishenari wake usaidizi wa kimaadili na kihisia. Wamishenari mara nyingi huishi mbali na nyumbani na kituo chao cha kuwategemeza. Wakati fulani wanajisikia kutengwa, na wapweke, na wanahitaji msaada wa kimaadili. Wakristo walioko nyumbani wanaweza kutoa msaada huo kwa kuandika barua na barua pepe zenye kutia moyo.

## KUWALENGA WASIOFIKIWA

Huduma ya Paulo ya umishenari ilikazia fikira za watu ambao hawajafikiwa. Aliandika hivi: "Sikuzote imekuwa nia yangu kuhubiri injili mahali ambapo Kristo hajulikani, ili nisije nikajenga juu ya msingi wa mtu mwingine" (Rum. 15:20).

Vivyo hivyo, kila mpango wa umisheni wa kanisa la Pentekoste la mahali pamoja lazima uunganishe kulenga makundi ya watu ambao hawajafikiwa. Kundi la watu ambao hawajafikiwa ni kabila lisilo na ushuhuda wowote, linalojiendesha la kanisa. Watafiti wanasema siku za leo kuna zaidi ya makundi elfu saba ya watu ambao hawajafikiwa duniani. Watu hao ambao hawajafikiwa wanatimiza idadi zaidi ya watu bilioni tatu ambao hawawezi kupata habari njema juu ya Yesu. Wengi wa vikundi hivi vya watu ambao hawajafikiwa wanaishi Afrika. Kanisa la Kiafrika lazima liwaelekeze watu hawa waliopotea ili wamishenari wawafikie.[4]

[4] Unaweza kujua zaidi kuhusu vikundi vya watu ambao hawajafikiwa kwa kuingia kwenye tovuti www.JoshuaProject.net .

## ~ Sehemu ya 10 ~

# Mchungaji wa Kipentekoste na Ibada Maalum

## ~ Sura ya 41 ~

# Kufanya Harusi na Mazishi

Mara baada ya kumaliza chuo, Samweli alimwomba Esta waoane, naye akakubali. Wakiwa vijana wacha Mungu, walijitoa kubaki wasafi kingono hadi watakapofunga ndoa. Cha kusikitisha ni kwamba, kabla ya harusi, vita vya wenyewe kwa wenyewe vilizuka katika taifa lao. Kila mmoja wa familia zao walikimbilia nchi tofauti kutafuta hifadhi. Baada ya miaka miwili ya kutengana, Samweli na Esta walirudi katika nchi yao na kuungana tena. Harusi yao ilikuwa ya gharama ndogo tu, ila Roho wa Mungu alidhihirika waziwazi wakati wa sherehe hiyo. Tangu wakati huo, Samweli na Esta wamemtumikia Bwana kwa uaminifu na kulea watoto wacha Mungu.

Katika hadithi nyingine, Kristofa na Stefano walikuwa ndugu wawili wa karibu sana. Stefano alipoaga dunia ghafla, Kristofa aliumia moyoni. Ingawa yeye hakuwa Mkristo, ndugu yake alikuwa Mkristo. Stefano alikuwa amemtumikia Mungu kwa uaminifu kama shemasi katika kanisa lake. Kwa sababu ya huduma ambayo kanisa la mahali lilitoa kwa familia ya Stefano, heshima ya ibada ya mazishi, na huduma ya ufuatiliaji ya wachungaji, Kristofa na familia yake yote walitoa maisha yao kwa Kristo na wakawa washirika kanisani. Leo, Kristofa ni shemasi katika kanisa. Anahudumu katika nafasi ile ile ya huduma ambayo Stefano kaka yake aliwahi kuhudumu.

Sura hii itazungumzia kile ambacho Biblia inasema kuhusu harusi na mazishi na thamani yake kwa familia, kanisa, na jamii kwa ujumla. Pia itatoa ufahamu kwa wachungaji wa Kipentekoste juu ya kujiandaa, kuendesha, na kufuatilia harusi na mazishi. Ingawa maelezo ya jinsi mchungaji anavyopaswa kuendesha ibada hizi maalum yanaweza kutofautiana kutoka nchi hadi nchi, na kutoka utamaduni hadi utamaduni, sura hii itatoa miongozo ya jumla ya kuendesha sherehe hizi muhimu.

## SHEREHE YA HARUSI

Hakuna mahali popote ambapo Biblia imeweka miongozo dhahiri kuhusu sherehe za arusi. Lakini inatoa mifano kadhaa ya harusi zilizoidhinishwa na Mungu. Kanuni zilizodhihirishwa kutokana na mifano hii zinaweza kumwongoza mchungaji wa Kipentekoste katika kuandaa na kuongoza sherehe za harusi.

Mfano mmoja ni simulizi la Biblia jinsi Mungu alivyowaleta Adamu na Hawa pamoja kama mume na mke (Mwa. 2:18-25). Baada ya kuwaumba, Mungu aliwaleta pamoja katika ile inayoweza kuitwa kwa usahihi, “arusi ya kwanza”. Kutokana na wao kuwa pamoja, Biblia inasema walifanyika “mwili mmoja” (mst. 24; taz. Mt. 19:5-6).

Baadaye katika Mwanzo, Biblia inaeleza kuhusu ndoa ya Isaka na Rebeka (Mwa. 24:1-67). Inaeleza jinsi Mungu alivyomwongoza mtumishi wa Abrahamu kwa msichana mrembo Mkaldayo anayeitwa Rebeka. Baada ya kumweleza kilichomleta, msichana huyo alikubali kurudi naye Kanaani ili awe mke wa Isaka. Alipokutana na Isaka kwa mara ya kwanza, alichukua utaji wake na kwa heshima akajifunika kulingana na desturi ya wakati huo. Kisha mtumishi huyo alimweleza Isaka jinsi Mungu alivyomsaidia kumpata Rebeka. Isaka akamchukua Rebeka na kumwingiza hemani mwa marehemu mama yake Sara na kumwoa. Alimpenda Rebeka sana na alipata faraja kwake. Hadithi hii ya Isaka na Rebeka inaonyesha kwamba ikiwa mtu ataomba na kumtafuta Mungu, atamwongoza kwa mwenzi mwaminifu ambaye pamoja naye wanaweza kushiriki furaha, faraja na raha za ndoa.

Sulemani alitangaza kwamba, “Yeye apataye mke apata mema na kupata kibali kutoka kwa Bwana” (Mit. 18:22). Bila shaka kinyume chake ni kweli pia: yeye apataye mume apata mema na kupata kibali kutoka kwa Bwana. Sulemani anapanua ukweli huu katika Wimbo Ulio Bora, ambapo anatoa picha nzuri ya upendo wa kimapenzi katika ndoa. Kuingia katika ndoa ya kimungu ni jambo la heri.

**Yesu Alibariki Ndoa**

Yesu alikuwa na mengi ya kusema kuhusu utakatifu wa ndoa (Mt. 5:31-32; Mk. 10:1-12). Zaidi, alionyesha anavyothamini sherehe za arusi kwa kuhudhuria moja katika kijiji cha Kana huko Galilaya. Hapo, alibariki tukio hilo kwa kugeuza kimuujiza maji kuwa divai, akawaokoa wahusika kutokana na aibu hadharani (Yoh. 2:1-11). Ukweli kwamba hii ilikuwa ishara ya kwanza ya kimuujiza ya Yesu katika Injili ya Yohana inasisitiza umuhimu anaoweka juu ya ibada ya ndoa.

Zaidi ya hayo, Biblia hutumia mafumbo ya ndoa na arusi ili kuonyesha uhusiano wa karibu wa Mungu na watu Wake. Kwa mfano katika Agano la Kale, Biblia inataja taifa la Israeli kama bibi-arusi, au mke wa Mungu (Isa. 62:5; Yer. 3:14). Vivyo hivyo katika Agano Jipya, Paulo analielezea Kanisa kama bibi-arusi wa Kristo (Efe. 5:23-32). Kwa kutumia mifano kama hiyo, manabii na mitume walikuwa wakitangaza upendo wa Mungu na kujitoa Kwake kwa watu wake. Na kwa kumaanisha, walikuwa wakitangaza jinsi Mungu anavyothamini sana taasisi ya ndoa.

**Umuhimu wa Sherehe ya Harusi**

Harusi za kanisa huongeza hali ya wanandoa kujitambulisha na jamii ya waaminio. Pia huongeza kujitoa kwa wanandoa kila mmoja kwa mwingine. Mungu alimfanya Hawa kutatua upweke wa Adamu. Kuhusu Adamu, Mungu alitangaza, "Si vema huyo mtu awe peke yake" (Mwa. 2:18). Ndivyo ilivyo kwa wawili waliofunga ndoa. Si vyema kwao kuwa peke yao, yaani kujitenga na jumuiya ya waamini. Kama Mungu alivyo na mahusiano: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu - aliwaumba wanadamu waishi katika jumuiya.

Barani Afrika, harusi ya mwanamume na mwanamke si jambo binafsi. Ni tukio la watu wote, la hadhara, la kusherehekewa kwa furaha na jamii nzima. Harusi inaonyesha kwamba wanandoa ni sehemu ya jamii ya waaminio, yaani Kanisa. Ikiwa mume au mke anatoka mbali, upendo na kujaliwa kunako-onyeshwa na familia yao mpya ya kanisa huwafanya wajisikie wamekaribishwa na kukubalika.

Harusi za Kikristo pia hutoa ujumbe wa kimaadili kwa jamii inayozunguka. Kila wanandoa wapya ambao wamefunga ndoa ipasavyo kanisani huwapa changamoto wenzao kufuata mfano wao. Katika ulimwengu wa kisasa, imekuwa jambo la kawaida japo la aibu, kwa mwanamume na mwanamke kuishi pamoja wakishirikiana kingono bila kufunga ndoa. Wenzi wanaofunga ndoa kulingana na

Neno la Mungu huongeza thamani ya kiadili katika jumuiya yao na kuwawekea wengine wa rika lao kielelezo kizuri.

**Maandalizi kwa Ajili ya Harusi**

Mafanikio ya sherehe ya harusi hutegemea sana maandalizi sahihi. Kama mchungaji wa Kipentekoste, unapaswa kujitayarisha, pamoja na bibi na bwana harusi, kwa njia nne:

*1. Maandalizi ya kiroho*. Kwanza, unapaswa kushughulikia maandalizi ya kiroho ya wahusika wa harusi. Ndoa ni zaidi ya mkataba wa kijamii, kama ulimwengu unavyotaka tuamini. Kwa mtazamo wa Mungu, ni agano takatifu kati ya mwanamume, mwanamke, na Mungu. Kwa hiyo imekuwepo kwa ajili ya mwanamume na mwanamke walio tayari kuishi katika uhusiano wa agano na Bwana Mungu wao. Harusi inapaswa kuonyesha kweli hizi takatifu.

Kama mchungaji, unapaswa kuwashauri wanandoa tarajiwa kuhakikisha kwamba wanaelewa uzito wa viapo wanavyokaribia kupeana. Hakikisha pia kwamba bibi na bwana harusi wamezaliwa mara ya pili. Ukigundua kwamba yeyote kati yao hajaokoka kikwelikweli, tafuta kuwaongoza kwa Kristo. Ikiwa wameokoka, lakini hawaishi maisha ya kujitoa kikamilifu, waongoze kuyakabidhi tena maisha yao kwa Kristo.

*2. Maandalizi ya kitamaduni*. Pili, kama mchungaji, lazima uzingatie suala la maandalizi ya kitamaduni. Tamaduni tofauti za Kiafrika zina mila na desturi tofauti zinazohusu harusi. Kwa mfano, katika tamaduni nyingi za Kiafrika, ndoa halali lazima itanguliwe na malipo ya mahari. Ukijikuta katika mazingira kama hayo, hakikisha kwamba wahusika wanatekeleza mahitaji ya kimila kabla ya siku ya arusi — mradi tu mahitaji hayo hayakiuki Maandiko au desturi za kanisa. Inaweza kuwa aibu ikiwa mahitaji ya kitamaduni ambayo hayajatatuliwa yatatakiwa kutatuliwa wakati wa ibada ya harusi kanisani.

*3. Maandalizi ya kisheria.* Tatu, lazima uhakikishe kuwa wewe na wahusika wa harusi mmeshughulikia masuala yoyote ya kisheria yanayotakiwa kwa ajili ya harusi. Kwa mfano, lazima uhakikishe kuwa leseni ya ndoa imepatikana kutoka kwa mamlaka husika ya serikali. Zaidi, hakikisha kuwa hakuna mhusika aliye na mwenzi mwingine, au aliye hai. Katika nchi zingine, hatua za kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi ya mchungaji yeyote anayekiuka sheria za ndoa.

Mchungaji mmoja alipuuza hilo na kujiletea aibu yeye na kanisa lake. Wakati wa ibada ya arusi, alisema, “Ikiwa mtu yeyote anaweza kuonyesha sababu yoyote

halali kwa nini mwanamume huyu hawezi kuoana na mwanamke huyu, na aseme sasa au anyamaze milele.” Cha kumshangaza kila mtu ni kwamba, mwanamke mmoja kijana aliinua mkono wake. Alisema, “Sitaki kusimamisha arusi, kwa kuwa anayeolewa ni dada yangu. Lakini, huyo mwanaume anayemuoa ni baba wa mtoto wangu. Aliahidi kunioa kabla ya kubadili mawazo yake na kwenda kwake.” Baada ya vurugu kubwa, hiyo harusi iliahirishwa. Tukio hili la kufedhehesha lingeweza kuepukwa kama mchungaji angefanya uchunguzi sahihi mapema, na kwa ukamilifu.

*4. Maandalizi ya sherehe.* Hatimaye kama mchungaji, lazima uhakikishe kwamba maandalizi ya sherehe yamefanyika kabla ya harusi. Unapaswa kukutana na wahusika ili kuhakikisha kwamba wanaelewa sherehe ya arusi ya Kikristo ni ibada inayofanywa katika uwepo wa Mungu.

Mavazi ya arusi ya mchungaji, bibi-arusi, bwana harusi, na wahudumu wote yanapaswa kuendana na tukio hilo. Bwana harusi na bibi harusi wanapaswa kuvaa kwa heshima. Bibi-arusi, wasichana wanaomsindikiza na wageni wa kike wanapaswa kuvalia vizuri lakini kwa staha na kiasi. Iwapo wanandoa na wasindikizaji wao watachagua kuvaa mavazi ya kitamaduni, huenda ikambidi mchungaji arekebishe mavazi yake yaendane na tukio kwa kiwango atakachoweza.

Tambulisha utaratibu utakaotumia, wa harusi.[1] Vile vile jaribu kupitia utaratibu wako pamoja na ibada nzima pamoja na bibi na bwana harusi na kuzungumzia kila sehemu husika pamoja nao. Kwa njia hii, wataelewa vizuri ahadi watakazopeana punde. Kabla ya harusi, jengo na eneo la kanisa vifanyiwe usafi stahiki.

### Kuifunga Harusi

Ibada ya arusi ina sehemu tatu muhimu: mahubiri, wahusika kupeana nadhiri za ndoa, na kutiwa sahihi hati za kisheria.

*1. Mahubiri.* Mahubiri yanatakiwa kukazia kujitoa kwa wahusika kwa Mungu, uaminifu wa kila mmoja kwa mwenzake, na malezi ya watoto wanaomcha Mungu. Ingawa wanandoa ndio walengwa wakuu, ujumbe ni kwa wote waliopo -

---

[1] Sherehe za harusi zinaweza kupatikana katika, *The Minister's Service Book,* kilichoandaliwa na Myer Pearlman. Unapaswa kuwa na nakala ya kitabu hiki au nyenzo nyingine iliyopendekezwa na dhehebu lenu.

walioolewa na wasioolewa. Ujumbe uwe mfupi, usichukue zaidi ya dakika kumi na tano au ishirini.

*2. Kupeana nadhiri.* Tukio hasa la ndoa, ambalo ni kupeana nadhiri na pete, lipewe heshima stahiki. Kabla ya ibada, fanya marudio na wanandoa kuhusu kupeana nadhiri na pete. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba wanaepuka makosa yanayoleta aibu wakati wa sherehe yenyewe.

*3. Kutia saini hati.* Kama mhudumu unayetambulika rasmi, jukumu la mchungaji wa Kipentekoste katika ibada ya harusi ni kiroho na kisheria. Unapaswa kutimiza hayo yote mawili kwa njia sahihi. Kabla ya ibada, hakikisha kwamba nyaraka zote za kisheria ziko sahihi. Wanaotakiwa kisheria kutia sahihi hati hizi wanapaswa kujulishwa mapema. Hakikisha kuwa watu hao wapo na wanafahamu wajibu wao.

Mwishowe, toa maelekezo ya kusainiwa maeneo husika. Baada tu ya kila sahihi inayohitajika kuwekwa, toa hati hizo kwa maarusi husika mbele ya watu wote – hasa kwa bwana harusi, ambaye ana jukumu kubwa zaidi la kuifanikisha ile ndoa. Baada tu ya hizo nyaraka kutolewa, watangaze wana ndoa hao kuwa mume na mke. Halafu waambie wale wanandoa wapya kupiga magoti mbele ya Mungu. Kuwe na mito au vitambaa safi, kama inawezekana. Kisha weka mikono juu yao na kuwaombea baraka. Ibada inahitimishwa kwa bwana harusi kumbusu bibi harusi (ikiwa utamaduni unaruhusu, na wao wenyewe wakikubali) na baraka za mwisho.

## HUDUMA YA MAZISHI

Kifo cha Getruda kilipotangazwa, mji wote ulitikisika. Jamii nzima iliomboleza pamoja na familia yake kwa kuondokewa naye. Wanaume, wanawake, vijana, na watoto wote waliomboleza. Getruda alikuwa shemasi wa Assemblies of God. Kwa sababu ya tabia yake ya Kikristo na ukarimu wake, alipendwa na wote.

Wakati wa mazishi yake, mchungaji alitoa ujumbe wa faraja. Pia alihubiri kuhusu tumaini katika Kristo. Mwishoni mwa mahubiri, mchungaji aliwaalika watu wajitokeze kumpokea Kristo kama Mwokozi. Wengi waliitikia na kutoa maisha yao kwa Kristo. Kwa sababu ya maisha ya Getruda na hekima ya mchungaji wake katika kuendesha ibada ya mazishi, mema mengi yalifuata, sio tu kutokana na maisha yake, bali pia kutokana na kifo chake.

## Faida za Ibada ya Mazishi

Waafrika wanaishi maisha yao katika jamii. Maadili yao binafsi hufafanuliwa na kuimarishwa na wale walio karibu nao. Hivyo, mtu katika jamii anapokufa, ibada ya mazishi huwaleta watu wote pamoja. Watu wa tabaka mbalimbali, bila kujali dini zao, hukusanyika ili kutoa heshima zao za mwisho kwa aliyeaga dunia. Pia wanakuja kuonyesha mshikamano wao na familia inayo omboleza.

Ibada ya mazishi barani Afrika ina malengo mengi. Kwanza, huwapa familia na marafiki fursa ya kuja pamoja na kuomboleza. Wanapofanya hivi, mioyo yao inafarijiwa na kuimarishwa. Tena, ibada ya mazishi husaidia kuwapa waombolezaji hisia ya mambo kumalizika. Huwawezesha kukubali kuondokewa kwao, na kwa nguvu za Mungu, kuendelea na maisha yao. Mwishowe, ibada ya mazishi inatoa fursa nzuri kwa mchungaji wa Kipentekoste kushirikisha ujumbe wa Kristo kwa wasiomjua. Wengi ambao hawatawahi kuhudhuria ibada ya kawaida ya kanisa watakuja kwenye mazishi. Mchungaji wa Kipentekoste mwenye hekima atatumia fursa hii kwa busara, ila kwa msisitizo, kushirikisha ujumbe wa wokovu.

## Kuwahudumia Wafiwa

Ukiwa mchungaji wa Kipentekoste, huduma yako kwa waliofiwa huanza mara tu unapopata habari za kifo cha mtu huyo. Unapaswa kuwa tayari kukatiza ratiba yako na kuwafikia mara moja wapendwa wa marehemu. Hii itakuwa ishara ya kwanza kwa familia kwamba unawajali. Ingawa maneno ya faraja yanafaa na ni sahihi, pengine itakuwa vizuri kutokuwa na maneno mengi hapo mwanzoni. Keti tu na kulia na familia yenye huzuni. Kuwepo kwako, maneno machache ya faraja na sala ni kawaida tu inayohitajika katika hatua hii.

Baadaye ni vizuri uitembelee ile familia tena, wewe na viongozi wengine wa kanisa. Wakati wa ziara hii, ongoza wimbo mmoja au mbili, toa ujumbe mfupi, na uombe kwa ajili ya familia. Pia waweza kusoma Maandiko machache yanayofaa. Zaidi ya hayo, wewe na timu yako ya uongozi mnaweza kutaka kutoa usaidizi wa kifedha kwa niaba ya kanisa. Hilo husaidia hasa wakati familia iliyofiwa inapokuwa haiwezi kumudu gharama ya mazishi.

## Kujiandaa kwa Huduma

Wewe na timu yako ya uongozi mnapaswa pia kuwa na muda wa kuketi na familia inayoomboleza ili kupanga ibada ya mazishi. Wakati wa mkutano huu, unaweza kusoma Maandiko na historia ya marehemu. Ni vizuri kuheshimu

matakwa ya familia kuhusu nani apewe hizo kazi. Mahubiri ya mazishi kwa kawaida hutolewa na mchungaji wa marehemu. Lakini, ikiwa kwa sababu fulani familia inaomba mhudumu mwingine atoe mahubiri, usikatae kubadilisha hiyo kawaida.

**Ibada ya Mazishi**

Huduma ya mazishi yenyewe inatakiwa kuwa na mambo kadhaa muhimu. Kwanza, nyimbo zinazofaa zinapaswa kuchaguliwa kwa ajili ya tukio. Pili, hiyo ibada inapaswa kuhusisha mahubiri yanayotolewa na mhudumu stahiki, anayeheshimika (kama si wewe mchungaji). Ikiwa marehemu aliishi maisha ya Kikristo ya kupigiwa mfano, mahubiri yanaweza kuwa ya wasifu. Vinginevyo, ujumbe rahisi unapaswa kuhubiriwa kusisitiza wokovu na ukweli wa maisha yaliyoko baada ya kifo.

Washirika wa kanisa na marafiki wanapaswa kuruhusiwa kutoa heshima zao kwa njia ambazo zitaheshimu kumbukumbu ya marehemu na kufariji familia. Wale watoao heshima watiwe moyo kufanya kwa kifupi ili ibada ya mazishi isiwe ndefu sana na kuichosha familia badala ya kuwa baraka.

Unapaswa pia kufupisha maziko. Kwa kawaida hayo huwa na wimbo mmoja unaofaa, maombi, na maombezi yanayotolewa na mchungaji aliyepangwa rasmi. Simamia muda ili kuhakikisha kwamba mwili wa marehemu umezikwa kabla ya jioni.

**Ufuatiliaji**

Wajibu wako kama mchungaji hauishii kwenye ibada ya mazishi. Baada ya maziko, wewe na wazee wako wa kanisa muandamane na familia hadi nyumbani kwao. Hapo, utatoa maneno ya mwisho ya faraja na kuwaombea. [Wakati mwingine – kutegemeana na eneo, kutakuwepo kuvunjwa kwa matanga, yaani kumaliza maombolezo kwa watu wote isipokuwa kwa familia.] Kadiri siku zinavyopita, itembelee familia iliyofiwa na kukaa nao kwa muda mfupi. Na unapaswa kutafuta fursa za kushirikisha wanafamilia Injili, hususan wale wasiomjua Bwana.

---

Harusi na mazishi ni nyakati nzuri kwa mchungaji wa Kipentekoste na kanisa kuonyesha upendo na kuwajali washirika wa kanisa na wengine katika jamii. Anapaswa kuwa makini sana katika kupanga na kuendesha ibada hizi kwa kujali upendo na heshima.

~ Sura ya 42 ~

# Kuendesha Meza ya Bwana, Kuweka Wakfu, na Kuingiza Kazini

Mchungaji wa Kipentekoste mara nyingi huitwa kusimamia ibada zingine takatifu na sherehe mbalimbali. Ni vizuri shughuli hizo zifanywe kwa ustadi na heshima stahiki. Sura hii ipo ili kumsaidia mchungaji wa Kipentekoste katika eneo hili muhimu la huduma.

## UBATIZO WA MAJI

Ubatizo wa maji ni wa kwanza kati ya ibada mbili takatifu zilizoanzishwa na Yesu. Yeye mwenyewe alibatizwa majini, akiweka kielelezo kwa wale wote watakaomfuata (Mt. 3:13-17). Tena, aliliagiza Kanisa Lake kwenda na kufanya wanafunzi kutoka kwa mataifa yote, na "kuwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu" (Mt. 28:19-20; taz. Mk. 16:15-16).

Kanisa la kwanza lilifuata kwa uangalifu maagizo ya Yesu kwa kuwabatiza waamini wapya katika maji mara tu baada ya kuokoka kwao (Mdo. 2:37-41; 8:12-13, 36-38; 9:17-18; 10:47-48; 16:13-15, 31-33; 18:8; 19:5). Kwa kuwa ubatizo wa

maji ni agizo la kiungu, si jambo la hiari. Basi wewe kama mchungaji wa Kipentekoste, lazima ujitayarishe kwa uaminifu na ustadi kutekeleza agizo hili.

**Maana Yake**

Ubatizo wa maji ni tendo la utii kwa mtumishi na kwa mwamini mpya. Ni ukiri hadharani wa imani ya mfuasi mpya katika Kristo na kujitoa kwake kumfuata Bwana wake kikamilifu. Ubatizo wenyewe hauokoi. Ila ni onyesho la "dhamiri safi kwa Mungu" kwamba mtu amekwisha kuokolewa (1 Pet. 3:21). Ubatizo wa maji ni mfano wa kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu (Rum. 6:3-11). Zaidi huonyesha kifo cha mwamini mpya kwa dunia na kufufuka kwake katika maisha mapya ndani ya Kristo (2 Kor. 5:17). Zaidi ya hayo, ubatizo wa maji unaonyesha kujitoa kwa mwamini mpya kuungana na Kristo katika kutimiza utume wake (Mt. 3:15).

**Mhusika**

Yeyote anayemwamini Yesu Kristo kwa dhati kama Bwana na Mwokozi, anaweza na ni lazima abatizwe katika maji. Ibada inapaswa kufanyika mara baada ya kuokoka. Lakini, kabla ya kumbatiza mtu, ni vema kumhoji kwanza ili kuhakikisha kama amezaliwa mara ya pili kweli, na kwamba anaelewa kikamilifu maana ya tendo hilo.

**Namna (au Jinsi)**

Njia ya kimaandiko ya ubatizo ni kwa kuzamishwa kabisa katika maji. Neno "kubatiza" maana yake halisi ni kuzama au kuzamisha. Vile vile, kuzamishwa kunaendana zaidi na mfano wa kufa, kuzikwa, na kufufuka (Rum. 6:2-4).

Unaweza kutumia utaratibu ufuatao katika kuwabatiza Wakristo wapya katika maji. Ingia majini na mhusika. Kisha mwombe kutoa ushuhuda mfupi wa jinsi alivyompata Kristo kama Mwokozi. Kisha mwulize maswali yafuatayo:

- "Je, unakiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana na Mwokozi wako?"
- "Je, unaukana ulimwengu, mwili na shetani, na kujikabidhi kabisa kwa Kristo na mapenzi yake maishani mwako?"
- "Je, unajitoa mwenyewe mbele za Mungu na Kanisa Lake ili kutembea katika upya wa uzima kwa namna impasayo Bwana?"
- "Je, utajikabidhi kikamilifu kwa Kristo na utume Wake, ukitafuta kuwaongoza wengine kumwamini Yeye?"

Mhusika anapaswa kujibu "ndiyo" kwa kila swali.

Baada ya hayo yote utamzamisha mhusika katika maji, ukisema, "Kwa sababu ya ukiri wako kwamba unamwamini Kristo kama Bwana na Mwokozi wako, na kwa sababu umejitoa mwenyewe kuacha yote ili kumfuata, ninakubatiza wewe (taja jina lake kamili), katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina." [Unapotamka majina ya Utatu,uwe unamshusha ndani ya maji hadi yamfunike kabisa. Kisha, mtoe!]

**Vifungu vya Biblia**

Soma baadhi au vifungu vyote vya Biblia vifuatavyo wakati wa ibada ya ubatizo:

- Ubatizo wa Yesu (Mt. 3:13-17; Mk. 1:9-11)
- Agizo Kuu (Mt. 28:18-20; Mk. 16:14-20)
- Siku ya Pentekoste (Mdo. 2:36-41)
- Kuhusu towashi wa Kushi (Mdo. 8:36-39)
- Mafundisho ya Paulo juu ya ubatizo (Rum. 6:3-11; Gal. 3:26-29; Kol. 2:11-15).

## MEZA YA BWANA (USHIRIKA MTAKATIFU)

Ushirika Mtakatifu ni wa pili kati ya ibada mbili takatifu zilizoanzishwa na Bwana Yesu (Mt. 26:26-29; Lk. 22:14-20; 1 Kor. 11:23-26). Pia inaitwa "kuumega mkate" (Mdo. 2:42) na "Chakula cha Bwana" (1 Kor. 11:20) au Meza ya Bwana. Neno "ushirika" linatokana na neno la Kilatini cena, ambalo linamaanisha "mlo wa pamoja jioni." Yesu alianzisha ibada hii wakati wa mlo wa mwisho na wanafunzi Wake katika chumba cha juu. Ingawa ubatizo wa maji unafanywa mara moja tu, na ni ishara ya mwamini kuingia katika maisha yake mapya ndani ya Kristo, ushirika unafanyika mara kwa mara, na huzungumzia safari ya Mkristo pamoja na Bwana.

**Maana Ushirika Mtakatifu**

Ushirika humkumbusha mwamini juu ya dhabihu ya Yesu msalabani. Mkate uliomegwa hukumbusha mwili wake uliovunjwa, na kikombe hukumbushia damu yake iliyomwagika (Lk. 22:19-20). Katika 1 Wakorintho sura ya 11, Paulo anazungumza juu ya mambo matano tunayopaswa kufanya wakati wa huduma hiyo ya ushirika.

1. Tunapaswa kukumbuka kifo cha Kristo msalabani (mst. 24-25).
2. Tunapaswa kutafakari maana ya Agano Jipya (mst. 25; taz. Mt. 26:28).

3. Tunapaswa kutazamia kurudi kwake upesi (mst. 26; taz. Mt. 26:29; Lk. 22:16-18).
4. Tunapaswa kukusanyika pamoja kwa umoja sisi kwa sisi (mst. 18-21, 33).
5. Tunapaswa kujitoa wenyewe kwa utume wa ukombozi wa Kristo (mst. 26).

**Wanaoweza Kushiriki**

Makanisa mengi ya Kipentekoste yanaendesha ushirika wa wazi. Maana yake ni kwamba, wanawakaribisha kwenye Meza ya Bwana wale wote ambao wamempokea Kristo kweli kama Mwokozi na wanamtumikia kwa uaminifu. Mshirika hatakiwi kuwa wa kanisa hilo au dhehebu fulani. Baadhi ya makanisa ya Kipentekoste yanazuia ushirika kwa wale ambao hawajabatizwa katika maji. Ni vizuri ujue sera ya kanisa lako la kitaifa kuhusu mambo haya, na kuifuata. Kila mtu anayepokea ushirika anapaswa kuchunguza moyo wake ili kuepuka hukumu ya Mungu (1 Kor. 11:27-29).

**Mara Ngapi?**

Biblia haitoi maagizo maalum kwamba kanisa liendeshe ibada ya ushirika mara ngapi. Ila inaonyesha kwamba ushirika unapaswa kufanywa mara nyingi na mara kwa mara. Baadhi ya makanisa huendesha Meza ya Bwana kila Jumapili asubuhi, ambapo wengine huifanya kila mwezi au kila baada ya robo mwaka. Jambo kuu ni kwamba unapaswa kupanga na kuandaa Meza ya Bwana katika kanisa lako mara kwa mara.

**Ibada Yenyewe**

Ushirika Mtakatifu ni sherehe takatifu. Kwa hiyo, haipaswi kuharakishwa, ila inapaswa kufanywa kwa utaratibu na kwa heshima. Chagua wanaume na wanawake wa kiroho ili kusaidia. Hao ni pamoja na wazee wa kanisa, mashemasi, au wachungaji wasaidizi. Wape maelekezo kabla ya ibada wale wanaokusaidia ugawaji jinsi ushirika utakavyoendelea.

Anzisha ibada kwa mahubiri mafupi au kwa kusoma kifungu cha Biblia kinachofaa. Kisha omba na kuwagawia mashemasi mkate na kikombe. Kisha mashemasi watasambaza vitakavyotumiwa kwa kusanyiko. Kila mtu akishapokea mkate na kikombe, soma mistari ifaayo (yaani, 1 Kor. 11:23-26). Kisha kusanyiko litakula na kunywa pamoja.

Kwa kufuata mfano wa Yesu katika Mathayo 26:26-29, ni vizuri uunganishe zile sehemu tano za hiyo ibada, kama ifuatavyo: shukrani, usomaji wa Maandiko, usambazaji wa mkate na kikombe, uimbaji wa nyimbo, na sala. Huo ushirika unaweza kufanyika wakati wowote unaofaa katika ibada.

**Vifungu vya Biblia**

Unaweza kusoma vifungu vifuatavyo vya Biblia wakati wa ibada ya ushirika:

- Yesu anaanzisha Ushirika Mtakatifu (Mt. 26:17-29; Mk. 14:12-25; Lk. 22:7-20)
- Utaratibu wa kanisa la kwanza (Mdo. 2:42-46; 20:7)
- Paulo anafafanua Ushirika Mtakatifu (1 Kor. 10:16; 11:18-31).

## KUWEKA WATOTO WAKFU

Makanisa mengi ya Kipentekoste barani Afrika huweka wakfu watoto kwa Bwana mbele ya watu. Ingawa sio agizo la kanisa kama ubatizo wa maji au Ushirika Mtakatifu, ni kitu muhimu sana.

Katika Agano la Kale, watoto waliwasilishwa kwa Bwana na kutahiriwa kulingana na Sheria ya Musa (ling. Kut. 13:2, 12-13, 15; 22:29; 1 Sam. 1:20, 24-28; 3:19). Hana alimweka wakfu Samweli mwanae, kwa Bwana, akisema, "Basi sasa nimemkabidhi kwa Bwana. Maisha yake yote ametolewa kwa Bwana" (1 Sam. 1:28). Wazazi wa Yesu walifuata desturi hii ya kale kwa kumweka wakfu kwa Bwana (Lk. 2:22-38, 40). Yesu mwenyewe "aliwakumbatia watoto, akaweka mikono yake juu yao na kuwabariki" (Mk. 10:16).

**Maana**

Wakati wa ibada hii, ni muhimu kusisitiza kwamba kuwatoa watoto kwa Bwana si sawa na ubatizo wa watoto wachanga. Kuweka wakfu mtoto hakumwokoi mtoto, wala hakumfanyi mtoto kuwa Mkristo. Ni kitendo cha kujiweka wakfu kwa upande wa wazazi ambapo wanajitoa kumlea mtoto "katika adabu na mafundisho ya Bwana" (Efe. 6:4).

Kuweka wakfu mtoto ni tendo la hadhara la kumshukuru Mungu kwa zawadi nzuri ambayo amewapa wazazi. Ni wakati ambapo kusanyiko lote linaweza kufurahi pamoja na wazazi. Kwa pamoja wanaweza kujitoa kumzunguka mtoto kwa upendo na kumshauri katika imani.

### Ibada Yenyewe

Ibada ya kuwekwa wakfu kwa mtoto inaweza kutofautiana kanisa hadi kanisa na utamaduni hadi utamaduni. Kwa kawaida hufanyika kama sehemu ya ibada ya Jumapili asubuhi. Inaweza kuwa na sehemu nne: (1) mchungaji anaweka mikono juu ya mtoto na kuomba baraka za Mungu juu yake; (2) mchungaji anaendelea na maombi yake kwa kumwomba Mungu awape hekima wazazi katika kumlea mtoto ili amtumikie Mungu; (3) mchungaji anatoa agizo kwa wazazi, akiwahimiza wamlee mtoto, kumpenda na kumtumikia Bwana; na (4) mchungaji anatoa wito kwa kanisa kuwasaidia wazazi kumlea mtoto katika njia za Mungu.

### Vifungu vya Biblia

Vifungu vifuatavyo vya Biblia vinaweza kusomwa wakati wa kuwekwa wakfu kwa mtoto:

- Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu (Mwa. 18:19)
- Mlee mtoto (Mit. 22:6)
- Sisitiza amri za Mungu kwa watoto (Kum. 6:6-9)
- Hana anamweka wakfu Samweli kwa Bwana (1 Sam. 1:20-2:26).
- Yesu anawabariki watoto (Mt. 19:13-15; Mk. 10:13-16; Lk. 18:15-16)
- Mariamu na Yusufu wanamleta Yesu (Lk. 2:22-38, 40)
- Kufundisha watoto (Efe. 6:4)

## KUWEKA VIONGOZI

Agano la Kale na Agano Jipya linazungumza kuhusu viongozi kuwekwa kwenye nafasi zao (au kuingizwa kazini). Bwana alimwamuru Musa kuwaweka wakfu Haruni na wanawe katika ukuhani (Kut. 29:1-27; Law. 8:1-36; Hes. 3:3). Baadaye alimwamuru Musa kufanya vivyo hivyo na Walawi ambao wangetumika katika hekalu (Hes. 8:5-22).

Katika kanisa la kwanza, mitume waliweka mikono juu ya mashemasi wa kwanza ili kuwaingiza kwenye nafasi zao (Mdo. 6:6). Vivyo hivyo, kanisa la Antiokia liliweka mikono juu ya Barnaba na Sauli, wakiwakabidhi katika kazi ya Bwana (Mdo. 13:2-3). Tena, Paulo alimwamuru Tito kuwateua wazee katika makanisa katika miji mbalimbali (Tito 1:5). Usemi wa Kiyunani uliotafsiriwa "teua" katika kifungu hiki ni kathistēmi, unaomaanisha "kuweka wakfu" au "kuingiza madarakani."

Ibada ya kuweka viongozi itasaidia kanisa kujua ni nani anayeshikilia nafasi fulani katika kanisa. Pia itawasaidia kujua majukumu ya ofisi. Itaboresha zaidi uaminifu wa ofisa huyo mpya machoni pa kusanyiko. Pia, ibada ya kuweka wakfu ni wakati wa kumkumbusha mhusika kwamba yeye ni mtumishi wa Kristo, na kwa sababu hiyo, amekabidhiwa mamlaka yake. Kwa hiyo, yeye si mtawala, bali mtumishi wa Bwana ambaye ndiye mmiliki wa kundi (1 Pet. 5:1-4).

**Ibada Yenyewe**

Kama mchungaji, utaanza ibada ya kuweka wakfu kwa kuwaita hao viongozi wapya waliochaguliwa wafike mbele ya kanisa. Kisha utasoma kifungu cha Maandiko kinachofaa na kuwatambulisha watendaji wapya kwa kusanyiko. Utapenda kueleza kusanyiko kwa ufupi majukumu ya kila nafasi. Kisha utaweka mikono juu ya hao watendaji wapya, ukimwomba Mungu awajaze Roho na kuwabariki katika utendaji wa huduma zao.

Hapa tendo la kuwekea watu mikono linaweza kuwa zaidi ya ibada. Katika Agano Jipya, watu mara nyingi walijazwa na Roho wakati walipowekewa mikono (Mdo. 8:17; 9:17-19; 19:6). Paulo alimkumbusha Timotheo "kuchochea karama ya Mungu, iliyo ndani yako, uliyopokea kwa kuwekewa mikono yangu" (2 Tim. 1:6). Mtume alikuwa akimaanisha karama ya Roho Mtakatifu ambayo Timotheo aliipokea wakati huo. Basi, watayarishe wahusika mapema, na kuwaambia, "Ninapoweka mikono juu yako, fungua moyo wako kwa Mungu ili ujazwe (au ujazwe tena) na Roho Mtakatifu."

**Vifungu vya Biblia**

Unaweza kusoma kifungu kimoja au zaidi kati ya vifungu vifuatavyo vya Biblia wakati wa uwekaji wakfu viongozi wa kanisa:

- Kuchaguliwa kwa wale Saba (Mdo. 6:1-7)
- Karama za huduma anazotoa Kristo (1 Kor. 12:28-31)
- Mawakili wa karama za Mungu (1 Pet. 4:10-11)
- Usiidharau karama yako (1 Tim. 4:9-16)
- Chochea karama ya Mungu (2 Tim. 1:1-8).

## KUWEKA MAJENGO WAKFU

Kuweka jengo wakfu ni tendo takatifu la kutenga nyumba au kitu kwa Mungu ili kitumike kwa ajili Yake tu, na kwa namna ya kipekee. Zoezi la kuweka wakfu majengo kwa Bwana linapata maana yake katika Maandiko. Mara kadhaa,

Waisraeli waliweka wakfu majengo kwa Bwana. Wakiwa nyikani, Musa na kusanyiko waliweka wakfu maskani au Hema kwa Yehova Mungu (Kut. 40:1-38). Pia waliweka wakfu madhabahu kwa Bwana (Hes. 7:10-11, 84-88). Miaka mingi baadaye, Ezra "alisherehekea kuwekwa wakfu kwa nyumba ya Mungu kwa furaha" (Ezra 6:16).

Mfano bora zaidi wa kuweka wakfu katika Biblia ni kuwekwa wakfu kwa hekalu la kwanza huko Yerusalemu. Sulemani alipomaliza kujenga hekalu, alipanga karamu kubwa na sherehe (1 Waf. 8). Wakati huo, mfalme aliongoza ibada ya kuweka wakfu ambapo alimwalika Mungu aje kukaa katika jengo hilo (1Wafalme 8:13-53).

**Kwa Nini?**

Leo, tunapoweka wakfu majengo ya kanisa kwa Bwana, tunayatenga kwa ajili Yake na kwa makusudi yake ya kipekee kama walivyofanya akina Musa, Ezra, na Sulemani. Tunamwambia Mungu, "Tunaweka wakfu jengo hili (au chombo/kitu hiki) Kwako, na litatumika (au kitatumika) kulileteа Jina Lako utukufu na kuendeleza kazi Yako duniani."

Kama Wakristo wa Kipentekoste, tunaelewa kwamba Roho wa Bwana anakaa ndani ya watu wa Mungu (1 Kor. 3:16), na kwamba Yeye huwawezesha kwa ajili ya huduma (Mdo. 1:8). Lakini tunaelewa pia kwamba wakati fulani uwepo wa Mungu unaweza kuja na kujaza majengo. Hiki ndicho kilichotokea Siku ya Pentekoste wakati "ghafla sauti kama ya upepo mkali ikatoka mbinguni, ikajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi" (Mdo. 2:2). Kristo ameahidi kudhihirisha kuwepo kwake wakati wawili au watatu watakapokusanyika kwa jina Lake (Mt. 18:20).

Madhumuni ya ibada ya kuweka wakfu ni kumshukuru Mungu kwa msaada aliotoa kwa kanisa katika kuwawezesha kukamilisha jengo hilo jipya. Pia ni kuweka wakfu matumizi ya jengo jipya kwake na kwa makusudi yake. Katika ibada, kusanyiko humwalika Bwana kushuka na kudhihirisha uwepo Wake kama alivyofanya katika Maandiko. Zaidi ya hayo, washirika wanajikabidhi tena kwa Mungu na utume wake wa ukombozi.

**Huduma ya Kujitolea**

Ibada ya kuweka wakfu inapaswa kuongozwa na mchungaji au kiongozi wa dhehebu aliyealikwa. Ni vizuri kuwa na ibada hiyo siku maalum ambapo wageni

waheshimiwa wataweza kuhudhuria. Huduma ya kuweka wakfu inaweza kuwa na haya yafuatayo kwa sehemu kubwa:

- Kukata utepe
- Maombi ya kuweka wakfu
- Utambulisho wa wageni maalum
- Usomaji wa maandiko
- Shuhuda
- Ibada
- Sadaka ya shukrani
- Mahubiri
- Kutembelea jengo jipya (au kukagua/kutazama chochote kinachowekwa wakfu)
- Chakula cha pamoja.

**Vifungu vya Biblia**

Vifungu vifuatavyo vya Biblia vinaweza kusomwa wakati wa ibada ya kuweka jengo wakfu:

- Kuwekwa wakfu kwa hekalu (2 Nya. 6:1-2, 17-20, 40; 7:1-5).
- Nyua za Bwana (Zab. 84)
- Twendeni katika nyumba ya Bwana (Zab. 122).

---

Kufanya ibada ya Ushirika Mtakatifu, kuwekwa wakfu kwa watoto, kuwekwa wakfu kwa viongozi wa kanisa, na kuwekwa wakfu kwa majengo ya kanisa na mali au vitu ni sehemu muhimu ya uhai wa kanisa la Kipentekoste. Mchungaji wa Kipentekoste hana budi kuendesha ibada hizi kwa heshima na taadhima zinazostahili.

# Viambatisho

# ~ Nyongeza ya 1 ~
# Tamko la Imani la Umoja wa Assemblies of God Duniani

Tamko hili la imani limekusudiwa kuwa msingi kwa ajili ya imani, ushirika, na ushirikiano kati yetu. Hili tamko halijavuviwa, lakini kinachoelezwa ndani yake ni cha muhimu sana kwa huduma ya kweli ya Kipentekoste. Hatusemi kwamba hili tamko linagusa kweli zote za Biblia, ila, linakidhi mahitaji yetu kuhusu haya mafundisho muhimu.

## 1. UVUVIO WA MAANDIKO

Tunaamini kwamba Maandiko, Agano la Kale na Agano Jipya, yamevuviwa na Mungu kwa maneno na ni ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu, kanuni isiyoweza kukosea, yenye mamlaka ya imani na mwenendo. Uvuvio wa kimungu unaenea kwa usawa na kikamilifu katika sehemu zote za maandishi ya awali, ukihakikisha kuaminika kwake (2 Tim. 3:15-17; 2 Pet. 1:21).

## 2. UMILELE WA MUNGU

Tunaamini katika umoja wa Mungu mmoja wa kweli na aliye hai ambaye ni wa milele, anayeishi, ambaye amejidhihirisha katika nafsi tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu (Mt. 3:16-17; 28:19).

*a. Mungu Baba.* Tunamwamini Mungu Baba, nafsi ya kwanza ya Utatu, anayeishi milele kama Muumbaji wa mbingu na dunia, Mtoa Sheria, ambaye vitu vyote vitawekwa chini Yake, ili aweze kuwa yote katika yote (Mwa. 1:1; Kumb. 6:4; 1 Kor. 15:28).

*b. Bwana Yesu Kristo.* Tunamwamini Bwana Yesu Kristo, nafsi ya pili ya Utatu, aliyekuwa na bado ndiye Mwana wa Mungu wa milele. Tunaamini kwamba alifanyika mwili kwa Roho Mtakatifu na kuzaliwa na bikira Mariamu.

Tunaamini kuhusu maisha Yake bila dhambi, huduma yenye miujiza, kifo Chake badala yetu kwa ajili ya ukombozi, kufufuka kwake katika mwili, kupaa kwake kwa ushindi, na kutuombea kwake endelevu (Isa. 7:14; Mdo. 1:9; 2:22; 10:38; 1 Kor. 15:4; 2 Kor. 5:21; Ebr. 7:25-26; 1 Pet. 2:22).

*c. Roho Mtakatifu.* Tunamwamini Roho Mtakatifu, nafsi ya tatu katika Uungu, atokaye kwa Baba na Mwana, na aliyeko daima na mtendaji katika kazi ya kuonyesha dhambi na kumzaa mwenye dhambi mara ya pili, na kumtakasa mwamini katika kweli yote (Yoh. 14:26; 16:8-11; Rum. 8:14-16; 1 Pet. 1:2).

## 3. ANGUKO LA MWANADAMU

Tunaamini kwamba binadamu waliumbwa wakiwa wema na sahihi. Lakini, kukosea kwa hiari yao kulisababisha kutengana na Mungu, na hilo likaleta kifo cha kimwili pamoja na cha kiroho, ambako ni kutengwa na Mungu (Mwa. 1:16-27; 2:17; 3:6; Rum. 5:12-19).

## 4. KUOKOLEWA KWA MWANADAMU

Tunaamini kuhusu wokovu kwa kumwamini Kristo, aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu, akazikwa na kufufuka toka wafu siku ya tatu. Kwa damu Yake ya upatanisho, wokovu umetolewa kwa binadamu wote kwa njia ya dhabihu ya Kristo msalabani. Jambo hili linajulikana pia kama kuzaliwa mara ya pili, na ni kazi inayotokea papo hapo, inayofanywa na Roho Mtakatifu. Mwenye dhambi anayeamini anafanywa upya, anahesabiwa haki na kufanywa mwana katika familia ya Mungu. Pia anakuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, na mrithi wa uzima wa milele (Yoh. 3:5-6; Rum. 10:8-15; Tito 2:11, 3:4-7; 1 Yoh. 5:1).

## 5. UPONYAJI WA KIUNGU

Tunaamini kwamba kukombolewa kutoka magonjwa ni kitu kilichomo katika ukombozi na ni fursa kwa ajili ya waamini wote (Isa. 53:4-5; Mt. 8:16-17; Yak. 5:14-16).

## 6. KANISA NA UTUME WAKE

Tunaamini kwamba Kanisa ni mwili wa Kristo na makao ya Mungu kwa njia ya Roho, na ni shahidi wa uwepo wa ufalme wa Mungu katika dunia ya sasa, lenye kuwahusisha watu wote waliozaliwa mara ya pili (Rum. 14:17-18; 1 Kor. 4:20; Efe. 1:22-23; 2:22).

Tunaamini kwamba utume wa kanisa (1) ni kutangaza habari njema za wokovu kwa binadamu wote, (2) ni kuwajenga na kuwafundisha waaminio ili wafanye huduma ya kiroho, (3) ni kumsifu Bwana kupitia ibada, na (4) ni kuonyesha huruma ya Kikristo kwa wote wanaoteseka na kuumia (Mt. 10:42; 28:19-20; Efe. 4:11-13).

## 7. MAAGIZO YA KANISA

Tunaamini kwamba ubatizo wa maji kwa kuzamishwa ni kitu kinachotazamiwa kwa wote waliotubu na kuamini. Kwa kufanya hivyo, wanatangaza kwa dunia kwamba wamekufa pamoja na Kristo na kufufuliwa pamoja Naye ili kuenenda katika upya wa uzima (Mt. 28:19; Mdo. 10:47-48; Rum. 6:4).

Tunaamini kwamba Meza ya Bwana ni tangazo la kuteswa na kufa kwa Bwana wetu Yesu Kristo, na ni ibada inayotaka waamini wote kushiriki hadi Bwana arudipo (Lk. 22:14-20; 1 Kor. 11:20-34).

## 8. UTAKASO

Tunaamini kwamba utakaso ni tendo la kutengwa kutokana na kila kilicho kiovu, na kuwekwa wakfu kwa ajili ya Mungu. Kwa uzoefu, ni kitu kinachotokea papo hapo lakini pia ni endelevu. Hutokea katika maisha ya aaminiye kwa yeye kutwaa nguvu za damu ya Kristo na uzima wa kufufuka kwake kwa njia ya Roho Mtakatifu. Yeye humfanya mwamini kumwona Kristo, humfundisha kupitia Neno na kuzalisha tabia ya Kristo ndani yake (Rum. 6:1-11; 8:1-2, 13; 12:1-2; Gal. 2:20; Ebr. 10:10, 14).

## 9. UBATIZO KATIKA ROHO MTAKATIFU

Tunaamini kwamba ubatizo katika Roho Mtakatifu ni tendo la mwamini kupewa nguvu za kuishi na kutumika kwa ajili ya Kristo. Tukio hili ni tofauti na kuzaliwa mara ya pili, na liko peke yake, na hupokelewa kwa imani, na linaambatana na udhihirisho wa kunena kwa lugha kama ushahidi wa kwanza, kwa kadiri Roho anavyojalia kutamka (Lk. 24:49; Mdo. 1:8; 2:1-4; 8:15-19; 11:14-17; 19:1-7).

## 10. KARAMA ZA ROHO MTAKATIFU

Tunaamini katika utendaji wa siku hizi wa zile karama tisa za kiungu za Roho Mtakatifu (1 Kor. 12) na zile karama za huduma atoazo Kristo (Efe. 4:11-13) kwa ajili ya kujengwa na kupanuka kwa kanisa.

## 11. MWISHO WA WAKATI

Tunaamini katika kurudi kibinafsi hivi karibuni kwa Bwana wetu Yesu Kristo kabla ya utawala wa miaka elfu, ili kujikusanyia Wake. Tukiwa na hilo tumaini lenye baraka na matarajio ya dhati, tunajitakasa, kama naye alivyo mtakatifu, ili

tuweze kuwa tayari kukutana naye anapokuja (Yoh. 14:1-3; Tito 2:13; 1 Thes. 4:15-17; 1 Yoh. 3:2-3; Uf. 20:1-6).

Tunaamini kwamba binadamu wote watafufuliwa miili, na kwamba kutakuwa na raha ya milele iliyo halisi kwa wote wanaomwamini Bwana wetu Yesu Kristo kwa dhati, na kwamba adhabu ya milele iliyo halisi ndilo fungu la wote ambao majina yao hayajaandikwa katika Kitabu cha Uzima (Yoh. 5:28-29; 1 Kor. 15:22-24; Uf. 20:10-15).

# ~ Nyongeza ya 2 ~
# Karama za Udhihirisho za 1 Wakorintho 12:8-10

**Karama Za Ufunuo** (Kupewa kujua nia ya Mungu)

- Neno la maarifa: Ufunuo unaotolewa na Roho ambao ni sehemu ya maarifa ya Mungu
- Neno la hekima: Ufunuo unaotolewa na Roho ambao ni sehemu ya hekima ya Mungu
- Kupambanua roho: Ufunuo unaotolewa na Roho kuhusu roho yenye kujidhihirisha au kuhamasisha tendo au neno.

**Karama Za Kinabii** (Kusema maneno ya Mungu)

- Unabii: Neno lililoongozwa na Roho Mtakatifu kutoa ujumbe kutoka kwa Mungu
- Lugha za aina mbalimbali: Neno lililoongozwa na Roho Mtakatifu likitoa ujumbe wa Mungu, au maombi kwa Mungu, katika lugha isiyojulikana na mzungumzaji.
- Tafsiri za lugha: Neno lililoongozwa na Roho Mtakatifu likitoa maana ya ujumbe au maombi yaliyotolewa katika lugha.

**Karama Za Nguvu** (Kutenda kazi za Mungu)

- Imani: Msukumo wa imani kwa nguvu za Roho ili kukamilisha kazi iliyotolewa na Mungu
- Karama za uponyaji: Uponyaji wa magonjwa na maradhi mbalimbali kwa nguvu za Roho
- Miujiza: Kuachiliwa kwa nguvu za Mungu kwa njia ya Roho ili kukamilisha kazi maalum ya Mungu. (Kumbuka: Hii karama inaweza pia kuitwa kwa usahihi zaidi "matendo ya nguvu" au kutokana na neno la Kiyunani - energemata dunameon - "utendaji kazi wa nguvu."

# ~ Nyongeza ya 3 ~
# Ufupisho wa Vitabu vya Biblia

**Agano la Kale**

Mwanzo—Mwa.
Kutoka—Kut.
Mambo ya Walawi—Law.
Hesabu—Hes.
Kumbu la Torati—Kumb.
Yoshua—Yosh.
Waamuzi—Amu.
Ruthu—Ruthu
1 Samweli—1 Sam.
2 Samweli—2 Sam.
1 Wafalme—1 Waf.
2 Wafalme—2 Waf.
1 Mambo ya Nyak—1 Nya.
2 Mambo ya Nyak—2 Nya.
Ezra—Ezra
Nehemia—Neh.
Esta—Esta
Ayubu—Ayu.
Zaburi—Zab.
Mithali—Mit.
Mhubiri—Mhu.
Wimbo Bora—Wimbo
Isaya—Isa.
Yeremia—Yer.
Maombolezo—Ombo.
Ezekiel—Eze.
Daniel—Dan.
Hosea—Hos.
Yoeli—Yoe.
Amosi—Amo.
Obadia—Oba.
Yona—Yona
Mika—Mik.
Nahumu—Nah.
Habakuki—Hab.
Sefania—Sef.
Hagai—Hag.
Zekaria—Zek.
Malaki—Mal.

**Agano Jipya**

Mathayo—Mt.
Marko—Mk.
Luka—Lk.
Yohana—Yoh.
Matendo—Mdo.
Warumi—Rum.
1 Wakorintho—1 Kor.
2 Wakorintho—2 Kor.
Wagalatia—Gal.
Waefeso—Efe.
Wafilipi—Flp.
Wakolosai—Kol.
1 Wathesalonike—1 Thes.
2 Wathesalonike—2 Thes.
1 Timotheo—1 Tim.
2 Timotheo—2 Tim.
Tito—Tito
Filemoni—Flm.
Waebrania—Ebr.
Yakobo—Yak.
1 Petro—1 Pet.
2 Petro—2 Pet.
1 Yohana—1 Yoh.
2 Yohana—2 Yoh.
3 Yohana—3 Yoh.
Yuda—Yuda
Ufunuo—Uf.

AFRICA'S HOPE

AFRICA'S
HOPE